JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA MTIHANI WA CEKENAS
MUHULA WA PILI MWAKA 2018
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari
102/1
KISWAHILI
INSHA

1. Wewe ni katibu wa kamati iliyoteuliwa na rais kuchunguza chanzo cha kudorora kwa usalama nchini. Kamati imepewa muda wa miezi mitatu kuwasilisha ripoti.
   Andika ripoti miliowasilisha.
2. Utelekezaji wa mtoto wa kiume katika nchini ni janga kuu. Jadili.
3. Mpiga mbizi nchi kavu huchunua usowe.
4. Andika insha inayomalizia kwa:
   …. Alianza kubabaika kijasho kikaanza kumtoka kwapani. Nikatambua moja kwa moja kuwa yeye ndiye mkosa!

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA MTIHANI WA CEKENAS
MUHULA WA PILI MWAKA 2018
Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Sekondari
102/2
KISWAHILI
Karatasi ya Pili
(LUGHA)

1. **UFAHAMU (ALAMA 15)**

Soma kifuatacho kisha ujibu maswali.

Lugha inaweza kuelezwa kwa jumla kuwa ni mfumo wa kueleza chanzo au kiini cha mawasiliano na sote tunakubaliana kuwa matumizi yake yameanza tangu kuumbwa kwa binadamu kwani ni vigumu kukisia kuwepo kwa jamii ya watu bila lugha ya mawasiliano yoyote ile.

Katika taifa lolote,huwepo na lugha moja au hata zaidi ya moja ambayo huwa ndicho chombo zatika cha mawasiliano ya taifa katika nyanja za:elimu, maandishi, siasa na biashara.Kwa mfano mataifa ya Kanada hutumia lugha mbili kwa usawa kama lugha za taifa na za kikazi. Maana ya lugha ya taifa ni lugha moja ambayo huteuliwa kutumika katika shughuli zote za taifa hasa katika nchi yenye lugha nyingi za kikabila. Lugha ya taifa ni muhimu sana kwa maisha na maendeleo ya taifa lolote lile.Lugha hii huwa ndiyo kiungo cha kueneza umoja na uelewano miongoni mwa jamii nyingi tofauti na huwa kama kitambulisho kwao kwa kuwa wao ni ndugu wa jamii moja kubwa, yaani taifa lao.

Kenya ni mfano mzuri wa taifa lenye lugha nyingi zinazozidi 40 za vikundi vidogo vidogo vya kikabila.Hapo kabla ya miaka mia moja hivi iliyopita kila kimojawapo cha vikundi hivi kilijitambulisha kama taifa huru.Baada ya kuja kwa serikali ya kikoloni na hasa baada ya Kenya kujinyakulia uhuru,haja ya kuunganisha raia wote chini ya taifa moja lenye uongozi na shabaha moja lilikuwa ndilo jambo lililozingatiwa sana.Kwa hivyo utamaduni wa taifa la Kenya ni mchanganyiko wa tamaduni za watu wengi wenye mila,desturi,imani na itikadi tofauti. Utamaduni humaanisha jumla ya amali na tabia za watu wa jamii fulani. Amali hizi zinafungamanisha fikira, ustaarabu, mila, taasisi na sanaa za aina zote za jamii inayohusika. Ili kujieneza na kujiimarisha,taifa huhitaji chombo hicho kuwasiliana na kuwaunganisha watu wake wenye asili mbalimbali.Chombo hicho huwa ni lugha ambayo siyo tu kwamba ni sehemu ya utamaduni wa jamii bali pia ni njia muhimu sana ya kutawanyia na kustawishia ule utamaduni.

Katika taifa lenye lugha nyingi kama Kenya kwa mfano,lugha ya taifa inayozungumzwa na kueleweka na idadi kubwa ya raia ambayo imekiuka mipaka na tofauti za kikabila ni njia muhimu sana ya kueneza maongozi ya taifa, bendera ya taifa, ndicho kielelezo cha taifa lolote lile lililo huru. Lugha kama hiyo huvunja na hukomesha hisia za kibinafsi na kikabila na badala yake kuunda moyo wa uaminifu wa kitaifa.

Zaidi ya kuwa chombo cha mawasiliano, lugha ni kielelezo cha fikira na hisia za binadamu.Lugha ya watu fulani haituelezi tu ujuzi au maarifa yao bali pia mtazamo wao kimaisha, falsafa na mawazo yao.

Kwa ufupi lugha hutufahamisha namna akili za watu waizungumzayo ile lugha zinavyofikiri na kutafanya maazimio.Lugha ni sehemu ya utamaduni wa taifa ilimozaliwa na lazima lugha hiyo ifunzwe katika muktadha wa maisha ya jamii ihusikayo.Utamaduni wa jamii havitenganiki na lugha yake.

MASWALI

a) Ni nini fasiri ya neno lugha? (alama 2)
b) Tofautisha baina ya lugha ya taifa na lugha ya kikazi. (alama 2)
c) Kwa nini lugha ya taifa huhitajika sana katika nchi kama Kenya? (alama 2)
d) Taja kazi **tatu** kuu zinazotekelezwa na lugha ya taifa. (alama 3)
e) Eleza maana ya msamiati ufuatao kulingana na taarifa. (alama 3)
   (i) Haiyamkiniki: ……
   (ii) Amali na tabia za watu :…….....
   (iii) Kielelezo:…….……
   (iv) Muktadha wa maisha ya jamii: …….
f) Eleza majukumu mawili ya lugha kwa ujumla. (alama 2)

2. UFUPISHO: (ALAMA 15)

Soma kifungu kifuatasho kisha ujibu maswali.

Kwa kawaida, binadamu huishi kwa kutangamana na binadamu wenzake. Katika kutangamana huku, watu huathiriwa kitabia, kifikira, kimavazi na kimaisha kwa jumla. Watu wote katika jamii wana uwezo wa kuathiri na kuathiriwa na wenzao wa umri mmoja. Hata hivyo, walio katika hatari ya kuathiriwa zaidi na mahirimu wao ni vijana. Hali hii ya kuathiriana huitwa shinikizo-rika au shinikizo-marika. Vijana huaminiana na kuthaminiana sana. Kwa sababu hiyo, ni rahisi sana kuingizwa katika mitego na wenzao. Isiaminiwe kuwa vijana pekee ndio wanaoathiriwa na shinikizo-rika. La hasha! Watu wazima pia huwafuata wenzao mithili ya bendera kufuata upepo. Mwenzake akinunua gari, yeye pia hukimbilia mkopo kununua gari la sampuli iyo hiyo bila kuwazia kima cha kibindo chake.

Wataalamu wa saikolojia husema kuwa kukabiliana na tatizo la shinikizo-rika si rahisi kwa sababu shinikizo-rika huleta mtafaruku wa kinafsi akilini mwa anayeathiriwa. Nafsi moja humshawishi kufuata wenzake huku nyingine ikimnasihi kuandamana upekee au ubinafsi wake. Shinikizo-rika huathiri sana mahitaji ya kisingi ya binadamu. Ikumbukwe kuwa mahitaji haya ya kimsingi ni ya kila mwanadamu, nayo ni kama vile kupata lishe, hewa safi, kupenda na kupendwa miongoni mwa mengine. Kila mtu hutaka kujihusisha na kundi la watu ambao watamfanya kuhisi kuthaminiwa na kukubalika. Kutokana na haja ya kutaka kukubalika, anayetaka kutambuliwa huridhia matakwa ya wenzake bila hata kuyawazia.

Shinikizo-rika hujittokeza kwa sura nyingi. Mathalani, vijana huwafanya wenzao kuona kuwa wana hatia wasipoafiki kutekeleza kama wanavyoshinikizwa. Kauli kama vile 'tulifikiri wewe ni mmoja wetu' au 'usiposhirikiana nasi utakuwa umetuvunja moyo' hutamalaki. Wanaokataa kushinikizwa hubezwa na kufanyiwa stihizai na wenzao na hata kutengwa. Vitisho hutolewa, wakati mwingine, na anayeshinikiswa akidinda, mabavu hutumika.

Ni muhimu kwa watu, hasa vijana, kufahamu kuwa shinikizo-rika lipo na wanapokabiliwa na tatizo hilo, watambue kuwa wana haki ya kusimama kidete kutetea msimamo wao dhidi ya wenzao. Kumbuka, baridi huwazizima kondoo kwa namna tofauti.

Kama njia moja ya kukabiliana na shinikizo-rika, wanasaikolojia wanapendekeza watu kujiamini na kuelewa kwamba wana haki ya kuwa tofauti na kuwa na upekee wao. Mtu anapojiamini na kushikilia msimamo wake, anaweza kujiepusha na madhara yatokanayo na shinikizo-rika. Asiyejiamini huwa mwepesi sana wa kuingizwa katika lindi la mashaka na wenzake.

Maswali

(a) Bila kupoteza maana, fupisha aya ya kwanza na ya pili kwa **maneno (40)**. **(alama 8, 1 ya utiririko)**

Nakala chafu

Jibu

(b) Fupisha mambo muhimu ambayo mwandishi amezingatia katika aya tatu za mwisho. (maneno 30)

3. MATUMIZI YA LUGHA: (ALAMA 4)

(a) Tofautisha kati ya: (i) / e / (ii) / u / (alama 2)
(b) Onyesha **muundo** wa **silabi** ya kwanza katika maneno yafuatayo:

(alama 2)
(i) Nyakua
(ii) Chura

(c) Tunga sentensi kwa kutumia kibadala cha kiasi jumla. (alama 2)

(d) Changanua sentensi ifuatao kwa kutumia **jedwali**.
(alama 4)
Mkongojo mrefu sana ulioletewa babu utauzwa na fundi mcheshi.

(e) Andika **kinyume** cha sentensi ifuatayo:
Mtoto msichana anathema dawa.
(alama 2)

(f) Kanusha: (alama 2)
Nikimpiku masomoni nitatuzwa zawadi.

(g) Andika katika usemi halisi.
(alama 3)
Chifu wetu alitwambia kuwa watu wanaopenda kukaa bwerere huishia kuwa wezi wa mabavu.

(h) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo mabanoni.
(alama 2)
(i) (-la) (kauli tendeshea)
(ii) Toa (tendeka)

(i) Eleza matumizi ya alama zifuatazo za uakifishi. (alama 2)
(i) **!**
(ii) **?**

(j) Bainisha mofimu **–Li-** katika tungo hili. (alama 3)
Alivyolikimbilia

(k) Tunga sentensi moja yenye shamirisho hizi.
(alama 3)
(i) Kipozi
(ii) Kitondo
(iii) Ala

(l) Ainisha vishazi. (alama 2)
Mhamiaji haramu aliyeshikwa amefikishwa mahakamani.

(m) Andika katika wingi <u>karibu</u>.
(alama 2)
Mtu yuyo huyo aliubeba mzigo uo huo licha ya kukanywa.

(n) Andika sentensi ifuatayo katika watati ujao timilifu.
(alama 2)
Mbunge alitawazwa kabla ya mpinzani wake kufika.

(o) Andika kwa wastani. (alama 1)
Magoma haya yatachezwa wanjani.

(p) Taja na utoe mifano, matumizi <u>mawili</u> ya kiimbo.
(alama 4)

(q) Eleza maana mbili za sentensi. (alama 2)
Nenda ukaniletee mbuzi.

4. <u>SEHEMU YA D: ISIMU JAMII (ALAMA 10)</u>

(a) Eleza mitazamo mine kuhusu chimbuko la Kiswahili. (alama 4)

(b) Eleza njia za uundaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili.
(alama 6)

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA MTIHANI WA CEKENAS
MUHULA WA PILI MWAKA 2015
102/3
KISWAHILI
FASIHI
KARATASI YA TATU

1. **SWALI LA LAZIMA**
MSTAHIKI MEYA
Uvundo haswa! Hata wageni sijui wataonaje hali hii. Aibu kubwa inatungojea kama watakuja!
a. Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b. Jadili hulka zozote **mbili** za msemaji zinazojiktokeza katika muktadha huu. (alama 4)
c. Thibitisha kuwa Cheneo ilikuwa imejaa 'uvundo.' (alama 12)

SEHEMU YA B: RIWAYA:
KIDAGAA KIMEMWOZEA – KEN WALIBORA
Jibu swali la 2 au 3

2. Ujenzi wa jamii mpya ni wajibu wa vijana. Thibitisha ukweli wa kauli hii ukirejelea riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 20)
AU
3. "Lowela tunapendana mno na ni msiri wangu wala hakuogopa kuniambia yaliyojiri.
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Fafanua 'yaliyojiri' kwa mujibu wa msemaji. (alama 8)
(c) Lowela ni kielelezo kibaya cha msichana wa kisasa. Thibitisha. (alama 8)

SEHEMU C: HADITHI FUPI: DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE
Jibu swali la 4 au 5

4. Eleza kwa Kutolea mifano uozo wa jamii katika diwani ya Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine. (alama 20)
AU
5. Kanda la Usufi.
Muhula wa tatu wa kidato ulipoanza alijiunga na wanafunzi wengine.
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Eleza dhana ya utatu katika hadithi Kanda la Usufi. (alama 4)
(c) Thibitisha ukweli wa methali hii 'mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi. (alama 8)
(d) Eleza umuhimu wa mhusika mkuu katika hadithi. (alama 4)

SEHEMU YA D: USHAIRI
Jibu swali la 6 au 7

6. **Soma shairi hili kasha ujibu maswali yanayofuata:**
Jukwani naingia, huku hapa pasokota,
Kwa uchungu ninalia, hii tumbo nitaikata,
Msiba mejiletea, nimekila kiso takata,
We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?

Wazee hata vijana,wote umewasubua,
Huruma nao hauna, heshima kawakosea,
Ukambani na Sagana, hata mbwa wararua,
We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?

Wahasibu ofisini,kibwebwe mejifunga,
Miaka mingi vitabuni, ili wasikose unga,
Nadhari wanadhamini, hesabu wanazirenga,
We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?

Wapenzi wa kiholela, pia wanakuogopa,
Baada yao kulala, wana wao wanatupa,
Wakihitaji chakula, wanachokora mapipa,
We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?

Wafugaji hata nao, kama dawa wakwamini,
Hawajali jiranio, wamesusia amani,
Wanaiba ng'ombe wao, na kuzua kisirani,
We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?

Nayo mizozo ya maji, kaonekana kwa mara,
Hiyo nayo ni dibaji, sababu sio harara,
Njaa wahepe wenyeji, huo ndio mkarara,
We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?

Ningeweza kukuuza, ingekuwa siku njema,
Tena kwa bei ya meza, sokoni nimesimama,
Wala tena singewaza, kuhusu wali na sima,
We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?
Hatima umefikika, naenda zangu nikale,
Mate yanidondoka, kwa mnukio wa wale,
Naomba kwenda kukaa, wala sio nikalale,
We tumbo nitakupani, uwe umetosheka?

Maswali

(i) Lipe anwani mwafaka shairi hili. (alama 2)
(ii) Shairi hili ni la aina gani? Toa sababu.
(alama 2)
(iii) Huku ukitolea mifano mwafaka, taja arudhi zilizotumiwa katika ubeti wa tatu.
(alama 4)
(iv) Andika ubeti wa nne kwa lugha nathari. (alama 4)
(v) Thibitisha kuwepo kwa idhini ya ushairi. (alama 2)
(vi) Taja madhila anayoelezea mtunzi wa shairi hili yaletwayo na tumbo.
(alama 4)
(vii) Elezea maana ya maneno yafuatayo.
(alama 2)
(a) Dibaji
(b) Harara

AU

7. **FASIHI SIMULIZI**.

i. (i) Eleza maana ya misimu.
(alama 2)
(ii) Eleza dhima ya misimu. (alama 4)

ii. Taja aina **nne** za ngomezi za kisasa.
(alama 4)

iii. Eleza sifa **nne** za maapizo.
(alama 4)

iv. Eleza kikwazo **vitatu** vinavyokumba Fasihi simulizi.
(alama 6)

MTIHANI WA MWIGO WA CEKENA 2015
102/1
KISWAHILI KARATASI YA 1
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

1. **Swali la Lazima**

Sura

- Anwani – Herufi kubwa
- Utangulizi
- Njia za utafiti
- Matokeo – Angaa hoja tano.
- Mapendekezo – Yaoane na matokeo / matatizo.
- Hitimisho
- Jina
- Cheo
- Sahihi

Majibu / Hoja

a. Ukosefu wa kazi kwa vijana.
b. Idadi chache ya maafisa wa usalama.
c. Imani potovu – dini / utamaduni.
d. Ufisadi
e. Utepetevu wa uongozi.
f. Ukosefu wa motisha kwa walinda usalama.
g. Vifaa / zanaa duni za usalama.
h. Teknolojia – mtandao.
i. Ubinafsi.

Mwalimu akadirie hoja nyingine.

2. Utelekezaji wa mtoto wa Kiume

Jinsi ametelekezwa

- Kukosa waelekezi
- Kuwachwa kujikidhi pekee.
- Kutopigwa debe kama msichana.
- Kutwikwa majukumu angali mchanga.
- Kutojaliwa na mashirika ya ufadhili.
- Vyama vya ku;igania mvulana kutowajibika.
- Kunyimwa nafasi ya masomo.
- Kukosa mashirika ya utafiti kuhusu wavuluna.

Janga

- Anaacha masomo
- Anaingilia dawa za kulevya na anasa.
- Anaungana na vikundi vya ugaidi.

- Wanakosa hadhi ya mwanamume.
- Kuchangia kuporomoka kwa misingi ya kifamilia.
- Kukosa viongozi wa kesho.

TANDIHI

1. *Lazima aonyeshe pande mbili, asipo atuzwe nusu ya alama.*
2. *Kuwe na kichwa au mada.*
3. *AtImize maneno kati 300 – 400*
4. *Kadiria hoja nyinginezo.*

3. Mtahiniwa atunge kisa kinachodhihirisha jinsi yeye / mtu mwengine alivyojiingiza katika janga na alivyopata madhara / matatizo.
4. Mtahiniwa abuni kisa kitakachooana na sentensi yenyewe.
   - Asipotumia robo tatu ya maneno katika sentensi aadhibiwe.

MTIHANI WA MWIGO WA CEKENA 2015
102/2
KISWAHILI KARATASI YA 2
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

1. UFAHAMU (ALAMA 15)

(a) Ni mfumo wa mawasiliano katika jamii yoyote ile. (alama 2)

(b) Lugha ya taifa na ile inayoteuliwa kutumia katika shughuli zote za taifa ambayo hueneza umoja na uelewano katika jamii ilhali lugha ya kikazi ni ile inayotumiwa kuendesha shughuli rasmi za taifa. (alama 2)

(c) (i) Huhitajika ili kueneza maongozi ya taifa ya kuleta ufahamikiano kote nchini.
(ii) Ili kuvunja na kukomesha hisia za kibinafsi na kikabila. (alama 2)

(d) (i) Ni chombo cha mawasiliano katika nyanja za elimu, biashara, maandishi na siasa.
(ii) Ni kiungo cha kueneza umoja na maelewano miongoni mwa jamii tofauti.
(iii) Ni kitambulisho cha utaifa. (alama 3)

(e) (i) Haiwezekani.
(ii) Matendo na hulka za binadamu.
(iii) Mfano
(iv) Mazingira (alama 4)

(f) (i) Ni chombo cha mawasiliano.
(ii) Ni kielelezo cha fikra na hisia za binadamu. (alama 2)

2. MAJIBU YA MUHTASARI

(a)
(i) Binadamu huishi kwa kutangamana.
(ii) Binadamu huathiriana kitabia, kifikiria, kimavazi na kimaisha.
(iii) Watu wote wana uwezo wa kuathiri na kuathiriwa.
(iv) Wanaoathiriwa zaidi ni mahirimu wao na vijana.
(v) Hali ya kuathiriana huitwa shinikizo-rika.
(vi) Wattu wazima pia huathiriwa na wenzao.
(vii) Watu wote wanaweza kuathiriwa na shinikizo-rika,.
(viii) Ni vigumu kukabiliana na shinikizo-rika. (alama 7, 1 ya utiririko)

(b)
(i) Shinikizo-rika hujitokeza kwa sura nyingi.
(ii) Kulazimisha watu kutenda kinyume na imani yao.
(iii) Wanaokataa kushinikizwa hubezwa na kugengwa na wenzao.
(iv) Pia wanaweza kutishwa kwa kutumia mabavu.
(v) Wanaoshinikizwa wasimame kidete na watetee msimamo wao.
(vi) Wanasaikolojia wanapendekeza watu wajiamini.
(vii) Asiyejiamini atahangaishwa na wenzake. (alama 6, 1 ya utiriko)

3. MATUMIZI YA LUGHA

(a) (i) / e /

1. Mbele
2. Kati
3. Mtandazo

(ii) / u /

1. nyuma
2. juu
3. mviringo

(b) Nyakua – KI / KKI – 1 x 1
Chura – KI ala 1 x 1

(c) Wachache walifika jioni. (1 x 2 = 2) (Kadiria kiwakilishi jumla)

(d)

S							
KN				KT			
N	V	E	S	T	H	N	V
mkongojo	mrefu	sana	ulioletewa babu	utauzwa	na	fundi	mcheshi

(12 x 1/3 = 4)

(e) Mtoto msichana amemeza dawa. (1x2 = 2)

(f) Nisipompiku masomoni sitatuzwa zawadi. (1x2)

(g) "Watu wanaopenda kukaa bwerere huishia kuwa wezi wa mabavu," chifu wetu alituambia. (6 x ½ = 3)
Au Chifu wetu alituambia, "Watu wanaopenda kukaa bwerere huishia kuwa wezi wa mabavu."

(h) (i) –La – Lishia (ala 1x1 =1)
(ii) toa – toleka (ala 1x1 = 1)

(i) Matumizi ya alama ya mshangao (!)

1. Kushangaa
2. Kuamrisha (ala 1x1 = 1)

Kiulizi
(i) Kuuliza swali (1 x 1 = 1)

(j) A
LI – wakati uliopita
vyo
li – mtendwa
kimbi
li – kauli

(k) Mwanafunzi alimwandikia rafikiye barua kwa penseli.
Kipozi – barua
Ala – penseli (alama 3 x1 = 3)
Kitendo – rafikiye (kadiria sentensi)
(Tanbihi: Mwanfunzi atuzwe alama kwa maneno aliyoyaelekeza.

(l) Mhamiaji haramu aliyeshikwa amefikishwa mahakamani.
a – kishazi tegemezi
b – kishazi huru

(m) Wingi karibu
Watu wawa hawa waliibeba mizigo ii hii licha ya kukanywa. (alama 1 x 2)

(n) Mbunge atakuwa ametawazwa kabla ya mpinzani wake kufika. (alama 1x2 =2)

(o) Ngoma hii itachezwa wanjani. (alama 1x1)
Mwanafunzi asiandike wastana wa kielezi.

(p) Matumizi ya kiimbo

- Swali
- Rai / ombi Kutaja (2 x 1 = 2)
- Amri
- Mshangao Kutunga sentensi (2 x 1 = 2)
- Taarifa

(q) Mbuzi – Kifaa cha kukunia nazi.

- Mnyama

4. ISIMU JAMII

(a) Mitazamo mine kuhusu chimbuko la Kiswahili.
- Kiswahili ni kibantu – ushahidi mwingi.
- Kiswahili ni kiarabu au lahaja ya kiarabu kwa kuwa kimekopa msamiati mwingi huko.
- Kiswahili ni krioli – kilitokana na ndoa baina ya waarabu na wabantu.
- Kiswahili kilitoka Kongo. (alama 4x1 = alama 4)

(b) Mbinu za kuunda maneno
- Kutohoa
- Tafsiri sisisi
- Kuunganisha maneno
- Uhamishaji wa maneno kutoka lugha mf. Ugali.
- Kukopa
- Tanakali za sauti
- Kuongeza viambishi / mnyambuliko.
- Ufupishaji / akronimu.

MTIHANI WA MWIGO WA CEKENA 2015
102/3
KISWAHILI KARATASI YA 3
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

1. (i) Mzungumzaji ni Siki, Mzungumziwa ni Diwani IIII, wako nyumbani kwa Diwani III. Wawili hao walikuwa wakizungumzia shida zinazowakumba Wanacheneo na hali mbaya ya uchafu wa kimazingira, Diwani III analamikia hali hii akisema kulikuwa na harufu kila pahali ndiposa Siki anatamka maneno haya.

(ii) **Jadili huka zozote mbili za msemaji zinazojitokeza katika muktadha huu.**
- Ni mtetezi wa haki: Anamtembelea Diwani III kwa lengo la kujadiliana naye kuhusu masaibu yanayowakumba wananchi na jinsi haki zao zinakiukwa na uongozi wa Meya.
- Msema kweli: Anaeleza ukweli kuwa hali ya uchafu mjini ilikuwa imefikia kiwango cha kuvunda.
- Amewajibika: Kwa sababu ameshuhudia maisha duni ya wananchi, anachukuwa jukumu la kumtembelea Diwani III ambaye ni mmojawapo wa viongozi wa baraza la mji ili hatua ichukuliwa ya kutatua matatizo ya wananchi.

(iii) **Thibitisha kuwa Cheneo ilikuwa imejaa uvundo.**
- Kusema kuwa Cheneo ilikuwa imejaa uvundo ni kuashiria kuwa kulikuwa na hali ya uozo katika jamii yenyewe. Jambo hili ladhihirika kwa njia zifuatazo:
  a. Kuna visa vya ufisadi: Meya akishirikiana na vibaraka wake kama Bili na Diwani I na II wanapanga njama ya kuuza fimbo ya Meya iliyokuwa mali ya umma kwa lengo la kupata fedha za kujilipa kwa kikao kisicho rasmi. Meya pia anaonekana kumiliki mashamba mengi ambayo ameyapata kwa njia isiyo halali na hata kugawa hizo ploti za umma kwa marafiki wake kama Bili.
  b. Meya anasema jinsi alivyomgawia Bili vipande vinne vya ardhi naye baada ya kuuza vipande vitatu amebakisha vitano.
  c. Kuna ukatili uliokithiri katika jamii hii: Meya anatumia askari wa baraza kuwatawanya wafanyakazi waliokuwa wakigoma kisha anacheka akifurahia jinsi waandamanaji hao walivyofyatuliwa risasi na wengine katika kufariki.
  d. Kuna uchafuzi wa mazingira: kutokana na kuchafuliwa kwa mazingira, kuna uvundo uliosheheni katika eneo hili. Wakati Meya alikuwa akinywa maji anahisi harufu akadhania ilikuwa inatoka majini lakini anaelezwa kuwa uvundo huo ulikuwa ukitokana na takataka.
  e. Kuna ubadhirifu wa mali ya umma: Meya na vibaraka wake wanabadhiri mali ya umma kwa kujilipa kwa vikao visivyo rasmi. Walipokuwa na kikao na madiwani wawili na Bili wanapendekeza kuwa wajilipe kwa kufanya kazi ya ziada yaani 'overtime'. Pia Meya anaonekana kutumia mali ya umma na fedha za baraza kujivinjari na marafiki wake kama Bili. Anazungumzza jinzi walivyojivinjari katika hoteli iitwayo Kajifahari pamoja na familia ya Bili.
  f. Kuna hali mbaya ya umaskini: Umaskini umekita mzizi katika Cheneo kiasi kwamba kuna watu wasioweza kujinunulia chakula. Mamake Dadavuo Kaole anategemea mabakio ya chakula kumlisha

mwanawe. Anasema kuwa mtoto huyo alikula chakula kisichochemshwa kwani hawezi gharamia hata makaa.

g. Kuna hali duni katika mazingira ya kazi: Waridi analalamikia uchafu katika hospitali akisema kwamba nzi walikuwa wanatawala hospitalini.
h. Kuna ukosefu wa huduma muhimu: Hospitali za umma hazina dawa huku viongozi nao wakizidi kutoa ahadi za uongo kwa wananchi wakiwahadaa kwamba dawa hizo zilikuwa zimeagizwa zikiwa bandarini.
i. Kuna unafiki wa kidini: Viongozi wa dini wanatumia dini kujinufaisha. Mhubiri anamwombea Meya aliyekuwa kiongozi dhalimu ili aongoze kwa muda mrefu. Pia anafurahia anapohidiwa kwamba baraza lingelipa sadaka ya shilingi laki moja kila mwezi kando na kugharamia petrol ya kumpeleka kumwombea Meya mara moja kwa juma.
j. Usaliti umekitiri katika jamii hii. Bili anamsaliti Meya kumpotosha kishauri na wakati Meya anashikwa, hajulikani aliko.

1. (i) Tumbo lisilotosheka/matatizo ya tumbo (1 x 2)
   (ii) Tarbia – mishororo mine 1 – Kutaja (2)
   1 – Kueleza
   (iii) Arudhi.
   Mishororo mine kila ubeti
   Vina vya kati ni, nga
   Vipande viwili – ukwapi na utao
   Kibwagizo
   Mizani – ukwapi (8) utao (8) (4 x 1)
   (iv) Lugha nathari
   Wapendanao mapenzi yasiyo na dhati wanakuogopa. Wapatao mimba, watoto wao hawajali.
   Watoto watakapo chakula huwa wanatafuta mapipani. Tumbo nikupe nini ili utosheke? (4 x 1)
   (v) Idhini ya mshairi.
   Inkisari mf. We – wewe nitakupani
   Kuboronga sarufi mf. Wafugaji hata nao – Hata nao wafugaji.
   Tabdila mf. Umewasubua – umewasumbua.
   Mazida mf. Mnukio – mnuko (2 x 1)

   (vi) Kukcsa heshima – hata mbwa wararua.
   Ufisadi – hesabu wanazirenga.
   Kutowajibikia wana – wanachokora mapipa.
   Wizi – wa ng'ombe.
   Mizozo/kutoelewana – mradi waliepe njaa. (4 x 1)

   (vii) Dibaji – Thibitisha/shalali.
   Harara – hasira/hamaki (2 x 1)

2. Vijana kujenga jamii mpya.
   (i) Amani na Imani wanakutana na kuamua kushirikiana licha ya kuwa tofauti.
   (ii) Madhubuti kuungana na tabaka la chini kuleta madbadiliko. Anakangamana na wote na kuhamia kibandani mwa Amani.
   (iii) Amani na madhubuti ambao ni vijana wanahimiza usawa na hivyo kugawia maskini ardhi.
   (iv) Amani na Imani kubadili Imani na mtazamo wa Wanasokomoko kuhusu walemavu/watu wenye mahitaji maalum na kumfanya Majisifu kuenzi wanawe kama binadamu kamili.
   (v) Amani na Madhubuti kusaka haki ya Yusuf na kumtoa gerezani.
   (vi) Amani kukataa kuishi katika nyumba ya Mtemi na kuamua kujenga yake mwenyewe.
   Haja ya bidii.
   (vii) Amani anaamini maridhiano katika jamii baada ya chuki. Anamshawishi Oscar
   Kambona alilipize kisasi kwa kumuua Mtemi. Pia alimsamehe majisifu kwa kumwibia mswada wake.
   (viii) Madhubuti anapendekeza jamii inayo dumisha maadili. Anakataa kazi anayotafutiwa kifisadi na babake.
   (ix) Imani anabadili taasubi ya kiume kwa kusema kuwa wanawake wasiwekwe pembeni katika kitabu atakachoandika.
   (x) Vijana (Amani) kupinga wizi wa miswada.

(xi) Amani analeta mfumo mpya wa kuendesha serikali na kuhimiza wananchi wawachunguze viongozi vizuri, wawapige msasa.
(xii) Amani na Imani wanataka jamii inayomlinda mtoto wanamlea mtoto japo si mtoto wao.
(xiii) Amani anahimiza uongozi usiwe unafumbiwa macho hata unapokuwa dhalimu.
(xiv) Amani na Imani kupiga vita Imani potovu ambazo zimepitiwa na wakati mf. Kutokunywa maji ya mto Kiberenge. Zozote 10 x 2 = 20

3. (a) Yalisemwa na Ben Bella.
- Katika barua.
- Kwa mashaka.
- Kuhusu uhusiano wao na sababu ya kuachana. Zozote 4 x 1 = 04

(b) Yaliyojiri.
- Lowela alikuwa mpenziwe Mtemi Nasaba Bora.
- Kwamba alikuwa amempachika mimba.
- Alipelekwa shambani Baraka kufichwa kule.
- Aliificha mimba kwa kufunga kamba tumboni.
- Alijifungua mtoto.
- Alichukuliwa na Mtemi Nasaba Bora na kumweka mlangoni pa Amani.Zozote 4 x 2 = 9

(c)
- Kuacha masomo akiwa mchanga.
- Kukosa nidhamu kwa kujiingiza katika mapenzi nje ya ndoa.
- Kutupa mtoto – Aliikubali achukuliwe.
- Mtoro – Kutoroka nyumbani hivyo kuwasumbua wazazi.
- Anavunja ndoa ya wenyewe. Zozote 4 x 2 = 8

4.
Ulevi – Maeko.
Uzinzi – Samaki wa nchi za Joto.
Ubaguzi – Damu Nyeusi
Tama – Tazamana na Mauti.
Utelekezaji wa watoto – Mzizi na matawi.
Ujambazi – Gilasi ya mwisho makaburini.
Unyanyavaji safi – Samaki wa nchi za joto.
Uanyaji mamba – Samaki.
Upigaji wa wanawake – Maeko, Mwana wa Dorubini.
Uongozi mbaya – kikaza.

5. (a)
- Maelezo ya mwanadishi.
- Kumhusu Sela.
- Alikuwa ametungwa mimba.
- Alifukuzwa shuleni. Zozote 4 x 1 = 4

(b)
- Sela alikuwa mwanafunzi wa kidato cha tatu.
- Alifukuzwa muhula wa tatu.
- Mwalimu Mkuu wa shule ya Timotheo aliita majina ya wasichana watatu.
- Sela alikaa nyumbani kwa muda wa miezi mitatu.
- Sela alimwita Rozina mara tatu. (4 x 1)

(c)
- Masazu anamlaumu Sela kwa kupata mamba.
- Wasichana waliwacheka waliofukuzwa shuleni.
- Majirani wa Mzee Butali waliwacheka.
- Hata waalimu waliona kama ni mzigo wa wale wasichana wenyewe.
(Aeleze dhana ya kanda la usafi na aihusishe katika jibu lake) Zozote 4 x 2 = 08

(d) Umuhimu wa Sela.
- Kielezi cha wasichana wachanga wanaopata mimba kabla ya ndoa.
- Kielelezo cha jinsi wasichana wanavyodanganywa na kulazimika kuacha masomo.

– Mfano mzuri wa majuto. Zozote 2 x 2 = 04

7. Misimu

(a)

(i) Ni maneno au semi zinazozuka katika kindi fulani la watu na huweza kutoweka au kubaki na kusanifishwa kuwa lugha sanifu.

(ii) Umuhimu wa misimu

1. Kuongeza msamati katika lugha.
2. Watu kujitambulisha na kundi fulani.
3. Kupamba lugha ya wanaohisika.
4. Kuburudisha.
5. Kuhifadhi siri.
6. Hukuza utangamano/uhusiano.
7. Hukuza lugha.
8. Huhifadhi utamanduni.
9. Huendeleze historia.
10. Huondoa urasmi katika mazungumzo.
11. Hutafusdi lugha.

(b) Aina za ngomezi za kisasa.

– Rununu.
– Kengele.
– King'ora.
– Mlio wa ambulensi.
– Kipenga.
– Filimbi.

(c) Sifa za maapizo.

– Hutolewa kwa waendao kinyume na maadili ya jamii.
– Huandamana na viapo mbalimbali.
– Yanaweza kutolewa moja kwa moja na anayeathirika au na mtu mwingine kwa niaba yake.
– Huamini wa yataleta maangamizi katika jamii.
– Hutumia lugha kali ya kuogofya.
– Lugha yake ina ufasaha mwingi/ulumbi.

(d)

– Uvumbuzi wa vyombo vya mawasiliano kama tarakilishi.
– Mitambo ya kuchapisha na kuhifadhi maandishi.
– Dini ya Kikristo ambayo inapuuza baadhi ya vitendo au miviga ya F.S.
– Elimu ya kisasa haitambui wala kuthamini F.S.
– Waandishi wengi wa Kiafrika hawashughuliki F.S.
– Vifo vya fanani.
– Ushindani wa F.S. na burundani ya kisasa.

MTIHANI WA MWIGO – WILAYA YA KAHURO/KIHARU
KIDATO CHA NNE - 2015
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari
102/1
INSHA
KARATASI YA KWANZA
JULAI/AGOSTI 2015

Swali la Lazima.

1. Mwandikie barua pepe rafiki yako anayeishi nchi jirani ili ahudhurie siku ya arusi yako. Barua pepe hiyo iandamane na ratiba ya siku hiyo.
2. Jadili hatua zinazoweza kuchukuliwa kukabiliana na ukabila nchini Kenya.
3. Andika kisa kinachothibitisha ukweli wa methali painamapo ndipo painukapo.
4. Tunga kisa kinachoanza kwa maneno yafuatayo:
   Nilijaribu kuuinua mguu wangu uliojaa maumivu kutokana na jeraha …

MTIHANI WA MWIGO – WILAYA YA KAHURO/KIHARU
KIDATO CHA NNE - 2015
Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari
KISWAHILI
102/2
Karatasi ya 2(LUGHA)
Julai/Agosti 2015

SEHEMU A: UFAHAMU (ALAMA 15)
Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Ni fedheha kuona taifa ambalo halijakuwa likitambua msamiati wa shibe kwa zaidi ya miongo miwili sasa limeacha chakula kiharibike mashambani kutokana na ukosefu wa soko. Taarifa kuwa ni zamu ya wakulima wa mahindi kukadiria hasara baada ya wenzao wa maziwa ni za kuhuzunisha. Inasemekana wakulima wa zao la mahindi katika mikoa ya pwani, mashariki, kati na Bonde la ufa wanendelea kuhesabu hasara kutokana na ukosefu wa soko la mahindi kutoka kwa serikali.

Hii ni hata baada ya serikali kuwapatia na kuwauzia pembejeo kwa bei nafuu kama njia mojawapo ya kuimarisha uzalishaji wa chakula nchini. Kinachovunja moyo zaidi ni habari kuwa serikali iyo hiyo ilitoa ahadi ya kununua mazao yote ya wakulima hao kama njia mojawapo ya kuwatia moyo katika kazi yao.

Kando na wakulima wa kibinafsi, ilitumia mamilioni ya pesa za umma kuzindua miradi ya kilimo cha mahindi kwa kunyunyizia mashamba maji na mazao yake pia yanaharibikia. Wakulima wa mradi wa kilimo cha kunyunyizia mashamba wa Hola, kwa mfano, wameathirika pakubwa kutokana na ukosefu wa soko la mazao yao. Imekuwa ikijikokota kutokana na sababu kadhaa ikiwemo ukosefu wa fedha za kununua mahindi.

Hii ni hata baada ya uchunguzi kuonyesha kuwa usalama wa chakula nchini umedorora kutokana na kiangazi cha muda mrefu. Mbali na kutokuwepo kwa utaratibu wa kununua mahindi kutoka kwa wakulima hao halmashauri ya nafaka haina uwezo wa kuwashughulikia wakulima wote nchini.

Hii ni kwa sababu wakulima wengi hawapati huduma za halmashauri hiyo ambayo imejikita katika maeneo yaliyokuwa yakizalisha chakula kwa wingi miaka iliyopita. Eneo la Hola, kwa mfano, liko mbali kutoka kwa kituo cha halmashauri hiyo kwa sababu eneo hilo ni kame.

Ni kutokana na muktadha huu serikali inapaswa ichukue hatua za haraka kuepusha kuharibika kwa zao la mahindi nchini. Serikali inapaswa kutenga fedha zaidi za kununua mahindi kutoka kwa wakulima. Inakisiwa kuwa hasara zaidi inatarajiwa kutokea ikiwa pesa zaidi hazitatengwa kwa sababu idadi ya wakulima wanaovuna mahindi inatarajiwa kuongezeka.

Maswali

1. (a) Kwa nini chakula kinaharibikia mashambani?
(alama 2)
(b) Serikali ilichangia vipi katika kuimarisha uzalishaji wa chakula?
(alama 2)
(c) Eleza vile halmashari ya nafaka haijaweza kuepushia wakulima wa mahindi hasara.
(alama 1)
(d) Kwa nini wakulima wa maeneo kame hawajashughulikiwa na halmashuri ya nafaka?
(alama 1)
(e) Kutokana na taarifa hii serikali inaweza kutatua tatizo la wakulima kwa njia gani? (alama 1)
(f) Pendekeza namna taifa linaweza kuepuka na kupambana na uharibifu wa chakula mashambani.
(alama 3)
(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika taarifa. (alama 3)
    (i) Miongo
    (ii) Pembejeo
    (iii) Umedorora

SEHEMU YA B: UFUPISHO: (ALAMA 15)
Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata:

Katika safu yangu hii sina lengo la kuzishambulia dini zetu na namuomba Mungu sana asiniandikie dhambi kutokana na ninayotaka kuyaandika. Lakini nashawishika kuikumbusha jamii yangu ambayo inatufanya watu tuzione dini zetu zinamkandamiza mwanamke. Dini zetu kubwa kama Uislamu na Ukristo zinatuelekeza mwanamke kumheshimu mumewe na kumsikiliza anachosema, lakini kwa yeye kufuata maadili ya dini na si kukuambia uue ukakubali.

Wakati dini inasema utekeleze amri ya mumeo na wao wameelezwa mambo ya kuwafanyia wanawake, ikiwa ni pamoja na kuwaheshima na kuwaridhisha kadri ya uwezo wao.

Kutokana na hilo la amri, wanaume wengi ndio wamechukua kama tiketi ya kunyanyasa mwanamke na hata kumnyima fursa ya kujiendeleza kielimu na hata kufanya shughuli za kuongeza kipato. Unakuta familia ni ya kimaskini, baba hana fedha za kutosha kuihudumia familia yake, lakini baba huyo anataka kujishughulisha
na shughuli yoyote ya kumuingizia kipato kinachoweza kuwasaidia wote na matokeo yake kuendelea kuwepo, kwenye dimbwi la umasikini. Wengine kwa hofu ya kupata changamoto kutoka kwa wake zao wanawakatalia wanawake walio wao kujiendeleza kielimu au kutafuta mwanamke asiyeelimika ili asiweze kuhoji mambo kadhaa ndani ya nyumba.

Hili limebainishwa hivi karibuni na shirika moja lisilo la kiserikali huko kigoma ambapo katika utafiti wao asilimia 90% ya wanawake wa vijijini wanashindwa kutoa hoja kutokana na uelewa wao duni na kutoa sababu ya kuwa hiyo ni kutokana na ukosefu wa elimu, masuala ya kidini yanayomwelekeza mwanamke kufuata amri
za mumewe, mila na desturi kadhaa.

Dini zote zinaeleza wazi umuhimu wa mtu kupata elimu bila kubagua kama ya kiislamu inavyosema; mtu anapata thawabu anapotafuta elimu na anatakiwa aitafute popote bila kujali umbali na hata ikiwezekana kufika China ambapo inaaminika ni mbali.
Sijawahi kuona wala kusikia dini ikisema mwanamke asipate elimu lakini baba zangu na kaka zangu wanaume wanalipotosha hili kutaka kuendelea kumkandamiza mwanamke bila kufikiri kuwa mwanamke ni msaada mkubwa kwao na kwa maendeleo ya taifa lote; ikiwa leo tupo katika harakati za kupata maendeleo na nchi hii hivi kweli tutafanikiwa?

Mapambano ya kuleta maendeleo yaanze katika ngazi ya familia kwa kuondoka kwa ujinga wa kumkandamiza mwanamke ili naye aelimike, aweze kujenga hoja, aweze kujitafutia kipato na mwisho kusaidia katika maendeleo ya familia ambayo kwa njia nyingine ndiyo maendeleo yenyewe ya taifa hili.

(a) Fupisha aya tano za kwanza. **(Maneno 70).**
(b) Mwanamke anaweza kuendelezwa vipi. Rejelea aya mbili za mwisho. **(Maneno 50)**.

SEHEMU YA C: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

A Taja aina **mbili** kuu za ala za sauti kisha utoe mfano mmoja mmoja.

(alama 2)

B Taja maneno yenye **miundo** ifuatayo ya silabi.

(alama 2)

(i) KKKI _____

(ii) Irabu pekee (II) _____

C Eleza ni kwa nini neno umma ni la asili ya kigeni. (alama 1)

D Viambishi vilivyopigiwa **mstari** vinawakilisha dhana zipi za kisarufi?

(alama 2)

(i) Udhaifu _____

(ii) Walani? _____

E Neno lifuatalo liko katika ngeli gani? (alama 1)

(i) Matukio _____

F Andika kwa **msemo** wa taarifa:

(alama 2)

Askari: Ulikuwa unaelekea wapi uliposhambuliwa?

Jirani: Nilikuwa nikienda sokoni jana.

G Onyesha **vishazi** katika sentensi ifuatayo kisha **uelezee** ni vya aina gani.

(alama 2)

Ajapo tutamlaki kwa shangwe.

H **Sahihisha** sentensi ifuatayo.

Mtu ambaye aliyechukua kitabu chenye kilikuwa hapa arudishe.

(alama 1)

I Tumia mzizi **–w-** katika sentensi kama:

(alama 2)

(i) Kitenzi kisaidizi.

(ii) Kitenzi Kishirikishi.

J Tunga sentensi moja kubainisha matumizi ya **'na'** kama.

(alama 2)

(i) Kihusishi cha 'na' ya mtenda.

(ii) Kiunganishi

K Weka kirejeshi **'O'** tamati kwenye kitenzi **chunga** kisha ukitungie sentensi. (alama 1)

L Eleza na utoe mifano ya mazingira **mawili** ambapo mistari mshazari hutumika.

(alama 2)

M Nyambua kitenzi ja jiwe katika kauli ya kutendewa kisha **utunga** sentensi. (alama 1)

N (i) Eleza dhana ya shamirisho.

(alama 1)

(ii) Onyesha aina tofauti za **shamirisho** katika sentensi hii.

Ali alimnunulia Asha viatu kwa pesa zake.

(alama 2)

O Tumia kivumishi kionyeshi cha karibu pamoja na nomino katika ngeli ya I-ZI kisha utunge sentensi katika **ukubwa - wingi**. (alama 2)

P Yakinisha sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali **timilifu wingi**. (alama 2)

(i) Msomi hakutuzwa siku hiyo.

Q Eleza **matumizi** ya kwa katika sentensi hii. (alama 3)

(i) Kwa nini umeishi kwao kwa miaka mingi?

R Eleza maana **tatu** zinazopatikana katika sentensi hii.

(alama 3)

(i) Alikuwa amenijuza kuwa angefika kwao.

S Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya **mishale**. (alama 4)

(i) Kuku na mbuzi ni mifugo.

T Eleza maana ya nomino. (alama 1)

SEHEMU YA D: ISIMU JAMII: (ALAMA 10)

(a) Ali: Wee kuja hapa. Wewe ni nani? Sema haraka!

Ebo: Mimi … ni … afande ni Ebo

Ali: Unatoka wapi sa ii? Hapa hakuna sheria?

Ebo: Samahani mkubwa. Mimi niku…

Ali: Mkubwa wa nani? Wakubwa wako ofisini.

Ebo: Pole mzee.
Ali: Mzee gani? Hii mtu lazima niiwekwa store. Yaani self-contained.
Toa viatu.
Ebo: Tafadhali Bwana Askari, nilichelewa …
Ali: Mimi sitaki hadithi! Hizo pelekea nyanya yako, eh. Fanya haraka!
Ebo: Naomba mkubwa …
Ali: Hapa si kanisani. Unaomba! Hata …

Fafanua sifa tano za sajili hii. (alama 5)

(b) Eleza maana ya istilahi zifuatazo za isimu jamii.
(alama 5)
(i) Lugha ya taifa.
(ii) Lugha ya ishara
(iii) Lugha mwiko
(iv) Sajili za lugha
(v) Uchanganyaji msimbo.

MTIHANI WA MWIGO – WILAYA YA KAHURO/KIHARU
KIDATO CHA NNE - 2015
Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari
102/3
KISWAHILI
KARATASI YA TATU (FASIHI)
JULAI/AGOSTI, 2015

SEHEMU A: USHIAIRI
SWALI LA LAZIMA

1. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo.

LONGA
Longa Longea afwaji, watabusarika,
Longa uwape noleji, watanusurika,
Longa nenea mabubu, sema na viduko.

Longa usichachawizwe, tamka maneno,
Longa usitatanizwe, mbwa aso meno,
Longa usidakihizwe, kishindo cha funo.

Longa yote si uasi, si tenge si noma,
Longa pasi wasiwasi, ongea kalima,
Longa ukuli kwa kasi, likate mtima,
Longa zungumza basi, liume ja uma.

Longa japo ni kombora, kwa waheshimiwa,
Longa liume wakora, kwani wezi miwa,
Longa bangu na papara, hawakuitiwa,
Longa bunge si kiwara, si medani tawa,
Longa ni simbamarara, wanaturaruwa.

Maswali
(a) Tambua nafsineni katika nudhumu hii.
(alama 1)
(b) Onyesha vile kibali cha utunzi wa mashairi kilivyotumiwa kukidhi mahitaji ya kiarudhi.

(alama 3)

(c) Kwa kutoa maelezo mwafaka, tambua bahari **nne** zilizotumiwa na mtunzi kwenye shairi hili.
(alama 8)

(d) Onyesha vile shaha alivyofua dafu kutumia mbinu zifuatazo.
(alama 5)
(i) Anafora
(ii) Usambamba wa kiusawe.
(iii) Usambamba wa kifahiwa/dhamira.
(iv) Tabaini.
(v) Jazanda

(e) Tambua toni ya shairi hili. (alama 1)

(f) Neno kasi ni adhidadi. (alama 1)

(g) Neno afwaji limetumika kumaanisha nini katika shairi hili. (alama 1)

SEHEMU B: MSTAHIKI MEYA

2. "Mimi na Meya ni mfano wa mafuta na maji. Hatuonani uso kwa uso."
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili.
(alama 4)
(b) Ni mbinu gani ya lugha iliyotumika katika dondoo na inamaanisha nini?
(alama 2)
(c) Kwa kurejelea tamthilia nzima, thibitisha kuwa Meya ni sawa na mafuta na wengine ni maji.
(alama 14)

AU

3. Thibitisha ukweli wa msemo kuwa sikio la kufa halisikii dawa kwa mujibu wa Tamthilia ya Mstahiki Meya

(alama 20)

SEHEMU C: DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE
KANDA LA USUFI

4. "Wanafunzi hao wawili waliandamana hadi ilipokuwa kliniki ya shule."
(a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
(b) Kwa kurejelea hadithi kanda la usufi thibitisha kuwa sekta ya elimu inakabiliwa na changamoto myingi. (alama 10)
(c) Wanafunzi wanaorejelewa walikuwa wamekutana kisadfa.
Toa mifano mingine **mitatu** ya sadfa kutoka kwenye hadithi hii.
(alama 6)

AU

5. **MIZIZI NA MATAWI**
Thibitisha kuwa majina Sudi na Kudura ni ya kimajazi. (alama 20)

SEHEMU YA D: KIDAGAA KIMEMWOZEA

6. Mwandishi wa Kidagaa Kimemwozea amenuia kujenga jamii mpya.
Tetea kauli hii. (alama 20)

AU

7. "Hatimaye Tarishi alikuja na barua moja ya Mtemi na nakala ya siku hiyo ya gazeti la Tomoko Leo: Mtemi Nasaba Bora akapokea barua hiyo na gazeti toka kwa tarishi aliyekuwa kanywea si haba."

(a) Jadili mambo yaliyomshtua Mtemi Nasaba Bora kuhusiana na barua na gazeti alizopokea siku hiyo.

(alama 10)

(b) Onyesha jinsi madhubuti alivyoendeleza uasi dhidi ya babake.
(alama 10)

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

8. (a) Maigizo ni nini? (alama 2)
(b) Fafanua sifa zozote **tano** za maigizo. (alama 10)

(c) Eleza dhima ya michezo ya watoto. (alama 8)

MTIHANI WA MWIGO - WILAYA YA KAHURO/KIHARU 2015
102/1
KISWAHILI KARATASI YA 1
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

1. Sura ya barua pepe izingatie:
   Kutoka:
   Kwa:
   Nakala kwa:
   Kuhusu/mada
   Salamu
   Mwili
   Jina la mwandishi

   Ratiba
- Kichwa kiwe kamili yaani kiwe na neno ratiba, inahusu nini, tarehe na mahali pa tukio.
- Iwe na safu mbili: Moja ya saa na nyingine ya matukio.
- Saa iandikwe kwa majira; mfano saa 8.00 asubuhi (mfumo wa kimataifa).
- Yaweza kuwa na jina la mtayarishi.

2. Kukabili ukabila.
- Kazi zitolewe kwa wote bila ubaguzi.
- Watu wakubaliwe kuishi popote.
- Watu wafanyie kazi maeneo tofauti tofauti.
- Ndoa baina ya makabila zihimizwe.
- Viongozi wakome kuchochea makabila yao dhidi ya mengine.
- Wakati wa uchaguzi, viongozi watoke makabila yote.
- Michezo mbalimbali ihimizwe katika maeneo mbalimbali.
- Katiba ya nchi ifuatwe. (Kadiria hoja nyingine)

3. Mtahiniwa atunge kisa kinachothibitisha ukweli wa methali.
   Mtu aliyekuwa wa hali duni anaweza kuimarika na kuwa mtu wa hadhi au wa kuheshimika.
4. Kisa kionyeshe alivyopata jeraha (atumie mbinu rejeshi) na akiendeleze kisa bila kuongeza maneno kwenye kianzio au kuongeza maneno.

   Onyesha makosa ifuatavyo:
   Sarufi =
   Hijai -
   Msamiati mzuri
   Msamiati usiofaa X
   Neno ambalo halipo ^

   Urefu (Usituze zaidi ya alama zilizoonyeshwa)

   Robo $\frac{xx}{05}$

   Nusu $\frac{xx}{05}$

   Robo tatu $\frac{xx}{15}$

   Kamili $\frac{xx}{20}$

MTIHANI WA MWIGO – WILAYA YA KAHURO/KIHARU 2015
102/2
KISWAHILI KARATASI YA 2
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

SEHEMU A: UFAHAMU

1. (a)
– Ukosefu wa soko la mahindi.
– Wingi wa chakula kutokana na wakulima kutiwa moyo. (2 x 1)

(b)
– Kuwapatia na kuwauzia wakulima pembejeo kwa bei nafuu.
– Serikali kutoa ahadi ya kununua mazao ya wakulima.
– Kuzindua miradi ya kilimo cha mahindi kwa kunyunyizia mashamba maji. (2 x 1)

(c)
– Kukosa utaratibu wa kununua mazao
– Kukosa uwezo wa kuwanunulia wakulima wote mahindi.
– Umbali kutoka kwa mahali chakula kinakuzwa. (3 x 1)

(d)
– Ukosefu wa fedha na kuwa mbali kimasafa.
– Imepiga kambi maeneno yanazalisha nafaka tangu jadi. (1 x 1)

(e) Kutenga fedha nyingi za kununua mahindi kutoka kwa wakulima wengi. (1 x 1)

(f)
– Kununua mazao kwa kutenga fedha.
– Kujenga maghala mengi. (2 x 1½ = 3)

(g) (i) Miongo – Kipindi cha miaka kumi – kumi.
(ii) Pembejeo – Mahitaji muhimu katika kilimo k.m mbegu. Mbolea.
(iii) Umedorora – Enda chini, zorota, haribika. (alama 3)

SEHEMU B: UFUPISHO

2.(a)
(a) Sina lengo la kuzishambulia dini zetu na namuomba mungu asiniandikie dhambi.
(b) Dini za uislamu na ukristo zinatuelekeza mwanamke kumheshimu mumewe na kumsikiliza anachosema.
(c) Dini imewapa wanawake jukumu la kufuata amri ya mumeo.
(d) Wanaume wengi wamechukua amri hii kunyanyasa na kuwanyima fursa ya elimu na hofu ya kupata kipato.
(e) 90% ya wanawake hawatoi hoja kwa sababu wao wameiamini kuwa dini.
(f) Wanaume huwa na hofu ya kupata changamoto kutoka kwa wake waliojiendeleza kielimu.
(g) Dini zinaeleza umuhimu wa mtu kupata elimu bila kubagua.
(Hoja – 6, Mtiririko 2, Jumla alama 8)

(b)
– Kwa kupata elimu.
– Asikandamizwe kwa vyovyote.
– Tutambue umuhimu wa mwanamke katika ujenzi wa taifa.
– Atafute kipato cha familia.
– Aweze kutoa maoni ya ujenzi wa nchi.
– Imani potovu za kidini zitupiliwe mbali. (Mtiririko – 1 (alama 6)

3. **Sarufi na matumizi ya lugha** (alama 40)

A (i) Ala tuli – meno, kaakaa gumu, ufizi, koromeo n.k.
(ii) Ala sogezi – midomo, ulimi. (4 x ½ = 2)

B (i) KKKI – Mbwembwe, nywa
(ii) I I – Oa, ua (2 x 1 = 2)

C Umma – Lina muundo wa konsonanti mbili zinazofanana zikifuatana. (1 x 1)

D (i) Udhaifu – Unominishaji/Ngeli
(ii) Walani? – Swali/Kiulizi (2 x 1)

E Ngeli ya Li – Ya (1 x 1)

F Askari alimuuliza jirani alikuwa akielekea wapi aposhambuliwa naye jirani akamjibu kuwa alikuwa akienda sokoni siku hiyo jioni (4 x ½ = 2)

G Ajapo – Kishazi tegemezi, tutamlaki kwa shangwe – Kishazi huru. (2 x 1)

H Mtu aliyechukua kitabu kilichokuwa hapa arudishe au mtu ambaye alichukua kitabu kilichokuwa hapa arudishe. (1 x 1)

I (i) Kitenzi kisaidizi – Amekuwa akicheza mpria.
(ii) Kitenzi kishirikishi – Ali amekuwa mwizi. (2 x 1)

J Shamba la Bw. Komu lililimwa (1) Hassani, Ali (2) Hamisi.
(i) Kihusishi cha 'na' ya mtenda – na Hassan
(ii) Kiunganishi cha kuongeza – Ali na Hamisi

K (i) Achungaye, wachungwao, kichungwacho n.k (1 x 1)
(Sentensi iwe sahihi)

L (i) Tunapoandika kumbukumbu 2/2015:
(ii) Maneno yenye maana sawa: Paka/nyau, mamba/ngwena.
(iii) Tunapoandika tarehe 10/10/2016.
(iv) Au/ama: Kisu/Kijiko. (3 x 1)

M Ja – jiwa. Alijiwa na askari jana. (1 x 1)

N (i) Ni nomino inayoathiriwa na kitenzi (mtendwa, mtendewa) (1 x 1 = 1)
(ii) Asha – Kitondo
Viatu – Kipozi
Pesa – ala Zozote (2 x 1 = 2)

O Madege hayo yalitua hapa jana. (2 x 1 = 2)
P Wasomi watakuwa wakituzwa siku hizo. (2 x 1 = 2)

Q Kwa – Kiulizi
Kwao – Umiliki wa mahali
Kwa – Muda/Kipindi

R (i) Yeye mwenyewe alikuwa amenifahamisha kuwa angefika kwa watu wengine.
(ii) Yeye mwenyewe alikuwa amenijuza angefika kwao yaani nyumbani anamotoka yeye.
(iii) Mtu mwingine angefika kwa aliyenijuza.

S S → KN + KT ½
KN → N + U + N ½
N → Kuku ½
U → na ½
N → mbuzi ½
KT → t + N ½
t → ni ½
N → Mifugo ½

T Nomino ni neno linalotaja watu, vitu, viumbe mimea, dhana na mahali. (1 x 1 = 1)

SEHEMU C: ISIMU JAMII

4. (a)
- Lugha yenye ukali kw. Polisi.
- Lugha ya kudhadisi/maswali ni majibu.
- Kuchanganya ndimi.

- Lugha isiyozingatia kanuni za kisarufi.
- Lugha ya unyenyekevu kwa mshukiwa.
- Lugha ya kuamrisha.
- Lugha inayoeleweka kwa urahisi
- Lugha ya misimu.

(5 x 1 = 5)

(b) Eleza maana ya istillahi zifuatazo za isimu jamii.

- Lugha ya taifa – Ni lugha iliyotenliwa kama kitambulisho na ustaarabu wa taifa zima.
- Lugha ishara – Ni lugha inayotumia ishara kama mikono, uso ni macho katika kuwasiliana.
- Lugha mwiko – Lugha inayomfunga mtu kuitumia kwa mujibu wa jamii yake.
- Sajili za lugha – Mitindo mbalimbali ya matumizi ya ile lugha moja.
- Uchanganyaji msimbo – Ni hali ambapo wazungumzaji wa lugha wanazungumza katika
- lugha moja kisha hapa na pale wanatoka kidogo katika lugha hiyo na kuingilia lugha ya pili au ya tatu kwa muda mfupi na kisha kurejelea lugha ya awali.

MTIHANI WA MWIGO-WILAYA YA KAHURO/KIHARU 2015
102/3
KISWAHILI KARATASI YA 3
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

1. **MAJIBU YA SHAIRI**

(a) Nafsineni ni mwananchi/raia/mzalendo/mtetezi wa haki za binadamu/za wanyonge.
(b) (i) Tabdila – Kuleta urari wa vina mfano: usitatanizwe, wanaturararuwa.
(ii) Inkisari – Kuleta urari mizani mfano: aso.
(iii) Utohozi – Hi kuleta urari wa vina na mizani mfano: noleji.
(c) (i) Sakarani – Shairi ni mseto wa bahari kadha mfano tathmina, utatu, ukaraguni n.k.
(ii) Kikwamba neno longa linaanzia na kurudiwa kila ubeti.
(iii) Ukaraguni – Vina vya ukwapi na utao vinabadilika kila ubeti.
(iv) Mathnawi – Shairi limegawika vipande viwili kila mshororo.
(v) Kikai – Mizani katika utao ni michache (6) ilhali. Mizani ya ukwapi ni mingi (8).
(vi) Sabilia – Halina pambio bali lina kituo.
(d) (i) Anafora – huu ni urudiaji/uradidi neno longa imerudiwarudiwa.
(ii) Usambamba wa kiusawe – neno longa lina maana sawa na nena, sema, zungumza, ongea, kuli, tamka na ambayo yametumiwa kwenye shairi.
(iii) Usambamba wa kifahiwa/dhamira – mtunzi anadhamiria kusisitiza haja ya kuwaumbua na kuwasuta wabunge walafi na wenye kuzua balaa.
(iv) Tabaini - Si uasi si tenge si noma.
- Si kiwara si medani
(v) Jazanda – Mabubu – Wenye kujitia hamnazo
- Kishindo cha funo – tishio hafifu/tishio la nyamarero
(e) Toni – ghadhabu/hasira
(f) Adhidadi – pole/taratibu
(g) Afwaji – kaumu/halaiki/umati wa watu

2. **MSTAHIKI MEYA**

(a) Maneno ya Siki akimwambia Diwani III Nyumbani kwa Meya wakiwa wamestarehe barazani. Siku alikuwa ameenda kumtembelea kumwomba amshawishi Meya aboreshe hali ya maisha hasa kwa kuboresha hospitali (kuleta dawa). (1 x 4)
(b) ***JAZANDA*** (1 x 1)
Maana: Ingawa wote wawili ni binamu, huwasikilizani wala kushirikiana (1 x 1)

(c)
- Anaishi maisha ya kifahazi raia wakikosa mahitaji ya kimsingi k.m. Chukula, dawa n.k.
- Alijilimbikizia mali huko raia wakiteseka.
- Hawajibiki kazini/hajali kuhusu utenda kazi.
- Ana kiburi. Hataki kuitwa kwa jina na Siki.
- Anadharau na kupuuza wawkilishi wa wafanyikazi kwa kuwaambia wanampotezea wakati.
- Anapuuza ushauri wa Siki na Diwani III na kusikiza wa Bili, Diwani I na Diwani II.
- Hashughulikii malalamishi ya wafanyikazi.
- Ni fisadi: Aunga mkono wizi wa fimbo ya Meya na kuiuza ili wafaidike peke yao.
- Anatumia udikteta kuidhinisha baadhi ya maamuzi ya kujinufaisha pamoja na marafikize.
- Atumia askari kunyamazisha wanaogoma.
- Amlipa mhubiri ili amwombee yeye na baraza. Maombi hayawajali wengine.
- Kutumia Mayors Act dhidi yaw engine.

(Hakiki hoja zingine zinazo – 7 x 2 = 14 onyesha Meya yu na mamlaka zaidi).

3. Thibitisha ukweli wa msemo kuwa sikio la kufa halisikii dawa kwa mujibu wa tamthilia ya Mstahiki Meya.
(i) Meya alikataa kusikiliza ushauri wa Siki kuwa watu waliomchagua wanamlilia awatatulie matatizo yaliyowakabili hasa kwa kuwaongezea mshahara.
(ii) Siki alimsihi Meya anyooshe mengi yasiyonyooka ili watu wasilipuke lakini Meya hakumsikia; aliendelea na maovu na mapuuza yake.

(iii) Siki alimwambia Meya kuwa kuna watu wanaokufa kwa ukosefu wa dawa na njaa lakini Meya alimpuuza na kusema kuwa Baraza analoongoza ni dhabiti kuliko mengine jirani.

(iv) Meya anapoamrisha nyimbo za kizalendo ziimbwe kabla na baada ya vipindi marufu ili kuamsha uzalendo, Siki anamshauri kuwa nyimbo hazitawashibisha na kukata kiu ya uhitaji wa watu lakini Meya hakulitilia maanani.

(v) Siki anapomtahadharisha kuwa kulipisha watu matibabu hospitalini kunapinga mpango wa afya bora nay a bure Meya anasema malengo yale ni upuuzi.

(vi) Siki pia alimtahadharisha Meya hatari ya kufuata maamuzi ya mataifa fadhili bila kushirikisha
watu wao kwani huo ni ukoloni mamboleo. Badala ya kusikiliza ushauri huu Meya anamwita mlinzi wake amfukuze pale.

(vii) Diwani III alimwonyesha Meya hatari ya kuongezea madiwani mshahara na kuwaacha wafanyakazi wengine lakini akapuuza.

(viii) Meya pia anapuuza ushauri wa Diwani III kuwashughulikia wafanyakazi ili kuepuka tisho la mgomo. Anaonelea kuwa watalazimishwa na mahitaji ya kila siku kusitisha mgomo na kurudi kazini.

(ix) Meya pia anapuuza ushauri wa Diwani III kuwadhamini wafanyakazi kwani wanawahitaji, badala
yake anasema hata wakigoma wataajiri wengine.

(x) Meya anapuuza ushauri wa Diwani III kuwa kuchukua mikopo kwa wafadhili kungewaachia vizazi vijavyo mzigo wa kufidia. Meya haoni haja ya kujali ya badaye.

(xi) Kwa muda Meya anaepuka kuzungumza na wafanyakazi kuhusiana na hali yao ili kuzima mgomo
kwa kuamini kuwa uhitaji ungewafanya warudi kazini.

(xii) Anapokubali kuongea na viongozi wa wafanyakazi haonekani kutilia maanani mazuungumzo yao
na kwa hivyo wanamwacha.

(xiii) Mapuuza haya yanasababisha mgomo mkubwa wa wafanyakazi uliosababisha wageni aliotarajia kutoweza kuhudhuria mkutano.

(xiv) Yeye na madiwani wake waaminifu wanakamatwa na polisi na kupelekwa katika Makao Makuu kueleza hali ya mambo.

(xv) Hatimaye alitambua kuwa baadhi ya madiwani waliojifanya waaminifu walimdanganya.

(xvi) Anajuta na kusema ni heri angemsikiliza Diwani III (Bwana Uchumi na Kazi) kwa kutambua kuwa ingawa hakupenda maoni yake anaona yalikuwa ya kweli. Zozote 10 x 2 = 20

4. **KANDA LA USUFI**

(a) Maneno haya ni ya msimulizi.
Arejelea Sela na Masazu wakati Sela alijitolea kumsaidia.
Masazu aliyejifanya mgonjwa ikiwa mbinu ya kumnasa.
Ni katika shule ya Askofu Timotheo ambako wanafunzi kutoka shule mbalimbali walikuwa wameenda kwa
mashindano ya muziki. (4 x 1 = 4)

(b)
- Wasichana wa Askofu Timotheo kupata mimba na kufukuzwa.
- Baadhi ya wanafunzi k.m. Masazu hutoka shuleni mwao kwenda za wasichana sio kwa sababu za tamasha bali kupata wachumba.
- Wasichana wajawazito hukosa makini darasani.
- Wavulana nao hukosa kutia bidii kwa sababu ya mawazo k.m. Masazu alikosa kupita vizuri.
- Wanafunzi kutumia muda mwingi kuandikiana barua za mapenzi badala ya kusoma. (5 x 2 =10)

(c)
- Sela na Masazu kufika kwenye kliniki na kukutana na Sista akitoka wakakutania mlangoni.
- Sista 'aliyemsaidia' Masazu ndiye bado alimpima Sela mjamzito alikuja kufukuzwa shule.
- Kutumbukia kwa Sela majini na hivyo kutomfikisha nyumbani mtoto waliyemjia.
- Mvua kubwa kunyesha usiku wa kumtorosha Kadogo. (3 x 2 = 6)

5. **MAJAZI**

Sudi – maana yake ni bahati njema.
Sudi alikuwa na bahati kuokotwa na Bi. Mkubwa pipani kabla hajakata roho.

Sudi alikuwa na bahati ya kulelewa na Bi. Mkubwa vizuri.
Sudi alikuwa na bahati ya kuelimishwa.
Sudi alikuwa na bahati ya kupata kazi nzuri.
Sudi alikuwa na bahati ya kurithishwa nyumba.
Sudi alikuwa na bahati ya kumpata mamake mzazi bila kumtafuta. (7 x 2 = 14)
Kudura – Maana yake ni nguvu za Mwenyezi Mungu.
Ni kudura mama mzazi wa Sudi kupata kazi.
Ni kudura kuwa anayemwajiri kazi ni mwanawe.
Ni kudura kupata mwanawe aliyemtupa pipani zamani. (3 x 2 = 6)

6.

- Jamii mpya ambayo haitakuwa na unyanyasaji k.v. kunyang'anya wanyonge mali yao/mashamba yao kama alivyofanya Mtemi Nasaba Bora kwa familia za Amani na Imani.
- Jamii mpya ambayo haitakuwa na ufisadi k.v. Mtemi Nasaba Bora alivyohonga wakuu serikalini ili mwanawe madhubuti aajiriwe katika jeshi.
- Jamii inayotekeleza haki siyo yenye kufunga jela watu wasio na hatia kama alivyofungwa Yusufu ami yake Amani kupitia mipango ya Mtemi.
- Jamii isiyotekeleza mauaji kwa watu wasio na hatia kama alivyouawa Chichiri Hamadi babaye Amani kupitia njama iliyohusisha Mtemi.
- Jamii isiyo na ukatili k.v. Mtemi Nasaba Bora alivyotupa kitoto chake kichanga mlangoni pa Amani. Alivyompiga Amani nusura amuue, alivyokataa kushughulikia matibabu ya Bob D. J baada yakung'atwa na mbwa wake n.k.
- Jamii yenye viongozi waliowajibika na kutumika wananchi sio kujifaidi na kuwakandamiza kama alivyokuwa Mtemi Nasaba Bora.
- Jamii inayotambua na kuauni mashujaa wa zamani k.v. Mzee Matuko Weye alivyopigana vita vikuu vya dunia na Chwechwe Makweche aliyechezea Tomoko soka ya kimataifa.
- Jamii isiyopuuza walemavu Mwalimu Majisifu hakuthamini watoto wake wane walemavu lakini Imani alimfanya abadilike.
- Jamii isiyo na uzinifu na yenye ndoa zilizo na uaminifu. Nasaba Bora alitembea na wasichana wadogo kama Lowela Maozi.
- Jamii yenye vijana wanaoweza kungoja hadi waoane kabla ya kushiriki mapenzi kama wanavyofanya Amani ns Imani.
- Jamii yenye waandishi wanaochapishiwa miswada yao ikiwa mizuri sio inayoibwa na kutumika na wengine.
- Jamii yenye watu ambao hawataendelea kunyamaza wakinyanyaswa lakini watajikombokoa kwa kufanya mapinduzi k.v. Amani na Madhubuti.
- Jamii yenye kujali masilahi ya wengine na kugawa rasilimali zilizopo kwa maskini kama alivyofanya Amani kwa Matuko Weye, Bob D.J na wengine.
- Jamii yenye msamaha na isiyo na kisasi. Amani alikuwa na nafasi amdhuru Mtemi Nasaba Bora lakini akaamua alipe ubaya kwa wema.
- Jamii yenye huduma bora za kimsingi kwa wananchi k.m afya sio kama vile Zahanati ya Nasaba Bora ilivyokuwa. Zozote 10 x 2 = 20

7. (a) Jadili mambo yaliyomshitua Mtemi Nasaba Bora kuhusiana na barua na gazeti alizozipokea siku hiyo.

- Hakuona picha yake katika gazeti la Tomoko Leo kama ilivyokuwa wakati nduguye Mwalimu Majisifu alikuwa mhariri wa gazeti hilo licha ya kutoelewana kwao.
- Katika barua aliyopokea mtoto wake madhubuti aliyekuwa masomoni. Urusi alimwarifu juu ya kurejea kwake nyumbani na angetaka mpango wa kumtafutia ajira jeshini au popote uisitishwe, kwa sababu hataki ajira inayotokana na mlungula.
- Madhubuti pia alisema kuwa alitaka kusimama kwa miguu yake mwenyewe apate au akose kwa kustahiki au kushtahili kwa sababu ya jadi yake.
- Madhubuti alimwambia babake alikuwa amechoka na ingawa alimpenda kulikuwa na vitendo vyake ambavyo hakuwa akivipenda.
- Mtemi Nasaba Bora alipomaliza kusoma barua alikasirika na kugonga meza kwa kuona kuwa madhubuti hajui dunia inavyozanguka.
- Pia alikasirika kwa kuona Madhubuti alivyokuwa amejitambulisha na mamake(Madhubuti Zuhura) badala ya kujitambulisha naye kama baba yake. (5 x 2 = 10)

(b) **Onyesha jinsi Madhubuti alivyoendeleza uasi dhidi ya babake**.

- Katika barua aliyomwandikia babake alipokaribia kurudi nyumbani alitaka mipango ya kutafutiwa kazi jeshini au popote isitishwe kwa sababu hukutaka kazi iliyotokana na mlungula.
- Madhubuti alimwambia babake kuwa ingawa alimpenda kulikuwa na vitendo vyake ambavyo hakupenda.
- Madhubuti alimaliza barua yake kwa kujiita Madhubuti Zuhura badala ya kujitambulisha na babake.
- Alipendana na kushirikana na mfanyikazi wao Amani kwa sababu mitazamo yao ilishabihiana. Hatimaye alihamia kibandani alimokaa Amani.
- Madhubuti alichukia vitendo vya babake vya kupoka, kupiga pute, kulimbikiza mali haramu na kuhalalisha haramu kwa sababu vilifanya bara la Afrika kuchekwa katika kila pembe ya dunia.
- Alimwomba Amani ashirikiane naye katika kuwazidua watu kwa lengo la kukomesha udhalimu kuanzia pale kwao wanapofanyiwa udhalimu na baba yake.
- Madhubuti alifuata kwa kukubali babake ampeleke masomoni ng'ambo kwa pesa alizowaitisha watu kwa nguvu ingawa alikuwa amefaulu kuingia katika Chuo Kikuu pale nyumbani kwao.
- Anahiari kujiua kinasaba ili azaliwe upya na asiwe na uhusiano wowote na Nasaba ya Mtemi Nasaba Bora.
- Madhubuti alikubaliana na Amani waongoze mapinduzi kwa tahadhari wasije wakatoa viongozi dhalimu na kuingiza mwingine dhalimu zaidi.
- Madhubuti alipopata ajira mjini Songoa alianza kuchunguza jinsi babake alivyopata kumiliki mashamba mengi makubwa. (5 x 2 = 10)

8.

(a)
- Maigizo ni sanaa ya mazungumzo yanayoambatana na matendo.
- Ni hali ambapo watendaji hutenda na huiga matendo ya watu au viumbe katika jamii. (1 x 2 = 2)

(b)
- Hutolewa au huigizwa mbele ya hadhira.
- Uigizaji huhitaji uwanja maalum wa kutendea au mandhari.
- Hufangamana na shughuli za kijamii kama vile utambaji wa hadithi na sherehe.
- Sharti kuwe na tendo la kuigizwa.
- Waigizaji huvaa maleba yanayooana na hali wanazoigiza.
- Maigizo huiga hali ya maisha ya jamii kisiasa, kiuchumi na kitamaduni kwa nia ya kuonyesha mafanikio, udhaifu na migogoro katika nyanja za maisha.
- Huwa na muundo mahsusi wa mtiririko wa matukio.
- Yanaweza kuambatana na ngoma pamoja na uimbaji wa nyimbo au ukariri wa tungo za kishairi.
- Hutumia lugha yenye ufundi mkubwa.
- Wakati mwingine hutumia ishara. Zozote (5 x 2 = 10)

(c) **Dhima ya michezo ya watoto**.
- Hukuza kipawa cha uigizaji miongoni mwa watoto.
- Hukuza ubunifu.
- Ni nyenzo ya kukashifu matendo hasi ya watu wazima.
- Hutambulisha na kusawiri falsafa ya jamii kuhusu malezi na majukumu ya wanajamii.
- Huwapa watoto ukakamavu na kuwawezesha kujiamini wakiwa wangali wachanga.
- Hukuza utangamano/ushirikiano/umoja.
- Huimarisha uwezo wa kukumbuka.
- Huwawezesha kupata mikakati au maarifa ya kukabiliana na hali mbalimbali katika maisha.
- Huburudisha.
- Huendeleze utamaduni wa jamii husika.
- Huhifadhi historia ya jamii husika. n.k. Zozote (4 x 2 = 8)

MTIHANI WA PAMOJA WA WILAYA YA KIRINYAGA YA KATI - 2015
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari
102/1
KISWAHILI
INSHA
KARATASI YA KWANZA
JULAI/AGOSTI 2015

1. **LAZIMA**.
   Kumekuwa na visa vingi vya ukosefu wa usalama nchini. Wewe kama katibu wa jopo lililoteuliwa na Waziri wa Usalama nchini, andika ripoti kuhusu suala hili.
2. Teknolojia ya kisasa imechangia kudhurika kwa maadili ya vijana wetu. Jadili.
3. Tunga kisa kinachooana na methali ifuatayo.
   "Wema hufa mwili, hawafi jina."
4. Andika insha itakayoishia kwa
   … Ilinichukua muda mrefu kuyaamini niliyoyaona!

MTIHANI WA PAMOJA WA WILAYA YA KIRINYAGA YA KATI - 2015
Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari
102/2
KISWAHILI
Karatasi ya pili
(LUGHA)
Julai/Agosti 2015

SEHEMU YA A: UFAHAMU (ALAMA 15)
Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Ulimwengu unapaswa kuzuka na mbinu za kulitadarukia tatizo ambalo linakwamiza juhudi za maendeleo. Umaskini unaoyakabili mataifa yanayoendelea, unayatosa kwenye dhiki kubwa huku mataifa ya kimagharibi yakipiga hatua kubwa kimaendeleo. Ufa uliopo baina ya mataifa yanayoendelea na yale yaliyoendelea kama vile Marekani, nchi za Ulaya na Ujapani unapanuka kila uchao.

Vyanzo vya umasikini huu ni anuwai mathalan, ufisadi uongozi mbaya, turathi za kikoloni, uchumi kuegemezwa kwenye kilimo kinachotegemea mvua isiyotabirika, idadi ya watu inayoupiku uwezo wa uchumi wa taifa linalohusika na ukosefu wa nyenzo na amali za kuwakwamua raia kutoka lindi la umaskini. Ukosefu wa elimu na nafasi adimu za ajira huchangia pia katika tatizo hili.

Jamii ya ulimwengu inapaswa kuelewa kuwa umaskini, unaothiri nchi fulani una athari pana sana. Uvunjifu unaotokana na umaskini unaweza kuwa mboji ambako matendo mabaya huchipuka. Raia maskini huweza kushawishiwa haraka kujitosa kwenye matendo ya kihalifu ili kujinasua kutoka dhiki ile. Hii inaweza kuwa mbegu ya kuatika maovu kama ugaidi na uhalifu wa kila aina.

Mataifa ya magharibi yanapaswa kuyaburia madeni ya mataifa yanayoendelea kama njia mojawapo ya kupambana na umaskini. Asilimia kubwa ya pato la kitaifa katika mataifa mengi hutumika kuyalipa madeni hayo. Katika hali hii inakuwa muhali kwa mataifa hayo kujikwamua kutokana na pingu za umasikini. Njia nyingine ni kustahabu kutoa ruzuku za kimaendeleo badala ya mikopo kwa nchi zinazoendelea.

Kwa upande wake, mataifa yanayoendelea yanapaswa kuibuka na mikakati bora ya kupambana na umaskini. Ni muhimu pawepo na sera zinazotambua ukweli kuwa asilimia kubwa ya raia wa mataifa hayo ni maskini. Pana dharura ya kuzalisha nafasi za ajira, kupanua viwanda hususan vinavyohusiana na zaraa ambayo ni tagemeo kuu la mataifa mengi, kuendeleza elimu na kuimarisha miundo msingi. Ipo haja pia ya mataifa haya kuhakikisha kuwa mfumo wa soko huru unaotawala ulimwengu sasa hauishii kuwa chanzo cha kufa kwa viwanda asilia na kuendeleza umaskini zaidi. Kwa ufupi, maamuzi yote ya sera za kiuchumi lazima yauzingatie uhalisi wa maisha ya raia wa mataifa hayo.

Maswali:
(a) Kwa nini umaskini umetamalaki katika mataifa yanayoendelea?
(alama 4)
(b) Madeni yana athari gani kwa mataifa yanayoendelea?
(alama 2)
(c) Ni mapendekezo yapi ambayo mwandishi anatoa kwa mataifa machanga kuhusu utatuzi wa tatizo la
umaskini? (alama 4)
(d) Mfumo wa soko huru una madhara gani kwa mataifa machanga?
(alama 2)
(e) Ukirejelea kifungu, eleza maana ya: (alama 3)
(i) Kulitadarukia.
(ii) Kuatika.
(iii) Kuyaburia madeni.

SEHEMU YA B: UFUPISHO
Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Kadiri jamii mbalimbali zinavyotagusana, ndivyo lugha zinazozungumzwa na jamii hizi nazo zinavyoingiliana na kuathiriana. Mojawapo ya athari hizi ni ukopaji wa msamiati. Jamii zinazopakana au kutagusana hukopa msaimiati kutoka kwa lugha jirani na kuutumia kuelezea dhana mpya zinazoingia katika utamaduni wao kupitia kwa mitagusano ya kijamii.

Lugha ya Kiingereza, kwa mfano, imekopa kutoka lugha nyingine kama vile Kifaransa na Kilatini. Mathalani, istilahi nyingi za kisheria zimekopwa kutoka lugha ya Kifaransa. Aidha, Kiingereza kimekopa kutoka lugha ya Kiswahili. Maneno ya Kiswahili kama vile mwalimu, jiko, mandazi, panga, buibui, ngoma na hata wananchi, sasa yameingia katika kamusi za Kiingereza, kumaanisha kuwa yamekubaliwa kama msamiati rasmi wa lugha ya Kiingereza.

Kiswahili nacho kimeathiriwa na lugha nyingine. Kimekopa msamiati wa Kiingereza na hata Kiarabu. Katika tungo nyingi za kishairi, kwa mfano, Utenzi wa Mwanakupona utapata msamiati wa Kiarabu uliotoholewa. Lugha nyingine ambazo zimeathiri Kiswahili ni pamoja na Kijerumani ambako msamiati kama vile 'shule' ulikopwa na kutoholewa kutokana na neno *schule*. Msamiati kama vile *'leso', 'karata' na 'mvinyo'* yamekopwa kutoka lugha ya Kireno, huku majina 'balozi' na 'bahasha' yakikopwa kutoka Kituruki.

Pamoja na ukopaji wa vipengele vya lugha, mtagusano wa lugha una athari nyingine. Lugha zinapokuja pamoja, mazingira ya wingi-lugha hazuka. Baadhi ya watu hujifunza zaidi ya lugha moja. Mtu anayeweza kuzungumza zaidi ya lugha moja anaweza kujieleza kwa urahisi kwa kuchanganya msamiati wa lugha tofauti. Aidha, anaweza kubadilisha msimbo kulingana na matilaba yake. Ikiwa anataka kukubalika na jamii-lugha anayotagusana nayo, atatumia lugha ya jamii hiyo ili kujinasibisha na kujitambulisha nayo. Wazungumzaji hupata visawe vya maneno kuelezea dhana zile zile, hivyo kuboresha mitindio yao ya mawasiliano.

Kadhalika, kutagusana kwa lugha kunaweza kusababisha kubuniwa kwa lugha ngeni ambayo inarahisisha mawasiliano. Wakati mwingine, watu wanaozungumza lugha tofauti wanapokutana, hubuni mfumo sahili wa lugha ili kufanikisha mawasiliano. **Pijini** ni mfano wa lugha iliyobuniwa kwa njia hii. Pijini huchota msamiati kutoka lugha zilizotagusana. *Sheng* ni mfano mwingine wa lugha ambayo ilibuniwa kutokana na kutagusana kwa lugha ya Kiswahili, lugha za kiasili na Kiingereza.
Japokuwa kuna faida nyingi za wingi-lugha, hasara pia zipo. Mazingira ya wingi-lugha huwapa wazungumzaji fursa ya kuchagua lugha wanayotaka kuwasiliana kwayo. Katika hali hii, lugha yenye ushawishi mkubwa kijamii, kiuchumi na kisiasa ndiyo ianyopendelewa zaidi. Wingi-lugha unaweza kusababisha kukwezwa kwa lugha moja na kudunishwa kwa lugha nyingine. Mathalani, kuwepo kwa lugha nyingi nchini kulizua haja ya kukwezwa kwa lugha ya Kiswahili huku lugha nyingine za kiasili zikipuuzwa.

Lugha hukua kwa kutumiwa. Lugha isipozungumzwa kwa muda mrefu, watu hupoteza umilisi ambao

huifanya kuwa vigumu kuirithisha kwa vizazi. Lugha inaweza pia kukosa wazungumzaji ikiwa wale wanaozungumza ni wachache, au ikaathiriwa na mtagusano na lugha nyingine iliyo na wazungumzaji wengi. Katika hali kama hii, lugha hiyo hukabiliwa na tisho la kudidimia au hata kufa. Ikiwa jamii lugha itakosa kudhibiti sera za matumizi ya lugha yake, baadhi ya lugha ama zitafifia au zitakufa na kusahaulika kabisa.

1. Bila kupoteza maana, fupisha aya za kwanza tatu. **(Maneno 50) (alama 6, 2 za mtiririko)**.
2. Kwa mujibu wa taarifa hii, mtagusano wa lugha una athari gani? **(Maneno 30)**
3. **MATUMIZI YA LUGHA: (ALAMA 40)**

(a) Andika sifa za **kutambulisha** sauti zifuatazo. (alama 2)
(i) /d/ _____
(ii) /th/ _____

(b) **Fafanua** dhana ya **mofimu**. Bainisha **mofimu** katika maneno yafuatayo. (alama 2)
(i) Samaki _____
(ii) Mtu _____

(c) Ainisha **viambishi** kwa kurejelea **majukumu** ya kisarufi katika neno hili. (alama 3)
Alijipelekea

(d) Maneno **yaliyopigiwa** mstari yametumikaje? (alama 2)
Pahali pema pako si pema pa mwenzako.

(e) Andika sentensi **mbili** kutofantisha **vitate** hii. (alama 2)
(i) Apisha
(ii) Apiza

(f) Andika sentensi ifuatayo **upya** ukibadilisha neno **lililopigiwa** mstari kuwa kivumishi. (alama 2)
Mgeni alipewa dawati mpya.

(g) Unda nomino m**bilimbili** kutokana na vitenzi hivi. (alama 2)
(i) Kagua _____
(ii) Hini_____

(h) **Kosoa** sentensi ifuatayo kisarufi. (alama 3)
Mahali kule pana siafu wengi.

(i) Tambua matumizi ya **'a'** katika sentensi ifuatayo. (alama 1)
Mwanafunzi acheza uwanjani.

(j) **Yakinisha** sentensi hii: (alama 2)
Usipofanya bidii hutapita mtihani.

(k) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya **kuamrisha**. (alama 2)
Tafadhali acheni kucheka ovyo.

(l) Andika kwa msemo wa **taarifa**: (alama 3)
"Sitakwenda sokoni leo ila nitakwenda kesho", Nikamjibu.

(m) Eleza matumizi **matatu** ya **kinyota**. (alama 3)

(n) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha matawi. (alama 4)
Mlango umevunjwa na fundi aliyeujenga.

(o) Onyesha matumizi ya **chagizo** ya **mfanano** katika sentensi. (alama 2)
Alitembea kitausi kupokea zawadi.

(p) Andika sentensi ifuatayo kwa **udogo/wingi**. (alama 2)
Mtoto mkaidi aliiba kitabu cha mwenzake.

(q) Tunga sentensi kuonyesha **matumizi** ya kiambishi **'ji'**. (alama 2)

4. **ISIMU JAMII**:
   Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.
   "Ndugu na madada, sote tumealikwa katika karamu hii ya Bwana kabla ya kujongea mezani pake, Bwana. Pana haja ya kutakasa nyoyo zetu na kujutia madhambi yetu. Sisi sote ni watenda dhambi na inastahili kumwendea ili aweze kutuondolea madhambi yetu."

   Maswali
(i) Weka maneno haya katika sajili yake. (alama 2)
(ii) Nini kimekufanya uchague sajili uliochagua katika swali (i).
   (alama 1)
(iii) Eleza sifa za matumizi lugha katika sajili hii.
   (alama 7)

MTIHANI WA PAMOJA WA WILAYA YA KIRINYAGA YA KATI - 2015
Hati Ya Kuhitimu Kisomo Cha Sekondari
102/3
KISWAHILI
KARATASI YA TATU
(FASIHI)
JULAI/AGOSTI, 2015

SEHEMU A: USHAIRI – LAZIMA

1. **SHAIRI A** **SHAIRI B**

Wewe,
Utazame mlolongo wa
Waja unaoshika njia likiwapo;
Unaofuata pembe za barabara zisokuwapo,
Kwenda kuisaka auni,
Kuitafuta kazi inayowala chenga.

Itazame migongo ya wachapa kazi,
Watokwao na jasho kapakapa na,
Wanaotafunwa uhai na jua liso huruma:
Wakiinua vyuma na magunia,
Wakiinua makontena,
Wakichubuka mashambani,
Wakiumia viwandani,
Wakiteseka makazini,
Halafu
Uangalie ule ujira wa kijungu meko,
Mshahara usokifu haja,
Nguo zisizositiri miili dhaifu,
Kilo chao kisichokuwa na machozi,
Na
Ujiangalie
Mwili wako unaomereta ujana wa ufanisi,
Gari lako la kifahari lililozibwa vioo,
Jumba lako la kujishasha kama uwanja mdogo,
Malaki ya pesa unayomiliki,
Ujiitapo mwajiri kwa raha, hunusi usaha wa hali yao?

Dunia kitendawili, hakuna ateguaye;
Dunia kama tapeli, hadaa nyingi ujuye;
Dunia mwenye akili, inampiku na yeye;
Dunia ina mizungu, tena yapika majungu.

Dunia na yake hali, hupumbaza hatimaye;
Dunia ina akili, binadamu sichezeye;
Dunia uwe na mali, huiwezi dhorubaye;
Dunia ina mizungu, tena yapika majungu.

Dunia wenye muali, ambao waichezeye;
Dunia kipigo kali, huwakumba hatimaye;
Dunia wakaja kuli, “menipata nini miye?”
Dunia ina mizungu, tena yapika majungu.

Maswali
(a) Je, mashairi haya mawili ni ya aina gani? Toa sababu.
(alama 2)
(b) Taja dhamira kuu katika kila shairi. (alama 2)
(c) Kwa kutoa hoja zozote **tatu** linganua mashairi haya kiumbo.
(alama 3)
(d) Taja na uelezee **nafsi-nenewa** katika mashairi haya mawili. (alama 2)
(e) Kwa kutolea mfano **mmoja mmoja** eleza matumizi ya mbinu hizi za kimtindo katika shairi la A.
(alama 2)
(i) Kweli-kinzani
(ii) Mishata
(f) Tambua **idhini** ya kishairi iliyotumika katika neno “Waichezeye” na uelezee dhima yake katika utoshelezi wa kiarudhi.
(alama 1)

(g) Dondoa mfano **mmoja mmoja** wa mbinu ya tashhisi kutoka kwenye mashairi yote mawili. (alama 2)
(h) Andika ubeti wa **tatu** katika **shairi la A** kwa lugha nathari. (alama 4
(i) Eleza maana ya msamiati huu kama ulivyotumika katika vifungu hivi. (alama 2)
(i) Inampiku.
(ii) Makontena.

SEHEMU YA B: MSTAHIKI MEYA: TIMOTHY AREGE

Jibu swali la **2** au **3**

2. "Nanyi vilevile msikate tamaa. Endeleeni kushinikiza kumwona Meya. Mlango hatimaye huenda ukasalimu amri ---"
(a) Eleza muktadha wa dondoo hii. (alama 4)
(b) Taja tamathali zozote **mbili** za lugha zilizotumika katika dondoo hii. (alama 4)
(c) Eleza ni kwa nini wanaorejelewa wanakaribia kukata tamaa. (alama 8)
(d) Eleza sifa **mbili** za mnenaji. (alama 4)
3. Viongozi katika bara la Afrika wameonyesha hali ya juu ya kutowajibika. Eleza dhana hii kwa kurejelea tamthilia ya Mstahiki Meya. (alama 20)

SEHEMU YA C: RIWAYA
KEN WALIBORA: KIDAGAA KIMEMWOZEA

*Jibu swali la **4** au **5***

4. "Ujenzi wa jamii mpya ni jukumu la vijana." Jadili kwa kurejelea riwaya hii. (alama 20)
5. Mwandishi kama huyo watu hukutana naye kwa nadra sana.
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Tambua mbinu iliyotumika katika kauli hii. (alama 2)
(c) Toa mifano mingine **saba** ya matumizi ya mbinu hii katika riwaya hii. (alama 14)

SEHEMU YA D: HADITHI FUPI: DAMU NYEUSI
KEN WALIBORA

*Jibu swali la **6** au **7***

6. "Alitembea kando ya barabara kwenye kijia cha wapitia njia huku akinyapia nyapia nyapunyapu na kupepesuka kama mlevi chakari".
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Anayerejelewa katika dondoo hili alikuwa anaenda wapi? (alama 2)
(c) Eleza sifa za anayerejelewa katika muktadha kuu. (alama 6)
(d) Mhusika huyu yuko na umuhimu gani katika hadithi husika? (alama 5)
(e) Eleza mbinu zozote **tatu** ambazo zimetumiwa na mwandishi katika Muktadha huu. (alama 3)
7. **MIZIZI NA MATAWI: ALI ABDULLA ALI**
(a) Eleza sifa mbili na umuhimu wa wahusika wafuatao katika hadithi ya **MIZIZI NA MATAWI**:
(i) Bi. Mkubwa. (alama 3)
(ii) Bi. Kidura. (alama 3)
(iii) Sudi Abdalla. (alama 4)
(b) Taja na ueleze jinsi maudhui ya mapenzi yanavyojitokeza katika hadithi hii.

(alama 10)

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

8. (a) Maghani ni nini? (alama 2)
   (b) Eleza sifa za maghani.
   (alama 6)
   (c) Fafanua aina zozote **tatu** za maghani.
   (alama 6)
   (d) Taja na ueleze umuhimu wa maghani.
   (alama 6)

MTIHANI WA MWIGO WA WILAYA YA KIRINYAGA YA KATI 2015
102/1
KISWAHILI KARATASI YA 1
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

1. **SWALI LA LAZIMA**
   SURA
   (i) Kichwa / Anwani ya ripoti.
   - Ripoti ni ya nini, nani, nani aliteua jopo na mwaka.

   (ii) Utangulizi
   - Nani alitaka ripoti iandikwe.
   - Muda waliopewa
   - Tatizo lenyewe
   - Wanajopo na vyeo vyao.

   (iii) Mbinu za uchunguzi
   - Mfano matumizi ya hojaji, mahojiano n.k.

   (iv) Matokeo ya uchunguzi
   - Ukabila
   - Dini
   - Umaskini
   - Ukosefu wa ajira
   - Misimamo tofauti ya kisiasa
   - Mifumo tofauti ya utawala.
   - Ugavi wa raslimali za nchi.
   - Makundi haramu.
   - Ukimbizi
   - Uhasama wa kiukoo
   - Kisasi
   - Tamaa ya mali na mamlaka.
   - Ufisadi. Tanbihi: mwanafunzi azingatie angaa hoja nane.

(v) Hitimisho
Tanbihi – Hitimisho liwe fupi na lioane na matokeo ya uchunguzi. (iwe aya moja)

(vi) Mapendekezo
- Huandikwa kwa kuorodheshwa kwa nambari.
- Yatoe suluhisho ama hatua za kuchukuliwa ili kudhibiti ama kusuluhisha tatizo la utovu wa usalama.

Mifano
(i) Serikali iwahamasishe wananchi umuhimu wa kuishi pamoja kwa amani.
(ii) Sheria iundwe ya kuwaadhibu wahalifu.
(iii) Mtazamo wa nyumba kumi utiliwe maanani.
(iv) Ugavi wa raslimali za nchi usawasishwe.
(v) Nafasi za ajira ziongezwe.
(vi) Idara ya elimu iongeze katika mtaala wa masomo somo la umuhimu wa utangamano wa wananchi.
Mwalimu atathmini hoja zozote zingine zinazofaa.

(vii) Mwisho
- Jina la mwandishi na sahihi
- Cheo
- Tarehe

2. Madhara ya teknolojia ya kisasa
(i) Uraibu
(ii) Uzembe kazini
(iii) Ubunifu kudorora
(iv) Utangamano
(v) Upweke
(vi) Mkengeuko (km. mavazi)
(vii) Matumizi ya dawa za kulevya.
(viii) Uzinzi
(ix) Ajali barabara kuongezeka.

Faida
(i) Hurahisisha mawasiliano.
(ii) Utafiti kupitia mtandao (elimu)
(iii) Upanuzi wa biashara
(iv) Usafiri kuimarika.

Tanbihi
(i) Mwanafunzi azingatie pande zote mbili, asipofanya hivyo aadhibiwe kwa kutolewa alama nne.
(ii) Mwanafunzi atoe msimamo wake.

3. Methali
- Mtahiniwa asimulie kuhusu mhusika ambaye maishani mwake alikuwa kipenzi cha kila mtu kwa wema wake.
- Aonyeshe mema aliyowatendea watu wengine kisha atumie sifa hizo kuonyesha jinsi hata baada ya kufa jina lake bado linaishi vinywani vya watu. Akumbukwe kwa pengo aliloacha.

4. Mdokezo
- Mwanafunzi atamatishe insha yake kwa maneno aliyopewa. Akiongeza mengine atuzwe alama ya 02.

MTIHANI WA MWIGO WA WILAYA YA KIRINYAGA YA KATI 2015
102/2

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

1. UFAHAMU

(a)

- Ufisadi
- Uongozi mbaya
- Turathi za kikoloni
- Uchumi kuegemezwa kwenya kilimo kinachotegemea mvua isiyotabirika.
- Idadi kubwa ya watu inayoupiku uwezo wa uchumi wa taifa linalohusika.
- Ukosefu wa nyenzo na mali za kuwakwamua raia kutoka lindi la umaskini.
- Ukosefu wa elimu na nafasi za ajira. Zozote (4x1 = alama 4)

(b)

Asilimia kubwa ya pato la kitaifa katika mataifa mengi hutumika kuyalipa madeni hayo. (2x1 = alama 2)

(c)

- Kuibuka kuwa mikakati bora ya kupambana na umaskini.
- Pawepo na sera zinazotambua ukweli kuwa asilimia kubwa ya raia wa mataifa hayo ni maskini.
- Kuzalisha nafasi za kazi kwa dharura.
- Kupanua viwanda hususan vinavyohusiana na zaraa ambayo ni tegemeo kuu la mataifa mengi.
- Kuendeleza elimu.
- Kuimarisha miundo msingi. (4 x 1 = alama 4)

(d)

Ni chanzo cha kufa kwa viwanda asilia na kuendeleza umasikini zaidi. (1 x 2 = alama 2)

(e)

- Kulitadarukia – kulishughulikia, kulitatua, kulikabili.
- Kuatika – kuanzisha kutia, kuzua.
- Kuyaburia madeni kuyasamehe madeni, kuyaondolea madeni. (3x1 = 3mks

2. MAJIBU YA UFUPISHO

(a) Hoja za kuzingatia

- Mitagusano ya kijamii hufanya lugha kuathiriana.
- Ukopaji wa vipengele vya lugha ni moja ya athari hizo.
- Msamiati hukopwa ili kueleza dhana ngeni.
- Lugha zote hukopa.
- Kiingereza kimekopa kutoka kilatini, kifansa na Kiswahili.
- Kiswahili nacho kimekopa kutoka kiingereza, kiarabu, kireno, kituruki na kijerumani.

(b) Hoja za kuzingatia

- Kuzuka kwa hali ya uwingi – lugha.
- Ukuaji wa lugha.
- Kuzuka kwa lugha mpya.
- Kudunishwa kwa lugha.
- Kufa kwa lugha.

3. MAJIBU YA LUGHA

(a) Sifa za sauti / d /

(i) Ni kipasuo.
(ii) Hutamkiwa kwenye ufizi
(iii) Ni sauti ghuna. (½ x 2)

Sifa za / th /

(i) Ni kikwaruzo / kikwamizo.
(ii) Hutamkiwa menoni.
(iii) Ni hafifu (si ghuna) (½ x 2)

(b) Ni kipashio kidogo cha neno ambacho hakiwezi kugawika zaidi na kina maana.

(i) Samaki (alama 1)
(ii) Mtu => m-tu.
(alama 1)

(c) alijipelekea

a	-	li	-	ji	-	pelek	-	e - a
nafsi ya umoja		wakati uliopita		mtendwa		mzizi	kauli	kiishio

(6 x ½ = alama 3)

(d) Pema – kivumishi
Pema – kiwakilishi (2 x 1 = alama 2)

(e) Apisha – kulitamka jina la Mungu kama njia ya uthibitisho.
Apiza – kutamkia mtu maovu. (2 x 1 = alama 2)

(f) Mwanafunzi mgeni alipewa dawati mpya. (2 x 1 = alama 2)

(g) Ukaguzi, mkaguzi, wakaguzi, kukagua. (½ x 2)
Mhini, uhini, kuhini , mhiniwa. (½ x 2)

(h) Mahali mle mna siafu wengi.
Pahali pale pana siafu wengi.
Mahali kule kuna siafu wengi. (alama 3)

(i) Hali isiyodhihirika. (1 x 1 = 1)


(j) Ukifanya bidii utapita mtihani. (2 x 1 = 2)

(k) Acheni kucheka ovyo! (2 x 1 = 2)

(l) Nilimjibu kuwa singeenda sokoni siku hiyo ila ningeenda siku iliyofuata. (alama 5)

(m) (i) Maana zaidi ya neno fulani.
(ii) Neno limeendelezwa vibaya.
(iii) Sentensi ina makosa ya kisarufi. (alama 3)

(n)



(o) Mwanafunzi atunge sentensi akitumia vielezi vya namna mfanano kama Alitembea <u>kitausi</u> kupokea zawadi. (alama 2)

(p) Vitoto vikaidi viliiba vijitabu vya wenzao. (alama 2)

(q) (i) Ukubwa
(ii) Kiambishi awali katika baadhi ya nomino katika ngeli ya LI-YA.
(iii) Kuonyesha uzoefu.
(iv) kujitendea (2x1 = alama 2)

4. <u>ISIMU JAMII</u>

(a) Hii ni sajili ya maabadini / dini.

(b) <u>Sababu</u>
(i) Matumizi ya maneno kama kutakasa nyoyo kabla ya kushiriki karamu ya Bwana.

(ii) Kumwendea Bwana atuondolee dhambi zetu. (Zozote 2x1 = 2)

(c) Sifa

(i) Matumizi ya msamiati maalum kwa mfano: Mungu asifiwe.
Alhadulillahi!
Shetani ashindwe!

(ii) Matumizi ya sentensi refu ili kuweza kueleweka vizuri na waamini.

(iii) Kudondoa kauli yaani kurejelea sehemu fulani katika maandiko matakatifu.

(iv) Uradidi wa maneno kurudiarudia maneno kama:
Mungu yu mwema
Mwenyezi Mungu
Amina n.k.

(v) Matumizi ya ishara na miondoko.
Anapohubiri hutumia ishara na miondoko mfano kuinua mkono, Kuruka kutoka hapa na pale.

(vi) Kuchanganya nyakati sana kwa mfano: naye akaondoka hapo waende upande wa mashariki.

(vii) Matumizi ya maneno yenye asili ya kigeni kwa mfano: majina ya wahusika Sila na Petero.

(viii) Matumizi ya lugha maalum kama vile tamathali za usemi, taswira, jazanda n.k. (7x1 = 7)

MTIHANI WA MWIGO WA WILAYA YA KIRINYAGA YA KATI 2015
102/3
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

1.
(a) Je, mashairi haya mawili ni ya aina gani.
A – huru – halijazingatia arudhi za utunzi wa ushairi.
B – tarbia – lina mishororo 4 katika kila ubeti.
- Kikwamba – neno 'dunia' laanzia kila mishororo.
- Mtiririko – vina vya kati na mwisho vina keketo.
- Mathnawi – kila mshororo una vipande viwili.
- Shairi la arudhi kwa sababu limezingatia arudhi za utunzi wa ushairi. *Kutaja na kueleza.*(alama 2)

(b) Taja dhamira kuu katika kila shairi.
A - Kukashifu viongozi wanaouwatesa wafanyakazi.
- Kuangazia haki duni ya ufanyakazi mikononi mwa waajiri katili.
B - Kuangazia jinsi binadamu afaa kutahadhari na dunia inayo dhuru / angamiza. (Hoja 1x2 = 2)

(c) Kulinganua mashairi haya kiumbo.

A	B
(a) lina beti 4	- lina beti 4
(b) idadi ya mishoro kila ubeti ni tofauti	- kila ubeti una mishororo 4
- vina vyatofautiana kwa kila ubeti	- vina vina keketo
- halina kibwagizo	- lina kibwagizo maalum
- mishororo haija gawika vipande vipande	- limegawika kuwili ukwapi na utao
- mizani yatofautiana kwa kila mshororo	- mizani ni sawa 8,8

Tatu za kwanza – kila hoja lama 1 x 3 = 3

(d) **Nafsi nenewa katika mashairi haya mawili**.
A – Mwajiri katili anayewadhulumu wafanyakaziakijitajirisha kwa jasho lao.
B – binadamu asiyetahadhari na dunia. *Kila hoja alama 1 x 2*

(e) **Matumizi ya mbinu hizi za kimtindo katika shairi la A**.
(i) Kweli – kinzani - kilio kisichokuwa na machozi.
- barabara zisizokuwapo.
(ii) Mishata - utazame mlolongo wa
- watokwao na jasho kapakapa na
- wanaotafunwa uhai na jua liso. *Ya kwanza al. 1 x 2*

(f) Tabdila badala ya waichezee – kupata urari wa vina 'ye'
Kutaja na kueleza umuhimu – alama 1

(g)

A	V
- Kazi inawala chenga	- dunia kama tapeli inahadaa
- Wanatafunwa uhai na jua	- dunia inampiku mwenye akili
	- dunia yapika majungu (alama 2)

(h) Ubeti wa tatu katika shairi la A kwa lugha nathari.
Pia mchunguze maskini na mapato ya kazi yake duni, yasiyotosheleza mahitaji yake, na anayevalia nguo zilizochanika na zisizosetiri mwili usio na nguvu, na hulia bila kutokwa na machozi. (hoja zozte 4x1 = alama 4)

(i) Maana ya msamiati.
(i) Inampiku – inamshinda / inamweza
(ii) Makontena – shehana / mizigo mizito / makasha. (hoja 2x1 = alama 2)

2. (a) (i) Msemaji ni Daktari Siki.
(ii) Anayesemewa ni Tatu mmoja wa wawakilishi wa wafanya kazi.
(iii) Wako katika ofisi ya Daktari Siki.
(iv) Tatu amekuja kumwona na kumsihi Daktari Siki aende aseme na Meya kama binamu yake kuhusu masaibu ya umma pengine huenda akamsikiliza. (alama 4)

(b) **Tamathali za lugha**.
(i) Msemo – msikate tamaa.

(ii) Tashihisi – mlango huenda ukasalimu amri. (alama 4)

(c) **Kwa nini wanaorejelewa wanakaribia kukata tamaa.**

- Mishahara duni
- Kulipwa mshahara nusu na hata mshahara kukosekana hata baada ya miezi mitatu.
- Kukosekana kwa dawa hospitalini.
- Madiwani kuongezewa mishahara huku wao wakipuuzwa.
- Madiwani kutolipa kodi.
- Ufisadi – unyakuzi wa ardhi ya umma, kuuza fimbo ya meya.
- Kukosekana kwa ajira kwa vijana wanaofuzu.
- Hali duni ya usafi wa mazingira.
- Vifo vya wagonjwa hospitalini.
- Njaa – watu kukosa lishe kiasi cha watoto kulishwa kiporo.
- Kukoseakana kwa vifaa vya kufanyia kazi. (hoja zozote 8x1 = alama 8)

(d) **Sifa za Siki**.

- Mshauri mwema
- Mzalendo
- Anawajibika
- Ni mtetezi wa haki
- Mwenye kujali maslahi ya wengine. (alama 4)

Tanbihi: Lazima mtahiniwa atoe maelezo ya kudhibitisho sifa hizo.

3. **MEYA**

- Meya kulinganisha ufanisi wa Cheneo na wa miji midogo na dhaifu, badala ya kuendelea kupiga hatua mbele wanapiga hatua kinyumenyume.
- Meya kujifanya hajui watu wanateseka. Amefumba macho kwa matatizo yao kama mshahara duni n.k.
- Meya kukataa kuonana na kuwasikiza viongozi wa wafanyakazi, hata anapokutana nao anapuuza mapendekezo yao.
- Kuna baadhi ya watu wanaomuunga Meya mkono, hataki kujua juu ya wengi. Wachache wanatosha.
- Nyimbo za kizalendo kabla na baada ya vipindi muhimu, miaka hamsini baada ya uhuru.
- Mipango ya miaka kumi inapuuzwa. Meya anasema kuwa wana mipango ya miaka kumi ni upuzi.
- Afya bora nay a bure ilihaidiwa wananchi; wanalazimika kulipa.
- Wananchi hawakushikirishwa katika maamuzi. Wengine kama Siki kutimuliwa nyumbani mwa meya, wanapojaribu kumwelezea malalamishi ya Raia.
- Mikutano kufanywa kwa nadra, kama tunavyoelezwa na Diwani 1. Hufanywa hasa wakati kuna jambo kama mgomo kutokea.
- Ahadi za uongo – shehena ya dawa kuwa bahari kuu.
- Uchafu kuenea kila mahali na uvundo kukoleza hata ndani mwa nyumba.
- Kujiongezea mishahara kama overtime, marupurupu.
- Kula viapo vya kuficha siri za wizi ama wa fimbo ya meya.
- Meya kutojua kuwa hakuna maji safi. Anapoelezwa kuwa maji yanayotumika katika hoteli za mjini yanayosombwa kwa punda kutoka mtoni anastaajabu. (zozote kumi) (10 x 2)

4.

- Amani na Imani wanakutana safarini na wanaamua kuandamana hata kama mbeleni hawakujuana.
- Madhubuti ambaye ni wa tabaka la juu anatangamana na Amani na hata kuhamia kibandani mwa Amani ili waendeleze juhudi za ukombozi.
- Amani na madhubuti wanahimiza usawa na kutekeleza suala hili kwa kugawia maskini ardhi.
- Amani na Imani wanabadilika mtazamo wa watu kwa walemavu.
- Amani na Imani wanachangia kutekelezwa kwa haki na Yusufu Hamadi anatolewa lawamani.
- Amani anajua umuhimu wa msamaha na maridhiano. Anahimiza Ocar Kambona asilipize kisasi kwa Mtemi Nasaba Bora.
- Madhubuti anapendekeza jamii inayodumisha maadili. Anakataa kazi aliyotafutiwa na babake kwa njia ya ufisadi.
- Imani anapinga taasubi ya kiume anapomwambia Amani asiwaweke pembeni wanawake katika kitabu anachoandika.

- Wanafunzi wa chuo kikuu wanapambana na wizi wa kitaaluma kwa kumwaibisha majisifu na kumfanya abadilike.
- Amani na Imani wanapania jamii mpya inayolinda haki za watoto kwa kumlea mtoto Uhuru japo si mtoto wao.
- Amani na Imani wanapuuza miiko isiyofaa kwa kuyanywa maji ya mto kiberenge. (10x2)

5. **RIWAYA – KIDAGAA KIMEMWOZEA**

(a) – Haya ni maelezo ya mwandishi akimrejelea mwalimu Majisifu. Hapa ni katika ukumbi wa chuo kikuu
cha Mkokotoni ambapo mwalimu Majisifu aliposhindwa kuwasilisha mhadhara na kujichanganya umati
ulipo fumukana baadhi yao walimjongelea mwalimu Majisifu ili angalau waweze kumsalimia mkononi
au kupiga picha naye. (alama 4)

(b) Kinaya – mwalimu Majisifu si mwandishi bora hata alishindwa kujieleza. (alama 2)

(c)
- Ni kinaya kuwa zahanati ya Nasaba Bora inajulikana kama mahali ambapo watu wanakwenda kujifia.
- Ni kinaya kuwa dini zote zinahubiri amani, udugu na rehema lakini maovu mengi hutendwa katika jina la Mungu.
- Fao alijihusisha kimapenzi na mwanafunzi wake.
- Wasimamizi wa timu ya Songoa F.C. walimpuuza Chwechwe makweche baada ya kuvunjika fupaja.
- Maneno ya Balozi kuwa kuondoka kwa mzungu kulileta heri.
- Nasaba Bora kusema watu wengi watahudhuria mazishi yake.
- Uso wa Imani kuonyesha tabasamu siku zote.
- Nyumbani kwao Imani kunaitwa Baraka.
- Nasaba Bora kuwafuta kazi wafanyikazi walionadhifisha mazingira yake. (zozote 7x2)

6. (a) **Majibu ya Damu Nyeusi – Ken Walibora**
- Haya ni maelezo ya mwandishi kumhusu Fikirini.
- Anaeleza jinsi mwanamume huyu alivoykuwa anatembea katika kijia akielekea katika chuo kikuu kule nchini marekani.
- Hii ni baada ya kuachwa na basi la abiria lililokuwa linaendeshwa na dereva mzungu.
- Alimwacha Fikirini katika kituo rasmi cha basi maksudi.
- Hii ni kutokana na ubaguzi wa rangi uliokuwa huko kwa sababu Fikirini alikuwa mweusi (damu nyeusi bila shida.
- Baadaye Fikirini aliweza kuibiwa vitu na Fiona (mwanamke muamerika mweusi) baada ya kumdanganya Fikirini kuwa angempeleka chuoni. (alama 4x1 = 4)

(b) Anayerejelewa hapa ni Fikirini na alikuwa anaenda chuo kikuu alikosomea. Alikuwa ni mwanafunzi wa somo la kiingereza katika chuo kikuu. (alama 1x2 = 2)

(c)
- Alikuwa mlevi. Akiwa Afrika mashariki. Alitembea sehemu mbalimbali katika nchi ya Kenya, Tanzania na Uganda akitafuta pombe a aina mbali mbali.
- Mvumilivu – alivumilia kuulizwa maswali ya ajabu na wahadhiri na wanafunzi amani waliokuwa wazungu.
- Alikubali mambo haraka – Fiona alipomwambia kuwa angempeleka chuoni kwa gari lake alikubali akamfuata haraka na kuingia ndani ya nyumba bila kuomba asubiri nje.
- Ni mtamaduni – Alipenda vyakula vya kiafrika sana kuliko vya marekani.
- Mwenye bidii – alipoachwa na gari la abiria anaamua kutembea kwa miguu akielekea chuoni badala ya kurudi chumbani pia kusoma hadi kwenda kutafuta elimu ya juu Amerika.
- Alikuwa na upweke – alipomwona Mwafrika mweusi kama yeye nchini Amerika alitamani awe rafikiye. (alama 6)

(d) **Umuhimu wa Fikirini**
- Ametumiwa na mwandishi kuonyesha jinsi wafrika wanavyodhulumiwa na wazungu. Fikirini alibaguliwa chuoni, barabarani na mkahawani.
- Anatumiwa na mwandhishi kuonyesha umuhimu wa kutia bidii katika masomo na kufikia viwango vya juu.
- Ni kielezo cha watu wavumilivu katika jammi. Akiwa Amerika alivumilia dhuluma za aina mbalimbali

alizotendewa na jamii ya Amerika.
- Ni kiwakilishi cha watu walio na mapenzi kwa nchi zao anapenda nchi za Afrika mashariki sana. Hii ni ishara ya uzalendo kamili.
- Anatumiwa kama kielelezo cha watu wanaopenda utamaduni wao, vileo chakula n.k. (zozote 5x1 = 5)

(e) **Mbinu za lugha**.
(i) Tanakali za sauti Ananyapianyapia nyapu nyapu na kupepesuka pepesu.
(ii) Tashbihi Mf. Ananyapia nyapu nyapu na kupepesuka kama mlevi chakari.
(iii) Taswira Mwandishi anatupatia picha ya jinsi Fikirini alivyokuwa akitembea kama mlevi juu ya barafu.
(iv) Tanakali ya sauti Mlevi chakari. (zozote 3x1 = 3)

7. **Mzizi na Matawi – Ali Abdula Ali**

(a)
- Bi.Mkubwa (mama mtu)
- Ni mdanganyifu / mwongo.
  Anadanganya Sudi kuwa baba yake alikuwa amefariki kabla ya kuzaliwa kwake.
- Ni mkarimu. Alimlea sudi akamwelimisha hadi ng'ambo kisha akampa nyumba yake airithi.
- Ni mwenya kuomba msamaha. Alimwomba msamaha Sudi kwa kumdanganya siku nyingi kuhusu asili na fasili yake.
- Ni mwenye huruma / utu: utu unamfanya kumchukua Sudi katika pipa la taka na kumlea kama mtoto wake.
- Msiri: Hakumfichulia Sudi kuhusu usawa wake. Alimdanganya umuhimu.
  - Kielezo cha watu wenye ukarimu: anamlea Sudi kama mwanawe na kumrithisha.
  - Kielelezo cha watu ambao husema ukweli baadaye bila kujali athari yake. Kumjua Sudi kuhusu usawa wake. (sifa alama 2 umuhimu alama 1 = 3)

(ii) **Bi Kidura**.
- Ni katili – ukatili wake unadhihirika anapowatupa Sudi katika pipa la takataka baada ya kumzaa aendelee na ana za ujana.
- Ni mcha Mungu – alimwomba Mungu msamaha kwa sababu ya dhambi ya kutupa mtoto wake baada ya kumzaa.
- Ni mwenye bidii. Alifanya kazi ya nyumbani kwa Bi. Mkubwa. Alimpikia, akafagia, akamfulia, akapiga deki n.k.
- Mpenda anasa – alimtupa mtoto wake mchanga kwenye pipa la takataka aendelee na anasa za ujana.
- Mwenye shukrani – aliwashukuru Sudi na Bi. Mkubwa kwa kumruhusu aishi nao. (alama 2)

Umuhimu
- Anaendeleza maudhui ya majuto. Anajuta baadaye kwa kumtupa mwanawe.
  Mwandishi anamtumia kuwaonya watu dhidi ya maamuzi mengine maishani: kumtupa mtoto.
- Kielelezo cha majuto kwambo mambo tufanyayo huweza kuleta majuto baadaye.
- Kielelezo cha utamaduni uliopitwe na wakati wa kutotaka kujulikana alikuwa na mtoto. (alama 1)

SUDI ABDALA
(i) Mwerevu – alisoma kwa bidii na kupata shahada ya udaktari wa wanasheria ulaya.
(ii) Mkarimu – ukarimu wake ulimfanya ampatie Bi. Kidura kazi na akaagiza apewe chakula, malazi na nguo.
(iii) Mpenda anasa – anaenda katika karamu ya sikukuu ya pasaka na kucheza densi na waridi. Pa alienda Tea Breeze akiwa na Radhia kustarehe huko.
(iv) Hakati tamaa. Hakukata tamaa ya kumuuliza Bi. Mkubwa kuhusu aliko baba yake.
(v) Jasiri. Anarudi nyumbani peke yake usiku bila uoga wowote.
(vi) Ni msamehevu. Anamsamehe Bi. Mkubwa kwa kumdanganya kuhusu baba yake. Alikuwa anamdanganya kuwa baba yake alikuwa ameaga dunia. Alimsamehe Bi. Kudura kwa kumzaa na kumtupa katika tupa.
(vii) Mwenye bidii – Alitia bidii akasoma hadi chuo kikuu udaktari katika wanasheria.

(viii) Mwenye kutafuta ukweli – mara kwa mara alikuwa anamuuliza Bi. Mkubwa kuhusu fasili na asili yake. Alikuwa anamuuliza mara kwa mara kwa sababu hakuridhishwa na jibu alilokuwa akipewa na mama huyu. (alama 2x1)

Umuhimu

i. Kielelezo cha vijana wenye heshima na bidii inayowainua maishani.
ii. Anatumiwa na mwandishi kuonyesha umuhimu wa kuwa na mtoto. (alama 2)

(b) **Maudhui ya mapenzi**.

- Bi. Mkubwa (Mama Mtu) na Bw. Abdalla walikuwa na mapenzi ya dhati. Bi. Mkubwa anamweleza Sudi kuwa walioana na Abdalla aliyekuwa mwarabu wa kutoka Mauye na kuishi kwa mapenzi kama mke na mume. Lakini mapenzi yao hayakudumu kwani Abdalla aliweza kufariki na kumwachia mkewe na mimba ya Sudi.
- Sudi alionyesha mapenzi kwa wasichana. Alipendwa sana na wasichana/ alipendwa sana na wasichana kwa urembo wake na utanashati.
- Sudi alipendwa na wanawake alipokuwa katika sherehe za karamu ya Pasaka Easter get together.
  Walitaka kucheza densi naye. Hangeweza kucheza na wote.
- Bi. Mkubwa anamwonyesha Sudi mapenzi ya kiwango cha juu. Aliutunza na kumlea Sudi vizuri na kumsomesha hadi akapata shahad a ya udaktari wa sheri.
- Bi Kidura alionyesha mapenzi kwa Sudi alipoajiriwa kwa Bi. Mkubwa hadi akashika uhusiano wake na Sudi. (5x2 = alama 10)

8. **FASIHI SIMULIZI**.

(a) Maana ya maghani

- Mashairi ya kukaririwa tu hayaimbwi.
- Hutolewa kwa kalima badala ya kuimbwa. (alama 2)

(b) **Sifa za maghani**.

- Ni tungo la kishairi. Yaani yana muundo wa ushairi.
- Husimulia matukio kwa kirefu hasa yanayotambwa.
- Hutungwa papo hapo na kusemwa mbele ya hadhira.
- Hutungwa kwa ufundi ukubwa.
- Huweza kutolewa na mtu mmoja au kundi ki watu.
- Anayeghani hujisifu / kusifu kitu / jambo fulani.
- Huwa na majigambo mengi.
- Huambatana na ala mbalimbali za muziki.
  (alama zozote 6x1 = 6)

(c) **Aina tatu za maghani**.

- Tondozi – Tungo zinazoghanwa na huwasifu watu, wanyama na vitu.
- Tendi - Huitwa pia ushairi wa ushujaa. Hujumuisha sifa zinazoonyehsa mafanikio ya mashujaa na mbolezi zinazoonyesha anguko la shujaa / mtawala.
- Rara – hadithi fupi na nyepesi za kishairi zinazopitishwa kwa mdomo.
- Huzungumzia tajriba ya maisha.
- Pembezi – Ni aina ya tondozi inayotolewa kusifu watu fulani pekee mf. viongozi, waganga mashuhuri, waelezi wazuri, wapenzi waliopigania pendo lao n.k.
- Sifo – Ni mashairi ya sifa ambayo hughanwa kumsifu mtu fulani kutokana na matendo yake ya kishuj (zozote 3x2 = 6)

(d) **Umuhimu wa maghani**.

- Kuburudisha: husisimua hadhira.
- Kuelimisha: huwaelimisha wanajamii kuhusu utamaduni wao.
- Husifu tabia hasa ya watu wenye tabia za kishujaa.
- Hukashifu tabia potovu ili kuwakosoa wanaohusika.
- Huhifadhi historia ya jamii – ili watu kuonea fahari jadi yao.
- Huendeleza lugha: Huimarisha stadi ya kuongea na kukuza ujasiri wa kuongea hadharani.
- Hueneza umoja / ushirikiano katika jamii watu hujumuika pamoja kusikiliza maghani na hii huleta utangamano. (zozote 6x1 = alama 6) Tanbihi: Mtahiniwa asipoelezea umuhimu hadhibiwe.

MTIHANI WA PAMOJA WA MOKASA 2015
Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari
102/1
KISWAHILI
Karatasi ya 1
INSHA

1. Kumekuwa na ongezeko la migomo ya wafanyakazi nchini katika siku za hivi karibuni. Wewe ni katibu wa tume iliyobuniwa na rais kusimamia suala hili. Andika ripoti
2. Ufisadi umechangia pakubwa kuwepo kwa maendeleo duni nchini. Jadili.
3. Andika insha inayoafikiana na methali Baniani mbaya kiatu chake dawa.
4. Andika insha itakayomalizikia kwa;
   …walipofungua mlango huo hatimaye,wengi hawakuweza kuzuia hisia zao.Waliangua vilio kwa maafa waliyoshuhudia.

MTIHANI WA PAMOJA WA MOKASA
102/2
KISWAHILI
Karatasi ya 2
LUGHA
UFAHAMU: (Alama 15)
Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Tokea muundo mpya wa serikali ya ugatuzi uanze kutekelezwa miaka miwili iliyopita, kumeendelea kushuhudiwa matatizo mengi hali iliyopelekea kushuhudiwa kwa msururu wa migomo na maandamano ya raia.Fujo za karibuni kabisa ni zile zinazoshuhudiwa katika miji mikubwa za wachuuzi na wafanyibiashara wakipinga hatua za serikali za kaunti kuwatoza ushuru takribani kwa kila huduma na bidhaa ikiwemo wanyama,kuku na ndege.La kuhuzunisha zaidi katika baadhi ya majimbo imeripotiwa kuwa raia wamelazimishwa kulipa ushuru kwa kutaka tu kuona maiti za jamaa zao kwenye vyumba vya kuhifadhia maiti!

Wanasiasa wameonekana kuwa na wakati mgumu kutetea mfumo huu mpya wa ugatuzi huku baadhi wakisema kwamba matatizo yanayoshuhudiwa kwa sasa yametokana na ugeni wa mfumo huo.Wengine wameinyoshea kidole serikali ya kitaifa kwamba ndiyo inayosambaratisha muundo huu.Wengine wanahoji kuwa bado ni mapema na kwamba kunatajika muda mrefu ili kufaulu
Ni wazi kwamba kumekosekana nidhamu bora ya kusimamia maisha ya raia nchini Kenya.Matatizo yanayokumba raia kwa sasa ni dalili kuwa mfumo wa serikali ya ugatuzi umeongezea chumvi kwenye kidonda badala ya kutibu.Swali ni je,hadi lini nidhamu ya kusimamia raia itakuwa ni suala la majaribio na makosa?

Hatua ya kuwarundikizia raia ushuru mkubwa ni kitendo cha unyonyaji na cha dhuluma kinachofaa kupingwa. La kufahamishwa hapa ni kwamba ushuru ndio njia kubwa ya kuzalisha mapato ya serikali zinazojifunga na mfumo wa kimagharibi wa kiuchumi wa kibepari ikiwemo Kenya.Asilimia 90 ya mapato ya serikali za kibepari huegemea ushuru. Kwa hivyo hatua ya serikali za kaunti katika kuwanyonya raia kwa kuwalipisha ushuru si ajabu bali ni thibitisho kuwa jamii ya Kenya inaongozwa na nidhamu ya kiuchumi ya ubepari mfumo wa unyonyaji na ukandamizaji.Ukweli unabakia kuwa ndani ya serikali za kibepari raia ndio hubebeshwa mzigo wa ushuru unaoishia matumboni mwa viongozi!

Miito ya mabadiliko ya katiba na ya miundo mipya ya kiutawala si lolote ila ni moja tu ya hatua za mfumo wa kibepari kujipa muda wa kuishi na kuziba aibu zake za kushindwa kusimimia maisha ya watu.Kufeli huku kwa mfumo huu kunashuhudiwa hadi kwenye nchi kubwa za kibepari kama Marekani na Uingereza hivyo nazo zimekumbwa tele na maandamano na fujo za raia wakilalamikia hali ngumu ya maisha.

Maswali

a) Yape makala haya anwani mwafaka. (alama 1).
b) Eleza mtazamo wa wanasiasa kuhusu utepetevu wa mfumo huu.
   (alama 3)
c) "Ugatuzi nchini Kenya ni mfumo wa kibepari" Thibitisha kauli hii kwa kurejelea makala

(alama 3)

d) Migomo ni zao la matatizo yaliyogatuliwa kutoka serikali kuu. Toa sababu nyingine zinazosababisha migomo katika serikali za ugatuzi
(alama 4)

e) Thibitisha jinsi mfumo wa ugatuzi umeongeza chumvi kwenye kidonda badala ya kutibu
(alama2)

f) Eleza maana ya maneno yafuatayo
(alama 2)
(i) Ugatuzi
(ii) Kibepari

UFUPISHO (Alama 15)

Soma makala yafuatayo na ujibu maswali.

Mojawapo kati ya misingi na nguzo za maendeleo ulimwenguni ni viwanda. Viwanda ni muhimu kwa kuwa ndivyo vinavyoigeuza malghafi yanayopatikana na kuwa bidhaa zinazoweza kutumiwa na watu. Katika nchi zinazoendelea, ambazo hazina uwezo mkubwa wa mitaji, viwanda vinavyoimarika ni vile vidogo. Hivi ni viwanda ambavyo huhusisha amali za mikono. Kuimarika kwa viwanda hivi vidogo kunatokana na sababu mbalimbali.

Nchi zinazoendelea huwa na masoko finyu hasa kwa kuzingatia uwezo wa ununuzi wa wanaolengwa na bidhaa za viwanda. Katika msingi huu, viwanda vikubwa vitawiwa vigumu kufanya biashara katika mazingira ambako masoko yake ni finyu au utashi wa bidhaa zake sio mkubwa. Viwanda vidogo pia vina uwezo wa kuwaajiri wafanyakazi wengi hasa kwa kuwa havina uwezo wa kugharamia mashine.Uajiri huu wa wafanyakazi wengi ni muhimu katika maeneo mengi ambako tatizo la uajiri ni mojawapo wa matatizo sugu. Tofauti na mataifa ya kitasnia, mataifa yanayoendelea hayana mifumo imara ya kuwakimu watu wasiokuwa na kazi. Utegemezi wa jamaa wanaofanya kazi kwa hivyo unakuwa nyenzo ya pekee ya kuyamudu maisha.

Kuanzisha viwanda vidogo vidogo hakuhitaji mtaji mkubwa tofauti na viwanda vikubwa. Hali hii inasahilisha uwezekano wa watu wengi kujasurisha shughuli yoyote ile. Sambamba na suala hili ni kuwa ni rahisi kujaribisha bidhaa mpya kwa kiwango kidogo cha kiwanda kidogo. Ikiwa mzalishaji yeyote atazalisha bidhaa mpya kwa mapana, kwa mfano kama ilivyo kwa viwanda vikubwa, pana uwezekano wa kupata hasara kubwa. Huenda utashi wa bidhaa hizo uwe mdogo ukilinganishwa na ugavi wa bidhaa zenyewe.

Majaribio mazuri huwa ni kwa kiwango kidogo. Kuwepo kwa viwanda vidogo huwa ni chocheo kubwa la usambazaji wa viwanda hadi maeneo ya mashambani. Hali hii inahakikisha kuwa nafasi za ajira zimesambazwa nchini hali ambayo inasaidia kuhakikisha kuwa pana mweneo mzuri wa kimapato nchini. Mweneo huu wa mapato unachangia katika kuboresha uwezo wa kiununuzi wa umma. Huu ni msingi muhimu wa maendeleo. Upanuzi na ueneaji wa viwanda vidogo vidogo ni msingi mkubwa wa kujitegemea kiuchumi. Aghalabu viwanda vikubwa huegemea kwenye mitaji ya mashirika ya kimataifa na huwa msingi wa kuendelezwa kwa utegemezi wa kiuchumi.

Licha ya faida zake, ueneaji au kutanda kwa viwanda hukabiliwa na matatizo mbalimbali. Tatizo la kwanza linahusiana na mtaji. Lazima pawepo na mbinu nzuri za kuweka akiba ili kuwa na mtaji wa kuanzishia biashara. Njia mojawapo ya kufanya hivi ni kwa kutegemea masoko ya mitaji ambayo katika mataifa mengi hayajaendelezwa vyema. Inakuwa vigumu katika hali hii basi kupata pesa kwa uuzaji wa hisia kwenye masoko hayo.

Tatizo jingine linalotokana na ukosefu wa mikopo ya muda mrefu ya kibiashara kwa wenye viwanda vidogo vidogo. Mikopo ya aina hii huwa muhimu hasa pale ambapo anayehusika ana mradi wa kununua vifaa kama mashine. Mikopo ya muda mfupi inayopatikana kwenye mabenki huweza kuwashinda wengi kutokana na viwango vya riba kuwa juu. Haimkiniki kwa viwanda kama hivi kukopa kutoka nje ya nchi zao. Juhudi za kuendeleza viwanda hivi huweza pia kukwamizwa na tatizo la kawi kama vile umeme. Gharama za umeme huenda ziwe juu sana. Isitoshe, si maeneo yote ambayo yana umeme. Matatizo mengine huhusiana na ukosefu wa maarifa ya kibiashara, ukosefu wa stadi za ujasiriamali au kuwa na ujasiri wa kujiingiza kwenye shughuli Fulani na miundo duni.

Ili kuhakikisha kuwa viwanda vimekuzwa na kuendelezwa pana haja ya kuchukua hatua kadha. Kwanza,

kuwepo na vihamasisho kwa wanaoanzisha viwanda vidogo vidogo kama vile punguzo la kodi, kuhimiza kuanzishwa kwa viwanda vidogo vidogo na kusaka kuyapanua masoko kwa ajili ya bidhaa zinazozalishwa na viwanda hivyo. Aidha kuanzishwa na kupanuliwa kwa taasisi za kuendeleza upanuzi huo. Pana haja ya kuwekeza kwenye rasilimali za kibinadamu; kuelimishwa na kupanua uwezo wao wa kuyaelewa mambo mbalimbali. Miundo msingi haina budi nayo kupanuliwa na kuimarishwa.Upo umuhimu pia wa kuongeza kasima inayotengewa maendeleo na ukuzaji wa viwanda ili kuharakisha maendeleo yake pana umuhimu wa kupambana na ufisadi unaoweza kuwa kikwazo kikubwa. Inahalisi kutambua ikiwa viwanda vitatanda nchini, uchumi wa nchi nao utawanda.

(a) Kwa **maneno 65-75,** eleza ujumbe muhimu unaopatikana katika aya ya pili hadi ya nne.
(alama 8,1 utiririko)

Maandalizi
Jibu

(b) Kwa **maneno (50-55)** fafanua mambo yanayotinga ukuaji wa viwanda. **(alama 5, 1 utirirko)**
Maandalizi
Jibu

MATUMIZI YA LUGHA **(alama 40)**

a) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya ukubwa (alama 2)
Nyuso za vijana wale zilichujuka walipoanguka

b) Tumia **KI** katika sentensi kuonyesha masharti yanayowezekana
(alama 2)

c) Tunga sentensi sahihi ukitumia kitenzi **'abudu'** katika kauli ya kutendesheana
(alama 2)

d) Akifisha (alama 4)
aisee yale mawimbi ya tsunami yaliyotokea bahari hindi yaliangamiza biashara nyingi sana alisema bomet

e) Changanua sentensi hii kwa njia ya mstari.
(alama 4)
Rais alihutubu lakini walimpuuza

f) Huku ukitolea mfano eleza tofauti kati ya kishazi huru na kishazi tegemezi
(alama 3)

g) Ainisha sentensi ifuatayo kwa kuzingatia jukumu lake (alama 2)
Pika ugali kwa kuku kila Jumamosi ukitumia gesi

h) Tunga sentensi moja ya kuonyesha rai (alama 1)

j) i Eleza maana ya chagizo (alama 2)
ii. Bainisha chagizo katika sentensi ifuatayo (alama 1)
Shamba lilipaliliwa haraka na mkulima

k). Andika katika usemi wa taarifa (alama 3)
"Hicho kijicho cha paka cheupe leo marufuku kwangu" alisema Mzee Kambumbu

l) Tunga sentensi moja ukitumia kitenzi kimoja kilichoundwa kutokana na nomino **zawadi**
(alama 2)

m). Tambua matumizi ya kiambishi **ji** katika sentensi ifuatayo
(alama 2)
Jino la jitu hilo lililiwezesha kujilia chakula kingi kuliko mkimbiaji yule

a) Tunga sentensi moja kuonyesha maana ya neno: **ilmradi.**
(alama 2)

b) Andika sentensi moja ukitumia kihisishi cha bezo
(alama 1)

c) Ainisha viambishi katika neno **waliibiana**
(alama 2)

d) Nini maana ya kiimbo? (alama 1)

e) (i) Vokali ni nini? (alama 1)
(ii) Eleza sifa mbili za sauti ifuatayo **/i/** **(**alama 2)

f) Panda ni kuatika mbegu ardhini au kuparaga mti. Andika maana nyingine mbili
(alama 2)

ISIMU JAMII (Alama10)

a. Eleza nadharia tatu kuhusu chimbuko la Kiswahili.
(alama6)

b. Fafanua istilahi zifuatazo: (alama 4)

i. UwiliLugha
ii. LinguaFranka
iii. Misimu
iv. Sajili

MTIHANI WA PAMOJA WA MOKASA
Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari – Kenya
102/3
KISWAHILI
Karatasi ya 3
FASIHI
SEHEMU YA A : USHAIRI

1. **Swali la Lazima**.

Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.

Naujuwa mwanzo wake, vile ulivyochipuza,
Kilofanya mkereke, na kisichowaumiza,
Ya kuwa sepata mke, katu hakuwapendeza,
Nenani mutamaliza, yeye nampenda vivyo !

Mwasema matako hana, yako sawa kama meza,
Tena pua yako pana, kama ya kubandika,
Lakini mimi naona, yenu sitoyasikiza,
Nenani mutamaliza, yeye nampenda vivyo !

Kipita nae pahali, sakubimbi hubwagiza,
Nzitonzito kauli, asengenywazo aziza,
Nywele za kipilipili, hasongi asongomeza,
Nenani mutamaliza, yeye nampenda vivyo !

Munenayo ni mazito, hadi yeye humliza,
Bali kwangu ni matoto, muhali kunichukiza,
Japo miguuye fito, haitoshi mtembeza ?
Nenani mutamaliza, yeye nampenda vivyo !

Nataka watowa khofu, kwa munayo mtangaza,
Si yule mpenda pofu, kawambia ni kengeza,
Ni mwenyewe nimeshufu, muhali kunigeuza,
Nenani mutamaliza, yeye nampenda vivyo !

Tafadhalini mwachie, musilumbe kumaliza,
Unyonge musitumie, kila siku kumaliza,
Haya ni yeye na mie, yawaje mukachagiza,
Nenani mutamaliza, yeye nampenda vivyo !

Hakujiumba mwenyewe, musighafilike wenza,
Aloumba mimi nawe, ndiye aliyemtweza,
Tusijitie kiwewe, tukakufuru muweza,
Nenani mutamaliza, yeye nampenda vivyo !

<u>Maswali</u>

a) Eleza bahari za shairi hili kwa kutoa ithibati kamili (alama 3)
b) Kwa kutoa mifano mwafaka, eleza methali zozote mbili kwenye shairi (alama 4)
c) Bainisha mambo yoyote manne nafsineni anayazungumzia (alama 4)
d) Fafanua idhini ya mshairi (alama 4)
e) Andika ubeti wa tatu kwa lugha tutumbi (alama 3)
f) Eleza maana za vifungu hivi kama vilivyotumika kwenye shairi
   (i) Sakubimbi hubwagiza (alama 1)
   (ii) Musighafilike wenza (alama 1)

SEHEMU YA B : RIWAYA
Said A. Mohamed : *Kidagaa Kimemwozea*
Jibu swali la 2 au la 3

2. 'Alaa ! Mtoto mdogo hata ubwabwa haujakutoka shingoni unakimbilia nini……. ?'
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili
   (alama 4)
   b) Bainisha tamathali mbili za usemi katika dondoo. (alama 2)
   c) Kwa kutoa mifano mitatu, onyesha kwamba kwa hakika ubwabwa ulikuwa umemtoka shingoni anayerejelewa
   (alama 6)
   d) Asasi inayorejelewa katika muktadha huu inakumbwa na matatizo mengi. Kwa kurejelea riwaya nzima, jadili matatizo yoyote manne kwa mifano mwafaka
   (alama 8)
3. Kifo cha Uhuru ni jazanda ya hali ya mambo katika jumuiya ya kidagaa kimemwozea. Thibitisha.
   (alama 20)

SEHEMU YA C : TAMTHILIA

T. Arege : *Mstahiki Meya*

Jibu swali la 4 au 5

4. • • •Nashukuru sasa umeanza kuona mambo yanavyostahili kuenda.
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili
   (alama 4)
   b) Fafanua sifa za msemaji (alama 4)
   c) Eleza umuhimu wa msemewa
   (alama 4)
   d) Jadili jinsi maudhui yoyote manne yanayodokezwa katika dondoo yanavyojitokeza katika tamthilia nzima (alama 8)
5. Tamthilia ya Mstahili Meya ni kiakisi cha mataifa ya ulimwengu wa tatu. Jadili
   (alama 20)

SEHEMU YA D : HADITHI FUPI

K. Walibora na S.A. Mohamed : *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*

Jibu swali la 6 au 7

6. Huku ukitoa mifano maridhawa, onyesha jinsi wanawake wamesawiriwa katika Diwani ya Damu Nyeusi kwa kurejelea hadithi zozote tano.
7. '…..Nimegundua amekuwa akininyima uzuri wa mandhari ya makaburini siku zote hizi.'
   a) Eleza muktadha wa dondoo (alama 4)
   b) Tambua mbinu ya lugha inayojitokeza katika dondoo hili (alama 1)
   c) Huku ukirejelea diwani ya Damu Nyeusi, onyesha jinsi mbinu hii ilivyotumiwa katika hadithi zozote tano (alama 15)

SEHEMU YA E : FASIHI SIMULIZI

8. a) Eleza maana ya maigizo
   (alama 2)
   b) Fafanua dhima tano za michezo ya chekechea
   (alama 10)
   c) Eleza sifa nne za mivigha (alama 8)

MTIHANI WA PAMOJA WA MOKASA 2015
Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari
KISWAHILI
Karatasi ya 1
INSHA
MWONGOZO

1. Kumekuwa na ongezeko la migomo ya wafanyakazi nchini katika siku za hivi karibuni. Wewe ni katibu wa tume iliyobuniwa na rais kuzamia suala hili. Andika ripoti
   Muundo.
- Hii ni insha ya ripoti rasmi.
  Kichwa
- Anwani andikwe kwa herufi kubwa na iwe kamilifu.
- Anwani ibaini kiini cha ripoti(suala kuu linalochunguzwa)
- Bainisha kipindi cha ripoti

2.0 Utangulizi
- Mteuzi
- Haja au sababu
- weka wazi muda ambao uchunguzi ulifaa kuchukuwa
- Wahusika (majina ya wanachama yaorodheshwe kuanzia kwa jina la mwenyekiti).

2.0 Mbinu za kukusanya data
- Kuzuru
- Kuhoji
- Hojaji.

3.0 Matokeo
3.1 mishahara midogo
3.2 mazingira magumu ya kikazi
3.3 ukosefu wa vifaa muhimu vya kazi
3.4 mapendeleo kazini
3.5 uwepo wa sheria/kanuni kandamizi
3.6 Ukosefu wa kandarasi
3.7 Dhuluma za mapenzi
3.8 Ufisadi
3.9 kufutwa /kucheketwa kwa wafanyakazi
3.10 kucheleweshwa kwa marupurupu ya uzeeni

4.0 MAPENDEKEZO
4.1 Pana haja ya kubuni utaratibu wa kuimarisha mishahara ya wafanyakazi
4.2 Washika dau kuhakikisha kuwa mazingira ya kazi ni wezeshi
4.3 Kuwepo kwa vifaa muhimu vya kazi
4.4 Kuwe na hali ambapo wafanyakazi wote wanachukuliwa sawa kazini
4.5 Maadili ya kikazi kuzingatiwa
4.6 Kubuniwa kwa sheria zisizovunja motisha ya wafanyakazi
4.7 Kila mfanyakazi kupewa kandarasi kama njia ya kuonyesha uthabiti wa kazi
4.8 Wafanyakazi wanaostaafu kupewa marupurupu yao kwa wakati ufaao
4.9 Waajiri kukoma kuwafuta/kuwacheketa wafanyakazi kiholela

5.0 Hitimisho
- Ripoti ihitimishwe kwa kufanya rejea ya matokeo ya utafiti
- Jopo lionyeshe namna ambavyo utafiti huu utakuwa wa manufaa kwa taifa kwa jumla hasa katika mchakato wa kupunguza au na kuondoa kabisa migomo ya wafanyakazi nchini.
- Tume idhihirishe wazi kuwa kubuniwa kwake kulikuja kwa wakati unaofaa
- Katibu aonyeshe ni vipi ambavyo utafiti huu utasaidia katika kuzuia migomo katika siku za halafu

Kitambulisho – Ripoti imeandaliwa na;
- Sahihi
- Jina
- Cheo
- Tarehe .

Tanbihi.
1. Asipozingatia muundo wa ripoti aondolewe alama 4 za sura.

Lazima awe na vipengele vinne au zaidi.
2. Hoja zisipungue tano la sivyo atakuwa amepungukiwa kimaudhui.
3. Mtahiniwa atimize urefu wa insha.**(Maneno 400)** Viwango mbalimbali vya urefu vizingatiwe katika kumkadiria mtahiniwa.
4. Jina la mwanafunzi lijitokeze kama katibu la sivyo atakuwa amepungukiwa kimtindo.
5. Atakayeandika ripoti ya kawaida na awe amezungumzia vipengele hivi atakuwa amepotoka – **Atuzwe D 03/ 20.**
6. Atakayekosa kujihusisha katika uandishi wa ripoti atakuwa amejitungia swali. **Atuzwe D – 02/20**

2. Ufisadi umechangia pakubwa kuwepo kwa maendeleo duni nchini. Jadili

Hili ni swali la kujadili. Mtahiniwa anahitajika ashughulikie pande zote mbili za mada.

- Mtahiniwa aweza kukubaliana na mada kuwa kwa kiwango kikubwa maendeleo duni yamechangiwa na ufisadi na kuwepo kwa ufisadi au aonyeshe kuwa si kwa kiwango kikubwa vile kwani kuna sababu nyingine zinazochngia maendeleo duni nchini.
- Kwa vyovyote vile, pande zote za mada zishughulikiwe. Haijailishi kama upande mmoja utakuwa na hoja nyingi kuliko upande mwingine.

Baadhi ya hoja ni:

Kuunga mkono

- Kwa sababu ya hongo, kiasi fulani cha pesa za miradi hutolewa kama hongo. Hali hupunguza kiasi cha pesa za kuteleleza mradi husika.
- Kwa sababu ya ufisadi, utekelezaji wa miradi huwa wa kiwango cha chini.
- Wanaofaa kuhakikisha kuwa kuna viwango vya juu vya utekelezaji wa miradi huhongwa na hivyo kuidhinisha kazi duni.
- Kandarasi za miradi ya maendeleo hutolewa kwa wanakandarasi fisadi ambao pengine hawana ujuzi katika kufanikinisha mradi husika au ambao watatumia vifaa duni ili faida yao iwe kubwa.
- Wafadhili hukataa kuipa nchi pesa za kufadhili miradi fulani kwa hofu ya pesa hizo kutumika vibaya, hivyo basi miradi mingi haipati pesa za kutosha.
- Kuna ubadhirifu wa pesa za miradi na wanaosimamia hazina za maendeleo hivyo kuinyima miradi ya maendeleo pesa zinazohitajika.

Kupinga

- Hakuna pesa za kutosha nchini za kufadhili miradi mingi ya maendeleo.
- Utekelezaji mbaya wa miradi waweza kutokana na ukosefu wa vifaa bora nchini kwa hivyo vinavyotumiwa vikawa na matokeo duni.
- Kwa sababu ya siasa, miradi ya maendeleo ikatelezwa visivyo hasa katika sehemu ambayo ni ngome ya mpinzani.
- Wakati mwingine pesa za kutekeleza miradi hutumika kununulia vitu kama magari, kulipa mishahara, kulipa marupurupu nk badala ya kugharamia miradi.

TANBIHI

Zingatia hoja zozote nyingine mwafaka.

3. Baniani mbaya kiatu chake dawa.

Maana.kiatu cha baniani ni kitu au kundi la watu limechukia au kudharau

Dawa: Kitu husika huendakikawa ndicho jibu au jawabu au suluhisho kwa tatizo fulani maishaninmwa mtu au katika jamii

Mtahiniwa aandike kisa kuthibitishabmatumizi haya ya methali

Mtahiniwa nyingine zenye maana sawa ni;

- Matango na matikiti ndio maponya nja
- Wembamba wa reli gari moshi hupita
- Nyumba nzuri si mlango fungua uingie

Utuzaji

(i) Pande zote za methali zishughulikiwe.Anayeshughulikia upande moja asipite alama C 08/20
Anayetaja tu upande wa pili bila maelezo kikamilifu achukuliwe kuwa amelenga lakini ana udhaifu wa maudhui

(ii) Anayekosa kulenga katika kisa chake amepotoka kimaudhui alama D 03/20

Swali la nne

Mtahiniwa ahitimishe insha yake kwa maneno aliyopewa
Kisa chake kifungamane na mawazo ya kauli aliyopewa
Kisa kilenga tukio lilizua taharuki miongoni mwa wahusika
Tukio lenyewe lazima lidhiirishe maafa /maangamizi

Lazima litokee kwenye sehemu iliyozingirwa kama vile ndani ya nyumba,katika gari n.k
Mtahiniwa atumie nafsi ya tatu hali ya wingi(warejelewa)
Atumie wakati uliopita.

MOKASA 2015
102/2
MWONGOZO
UFAHAMU

(a) Changamoto za Ugatuzi/Matatatizo ya ugatuzi/Ugatuzi **(alama 1x1=01)**
(b)
- Ugatuzi ni mfumo geni. **(Alama 3x1=03)**
- Serikali kuu kutowajibika
- Kudai kuwa mfumo huu unahitaji mda zaidi

(c)
- Mfumo wa ugatuzi nchini umehusishwa matendo ya kibepari kama vile; **(alama 3x1=03)**
- Raia kupewa mzigo wa kulipa ushuru ili kuipa serikali mapato
- ushuru ndio njia kubwa ya kuzalisha mapato ya serikali zinazojifunga na mfumo wa kimagharibi wa kiuchumi
- viongozi kuwanyoya raia walio maskini

(d)
- Hali mbaya ya muundo msingi **(alama 4x1=04)**
- Viongozi kuendeleza ufisadi
- Ukosefu wa usawa katika ugavi wa rasilimali
- Viongozi kupuuza mchango wa wananchi

(e)
- Raia kulazimishwa kulipa ili kuona maiti za jamaa zao katika fuo **(alama 2x1=02)**
- Raia kurundikiziwa mzigo wa kulipa ushuru mkubwa
- Ushuru unaolipwa na wananchi hauwasaidii wananchi ila huishia mifukoni mwa viongozi

(f) (i) Ugavi wa mamlaka na rasilimali kutoka serikali kuu hadi mashinani **(alama 2x1=02)**
(ii)mfumo wa kiuchumi wa watu wachache kumiliki rasilimali kwa kuwapora wengine
Ondoa nusu alama kwa kila kosa la sarufi hadi makosa sita.
Ondoa nusu alama kwa kila kosa la tahajia hadi makosa sita.

UFUPISHO

(a)
- Nchi zinazoendelea huwa na masoko finyu
- Viwanda vikubwa hupata ugumu kufanya biashara katika masoko finyu
- Viwanda vidogo vinaweza kuwaajiri wafanyakazi wengi
- Kuanzisha viwanda hakuhitaji mtaji mkubwa
- Ni rahisi kujaribisha bidhaa katika kiwango kidogo cha kiwanda kidogo
- Viwanda vidogo huchochea usambazaji wa viwanda mashambani
- Hii husababisha ajira kusambazwa nchini
- Usambazaji huleta mweneo wa mapato kote nchini
- Huu ni msingi wa maendeleo
- Viwanda vidogo ni msingi wa kujitegemea kiuchumi

(b)
- Tatizo la kwanza ni mtaji.
- Ukosefu wa mikopo ya muda mrefu
- Mikopo ya muda mfupi inatozwa riba kubwa
- Lipo tatizo kubwa la kawi
- Gharama ya umeme huenda iwe ya juu
- Ukosefu wa maarifa ya kibiashara na ujasiriamali

M a – 8 s – 6 x ½ = 03
b – 5 h – 6 x ½ = 03
ut – 2 z – maneno 10 1z

MATUMIZI YA LUGHA

a) Majuso ya majijana yale yalichujuka yalipoanguka (4x ½)
b) Akisoma kwa bidii, atapita mtihani 2x1=02
Akirauka mapema,atapata basi
(lazima pawepo na vitenzi viwili)
c) Abudu-Abudishiana 1x2=02
Mf Wapenzi wale waliabudishiana baada ya kufunga nikahi.
d) "Aisee! Yale mawimbi ya Tsunami (yaliyotokea Bahari HIndi) yaliangamiza biashara nyingi sana."
Alisema Bomet. (Vitahiniwa 8x ½ =04)
e) S__S1+U+S2
S1__KN+KT
KN__N
N__Rais
KT__T
T__Alihutubu
U__lakini
S2__KN+KT
KN__O
KT__T
T__Walimpuuza**. 8x ½**

f) Kishazi huru hutoa maana iliyokamilika. Ni sentensi sahihi (alama 3)
Kishazi tegemezinhutoa maana isiyokamilika na hivyo hutegemea kingine kukamilika kimaana
Mf. Ingawa alifunza vizuri,walifeli mtihani.
k.t k.h
g) Ni sentensi agizi (ya masharti) 2x1=02
Au
Ni sentensi ya kuamuru (ya masharti)
h) K.m Kaondokeni (kadiria) 1x1=01
i) (i) chagizo-neno/maneno ambayo huchukua nafasi ya kielezi katika sentensi. (2x1=02)
Kikiondolewa hakiathiri maana ya sentensi
(ii) chagizo- Haraka (1x1=01)
j) Mzee Kambumbu alisema kuwa kile kijicho cha paka cheupe, siku hiyo kingekuwa marufuku kwake. (6x ½ =03)
k) Zawadi(N)- zawidi(T)
k.m Alizawidiwa kwa kupasi mtihani (1x2=02)
l) Jino Ngeli ya LI-YA (4x ½)
i. Jitu-ukubwa/uduni wa kitu
ii. Kujilia-kirejeshi/kujirejelea
iii. Mkimbiaji-mazoea/uzoefu
m) Ilimradi-ili,iwapo,kwa masharti kwamba,mradi. (Alama 1x2=02)
Mf. Nitaruka maji ilimradi nipewe zawadi
n) Kihisishi cha bezo k.m mmm! Po! Nyoo! Mnh! Ngoo! Mawe! Ebo! Wapi! Zii! Aka! 1x1=01
o) Wa- nafsi (alama 4x ½ =02)
li-wakati uliopita
an-kauli ya kutendana
a-tamati
p) Kiimbo-ni kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti wakati wa utamkaji (alama 1x1=01)
Ni kiwango cha utoaji wa sauti kutegemea ujuu na uchini wake unaowezesha kupata tofauti za hisia za msemaji
q) (i) Vokali- ni sauti zinazotamkwa hewa inapotolewa bila kikwazo/kuzuiliwa (alama 1x1=01)
(ii) /i/ ni sauti ya mbele ya kinywa (alama 2x 1 =02)
Ni sauti ya juu ya kinywa
Midomo hutandazika inapotamkwa
r) Kugawika kwa njia (Alama 2x1=02)
Ingia katika chombo cha kusafiria
Paji la uso
Pembe kubwa inayopigwa nchani
Manati/chombo cha kurushia mawe

ISIMUJAMII

a)

- Kiswahili ni lugha ya Kibantu - Lugha ya Kiswahili ina maneno mengi ya Kibantu hivyo basi chimbuko lake ni Kibantu.
- Kiswahili imetokana na lugha ya Kiarabu - Lugha hii ina maneno kadha ya Kiarabu. Hii yaonyesha kuwa ni lugha ya Kiarabu.
- Kiswahili ilitokana na mchanganyiko wa lugha ya Kibantu na Kiarabu - Maneno mengi ya Kiswahili yana asili ya aidha Kibantu ama Kiarabu. Hii yaonyesha kuwa lugha hii ni uzawa wa lugha hizi mbili. (Hoja 3 x 2 = 6)

b)

- Uwili lugha- uwezo wa mtu kuzungumza lugha mbili
- Lingua Franka- lugha inayounana na mazingirganisha watu wanaozungunza lugha tofauti
- Misimu- semi za mda zinazotumika na kikundi fulani cha watu na hutoweka kwa baada ya mda.
- Sajili- matumizi ya lugha kulingana na mazingira 4x1=04

<u>Jinsi ya kusahihisha matumizi ya Lugha</u>

- Ondoa nusu ($^1/_2$) kwa kila kosa la sarufi (s) litokeapo kwa mara ya kwanza kwa kila kijisehemu lakini isipite nusu ya alama alizopata katika kijisehemu hicho.
- Ondoa nusu alama ($^1/_2$) kwa kila kosa la tahajia (h) litokeapo mara ya kwanza hadi makosa sita katika swali lote yaani: *(6 x ½ = 03)*

<u>Jinsi ya kusahihisha Isimu Jamii</u>

- Ondoa nusu (½)alama kwa kila kosa la sarufi (s)litokeapo kwa mara ya kwanza kwa kila kijisehemu lakini isipite nusu ya alama alizopata (si alizotengewa) katika kijisehemu hicho.
- Ondoa nusu (½) alama kwa kila kosa la hijai (h) litokeapo kwa mara ya kwanza hadi makosa sita yaani *(6 x $^1/_2$ =03)*

MTIHANI WA PAMOJA WA MOKASA - 2015
KISWAHILI
102/3
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

1. **Shairi**
   a) Bahari za shairi
- Tarbia – Lina mishororo 4 katika kila ubeti
- Mathnawi – Lina pande 2 katika kila mshororo
- Ukara – Vina vya nje vinatiririka ilhali vya ndani havitiririki. (zozote 3 x 1 = 3)

   b) Methali
   (i) Akipenda, kipofu huita kengeza (ubeti wa tano)
- Mwenyewe amemkubali alivyo na hawawezi kumgeuza ingawa wanamsengenya.

   ii) Aliyekupa wewe kiti ndiye aliyenipa mimi kumbi (ubeti wa saba)
- Hakuna aliyejiumba hivyo waache kusema udhaifu wake.

   iii) Pilipili usiyoila yakuashani? (ubeti wa 6 mStari wa 3)
   (zozote 2 x 2 = 4)

   c) Maudhui
- Msimulizi anampenda vile alivyo – mwenyewe amemkubali
- Wanakerwa kwani hawana mke
- Wanayoyasema hayawahusu wao bali ni kati yake na yeye
- Anayezungumziwa hakujiumba mwenyewe bali ni mungu (muumba)
- Anawaambia wasitumie udhaifu wake kumsengenya
- Ingawa wanayoyasema yanamliza Aziza, yeye hajali.
- Wadaku wanatahadharishwa wasikufuru (zozote 4 x 1 = 4)

   d) Uhuru/idhini ya mshairi
- Tabdila k.m. nae – naye
- Mutafanya – mtafanya
- Inkisari k.m kilofanya – kilichofanya
- Nampenda – ninampenda
- Kuboronga sarufi k.m – Hadi yeye humliza – hadi humliza yeye
- Lahaja k.m naujuwa – naujua
- Khofu – hofu (zozote 2 x 2 = 4)

   e) Lugha nathari/tutumbi
- Nikipita naye popote wadaku/wafitini wanamsengenya Aziza kwa maneno mazito k.m kuwa hatengenezi nywele. Semeni tu mtasita (au mtaacha) mjue mimi ninampenda alivyo) (3 x 1 = 3)

   Au

   Msimulizi anasema kuwa akienda na Aziza popote wadaku wanatoa maneno mazito ya kumsengenya k.m hatengenezi nywele. Anawaeleza waendelee tu bali yeye anampenda alivyo. (3 x 1 = 3)

f)
   (i) Sakubimbi hubwagiza – wadaku (wasengenyaji hutupa maneno ovyo).
   (ii) Musighafilike wenza – msiumie/msighadhabike (2 x 1 = 2)

2. **Riwaya**
   a)
- Ni maneno ya muuguzi
- Alikuwa anamweleza Imani
- Wako katika zahanati ya Nasaba Bora
- Imani na Amani walikuwa wamempeleka kitoto Uhuru zahanatini anapokuwa mgonjwa ndipo muuguzi anamwuuliza sababu za kuzaa mapema. (4 x 1 = 4)

   b) (i) Nidaa k.m Alaa!
   (ii) Msemo/kitendawili k.m Ubwabwa haujakutoka shingoni (zozote 2 x 1 = 2)

   c)
- Imani alivunja mwiko kwa kunywa maji ya mto kiberenge akiwa na Amani.
- Kama mtu mzima, Imani aliwapenda na kuwalea watoto walemavu kwa kuwaonyesha imani.
- Anajitolea kama mtu mzima kumlea kitoto Uhuru kwani alitambua kuwa Amani hangeweza.
- Imani alikuwa mtambuzi kama mtu mzima kwa kueleza kisa chake ili kumshinikiza Amani kujieleza Pasi na kusisitiza.

- Imani alikuwa mwerevu na alitambua wakati unaofaa kumweleza Amani kisa cha nduguye kwa kusema haifai kupelekea kilio matangani.

(zozote 3 x 2 = 6)

d) Asasi ya kimatibabu/zahanati/afya

- Uzembe/uvivu kazini k.m wauguzi wanafuma fulana kazini.
- Kutowajibika kazini k.m wauguzi wanadai kuwa hawangemtibu Uhuru kwa sababu ni sikukuu/siku ya sherehe.
- Huduma hafifu/mbovu k.m D.J anakimbilia daktari wa kienyeji ilhali kuna zahanati.
- Ufisadi/wizi k.m Mtemi Nasaba Bora walipewa pesa za kujenga hospitali lakini wakaiba kiasi fulani cha pesa hizo, hivyo kujenga zahanati tu. (zozote 4 x 2 = 8)

3. Kifo cha Uhuru ni jazanda ya hali ya mambo katika jumuiya ya Kidagaa Kimemwozea.

- Uhuru haumo katika jumuiya hii kwani ulitoweka/ulikufa punde baada ya mkoloni kuutoa na kuondoka ifuatavyo.
- Wafanyakazi hawana haki Mtemi Nasaba Bora anawafuta kazi apendavyo, wanalipwa mshahara duni mfano DJ na kupigwa k.m Amani.
- Ajira ya watoto ambao wanapaswa kuwa shuleni inaendelezwa, mfano DJ na wenzake ni wachunga mifugo, Imani anaajiriwa nyumbani kwa majisifu.
- Waandishi chipukizi kwa mfano Amani wanatapeliwa miswada yao na wahariri kama vile majisifu.
- Watu wasio na hatia wanatiwa mbaroni kwa makosa ya kusingiziwa kwa mfano Yusufu, Amani, Imani na Matuko weye.
- Walemavu wanadunishwa na kufungiwa wasipate malezi yanayowastahiki.
- Maskini wanalazimishwa kuchangia masomo ya watoto wa matajiri kwa mfano masomo ya Madhubuti kule urusi.
- Wanawake wanadhulumiwa na wanaume. Kwa mfano, Mtemi Nasaba Bora kumpiga Zuhura kwa kimsingizia kuwa na jicho la nje. Nasaba Bora kumshurutisha Lowela kufunga mimba kwa kamba na kumnyang'anya kitoto chake Uhuru.
- Kifo cha Uhuru kusababisha kutiwa mbaroni kwa Amani na Imani ilhali waliosababisha kifo chake ni wauguzi kwa kukataa kumpa matibabu na Mtemi Nasaba Bora aliyemtupa mlangoni pa Amani pasi na kujali baridi.
- Mtemi Nasaba Bora kunyakua mashamba ya watu wengine kwa kughushi faili k.m la chichiri Hamadi, mwinyihatibu Mtembezi n.k.
- Mauaji ya wanatomoko ndipo mali yao iweze kutwaliwa – mamake Imani na Chichiri Hamadi.
- Mashujaa wa kweli wa Tomoko kama vile Matuko Weye na chwechwe makweche kutotambuliwa badala yake matuko anaishi maisha ya kimaskini na kuhangaishwa kwa kutiwa selini ilhali chwechwe makweche anaoza fupaja likakatwa na kulazimika kurudi kijijini.
- Haki ya wanafunzi kusoma kukiukwa majisifu haendi darasani ila mtindini. Wasichana wanafunzi wanapachikwa mimba na walimu kwa mfano Fao anampachika mwanafunzi mimba na hachukuliwi hatua yoyote.
- Wauguzi kukiuka haki ya wagonjwa kupata matibabu kwa mfano Uhuru, Amani na DJ.
- Viongozi kutoa hotuba zao katika lugha ya kiingereza isiyoeleweka kwa raia wengi badala ya Kiswahili. Hotuba ya Rais wa Tomoko inaandikwa kwa kiingereza na kusomwa na Mtemi Nasaba Bora kwa umati usioelewa.
- Wanatomoko kulazimishwa na Askari kuhudhuria sherehe za siku ya wazalendo ambako wanachomwa na jua na kunyeshewa.
- Picha ya Mtemi Nasaba Bora kutokea katika gazeti la Tomoko kwa sababu majisifu; nduguye ndiye mhariri. (Badala ya usawa kuna unasaba).
- Mtemi Nasaba Bora kuwataka raia kuchanja mbwa ilhali hawachanji wake.
- Raia wengi wa Tomoko hawana rasilmali ya shamba inayomilikiwa na wachache k.m DJ. Amani, Imani, Weye n.k (Hoja zozote 10 x 2 = 20)

4.

a) i) Mzungumzaji ni Bili
   ii) Anamwambia meya sosi
   iii) Wako ofisini mwa Meya
   iv) Wanazungumza kuhusu mpango wa kumnyang'anya mwanakandarasi kandarasi yake kumshinikiza kwenda mahakamani kisha wapate mgao wao. (zozote 4 x 1 = 4)

b) **Sifa za Bili**

- Ni fisadi k.m Anamhimiza meya kupeleka kesi mahakamani ilia pate mgao wake.
- Mpenda anasa k.m wanaenda mkahawa wa kajifahani kujistarehesha
- Laghai/mnafiki k.m anamtoroka meya mambo yanapoharibika
- Mjanja k.m Anadai dawa ya adui ni kummegea unachokula.
- Barakala k.m anamdanganya meya kuwa yuko Pale kwa ajili yake (uk 28)
- Mbinafsi k.m anamweleza meya asimsahau na pia Tumbo ndilo muhimu. (zozote 4 x 1 = 4)

c) **Umuhimu wa meya**

- Anadhihirisha athari za utawala mbaya
- Tunaona mchango wa vibaraka wanaopotosha viongozi (ushauri mbaya)
- Kupitia kwake tunatambua tabia za wahusika wengine kama Siki, Bili n.k.
- Anaendeleza maudhui ya udhalimu, utegemezi, ukoloni mamboleo n.k (zozote 4 x 1 = 4)

d)

- Ubadhirifu wa mali – Meya na Bili wanakwenda kujistarehesha
  Bili analipwa kushauri meya ilhali si mfanyakazi wa baraza
- Ubinafsi – Bili anasema jina si kitu bali tumbo ndilo muhimu.
- Uongozi mbaya – Meya anaongezea baraza nakisi ya pesa,Kuna migomo mingi cheneo.
- Ufisadi – Bili ananfanya mpango wa kuiba fimbo ya meya
  Mtu anayang'anywa kandarasi yake kwa madai kuwa ni meya mwingine aliyempa kandarasi hiyo.
  (zozote 4 x 2 = 8)
  (Tathmini hoja nyingine).

5. Tamthilia ya Mstahiki Meya inaafiki mataifa ya Afrika kwa sababu matukio mengi katika kitabu ni sawa na yale yanayotokea katika mataifa mengi.
   1. Ufisadi
   2. Umaskini
   3. Ukoloni mamboleo
   4. Ukosefu wa dawa hospitalini
   5. Ukosefu wa lishe bora
   6. Utegemezi wa misaada
   7. Ukaragosi
   8. Uongozi mbaya
   9. Vitisho
   10. Propaganda
   11. Matumizi mabaya ya vyombo vya dola.
   12. Kutowajibika kwa viongozi
   13. Mishahara duni
   14. Ubadhirifu wa mali
   15. Unafiki wa kidini
   16. Ushauri mbaya
   17. Ujinga wa wananchi kuwachagua viongozi wabaya.
   18. Uzalendo wa kijinga
   19. Mapinduzi
   20. Wafanya kazi kujiuzulu.
   21. Ukosefu wa maji safi
   22. Uundaji wa kamati zisizowajibika.
   23. Matumizi mabaya ya wanakandarasi
   24. Uchafuzi wa mazingira.

   (zozote 10 x 2 = 20)

   (Maelezo ni lazima. Mwanafunzi arejelee kutoka katika tamthilia)

6. **Mke Wangu**

- Ni wawajibikaji. Aziza alitaka ajifulie nguo, ajipikie na ajioshee vyombo.
- Wepesi wa hasira. Aziza alikasirika sana mume wake alipotamaniwa na Seluwa.
- Ni washamba. Aziza alikataa kuvaa viatu kwa madai kuwa ni ngozi ya ngombe aliyekufa.
- Ni wadaku k.m Seluwa alikuwa na kidomo.

Samaki wa Nchi za Joto

- Wenye bidii. Miriam na Christine waliweza kusoma hadi chuo kikuu cha Makerere kutokana na bidii yao.
- Wapenda anasa. Christine na Miriam walishiriki ulevi walipokuwa kwa Peter.
- Katili. Christine aliavya mimba

- Wajinga. Christine alishiriki ngono na Peter huku akidhani kuwa Peter alimpenda ilhali hawakuwa wamejadili chochote kuhusu uhusiano wao.

Damu Nyeusi

- Ni asherati. Fiona alitaka kujuana kimwili na Fikirini licha ya kutokuwa na uhusiano wowote kati yao Uk. 26. Do you want some good time?
- Ni laghai/matapeli. Fiona alimdanganya Fikirini alitaka kumbeba kwa gari lake.
- Ni katili. Fiona alitaka Bob amwue Fikirini kwa kumpiga risasi.
- Ni mwongo. Fiona alidai Fikirini alitaka kumnajisi.

Gilasi ya Mwisho Makaburini.

- Ni watani k.m. Asha anamtania Msoi
- Wapenda anasa. Asha na Josephina walikuwa wapenda anasa kwani kila wikendi walienda kwenye baa ya makaburini (exortic resort) ili kunywa na kula.
- Ni wawajibikaji. Asha na Msoi wanapofika kwa Msoi baada ya kutoroka kutoka kwenye baa ya makaburini, Asha alikwenda kupika chai.
- Ni washawishi k.m Asha anamshawishi Msoi kwenda kucheza.

Kikaza

- Ni wawajibikaji. Kina mama waliowahi mapema kwa mzee Babu walielekea moja kwa moja jikoni na kuandaa chai, uji na mihogo.
- Ni wachochezi. Bi Cherehani aliwachochea wanatekede kwenda Ikuluni na kumng'oa Bw. Mtajika kutoka uongozini.
- Ni wenye umoja na ushirikiano. Walishiriki katika ushonaji wa kikaza
- Wanajigamba k.m Bi. Mtajika anasema hakuna kiongozi kuliko yeye

(Wenye maringo) (zozote 5 x 4 = 20)

(Tathmini hadithi nyingine).

7.

a)

- Msemaji ni Msoi
- Alikuwa anamwambia Asha na Josephina
- Walikuwa katika baa ya Makaburini
- Msoi na Semkwa walifika kwenye baa na kuwakuta Asha na Josephina
- Msoi kwa kawaida alikaa kuyapa mava mgongo. Mara hii alikaa kuyatazama mava.
- Asha alitaka kujua kwa nini Msoi hakutaka kukaa mahali pake pa kawaida.

(zozote 4 x 1 = 04)

b) Mbinu ya kinaya (alama 1)

c)

I Mke Wangu

- Ni kinaya msimulizi anaona ndoa zao waliosoma zitavunjika hivyo anaamua kuoa mke asiyesoma lakini ndoa yake pia inavunjika.
- Ni kinaya kwa Aziza kumwita muuza madafu mumewe ilhali msimulizi ni mumewe.
- Msimulizi amesoma lakini bado anawategemea wazazi wake.

II Maskini, Babu Yangu

- Babu Maende anakutana na kifo chake baada ya kupona ugonjwa uliomleta mjini.
- Babake msimulizi ni mrakibu wa polisi ilhali babake mzazi anauawa na raia.
- Hata baada ya nchi kupata Uhuru, bado walikuwapo watu walioishi katika umaskini mkubwa.

III Samaki wa Nchi za Joto

- Christine anaona heri kuolewa katika familia ya kitajiri kuliko kufanya kazi ya serikali.
- Peter anadharau mkahawa mmoja mchafu ilhali alitoka familia duni huko cockney.
- Margaret anamshauri Christine dhidi ya kupata mimba lakini anampa dawa za kuzuia mimba.

IV Damu Nyeusi

- Bob anasema waafrika wameenda marekani kuwasumbua ilhali mwenyewe alikuwa mtu mweusi.
- Bob alivalia miwani ya jua ndani ya nyumba.

– Ni kinaya kuwa Fiona anamwita Fikirini ndugu lakini ndiye anamwiba tena.

V Tazamana na Mauti

– Crusoe ni mzee lakini Lucy anafariki kabla yake
– Lucy hakutosheka alipofika London bali tamaa yake ilizidi
– Ni kinaya Lucy kufariki baada ya kukabidhiwa mali. (zozote 5 x 3 = 15)

8.

a) Hii ni Sanaa ya mazungumzo ambayo huambatana na matendo. Wahusika huiga tabia, maneno au matendo ya watu wengine katika jamii kwa nia ya kuburudisha au kupitisha ujumbe fulani. (Maelezo kamilifu 2x1=2)

b) Umuhimu wa michezo ya watoto.

– Hukuza kipawa cha uigizaji.
– Hukuza ubunifu
– Ni njia ya kukashifu vitendo visivyofaa katika jamii.
– Huonyesha falsafa ya jamii kuhusu majukumu mbalimbali ya kijamii mfano (baba na mama) – kuonyesha majukumu yao katika jamii.
– Hukuza ukakamavu miongoni mwa watoto ambao huimarika wakuapo. *(Hoja zozote 5x2=10)*

c) Sifa za miviga

– Huandamana na matendo na kanuni fulani maalum kama vile ulaji wa kiapo, kupiga magoti, maapizo n.k.
– Huongozwa na watu mahususi katika jamii.
– Huandamana na utoaji wa mawaidha.
– Hufanyiwa mahali mahususi kwa mfano porini, msituni, pangoni, madhabahuni n.k.
– Huambatana na utamadamu wa jamii husika kwa mfano, ngoma, ulumbi, mawaidha n.k *(Hoja zozote 4x2=8)*

MTIHANI WA PAMOJA WA MAJARIBIO - KASSU
Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari
102/1
KISWAHILI
Karatasi ya 1

1. Wewe ni balozi mteule wa nchi yako katika nchi ya kigeni. Andika tawasifu utakayotoa katika siku ya kutoa stakabadhi zako kwa rais wa nchi uliyoteuliwa kuwa balozi.
2. Utumizi wa afyuni[mihadarati} katika taasisi za masomo nchini ni suala ambalo ni muhali kutatuliwa. Jadili.

3. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali: Mwenye kovu usidhani kapoa.
4. Andika kisa kitakachomalizikia kwa: ... hivyo ndivyo ukurasa mpya katika kitabu cha maisha yangu ulivyofunguka.

MTIHANI WA PAMOJA KASSU
Kiswahili
Karatasi ya 2
Lugha

1. **UFAHAMU**
   Soma taarifa ifuatayo kasha ujibu maswali.
   Historia ya katiba
   Katiba ni utaratibu wa sheria unaoweka mpango wa jamii kuendesha mambo.Ni muhimu kila raia ajue katiba ya nchi yake.

   Katiba yaweza kuwa imeandikwa au haikuandikwa. Katika jamii za jadi, katiba ilihifadhiwa na kupokezwa kwa mdomo. Mtindo wa kuandika katiba ulianza nchini Marekani mwaka 1787. Ingawa katiba hii imefanyiwa mabadiliko hapa na pale,bado ni ileile. Kenya ilipowekwa chini ya himaya ya Uingereza mwaka 1895, ilianza kutumia katiba ya Uingereza. Baada ya masetla wa kikoloni kujikita, Kenya kuwa koloni. Hii ililazimu pawe na katiba nyingine mwaka 1920. Waafrika waliupinga mfumo huu kwa sababu haukuwahusisha kikamilifu kwenye masuala ya uongozi. Utetezi wa wanasiasa uliilazimisha serikali ya Uingereza kuitisha makongamano mbalimbali kama vile lile la Devonshire na mengine ili kurekebisha katiba. Waafrika hawakuridhika. Wakaendelea kudai katiba mwafaka. Harakati hizi zilileta kuitishwa kwa kongamano la katiba la Lancaster. Lengo lilikuwa kuandika katiba itakayotumiwa nchini hadi leo. Kati ya wajumbe walioenda Uingereza kuandika katiba mwaka 1962 ni pamoja na Tom Mboya, Jean Marie Seroney, Julius Kiano, Jomo Kenyatta, Masinde Muliro, Oginga Odinga, Ronald Ngala, Daniel Arap Moi na James Gichuru. Wengine ni Martin Shikuku, Dennis Akumu, Taita Towett, Abdilahi Nassir, Jeremiah Nyaga na John Keen.

   Katiba ni kitovu cha taifa. Baina ya mambo inayotekeleza ni kuweka utaratibu na kanuni za utawala, kwa mfano, utawala wa kimikoa na serikali za wilaya. Pamoja na haya, katiba hufafanua vyombo vikuu vya serikali ,mamlaka yavyo na mipaka yavyo ya kutenda. Vyombo hivi ni bunge, mahakama, urais, jeshi n.k. Hali kadhalika, katiba hupambanua haki za raia.

   Hii hudumisha demokrasia na huwawezesha wananchi kupata uhuru na haki za kimsingi. Katiba hukinga haki za kila raia, hasa kutokana na udhalimu wa wengi au wenye uwezo mkubwa. Zaidi ya yote, katiba huimarisha asasi za umma ili kudumisha uwajibikaji.

   Katiba huhalalishwa na watawaliwa. Hii hutokea wanaposhirikishwa katika uandishi wake. Kuanzia miaka ya themanini, raia walianza kudai katiba igeuzwe. Mwamko wa kutaka mageuzi ulianza kwa harakati za kubadilisha mfumo wa kisiasa kutoka ule wa chama kimoja hadi ule wa demokrasia ya vyama vingi. Haja ya mfumo mpya wa kisiasa ulilenga kuwashirikisha wananchi katika utawala na kuondoa uimla.

   Harakati zilitia fora miaka ya tisini. Mambo yaliyochochea hali hii ni mengi. Kwanza, katiba iliyokuwa imeandikwa na watu wachache ilikuwa imefanyiwa marekebisho mengi. Marekebisho haya yalimpa rais mamlaka mengi juu ya serikali kuu na vyombo tofauti vya serikali. Pili, viongozi na watu wenye uwezo na utajiri walipuuza katiba. Raia walihisi wanadhulumiwa. Walipinga hali ya wachache waliomzunguka rais kunufaika huku umma ukitengwa. Tatu, kutokana na uongozi uliokuweko wakati huo, wanawake,

watoto na walemavu walidhulumiwa na kukosa uwakilishi ufaao.Hatimaye, pakawa na ongezeko la uharibifu wa mazingira, ufisadi na unyakuzi wa mali ya umma kama vile ardhi.

Waliopigania katiba mpya walikuwa na haja ya katiba ambayo uandikaji wake ungewahusisha Wakenya wote. Mwanzoni, serikali ilipinga wito wa mabadiliko. Lakini mnamo mwaka 2001 iliunda Tume ya Marekebisho ya Katiba ili kutekeleza mahitaji ya wananchi. Tume hii iliwahamasisha na kuwashawishi raia kutoa maoni. Tume iliandaa vikao katika maeneo ya ubunge 210 ambapo wananchi walitoa mapendekezo kuhusu marekebisho ya katiba waliyotaka.

Katika mapendekezo hayo raia walisisitiza mambo kadhaa. Jambo la kwanza ni utawala mwema na uwajibikaji wa viongozi na maafisa wa umma .Jambo lingine ni kulinda haki za binadamu zikiwemo za wanawake, watoto na walemavu. Raia walidai kanuni za usawa na ulinganifu. Aidha walitilia mkazo mahitaji ya msingi kama chakula, afya nzuri, makao, elimu, usalama, uchumi, na kadhalika.

Msingi wa mapendekezo hayo yote ni kuwepo na amani ya kitaifa, umoja na uadilifu ili kulinda maslahi ya wananchi wote na taifa.

Maswali :

(a) Eleza kilichosababisha kongamano la katiba la Lancaster
(alama3)
(b) Taja mambo matatu yaliyotiliwa mkazo na raia katika maoni yao kuhusu katiba.
(alama3)
(c) Eleza umuhimu wa katiba kwa mujibu wa taarifa.
(alama3)
(d) Taja sababu zilizochangia ubadilishaji wa katiba.
(alama3)
(e) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika taarifa.
(alama3)
(i) Kitovu
(ii) Harakati
(iii) Hamasisha

2. UFUPISHO

Soma makala haya kisha ujibu maswali yanayofuata.

Lugha ya Kiswahili ni lugha iliyoendelea sana. Leo hii lugha hii inasemwa na watu wote nchini Tanzania, Rwanda,Burundi, nchini Kenya, Nchini Uganda, Zaire, Malawi, msumbiji, Zambia, Somalia, Bukini (Madagascar) na Ngazija (Comoro), inasemwa na asilimia kubwa ya wananchi wa huko. Aidha lugha hii ina wasemaji si haba katika kisiwa cha Soktana nchini Oman.

Fauka ya maendeleo haya, Kiswahili kinatumika kwa minajili ya matangazo ya habari katika idhaa nyingi za mashirika ya habari ulimwenguni. Nchi zenye idhaa za Kiswahili ni kama vile hizi zetu za Afrika ya Mashariki na kati, Afrika ya kusini, Nigeria, Ghana, Uingereza, (shirika la B.B.C) Marekani (shirika la V.O.A), Ujerumani (shirika la Radio DeutchWelle, Cologne), Urusi (Radio Moscow), China, India nakadhalika.

Maendeleo mengine yanapatikana katika upande wa elimu. Marekani peke yake, kuna vyuo zaidi ya mia moja vinavyofundisha Kiswahili kama lugha muhimu ya kigeni. Huko Uingereza vyuo kama London, Carmbridge na Oxford vinafundisha lugha hii. Nchi nyingine ambazo zina vyuo vinavyofunza lugha ya Kiswahili ni kama vile Japan, Korea, Ghana, Nigeria na kadhalika.

Kweli Kiswahili kimeendelea jamani. Lakini je, kilianza vipi? Na ilikuwaje kikaweza kupiga hatua hizi zote?

Kiswahili kilianza kuzungumzwa na kabila dogo la watu walio kuwa wakiitwa wangozi. Watu hawa walikuwa wakiishi mahali palipoitwa shungwaya. Shungwaya ni nchi ya zamani iliyokuwa eneo lililoko katika nchi mbili jirani ambazo siku hizi ni Kenya na Somalia. Kabila hili la wangozi liliishi jirani na makabila mengine kama vile wajikenda, wapokomo, Wamalakote (au Waelwana) naWangazija (kabla hawajahamia visiwa vya Ngazija). Lugha ya wangozi siku hizo, ambayo ndiyo mzazi wa Kiswahili cha leo, ilijulikana kwa jina kingozi. Kama ilivyosemwa hapo awali, kingozi kilisemwa na watu wachache

sana.

Je lugha hii ilikuwaje mpaka ikapata maendeleo haya makubwa tunayoyashuhudia siku hizi? Ama kwa hakika, Kiswahili ni lugha iliyo bahatika tu.Inaweza kusemwa kwamba lugha hii ilipendelewa na mazingira na historia.

Jambo la kwanza, wageni waliotoka mashariki ya kati kufikia hizi janibu zetu Afrika ya mashariki walikaribishwa vizuri na hawa wangozi. Wakaingilia wageni na wenyeji kindakindaki, kidini, kitawala, kibiashara na kitamaduni kwa jumla. Punde si punde wangozi, ambao baadaye walijulikana kama waswahili na wageni hawa, wakaelimika katika dini (yakiisilamu), biashara na mambo ya utawala aina mpya. Lugha yao nayo ikapanuka pale ilipochukua msamiati wa kigeni hususan wa Kiarabu na Kiajemi na kuufanya uwe wake, ili kueleza kwa rahisi zaidi mambo haya mageni katika taaluma za dini, biashara, siasa na hata sayansi kama vile unajimu.Wakati huo, lugha ya Wangozi sasa ikaitwa Kiswahili wala sio kingozi. Tatizo hapa ni kuwa kwa vile Kiswahili kilichukua msamiati mwingi wa kigeni ili kuelezea taaluma hizi mpya, baadaye kimekuja shukiwa kwamba ni lugha ya kigeni ilhali ni lugha ya Kiafrika asilia, na kitovu chake ni nchi mpya za kiafrika ziitwazo Kenya na Somalia hii leo.

(a) Thibitisha kuwa Kiswahili kimekuwa lugha ya kimaitaifa (maneno 35 – 40) (alama 7)

Matayarisho:

Nakala Safi:

(b) Ukitumia maneno yako mwenyewe, eleza ujumbe ulio katika aya ya mwisho. (alama 8)

SARUFI

1. Eleza sifa bainifu za sauti /j/. (al 2)
2. Tofautisha mofimu huru na tegemezi kwa kutolea mifano mwafaka. (al 2)
3. Unda neno lenye silabi ifuatayo KIKKIKI (al 1)
4. Tia shadda katika sentensi ifuatayo (al 1)

   Wachezaji wamo uwanjani.
5. (i) Kiimbo ni nini? (al 1)
   (ii) Onyesha matumizi mawili ya kiimbo. (al 2)
6. Ainisha (al 3)

   Wasiorithishwa
7. Sahihisha sentensi ifuatayo. (al 2)

   Sukari zilizowekwa mfukoni zimenyeshewa
8. Eleza maana ya sentensi zifuatazo. (al 2)

   (i) Tunda lenyewe limeoza.

   (ii) Tunda lenye shimo halinunuliki
9. Kanusha sentensi ifuatayo. (al 2)

   Ningalifuzu katika mtihani wangu ningalituzwa.
10. Tunga sentensi na ubainishe kijalizo. (al 2)
11. Andika sentensi usemi halisi.

    Rais alisema kuwa wangepata tiba ya bure kama bunge lingepitisha mswada huo.
12. Tunga sentensi yenye muundo wa: (al 3)

    Kiima, kiarifa, yambwa tendwa, yambwa tendewa na yambua ala..
13. Changanua sentensi kwa kutumia jedwali. (al 4)

    Wachezaji vikapu watakifanikiwa katika mechi hiyo watatuzwa medali
14. Nyambua kitenzi hiki katika kauli iliyo mabanoni *pa* (tendeka) (al 1)
15. Bainisha virai katika sentensi hii. (al 3)

    Juma alikwenda mjini kwa miguu
16. Tunga sentensi kudhihirisha matumizi mawili ya <u>KU</u>. (al 2)
17. Onyesha matumizi mawili ya nukta mkato. (al 2)

18. Toa maana mbili ya sentensi ifuatayo: (al 2)
Laleni!

ISIMUJAMII: **(ALAMA 10)**

(a) (i) Eleza maana ya krioli. (alama 2)
(ii) Eleza sifa zozote tatu za krioli. (alama 3)

(b) (i) Eleza maana ya Lingua Franka (alama 2)
(ii) Tambua sifa zozote tatu za Lingua Franka (alama 3)

MTIHANI WA PAMOJA WA MAJARIBIO - KASSU
Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari
102/3
KISWAHILI
Karatasi ya 3
FASIHI
SEHEMU YA A: FASIHI SIMULIZI
SWALI LA LAZIMA

1. (a) Eleza sifa nne za kimtindo zinazopatikana katika methali za Kiswahili.
(alama 8)
(b) Eleza mbinu tatu ambazo hutumiwa kuzua misimu. (alama 6)
(c) Ni jukumu la jamii kudumisha fasihi simulizi. Dhihirisha. (alama 6)

SEHEMU YA B: HADITHI FUPI
DAMU NYEUSI
Jibu swali la 2 au 3

2 Diwani ya Damu Nyeusi imesheheni jamii ya watu dhulumati. Jadili ukirejelea hadithi za:
(a) Maskini, Babu Yangu.
(b) Mwana wa Darubini. (alama 20)

NDOA YA SAMANI

3. "Chambilecho Waswahili atafutaye hachoki, na akichoka keshapata."
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili.
(alama 4)
(b) Fafanua mtazamo wake Abu kuhusu maisha.
(alama 16)

SEHEMU YA C; RIWAYA
KIDAGAA KIMEMWOZEA - Ken Walibora
Jibu swali la 4 au 5

4. "……Moyo ulimpapa na kijasho chembamba kumtekenya juu ya mwanzi wa pua. Akahisi uchungu wa pua. Akahisi uchungu wa mwiba wa kujidunga…."
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili.
(alama 4)
(b) Tambua mbinu mbili za lugha zinazojitokeza katika dondoo hili.
(alama 2)
(c) Eleza umuhimu wa mrejelewa.
(alama 4)
(d) Ustawi wa nchi yoyote hutegemea vijana wake. Jadili ukiirejelea KIDAGAA KIMEMWOZEA.
(alama 10)

5. (a) Thibitisha jinsi mwandishi wa Riwaya ya Kidagaa Kimemwozea alivyofanikisha maudhui ya uwajibikaji.
(alama 10)
(b) Jadili mbinu ya sadfa katika Kidagaa Kimemwozea. (alama 10)

SEHEMU YA D; TAMTHILIA
Jibu swali la 6 au 7

6. " Huu ni ukoloni mamboleo"
(a) Eleza muktadha wa dondoo (alama 4)
(b) Fafanua umuhimu wa msemewa katika tamthilia hii
(alama 8)
(c) Eleza kwa tafsili namna ukoloni mamboleo unavyojitokeza katika tamthilia
(alama 8)

7. Jadili matumizi ya mbinu zifuatazo;
(alama 20)
(i) kinaya
(ii) methali
(iii) majazi
(iv) Uzungumzi nafsia

SEHEMU YA E; USHAIRI
Jibu swali la 8 au 9
Soma shairi hili kisha ujibu maswali.

8. Wenye vyao Watubana

1. Wenye vyao watubana, twaumia maskini,
   La kufanyiza hatuna, hali zetu taabani,
   Kwa sasa kilo ya dona, bei mia ishirini,
   Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana.

2. Washindana matajiri, kwa bei siyo utani,
   Na pigo kwa mafakiri, tunao hali ya chini,
   Wazeni kutafakari, wanyonge tu madhilani,
   Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana.

3. Limekuwa kubwa zogo, hakwendeki madukani,
   Fungu moja la muhogo, sasa shilingi miteni,
   Huo mkubwa mzigo, waelemea vichwani,
   Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana.

4. Si hichi wala si kile, hakuna cha afueni,
   Bei imekuwa ndwele, wenye macho lioneni,
   Ukiutaka mchele, pesa jaza mfukoni,
   Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana.

5. Waliko hao samaki, huko ndiko uchawini,
   Wachuuzi hawacheki, zimewatoka huzuni,
   Vibuwa havishikiki, kimoja kwa hamsini,
   Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana.

6. Maisha yetu viumbe, yamekuwa hilakini,
   Wenye vyao kila pembe, wametukaa shingoni,
   Nyama ya mbuzi na ng'ombe, sasa hali maskini,
   Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana.

7. Maji yamezidi unga, kwa lodi wa darajani,
   Kajitolea muhanga, kwa bei hawezekani,
   Mvao wake wa kanga, ni shilingi elifeni,
   Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana.

Maswali

(a) Fafanua toni ya shairi hili. (alama 2)

(b) Jadili dhamira ya nafsi neni.
(alama 2)

(c) Andika ubeti wa sita kwa lugha nathari. (alama 4)

(d) Fafanua kwa kutoa mfano, mbinu moja aliyotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiarudhi katika shairi hili.
(alama 2)

(e) Taja na ueleze bahari mbili za shairi hili ukizingatia: (alama 4)
   (i) Ubeti
   (ii) Vina

(f) Ujumbe unaowasilishwa katika shairi hili una hadhira lengwa tatu. Zitaje na utoe mifano.
(alama 6)

au

9. MKWARUZANO WA NDIMI

Huyo! Mshike huyo !
Hakuna bunduki wala kifani
Bomu na risasi hata hawazijui
Lakini mno wanashambuliana
Kwa ndimi zilizonolewa kwa makali
Vipande vya matusi silaha zao.

Yu imara mmoja wao
Akirusha kombora la neno zito!
Limtingishe adui wake
Na kumgusa hisia kwa pigo kuu
Pigo linalochoma moyoni kama kichomi
Kuchipuza joto la hasira na kisasi
Katika mapigano yaso na kikomo

Filimbi ya suluhu inapulizwa kuwaamua!
Nani anayekubali suluhu?
Roho zinakataa katakata
Huku ukaidi ukinyemelea na kutawala kote
Mapandikizi ya watu yakipigana
Vita shadidi visivyo ukomo
Vita vya ndimi!

Magharibi sasa
Jua linapungia mkono machweo
Nalo giza likinyemelea kwa kiburina
Kasi
Sisikii tena sauti za misonyo
Mate yawatesi yamekauka
Makanwa yao yamelemewa na uchovu
Sasa wameshikana mikono
Ishara ya suluhu.

Maswali

(a) Hili ni shairi la aina gani? (alama 1)
(b) Eleza dhamira ya mshairi. (alama 2)
(c) Eleza kanuni za utunzi alizotumia mshairi. (alama 4)
(d) Taja mbinu zozote tatu za kifasihi alizotumia mshairi. (alama 3)
(e) Jadili toni ya mshairi katika beti tatu za awali. (alama 2)
(f) Tambua matumizi ya mistari mishata na utoe mifano miwili. (alama 3)
(g) Andika mishororo ya kwanza mitatu katika ubeti wa 4 kwa lugha ya nathari. (alama 3)
(h) Toa maana ya msamiati huu. (alama 2)
    (i) Kombora
    (ii) Misonyo

MTIHANI WA PAMOJA WA MAJARIBIO - KASSU
Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari
102/1
KISWAHILI
Karatasi ya 1
INSHA(MWONGOZO)

1. **SWALI LA LAZIMA**

Hii ni insha ya kiuamilifu.
Haya ni maandishi ya mtu binafsi kuhusu sifa zake maishani (mambo mazuri ya kumjengea sifa)
Ya kuzingatiwa katika uandishi wa insha ya aina hii:-

a) Mada-Hufafanua anayetajwa katika tawasifu hiyo.
b) Nafsi- Huendelezwa katika nafsi ya kwanza.
c) Hujikita katika ujumbe kuhusu mtu binafsi yaani-
   i) Mwaka na mahali pa kuzaliwa
   ii) Aila/familia yake
   iii) Hali yake ya ndoa
   iv) Kiwango chake cha elimu-chuo kikuu,shule ya upili,ya msingi na ya vidudu.
   v) Mtahiniwa ajikite katika kutoa mambo yake mema kama vile vitendo na mafanikio yake ili aonekane kama **kielelezo katika jamii**.
   vi) Vyeti na tuzo zote alizopata mhusika hutajwa.
   vii) Ni vyema mtahiniwa aonyeshe tajriba yake katika kazi mbalimbali hasa katika nyanja ya kidiplomasia.
   viii) Ni vyema aangazie juhudi zake maishani kwa mfano amekuwa akijihusisha na shughuli zipi na amefaulu vipi katika kazi hizo.
   ix) Katika kujijenga, ni vyema ataje vipaji vyake mbalimbali hasa vinavyohusiana na kazi ya ubalozi/uhusiano mwema kati ya mataifa mbalimbali.
   x) Risala ya rais wa nchi yake pia iandikwe katika wasifu huu kama njia ya kumalizia tawasifu yake.

Tanbihi-Kazi hii ipangwe kiaya na mawazo yafulululize.
Akizingatia yoyote yale ambayo yanaonyesha kwamba anaweza kuifanya kazi hiyo,atakuwa amejibu swali.

2. **Utumizi wa afyuni[mihadarati} katika taasisi za masomo nchini ni suala ambalo ni muhula kutatuliwa. Jadili.**

KUUNGA MKONO

- Sheria hafifu inayowaruhusu wauzaji na watumiaji mihadarati kuendelea na shughuli zao.
- Kuporomoka kwa maadili ya kijamii na kushindwa kwa wazazi kuwathibiti watoto wao kwa kutowapa mawaidha.
- Vyombo vya habari vinachangia pakubwa katika kiwashawishi vijana kutumia mihadarati (runinga, redio, mtandao).
- Ukosefu wa wataalamu wa kutoa nasaha na mwelekeo kwa wanafunzi shuleni.
- Upungufu wa vielezo bora/mifano katika jamii kwani kuna watu wengi wanaotumia mihadarati katika jamii.
- Idadi kubwa ya wanafunzi ikilinganishwa na idadi ya walimu shuleni.
- Ufisadi: wanaowauzia vijana mihadarati hutumia hongo kufanikisha maovu haya, aidha mihadarati huingizwa nchini na matajiri wenye ushawishi.
- Baadhi ya majirani wa shule hudhani na hata kutumia njia hii kujipatia riziki.
- Shinikizo za wenzi huwasukuma vijana kutumia mihadarati.

KUPINGA

- Kutunga sheria kali zitakazowazuia watumiaJi na wauzaji wa mihadarati.
- Kuwashauri wazazi kuwa mstari wa mbele kuwazungumzia na kuwashauri watoto wao.
- Kuthibiti vyombo vya habari ili kupunguza matumizi ya mihadarati.
- Kuwaajiri na kuongeza wataalamu wa ushauri shuleni na vijijini.
- Serikali ikabiliane na ufisadi katika viwango vyote, ukiwemo unaoruhusu uagizaji wa mihadarati na ‘mabwenyenye’ walio na ushawishi.
- Kuwaelimisha watu kuhusu njia halali, au mbadala za kujipatia riziki k.m. kilimo, biashara na kilimo biashara n.k.
- Wanafunzi washauriwe kujisimamia kimawazo na kuepuka shinikizo za wenzi.

- Vijana kupewa nasaha kuhusu athari za utumizi wa dawa huizi za kulevya.
- Walimu kuhimizwa kuwa karibu na wanafunzi ili kutambua wale wanaoenda upogo.

TANBIHI

- Mtahiniwa anaweza kuwa na hoja nyingi za kuunga mkono na moja au zaidi za kupinga.
- Mtahiniwa anaweza kuwa na hoja nyingi za kupinga na moja au zaidi za kuunga.
- Mtahiniwa atoe msimamo wake.
- Katika hali zote mtahiniwa asiwe na chini ya hoja nane.
- Anayekosa kushughulikia pande zote mbili asipite alama 10.
- Mtahiniwa anaweza kutoa hoja sawa pande zote almradi atoe msimamo.
- Hakiki hoja zingine za mtahiniwa.

3. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali: Mwenye kovu usidhani kapoa.
   Msimulizi asimulie kisa kitakachoonyesha ukweli wa methali hii.
   Maana – Mtu ambaye amewahi kuwa mbaya hata akionekana kubadili mwenendo huenda akarudia maovu yake.
   Mtahiniwa aonyeshe:

a) Makosa mhusika aliyofanya.
b) Jinsi makosa hayo yalimfanya kubadili mwenendo wake.
c) Kurudia makosa yale au mengine mabaya zaidi.
   Kisa ndicho muhimu si utangulizi.
   Sehemu ya pili ya methali yaweza kuwa ya sentensi moja au kirai kimoja – ikubalike kuwa mtahiniwa amezingatia mada.

4. Andika kisa kitakachomalizikia kwa: ... hivyo ndivyo ukurasa mpya katika kitabu cha maisha yangu ulivyofunguka.

- Mtahiniwa asimulie kisa kitakachoonyesha mabadiliko yalivyotokea katika maisha yake. Mabadiliko haya yaweza kuwa mazuri au mabaya.
- Mtahiniwa atumie wakati uliopita; aonyeshe matukio yaliyomfikisha katika mabadiliko haya.
- Kisa kioane na mdokezo aliopewa.

MTIHANI WA PAMOJA WA MAJARIBIO - KASSU
Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari
102/2
KISWAHILI
Karatasi ya 2

1. **UFAHAMU MWONGOZO.**
MASWALI
(a) Eleza kilichosababisha kongamano la katiba la Lancaster (alama3)
- Waafrika hawakua wamehusushwa katika katiba ya mwaka wa 1920.
- Waafrika walitaka kuhusika katika masuala ya uongozi.
- Utetezi wa wanasiasa ulilazimu serikali ya uingereza kuitisha kongamano.

(b) Taja mambo matatu yaliyotiliwa-mkazo na raia katika maoni yao kuhusu katiba. (alama3)
- Utawala mwema na uwajibikaji wa viongozi.
- Kulinda haki za binadamu zikiwemo za wanawake, watoto na walemavu.
- Kanuni za usawa na ulinganifu.

(c) Eleza umuhimu wa katiba kwa mujibu wataarifa. (alama3)
- kuweka utaratibu na kanuni za utawala mf utawala wa kimikoa.
- Hufafanua vyombo vikuu vya serikali, mamlaka yavyo na mipaka yavyo ya kutenda.
- Hupambanua haki za raia.

(d) Taja sababu zilizochangia ubadilishaji wa katiba. (alama 3)
- Katiba iliyokuwa imeandikwa na watu wachache ilikuwa imefanyiwa marekebisho mengi.
- Viongozi na watu wenye uwezo na utajiri walipuuza katiba.
- Kutokana na uongozi uliokuweko wakati huo, watoto na watoto na walemavu walidhulumiwa na kukosa uwakilishi ufaao.

(e) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika taarifa. (alama 3)
- Kitovu : Chenye maana na umuhimu.
- Harakati : Shughuli za kufanya jambo fulani.
- Hamasisha : Kufanya jambo lieleweke na kukubalika.

UFUPISHO
2. Soma makala haya kisha ujibu maswali yanayofuata
(a) Thibitisha kuwa Kiswahili kimekuwa lugha ya kimaitaifa (maneno 35 – 40(alama 7)
Nakala Safi:
- Kiswahili huzungumzwa na watu wa nchi mbalimbali mf Tanzania, Burundi, Kenya nk
- Hutumiwa katika visiwa vya sokta(Oman)
- Hutumika katika idhaa mbalimbali mf BBC
- Hufundishwa vyuo vikuu Afrika na hata Marekani, Japani. Zozote 2×3=6
Alama 1mtiririko

b) Ukitumia maneno yako mwenyewe, eleza ujumbe ulioo katika aya ya mwisho.
- Wageni kutoka ng'ambo walikaribishwa vizuri.
- Wageni waliingiliana vyema na wenyeji.
- Wangozi waliitwa waswahili.
- Baadhi ya wenyeji walifunzwa kiislamu na biashara.
- Lugha ilienea kwa urahisi pamoja na sayansi.
- Kiswahili kilichukua msamiati wa kigeni kwa wingi.
- Pametokea dhana potovu kuwa lugha ya Kiswahili ni ya kigeni. Zozote 7×1=7.Alama 1 mtiririko.

SARUFI
1. Eleza sifa bainifu za saurit (j). (al 2)
Kipauso
Kaakaa gumu
Ghuna
2. Tofautisha mofimu huru na tegemezi kwa kutolea mifano mwafaka. (al 2)
Mofimu tegemezi – hutegemea mofimu nyinginezo ili kuleta maana
3. Unda neno lenye silabi ifuatayo KIKKIKI (al 1)
Matwana
4. Tia shadda katika sentensi ifuatayo wachezaji wamo uwanjani. (al 1)

Wacjezaji wamo uwanjani

5. (i) Kiimbo ni nini? (al 1)
   Ni kupanda na kushkuka kwa mawimbi ya sauti binadamu anapozungumza.
   (ii) Onyesha matumizi mawili ya kiimbo. (al 2)
   Taarifa – Mama amewasili
   Swali – Utasafiri lini?
6. Ainisha (al 3)
   Wasiorithishwa
   Wa – kiambishi cha nafsi ya tatu wingi
   si – kikanushi
   o – O' rejeshi
   rithi – Mzizi
   shw – kauti ya kutendeshwa
   a - kiishi
7. Sahihisha sentensi ifuatayo. (al 2)
   Sukari zilizowekwa mfukoni zimenyeshewa

   Sukari iliyowekwa mfukoni imenyeshewa
8. Eleza maana ya sentensi zifuatazo. (al 2)
   (i) Tunda lenyewe limeoza
   (ii) Tunda lenye shimo halinunuliki
   (i) Kusisitiza
   (ii) Umilikaji
9. Kanusha sentensi ifuarayo. (al 2)
   Ningalifuzu katika mtihani wangu ningali tuzwa.
   Nisingalifuzu katika mtihani wangu nisingalituzwa.
10. Tunga sentensi na ubainishe kilalizo. (al 2)
    Yeye ni mkurungezi.
11. Andika sentence usemi halisi.
    Rais alisema kuwa wangepata tiba ya bure kama bunge lingepitusha mswala huo.
    "Tutapata tiba ya burekama bunge litapitisha mswada huu," Rais alisema.
12. Tunga sentensi yenye muundo wa: (al 3)
    Kiima, kiarifa, yambwa tendwa, yanbwa tendewa na yambua ala.
    Mama alipika chakula ya mjomba kwa sufuria.
13. Changanua sentesi kwa kutumia jedwali. (al 4)
    Wachezaji vikapu watakifanikiwa katika mechi hiyo watatuzwa medali

S				
KN			KT	
N	V	S	T	N
Wachezaji	vikapu	wakifanikiwa katika mechi hiyo	watatuzwa	medali

14. Nyambua kitenzi hiki katika kauli iliyo mabanoni pa (tendeka) (al 1)
    Peka
15. Bainisha virai katika sentensi hii. (al 3)
    Juma alikwenda mjini kwa miguu
    KN – Juma
    KT – alikwenda mjini
    Ke – kwa miguu
16. Tunga sentensi ludhihirisha matumizi mawili ya KU. (al 2)
    Kiambishi kiwakilishi cha ngeli ya KU-KU kucheka huku kunapendeza
    Kuanzisha vitenzi vya silabi moja kula, kuja
    Kukanusha wakati uliopita sikumwona
17. Onyesha matumizi mawili ya nukta mkato. (al 2)
    Kutenganisha sentnsi mbili tulipowasili alikuwa sebuleni; alikota kutushughulikia
18. Toa maana mbili ya sentensi ifuatayo: (al 2)
    Leleni!

(i) Amri
(ii) Wingi wa wahusika

ISIMUJAMII: (ALAMA 10)

(a) (i) Eleza maana ya krioli. (alama 2)

– Ni pijini iliyoimarika na kuwa na watu wanayoizungumza kama lugha yao ya kwanza

(ii) Eleza sifa zozote tatu za krioli. (alama 3)

– Huwa na wenyeji kwa mfano; Krioli ya Haiti, Kridi ya Jamaica
– Huwa na miundo dhabiti ya kisarufi.
– Huwa na msamiati dhabiti unaoweza kutungiwa kamusi.
– Huwa na matumizi mapana katika Nyanja za siasa, muziki, vyombo vya habari na kadhalika.

(b) (i) Eleza maana ya Lingua Franka. (alama 2)

– Ni lugha inayotumiwa na watu walio na lugha tofauti kwa ajili ya mawasiliano kwa mfano Kiswahili katika eneo la Afrika Mashariki.

(ii) Tambua sifa zozote tatu za Lingua Franka. (alama 3)

– Huwa ni lugha ua mawasiliano kati ya watu wenye lugha zaidi ya moja.
– Yaweza kuwa lugha ya kwanza ya mzungumzaji au lugha ya pili na kwa watu wengine lugha ua kigeni
– Hukiuka mipaka ya kitamaduni
– Hukiuka mipaka ua kimaeneo - inaweza kutumiwa katika maeneo mapana.
– Hutumiwa na watu ambao lugha zao za mama ni tofauti

MTIHANI WA PAMOJA WA MAJARIBIO - KASSU
Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari
102/3
KISWAHILI P3
FASIHI MWONGOZO

SEHEMU YA A; FASIHI SIMULIZI
SWALI LA LAZIMA

1. (a) Eleza sifa nne za kimtindo zinazopatikana katika methali za Kiswahili.(alama 8)
(i) Takriri:urudiaji wa maneno
– Bandu bandu huisha gogo
– Haraka haraka haina Baraka
(ii) Taswira (picha)
– Njia mbili zilimshinda fisi
– Paka akiondoka panya hutawala
(iii) Sitiari:mithilisha kitu kimoja na kingine moja kwa moja
– Mgeni ni kuku mweupe
– Ujana ni moshi
(iv) Kejeli/dhihaka
– Uzuri wa mkakasi ndani kipande cha mti
– Maskini akipata matako hulia mbwata!
(v) Balagha:maswali yasiyohitaji jibu kwa vile jibu ni bayana
– Umekuwa mumumenye kuharibikia ukubwani?
– Pilipili usiyoila yakuashiani?
– Angurumapo samba mchezo ni nani?
(vi) Tashbihi:ulinganisho kwa kutumia kilinganishi
– Mapenzi ni kama majani popote penye rotuba hujiotea.
– Jambo usilolijua ni kama usiku wa kiza.
(vii) Kweli kinzani:hali inayopingana
– Mpanda ngazi hushuka.
– Kuinamako ndiko kuinukako
(viii) Chuku:maneno yasiyo ya kweli
– Polepole za kobe hufikisha mbali.
– Ukiwa makini utayaona macho ya konokono
(ix) Kinaya;kinyume na matarajio
– Ngoja ngoja huumiza matumbo
(iix) Tashihisi/uhaishaji/uhuishaji
– Sikio la kufa haliskii dawa
– Siri ya mtungi muulize kata {Zozote 4x2.sifa alama 1mfano1
(b). Eleza mbinu tatu ambazo hutumiwa kuzua misimu. (alama 6)
(i) Kutumia tanakali-neno mtutu_Bunduki/ hali ya kuachilia risasi
(ii) Utohozi wa maneno
Gava - Government.
Hedi - Head
Fadhee - Father
(iii) Maneno ya kawaida kupewa maana mpya
Toboa - faulu
Chuma - Bunduki
(iv) Matumizi ya tabdila
Njaro - Ndaro
(v) Kufupisha maneno
Kompyuta - komp.
(vi) Kutokana na umbo/rangi ya kinachorejelewa
Mfano Blue - Noti ya kitambo ya shilingi ishirini
Tangi - Mtu mwenye umbo nane
(vii) Ktumia isitara au jazanda
Golikipa - nyani

Mtu mlafi - Fisi

(viii) Kuunda maneno mapya kabisa;. mfano

Kuhanya - Usherati
keroro - Pombe
Kusikia ubao - Hisi njaa
Ni kubaya - hali si nzuri [3x2]

(c). Ni jukumu la jamii kudumisha fasihi simulizi. Dhihirisha. (alama 6)

- Kuendelea kufundisha Fasihi Simulizi shuleni
- Kufanya Fasihi simulizi kuwa hai kiutendaji kupitia shehere na halfa tofauti za kiserikali.
- Kuhifadhi tanzu mbalimbali ili vizazi vijavyo viweze kuzifahamu mfano kwa kurekodi.
- Kufanya utafiti wa kina kuhusiana na tanzu za Fasihi simulizi.
- Kuhakikisha kuwa lugha za kiasili hazififii kwa vile ndizo chanzo cha Fasihi Simulizi.
- Kuonyeshwa kwa fani mbalimbali za Fasihi simulizi kwenye vyombo vya habari kama runinga.
- Kuhimiza wanajamii hususan viongozi kuwasilisha ujumbe wao kwa kutumia fani za Fasihi simulizi kwa mgano hotuba, ulumbi, mawaidha nk.
- Kuhimiza wanajamii kuionea fahari jadi hii na kushiriki kikamilifu katika matumizi ya fani mbalimbali mfano mwiga.
- Kusisitiza uendelezwaji wa fani zake katika mashindano ya shule na hata baina ya shule tofauti kimaeneo na kitaifa. [3x2]

SEHEMU YA B; HADITHI FUPI

DAMU NYEUSI

2. Diwani ya Damu Nyeusi imesheheni jamii ya watu dhulumati. Jadili ukirejelea hadithi za:

- Dhulumati ni mtu/kikundi cha jumuiya ambacho kinawakandamiza wanajamii au baashi yao kwa njia kadha na kusababisha wao kuwa na vilio.

(a) Maskini, Babu Yangu.

- Jumuiya ya Wantantele walipinga ndoa kati ya wamidi ua makabila mengine (uk. 76)
- Babu maende alinawa kwa sababu ya ukabila. Kisa ni kuwa alikuwa anatembea na mjukuwe aliyefanana na watentelo. (uk. 79) - mwizi wa mtoto.
- Kila wakati babu wake msimulizi alitaja neno ukabila, ni bayana kuwa jumuiya iliegemea mirango ya ukabila.
- Pia alitaja ufisadi, kuonyesha kuwa dhulumati walifisidi mali ya umma na kiwanyima waja huduma bora.
- Uongozi katika mtaa wa kochokocho, ambao ni mchafu. Hii inadhihirisha uongozi usiojali maslahi ya wananchi.
- Babu anapojaribu kujitetea kuhusu mtoto mdogo/mjukuwe hasikizwi, anauawa.
- Watu wa kochokocho walifikiri kuwa ni lazima Maende ameroga Msimulizi ndipo alimwita babu - wanamuua.
- Kulikuwa na utabaka, matajiri waliishi katika sehemu nzuri kule sakata, mitaa ya ghorofa wa maskini waliishi mitaa ya madongoporomoka.

(b) Mwana wa Darubini.

- Kananda anajisiwa na mwajiri wake Mwatela na kimsababishia uja uzito.
- Anamdanganya kuwa angemuoa ili anyamaze na asimjulishe Maria ambaye ni mke wa Mwatela.
- Mwatela anampokonya mtoto, Mwakitawa na kusababisha utengano usiofaa wa mama na mwanawe angali mchanga.
- Anamwuuza kwa dereva mmoja kutoka kongo ambako kananda anaelekea nchi asiyoijua wala kuwa na jamaa wake.
- Dereva huyo baada ya kuishi naye na kumnajisi anamwuuza kama mtumwa.
- Mwatela aliwadanganya wazazi wa Kananda kuwa alikuwa ametoweka na hakujulikana aliko.
- Mwatela anampiga Maria, mkewe kila wakati anpokuja nyumbani mlevi Maria anapotaka kujua alikotoka.
- Mwatela anampa mtoto wake Mwakitawa kisu na hataki kumpiga nayo mamaye, Kananda kwa kisingizio kuwa ni jasusi ambapo Mwakitawa anampiga Kananda nusura amuue.
- Mwatela anamweleza Mwakitawa kuwa kuna 'adui' au 'jasusi' ambaye alikuwa ni mamaye mzazi. Hapa anamhadaa.
- Mwatela anafanya juu chini kumzuia Mwakitawa kuonana na mamake.

- Mwatela hamwelezi Mwakitawa ukweli kuhusu mamake.
- Mwatela si mwaminifu katika ndoa, anazini na Kananda bila mkewe kufahamu.
- Mwatela anakiuka haki za watoto kwa kumwajiri kananda kazi ya uyaya akiwa na umri mdogo.

Utahini
Maelezo ya neno 'Dhulumati' = al. 2
(Kila hadithi iwe na hoja 4 x 2) = al.16
Tanbihi hadithi moja iwe na hoja 5 zilizoelezwa vizuri. (alama 20)

NDOA YA SAMANI

3. "Chambilecho Waswahili atafutaye hachoki, na akichoka keshapata."
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

- Maelezo ya mwandishi.
- Yanajitokeza kama mawazo/masimulizi yake Abu kuhusu mtazamo wake maishani.
- Liche ya kuzaliwa na kulelewa katika maisha ya uchochole anajibidiisha na kuyaboresha maisha yake. [Zote 4x1]

(b) Fafanua mtazamo wake Abu kuhusu maisha.

- Kupata na kukosa hakutegemei uzawa. Licha ya Abu kuzaliwa katika umasikini halizinambadilikia baadaye anapoinuka kiuchumi. Umasikini haumzuii kuimarika kichumi.
- Bidii na stahamala ndizo nyenzo za pekee za kujiinua. Abu amechorwa kuwa mto mwenye bidii ambaye alikuwa na matumaini ya kupata riziki hivyo akajinyanyua kutoka kwenye uchochole.
- Vikwazo ni changamoto zinazotutia hamasa kujiimarisha. Kukataliwa kwake na Amali kunampamotisha ya kufikia ufanisi hata mkubwa zaidi ya ule wa awali. Umaskini unamsukuma kutafuta jinsi ya kujikomboa.
- Ni wajibu wetu kuwashughulikia jamaa zetu. Anapotononeka kihali awakumbuka kuwajengea wazazi nyumba na kuwatafutia nduguze ajira.
- Hapana pengine kama nyumbani. Baada ya kujiinua kiuchumi kule Uarabuni anarudi na kuekeza kwao nyumbani.
- Mngwana hasahau alikotoka/asili. Anaporudi nyumbani hawasahau wenziwe waliokuwa wakifanya vibarua pamoja. Anawapa ajira mara kwa mara ili kuwainua.
- Ndoa si ukubwa wa sherehe. Anaona vitu vingi anavyopaswa kuwa "wakweze' ili kumwoa Amali kama ubadhirifu. Haoni haja ya kuandaa harusi kubwa atakavyo Mama Zena.
- Ndoa inastahili kujengwa kwenye misingi ya ukweli. Anamkataa Amali anapotambua kiwa kukubali kwake (Amali) kuolewa naye kulishinikizwa na tama ya utajiri wake.
- Mkemwema hutunukiwa mja naye Mungu. Anamwomba Mungu ampe mke mzuri ambaye angemchukua jinsi alivyokuwa (bila kujali hali zake za kiuchumi).
- Kazi yoyote halali ni kazi mradi ikupe riziki. Abu anafanya vibarua vingi ili kujiimarisha kimaisha. Pia aendapo uarabuni anafanya kazi ya uhamali. Habagui ajira.
- Ili kujijenga uchumi mja anapaswa kuwajibika pato. Anadunduiza fedha anazopewa uarabuni hivi arudipo kwao anaweza kuekeza katika biashara ya uchukuzi.
- Utajiri/mali si kisingizio cha mtu kubadilika licha ya kupata mali nyingi anasalia kuwa myenyekevu kawa awali. Habadiliki.
- Tunapofanikiwa inatujuzu kuwanyanyua wengine katika jamii. Anawaajiri vibarua wenzake katika kazi tofauti tofauti alizozianzisha.
- Ndoa ni asasi muhimu katika kuindeleza jamii. Anafanya kila jitijadi kupata mke kama alivyotarajiwa kufanya na jamii yake.
- Mustakabali wetu unadhibitiwa na Mungu. Mungu ndiye mratibu wa mambo yote. Anatumia Methali/msemo "ya kesho ajua Mungu" ili kudhihirisha jinsi hali zilivyomwimarikia.

Hoja zozote 8 x 2 = alama 16

SEHEMU YA C; RIWAYA

KIDAGAA KIMEMWOZEA - Ken Walibora

4 (a) Maneno ni ya mwandishi
Anaregelea Mtemi Nasaba Bora.
Sababu: Baada ya Mtemi kusoma barua aliyopata kutoka kwa mpenziwe Lowela ya kutisha awaachilie Amani na Imani ili mapenzi yao yaendelee.
Mahala: Nyumbani kwake. (zote 4 x 1 = 4)

(b) (i) Methali:Mwiba wa kijidunga.
(ii) Tashhisi: Kijasho chembamba kumtekenya

(iii) Istiari: Mwiba wa kujidunga. (zozote 2 x 1 = 2)

(c) Umuhimu wa mtemi Nasaba Bora.

(i) Kielelezo cha viongozi wanaowadhulumu wananchi kwa kutumia mbinu za kikoloni.

(ii) viongozi wanavyotumia vyombo vya dola kuwanyanyasa wanyonge mf. Mauaji ya Chirchiri Hamadi./Kupigwa kwa mamake Imam.

(iii) Ni kielelezo cha viongozi wanaotumia vyeo vyao vibaya m.f. kuwalazimisha wananchi kumchangia pesa mwanawe kwende kusoma ng'ambo.

(iv) Kupitia kwa Mtemi tunapata sifa za wahusika wengi. Mf Amani ni mwenye utu. [anamshawishi Gadaffi asimmue Mtemi] (4 x 1)

(d)

- Amani na Imani kubadili imani ya wanasokomoko kwa kuyanywa maji ya mto Kiberenge.
- Amani na Madhubuti kuungana ili kupinga uongozi mbaya. Wanafichua uozo wa Mtemi na baadaye kugawia Dj, MatukoWeye shamba.
- Amani na Madhubuti wanashirikiana kurejesha haki mahakamani kwa kutafuta mashahidi kumtoaYusufu lawamani.
- Imani kubadilisha mtazamo hasi wa watu kuhusu walemavu.
- Imani na Amani wanamlea mtoto uhuru ili kuonyesha umuhimu wa haki za watoto.
- Dj. anabadilika baada ya kutoroka jela kwa kufanya kazi kwa bidii kwa Bw. Maozi ili kujitegemea.
- Amani anajenga nyumba yake mwenyewe ili kuonyesha umuhimu wa bidii, hategemei urithi.
- Amani anaendeleza amani baina ya wananchi ili kuleta mabadiliko .
- Kupitia kwa Amani, anatudhihirishia umuhimu wa kusameheana na kutolipiza kisasi.
- Amani anawaelekeze raia kuhusu uwajibikaji wao katika kuimarisha uongozi ,anawaonya dhidi ya kupuuza ukatili.
- Madhubuti kukataa kushirikishwa katika ufisadi. Anataka kujitafutia kazi mwenyewe bila kutoa hongo.
- Chwechwe Makweche na vijana wenzake kuiletea nchi ya Tomoko sifa kwa kuichezea timu ya taifa kandanda. (5 x 2 = 10)

5. (a) Uwajibikaji

- Amani anakilea kitoto Uhuru kama mwanawe baadaya Mtemi kukipagaza mlangoni kwake.
- Bi. Zuhura anawasaidia Amani na Imani kukilea kitoto Uhuru.
- Amani na Imani wanaishi katika kibanda kimoja lakini hawakiuki mipaka ya uhusiano wao.
- Imani anabadili mawazo yake kuhusu tendo la kujiua.
- Wafanyikazi wa Mtemi wanajitahidi kunadhifisha kasri.
- Amani anafunga safari ili kupata aliyemwibia mswada wake.
- Madhubuti anajitenga na ufisadi wa babake.
- Ben Bella anavunja uhusiano wake na Mashaka.
- Amani anafichua siri yake kwa Madhubuti kwa wakati ufaao.
- Amani na Imani wanafunga ndoa tu baada ya kukamilisha masomo. (10 x 1)

(b) Sadfa

- Kukutana kwa Amani na Imani pale ziwa Mawewa.
- Amani na Imani kukutana na Dj pale mto Kiberenge kisha anawapeleka kwa Mtemi.
- Amani kufika tu kwa Mtemi anapohitaji mchungaji.
- Majisifu kupata tu barua ya mwaliko wa kutoa mhadhara baada ya kubishana na Mkewe kuhusu ubingwa wake katika uandishi.
- Bi.Zuhura anapomwita Amani chumbani kwake Mtemi anawasili.
- Amani anafika tu pale ambapo Oscar kambona anataka kulipiza kisasa kwa Mtemi.
- Amani na Imani kuajiriwa na ndugu.
- Amani na Imani wanakutana wakati tu wote wameharibikiwa na mambo.
- Dj anapita kibandani kwa Amani wakati Amani anawaza kuhusu kile kitoto Uhuru. Dj anaenda kumwita Imani kumsaidia Amani.
- Kitabu anachopewa Amani kusoma pale pa Majisifu ni kidagaa ambacho ni kitabu chake.

SEHEMU YA D; TAMTHILIA

7. **(a)** Maneno haya yalisemwa na Siki akimwambia Meya.Daktari Siki alikuwa ameenda kumwona Meya nyumbani mwake ili kumjulisha kuhusu matatizo ya wanacheneo.[4x1]

(b)

- Meya anawakilisha viongozi fisadi. Meya anatumia mali ya umma kujitajirisha mwenyewe.
- Meya ni kielelezo cha viongozi wabinafsi. Meya anajali maslahi yake na familia yake.anajipatia vipande vya ardhi
- Meya anawakilishi viongozi dhalimu. Meya anawanyanyasa wafanyikazi wake kwa kulipa mshahara duni. Anapuuza malalamishi ya wafanyikazi
- Yeye ni kielelezo cha viongozi wabadhirifu. Anatumia pesa za baraza ovyoovyo. Anapanga kuandaa karamu kubwa ya kuwalaki Mameya kuwa nchi za nje. Anaagiza vileo kutoka Urusi.
- Meya anawakilisha viongozi dikteta. Meya atambui maoni ya wanacheneo katika uongozi wake. Anafanya mambo kulingana na uwezo wake.[4x2]

(c)

- Unyanyasaji Meya anatumia askari wa baraza kuwanyamazisha wanacheneo
- Ufisadi-Meya anatumia mali ya baraza kujinufaisha.Alishirikiana na Bili na madiwani kuuza fimbo ya Meya.
- Ubadhirifu. Meya anatumia pesa za baraza apendavyo.anapanga kuandaa karamu kubwa na mapokezi ya mameya
- Udikteta analazimisha mambo. Hatambui mchango wa wanacheneo
- Udhalimu. Mstahiki meya anawadhulumu wafanyikazi wa baraza. Wafanyakazi wanalipwa mshahara mdogo pamoja na kufanya kazi katika mazingira mabaya.anawatisha wafanyikazi waliogoma kwamba baraza linaweza kuwafuta kazi na kuwapa vijana ambao walikosa kazi baada ya kuhitimu kutoka chuo kikuu.
- Mapendeleo. Meya anaidhinisha nyongeza ya mishahara kwa madiwani huku akiwapuuza wanacheneo[4x2]

8. **(i) Kinaya**

Tendo la baraza la Cheneo kuwaongeezea madiwani mshahara ni kinaya.Meya alikubali haraka kuidhinisha nyongeza ya mshahara ilhali wafanyikazi wa baraza wanaendelea kugoma kwasababu ya mshahara mdogo.

Meya anawadanya wanacheneo kuwa dawa ziko njiani.Ukweli ni kuwa Meya anafahamu kwa hali ya matibabu katika zahanati imedorora

(ii) Methali

Ngoja ngoja hii haisaidii matumbo. Siki anamwambia Diwani wa III. Siki anarejelea hali ya ukosefu wa dawa.

Haraka haraka haina Baraka-Waridi alidai kuwa Meya alisema alipoulizwa kuhusu kuchelewa kwa dawa Mtu huvuna alichopanda . Diwani wa III anamwambia Siki. Alikuwa akirejelea namna baraza lilivyoongozwa na mstahiki meya. Anamaanisha kuwa meya angevuna mazao ya Uongozi mbaya.

Kelele za chura hazimzuii ng'ombe kunywa maji-Bili alimwambia Meya baada ya sauti iliyodai wafanyikazi wapewe malipo bora. Ilimaanisha kuwa malalamishi hayo haingezuia meya katika kutekeleza mipango yake.

Majazi

Bwana Sosi – jina hili linaashiria mtu mwenye kupenda mlo.Alalamika wakati aliletewa viyai vidogo na Gedi mpambe wake.

Bwana sosi anapanga karamu ya kupigiwa mfano. Aliagiza vinywaji katoka urusi na divai kutoka Ufaransa.

Waridi- ua linalopendeza. Matendo ya Waridi yalionekana ya kuleta afueni kwa wanacheneo.Anawapa wanacheneo matumaini kuwa dawa zingefika zahanatini.

Uzungumzi nafsia

Siki anajizungumzia akiwa ofisini mwake baada ya kupokea simu kutoka kwa Tatu. Anasema kuwa watu wenye njaa hawawezi kusikiliza chochote

Meya anasema na nafsi yake baada ya kuambiwa na Gedi kuwa mhazili wake amegoma.Alisema aligoma baada ya kupewa ajira.

[Ufafanuzi alama 1

Mifano 2x2=4]

Mbinu 4x5=20

SEHEMU YA D; USHAIRI

9 (a) Shairi huru kwa sababu halina arudhi (alama 2)

(b) Kuonyesha jinsi kugombana ni kubaya na wagambanao huchoka na wakapatana

(c) Anatumia mshororo toshelezi na mshata (alama 2)
- Amepanga beti
- Ametumia maneno mateule kama vile neno vita

(d) Istiara
- Vipande vya matusi silaha zao
- Mabalagha - Ni nani anayekubali suluhu ?
- Nidaa - Huyo ! amshuke huyo! (3x1)

(e) Toni ya kukerwa - anaonyesha kuchukizwa na vitu hivyo (alama 2)
(f) Wamepatana baada ya kuamuliwa (alama 2)
(g) Kuonyesha hisia za mshairi (alama 2)
(h) Mtu /Nafsi ya tatu inayoshuhudia magombano (alama 4)
(j) (i) silaha
(ii) malalamiko (2x1)
- Msanii anatuambia kuwa wakati wa jioni umefika
- Jua linapigia machweo kwaheri
- Giza linaingia kwa kishindo kikubwa (3x1)

10. (a) Ndege (alama 1)
(b) Mke nyumbani / mchumba (alama 1)
(c) Ukara - vina vya kati kubadilika vya kati vinatiririka
Mathnawi - vipande viwili
Tarbia - Mshororo minne (3x1)
(d)
- Mishororo minne
- Vipande viwili – ukwapi na tao
- Mizani 16 katika kila mshroro

Vima ri, ni
ri, ni
ri, ni
ni, wa (4x1)

(e)
- Tabdila - muruwa na heshima
- Inkisari ataka badala ya anataka
- Kuboronga sarufi - kama anavyo kubwa hasara (2x2)

(f) Mke mwema mwenye heshima nzuri ya kusifu , hata akifungwa atadhamini makao ana furaha kuishi kule . Mke anayeishi nyumbani amezidiwa nguvu
(4x1)
(g) Anashauri kuwa wake wanaishi katika ndoa ni wachache / wengi wana tama
(h) (i) atahama (1x2)
(ii) maneno (2x1)

TATHMINI YA PAMOJA YA KAUNTI NDOGO YA NANDI KASKAZINI 2015
Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari
102/1
KISWAHILI
INSHA
KARATASI YA KWANZA
MASWALI

5. Wewe ni katibu wa kamati ya maslahi ya klabu ya wasanii chipukizi mtaa wa Rehema. Andika kumbukumbu za mkutano uliofanywa hivi karibuni kujadili suala la usalama uliozorota.
6. Ufisadi umekuwa janga linalohitaji kujitolea ili kupiga vita. Jadili.
7. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali: Ulimi huuma kuliko meno.
8. Tunga kisa kinachomalizika kwa maneno haya:

……hapo ndipo iliponipambazukia kuwa nilikuwa naogelea baharini pekee, kinyume na wenzangu wote.

TATHMINI YA PAMOJA YA KAUNTI NDOGO YA NANDI KASKAZINI 2015
Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari
102/2
KISWAHILI
LUGHA
KARATASI YA PILI

1. **UFAHAMU (ALAMA 15)**

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Mafuta yanayopatikana kwenye fukwe za bahari, moshi wa magari, takataka na bidhaa nyinginezo zinazotupwa hapa na pale ni vichafuzi vya mazingira. Vichafuzi huathiri afya zetu na kuathiri wanyama na mimea. Wanadamu wanayachafua mazingira yao kwa kila aina ya bidhaa mbaya za kikemikali zinazotoka viwandani mwa kawi/nguvu. Bidhaa hizo ni matokeo ya maisha ya siku hizi anayoishi binadamu.

Licha ya ukweli huu, ni muhimu kujua kuwa uchafuzi wa mazingira haukuanza leo. Miaka na miaka iliyopita, viwanda vimekuwa vikitoa mawingu makubwa ya moshi yenye sumu. Hata hivyo, uchafuzi wa mazingira umeongezeka mara dufu kutokana na kuongezeka kwa viwanda. Uchafuzi umesambaa ardhini, kwenye anga na majini. Msambao huu unapatikana katika pembe zote za ulimwengu wetu. Je, kuna aina zipi za uchafuzi?

Kwanza, kuna uchafuzi wa hali anga. Huko juu angani kuna tabaka linalojulikana kama ozoni. Tabaka hili ni aina ya gesi ya oksijeni na linaunda kinga fulani dhidi ya miale ya jua. Miale hiyo ya jua huweza kusababisha saratani ya ngozi inapomfikia binadamu. Hata hivyo, uchafuzi wa mazingira unaelekea kuliathiri tabaka hili. Vilevile, baadhi ya kemikali zinazotumiwa katika jokofu au kwenye mikebe ya marashi ya kupulizia na upakiaji bidhaa, huuharibu ukanda huo.

Uchafuzi mwingine ni uchafuzi wa kiajali, uchafuzi huu hutokea bila binadamu kukusudia. Mfano mzuri ni meli inayovuja mafuta baharini. Mafuta haya huwaathiri na kuwaua wanyama wanaoishi baharini kama samaki na ndege na hata kuyaharibu mazingara yenyewe.

Miji mikubwa hukumbwa na uchafuzi mwingine unaohusiana na kuwako kwa idadi kubwa ya magari. Magari haya hutoa moshi unaochanganya gesi ambazo huungana na nyingine zinazoletwa na viwanda vikubwa. Mchanganyiko huu unapoungana na maji, husababisha mvua ya asidi. Mvua hii huweza kuiua mimea, kuathiri majengo na hata kuwaua wanyama wa pori ambao huenda wakayatumia maji hayo. Magari hayo hutoa moshi uliochanganyika na madini aina ya risasi ambayo huweza kuathiri siyo tu mazingira bali pia mfumo wa akili wa binadamu.

Uchafuzi mkubwa ni utupwaji ovyo wa takataka. Fauka ya hayo watu hufukia ardhini takataka ambazo huweza kuwa na matokeo mabaya kwa sababu ya kupenyeza kwenye udongo na maji yanayotumiwa na watu na mimea. Kila siku tunatupa takataka bila kujali wala kukubali. Takataka hizi ni kama makopo, mifuko ya plastiki, mabaki ya sigara au maganda ya matunda. Baadhi ya takataka ni hatari kwa wanyama na nyingine huweza pia kusababisha majanga kama moto. Aidha, hufanya mazingira yaonekane machafu.

Sote tuna jukumu kubwa la kuchangia kupunguza uchafuzi wa mazingira. Kwanza, kuelimisha na kutambua umuhimu wa usafi wa mazingira yetu. Tunapaswa kutia takataka zetu kwenye vijalala maalum au mahali tunapoweza kuzichoma na kuziteketeza. Tuhakikishe tunatunza vitu kama mifuko,

chupa na kadhalika ambavyo huweza kuundwa upya na kutumika tena. Hali kadhalika, katika miaka ya hivi karibuni, kumekuwepo na juhudi za kuwahimiza wenye magari kutumia mafuta ya gari ambayo hayana madini ya risasi. Kwa njia hii tutasaidia kuyaboresha mazingira yetu. Vilevile pana umuhimu wa kutilia mkazo utumiaji wa bidhaa ambazo zinaweza kuoza na kuvunjikavunjika au kusagika na kuwa sehemu ya udongo. Hatua ya kwanza ya kupambana na uchafuzi wa mazingira ni kujielimisha na kuwajibika. Kila mmoja akitoa mchango wake tutafanikiwa. Kumbuka; kinga na kinga ndipo moto uwakapo.

Maswali

(a) Uchafuzi ni nini? (alama 1)
(b) Ongezeko la viwanda umechangiaje uchafuzi wa mazingira? (alama 2)
(c) Tabaka la ozoni huathiriwaje na uchafuzi? (alama 2)
(d) Athari zipi zitatokea iwapo mazingira hayatatunzwa? Eleza. (alama 4)
(e) Kwa nini miji mkibuwa hukumbwa na uchafuzi kuliko sehemu nyingine? (alama 2)
(f) Eleza nui **mbili** za uchafuzi wa mazingira zilizotajwa katika kifungu hiki. (alama 2)
(g) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika kifungu: (alama 2)
    (i) Msambao:
    (ii) Makopo:

2. UFUPISHO: (ALAMA 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Ukeketaji ni mfumo wa upasuaji unaofanyiwa wanawake na wasichana sehemu nyingi duniani. Istilahi hii ya ukeketaji ina maana pana kwani inaweza kutumiwa kuelezea upashaji tohara kwa wasichana na ukataji wa sehemu za siri kwa wanawake.

Ukeketaji haupatikani tu katika bara la Afrika bali katika sehemu nyingi ulimwenguni. Umri ambapo ukeketaji hufanyika hutegemea jamii inayohusika. Mwanamke anaweza kufanyiwa ukeketaji siku chache baada ya kuzaliwa au baada ya kujifungua mtoto wake wa kwanza. Miongoni mwa jamii ambazo hupasha tohara wanawake, huthamini sana amali hii kwani kwao ni hatua muhimu ya mpito wa maisha katika jamii za jadi mwanamke hupitishwa kutoka rika moja hadi lingine, yaani kutoka utotoni na kuingia kwenye utu uzima. Ukeketaji unafungamana na sherehe ya kuwapa wasichana mafunzo kuhusu kanuni za uzazi, malezi na ndoa. Dhima kuu ya sherehe hiyo ya kuwapasha wasichana tohara inadaiwa ya kwamba ni kuwapunguzia wanawake uchu na kuhifadhi ubikira. Jamii nyingine hutekeleza tohara kwa sababu za kidini zinazoshikilia kuwa mwanamke aliyetahiriwa huwa nadhifu. Wengine wanaamini kuwa tohara huwafanya watoto wanapozaliwa kuwa na nafasi nzuri ya kuishi, ilhali wengine hupashwa tohara ili wapate waume wa kuwaoa. Kwenye jamii ambazo wanaume wanasisitiza tohara kama kigezo cha mwanamke kuolewa ukeketaji umeshamiri. Katika jamii kama hizi wanaume huwa hawataki kuoa wanawake ambao hawajatahiriwa.

Wanawake wenyewe huhakikisha ya kwamba watoto au wajukuu wao wanapelekwa kupashwa tohara. Wakati mwingine mipango ya siri hupangwa na kina mama hao pamoja na mangariba, kuhakikisha kuwa jambo hili linatekelezwa. Kwa hivyo jambo hili la ukeketaji lina utata miongoni mwa jamii nyingi ulimwenguni.

Hata hivyo ukweli ni kwamba swala zima hili la ukeketaji lina madhara makubwa na linamdhalilisha mwanamke. Katika hali ya upashaji tohara wanawake huvuja damu nyingi na aghalabu huaga dunia. Wale wanaopona huwa kwenye hatari ya kuambukizwa maradhi ya zinaa ambayo huharibu sehemu za uzazi. Kwani madaktari wanadai uchungu wa uzazi huwa mwingi na hudumu muda mrefu.
Kwa sababu tohara hufanywa mara moja kwa mwaka, wasichana wote wa rika moja hukusanyika mahali maalum ili kufanyiwa tohara. Kifaa ambacho hutumiwa sana ni wembe. Wembe huo hutumiwa kuwakatia wasichana wote ambao wanapashwa tohara katika kipindi hicho. Wembe huo hauchemshwi angalau kuua viini vinavyosababisha na kueneza magonjwa mbalimbali. Hali hii huwaweka wasichana hao kwenye hatari ya kuambukizwa ugonjwa hatari wa ukimwi. Licha ya hivyo wasichana waliotahiriwa nguvu za kinga dhidi ya magonjwa hupungua. Kwa hivyo wanaweza kupata magonjwa mengine ya kuambukiza kwa urahisi. Kwa hivyo ukeketaji ni tendo la hatari na la kumdhalilisha mwanadamu

ambalo linastahili kulaaniwa.

Maswali

(a) Ukizingatia mambo muhimu anayoeleza mwandishi, fupisha aya tatu za kwanza. (Maneno 70) (alama 9, 1 ya mtiririko)

Matayarisho

Nakala safi

(b) Eleza mambo anayoeleza mwandishi katika aya mbili za mwisho. (Maneno 50)(alama 6, 1 ya mtiririko)

Matayarisho

Nakala safi

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a) Eleza tofauti iliyopo kati ya jozi hii ya sentensi. (alama 2)
(i) Rehema alinikimbilia
(ii) Rehema alinikimbia

b) Yakinisha (hali ya kukubali) huku ukigeuza sentensi ifuatayo katika nafsi ya pili kwa umoja.
Nisiposamehewa na Mola sitapata amani mchana kutwa.
(alama 2)

c) Eleza kwa kutolea mifano matumizi **mawili** ya kiambishi maalu "Ku." (alama 2)

d) Andika sentensi zifuatazo kwa wingi. (alama 2)
(i) Ngoma ile inalia vibaya kwa kuwa imepasuka.
(ii) Ni mlango upi uliofungwa na wewe nilipoenda maktabani?

e) Tunga sentensi ukitumia vihisishi hivi. (alama 2)
(i) Ahaa!
(ii) Taib!

f) Geuza kitenzi kilichopigwa mstari kiwe jina bila kubadilisha maana ya sentensi.
(alama 2)
Walimu wanawajibika kuwakomeza vyema wanafunzi wao.

g) Andika sentensi zifuatazo kwa kufuata maagizo.
(alama 2)
(i) Watoto wanakumbana na dhiki kubwa kuna haki za watoto (Anza: Fauka ya ….)
(ii) Tarishi alikula staftahi. Tarishi alienda Ofisini (Anza: Licha ya ……..)

h) Andika neno jingine lenye maana sawa. (alama 2)
(i) Heshima:……..
(ii) Ruhusa:……

i) Eleza maana ya misemo ifuatayo.
(alama 2)
(i) Enda jongomeo:…….
(ii) Piga unyende:…….

j) Tunga sentensi ukitumia neno "kile" kama
(i) Kivumishi (alama 1)
(ii) Kiwakilishi (alama 1)

k) Eleza tofauti iliyopo kati ya tanakali hizi za sauti.
(alama 2)
Anguka chubwi na anguka tapwi.

l) Tunga sentensi za kuonyesha kuwa unaelewa tofauti kati ya maneno yafuatayo.
(alama 2)
(i) Gati
(ii) Kati

m) Tumia –enye au –enyewe kukamilisha sentensi zifuatazo.
(alama 2)
(i) Shule …… shida daima husaidiwa.
(ii) Kucheza …….... kulikuwa kwa kupendeza.

n) Tunga sentensi sahihi ukitumia vitenzi vifuatavyo vikiwa katika hali ya kufanyiza.
(alama3)
(i) La:……
(ii) Nywa:……
(iii) Fa:…….

o) Andika neno **moja** lenye sauti king'ong'o.
(alama 1)

p) Changanua sentensi ifuatayo ukitumia kielelezo cha mstari.
(alama 3)
Samaki huogelea mtoni.

q) Andika sentensi inayoonyesha 'ki' ya masharti. (alama 1)

r) Onyesha viambishi awali na tamati katika kitenzi. Alimkemea. (alama 2)

s) Bainisha matumizi ya 'ni' katika sentensi zifuatazo.
(alama 2)
(i) Ondokeni:…….
(ii) Kiptoo ni mwizi sugu:……

t) Eleza maana mbili zinazojitokeza katika sentensi hii.
(alama 2)
(i) Alimpigia simu

4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)

(a) Eleza majukumu **matatu** ya lugha ya taifa.
(alama 3)

(b) Fafanua mtindo wa lugha uliotumiwa katika taarifa ifuatayo huku ukieleza sababu za matumizi ya vitambulisho maalum vya lugha.
(alama 4)
Wananchi, mimi sina mengi. Hapana katika nyinyi asiyenielewa. Sina la kusema, ila ninawakumbusheni kuwa mnahitaji kiongozi atakayeshughulikia maslahi ya taifa zima. Mtu huyo ni mimi na ninajitahidi niwezavyo kujenga masoko, barabara, shule zaidi na mazahanati na maisha yenu yatakuwa ya raha zaidi.

(c) Thibitisha kuwa adabu za lugha hazizingatiwi miongoni mwa wanajamii siku hizi.
(alama 3)

TATHMINI YA PAMOJA YA KAUNTI NDOGO YANANDI KASKAZINI 2015
Cheti cha kuhitimu masomo ya kidato cha nne
102/3
KISWAHILI
FASIHI
KARATASI YA TATU
SEHEMU YA A: USHAIRI (SWALI LA LAZIMA) (alama 20)

8. **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

1) Nilifika Nairobi, jiji bora na mufti,
Palipojaa shababi, wazee na mabenati,
Nikasalimu kibibi, kanijibu eti fiti!
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

2) Kibibi kasonga kwangu, nimpe kiti asiti,
Nikaona mbele yangu, kwa mapozi kajiseti,
Sikupatwa na uchungu, wala chembe kibuhuti,
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

3) Kumwuliza wenda wapi, kanijibu marikiti,
Kwenye kazi au vipi, jibu lake nina deti,
Ana majibu mafupi, na taimu hawesti,
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

4) Mtu huyu hushangaza, lugha yake sijageti,
Hataki kunisikiza, ati mimi sina senti,
Bila doo aeleza, yu tayari kunibuti,
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

5) Punde dakika kidogo, nikaanza utafiti,
Naona ana mikogo, na haogopi umati,

Hawataki wa ushago, wenye koti bila noti.
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

6) Ni kibibi maridadi, ila mambo tofauti,
Asema mboga si fudi, bwana kunipa donti,
Chuma mobu sina budi, kujaza langu poketi
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

7) Ana fujo hatulii, sijaonapo laiti,
Arifu hunibalii, kamsosi hata switi,
Ebu acha uchalii! Huji homu kwa kufuti,
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

8) Na kutaka kualee, akawasha sigareti,
Hamuogopi madhee, asije kumripoti,
Pegi mbele ya fadhee, mkali kama ghosti,
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

9) Alipozidi udhia, nikaanza kumsweti,
Naye akaniwevia, kuniona simfati,
Sistee kaingia, kwa motii kalosti,
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

10) Nikabaki kudangana, la kusema silipati,
Lugha zetu kulingana, hakuna japo katiti,
Ndipo hatukuelewana, hadi kuenda benati,
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

11) Kudadisi kwa makini, tabia na harakati,
Za vijana wa mjini, zina nyingi atiati,
Tafadhali jikanyeni, ni huu ndio wakati,
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

12) Hunishangaza jamani, tuelezane kwa dhati,
Nairobi mitaani, pa watu watanashati,
Panasemwa lugha gani, na kanuni haifati!
Vijana na mabenati, kipi Kiswahili hiki?

MASWALI

(a) Mtunzi wa shairi hili ana dhamira gani? (alama 2)
(b) Taja na ueleze bahari mbili za shairi hili ukizingatia:
(alama 4)
d. Vina
e. Vipande
(c) Kwa kutoa mfano mmoja mmoja, onyesha aina **mbili** za idhini ya kishairi katika shairi hili.
(alama 4)
(d) Taja na ufafanue tamathali **mbili** za usemi zilizotumiwa katika shairi hili
(alama 4)
(e) Andika ubeti wa kumi katika lugha nathari.
(alama 4)
(f) Eleza maana ya msamiati ufuatao ulivyotumika. (alama 2)
(i) Shababi
(ii) Mikogo

SEHEMU YA B: RIWAYA – KIDAGAA KIMEMWOZEA – KEN WALIBORA

Jibu swali la 2 au 3

9. "Wema wako umeniua kabisa. Kuna mahakama ndani ya moyo wangu nanakojishtaki mwenyewe…."
(a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
(b) Taja na ueleze tamathali mbili zilizotumiwa kwenye muktadha huu.
(alama 4)

(c) Ukirejelea Riwaya nzima, jadili makosa ambayo mnenaji wa maneno haya anajishtaki kwayo.

(alama 12)

10. "Amani ni mhusika anayestahili kuigwa katika jamii." Thibitisha ukweli wa kauli hii ukirejelea Riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 20)

SEHEMU C: TAMTHILIA
MSTAHIKI MEYA (TIMOTHY M. AREGE)
Jibu swali la 4 au 5

11. "Tunaweza kutangaza katika vyombo vya habari. …. Watu wengi huko nje wana njaa."
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Fafanua sifa **mbili** za mzungumzaji wa dondoo hili.
(alama 2)
(c) "Hali inayoipata Cheneo katika muktadha ambambo dondoo hili limekitwa ni msiba wa kujitakia." THibitisha.
(alama 14)
12. Anwani 'Mstahiki Meya' ni kinaya. Jadili. (alama 20)

SEHEMU YA D: HADITHI FUPI.
K. Walibora na S.A. Mohammed - Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine.
Jibu swali la 6 au la 7
"Damu Nyeusi" (K. Walibora)

13. "Waafrika hupitia matatizo mbalimbali wakiwa masomoni ughaibuni." Jadili.
(alama 20)
au
"Ndoa ya Samani" (Omar Babu)
14. "Hapa huingii bila kunionyesha mkono."
(a) Fafanua muktadha wa dondoo hili.
(alama 4)
(b) Eleza sifa **mbili** za msemaji katika dondoo hili. (alama 4)
(c) Jadili maudhui sita yanayojitokeza katika hadithi hii.
(alama 12)

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

15.
(a) Eleza sifa **tano** bainifu za fasihi simulizi. (alama 5)
(b) Taja njia **mbili** za kisasa za kuhifadhi fasihi simulizi.
(alama 2)
(c) (i) Eleza sifa za misimu. (alama 7)
(ii) Taja njia mbalimbali za kuunda misimu katika jamii. (alama 6)

WILAYA YA NANDI KASKAZINI 2015
102/1
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

1. Hii ni insha ya kiuamilifu –
- Sura ya kumbukumbu izingatiwe:
- Kuwe na anwani, mahali, tarehe na saa.
- Orodha ya waliohudhuria.
- Waliotuma udhuru.
- Waliokosa kutuma udhuru.
- Waalikwa wengine.
- Ajenda.

Maudhui yagusie yafuatayo:
- Visa vya kuzorota kwa amani K.V. ujangili, utekaji-nyara, ujambazi, dhuluma mbalimbali kwa umma, ujambazi na uhalifu mtaani, mauaji, ubakaji, wizi, K.V wa mifugo nk.
*ataje wahasiriwa, wahusika.
- Hatua za kudhibiti usalama k.v. mpango wa nyuma kumi.

2. Hii ni insha ya mjadala.

- Mtahiniwa aweza chukua upande wa kuunga mkono au kupinga kwa kutoa hoja maridhawa.
- Kisha atoe msimamo baadaye kuhusu upande anaouegemea.
- Asiegemee upande mmoja tu.

Hoja za kuunga mkono

- Raia wajiletee dhidi ya udhalimu wa mafisadi wanaojinufaisha kwa hadaa.
- Umma uwe macho na kupaza sauti dhidi ya wale wanaokula au kutoa milungula / hongo.
- Idara za kijasusi ziwe macho ili wanaopiga vita ufisadi wasiangamizwe.
- Wanaopiga vita wawe tayari hata kuwashtaki marafiki zao.
- Utaratibu ubuniwe ili kuweza kuwanasa mafisadi bila kubagua.
- Tume ya kupambana na ufisadi iongozwe na watu wasiokuwa na doa au kushawishika.
- Sheria kali za kukabiliana na mafisadi zahitajika.

Hoja za kupinga

- Ufisadi haujakita mizizi kama vile vyombo vya habari vingependa tuamini.
- Ni viongozi tu ambao huendeleza ufisadi ikilinganishwa na raia / umma.

3. Mtahiniwa atoe kisa kinachoafikiana na maana kuwa maneno aliyoyasema mtu yameweza kuzua madhara au matatizo makubwa, k.v. – uchochezi unasababisha:

1. chuki
2. vita
3. kuchomeana makazi
4. kuharibu mali na
5. kufurushwa kwa watu na kuwafanya kuwa wakimbizi.

4. Mnenaji asawiriwe aking'ang'ania kufanya jambo walilopatana na wenazake.

1. wenzake hawafanyi vile.
2. Ndiye tu anaendelea na jambo hilo.

Tanbihi

Mtahiniwa asipomalizia maneno hayo amepotoka atuzwe (D 02/20) atakuwa amejitungia swali.

WILAYA YA NANDI YA NANDI KAZKAZINI 2015

102/2

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

5. **UFAHAMU**

(a) Kuingiza bidhaa au gesi zisizohitajika katika mazingira.

(b) Huongeza gesi zinazoharibu ukanda wa ozoni.

(c) Gesi zinazotokana na jokofu, marashi ya upakiaji bidhaa huharibu ukanda wa oksijeni unaokinga miale mibaya ya jua.

(d)

- Mvua ya asidi huua mimea, kuathiri majengo na kuwaua wanyama.
- Madini ya risasi huathiri mfumo wa akili ya binadamu.
- Huweza kusababisha majanga ya moto.
- Huathiri afya za binadamu.

(e) Idadi kubwa ya magari – magari haya hutoa moshi unaochanganya gesi ambazo huungana na nyingine zinazoletwa na viwanda vikubwa.

(f)

- Uchafuzi wa hali ya anga.
- Uchafuzi wa kiajali.

(g)

- Msambao – maenezi.
- Makopo – vyupa vya plastiki. Aondolewe hadi alama 6.
- Sarufi – alama 3
- Hijai –alama 3
- Jumla –alama 6

6. UFUPISHO

(a)

- Ukeketaji ni upasuaji unaofanyiwa wasichana na wanawake.

- Hupatikana barani Afrika na sehemu nyingi ulimwenguni.
- Umri ambapo ukekeaji hufanyika hutegemea jamii.
- Mwanamke anaweza kufanyiwa ukeketaji siku chache baada ya kuzaliwa au baada ya kujifungua mtoto wake wa kwanza.
- Jamii huthamini amali hii kwani ni hatua ya mpito wa maisha.
- Hufungamana kuwapa wasichana mafunzo kuhusu kanuni za uzazi, malezi na ndoa.
- Dhimu kuu ni kuwapunguzia wanawake uchu na kuhifadhi ubikira.
- Wanaume husisitiza tohara kama kigezo cha mwanamke kuolewa.
- Wanawake wenyewe huhakikisha watoto au wajukuu wanapashwa tohara.

(b)

- Ukeketaji una madhara na unadhalilisha wanawake.
- Wanawake huvuja damu na aghalabu huaga dunia.
- Wale wanaopona huwa na hatari ya kuambukizwa maradhi ya zinaa.
- Madaktari wanadai uchungu wa uzazi huwa mwingi na hudumu muda mrefu.
- Wembe utumiwao hauchemshwi kuua viini.
- Wasichana wanaotahiriwa nguvu za kinga dhidi ya magonjwa hupungua.
- Ukeketaji humdhalilisha mwanamke na unastahili kulaaniwa. (Aondolewe hadi alama 3)

7. MATUMIZI YA LUGHA

(a) (i) Rehema alikimbia kuja upande nilipokuwa / upande wangu kunilaki / kwa niaba. (alama 1)
(ii) Rehema alinitoroka kwenda mbali nami. (alama 1)

(b) Ukisamehewa na Mola utapata amani mchana kutwa. (alama 2)

(c) Kiambishi 'ku'

- Hutumiwa kama kiambishi ngeli cha nomino zinazoundwa kutokana na vitenzi (kuchuuza).
- Hutumiwa kama kiambishi cha upatanisho wa kisarufi (mf. Kuigiza kuzuri kulituzwa)
- Hutumiwa kama kiambishi cha kuonyesha mahali lakini bila kudhihirisha sehemu mahususi (mf. huku)
- Kiambishi hutumiwa pamoja na vitenzi vyenye silabi moja (mf. ku-cha, ku-fa).
- Hutumiwa kusimamia wakati katika ukanusho wa sentensi za wakati uliopita (mf. hakuenda).

(Hoja zozote 2 x 1 = alama 2)

(d) (i) Ngoma zile zinalia vibaya kwa kuwa zimepasuka. (alama 1)
(ii) Ni milango ipi iliyofungwa na ninyi tulipoenda? (alama 1)

(e) (i) Ahaa! – Hutumiwa kuonyeshea furaha au hata mshangao; huonyesha pia mgutuko baada ya kutambua jambo mf. Ahaa! Alisema na kuruka juu kwa furaha baada ya kusikia kuwa alifuzu kazi.
a. Taib! Hutumiwa kuonyesha kupendezwa na jambo au kukubaliana na hali fulani. Mf. Taib! Naona umefaulu sasa.

(f) Walimu wana wajibu wa kufanya wanafunzi wao wakomae vyema. (alama 2)

(g) (i) Fauka ya kuwa na haki za watoto, watoto wanakumbana na dhiki kubwa. (alama 1)
(ii) Licha ya tarishi kula staftahi, alienda ofisini. (alama 1

(h) (i) Heshima – staha, taadhima. (alama 1)
(ii) Ruhusa – kibali, idhini. (alama 1)

(i) Maana
(i) Enda jongomeo – Fariki, kufa (alama 1)
(ii) Piga unyende – Lia kilio kinachoonyesha hofu. (alama 1)

(j) (i) Neno "kile" kama kivumishi.
K.m kiti kile kinafanana na cha kakangu (baada ya jina).
(ii) 'Kile' kama kiwakilishi.
Mf. Kile kilinunuliwa juzi kwa bei ghali (badala ya jina)

(k) Anguka chubwi – Kuanguka majini au kwenye kitu kiowevu.
Anguka tapwi – Kuanguka matopeni.

(l) Atunge sentensi kuonyesha:
(i) Gati – Ni mahali pa kushika pwani kutoka chomboni.
(ii) Kati – Ni baina ya kitu na kingine.
Waandike sentensi za kutofautisha maana kwenye kila jozi. Mtahiniwa akitoa maana bila sentensi, atuzwe nusu (½) alama badala ya alama moja.

(m) (i) Yenye
(ii) Kwenyewe (alama 2)

(n) (i) La – lisha
(ii) nywa – nywisha / nywesha
(iii) fa – fisha (alama 3)

(o) Ng'ombe
Nyanya
Ngano (Mwalimu akadirie mengine) (alama 3)

(p) Samaki huogelea mtoni. (alama 3)
S ⟶ KN(N) + KT(T + E)

(q) Ukimwona mwambie namwita.

(r) Alim-awali.
ea-tamati

(s) (i) Amri
(ii) Kitenzi kishirikishi kipungufu.

(t)
- Kwa niaba
- Kumpa ujumbe kupitia kwa simu.

Makosa ya sarufi yaondolewe kila yanapotokea hadi nusu ya alama alizotuzwa katika kila kijisehemu. Makosa ya hijai yaondolewe hadi alama 3.

8. ISIMU JAMII

(a)
- Huunganisha watu wa taifa.
- Huziba mipaka ya kikabila.
- Hukuza utamaduni wa kiafrika.
- Hukuza uzalendo.
- Hutambulisha watu wa taifa fulani.
- Huleta maendeleo ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kisayansi kutokana na umoja wa kitaifa kilugha.
- Hufanikisha harakati za uongozi.
- Husawazisha watu kilugha kwa sababu hisia zitakuwa sawa. (Hoja zozote 3x1 = alama 3)

(b)
(i) Lugha ya mwanasiasa.
a. Husema mengi ingawa huwaambia watu kuwa ana machache.
b. Hujisifu mwenyewe.

(c)
(i) Watu hawazingatii usanifu wa lugha tena na hutumia sheng' pakubwa katika mazungumzo yao.
(ii) Watumiaji wa sheng' hawazingatii umri na vyeo vya wanaozungumziwa.
(iii) Tatizo la sheng' limekuwa chanzo cha kuzorota kwa viwango vya lugha katika shule.
(Hoja 3x1 = alama 3)

<u>MAKOSA YA HIJAI</u>
Haya ni makosa ya maendelezo na yanatatiza matamshi.
1) Kutenganisha neno kama aliye kuwa.
2) Kuungaisha maneno kama kwavile
3) Kukata silabi vibaya kama ng-ano.
4) Kuandika herufi isiyofaa katika neno kama tata badala ya dada.
5) Kuacha herufi inayofaa katika neno kama tbia.
6) Kuongeza herufi isiyofaa katika neno kama 'piya'
7) Kuacha alama inayotarajiwa kuwepo katika neno kama 'ngombe' badala ya ng'ombe.
8) Kutoandika kistari cha kukata neno ufikiapo pambizo au mwisho wa mstari.
9) Kuandika neno kwa ufupi k.v.
- Kila kosa liadhibiwe mara mbili kwenye maneno mawili tofauti.

<u>MAKOSA YA SARUFI</u>
Haya ni makosa yanayotatiza maana au kukiuka sheria za sarufi.
1) Kuakifisha vibaya k.m. nukta, koma n.k.
2) Kutumia herufi kubwa au ndogo visivyo / pahali si pake.
3) Matumizi mabaya ya ngeli, viambishi, nyakati, mnyambuliko n.k.
4) Kuacha au kuongeza neno katika sentensi.
5) Kuchora kistari mwanzo wa sentensi.

6) Miundo mibaya ya sentensi.

MATUMIZI YA HERUFI KUBWA

1) Mwanzo wa sentensi
2) Majina ya pekee kama:

(i) Watu
(ii) Mahali k.m. miji, nchi n.k.
(iii) Siku za juma k.m. Ijumaa
(iv) Majina ya miezi k.m. Januari
(v) Mashirika na taasisi.
(vi) Masomo k.m. Fizikia.
(vii) Vitabu kama Asali Chungu.
(viii) Makabila k.m. Hausa.
(ix) Lugha k.m. Kiswahili.
(x) Majina ya Mungu kama Rabuka, Yahweh n.k.

- Tuza alama zaidi kabla ya kuadhibu kosa la hijai.
- Usiondoe zaidi ya nusu ya alama ulizotuza katika jibu la mtahiniwa.

WILAYA YA NANDI KASKAZINI 2015
102/3
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

1. **SEHEMU YA A – USHAIRI**

(a)
- Anahimiza matumizi bora ya Kiswahili miongoni mwa vijana na mabenati.
- Kuonyesha jinsi vijana wa Nairobi / Jijini hutumia Kiswahili kwa njia isiyofaa / isiyoeleweka na wazee / wengi.
- Kuonyesha jinsi vijana wa mjini walivyopotoka kimaadili. (1x2= alama 2)

(b)
(i) Vina – Ukara
Vina vya ukwapi vinabadilika ilhali vya utao vinatiririka ubeti hadi mwingine.
(ii) Vipande – Mathnawi
- Kila mshororo umegawika katika vipande viwili: ukwapi na utao. (2x2= alama 4)

(c)
- Matumizi ya sheng' lugha ya mtaani k.m. ushago, madhee, fadhee, doo.
- Utohozi – deti, taimu, fudi, sigareti n.k.
- Kuboronga sarufi / sintaksia ngeni.
- La kusema silipati – silipati la kusema.
- Kipi Kiswahili hiki – Kiswahili hiki ni kipi
- Ni huu ndio wakati – wakati ndio huu.
- Inkisari – wenda – unaenda. yu – yuko. Idhini na mfano. (2x2= alama 4)

(d) Tashbiha / Tashbihi
- Mkali kama ghosti.
- Maswali balagha
- Kibwagizo …kipi Kiswahili hiki. (2x2= alama 4)

(e) Mshairi anasema kuwa <u>alibaki</u>
(i) <u>kudangana / kutafuta na hakupata la kusema.</u> Anaendelea kusema kuwa <u>lugha zao hazikulingana / kufanana hata kidogo.</u>
(ii) Anaongeza kuwa <u>hali hii iliwafanya wasielewane.</u>
(iii) Hadi benati <u>alipoondoka.</u> Anasisitiza kwa <u>kuwauliza vijana na mabenati aina ya Kiswahili</u>
(iv) <u>Wanachokitumia.</u> (4 x 1 = alama 4)

(f) (i) Shababi <u>– kijana.</u>
(ii) Mikogo – maringo / majitwezo / mashobo / majitapo / majishawo. (1 x 2 = alama 2)

2. **RIWAYA**

(a) Msemaji – Mtemi Nasaba Bora.
Msemewa – Amani
Mahali – Sebuleni katika kasri la mtemi / nyumbani mwa mtemi.
Kisa – Baada ya Amani kumwokoa. Mtemi Nasaba Bora asilipuliwe na Gaddafi na kumfanya aungame maovu yake. (4x1 = alama 4)

(b) Tashihisi / uhuishaji – wema wako umeniua.
Jazanda – moyo kuwa mahakama. Kutaja 1, mfano 1 (2 x 2 = 4) za kwanza mbili

(c)
- Wizi wa mashamba ya wanyonge – Chichiri Hamadi, mamake Imani.
- Uzinifu / uasherati – Lowela / Kushiriki mapenzi na msichana mchanga.
- Kusingizia watu makosa / kutoa hongo – Yusuf Hamadi.
- Mapigo – Amani / Kumpiga Amani kikatili.
- Kumpagaza Amani mzigo – mtoto Uhuru.
- Anawafungia Amani na Imani korokoroni bila makosa.
- Amtaliki mkewe kwa shutuma tu – mke amekuwa mwaminifu.
- Anawafuta wafanyakazi wake kiholela.
- Kuficha faili katika wizara ya ardhi.
- Kumficha Lowela ilhali wazaziwe wanamtafuta.
- Hakuchanja mbwa wake – hakujali Dj alipoumwa na Jimmy.

- Alifuja pesa za kujengea hospitali – akajenga zahanati.
- Hakumjali mama anayejifungua kando ya barabara. (kutaja-1, kueleza1) (6x2 = alama 12)

3. **RIWAYA**

(i) Mwenye utu
- Anampa Dj SHATI.
- Alikubali kuandamana na Imani hadi Sokomoko.
- Aliokoa maisha ya Mtemi – kulipuliwa na Gaddaffi.
- Aligawia maskini shamba – k.m. Dj.
- Alikubali kukilea kitoto alichokiokota.

(ii) Mzalendo Halisi
- Alihudhuria sherehe ya siku ya wazalendo.
- Alishrikiana na Madhubuti kukomboa Tomoko.
- Alimkabili Mtemi na kumkosoa dhidi ya udhalimu.
- Anahimiza watu kutokubali dhuluma.

(iii) Msiri
- Hakumwambia Imani sababu ya kutafuta ajira Sokomoko.
- Hakumwambia yeyote kuwa aliwahi kusoma hadi chuo kikuu ila Madhubuti alipogundua ujuzi wake.
- Alijua kuwa Mtemi ndiye aliyemuua babuye na kumfungisha Yusuf – hakamwambia yeyote.
- Alijua kuwa mwalimu Majisifu ndiye aliyeiba mswada wake na kuchapisha; aliiweka siri.
- Alimficha Imani asili yake.

(iv) Ni msamehevu.
- Alimsamehe Mwalimu Majisifu kwa kumwibia mswada.
- Alimsamehe Mtemi – baada ya kumpiga na kuiba shamba.

(v) Ni mtetezi wa haki / mkombozi
- Anapinga dhuluma zilizofanyiwa wanyonge.
- Aliwarudishia walionyang'anywa mashamba yao.
- Aliwahimiza watu kutokubali dhuluma – hotuba yake.

(vi) Ni jasiri
- Alimwokoa Mtemi asilipuliwe na Gaddafi.
- Alimwambia Gaddafi ampige risasi.
- Alimkabili Mtemi kwa maswali mazito.
- Kuvunja mwiko na kunywa maji ya mto Kiberenge pamoja na Imani.

(vii) Ni kijana mpole
- Hakujibizana na askari alipokuwa seli.
- Alifanya kazi kwa Mtemi kwa unyenyekevu.
- Alikaa kwa upole kwa mwalimu Majisifu na kusoma vitabu.
- Aliwasihi wauguzi katika hospitali ya Nasaba Bora wamtibu mtoto Uhuru.

(viii) Mwenye bidii
- Alisoma na kupita mitihani – akaenda chuo kikuu.
- Alifanya kazi kwa bidii kwa Mtemi – akapendwa na Zuhura na wafanyakazi wengine.

(ix) Mchunguzi / jasusi hodari
- Alifanya ujasusi wa kina na kulikomboa shamba la babuye.
- Alichunguza na kuthibitisha kuwa Mtemi ndiye aliyemfunga Yusufu.

(x) Mvumilivu
- Alichukua miaka mingi kufanya uchunguzi kuhusu wizi wa shamba la babuye, kufungwa kwa amu yake, na mswada wake.

(xi) Ni msomi
- Alielewa maana na lengo la elimu.
- Alipita mtihani.
- Alifika chuo kikuu.
- Alivichambua vitabu vya fasihi – alilinganisha na maisha halisi ya jamii. (zozote 10x2 = 20)

TANBIHI: Mtahiniwa atoe sifa na mfano wake.

4. **MSTAHIKI MEYA**

(a) Msemaji – Diwani wa I
Msemewa – Meya, Diwani II

Mahali – ofisini mwa meya.
Sababu / kisa – Baada ya wafanyakazi wote wa baraza kugoma walipokuwa wanawatarajia wageni. (alama 4x1 = alama 4)

(b)
- Ni kibaraka / kikaragosi – anakubaliana na mikakati yote ya Meya pasi kuuliza swali.
- Msaliti – kutoa ushauri mbaya bila kujali raia.
- Fisadi – kushiriki katika kuidhinisha malipo ya 'overtime', hataki kulipa kodi.
- Mwenye mtazamo finyu / asiyeona mbele – Haoni mantiki katika maelezo ya Diwani wa III kuwaza kuhusu vitu vidogo – mavazi. (za kwanza mbili) (1 x 2 = alama 2)

(c)
- Kupuuzwa kwa wafanyakazi / Meya hataki kufanya mazungumzo – 'diary' ya Meya imejaa. Meya hataki mazungumzo / Hayuko tayari kuzungumza na wawakilishi wa wafanyakazi.
- Diwani wa I na II wanashindwa kuwajibika kama washauri wa Meya. Wanashiriki katika njama za kulifilisi baraza.
- Uundaji wa kamati nyingi – unachangia gharama zaidi kwa baraza la mji.
- Meya anafanya maamuzi mabaya ya kifedha.
- Meya anaidhinisha malipo kwa watu wasio wafanyakazi wa baraza. Bili, mhubiri.
- Meya anadunisha huduma zilizopo – elimu / matibabu – anawasomeshea wanawe ng'ambo, mkewe kujifungulia ng'ambo.
- Meya anapuuza ushauri wa Diwani wa III kuhusu maswala ya fedha – kodi, nyongeza.
- Wanataaluma kama Siki kutoshiriki katika maswala ya siasa. Wasio na elimu / ujuzi ndio hutawala – Meya.
- Meya kumshauri mwanakandarasi wa awali kulishtaki baraza la mji – analimbikizia baraza deni.
- Usimamizi wa baraza umeshindwa kuwahalikishia wafanyakazi mazingira bora ya kufanyia kazi. Waosha vyoo hawana glavu.
- Viongozi kutowaongezea wafanyakazi mshahara licha ya kupanda kwa gharama ya maisha.
- Meya anacheka na kufurahi wakati askari wanawapiga waandamaji risasi na kuwatawanya – matumizi mabaya ya vyombo vya dola / ukosefu wa usalama.
- Wanaoandamana (kwa utulivu) wanaitiwa askari badala ya kushughulikiwa / kunyima wafanyakazi haki ya kugoma.
- Viongozi wanaendeleza wizi wa mali ya umma badala ya kupinga – kuiba ardhi, kuuza fimbo.
- Viongozi wanakosa kutekeleza ahadi walizowatolea raia waliowachagua.
- Viongozi wanafisidi nchi kwa kutengeneza mipango ya kimilenia ambayo hawazingatii / viongozi kutozingatia mipango ya maendeleo,
- Meya anawafanya wanacheneo kuwa wategemezi wa misaada.
- Viongozi wanasababisha kuzorota kwa hali ya usafi Cheneo kwa kutoshughulikia maslahi ya wafanyakazi. (zozote x2 = alama 14)

5. <u>MSTAHIKI MEYA</u>

Sababu za kuonyesha kuwa hakustahiki / hakufaa.
- Ubinafsi / tamaa – kuchukua vipande vya ardhi na kuwagawia rafikize / madiwani kutolipa kodi.
- Vitisho kwa wafanyakazi badala ya kuwasiliana nao vizuri. Kufuta kazi / kushinikiza raia wamuunge mkono.
- Kuajiri kwa mapendeleo / ubaguzi – mhazili wake – ufisadi.
- Baraza kukosa mahitaji muhimu – dawa, maji safi, chakula.
- Matumizi mabaya ya mamlaka / cheo – kulipa Bili, mhubiri.
- Kushiriki wizi wa mali ya umma – ardhi, fimbo.
- Kuhusisha marafiki katika uongozi wa baraza – Bili.
- Kukubali nyongeza ya mishahara ya madiwani / hakujali wafanyakazi.
- Ubadhirifu / ufujaji wa mali – divai, mvinyo. Kupeleka watoto ng'ambo.
- Kubagua / kupendelea / kutenga viongozi – Diwani III.
- Hakuviinua viwango vya elimu na matibabu Cheneo – anapendelea ng'ambo.
- Meya anapuuza ushauri wa wataalamu wa maswali mbalimbali / kuwatenga washauri bora.
- Wafanyakazi hawathaminiwi – mishahara duni, kuchelewa.
- Ametelekeza raia / hajali maisha / hali za wanyonge – mama Dadavuo.
- Mkosa utu / huruma – hajali vifo vya raia – 'mmoja tu.'

- Wananchi wanyonge wanalazimishwa kutoa kodi – madiwani wanatengwa.
- Meya ameshindwa kuwapa ajira raia wake – vijana wengi wamefuzu lakini hawana ajira.
- Kutotimiza ahadi / udanganyifu / propaganda.
- Matumizi mabaya ya vyombo vya dola – askari na vyombo vya habari.

6. **SEHEMU YA D**

- Kubaguliwa na wazungu – basi linampita
- Wahadhiri wanawanyima alama.
- Jaji anamtoza faini ya juu kuliko kawaida.
- Kutozwa faini wanapofanya makosa madogo k.m. kutofunga zipu.
- Kushtakiwa na kufungwa gerezani.
- Kuhadaiwa na kuporwa mali – alivyofanyiwa na Fiona / Bob.
- Baridi kali – hawakuzoea.
- Kushukiwa kuwa wezi – akiwa duka la jumla.
- Kuonewa k.m. kupewa alama chache katika mitihani vyuoni.
- Kutazamwa kwa dharau – mikahawani (aliposahau kufunga zipu).
- Kuulizwa maswali ya kukera / kuchosha kuhusu waafrika wenzao – mwaishi mitini kama tumbili.
- wasichana wenu wanakeketwa.
- Kulazimishwa washiriki ngono k.m. alivyofanyiwa na Fiona. (zozote 10x2 = 20)

7. (a) Msemaji – Bwana mmoja.
Msemewa – Msimulizi / Abu
Mahali – Mlangoni / kwa akina Amali.
Sababu / kisa – Hakutaka 'dadake' atoke kwao bila yeye kupewa kitu. (4 x 1 = alama 4)

(b)

- Mwenye tamaa ya mali – anaomba pesa msimulizi.
- Mbinafsi – angetaka afaidike binafsi.
- Mwongo / laghai – si kakake halisi wa Amani. (1 x 2 = alama 2) (za kwanza mbili)

(c) (i) Umaskini

- Kijijini mwa msimulizi kila mtu alikuwa maskini. Hakuna aliyeweza kumsaidia mwingine.
- Awali (miaka saba) msimulizi alikuwa fukara.
- Pesa ya msimulizi ilikataliwa mwanzoni – hangeweza kulipia mahari, kumlisha mke.

(ii) Tamaa ya mali

- Bwana aliyemzuia msimulizi mlangoni.
- Msimulizi alipewa orodha ndefu ya vitu vya thamani alivyohitajika kununua ili amwoe Amali.
- Msimulizi anakubaliwa kumwoa Amali – sasa ana mali.

(iii) Utabaka

- Maskini hana ruhusa ya kuoa kutoka tabaka la juu / kati.
- Msimulizi anapopata mali, anaruhusiwa kumwoa Amali.

(iv) Ubinafsi

- Mamake Amali – alipenda mali (alipogundua kuwa msimulizi ni tajiri).
- Amali hampingi mamake / haingilii.
- Familia yote ya Amali inapanga harusi bila kumhusisha Amali.
- Orodha ya vitu vya thamani

(v) Bidii / juhudi katika kazi.

- Msimulizi anafanya bidii ili aoe.
- Anaendeleza bidii akiwa Arabuni.
- Anatajirika na kupeleka posa mara ya pili.

(vi) Mila na desturi

- Mila zinakwamiza watu / zinawanyima watu haki k.m. mila ya mahari.
- Mjomba huhusishwa katika maswali ya ndoa.
- Matumizi ya nyimbo katika arusi – maana fiche.
- Bwana arusi anatozwa kiingilio / mahari.

(vii) Nafasi ya mwanamke katika jamii – anachaguliwa mume.
(viii) Nafasi ya wazazi katika ndoa ya wanao – wanamchagulia mume Amali.
(kutaja-1, kueleza 1 = 2) (zozote 6x2=alama 12)

8. (a)

- Huwa na fanani / msimulizi anayeonana ana kwa ana na hadhira yake.
- Huwa na hadhira mahususi / maalum – hadhira tendi / hai.
- Ina wahusika maalumu – binadamu, wanyama au viumbe wengine.
- Huwa na fomula – funguzi / kuanzia – fungia / kumalizia.
- Husambazwa / huwasilishwa kwa njia ya mdomo.
- Huambatana na utendaji / uigizaji – matumizi ya maleba.
- Huwa na wakati wa mazingira maalum ya uwasilishaji wake – asubuhi, usiku.
- Hurithjswa kutoka kikazi kimoja hadi kingine.
- Hapo awali, zilihifadhiwa akilini / kumbukizi / nyoyoni na katika mazingira.
- Hubadililika – hutegemea hadhira, wakati n.k.
- Huzaliwa, hukua na kufa.
- Ina historia ndefu – ni kongwe. (zozote 5x1 = alama 5)

(b)

- Maandishi – kwenye vitabu / majarida.
- Kupitia picha – kamera.
- Sinema / video / filamu.
- Tepurekoda / vinasa sauti / kanda za kunasa sauti.
- Diski za kompyuta / Diski tepetevu. (za kwanza mbili) (2x1 = alama 2)

(c)

- Huzuka na kutoweka / hubuniwa na kutoweka baada ya muda k.m. manyanga.
- Baadhi ya misimu husanifishwa na kukubaliwa katika lugha sanifu k.m. toa chai – hongo.
- Hujikita katika vikundi mbalimbali vya wanajamii k.m. vijana.
- Hutumia lugha ya kimafumbo k.m. machozi ya simba – pombe.
- Huwa na maana tofauti kutegemea wahusika na eneo / Hupata maana kutoka kwa watumiaji / muktadha. Hutumiwa na wanajamii katika mawasiliano yao katika kipindi fulani cha wakati / mahali maalum.
- Misimu si semi sanifu. (zozote 7x1 = alama 7)

(d)

- Kupitia utohozi / kugeuza mpangilio.
- Kwa kufupisha maneno.
- Kutumia ufananisho / sitiari – nyani, kasuku, nyoka.
- Kubadilisha maana ya kawaida ya maneno – toboa.
- Uvumbuzi wa maneno mapya – zii.
- Kuchanganya lugha – kurelax.

TATHMINI YA PAMOJA – SHULE ZA UPILI ZA JIMBO LA MACHAKOS.
Hati ya kuhitimu kisomo cha Sekondari Kenya (K.C.S.E)
102/1
KISWAHILI
KARATASI YA 1

1. **INSHA YA LAZIMA**
   Wewe ni katibu wa jopo lililoteuliwa kuchunguza changamoto zinazokabili uchapishaji wa vitabu vya Kiswahili nchini.Andika ripoti hiyo.
2. Samaki mkunje angali mbichi.
3. Serikali za ugatuzi zitakuwa na manufaa kwa maendeleo ya nchi.Jadili.
4. Andika insha itakayomalizika kwa maneno haya.....
   Niliyakumbuka maneno ya mwalimu mkuu,machozi yalitoka njia mbilimbili.Hayawi hayawi huwa.

TATHMINI YA PAMOJA – SHULE ZA UPILI ZA JIMBO LA MACHAKOS.
Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari Kenya (K.C.S.E)
102/2
KISWAHILI
KARATASI YA PILI
(LUGHA)

1. **UFAHAMU (ALAMA 15)**
   Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanoyofuatia.
   Malengo ya maendeleo ya Milenia
   Malengo ya maendeleo ya Milenia (yajulikanayo kwa kimombo kama Millenium Development Goals (MDG), Ni malengo manane ya nchi wanachama wa umoja wa mataifa, ambayo nchi hizi zilikubaliana kujitahidi kutimiza kufikia mwaka wa 2015.Azma ya kufikia malengo haya ilizinduliwa rasmi mnamo septemba 2000 katika azimio la millennia la umoja wa mataifa.Wakati wa uzinduzi, mataifa yote 189 wanachama wa umoja wa mataifa yalihusika.Kwa sasa, mataifa wanachama yameongezeka na kufikia 193 na yote yanajizatiti kutekeleza azma hii.

   Azma ya kwanza ni kukomeza au kupunguza umaskini uliokithiri kwa asili 50 miongoni mwa watu ambao kipato chao ni chini ya dola moja kwa siku.Aidha lazima hii inalenga kupunguza kwa kiasi hicho idadi ya watu wanaokumbwa na dhiki ya njaa kufikia mwaka wa 2015.Kwa kielelezo, kwa mfano vijiji viitwavyo ‘vijiji vya milenia’vilianzishwa katika nchi sahara,ambazo ni Uhabeshi, Ghana, Kenya, Malawi, Rwanda, Nigeria, Senegal, Tanzania na Uganda vilichaguliwa.Wakazi hawa wanapookolewa kutoka kwa ulitima, hatua zilichukuliwa vijijini humu yanaonyesha athari chanya.Kunayo matumaini.

   Lengo la pili lilikuwa kutimiza elimu ya msingi kwa wote chini ya wito ‘Elimu kwa wote’, yaani kwa kingereza Eduction for All (EFA) kufika mwaka wa 2015.Nchini Kenya, elimu ya msingi ilifafanuliwa upya katika katiba mpya ya 2010, ikawa yaanzia shule ya chekechea hadi kidato cha nne. Aidha imetajwa kuwa ya lazima, kwamba mtoto sharti ahudhurie masomo.Ina maana kuwa mzazi analazimika kumpeleka mtoto shuleni. Lengo pia lipo, kuhakikisha watoto wote wa jinsia za kike na kiume wanahitimu.

   Lengo jingine ni kuwania usawa wa kijinsia kwa kuhakikisha kuna nafasi sawa kwa wote.Katika janibu nyingi za wanachama wa umoja wa mataifa, wanawake kwa miaka ya ayami walionekana kuwa chini ya wanaume kutokana na taasubi ya kiume, mwanamke alifaa kuwa chini ya mwanamume.Hatua ya kwanza ya malengo ya maendeleo ya millennia inanuia kuondoa tofauti ya uwiano wa wasichana na wavulana katika elimu ya msingi hadi sekondari ifikapo mwaka 2005; na katika ngazi zote za elimu ifikapo 2015. Kuondoa utoro miongoni mwa wahudhuriao masomoni hutahakikisha usawa huu.

   Lengo la nne ni kupuuza vifo vya Watoto wa umri chini ya miaka mitano kwa theluthi mbili kufikia mwaka wa 2015. Jitihada zinatiwa kuhakikisha kuwa kina mama waja wazito hawazai njiti wala watoto wao hawaagi punde baada ya kuzaliwa.Changamoto imekuwa kwamba watoto wengi katika nchi zinazoendelea hufa kabla kufikia umri wa miaka mitano. Mapambano dhidi ya magonjwa kama vile kifaduro, polia na malaria yaliyosababisha vifo hivi pamoja na jitihada za kujizatiti za kufikia lengo hili.

   Kunayo azma ya kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za uzi ili kupunguza kwa robo tatu vifo

vya uzazi kufikia 2015. Kua kwa wajawazito kunaashiria huduma duni wakati wa kuhimili.Kina mama wengine katika nchi zinazoendelea hawahudhurii kliniki wakati wakati wa kulea mimba.Kwingineko, huduma hizi huwa mbali sana, huku namna za usafiri zikiwa duni.Kina mama huishia ama kuhudumiwa na 'wakunga' wasiohitimu au hata kujifungua pweke .Mataifa wanachama wanahimiza kuongezea zahanati na vituo vingine muhimu vya afya.Kadhalika jitihada zinatiwa kuwaelimisha kina mama na jamii kwa jumla kuhusu umuhimu wa kuhudhuria kliniki wakatiwa ujauzito na kuhakikisha mama yu salama wakati wa kujifungua.

Magonjwa sugu yanayotishia kuwamaliza walimwengu ni kikwazo cha jitihada za walimwengu kujiendeleza.Ndiyo maana lengo la sita ni kupambana na Ukimwi, malaria na magonjwa mengineyo.Kampeni zinaimarishwa katika jumuiya hii kuzuia kabisa na kupunguza maambukizo mapya ya Ukimwi.Jitihada zinatiwa kupunguza au kuzuia kabisa ugonjwa wa malaria au magonjwa mengine hatari. Vyombo vya habari, vituo tamba vilivyo na maafisa wa nyanjani vinatumiwa nyanjani katika mataifa wanachama ili kufaulisha kampeni hii.

Aidha wanachama wanalenga kuhifadhi mazingira kwa kujumuisha misingi ya maendeleo endelevu katika sera na program za nchi.Zinalenga kuzuia upotevu wa rasilimali ya mazingira kama vile miti na maji.Lengo lipokuhakikisha kuwa katika kipindi hiki wanachama watapunguza kwa asilimia 50 idadio ya watu wanaoshindwa kupata maji safi na salama – hii ni moja wapo ya malengo ambayo, kwa mujibu ya tovuti ya umoja wa mataifa www.un.org/milleniumgoals, kuna matumaini ya kutimiza zaidi ya 2015.

Mwisho kuna lengo la kujenga mshikamano wa maendeleo duniani, kwanza kwa kuboresha zaidi mfano wa Fedha na biashara duniani kuhakikisha ni wa usawa, unafuata sheria na kamwe hauna ubaguzi.Utawala bora; kushughulikia mahitaji ya kipekee ya nchi changa kama vile kuziondolea ushuru wa bidhaa muhimu,kuzipunguzia au kuziondolea madeni; kutoa misaada zaidi kwa nchi maskini zinazotia jitihada kutoa umaskini kushughulikia mahitaji muhimu, ya visiwa vidogo na nchi zisizo na bandari miongoni mwa nchi zinazoendelea; kuwapa vijana ajira bora; kushirikiana na sekta za kibinafsi ili kuimarisha teknolojia ya kisasa hasa katika habari na mawasiliano ni baadhi ya yanayozingatiwa kulenga kutimiza mshikamano huu.

MASWALI.

1. Malengo ya maendeleo ya milenia ni nini?
   (Alama 2).
2. Ni wachochole wa kiwango gani wanaolengwa kuinuliwa na hatua za malengo ya maendeleo ya milenia?
   (Alama 1)
3. Taja vipengele viwili muhimu kuhusu elimu katika katiba mpya ya Kenya vinavyo changia kufikia malengo ya maendeleo ya milenia?
   (Alama 2)
4. Gusia changamoto tano zinazowakabili kina mama wajawazito katika ulimwengu wa tatu.
   (Alama5)
5. Kampeni dhidi ya magonjwa sugu inafanywa kwa namna gani. (Alama 2)
6. Hali ya maji inatarajiwa kuwaje kufikia 2015. (Alama 1)
7. Eleza maana ya vifungu hivi. (Alama 3)
   a) Hawazai njiti
   b) Vifo vya uzazi.

UFUPISHO: (Alama 15)

Soma kifungu kisha uyajibu maswali yanayofuata.

Nidhamu ni kitu cha maana sana maishani mwa binadamu. Kila mwanafunzi anapaswa kuwa na nidhamu ya hali ya juu sana.Akiwa na nidhamu hiyo, atakuwa mtu mwadilifu, anayeweza **kustahiwa** na kusadikika katika mambo, shughuli na hali tofauti.

Kwanza, mtoto mwenye nidhamu huwa kama anga au nuru nyumbani mwao, shuleni na pia katika jamii.Watu wote wanampenda na kumheshimu. Wazee kwa **vijulanga** wote wanamtegemea kama msimamizi wa mambo **nyeti** ya maisha yao. Kwa hivyo, ni **dhahiri shahiri** kwamba mwadilifu hunufaika sana, kinyume na mkaidi ambaye wahenga walimwambia kwamba atakosa kufaidi hadi siku ya Idi.

Pili, huwadia nyakati ambapo huwa kuna jambo la busara, **mathalan**i jukumu ama dhima fulani ambayo huhitaji tu mwakilishi mmoja darasani, shuleni au katika jamii. Watu hapana shaka watamteua yule

mwadilifu kuchukua nafasi kama hiyo. Ndio maana viranja wanaoteuliwa shuleni, huwa ni wanagenzi ambao tayari wamekwisha tiliwa katika mizani na kupigwa msasa madhubuti.

Vile vile, mwadalifu daima atajiepusha na shutuma na majanja yote yanayoweza kuchipuka. Kuna msemo maarufu, kwa busara yake iliyobusarisha mwadilifu kwamba “aliye kando haangukiwi na mti.”Pia waliambiwa kwamba, “ pilipili usiyoila yakuwashiani?”

Ni bayana kutokana na misemo hiyo miwili kwamba mwenye nidhamu hawezi kuhusishwa na majanga hatari yanayoweza kuyakumba watu.

Walakini ni vyema kujiuliza, je, nidhamu huanzia wapi, na kwa nini kuna baadhi ya ‘watoro’ ambao ni utovu wa nidhamu? Utovu wa nidhamu huanzia awali sana maishani mwa mja. Mtoto anapozaliwa, anategemea miongozo na mielekeo ya watu wazima ambao wakomazingirani mwake.Ndipo wakale wale waliokaramka walisema kwamba mtoto akibebwa, hutazama kisogo cha nina.
Hivi ni kusema kwamba, nidhamu au utovu wa nidhamu huanzia nyumbani hadi shuleni, kisha hupanuka hadi kufikia kiwango ambapo mja anatangamana na watu wote katika maisha yake.Ikiwa sehemu moja ya ukuaji wa nidhamu maishani mwa mja itasambaratika, basi hawezi akawa mkamilifu kinidhamu maishani mwake.
Kwa vile ni bayana kwamba mabaya yote ayatendayo duniani hulipwa na Mola papa hapa duniani,watovu wa nidhamu wote huishia kuangamia, ama kujuta mno kwa amali zao potovu.Ni kheri mja kujihidi mwenyewe, kwani uhalifu haulipi chochote.

a) Nini umuhimu wa nidhamu? (maneno kati ya 50-55) (al. 1 ya mtiririko)
(alama 7)
Matayarisho
Jibu

(b) Bila kubadilisha maana, fupisha aya nne za mwisho. (tumia maneno 55-60)
(alama 1 mtiririko)
(alama 8)
Matayarisho
Jibu

MATUMIZI YA LUGHA.

a) Taja sifa tatu kuu za sauti /k/
(alama 3)
b) Andika sentensi hii katika msemo halisi
Mwalimu alimuambia mwanafunzi amalize kazi hiyo haraka
(alama 2)
c) Huku ukitoa mifano, eleza maana ya silabi funge
(alama 2)
d) Weka nomino hizi katika ngeli zake (alama 2)
Mbalungi
Mturuki
e) Andika sentensi ifuatayo kwa wingi, wakati uliopita hali ya kuendelea
(alama 2)
Mwalimu humuadhibu mwanafunzi mwenye hatia.
f) Changamua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha jedwali
(alama 4)
Omondi anaazimia kuwa mhasibu Lakini hatii bidii masomoni
g) Yakinisha katika nafsi ya tatu wingi (alama 2)
Sijasafiri kwenda marekani
h) Bainisha matumizi ya kiambishi ‘ku’ katika sentensi hii (alama 20)
Naomi atakupikia chai alafu aende kule uwanjani
i) Onyesha virai katika sentensi zifuatazo na ueleze ni vya aina gani.
(alama 2)
   i) Anachukia kusoma riwaya yenye masuala ya kisiasa.
   ii) Watoto wa kike hudunishwa katika jamii nyingi
j) Onyesha matumizi mawili ya alama zifuatazo za uakifishaji
(alama 4)
Koloni (:)

Kistari kifupi (-).

k) Bainisha aina za vitenzi katika sentensi ifuatayo.
Walimu ni watu wasiopendwa wanaposema ukweli kuhusu wanafunzi
(alama 3)

l) Eleza sifa mbili za vishazi tegemezi (alama 2)

m) Onyesha matumizi ya kiimbo katika sentensi hii
Ondoka hapa! (alama1)

n) Andika neno lenye maana sawa na (alama 2)
Hawala
Katani

o) Eleza maana ya sentensi hii (alama 2)
Ningalikuwa na pesa ningalinunua gari na ningalistarehe.

p) Eleza tofauti iliyopo kati ya sentensi hizi (alama 2)
Tulipofika hoteleni tulipewa soda na chupa.
Tulipofika hotelini tulipewa soda kwa chupa

q) Kanusha katika ukubwa (alama 1)
Mwizi huyu aliiba kisu na ng'ombe wa mwanamke yule.

ISIMU JAMII

a) Eleza sababu zozote sita zinazochangia kufa kwa lugha.
(alama 6)

b) Taja mambo yoyote manne yanayofanywa na serikali yetu kuimarisha lugha ya Kiswahili
(alama4)

TATHMINI YA PAMOJA – SHULE ZA UPILI ZA JIMBO LA MACHAKOS.
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya.(K.C.S.E)
102/3
Kiswahili
Karatssi ya 3

1. **SEHEMU YA A: SHAIRI (Lazima) (alama 20)**

Nimechoka
Nilivyofikisha hapa, na juu kupandishwa
Na kwa hila gani, au, zilipofungwa
Ncha za waya hii ngumu ya maisha, sijui.

Wanadamu wameinama.Wanasali kwa haraka sasa.
Utafikiri wanahesabu mchanga utakaojaza kaburi langu.
Vichwa vyeupe vinacheka.Kingine kinasema tena:
"Mnaliona Hilo! Joga !" Vichwa vinachela.Wanasali.
"Nyinyi nyote hamna akili!Mnaniudhi!
Hamwoni hali yangu!" Napiga kelele.Lakini vichwa
Havitishi,na wanadamu hawatingishiki.

Sauti ya baba inasema kwa msisitizo
"Najua utafika wakati itakulazimu kudondoka.
"Lakini unazo nguvu bado,na usikate tamaa,
Ila usitegemee kusifiwa au kusaidiwa;
Vichwa vyote hivi vilidondoka kutoka umbali huo,
Nawe kudondoka,utadondoka!

Ninaendelea kuning'inia.Nimechoka.Mikono
Inaniuma;hatari ya vitimbo.Vinacheka.Wanasali
Sasa wanaimba.Sitaki nyimbo zao;maana
Mimi bado nimeniong'inia na vitimbo having'oki.
Lakini pole pole ninaanza kutabasamu.
Sijafikia hatua ya kucheka;maana nimechoka,
Kichomi kimenipata na sijadondoka

Lakini najiona nimening'inia kama ndege
Aliyenaswa na mtego wa mtoto mdogo

Mimi,Lakini ni mwanadamu na akili zangu
Timamu.Ninaweza kudondoka, kama nikipenda.

Lakini ninaogopa chini yangu naona miti
Iliyochongwa ikifuata usawa wa waya hii,
Ikingoja kwa hamu,kama mshikaki kunichoma,
Kunitoboa na kufurahia kimya kimya,
Uzuri wa kupita katika mwili mwororo wa binadamu.
Lazima nishike kwa nguvu nisianguke kama kifurushi
Cha pamba cha mtoto mdogo kilichokwisha pimwa.

Mikono inaniuma, na waya imekwishanikata vidole.
Damu imetiririka hadi kwapani;kujipangusa siwezi.
Nimechoka.Kadiri niendeleavyo kunig'inia, ndivyo
Sura yangu ionyeshavyo vizuri alama za uchovu.
Ninatazama huku na huko kuwatafuta wenye huruma.
Lakini wanadamu wote wazima wanainamisha vichwa
Chini kama kwamba hawanijui;hata jamaa zangu!

Ninaendelea kuning'inia kama picha iliyotundikwa
Katika shamba la mawele, na mwenye shamba
Huvuta waya kutoka nyumbani,itingishike kuwatisha
ndege.
Machozi yananitoka,kuyapangua siwezi.
Ninajitahidi kutoa sauti kwa nguvu;
"Jamani e! Nisaidie! Ng'oeni hivyo vitimbo!"
Lakini wanadamu wameinama.Wanaanza sasa kusali.

Kati ya vitimbo, vichwa vinazuka ardhini
Ukweli wa maisha unakuwa kama ndoto ya uwongo.
Kichwa kimoja kinasema kwa sauti "Mnaliona Hilo!"
Halafu vichjwa vyote vyeupe vinacheka.Ninashangaa.
Ninashangaa zaidi kusikia sauti ya baba
Ikicheka miongoni mwa vichwa hivyo vyeupe.
Siyaamini macho,siyaamini masikio, sikiamini kichwa.

Maswali:

1. Shairi hili ni la "udhanaishi" Fafanua kauli hii. (alama 4)
2. Eleza kwa kutoa mifano miwili, jinsi msanii alivyotumia tamathali zifuatazo (alama 6)
   (a) Jazanda
   (b) Uhuishi
3. Andika ubeti wa saba kwa lugha tutumbi. (alama 4)
4. Eleza maana ya mishororo "vichwa vyote hivi vilidondoka kutoka umbali huo, nawe kudondoka utadondoka".

   (alama 2)
5. Eleza umbo la shairi hili. (alama 4)

SEHEMU B: RIWAYA

<u>Kidagaa Kimemwozea</u>

2. "....usiniweke pembeni kama tanbihi, mimi na wanawake wenzangu kama wanaume wengine wafanyavyo waandikapo..."
   a) Fafanua muktadha wa dondoo hili
   (alama 4)
   b) Fafanua mbinu mbili za uandishi zilizotumika hapa
   (alama 2)
   c) Hakiki usawiri wa wahusika wa kike katika riwaya hii (alama 14)
3. Wananchi wa Tomoko wamesalia katika ndoto ya uhuru.Dhibitisha ukweli wa kauli hii.
   (alama 20)

TAMTHILIA

<u>Mstahiki Maya</u>

4. "Si ninyi nd'o mjuao wanangu!..nilikiona afadhali".
   (a) Eleza muktadha wa maneno haya
   (alama 4)

(b) Taja na utolee mifano ya mbinu zozote mbili za uandishi zilizotumika katika kifungu hiki. (alama 4)

(c) Fafanua maudhui yanayorejelewa na dondoo hili. (alama 12)

5. "Mtu huvuna alichopanda.Ukipanda pojo huwezi kuvuna kunazi.
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili.
   (Alama 4)
   b) "Ukipanda pojo huwezi kuvuna kunazi" ina maana gani kulingana na muktadha huu.
   (Alama 6)
   c) Taja na ueleze matendo mengine manne ya kuonyesha kuwa walipanda pojo na kuvuna pojo si kunazi.
   (Alama 8)
   d) Taja tamathali za usemi zilizotumiwa katika dondoo hili. (Alama 2)

SEHEMU YA D: HADITHI FUPI

Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine

Ken Walibora na Said A.Mohaned

Jibu swali la 5 au na 6

7). "Kama alivyoshinda nani Yule....nunez?"
   a) Liweke dondoo hili katika muktadha wake.
   (Alama 4)
   b) Linganua sifa nne za msemaji na msemewa katika dondoo hili.
   (Alama 8)
   c) Kwa kurejelea hadithi nzima eleza hisia za utamaduni ulipitwa na wakati. (Alama 6)
   d) Ni mbinu zipi za lugha zilizotumika katika dondoo hili? (Alama 2)

8). Mwanamke katika diwani ya Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine amepewa nafasi finyu. Fafanua kwa kuzingatia hadithi zozote nne. (Alama 20)

SEHEMU YA E.FASIHI SIMULIZI (Alama 20)

9. a) Eleza maana ya maghani
   (alama 2)
   b) Fafanua sifa nne za maghani (alama 4)
   c) Taja njia zozote nne za kuhifadhi kazi za fasihi simulizi katika jamii.
   (alama 4)
   d) Fafanua hatua za ukusanyaji wa data katika fasihi simulizi
   (alama 5)
   e) Eleza matatizo yanaokabili fasihi simulizi katika jamii ya sasa (alama 5)

TATHMINI YA PAMOJA – SHULE ZA UPILI ZA JIMBO LA MACHAKOS.
Hati ya kuhitimu kisomo cha Sekondari Kenya (K.C.S.E)
102/1
KISWAHILI
KARATASI YA 1
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

SWALI LA LAZIMA
Ripoti iwe na yafuatayo:

a) Kichwa : Kilenge mada kwa kuonyesha ni ripoti ya uchunguzi wa jopo hii.
b) Utangulizi : Utangulizi huonyeshaaliyeitaka ripoti hii.
- Wanajopo.
- Sababu za kutaka ripoti hii itolewe.
- Malengo ya ripoti.
- Utaratibu wa kupata habari kama kuhoji wazazi, wanafunzi washirika wengine.

c) Mwili – Ubebe matokeo ya uchunguzi
- Yaandikwe kwa vichwa vidogo vidogo.
  Mapendekezo – kamati itoe mapendekezo kulingana na uchunguzi waliofanya.
  Hitimisho – Wito wakatibu , sahihi na jina la katibu.

HOJA
- Ukosefu wa soko
- Uandishi wa vitabu vya Kiswahili mara nyingi huamuliwa na mahitaji ya shule
- Kuna wandishi wengi wa vitabu vya kiingereza nchini Kenya kuliko wale wa Kiswahili
- Inadaiwa kuwa wanaoteua vitabu hivyo huchagua majina ya waandishi na wala sio yaliyomo kwenye vitabu.
- Mwandishi wa vitabu vya Kiswahili pia anaweza kuwa na matatizo ya kimaudhui na kifani katika uandishi wake.
- Mfumo wa elimu nchini Kenya hasa katika shule za msingi na za upili haujatilia mkazo somo la utunzi wa kisanaa kwa muda mrefu.
- Nchini Kenya hakujawa na chuo cha uandishi ambachpo kingekua na jukumu la kutoa mafunzo kwa waandishi.
- Ukosefu wa marejeleo muhimu ni tatizo kubwa kwa waandishi wa Kiswahili.
- Ukosefu wa vifaa vya uandishi kama vile kompyuta shughuliya uandishi huhitaji muda mrefu ambao mara nyingi waandishi hawapati kwani wengi wao ni walimu shuleni au wahadhiri vyuoni.Gharama kubwa kutoka kupokelewa kwa mswada hadi kitabu kinapomfikia msomaji.
- Matatizo ya uuzaji na usambazaji wa vitabu hadi kwa wasomaji.Baadhi ya mashirika ya uchapishaji hayako tayari kuchapisha vitabu vya waandishi chipukizi.

TANBIHI.
- Lazima arejelee uchapishaji wa vitabu vya Kiswahili wala si vitabu kwa jumla.
- Afafanue angalau hoja tatu zinazoonyesha changamoto zinazokabili uchapishaji wa vitabu.
- Ni muhimu mtahiniwa atoe mapendekezo jinsi ya kukabiliana na changamoto hizi kwani ripoti haikamiliki pasi nayo.

BAADHI YA MAPENDEKEZO.
- Wananchi wahamasishwe kuhusu umuhimu wa kusoma na kununua vitabu vya Kiswahili.
- Wananchi waelezwe umuhimu wa lugha ya Kiswahili.
- Waandishi chipukizi watiwe motisha kwa vitabu vyao kuandikwa.
- Kutilia mkazo kwa masomo yanayohusiana na sanaa ya uandishi.
- Kuendelezwa kwa vyuo vinavyofundishwa taaluma ya sanaa na uandishi nchini.
- Taasisi za elimu ziwezwe kuteua vitabu vya wandishi chipukizi kutumiwa kwa masomo.
- Mtahiniwa awe na angalau mapendekezo matatu yaliyoelezwa.

SWALI LA PILI.
- Mwanafunzi atunge kisa kinachooana na methali ina maana sawa na: usipoziba ufa utajenga ukuta.
- Maana ni vizuri kulainisha mambo kabla hayajaaribila
- Kisa kilenge mhusika aliye kosa kurekebisha tabia zake mapema na baadaye anaharibika.
- Mtahiniwa aonyeshe pande zote mbili
- Akionyesha upande mmoja hajajibu.

SWALI LA TATU.

MANUFAA

- Ugatuzi sawa wa rasilimali za nchi.
- Huduma zitakuwa karibu na wananchi.
- Uokoaji wa wakati wanaposhughulika swala flani.
- Wananchi watahusika vilivyo katika mpango wa Majimbo yao.
- Kubuniwa kwa nafasi za kazi
- Ushindani chenya baina ya majimbo.

HASARA

- Ukabila
- Huenda sehemu moja ya jimbo ikabaguliwa

SWALI LA NNE

- Mtahiniwa aandike kisa kitakachoonyesha majuto baada ya kujipata taabani.Hii iwe baada ya maelekezo kutoka kwa mwalimu mkuu yaliyoambulia patupu.

Au

- Mwanafunzi aandike kisa kitakachoonyesha furaha baada ya kufuata ushairi wa mwalimu mkuu ushinde wake usababishe furaha isiyo na kifani inayoambatana na kilio (machozi ya furahi)

INSHA

MWONGOZO

Utangulizi

Karatasi hii imedhamiria kutathmini uwezo wa mtahini wa kuwasiliana na msomoji na kuwasilisha ujumbe kimaandishi, akizingatia mada aliyopewa.Mawasiliano haya yatategemea ukwasi wa lugha ya mtahiniwa .Kwa kutegemea maagizo ya swali lenyewe na umahiri wa lugha, ni lazima kutulia mkazo mtindo, mada na uwezo na mtahiniwa kufuata maagizo vilivyo.Mtahini lazima aisome insha yote huku akizingatia sarufi, hijai, hoja, msamiati na mtindo ili aweze kuikadiria kwa kurejelea viwango mbalimbali vilivopendekezwa.

VIWANGO MBALIMBALI

D – (D YA CHINI) MAKI 01 - 02

1. Insha haina mpangilio maalum na haieleweki kwa vyovyote vile.
2. Kujitungia swali tofauti na kulijibu.
3. Kuandika kwa lugha isiyo Kiswahili au kuchanganya Ndimi.
4. Kunakili swali au maswahili na kuyakariri.
5. Kunakili swali au kichwa tu.

D – WASTANI MAKI 04 – 05

1. Mtiririko wa mawazo haupo.
2. Mtahiniwa amepooka kimaudhui.
3. Matumizi ya lugha ni hafifu mno.
4. Kuna makosa mengi ya kila aina.

D+ (D YA JUU) MAKI 04 - 05

1. Insha huwa na makosa mengi ya kila aina, Lakini unaweza kutambua kile ambacho mtahiniwa anajaribu kuwasilisha.
2. Hoja hazikuelezwa kikamilifu / mada haikukazwa vilivyo.
3. Mtahiniwa hana uhakika wa matumizi ya lugha.
4. Mtahiniwa hujirudiarudia.
5. Insha itakayozingatia sura lakini ikose maudhui ikadiriwe hapa.
6. Insha ya urefu wa robo yaani, isiyozidi maneno 174 isipite kiwango hiki.

C- (C YA CHINI) MAKI 06- 07

1. Mtahiniwa ana shida ya kuwasilisha na kutiririsha mawazo yake.
2. Mtahiniwa hana msamiati wa kutosha wala miundo ya sentensi ifaayo.
3. Mtahiniwa anafanya makosa mengi ya sarufi , ya hijai na ya msamiati na insha haieleweki kwa urahisi.

C WASTANI MAKI 08

1. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe lakini kwa njia hafifu.
2. Dhana tofauti hazijitokezi wazi.
3. Mtahiniwa hana ubunifu wa kutosha.
4. Mtiririko wa mawazo ni hafifu na hana ufundi wa lugha unaofaa.

5. Amejaribu kuishughulikia mada aliyopewa.
6. Ana shida ya uakifishaji.
7. Anafanya makosa mengi ya sarufi, ya hijai na ua msamiati lakini bado insha inaeleweka.

C+ (C YA JU) MAKI 09- 10

1. Anawasilisha ujumbe vizuri akizingatia mada lakini bado insha inaeleweka.
2. Dhana tofauti zimejitokeza japo kwa njia hafifu.
3. Kuna mtiririko wa mawazo japo hana ufundi wa lugha unaofaa.
4. Misemo na methali zimetumika kwa njia hafifu.
5. Anashida ya uakifishaji.
6. Kuna makosa ya sarufi ya msamiati na hijai yanayoathiri mtiririko wa mawazo.
7. Insha ya kiwango cha nusu, yaani maneno 175- 274 isizidi kiwango hiki.

B – (B YA CHINI) MAKI 11- 12

1. Anawasilisha ujumbe vizuri kwa kueleza hoja tofauti akizingatia mada.
2. Ana mtiririko mzuri wa mawazo.
3. Anatumia mifano michache ya msamiati unaovutia
4. Makosa yanadhihirika / ni kiasi

B (B YA CHINI) MAKI 13

1. Anathihirisha hali ya kuimudu lugha.
2. Mawazo yake yanathihirika akizigatia mada.
3. Anateua na kutumia mifano michache ya misamiati mwafaka.
4. Sanja yake ni mzuri.
5. Makosa ni machache.

B+ (B YA JUU) MAKI 14 - 15

1. Mawazo yake yanadhihirika na anajieleza waziwazi.
2. Anawasilisha ujumbe kwa njia inayovutia na kwa urahisi akizingatia mada.
3. Ana mchanganyiko mzuri wa msamiati unaovutia.
4. Sarufi yake ni nzuri.
5. Uakifishaji wake wa sentensi ni mzuri.
6. Makosa ni machache ya hapa na pale.
7. Insha ya urefiu wa robo tatu, yaani maneno 274 – 374, isipite kiwango hiki.

A- (A YA CHINI) MAKI 16- 17

1. Anadhihirisha ukomavu wa lugha.
2. Mawazo yake yanadhihirika na anaishughulikia mada.
3. Ana mtiririiko mzuri wa mawazo.
4. Msamiati wake ni mzuri na unavutia.
5. Sarufi yake ni nzuri.
7. Makosa ni machache yasikusudiwa.

A WASTANI MAKI – 18

1. Anawasilisha ujumbe vizuri kulingana na mada.
2. Anajieleza kikamilifu akitumia lugha ya mnato.
3. Anatoa hoja zilizokomaa.
4. Anatumia msamiati wa hali ya juu na unaovutia zaidi.
5. Anatumia miundo tofauti tofauti ya sentensi kiufundi.
6. Makosa ni nadra kupatikana.

A+ (A YA JUU) 19 – 20

1. Mawazo yanadhihirika zaidi na mada imeshughuliwa vilivyo.
2. Anajieleza kikamilifu akitumia lugha ya mnato.
3. Hoja zake zimekomaa na zinashawishi.
4. Msamiati wake ni wa hali ya juu na unavutia zaidi.
5. Sarufi yake ni nzuri zaidi.
6. Anatumia miundo tofauti tofauti ya sentensi, kiufundi.
7. Makosa yote kwa jumla hayazidi matano.

ALAMA ZA KUSAHIHISHA

= = = Hupigwa chini ya sehemu ambapo kosa la sarufi limetokea kwa mara ya kwanza tu.

_ Hupigwa chini ya sehemu au neno ambapo kosa la hijai limetokeza kwa mara ya kwanza tu.

✓ Hutumiwa kuonyesha hoja inapokamilika pambazoni kushoto.

/\ Hutumiwa kuonyesha kuacha kwa neno / maneno.

√ Hutumiwa kuonyesha msamiati bora. Alama hii hutiwa juu ya neno lenyewe.

X Hutumiwa kuonyesha msamiati usiofaa. Alama hutiwa juu ya neno lenyewe.

Kila ukurasa uwe na alama ya chini katikati ili kuthibitisha kuwa mtahini ameupitia ukurasa huo.
Baada ya kutoa tuzo, lazima mtahini aandike udhaifu wa mtahiniwa.
Mfano wa kutuza:
Robo Tatu
C 08/20
Udhaifu
Urefu
Maudhui
Hijai
Sarufi

TATHMINI YA PAMOJA – SHULE ZA UPILI ZA JIMBO LA MACHAKOS.
Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari Kenya (K.C.S.E)
102/2
KISWAHILI
KARATASI YA PILI
(LUGHA)
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

1. Majibu ya Ufahamu.
1. Malengo manane ya nchi wanachama wa umoja wa mataifa,ambayo nchi hizi zilikubaliana kujizatiti kufikia mwaka wa 2015. (Alama 2)
2. Maskini ambao kipato chao ni cha chini ya dola moja kwa siku. (Alama 1)
3. i) Inaanzia shule ya chekechea hadi kidato cha nne. (Alama 2)
   ii) Ni ya lazima, yaani mtoto sharti ahudhurie masomo. (Alama 1)
4. i) Kutohudhuria kliniki wakati wa kulea mimba.
   ii) Huduma kwa wajawazito kuwa mbali sana.
   iii) Namna za usafiri kuwa duni.
   iv) Kuhudumiwa na 'wakunga' wasiohitimu au hata kujifungua pweke.
   v) Ukosefu wa kinga muhimu na lishe bora. (zozote 3 alama 5)
5. Kwa kutumia vyombo vya habari na vituo tamba vilivyo na maafisa wa nyanjani. (Alama 2)
6. Kupunguza kwa asilimia 50 idadi ya watu wanaoshindwa kupata maji safi na salama . (Alama 2)
7. i) 'Hawazai njiti' – Mimba hazitoki . (Alama 1)
   ii) 'Vifo vya uzazi'- vifo vinavyotokea wakati kina mama wanajifungua. (Alama 1)

2. **NIDHAMU**
(a) Nidhamu (alama 1)
(b) Umuhimu wa nidhamu:

- Mwenye nidhamu ni nuru nyumbani hata shuleni.
- Anakuwa kiongozi wa wote / watu humtegemea
- Kiatu humpenda.
- Anajiepusha na shutalma na majanga.
- Kijumla anastahiwa.
- Hupata fursa ya kuteuliwa miongoni mwa wengi kwa dhima fulani.

(Hoja 6X 1 = alama 6, mtiririko al. 1, jumla alama 7)

(c) Muhtasari wa aya nne za mwisho.
i) Mwadilifu hajipati katika matatizo mengi.
ii) Lakini utovu wa nidhamu huanzia ututoni na mtoto huiga tabia za wazazi wake na huendelea shuleni.
iii) Utovu wa nidhamu hulipwa kwa adhabu mumu humu / watu wajirekebishe.

Makosa
Sarufi ½ x 10 = alama5
Hijai ½ x 6 = alama 3

Adhibu kila kosa la sarufi na hijai linapotokea

3. MAJIBU

a) Kipasuo, hafifu, hutamkwa katika kaakaa laini

b) "Maliza kazi hii haraka," mwalimu alimwambia mwanafunzi.

c) Silabi funge huishia kwa konsonanti mfano
Ma-k-ta-ba

d) U-i
A – wa

e) Walimu walikuwa wakiwaadhibu wanafunzi wenye hatia

f)

S								
S1					S2			
KN	KT			U	KN	KT		
N	T	T	KN N		Ø	T	E	E
Omondi	anaazimia	kuwa	mhasibu	lakini		Hatii bidii masomoni		

g) Wanasafiri kwenda Marekani

h) Naomi atakupikia chai halafu aende kule uwanjani
mahali nafsi ya pili umoja

i) Riwaya yenye masuala ya kisiasa ni – kirai nomino
Watoto wa kike – kirai husishi

j) Koloni – hutenganisha jina la mhusika na maneno anayoyasema katika tamthilia
mfano
Mbua: Je alifika jana?
Hutanguliza orodha.mfano
Mama alinunua mboga : Nyama, nyanya na kitunguu.
Kistari kifupi (-)
Hutenganisha silabi za maneno
Kuonyesha neno linaendelea katika mstiari unaofuata baada ya kukosa kutoshea katika mstari
mfano
Ame-wasili

k) ni- kitenzi kishirikishi kipungufu
Wasiopendwa, wanaposema – vitenzi sabamba

l) Havikubaliki kama sentensi kamili
Hata kikiondolewa maana ya sentensi haipotei.
Hutambulishwa na vitambulishi vya utegemezi kama vile 'o' rejeshi

m) Amri

n) Hawala-Hundi / cheki
Katani – mkonge

o) Kitendo hakijatendeka na hakuna uwezekanao.

p) i) Walipewa soda na vile vile chupa
ii) Walipewa soda iliyokuwa kwenye chupa
iii) Walipewa soda iliyokuwa kwenye chupa

q) Jizi hili halikuiba jisu na gombe la jana jike lile

4. ISIMU JAMII.

a) Kiuchumi – maendeleo na ubunifu wa viwanda yanafanya watu kuhamia mijini .Watu wanapohamia mijini wanaacha kuzungumza lugha moja na kuanza kuzungumza nyingine kwa ajili ya mawasiliano

b) Uchache wa wazungumzaji – idadi ya watu wanaozungumza lugha fulani inapopungua lugha hiyo

inakabiliwa na tisho la kufifia
c) Kutoungwa mkono na taasisi balimbali k.v elimu dini na vyombo vya habari hukabiliwa na tisho la kufa
d) Hadhi – lugha ambazo hazina hadhi kuishia kufa
e) Ndoa za mseto – watu wanapo changanyikana kupita ndoa za mseto husababisha lugha zingine kudidima
f) Kuhama kwa watu – kuhama kutoka sehemu moja hadi nyingine luga zao huadhiriwa
g) Sababu za kisiasa
h) Athari za elimu zozote 6x1

(b)
- Kiswahili kufanywa lugha ya Taifa / rasmi
- Katiba ilipitisha Kiswahili kiwe lugha rasimi nchini
- Kiswahili kufanywa somo la lazima shule za upili / msingi
- Shughuli za lazima bunge kuendelezwa kwa lugha ya kiswahili
- Vyombo vya mawasiliao kutumia lugha ya Kiswahili
- Vitabu vingi kuchapishwa kwa lugha ya Kiswahili zozote 4 x1

TATHMINI YA PAMOJA – SHULE ZA UPILI ZA JIMBO LA MACHAKOS.
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya. (K.C.S.E)
102/3
Kiswahili
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

1. SHAIRI (alama 20)
- Ugumu wa maisha unaofananishwa na kufungwa kwa waya
- Hakuna mtu wa kumsaidia ila tu watazamaji wanamcheka
- Ukweli wa maisha umekuwa kama ndoto ya uwongo –alitarajia mema lakini umegeuka vitendawili
- Machozi na damu zinamtiririka bila wa kumhurumia na kumpanguza
- Babake ni mmoja wa wanaomcheka kisha anamsisitizia kwa atadondoka tu
- Vitumbo vimechongwa chini yake tayari kumtoboa
- Vichwa vimezuka ardhini –ishara ya wengi waliopitia njia hii gumu ya maisha Alama 4

2. Eleza kwa kutoa mifano miwili miwili jinsi msanii alivyotumia tamathali zifuatavyo: (al.6)
- Jazanda
- Tashihisi
- Taswira
- Jazanda
  i) Vitimbo – Vikwazo katika maisha vinavyolemeza
  ii) Waya – mhusika (binadamu)
  iii) Kichomi –maisha magumu ya kukatisha tama
  iv) Vichwa – Jazanda ya watangulizi wake waliopitia hali hii gumu.

(b) Tashihisi
- Kichwa kinasema kwa sauti
- Vitumbo vikingoja kumtoboa
- Vichwa vinacheka
- Kichomi kinampata

3. Andika ubeti wa saba kwa lugha tutuni (al 4)
Mzunguzaji anasema kwamba sauti ya baba inamwarifu kwa kusisitiza kuwa hilo ndilo njia na ana nguvu lakini wakati utafika na atadondoka.Anaelezwa asitarajie msaada na sifa.Anaelezwa kuwa watangulizi wake walipita mkondo huo wa maisha.

4. Eleza maana ya mshororo “vichwa vyote hivi vilidondoka katika umbali uo, nawe kudondoka utadondoka” (al 2)
Wengi wamepita matatizo / ugumu huo na huu mkondo wa maisha na ni lazima hayakumbali na kujizatiti.Mwisho ukifika ataondoka.

5. Eleza umbo la shairi hili (al 4)
- Lina beti nane

- Beti zote zina mishororo saba isipokuwa ubeti wa saba
- Mishororo inatofuatiana, mingine mirefu na mingine mifupi.
  mfano ubeti 8 mshororo wa mwisho " kichomi kimenipata na sijaondoka"
  a) Halina mpangilio maalum wa vipandi
  b) Halina mtiririko wa vina.

2. a) Mktadha wa dondoo

– Dondoo hili lapatikana mwishoni mwa riwaya.
– Ni kauli ya Imani akimsemea Amani.
– Punde baada ya sherehe ya amu yake Amani kuachiliwa huru,Imani anamshajisha Amani kuandika tawasifu yake.
– Anamrai awasawiri vilivyo wanawake katika tawasifu ile. (alama 4*1=4)

b) Mbinu za uandishi.

– Nahau- usiniweke pembeni
– Tashbihi – kama tanbihi (Alama 2*1=2)

c) Usawiri wa Wahusika wa kike.

– Mwandishi ameweka sambamba wahusika hawa.
– Kuna wale wenye utu- Imani na Zuhura.
– Kuna wale wasio nao-Lowela,Michelle,na Mashaka.
– Walezi wema – Imani na Zuhura.
– Walezi wasio wema ni kama Lowela.
– Waadilifu kama Imani na mama yake.
– Wasio waadilifu kama Lowela.
– Wanaowajibika kazini kama imani na mama yake.
– Wa umri wa makamo kama Dora na Zuhura.
– Aidha kuna vijana kama Imani,Lowela na Mashaka.
– Jasiri- Imani na kwa kiwango fulani, Dora.
– Wengine wanaonekana kuishi kwenye vivuli vya wanaume (Hoja 7*2=14)

3. Katika nchi ya Tomoko, uhuru ni ndoto ambayo bado haijatimia. Jadili.

– Nchi ya Tomoko iliwahi kutawaliwa na waliodhulumu wenyeji – waliyatwaa mashamba yao, wakawakataza kufuga au kupanda mazao yaletayo fedha.Walishurutishwa kuwafanyia walowezi hawa kazi huku wakiishi katika mabanda. Walio mamlakani wanaendelea kuwadhulumu wanyonge.
– Waafrika walipochukua hatamu za uongozi mambo hayakubadilika . Walio mamalakani wanaendelea kuwadhulumu wanyonge.
– Mashamba yao yanatwaliwa mfano shamba la Chichiri na Mwinyihatibu.
– Wanafungwa jela kwa visingizo kama vile Yusuf na Amani.
– Vyombo vya Dora vinatumiwa kuendeleza matakwa ya watawala.
– Wanyonge wanafanyizwa kazi za kijungu jiko
– Lugha ya kikoloni ndiyo inayopendelewa nawatawala hawa weusi.
– Hawana uhuru wa kujiamulia mambo – Imani anatishwa na askari kwa kutohudhuria sherehe.Wananchi wamejazwa uoga.
– Ukosefu wa huduma muhimu kama vile matibabu.
– Uhuru wa kunena haupo mfano Matuko Weye anawekwa seli kwa kauli yake.
– Ukabila na ukoo unatumiwa katika kugawa nyadhifa na kazi – Nasaba Bora alipewa cheo cha utemi kwa upendeleo.
– Kitoto Uhuru ni ishara ya uhuru usio kamili , usiotunzwa na waliopewa jukumu la kuutunza.kufa kwake ni ishara ya utovu wa uhuru kamili.
– Ndoto huenda itatimia baada ya ukombozi wa pili ulioongozwa na Madhubuti na Amani.Madhila yatakomeshwa na haki kudumishwa. (Hoja zozote 10*2=20)

4. (a) Muktadha

– Yalisemwa na mamake Dadavuo Kaole.
– Alikuwa amweleza Daktari Siki.
– Walikuwa hospitalini.
– Hii ni baada ya mama kumpa mtotowe chakula cha mbwa kilichomfanya aendeshe.

(b) Nidaa – si nyinyi nd'o mjuze wanangu!

Mdokezo----nilikiona afadhali
Lahaja- nd'o
Tasifida- wanangu!

(c) Uongozi mbaya

- Migomo ya wafanyikazi.
- Ukosefu wa vifaa muhimu vya kufanyia kazi.
- Umaskini.
- Udikteta.
- Ukosefu wa dawa.
- Mapuuza.
- Propaganda.

5.

a) Msemaji ni Diwani III✓ na alikuwa akimwambia Daktari Siki ✓nyumbani kwa Diwani III ✓alipomtembelea kutaka kujua hali ya mji wa Cheneo. Binamu yake Siki aliyeitwa Susi ambaye alikuwa Meya hakutaka kuelewa hali ya watu.Daktari alikuwa anataka Diwani III azungumze na Meya kuhusu ukosefu wa dawa hospitalini✓ (asipotaja msemaji sufuri) (alama 4)

b) Ukipanda pojo huwezi kuvuna kunazi. Kauli hii ina maana kwamba unapofanya jambo baya kimakosa hutarajii kupata mazuri baadaye. Watu walimchagua Meya ambaye alijaa ubinafsi, mwenye tama na katili. Meya huyo anawanyanyasa watu na kuwatesa . Alikataa kushughulikia maslahi ya wafanyakazi wa baraza la mji, kwa kuwa walichagua mtu asiyefaa isingewezekana kutarajia mema yoyote kutoka kwake. (Hoja zozote tatu, alama 6)

c) Kuna matendo mengi ya kuonyesha kuwa watu wa Cheneo walipanda pojo na kuvuna pojo si kunazi. Walichagua viongozi wabaya, waovu na hatima yake walivuna machungu ya uongozi mbaya.Meya alitoa kauli zozote kuwafurahisha watu Lakini hakutekeleza aliyoyasema. Alisema kuwa dawa zilikuwa njiani na zingefika baada ya siku tatu jambo ambalo halikuwa kweli.Hili ni tendo linaloonyesha uongozi mbaya.Alikuwa kinara wa baraza la mji na alikuwa na mamlaka ya kuamua mgao wa ardhi ya ummma.Alitumia nafasi hiyo vibaya kwa kunyakua vipande vinane vya ardhi na kumgawia rafiki ya Bili vine.Meya alitoa kandarasi kwa njia isiyofaa na aliposhitakiwa na mwanakandarasi wa zamani aliyepewa mkataba kisheria,Bili alimshawishi Meya kushirikiana na mwanakandarasi huyo ili kujipatia fidia kutoka katika baraza la mji na kisha wao kupata mgao wao.Meya alishirikiana na Bili, Diwani I na II kuuza fimbo ya Meya.Wafanyakazi waliogoma wakidai haki zao za; nyongeza ya mishahara, gharama kuwa ghali maishani , ukosefu wa dawa na mengineyo, walifurushwa vibaya na askari kwa amri ya Meya.Mji unachafuka na viongozi wa baraza chini ya Meya hawakujali kulishughulikia hilo.

d) Takriri -panda,vuna
Methali – mtu huvuna alichopanda. (Akataja ½, mifano ½)
DAMU NYEUSI

a) Ni maneno ya msimulizi.Anawaza haya baada ya kushindwa kumtoa ushamba mkewe.Ni baada ya kujipa moyo tena wa kutaka kumtoa kinyangaa.Aziza kwa kutaka kujua sababu yake kutovaa viatu nyumbani kwake.Hofu yake sasa ni kuwa hakutaka waliojifunga kuja kumtazama mke wangu namna alivyojirekebisha waondoke na zawadi za vichekesho. (al.4)

b)

Msimulizi	Aziza
- Ni mbaguzi ambaye aliamini watu wa daraja la chini hawakupaswa kuchangamana na watu wa daraja la juu.	- Hana ubaguzi na alichangamana na kila mtu
- Anaathirika na tamaduni za kigeni na kupuuza tamaduni asilia	- Ni mwanajadi ambaye hataki kuathiriwa na usasa.Angali anang'ang'ana mambo ya jadi kama vile kutembea bila viatu.
- Anaathirika na elimu na utajiri katika familia na kuzidharau kazi zingine hata	- Ni mkulima na mfanyikazi.Hili linadhibitika katika mikono yake ambayo imekomaa kutokana na kufanya kazi ngumu.

- Ni msomi na alizaliwa katika familia ya wakwasi	- Alitoka familia ya walala hoi na hakupata elimu yoyote.

(Asipolinganisha mwanafunzi amekosea) (alama 8)

c)

- Kuchaguliwa mke. Kijana wa kiume katika jamii alioa kutokana na mke aliyechaguliwa na wazazi wake.
- Wana pia walilazimishwa kuoa au kuolewa wakishafika umri wa ndoa.
- Wanawake kudhunishwa kama vile kudai kuwa ndio wanaohitaji maongozi ya mume na si kinyume chake (al.6)

d)

- Mbinu zilizotumika
- Tashbihi
- Balagha (al.2)

6. Mke wangu
- kuchaguliwa mume
- Waliosoma na kwenda mijini kuchukuliwa kama wajuaji na kuharibika kimaadili.
- Anaonekana kuwa ndiye anayehitaji maongozi ya wanaume na si kinyume chake.
- Mke ndiye anayepaswa kustaarabishwa na mwanamume na si kinyume chake.

Maeko
- Mume amepewa haki ya kumpiga mkewe lakini mke hana ruhusa ya kumpiga mume.
- Mke anafanywa ngoma na pia kutusiwa vibaya.
- Kupigwa kwa wake haichukuliwi hatua yoyote ya kisheria.
- Hana usemi mbele ya mume.Anakesha kumngoja mume asijue anakotoka.
- Ni kiumbe duni mbele ya mwanamume.

Kanda la usufi
- Analaumiwa wana wanapokosa. Mama yake Sela analaumiwa pale Sela anapopata ujauzito.
- Sela anaposhika mimba anafukuzwa shuleni ilhali Masazu hakuathirika.
- Anatwikwa mzigo wa ulezi, mamake Sela ndiye anaonekana ana jukumu la kumlea mjukuu wake japo ni fukara.
- Mzee Butali ,baba yake Sela,anakasirika kuwafukuza mama na bintiye Sela.

Mwana wa Darubini
- Kubakwa na kulazimishwa kufanya mapenzi kinyume na matakwa yake kama vile kananda.
- Kunyang'wa mtoto kama vile kananda
- Kuchaguliwa ume-mwatela kumkabithi bwana mkongo kananda kama mke wake.
- Hana uwezo wa kufanya maamuzi apendavyo.
- Kananda anauzwa baada ya muda kama mtumwa na bwana Mkongo.

Kikaza
- Ni chanzo cha matatizo –Kuvunjwa kwa masharti ya kikazi katika jamii inatokana na Bi.Mtajika kuingiliamadaraka ya mumewe na kujifanya kiongozi.
- Wanabaguliwa na kunyimwa nafasi za uongozi.
- Kiumbe aliyejielewa na kuingilia wajibu usio wake kiasi kwamba akipewa fursa ya kusalimu wanakijiji
- anachukua saa nzima.
- Ni kiumbe cha kushangaza, kukasirisha na kuudhi. (zozote nne)

7.

a) Maghani –Ni ushairi ambao hutolewa kwa kalima badala ya kuimbwa.Hushughulikia maswali ya kijamii k.v kazi, maombolezi au siasa kama ilivyo katika nyimbo tofauti na nyimbo maghani hayaimbwi 2x1 = 2

b) Sifa za maghani
- Ni tungo za kishairi. Hii ina maana kuwa yana sifa za kishairi za kuwa na mapigo ya kimziki
- Husimulia matukio kwa kirefu hasa yanayotambwa.
- Hutungwa papo hapo na kusemwa au kutongelewa Mbele ya hadhira.
- Huweza kutolewa na mtu mmoja au kundi la watu.
- Huwa na majisifu (majigambo)
- Huwa na uigizaji /utendaji
- Hutumia tamadhali za usemi kwa wingi

c)
- Kuandika
- Kunasa sauti – tepurekodi
- Kamera
- Video
- Sinema /filamu
- Akilini 4=Alama 4

d)
- Maandalizi- kuhusisha uteuzi wa mada, utambuzi wa malengo yaliyowazi katika mawanda ya utafiti,
- utambulizi wa mazingira na wakati ufaao na mbinu za ukusanyaji wa data.
- Ukusanyaji wa data yenyewe kwa kuhoji kushuhudia, kurekodi na hata kushirikisha.
- Kurekodi data kwa kuandika kupiga chapa au video
- Kuchunguza data ili kutafsiri na kuandika upya neno kwa neno bila kupotosha maana ya lugha asili
- Kuchambua na kufasili data bila kupotosha maana
- Kuchambua na kufasili data ili kupata matokeo kamili ya utafiti

Hatua za mwanzo 5 x 1 =Alama

e)
- Ukosefu wa utafiti madhubuti
- Ukosefu wa walimu waalewa
- Vitabu virejelewa havipo
- Alama kuwa haina manufaa katika kuelimisha watu
- Baadhi ya vipera ni kinyume cha maadili ya kidini
- Vijana wa sasa hawaonei fasihi hii fahari
- Fasihi andishi yaelekea kuzingatiwa mno. zote 5 =Alama 5

SUNSHINE
102/1
KISWAHILI
INSHA
KARATASI 1
SWALI LA LAZIMA

1. Kumetokea shambulizi la kigaidi katika nchi jirani. Wewe kama balozi mwandikie raisi na watu wa nchi hiyo risala ya rambirambi.
2. Dhuluma dhidi ya wanawake imekita mizizi ndini. Jadili.
3. Mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi.

…Na huo ndio ukawa mwanzo mpya.

SUNSHINE
KARATASI 102/2
KIDATO CHA NNE
SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA
MTIHANI WA KABLA YA MWIGO

UFAHAMU (ALAMA 15)
Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali.

Suala la mahusiano ya wanadamu katika jamii, uainishaji wake na uathihirikaji wake limewashughulisha wataalamu wa elimu jamii kwa dahari ya miaka. Suala hili huwatafakarisha wataalamu hao kutokana na umuhimu wake katika maisha ya binadamu msingi mkuu wa uainishaji wa mahusiano hayo ni kukichunguza kipindi cha mahusiano yenyewe. Yapo mahusiano baina ya waja ambayo yanachukua muda mfupi, kwa mfano saa au dakika chache, na mengine ambayo huenda yakachukua miaka ayami.

Mahusiano ya muda mrefu kabisa ni yale yanayojulikana kama mahusiano ya kudumu. Inamkinika kudai kuwa miundo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi huweza kuyadhibiti mahusiano hayo kwa kiasi

kikubwa. Watu wengi huitikadi kuwa uhusiano uliopo baina ya mtu na jamaa yake utachukua muda mrefu, na kwa hivyo ni uhusiano wa kudumu. Hali hii hutokana na uhalisi kuwa tunahusiana na jamaa zetu kwa kipindi kirefu labda tangu ukembe hadi utu uzima wetu. Uhusiano huu hautarajiwi kuvunjwa na umbali wa masafa baina yetu; tunaendelea kuwasiliana kwa barua au, katika enzi hii ya utandawazi, kwa kutumia nyenzo za teknohama kama mtandao na simu za mkononi, na kudumisha uhusiano wetu wa kijamaa. Hata hivyo, inawezekena baadhi ya mahusiano ya kijamaa yasiwe ya kudumu. Mathalan, uhusiano uliopo baina ya mke na mume, na ambao unatarajiwa kuwa wa kudumu au kipindi kirefu, unaweza kuvunjwa kwa kutokea kwa talaka. Talaka hiyo inavunja ule uwezekano wa uhusiano wa kudumu unaofumbatwa na sitiari ya pingu za maisha.

Katika ngazi ya pili, mahusiano ya koindi cha wastani, kuna mahusiano yanayohusisha marafiki zetu maishani, shuleni au kwenye taasisi zozote zile, majirani zetu, wenzetu katika mwahali mwa kazi, washirika kwenye sehemu za ibada au za burudani na wenzetu kwenye vyama tofauti na makundi ya kujitolea. Inawezekana kudahili kuwa baadhi ya mahusiano haya, hususan baina ya marafiki na majirani huweza kuwa ya miongo na daima. Hali hii huweza kutegemea muundo na mfano wa jamii. Kwa mfano, kwa majirani wanaoishi kwenye janibu, fulani mahususi, na kwa miaka tawili bila ya kuhajiri. Uhusiano wao na majirani huweza kuwa wa kudumu. Hali hii **inasigana** na hali iliyoko kwenye maisha ya mijini. Maisha ya mijini yana sifa ya kubadilkikabadilika. Isitoshe, kutokana na mfumo wa maisha ya kibepari **yameghoshi** ubinafsi mwingi. Mawimbi ya mabadiliko na ubinafsi uweza kuumomonyoa ukuta wa uhusiano wa kudumu.

Mwelekeo wa maisha ya siku hizi ya uhamaji kutoka maeneo au viambo walikoishi watu unasababisha kupombojea kwa mahusiano ya kudumu baina yao na majirani zao. Uhusiano kati ya wenza katika mazingira ya kazi unahusiana kwa kiasi fulani na ule wa majirani. Vimbunga vya ufutwaji kazi, ubadilishaji wa kazi, hali zisizotegemewa na mifumo ya kimataifa pamoja na hata mifumo ya kisiasa huweza kuathiri mshikamano wa wanaohusika kazini.

Kiwango cha mwisho cha mahusiano ni uhusiano wa mpito au wa muda mfupi. Mahusiano ya aina hii hujiri katika muktadha ambapo pana huduma fulani. Huduma hizi zinaweza kuwa dukani, kwenye sehemu za ibada, kwenye kituo cha mafuta, kwa kinyozi, kwa msusi na kadhalika. Kuna sababu kadha zinazotufanya kuyazungumzia mahusiano ya aina hii kama ya mapito. Kwanza, uwezekano wa mabadiliko ya anayeitoa huduma hiyo ni mkubwa. Si ajabu kuwa unaporudi kwa kinyozi au msusi untambua aliyekushughulikia hayupo. Hata hivyo, kuna **vighairi** hususa pale ambapo mtoa huduma anayehusika ni yule mmoja.

Mahusiano ya mpito yanatawaliwa na “uhusiano wa chembe chembe”. Uhusiano wa chembe chembe, bidhaa ya mfumo wa kibepari, unamaanisha kuwa kinachomshughulisha mtu ni chembe ndogo tu ya mwenzake. Chembe hiyo inaweza kuwa huduma, kwa mfano, gazeti analokuuzia mtu, kiatu anachokushonea, nguo anazokufulia, ususi anaokufanyia n.k. Mahusiano ya aina hii yametovukwa na hisia za utu na ni zao la mifumo ya kisasa na kiuchumi na kijamii. Mtu anayehusiana na mwenzake kwa misingi ya chembe ndogo tu, huenda asijali kama mwezake amekosa chakula, amefutwa kazi, amefiliwa na kadhalika.

Suala kuu tunalopaswa kujiuliza nji: Je, tunahusiana vipi na jamaa zetu, taasisi zetu, marafiki zetu na majirani zetu? Je, uhusiano wetu na raia wenzetu ni w aaina gani? Je, uhusiano wetu na nchi yetu ni wa mpito au ni wa kudumu?

(a) Taja kigezo muhimu cha kuzungumzia mahusiano. (al 1)
(b) Eleza imani ya watu kuhusu uhusiano baina ya jamaa. (al 1)
(c) Fafanua athari ya technolojia kwenye mahusiano ya watu. (al 2)
(d) Eleza sababu nne kuu za kuharibika kwa mahusiano katika maisha ya leo. (al 4)
(e) Taja sifa kuu ya mahusiano ya muda mfupi. (al 2)
(f) Je, kifungu hiki kina ujumbe gani mkuu? (al 2)
(g) Eleza maana ya maneno yafutayo kama yalivyotumiwa katika kifungu. (al 3)
(i) inasigana……
(ii) yameghoshi……
(iii) vighairi……..

UFUPISHO (ALAMA 15)

Ujambazi wa kimataifa ni tatizo lililowasumbua walimwengu kwa muda mrefu sana. Serikali nyingi

zimetumia mapesa mengi kwa miaka mingi sana zikijitahidi kupambana na janga hili. Hata hivyo, fanaka haijapatikana, wala haielekei kamwe kuwa itapatikana leo au karne nyingi baadaye.

Yumkini tatizo kubwa lililopo ni kuhusu jelezi la dhanaya "ujambazi" tena "wa kimataifa". Hili ni tatizo mojawapo na yapo mengi sana. Tatizo la pili ni kiburi. Kuna wale watu binafsi na hasa viongozi w anchi kubwakubwa na serikali zao zilizojiaminisha kuwa ujambaz ni balaa kweli, tena belua, lakini huo ni wa huko, wala hauwezi kuwagusa licha ya kuwashtua wao.

Kulingana na maoni watakaburi hao, ujambazi ni wa watu 'washenzi' wasiostaarabika, wapatikanao katika nchi zisizoendelea bado. Ujambazi peke wanaouona unafaa kukabiliwa ni dhidi ya mbubujiko wa madawa ya kulevya uliosababishwa na vinyagarika kutoka nchi hizo maaluni za "ulimwengu wa tatu". Kulingana na wastaarabu wa nchi zilizoendelea, vinyangarika hivi ndivyo hasa adui mkubwa wa ustaarabu ulimwenguni na ni sharti vifagiliwe mbali bila huruma. Baada ya kusawasagwa, ulimwengu mstaarabu utazidi kutononoka na ahadi ya mbingu hapa ardhini itakamilika.

Imani ya watu hawa ya kuwa ujambazi wa kimataifa, hata iwapo upo, hauwezi kuwashtua wala kuwatingisha wao ilikuwa kamili na timamu. Ilikuwa kamili na timamu hadi hapo mwezi Septemba tarehe 11 mwaka wa 2001, ndege tatu za abiria zilipoelekezwa katika majumba mawili ya fahari, yenye urefu wa zaidi ya ghorofa mia moja na kuyatwangilia mbali. Mshtuko na kimako! Kimako kwa kuwa, kabla ya siku hiyo, Wamarekani hawangeweza kudhani kwamba ingewezekana taifa lolote au mtu yeyote kuthubutu kushambulia nchi yao, taifa wasifa lililojihami barabara dhidi ya aina yoyote ile ya uchokozi kutoka pembe lo lote la dunia.

Hakuna ulimwenguni mzima, aliyeamini kuwa Marekani ingeweza kushambuliwa. Kwa ajili hiyo, mshtuko uliitingisha ardhi yote na huzuni ilitanda kote, kama kwamba sayari nzima imeshambuliwa, wala sio Marekani pekee.

Mintarafu hiyo, Marekani ilipolipiza kisasi kwa kuwaunguza waliokuwemo na wasiokuwemo kwa mabomu hatari huko Afghanistan, idadi kubwa ya watu duniani ilishangilia na kusherehekea. Kwa bahati mbaya, tafsiri ya shambulizi la minara-pacha na Newyork na lile la Pentagon, uti wa uwezo wa kivita wa Marekani, ulizorota. Kuna wengi waliodhani huo ni mwanzo wa vita vya Waislamu dhidi ya Wakristo na kwa muda, Waislamu wote wakashukiwa kimakosa kuwa ni majambazi wa kimataifa.

(a) Bila kubadilisha maana, fupisha aya tatu za kwanza. (maneno 65 – 75) (al 10, 2 za utiririko)
Matayarisho
Nakala safi

(b) Ukizingatia aya tatu za mwisho, fafanua fikira za watu na mambo yote yaliyotokea baada ya Septemba tarehe 11, 2001. (maneno 65 – 75) (al 10, 2 za utiririko)
Matayarisho
Nakala safi

MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

(a) Silabi ni nini? (al 2)

(b) Tenga silabi katika maneno yafuatayo kisha uandike aina yake. (al 2)
(i) igwa
(ii) Oa

(c) Dhihirisha panapotiwa shadda katika maneno yafuatayo. (al 2)
(i) Galagala ……
(ii) Teketeza ……..

(d) Bainisha nomino katika sentensi zifuatazo kisha utaje aina zake. (al 2)
(i) Uhubiri wa mama huyu una mvuto mkubwa
(ii) Kabati hili limevamiwa na wadudu wengi waharibifu.

(e) Eleza matumizi ya kihusishi kwa katika sentensi ifuatayo. (al 2)
Tahadhari huandikwa kwa hati nzito.

(f) Tenga viambishi na mzizi katika neno lifuatalo. (al 2)
Siji.

(g) Unda nomino kutokana na kivumishi kifatacho. (al 1)
Tepetevu

(h) Pigia mstari na kuainisha kirai katika sentensi ifuatayo. (al 2)
Haifai kujenga karubu na nyaya za umeme

(i) Bainisha shamirisho kitondo katika sentensi ifuatayo. (al 2)

Mzalendo amemwandikia mhariri barua.

(j) Eleza kama sentensi ifuatayo ni sahili, ambatano ama changamano. (al 2)

Tulipewa ratiba ya shughuli hiyo lakini hatukuitia maanani

(k) Bainisha vishazi huru na vishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo. (al 2)

Simu tamba ambayo ameninunulia imenirahisishia mawasiliano

(l) Kanusha sentensi ifuatayo. (al 2)

Ninamtarajia mpwa wangu awasili leo

(m) Andika katika wingi. (al 2)

Huzuni aliyokuwa nayo yatima huyu ilinitia kite na imani.

(n) Andika kinyume cha neno lililopigwa mstari. (al 1)

Mhalifu huyu <u>alitunga</u> mimba

(o) Bainisha matumizi ya **KI** katika sentensi ifautayo. (al 1)

Jua limekuwa likiwaka tangu Januari

(p) Bainisha matumizi ya **ka** katika sentensi ifuatayo: (al 1)

Sungura alifika nyumbani akamsalimu mkewe, akafululiza msalani akaoga

(q) Akifisha sentensi hii: (al 2)

Mmea wa pareto ni muhimu mno nchini akasema afisa wa kilimo

(r) Badilisha katika usemi wa taarifa: (al 2)

“Tutakusaidia ikiwa utashirikiana nasi,” afisa wa usalama akasem.

(s) Andika katika ukubwa ukizingatia neno lililopigwa mstari. (al 1)

Aliyerembesha <u>uso</u> kwa poda.

(t) Bainisha maana mbalimbali za sentensi ifuatayo: (al 3)

Mwalimu amempigia wanafunzi simu

(u) Silabi mwambatano ni nini? (al 1)

(v) Tunga sentensi moja udhihirishe maana mbili za neno hili: <u>Rudi</u> (al 1)

(w) Pigia mstari vivumishi katika sentensi ifuatayo kisha uandike aina yake. (al 2)

Bibi huyu ni mpole uso wake wenye haya huuinamisha kila mara.

SUNSHINE
102/3
KISWAHILI
FASIHI YA KISWAHILI
MTIHANI WA KABLA YA MWIGO 2015
SEHEMU YA A
LAZIMA
FASIHI SIMULIZI (ALAMA 20)

(a) Toa sifa mbili za fasihi simulizi. (al 2)
(b) Taja na ufafanue aina mbili za hadhira wa fasihi simulizi. (al 2)

(c) Hadithi za kisalua ni nini? (al 1)
(d) Fomyula ya kuhitimsha ina umuhimu gani? Toa hoja mbili. (al 1)
(e) Eleza sifa mbili za hadithi za mazimwi. (al 2)
(f) Ni nini dhima ya misimu katika jamii? (al 2)
(g) Ushairi simulizi ni nini? (al 1)
(h) Taja sifa mbili za hodiya. (al 2)
(i) Eleza sifa tatu za mwigizaji bora. (al 3)
(j) Eleza sifa mbili za ngoma. (al 2)
(k) Tofautisha kati ya malumbano ya utani na maapizo. (al 2)

SEHEMU YA B: RIWAYA
KIDAGAA KIMEMWOZEA: KEN WALIBORA

1. "We bwana unafikiri natumia petroli nini?"
   (a) Uweke usemi huu katika muktadha wake. (al 4)
   (b) Huku ukitoa mifano, eleza mbinu mbili za lugha zilizotumiwa na mwandishi katika dondoo hili. (al 4)
   (c) Eleza migogoro yoyote sita inayojitokeza katika riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (al 12)
2. Udhalimu ni maudhui makuu katika riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. Thibitisha. (al 20)

SEHEMU C: HADITHI FUPI
DAMU NYEUSI: KEN WALIBORA & S. A. MOHAMMED

1. "Wenzangu wote, mwafahamu hadithi ya kobe?"
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al 4)
   (b) Fafanua sifa 4 za msemaji. (al 4)
   (c) Kwa kiurejelea dondoo taja mbinu inayojitokeza katika hadithi inayorejelewa na msemaji. Kisha ufafanue kwa mifano mwafaka. (al 12)
2. Kwa kurejelea hadithi zifuatazo jadili maudhui ya:
   (i) Tamaa na ubinafsi katika Samaki wa Inchi za Joto.
   (ii) Ushirikina katika Gilasi ya Mwisho Makaburini.

SEHEMU D: TAMTHILIA
MSTAHIKI MEYA: TIMOTHY AREGE

(i) "Si vyombo vya habari, si wanasiasa. Si wasomi."
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al 4)
   (b) Taja na ufafanue mbinu ya lugha katika dondoo hili. (al 2)
   (c) Fafanua sifa zozote nne za msemaji. (al 4)
   (d) Umaskini ni tatizo kuu katika cheneo. Tetea kauli hii huku ukitoa mifano mahususi. (al 10)

(ii) Mwandishi wa Mstahiki Meya ametumia mbinu ya majazi kufanikisha ujumbe wake. Jadili. (al 20)

SEHEMU E: MASHAIRI

Shairi

Mapenzi kitu ajabu, yakutia bumbuwazi
Yakufanya uwe bubu, kujibu huwa huwezi
Shubiri kwako zabibu, na vitamu huviwezi.

Wamkuta kaemewa, asemayo hayajuwi
Aumba akiumbuwa, aona maruwiruwi
Vigumu kumuopowa, na kwa ngisi kumvuwi.

Hukumbuka ya zamani, yote walofanyiana
Nyumbani barabarani, ayaona kama jana
Akili yake na nyani, aruka ingagongana.

Wangoja nyota ya jaha, kutwa wewe unahaha
Mawazo yako silaha, akukwaaye usaha
Usifanyiwe msaha, waugeuza karaha.

Kalelewa kaleleka, utani kwake ni mwiko
Njiani yeye na kaka, hapokei mauliko
Ghadhabu zake zap aka, hapendi maziko.

Na Hashil S. Hashil

1. Andika kichwa mwafaka cha shairi hili. (al 1)
2. Eleza umbo la shairi hili. (al 4)
3. Tambua tamathali za usemi alizozitumia msanii. (al 4)
4. Taja na ufafanue uhuru wa mshairi. (al 2)
5. Andika ubeti wa tatu kwa lugha tutumbi. (al 4)
6. Fafanua mambo matatu yanayohusishwa na mapenzi. (al 3)
7. Taja nafsi katika shairi hili. (al 1)
8. Taja toni ya mshairi huyu. (al 1)

Chaguo shairi moja kasha ujibu maswali.

Mtazameni ….nguzo ya Afrika
Mtumwa wa watumwa waliridhiya
Amekita jembe lake akilisujudia
Kwa tambo lililoumbuka na kusekehea
Uso ukifuka ukata ulojifanya tabia
Na machungu ya maonevu alovumilia.

Moyo wake mzito ulokokomaa kama kuni
Haujui tena kutarajia wala kutamani
Umekufa ganzi, kutohisi raha huzuni

Basi iteni fikira mambo ukiyafikiri
Siku hamaki yake itakapochafuka kama bahari
Siku ukweli wa hali yake utapodhihiri

Umejiandalia vipi…
Huo mkono ulomuumbua na kumkausha
Kizo pumzi zilomzima taa ya maisha
Kumfunga kizuizi , gizani kumtowesha

Ni jawabu gani alowekewa na wakati
Kuipoza ghadhabu ya kiu ingawa katiti
Kuikiwaza hamaki ya njaa hii ya dhati
Jnjaa ya maisha itakayo kushibishwa.

1. Lipe shairi hili kichwa mwafaka. (al 2)
2. Taja nafsi neni katika shairi hili. (al 2)
3. Andika mifano ya uhuru wa mshairi katika shairi hili. (al 4)
4. Eleza mbinu za lugha zilizotumiwa. (al 4)
5. Eleza sifa zilizomkabili mzungumzaji. (al 4)
6. Tambua mishororo miwili mishata. (al 2)
7. Fafanua umuhimu wa mistari mishata. (al 2)

SUNSHINE
MTIHANI WA KABLA YA MIGWI 2015
INSHA
MWONGOZO KARATASI YA KWANZA

1. Anwani ya mwandishi
2. Mada –Herufi kubwa na ipigiwe mstari
   Mada itaje ni risala kwa nani kwa nini na kuhusu nini.
3. Mtajo utategemea mwandikiwa
   Mf Kwa rais na wananchi wa--------
   Wazalendo wa_____
   Raia_____
   Watu wa_____
4. Utangulizi –uonyeshe masikitiko/huzuni nk.

_ Mwili
_ Changamoto za kigaidi
_ Namna mataifa yanakabiliana na ugaidi
_ Kisa cha mashambulizi katika nchi zingine
_ Kuhimiza taifa hilo kujasirika /kutia moyo
_ Kutia juhudi na mikakati dhidi ya ugaidi
_ Uhamaji/swala la wakimbizi
_ Mashirika yasiyo ya kiserekali
_ Usalama katika Nyanja na sehemu zilizo na watu wengi
_ Benki bandia kupitisha fedha
_ Kutoa msimamo wake kuhusu swala hilo/mo Asitoe msimamo wake.

5. Hitimisho

_ Jina lake na sahihi kuandikwa.
DHULUMA DHIDI YA MWANAMKE.

1 .Kichwa
Herufi kubwa na ipigiwe kistari

2. utangulizi
Kueleza maana ya Dhuluma na kutolewa mifano mbalimbali.

3. mwili
Kujadili hoja

a. Ukeketaji
b. Ndoa za mapema
c. Kuvuliwa nguo hadharani
d. Kubezwa na kudharauliwa hadharani
e. Ubakaji
f. Kupigwa na wanaume
g. Kudhulumiwa kazini –kimapenzi
   1. Kupuuzwa
   2. Kunyimwa vyeo
   3. Majukumu mengi
h. Kutengwa katika kurithi mali haswa wajane
i. Jamii hutenga wasichana kielimu.
j. Nafasi za kazi

Hakiki mifano mingine
Hoja zisipungue sita.
Maneno 400.

3. MZIGO WA MWENZIO NI KANDA LA USUFI
Methali

1. Kichwa –kiandikwe katika herufi kubwa na kipigiwe kistari
Yaweza kuwa sehemu ya methali au kudokeza methali hiyo .mf mzigo wa mwenzio

2. Utangulizi
Anaweza kutoa maana ya juu na ndani ya methali na matumizi ya methali.
Anaweza buni kisa ambacho kinadhihirisha pande mbili za methali.

1. Nani alikuwa na tatizo (mzigo)

2. Aliyepuuliza mbali tatizo hilo(kanda la usufi).
3. Makundi mawili yajitokeze.
   Hitimisho
_ Muktasari wa kisa.
_ Funzo lidhihirike la methali husika
   Maneno 400
4……Na huo ukawa mwanzo mpya.
1. Kichwa
   -Mwanafunzi abuni kichwa cha insha.
2. Mwili
_ Atunge kisa kinachohusiana na kichwa na kilichovutia.
_ Atumie lugha ya mvuto mkubwa.
_ Kuwepo na mtiririko mzuri wa kisa husika.
3. Hitimisho
_ Amalize insha kwa maneno aliyopewa,bila kuongeza wala kudondoa.
_ Asipomaliza au aongeze apate bahshish

SUNSHINE
KARATASI 102/2
KIDATO CHA NNE
MWONGOZO

UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali.

(a) Taja kigezo muhimu cha kuzungumzia mahusiano. (al 1)
Kipindi cha mahusiano yenyewe.

(b) Eleza imani ya watu kuhusu uhusiano baina ya jamaa. (al 1)
Ni uhusiano wa kudumu / huchukua muda mrefu / uhusiano wa kipindi kirefu / ni wa milele / huanzia utotoni hadi utu uzima

(c) Fafanua athari ya technolojia kwenye mahusiano ya watu. (al 2)
Huwezasha watu au jamaa wako mbali kuwasilianan au hudumisha uhusiano wa kijamii.

(d) Eleza sababu nne kuu za kuharibika kwa mahusiano katika maisha ya leo. (al 4)
(i) Talaka – huvunja uhusiano baina ya mke na mume
(ii) Ubadilishija wa kazi
(iii) Mifumo ya kimataifa na kisiasa
(iv) Mabadiliko ya maisha ya mjini
(v) Uhamaji
(vi) Kufutwa kazi (zozote x4 x 1 = 4)

(e) Taja sifa kuu ya mahusiano ya muda mfupi. (al 2)
Hatuwaliwa na uhusiano wa chembechembe.

(f) Je, kifungu hiki kina ujumbe gani mkuu? (al 2)
Mahusiano katika jamii / aina za mahusiano katika jamii.

(g) Eleza maana ya maneno yafutayo kama yalivyotumiwa katika kifungu. (al 3)
(i) inasigana – inapiganan / inakizana / inatofautiana / inahitilafiana
(ii) yameghoshi - yamejaa / jamebeba / yamesheheni / yamerundika
(iii) vighairi kinyume / vinyume / tofauti

UFUPISHO (ALAMA 15)

(a) Bila kubadilisha maana, fupisha aya tatu za kwanza. (maneno 65 – 75) (al 10, 2 za utiririko)
Matayarisho

a) Ujambazi wa kimataifa umewasumbua walimwengu
b) Serikali nyingi zimejitolea kupambana na janga hili
c) Fanaka haijapatikana
d) Tatizo kubwa ni jelezi la dhana ya ujambazi wa kimataifa
e) Tatizo jingine ni kiburi cha mataifa makubwa kuona hayawezi. Kufikwa na ujambazi.

f) Kwao ujambazi unaofaa kukabiliwa ni wa dawa za kulevya
g) Unasababishwa na vinyang'arika kutoka ulimwengu wa tatu
h) Vinyang'rika hizi ni sharti vifangiliwe ili ustaarabu udumishwe.
i) Watakaburi hawa wanaamini kuwa ujambazi ni wa watu washenzi katika mchi zisizoendelea.
(zozote 7 x 1 = 7, utiririko 1) = alama 8

(b) **Ukizingatia aya tatu za mwisho, fafanua fikira za watu na mambo yote yaliyotokea baada ya Septemba tarehe 11**, 2001. (maneno 65 – 75) (al 10, 2 za utiririko)
Matayarisho
(a) Wamarekaru walishtuka na kumaka kuwa taifa lolote au mtu yeyote angethubutu kuwashambulia
(b) Hakuna aliyeamini kuwa marekani ingeweza kushambuliwa
(c) Huzuni ilitanda ulimwenguni kote
(d) Marekani ulipiza kisasi kwa kuwaunguza waliokuwemo na wasiokuwemo kwa mahomu Afghanistan
(e) Wengi duniani walisherehekea
(f) Tafsiri ya shambulizi hili ilizorota
(g) Wengi walidhani kuwa ulikuwa mwanzo wa vita vya waislamu dhidi ya wakristo.
(h) Waislamu wote walishukiwa kimakosa kuwa ni majambazi.
Zozote 6 x 1 = 6
Utiririko 1
7

MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

(a) Silabi ni nini? (al 2)
……***Pigo kamili la sauti katika neno***

(b) Tenga silabi katika maneno yafuatayo kisha uandike aina yake. (al 2)
(i) igwa
i-gwa
(ii) Oa
o-a Dhihirisha panapotiwa shadda katika maneno yafuatayo. (al 2)
(i) Galaga'la ……
(ii) Tekete'za ……..

(c) Bainisha nomino katika sentensi zifuatazo kisha utaje aina zake. (al 2)
(i) Uhubiri wa mama huyu una mvuto mkubwa
……***Uhubiri- dhahania*** ……***Mama-kawaida. Mvuto-dhahania***
(ii) Kabati hili limevamiwa na wadudu wengi waharibifu.
Kabati – kawaida ***Wadudu – kawaida*** Eleza matumizi ya kihusishi kwa katika sentensi ifuatayo. (al 2)
Tahadhari huandikwa kwa hati nzito.
Jinsi – au chombo/kitumizi

(d) Tenga viambishi na mzizi katika neno lifuatalo. (al 2)
Siji.
Si-j-i

(e) Unda nomino kutokana na kivumishi kifatacho. (al 1)
Tepetevu
……***Utepetevu***……Pigia mstari na kuainisha kirai katika sentensi ifuatayo. (al 2)
Haifai kujenga karubu na nyaya za umeme ***RT***
…***Karibu na –RN*** …***Nyaya za umeme RN***

(f) Bainisha shamirisho kitondo katika sentensi ifuatayo. (al 2)
Mzalendo amemwandikia mhariri barua.
Barua-shamirisho kipozi ……***Mharir- shamirisho kitondo***

(g) Eleza kama sentensi ifuatayo ni sahili, ambatano ama changamano. (al 2)
Tulipewa ratiba ya shughuli hiyo lakini hatukuitia maanani
Ambatano: zaidi ya wazo moja

(h) Bainisha vishazi huru na vishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo. (al 2)
Simu tamba ambayo ameninunulia imenirahisishia mawasiliano
ambayo ameninunulia-kishazi tegemezi
Simu tamba imenirahisishia mawasiliano-kishazi huru.

(i) Kanusha sentensi ifuatayo. (al 2)

Ninamtarajia mpwa wangu awasili leo
Simtarajii mpwa wangu awasili leo.

(j) Andika katika wingi. (al 2)
Huzuni aliyokuwa nayo yatima huyu ilinitia kite na imani.
Huzuni waliyokuwa nayo mayatima hawa ilitutia kite na imani.

(k) Andika kinyume cha neno lililopigwa mstari. (al 1)
Mhalifu huyu alitunga mimba
Mhalifu huyu alitungua mimba.

(l) Bainisha matumizi ya **KI** katika sentensi ifautayo. (al 1)
Jua limekuwa likiwaka tangu Januari
Hali ya kuendelea.

(m) Bainisha matumizi ya **ka** katika sentensi ifuatayo: (al 1)
Sungura alifika nyumbani akamsalimu mkewe, akafululiza msalani akaoga
Ka- mfululizo wa vitendo/utokeaji wa vitendo vingi kwa wakati mmoja.

(n) Akifisha sentensi hii: (al 2)
Mmea wa pareto ni muhimu mno nchini akasema afisa wa kilimo
"Mmea wa pareto ni muhimu mno nchini," akasema afisa wa kilimo.

(o) Badilisha katika usemi wa taarifa: (al 2)
"Tutakusaidia ikiwa utashirikiana nasi," afisa wa usalama akasema.
Afisa wa usalama alisema kuwa wangemsaidia ikiwa angeshirikiana nao.

(p) Andika katika ukubwa ukizingatia neno lililopigwa mstari. (al 1)
Aliyerembesha uso kwa poda.
Aliyerembesha juso kwa poda.

(q) Bainisha maana mbalimbali za sentensi ifuatayo: (al 3)
Mwalimu amempigia wanafunzi simu
i) Ametumia simu kama chombo kumpiga mwalimu.
ii) Amepiga simu kwa niaba ya mwanafunzi.
iii) Amempiga kwa sababu ya simu.

(r) Silabi mwambatano ni nini? (al 1)
Ni silabi ambayo ina muundo wa zaidi ya konsonanti moja

(s) Tunga sentensi moja udhihirishe maana mbili za neno hili: Rudi (al 1)
Rudi – adhibu mwana
Rudi – Rejea

(t) Pigia mstari vivumishi katika sentensi ifuatayo kisha uandike aina yake. (al 2)
Bibi huyu ni mpole uso wake wenye haya huuinamisha kila mara.
Huyu – Kivumishi kiashiria.
Wake – kivumishi kimilikishi.
Wenye – Kivumishi cha pekee.

ISIMU JAMII

Maenezi ya Kiswahili Afrika Mashariki punde baada ya uhuru yalikuwa na chagamoto tele. Fafanua zozote tano. (al 10)

(a) Uhaba mkubwa wa wataalamu wa Kiswahili
(b) Athari kutoka kwa lugha ya kwanza.
(c) Watu kuchangamka lugha nyinginezo ka vile kiingereza, kijerumani.
(d) Imani potovu – lugha ya Kiswahili ni duni
(e) Uhaba wa walimu wa Kiswahili.
(f) Uhaba wa vitabu vya Kiswahili.
(g) Kutokuwepo kwa sera ya lugha kutoka kwa baadhi ya serikali za mataifa ya Afrika mashariki.
(h) Uhaba wa pesa za kutafikia
(i) Nchi za Afrika za kukuza na kuendeleza Kiswahili
Zozotte 5 x 2 = 10
Lazima afafanue.

SUNSHINE
PAPER 3
MWONGOZO

1. Msemaji – Dora
   Msemewa – mwalimu majisafu
   Mahali – nyumbani kwao
   Sababu – Kutelekeswa kwa kazi zote za kuwalinda wanao walemuvu bila usaidizi wa mumewe majisifu. (1 x 4)

(b) Utohozi – Petroli
Swali balagha : "wewe unafikiri ninatumia petrol nini? (2 x2)

(c) Migogoro

(i) Migogoro ya kindugu
Bwana mtemi na familia yake wanakinzana. Madhubuti amekuwa mwasi kwa babake. Mtemi na mkewe wanasomeana kila mara. Mtemi pia anashiriki mapenzi nje ya ndoa.
Bwana majisifu na mkewe dora vile vile wana migogoro kuhusu ulezi wa wanao vilema.

(ii) Migogoro kati ya watawal na watawaliwa
Mtemi na nduguye hawapikiki chungu kimoja. Wao wanazomeana kila mara. Hali inayowafanya wasiwasiliane ufanisi au matatizo yao.

(iii) Migogoro kati ya watawala na wataliwa
Mzee matuko weye anatiwa nguvuni kwasababu ya kumwambia mtemi wazi wazi kuwa utawala wake ni mbaya na anafua kuondoka uongozini. Mtemi anawadhuklumu wanasokomoko kwa kunyakua shamba zao kama ule la chichiri Hamadi.

(iv) Migogoro ya waajiri na waajiriwa
Mtemi Nasaba bora anawaajhiri na kufata kazi wafanya kazi wakati wowote. Akiona wanafanya kazi vyema anawapiga kalamu. Wafanyakazi wengi sokomoko wanafanya kazi za sulubu zilizo na mishahara ya kijungu jiko.

(v) Migogoro ya mashamba
Wanasokomoko na Tomoko kwa ujumla wanamlaumu mtemi kwa kuwapokonya mashamba yao. Amani hana furaha kwa sababu ya shamba lao kuchukuliwa na Bwana Mtemi.

(vi) Migogoro ya kimapenzi

Majununi na mitchelle wamekuwa na huba. Hata hivyo Mitchelle anamkataa majununi kwa kusingizia nyumba. Mashaka anaamua kutotoka shuleni kwa sababu ya mapenzi yake kuvunjika.

Mengine

(vii) Migogoro ya kinasaba
(viii) Migogoro ya kijinsia
(ix) Migogoro ya askari na wanachi
(x) migogoro ya setka katika uandishi
(xi) migogoro ya elimu

1. Wanasokomoko wanapokonywa mashamba
   Mtemi anampokoonya chichir Kamadi shamba lake la ekari mla mbili sabini. Alichukuwa shamba lake marehemu mwinyi hatika mtembezi. Na pia alipofanya kazi katika wazara ya Ardhi na makao aliweza kutendeneza hatimiliki bandia za mashamba.
2. Kuuawa na viongozi
   Mtemi aliwahonga majambazi ili waweze lumuua chichir hamadi iliaweze kuchukua shamba lake. Askari waliobimwa na mtemi walimpiga mamake Imani na kusababisha kifo chake.
3. Wanarochi wanadhulimiwa kupita ufisadi
   Mtemi pamoja na wasimamizi wanabumia pesa zilizotaliwa kujenga hsopitali kujenga zahanati na kasha kujifaidi na pesa hizo mifukuni mwao.
4. Yusuf anadhulumiwa kwa kufungwa kifungo cha maisha kwa kusingiziwa kumuua babake chichir Hamadi.
   Amani na Imani wanafungwa kwa kusingiziwa kumuua kititi uhuru.
5. Waandishi wanadhulumiwa kwa kuibiwa miswada yao kwa njia za kilaghai na watu amabo hawana vipawa. Amani anaibiwa mswada na mwalimu majisifu.
6. Wagonjwa zahanitini wanadhulumiwa kwa kutopewa huduma bora pale zahanitini. Wauguszi ni wazembe kazini, wanawadhihaki na kukejeli wanaowaleta wagonjwa wao mfano Amani na Imani wanapompeleka kitoto Uhuru.

7. Wananchi wanalazimishwa kutoa ngeje za kuwapeleka watoto wa viongozi kusomea ughaibuni. Mtemi analazimu wanasokomoko kutoa pesa za mwanake kwende kusomea ughaibuni.
8. Waajiri wanawadhulumu waajiriwa kwa kuwapa kazi za sulubu ambazo malipo yake ni ya kijingujiko. Mtemi anampiga fagio mfanyikazi wake. Amani anatanya kazi ya kukama ng'ombe nk.
9. Wakoloni wanawadhulumu waafrika walipokuwa barani Afrika. Waafrika hawakuruhusiwa kupanda mimea iletayo fadha na figuo wa gredi.
10. Vyombo vya dola vilivyochini ya utawala mbaya wa mtemi unawadhuluma watu. Askari wanawapiga na kudhulumiwa watu wasiokuwa na hatia mamake Imani anaaga kutokana na kichapo cha Askari.

1. (a)

(i) msemaji ni mzee babu
(ii) msemewa ni wanatekede
(iii) mahali kwa mzee babu
(iv) sababu walikuwa wamekusanyika kwa mzee babu ili wafumbuliwe fumba la matatizo yanayowakumba.
(4 x 1 = 4)

(b)

(i) Ni msiri – Alijua mengi lakini aliyatoa kwa njia ya hadithi mafumbo na ushairi
(ii) ni mwenye busara – Anahifadhi mavuno anyayoletewa ili kuwafaa wanakijiji hao wakati wa upungufu wa chakula.
(iii) ni mwenye mawazo mapevu – Anawambia wanakijiji kwamba si kila panapo mawingu meusi na mazito mvua hunyesha.
(iv) ni mzalendo – Anakipenda kijiji chake ndio maana anashirikiana na wenzake kutafuta suluhisho.
(za kwanza 4 x 1 = 4)

(c) Jazanda / istiara (al 1 x 2 = 2)
Mifano
Hadithi ni ya Kobe na ndege

(a) Kobe anawakilisha viongozi wenye tama na ubinafsi kama vile Bwana Mtajika. Kobe ananyakua vyote anavyopewa huko mbinguni.
(b) Kobe pia anawakilisha viongozi wanjanja na wanafiki kama vile Bwanan Mtajika na Mchupa. Kobe anajifanya mwema anachangiwa manyoya na ndege kasha anawasaliti.
(c) Kobe anaonyesha ubaguzi wa viongozi – Anakula kwanza na kuwapa ndege makombo.
(d) Kobe kuanguka ardhini ni luonyesha kuanguka kwa uongozi mbaya. Uongozi wa Bwana Mtajika unaporomoka.
(e) Ndege kumchangia Kobe manyao ni ishara ya ushirikina wa wanatekede kupinga kura na kumwezesha kupata mamlaka.
(f) Kupewa makombo kwa ndege inaonyesha dhuluma wanazopata wanyonge.
(g) Ndege kuchukua / kumnyang'a Kobe manyoa inaonyesha nguvu walizonaza wanyonge.
(zozote 5 x 2 = 10)

Ubinafsi:

- mapenzi kati ya Chritine and Peter yanalenga mahitaji yao ya kibinafsi.
- Peter aliwapunja wavuvi pesa ili ajinufaishe yeye mwenyewe akiuza samaki ghali huko ng'ambo.
- Christine anatamani kuolewa katika familia ya kitajiri. Anajiona kama ng'ombe wa kizungu kwa vile amesome.
- Chrisitne hamuulizi Peter kuhusu msichan anayetembea naye kwa kuhofia kukitia mchange kitumbua cha uhusiano wao.
- Peter aliwapenda wasichana ili kutimiza haja zake kimwili sio kuwaoa.
- Peter alijitia kuwahurumia wafanyikazi wake bure, alitaka tu wamzalishie mali.
- Peter alijitia kumpenda Zac hata akiwa na hali yake ya kimaskini ili afanyiwe kazi na aletewe wasichana.
(zozote 5 x 2 = 10)

Ushirikina

- Msoi anaamini ndoto anazoota kuwa ziliandama na matukio fulani. Ndoto zake ziliaminika kuwa za kweli.
- Msoi aliamini kuwa lazima kungekuwa na kitu kibaya amabcho kingetokea katika Baa hiyo ya Makaburini.
- Alipojikwa na bakuli lake la maua lilivunjika vipande vipande aliamini iliashivia mkosi ambao ungetokea, aliamini ilikuwa kama anakanywa.
- Kubana kidole chake mlangoni mwa gari aliamini ni onyo la kutoenda huko walikokuwa wanaenda

kwani kungetokea balaa.
- Alikuja kuichukia Baa la Makaburini kw akuwa ilikuwa karibu na makaburini au mavani Alilisi kungekuwa na mkosi.
- Akiwa kwenye baa anabadili mtindo wake wa kukaa wa kawaida anaangalia upande wa makaburini akidhani ndoto yake ingetabirika wakati wowote.
- Kutumbua macho kulionyehsa kuwa sasa mambo aliyotabiri yamewadia alipoona vizuu.
(zozte 5 x 2 = 10)

MSTAHIKI MEYA

(a) Msemaji – Waredi
Msemewa – Siki
Mahali – Zahanatini
Lini
(b) Tabaini – Ni mbinu ambayo
(c) Msemaji ni Waridi
- anashawishika kwa haraka – Anaamini yale wanayosema wanasiasa, vyombo vya habari na wasomi eti nchi yake ni maskini
- Mwenye kiburu – Anamkaripia mama Dddavue kaole kwa maneno makali bila kujali hali ya motto wake. Pia mkali / mgomvi.
- Mtiifu – Anafuata maagizo ya kutowatibu watu wasio na fedha.
- Mtamaushi – Anaamua kuacha kazi baada ya kuona kuwa mazingira na hali ya kazi hayabadiliki.
- Mbinafsi – Hakuwafikiria wagonjwa wake anapoamua kuacha kazi zahanatini.
- Ana msomamo thabiti – Anaamua kuacha kazi baada ya kuona hali mbaya ya kazi.
- Mwoga – Anaogopa anaposikia fununu za mgomo wa maandamano.
(Mwanafunzi ataje sifa na kuidhibitisha)
(Maelezo yaelekeana na sifa)

<u>Umaskini</u>

(a) Baraza haliwezi kutoa huduma bora kw awanacheneo – maji safi
- Usafi w mazingira km takataka
- Dawa zahanatini
(b) Mchi kutegemea mataifa ya kibepari kwa mikopo.
(c) Baraza kushindea kulipa mishahara kwa wakati, wanaichelewesha na hata wakati mwingine kupila nusu. Barasa limefilisishwa na wizi / ubadhirifu wa Meya na Washauri wake.
(d) Wagonjwa zahanatini hawawezi kugharimia matibabu yapo. Hawana hata karatasi za kunakilia uabalesio wao.
(e) Wafanyikazi wa Baraza kutembea kwa miguu na kwa masaa mengi kufika kazini kwani hawana nauli.
(f) Wafanyikazi wanakosa pesa za kununua chakula wala makombo kinachowadhuru.
(g) Wanakopsa pesa za kugharimia mahitaji ya kimsingi – makao, kiberiti ili kutokosa chakula.
(h) Watoto wao waugua magonjwa yasababishwayo na ukosefu wa lishe bopra – utapia – mlo
(zozote 5 x 2 = 10)

Matumizi ya mbinu ya majazi katika mstahiki Meya

(a) Bwana sosi – Kukotana na neno la kiingere za:
(i) ‘source’ – chanzu cha yeye ndiye chanzo cha matatizo mengi ya wanachenea
(ii) ‘Source” – kutia ladha. Maisha ya vibaraka wake yalipata ladha kwa kupewa mishahara ya juu na marupurupu mengine.
(iii) Aina ya msimu – ‘sosi’ unao – maarisha kula. Alikuwa mlafi. Pia alitumia cheo chake kula na kujitajirisha na mali ya wanacheneo.
(b) Mstahiki Meya - Alistahikli kuondolewa mamlakani kwa kuwatesa wananchi.
- Alistahiki kulaumiwa kwa matatizo ya wanacheneo
(c) Bwana uchumi n akazi – maswala ya kiuchumi na kazi Barazani.
(d) Bwana usalama – alishughulika na usalama.
(e) Bwanan uhusiano mwema – alihakikisha kulikuwa na uhusiano mwema baina ya cheneo na majirani / nchi za nje.
(f) Siki – Msikivu - alisikiliza sana matatizo ya wanachi
- kinwaji kikali / kinawasha ulimi – alimghasi Meya kuboresha hali za maisha za wanacheneo.

(g) Bili – Orodha ya vitu pamoja na malipo yake. Yeye ndiye aliyepanga orodha za njia za kupora baraza.
(h) Waredi – Ua linalovutia lakini linalokauka mara linapotolewa mtini.
– Anajaribu juu chini kuwapa matumaini wagonjwa zahanatini lakini ajuapo ukweli anajiuzulu ghafla.
(i) Tatu – Anajaribu juu chini kuona matatiz ya wafanyikazi yametatutliwa.
(j) Beka – Nmeo la kuitikia hasa kwa wanawake. Aliitikia wito wa kutetea maslahi ya wafanyikazi.
(k) Cheneo – Kitu kilichoenea
(l) Kajifahari – samaki mkubwa kuliko kamba
- Mkahawa mkubwa tena wa kifahari.
(m) Shuara – Mji mdogo jirani – Mambo huko yalikuwa shwari.
(n) Kheri – Ana heri yaani mwenye amani, utulizu na salama.
(zozote 10 x 2 = 20)

MTIHANI WA PAMOJA WA SHULE ZA UPILI KAUNTI NDOGO YA MWINGI YA KATI
Kenya Certificate of Secondary Education
101/1
KISWAHILI
KARATASI YA 1

INSHA YA LAZIMA

1. Kumekuwa na visa vya upiganaji wa kabila zinazozozania mifugo katika Kaunti yako. Wewe kama gavana wa kaunti hiyo watumie waathiriwa risala ukiwaeleza hatua zinazoweza kuchukuliwa kupunguza vita hivyo.
2. Hatua ya serikali kuu kumpa kila mwanafunzi wa darasa la kwanza tarakilishi ni ya manufaa sana. Jadili.
3. Andika insha inayodhihirisha methali
   Mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani
4. Anza kwa
   Walipofungua mlango huo, wengi hawakuweza kuzuia hisia zao. Walitoa kwi! kwi! kwa maafa walioshuhudia…

MTIHANI WA PAMOJA WA KAUNTI NDOGO YA MWINGI YA KATI
Kenya Certificate of Secondary Education
102/2
Karatasi ya 2
LUGHA

SEHEMU YA A : UFAHAMU (AL. 15)

1. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.

Kabla ya kuzungumzia umataifa, tuanze udadisi wetu kuhusu neno ‘upeo wa Kiswahili”. Neno upeo linaashiria mchakato au tendo linalokwenda mbele hatua kwa hatua.

Ndani ya fikra hii ya upeo tunahitaji kujiiliza kwa nini lugha fulani imekwenda harakaharaka au inasotasota katika hali fulani. Nadhani jibu la swali hili haliwezi kukwepa historia ya Kiswahili na Jamii mbalimbali za Afrika Mashariki.

Kulingana na Prof. S.A Mohammed historia au asili ya Kiswahili haijatafitiwa vyema wala kuainishwa vya kutosha kuhusu mchipuko wa asili yake. Hii ni kwa sababu utafiti na uchambuzi wa asili ya lugha ya Kiswahili mpaka sasa hauna umakinifu tokea hapo kale. Mtazamo uliotumiwa kwa wakati wote wa historia ya Kiswahili ni mtazamo wa upekee wa kuegemea taaluma moja wa ‘Atomistic Approach’ unaotumiwa katika somo la isimu miundo na isimu historian a linganishi.

Hata hivyo, lugha si vipashio tu vya ndani ya muundo wa lugha; lugha si mfumo ndani ya mifumo ya lugha.

Kwa namna hii ukosefu wa mtazamo wa pekee unabainika wazi. Kwa hivyo, somo la ziada la Isimu Jamii lazima linahitajika katika kufanya utafiti na kugundua asili ya Kiswahili na hata katika kupanua lugha kwa mtazamo na mahitaji ya lugha yenyewe katika mapana ya Jamii husika za Kiswahili zenyewe.

Hata hivyo, katika kutafuta asili ya lugha ya Kiswahili upana wa mtazamo wa pamoja si mshikamano wa Isimu Jamii tu bali mtazamo mpana zaidi unaotarajiwa kuweka pamoja taaluma kadha wa kadha. Kwa mfano inakuwaje kuitafiti asili ya lugha ya Kiswahili bila ya kuitafiti Jiografia pana na ndefu ya lugha ya Kiswahili na ulingano na mpishano wa tamaduni na maumbile ya mwingiliano baina ya mtu na mtu, watu na watu katika jumuiya mbalimbali za Kiswahili.

Au inakuwaje kutotazama uhusiano wa karibu wa kuishi pamoja katika eneo ya mwambao ya Afrika Mashariki na majirani wao wa Afrika Mashariki? Prof. Mohammed hapa anaelekea kutuambia ni vigumu kutafiti asili ya lugha ya Kiswahili. Na hata tukifanya hivyo, inakuwaje wataalamu wanakimbia u-nje wa lugha ulioko ndani ya historia ya lugha ya Kiswahili katika asili au chipukizi zake? Inakuwaje wataalamu hao kutoangalia mfumo wa maisha ya wazawa wa lugha na wale wasiokuwa wazawa wa lugha hii, ambao lugha na tamaduni zao kwa kiasi zinafanana kwa juu juu au undani zaidi?

Je, kwa nini asili ya Kiswahili haitazamwi na kulinganishwa na kutofautishwa katika Nyanja mbalimbali za taaluma kama vile Fasihi simulizi, Ufinyazi, sosholojia, Antropolojia, Historia Simuliza, Taaluma za Tamaduni za kale zinazohusiana na Mazimu, Matambiko, Harusi, Mazishi, Vitiba, Sadaka n.k.

Maswali

a. Yape makala haya anwani mwafaka
(alama 2)
b. Kwa nini historia au asili ya Kiswahili haijatafitiwa vyema kulingana na S.A Mohammed
(alama 2)
c. Je, S.A Mohammed anapendekeza mambo yapi yazingatiwe katika utafiti wa asili ya lugha ya Kiswahili

(alama 5)
d. Ni nini umuhimu wa Isimu Jamii katika utafiti wa asili ya Kiswahili
(alama 2)
e. Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika kifungu
(alama 4)
i) Inasotasota
ii) Umakinifu
iii) Isimujamii
iv) U-nje

2. UFUPISHO (ALAMA 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Dhana ya kupatalizwa tuliyo nayo haitokani na hofu ya vita na sababu za vita hazikuzushwa na Sayansi. Utaalamu huu haukuunda vita, umeukuza ujuzi wa vita na kuupotoa.

Kwanza, pasi na shaka, Sayansi imeziongeza nguvu za wachochezi wa vita. Zana za kisasa zinaweza kufisha watu wengi zaidi wasijulikane walivyokufa na kuwaua kwa njia ya manyenzi zaidi kuliko zana za zamani. Kila silaha mpya zinazoundwa ni za maangamizi zaidi, ni za kutisha sana hata kuwapa watu kusema kuwa dola zitalazimika kuacha vita kwa hofu ya uharibifu utakaowapata hata wakiwa washindi. Lakini kweli ilivyo ni kuwa hakuna taifa lililosita kuanza vita kwa kucha ati silaha lililo nazo zitaangamiza waliomo na wasiokuwemo. Kuundwa kwa marisau ya kutikisa miji iliyo mbali, kuundwa kwa makombora ya atomiki, hewa za sumu zinazopaliza na kuzuia pumzi au zinazotawanya vidudu vya maradhi au vya kuua mimea, zana zote hizi hazijazuia wala hazitazuia vita.

Lakini lawama kubwa ni ya wataalamu wa sayansi maana utaalamu wenyewe una kunga kama za wachawi na waganga. Kila mtu azicha wala hajui la kuzifanya na hao wataalamu nao wamejiziba katika kunge la kunga hizi kupagaza waja na kujifanya waungu-wa-nti (miungu wa chini). Kwa sababu ya kujiepusha hivi na watu kile kilicho kimegeuka kuwa hofu na kitisho na kila mtu ataka amwepuke mtaalamu wa Sayansi kama

anavyomwepuka mchawi na mganga. Ni juu yao kuyaondosha maoni haya na ni juu yetu sote kutoirika vita Sayansi bali tuifanye chombo cha kudumisha amani.

Maswali

(a) Kwa kuzingatia mambo muhimu, fupisha aya za kwanza mbili (maneno 50-55) (alama 9, 2 utiririko)

Matayarisho

Nakala Safi

(b) Fupisha aya ya mwisho bila kupoteza maana asilia (maneno 40-45) alama 6, 1 utiririko

Matayarisho

Nakala Safi

SEHEMU YA C: MATUMIZI YA LUGHA NA SARUFI

a) (i) Eleza tofauti kati ya Irabu na Konsonati (alama 2)

(ii) Taja sifa za sauti /0/ (alama 2)

b) Ainisha vivumishi katika sentensi ifuatayo (alama 2)

Ukuta wa nyumba ile umebomoka

c) Tunga sentensi sahihi ukitumia msemo ufuatao (alama 1)

Taka Shujaa

d) Geuza sentensi ifuatayo katika hali ya “a” (alama 1)

Mwanafunzi hula wali

e) Yakinisha sentensi ifuatayo (alama 2)

Asipofika mapema hatampata

f) (i) Eleza maana ya kihusishi (alama 2)

(ii) Ainisha vihusishi katika sentensi ifuatayo (alama 3)

a. Mama atasafiri kutoka Ujerumani hadi Ufaransa.

g) Tunga sentensi moja kutofautisha vitate vifuatavyo (alama 2)

(i) Mbali (ii) Bali

h) Changanua sentensi ifuatayo kwa jedwali (alama 4)

Nilimuona mamba majini nilipopiga mbizi.

i) Eleza sifa mbili za sauti /ng’/ (alama 2)

j) Tunga sentensi ya rai (alama 1)

k) Andika kwa wingi

Kelele ya amchaye Mungu ni Baraka (alama 2)

l) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao (alama 4)

S – S1 + U + S2

S1 (T + E + E) Lakini S2 (N + V) (T + N)

m) Tofautisha kiwakilishi nafsi huru na kiwakilishi nafsi ambata katika sentensi (alama 2)

n) Andika katika usemi halisi (alama 3)

Mwalimu aliomba kitabu cha Kiswahili

o) Tunga sentensi ukitumia mofimu huru (alama 1)

p) Andika katika ukubwa wingi

Nguo iliwekwa kando ya mlango (alama 1)

q) Ni nini maana ya chagizo (alama 1)

r) Tunga sentensi yenye kishazi huru na kishazi tegemezi (alama 2)

s) Tunga sentensi ukitumia tanakali ya sauti ifuatayo ‘tifu’ (alama 1)

SEHEMU YA D: ISIMUJAMII (ALAMA 10)

1.

(a) Eleza changamoto zinazokumba lugha ya Kiswahili
(alama 5)

(b) Jadili hatua ambazo zimechukuliwa kuimarisha lugha ya Kiswahili
(alama 5)

MTIHANI WA PAMOJA WA SHULE ZA UPILI ZA KAUNTI NDOGO YA MWINGI YA KATI
Kenya Certificate of Secondary Education
102/3
KARATASI YA 3
FASIHI YA KISWAHILI

SEHEMU A: DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE
Ken Walibora na Said A. Mohammed
Swali la Lazima

1. … Hasadiki kama yote yaliyojiri yaliyokuwa mafamba au mazingaombwe au mambo halisi. Mambo mengine yanakuwa kama ndoto au jinamizi…
(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (alama 4)
(b) Eleza mambo yote yaliyojiri
(alama 10)
(c) Fafanua sifa tatu za anayerejelewa
(alama 6)

SEHEMU B: RIWAYA
KEN WALIBORA: KIDAGAA KIMEMWOZEA
Jibu swali la 2 au la 3

2. … Huyo mwendawazimu anakuja nini kwenye sherehe hizi?
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
(b) Jadili uhusiano uliopo baina ya mzungumzaji na maudhui
(alama 6)
(c) Taja mbinu ya lugha zilizotumika katika dondoo
(alama 2)
3. (a) Mwandishi wa kidagaa kimemwozea amemulika ukiukaji wa haki za kibinadamu. Jadili. (alama 10)
(b) Eleza jinsi mbinu rejeshi imetumika katika riwaya ya kidagaa
(alama 10)

SEHEMU C: TAMTHLIA:
TIMOTHY AREGE: Mstahiki Meya
Jibu swali la 4 au la 5

4. "…Sisi tunaamini kabisa tunachokitaka ni haki yetu na ya vizazi vingine…
(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (alama 4)
(b) Haki hizi zimekiukwa vipi? (alama 10)
(c) Eleza sifa za anayezungumza (alama 6)
5. (a) Linganua wahusika wafuatao katika Tamthlia ya Mstahiki Meya
(alama 12)
(i) Mstahiki Meya
(ii) Diwani III
(b) Methali ni mojawapo wa Tamathali za lugha zilizotumika katika Tamthilia ya Mtahiki Meya. Thibitisha (alama 8)

SEHEMU YA D: USHAIRI
Jibu swali ya 6 la 7

6. Angawa mdogo, dagaa, amekomaa
Kaanga kidogo, dagaa, atakufaa
Kalia kinaya, dagaa, h'ondoa njaa

Wa kwako udogo, kijana, sio balaa
Na sio mzigo, kijana, bado wafaa
Toka kwa mtego, kijana, sinyanyapaa

Nasaha kidogo, kijana, ukubwa jaa
Jikaze kimbogo, kijana, acha kukaa
Chimbua mhogo, kijana, usibung'aa

Na wake udogo, dagaa, ndani hukaa,

Kuliko vigogo, dagaa, hajambaa
Hapati kipigo, dagaa, hauna fazaa

Maisha si mwigo, kijana ushike taa
Sihofu magego, kijana, nawe wafaa
Kazana kidogo, kijana, kugaaga

Maswali

(a) Lipe shairi hili anwani mwafaka (alama 2)
(b) Eleza arudhi zilizofuatwa katika kutunga shairi hili (alama 4)
(c) Onyesha jinsi malenga alivyotumia uhuru wake (alama 3)
(d) Tambua bahari katika shairi hili (alama 3)
(e) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari (alama 4)
(f) Tambua mbinu za lugha zilizotumika katika shairi (alama 2)
(g) Eleza toni la shairi hili (alama 2)

7.

Eti
Mimi niondoke hapa
Niondoke hapa kwangu
Nimesaki, licha ya risasi
Vitisho na mauaji, siondoki

Mimi
Siondoki
Siondoki siondoki
Niondoke hapa kwangu!
Kwa mateke hata na mikuki
Marungu na bunduki, siondoki

Hapa
Siondoki
Mimi ni Pahame!
Niondoke hapa kwangu!
Fujo na ghasia zikizuka
Na kani ya waporaji, siondoki

Haki
Siondoki
Kwangu siondoki
Niondoke hapa kwangu!
Nawaje; waje wanaokuja
Mabepari wadhalimu, siondoki

Kamwe
Siondoki
Ng'oo hapa kwangu!
Katizame chini mti ule!
Walizikwa babu zangu, siondoki

Sendi
Nende wapi?
Si hapa kitovu changu
Niondoke hapa kwangu

Wangawa na vijikaratasi
Si kwamba hapa si kwangu, siondoki

Katu
Siondoki
Sihitaji karatasi
Niondoke hapa kwangu
Yangu mimi ni ardhi hii
Wala si makaratasi, siondoki

Maswali

a) Shairi hili ni la aina gani? Kwa nini (alama 2)
b) Taja masaibu anayopitia mzungumzaji (alama 4)
c) Eleza toni ya shairi hili (alama 2)
d) Eleza muundo wa shairi hili (alama 3)
e) Tambua matumizi ya mbinu ya usambamba (alama 2)
f) Andika ubeti wa tano kwa lugha nathari (alama 4)
g) Tambua idhini moja ya mtunzi (alama 1)
h) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi (alama 2)
   (i) Karatasi
   (ii) Nimesaki

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

8. (a) Ni nini maana ya ulumbi (alama 2)
   (b) Eleza sifa za mtendaji katika ulumbi (alama 8)
   (c) Ngomezi zina umuhimu upi katika Jamii (alama 8)
   (d) Toa mifano miwili ya ngomezi (alama 2)

MTIHANI WA PAMOJA WA SHULE ZA UPILI KAUNTI NDOGO YA MWINGI YA KATI
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
102/1
KISWAHILI

KARATASI YA KWANZA
INSHA

1. Risala

Hii ni insha ya Risala. Insha hii iwe na muundo ufuatao: -

i) Iwe na anwani ya mwandishi
ii) Iwe na mada ambayo itaandikwa kwa herufi kubwa na kupigiwa msitari
iii) Mtajo lazima uwepo
iv) Hitimisho iwe inaonyesha msimamo wa anayotuma Risala. Kisha ihitimishwe kwa jina la mwandishi na sahihi huandikwa. Pia cheo cha anayeandika.

Baadhi ya hoja ni: -

- Dini, wahubiri amani na utangamano wa kikabila
- Kuchagua viongozi waadilifu
- Kuhubiri umoja wa makabila
- Kuhimiza ndoa kati ya kabila mbalimbali
- Ugavi sawa wa rasilmali
- Kulinda mali asili za kabila mbalimbali
- Michezo katika makabila mbalimbali
- Kuhimiza uzalendo na utaifa

- Kuepukana na uongozi na viongozi wa kikabila
- Kuacha tamaduni zinazohubiri chuki/mgambo wa kikabila

Zozote 6 x 2 = 12
Muundo alama = 4
Lugha = 4
Jumla = 20

2. SWALI LA PILI

Manufaa

i) Tarakilishi itarahisisha ufunzaji wa masomo mbalimbali kwa upande wa mwalimu
ii) Itakuza na kuimarisha ubunifu miongoni mwa wanafunzi
iii) Hatua hii itamtanguliza mapema mwanafunzi katika ulimwengu wa tarakilishi na teknohama.
iv) Itasahihisha kuelewa haraka wa masomo kwa kurahisisha mada ngumu katika silibasi kwa mwanafunzi
v) Itaboresha matokeo ya mitihani kwa wanafunzi husika.
vi) Itaimarisha Uchumi wa watengenezaji wa tarakilishi na programu.
vii) Zitatumika katika utafiti
viii) Zitapunguza mzigo kwa wanafunzi wa kubeba vitabu vingi

Hasara

i) Ni ghali kutekeleza – itahitaji fedha nyingi
ii) Bila kuwepo kwa walimu walio na umilisi wa kutosha wa kompyuta, hatua hiyo haitakuwa na manufaa
iii) Kutakuwa na tatizo la usalama wa wanafunzi na tarakilishi zenyewe.
iv) Baadhi ya shule hazina miundo-msingi ya kutekeleza masomo kwa tarakilishi k.v. kawi na madarasa.
v) Zisipodhibitiwa, tarakilishi zitaweza kusababisha utovu wa maadili kwa wanafunzi kupitia mitandao

(hoja 5 katika kila upande)

Tanbihi

- Hii ni insha ya mjadala
- Iwe na upande wa kuunga na ule wa kupinga
- Katika hitimisho mwandishi aonyeshe msimamo wake

3. Methali

Mwanafunzi aandike kisa kitakacholenga maana ya methali hii kuwa anayekwenda nyuma na mbele ya jahazi huishia katikati ya chombo hicho. Hii ina maana kuwa enda uendako na kokote utakako lakini ukiwa bado u hai utarudi kwenu ulikotoka tu.

4.

- Hii ni insha ya mdokezo
- Lazima mwanafunzi aanze kwa maneno ya mdokezo
- Kisa kilenge mkasa wowote ule mfano:
- Uvamizi
- Kisa cha kujitoa uhai
- Ubakaji

MTIHANI WA PAMOJA WA SHULE ZA UPILI KAUNTI NDOGO YA MWINGI YA KATI
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
102/2
KARATASI YA 2 - LUGHA
MAJIBU YA UFAHAMU

(a) Upeo wa Kiswahili, Kiswahili, Historia ya Kiswahili n.k. (Mwalimu akadirie jibu) (1 x 2) Al. 2
(b) (i) Utafiti na uchambuzi hauna umakinifu
(ii) Mtazamo uliotumiwa unaegemea taaluma moja tu (2 x 1) Al. 2
(c) (i) Kutafiti jiografia pana na ndefu ya lugha ya Kiswahili
(ii) Kutazama uhusiano wa karibu wa kuishi pamoja
(iii) Kutazama u-nje wa lugha ulioko ndani ya historia ya lugha ya Kiswahili
(iv) Kuangalia mfumo wa maisha ya wazawa wa lugha na wasiokuwa wazawa.
(v) Kutazama na kutofautisha Nyanja mbalimbali za taaluma (Al. 5 x 1)

(d) Katika kupanua lugha kwa mtazamo na mahitaji ya lugha yenyewe katika lugha yenyewe (Al. 2)
(e) (i) Inasotasota – Polepole au kukweta
(ii) Umakinifu – Uzingatifu
(iii) Isimu Jami – Uhusiano wa lugha na Jamii
(iv) U-nje – Sifa za kawaida za lugha (Al. 4)

2. **UFUPISHO**

(a) (i) Dhana ya kupatilizwa inatokana na hofu ya vita
(ii) Sababu za vita hazikuzushwa na Sayansi
(iii) Sayansi imekuza ujuzi wa vita na kuupotoa
(iv) Imeziongeza nguvu za wachochezi wa vita
(v) Zana za kisasa zinaweza kufisha watu wengi
(vi) Hakuna taifa lililosita kuanza vita kwa hofu ya maangamizi
(vii) Uundwaji wa silaha hatari hautazuia vita (hoja 7)
(b) (i) Lawama ni kwa wataalamu wa Sayansi
(ii) Wamejiziba katika kunge za kupagaza waja na kujifanya waongo duniani
(iii) Kila mtu ataka awaepuke kwa hofu
(iv) Ni juu yao kuyaondosha maoni haya
(v) Tuifanye sayansi chombo cha kudumisha amani (hoja 5)

3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)

(a) (i) Wakati wa kutamka konsonanti sauti hubanwa ilhali katika kutamka irabu sauti haibanwi (1 x 2 = 2)
(ii) Sifa za sauti /0/
– Ni sauti ya kati
– Hutamkiwa nyuma ya ulimi
– Inapotamkwa midomo huwa imeviringwa (Zozote 2)
(b) Vivumishi
(i) Wa – Kivumishi cha 'a' – unganifu
(ii) Ile – Kivumishi kionyeshi (2 x1 = 2)
(c) Kutunga sentensi
Taka shufaa – Omba msamaha kwa kosa fulani
mf: Mirriam alimtaka shufaa rafiki yake kwa maudhi aliyomfanyia (1x1 = 1)
(d) Hali ya 'a'
Mwanafunzi hula wali – Mwanafunzi ala wali (1 x 1 = 1)
(e) Kukanusha
Asipofika mapema hatampata – Akifika mapema atampata (2 x 1 = 2)
(f) (i) Maana ya kihusishi – Ni neno linaloonyesha uhusiano baina ya neno na lingine au kati ya kundi la maneno na lingine (1 x 2 = 2)
(ii) Kuanisha vihusishi
Kutoka – Mahali
Hadi – Mahali (2 x 1 = 2)
(g) Kutunga sentensi
Mbali – tofauti
Bali – Kasoro (2 x 2 = 2)
Mwalimu akadirie jibu
(h)

S √ ½				
KN √ ½	KT √ ½			
√ ½	T √ ½	N √ ½	E √ ½	S √ ½
	Nilimwona	Mamba	Majini	Nilipopiga mbizi

Alama ½ x 8 = 4
(i) Sifa za sauti /ng'/
– Ni king'ong'o

– Si ghuna (1 x 2 = 2)

(j) Sentensi ya rai
Mwalimu akadirie jibu
Mwanafunzi atumie maneno kama vile
Naomba, tafachali, nisaidie, nakusihi n.k
Asitumie Nipe

(k) Wingi

Kelele	Za	Wamchao		Mungu	ni	Baraka
½	½	½	½		(4 x ½)	= 2)

(l) Kutunga kupitia muundo

mf: Alifika √ ½ mapema √ ½ sana √ ½ lakini mwalimu √ ½ wake √ ½ akamchapa √ ½ viboko √ ½ (alama 4)

(m) Tofauti kati ya kiwakilishi nafsi huru na nafsi ambata
Nafsi huru – Maneno kamili yanayotumika badala ya majina ya watu
Nafsi ambata – Viambishi vinavyoambishwa kwenye mizizi ya vitenzi ili kuwakilisha mtenda

(n) Usemi halisi

√ ½
" N aomba kitabu cha Kiswahili," Mwalimu alisema. ½ √ (6 x ½) (alama 3)
√ ½ √ ½ √ ½ √ ½

(o) Mofimu huru
Inayojisimamia kimaana mf: mtu, kalamu, bora nk. (1 x 1 = alama 1)

(p) Ukubwa – Wingi
Maguo yaliwekwa kando ya malango (2 x ½ = alama 1)

(q) Maana ya chagizo
Neno au maneno katika sentensi yanayotoa taarifa kuhusu kiarifa (kitenzi) al. 1

(r) Vishazi
Mg: mwanafunzi ataenda shuleni ingawa ana mafua
Mwanafunzi ataenda shuleni – kishazi huru
Ingawa ana mafua – Kishazi tegemezi) 2 x 1 = alama 2)

(s) Tanakali ya sauti tifu – kuanguka mchangani
Mwalimu akadirie jibu (1 x 1 = al. 1)

4. ISIMU JAMII

(a) Changamoto zinazoikabili lugha ya Kiswahili
– Hakuna sera maalum kutoka kwa serikali
– Kuna uhaba Mwingi/mkubwa wa waandishi
– Kuzuka kwa lugha ya sheng' ambayo ni maarufu miongoni mwa vijana
– Imani potovu kuwa lugha ya Kiswahili ni duni
– Kuzuka kwa lugha zingine k.v Kifaransa, Kiingereza
– Watumizi wa Kiswahili hawajali jinsi ya kutumia lugha
– Ukosefu wa fedha za kufanya utafiti wa kina wa somo la Kiswahili
(Zozote 5 x 1 al. 5)

(b) Hatua za kuimarisha lugha ya Kiswahili
– Lugha ya Kiswahili imeteuliwa kuwa lugha ya taifa
– Hutumika katika matangazo na taarifa za habari kupitia runinga
– Viongozi wa dini wanahubiri wakitumia lugha ya Kiswahii
– Kenya na Tanzania zimeunda mabaraza ya vyama mbalimbali vya kushughulikia maenezi k.v CHAKITA na BAKITA
– Lugha hii imetumiwa na wanabiashara
– Lugha hii hufunzwa katika shule na vyuo
– Shughuli za sanaa, maonyesho na muziki
– Uchapishaji wa vitabu *(Zozote 5 x 1 = alama 5)*

MTIHANI WA PAMOJA WA SHULE ZA UPILI
KAUNTI NDOGO YA MWINGI YA KATI
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
102/3
KARATASI YA TATU
FASIHI
HADITHI FUPI - Damu nyeusi na Hadithi nyingine

(a) Maneno haya ni ya mwandishi anamrejelea Fikirini. Ni baada ya Fikirini kupata kisanga cha kudanganywa na kuibiwa na Fiona kisha kuachiliwa na kuonywa asirudi huko tona. Baadaye anarudishiwa vitu vyake na kwenda chuoni.

(b) Mwanafunzi arejelee shida zote alizopata fikirini alipoenda ulaya kusomea huko. Baadhi ya majibu ni:

- Mhadhiri mzungu na wanafunzi darasani walikuwa wanamsaili maswali ya kumdhalilisha
- Alitozwa faini na polisi mzungu kwa kuvuka barabara huku taa za kuelekeza magari zimewaka rangi nyekundu
- Wahadhiri walitoa alama kwa kupendelea watu weupe na kukandamiza watu weusi
- Mama mzungu anapigia polisi simu anapoona hajafunga zipu ya suruali
- Dereva mzungu anapomwona Fikirini alijipurukusha kana kwamba hamna kituo rasmi pale na kumwacha.
- Fiona anamdanganya na kumpeleka Fikirini nyumbani kwake
- Fiona anamtaka Fikirini wafanye ngono naye
- Anamfungia kwa nyumba na kumwitia Bob anapoghairi kufanya mapenzi
- Anaamrishwa kuvua nguo zote
- Anatishiwa kuuliwa kwa kisu na pia anaelekezwa mtutu wa bunduki
- Ananyang'anywa pesa zote na stakabadhi zake ingawa zilirejeshwa baadaye

Zozote tano 5 x 2 = 10
(Taz: mwanafunzi anaweza rejelea kisa cha Fikirini na Fiona au matatizo yote yaliyomkumba)

(c) Sifa za Fikirini

- Ni mwenye bidii - Anajibidiisha kutafuta elimu ya juu marekani licha ya changamoto ambazo zinamkabili katika chuo kikuu. Anapoachwa na gari anaamua kwenda chuoni kwa miguu.
- Ni mvumilivu - Anapotukanwa, kudhalilishwa na kudunishwa na wanafunzi na wahadhiri wazungu anayavumilia matusi na kuendelea na elimu.
- Ni mwadilifu - Anakataa kufanya mapenzi na Fiona licha ya kutishiwa
- Ni mtiifu - Anatii yote anayoamrishwa na Bob na Fiona
- Ni mwenye kushawishika haraka. Anashawishika haraka kuundamana na Fiona (3 x 2) Mwalimu akubali hoja nyingine ya ukweli

2. RIWAYA: KIDAGAA KIMEMWOZEA

(a) Muktadha
Haya ni maneno ya mashaka akijizungumzia mwenyewe baada ya kukutana na matuko weye anapokuwa akienda msalani kuisoma barua aliyopewa na Ben Bella katika uwanja wa Uhuru.
(alama 4)

(b) Umuhimu wa Mashaka

- Ametumika kutahadharisha watu kuhusu kuwacheka vilema
- Ametumika kuonyesha umuhimu wa masomo/elimu kwa wanafunzi na umuhimu wa kutia bidii
- Ametumika vile vile kuwatahadharisha vijana dhidi ya kujiingiza katika mapenzi kabla ya ndoa.
- Ametumika kuonyesha, kuifichua hali ya kutowajibika kwa mwalimu majisufu ambaye hahudhuni vipindi shuleni
- Anaonyesha umuhimu wa kuwapa vijana uhuru.

(c) Umuhimu wa anayerejelewa
Anayerejelewa ni matuko weye

- Ametumika kufafanua/kueleza umuhimu wa uongozi bora
- Anaonyesha athari za umaskini katika Jamii
- Anaonyesha jinsi viongozi wanavyotepetea kazini kwani anadhalilishwa na kukosa kushughulikiwa
- Anaufichua uozo katika uongozi na kuonyesha kuwa viongozi wanaendeleza ukoloni mamboleo
- Ni kielelezo cha utetezi wa wananchi
- Anaonyesha umuhimu wa ucheshi

- Ametumika kuwazindua wananchi kuhusiana na haki zao
- Ametumika kueleza maswala ya ukoloni
- Mkongwe na dhuluma za wakoloni

(d) Mbinu za lugha

- Uzungumzi nafsia
- Maswali ya balagha

3. Ukiukaji wa haki za kibinadamu

1. Ajira kwa watoto (Mf: DJ)
2. Amani kudhulumiwa na Mtemi Nasaba Bora
3. Mshahara duni mf Amani na Imani
4. Ukosefu wa Elimu mf. D.J. Imani
5. Mateso (Imani na Amani kwenye seli pia matuko weye
6. Kupokonywa mali (familia ya Imani)
7. Kupuuzwa kwa chweche makweche baada ya kuumia
8. Mauaji (enzi za ukoloni)
9. Haki ya mapenzi (Bi. Zuhara)
10. Kupuuzwa kwa wagonjwa kwenye zahanati unaosababisha vifo (uhuru)

3b.

- Mwandishi anarejelea kisa cha Majununi alivyojenga nyumba mara tatu baada ya vita vya Dunia. Baadaye ilichukuliwa na mtemi Nasaba Bora. Kisa hiki kinaonyesha ujinga wa Major Noon.
- Imani alikumbuka alivyokutana na Amani mara ya kwanza karibu na ziwa Mawewa. Umuhimu wa kisa hiki ni kuwa Imani hakujiua.
- Baada ya Amani kukiokota kitoto, anarejelea kisa cha Fao. Kisa hiki kinaonyesha uvunjivu wa maadili katika Jamii
- Mtemi Nasaba Bora anapompata Amani chumbani na mkewe, anakumbuka jinsi mkewe alimpungia Amani mkono walipompita wakitoka kwenye sherehe za uhuru, jinsi alivyomtetea akiwa seli na hata anavyomtetea nyumbani. Umuhimu ni kumulika kinaya kilichopo
- Kisa cha familia ya Imani ilivyodhulumiwa kimetolewa kwa njia ya urejeshi
- Kisa cha msichana mlemavu mrembo aliyokuwa kwenye matwana na Nasaba Bora kimerejelewa wakati wa usimulizi
- Kisa cha DJ kufungwa katika jela ya watoto na alivyotoroka kimerejelewa kwa njia hii
- Kisa kilichopelekea maji ya kiberenge kutonywewa kimeelezwa kwa njia hii

Tanbihi: Mtahini lazima ataje wakati na mahali pa tukio katika kila jibu. Hoja hizi ni mwongozo tu. Mwalimu akubali hoja zingine za kweli Zozote 5 x 2 = 10

4

a) Maneno haya ni ya Medi (√1) , akiwaeleza Meya, Tatu (√1) na Beka… walipokuwa ofisini (√1) mwa Meya. Walikuwa wameenda (√1) kumweleza Meya matatizo wafanyakazi wanayoyapitia. (4 x 1)

b)

1. Mishahara duni
2. Vitisho (watafutwa kazi)
   Mazingira duni (wanaosha vyuo bila glavu na ukosefu wa maji
3. Wananyimwa uhuru wa kujieleza (wanapoandamana wanatawanywa na askari
4. Wanadanganywa kuwa dawa zitafika (Daktari siki na waridi)
5. Viongozi hawayasikilizi malalamishi yao (Meya anadai hakuna pesa)
6. Kutolipwa mishahara kwa wakati unaofaa
7. Kukosa kuhusishwa katika vikao vya maamuzi (wawakilishi hawahusishwi na pia Diwani III

c)

1. Jasiri - anamwambia Meya wao wanapata mishahara mikubwa huku wafanyikazi wakiumia
2. Mwajibikaji - Anataka kuona matakwa ya wafanyikazi yameshughulikiwa
3. Mwenye msimamo dhabiti - Halegezi kamba hadi aone maslahi ya wafanyikazi yameshughulikiwa
4. Ni mjanja - Anapanga mgomo unaofaa

5a.

Mstahiki Meya	Diwani III
Yeye ni katili - Anaidhinisha nyongeza ya mishahara kwa madiwani pekee	Mwenye utu - Anawajali wanacheneo
Mwoga - Anaogopa anapoelezwa kuwa mgomo ungekuwepo	Jasiri - Anamweleza Meya ukweli kuwa wafanyakazi ni muhimu
Fisadi - Anashirikiana na Bili kulifisidi baraza	Mwadalifu - Hashirikiani na madiwani wengine katika njama za kifisadi
Mwenye tamaa - Anatumia mali ya baraza la mji kwa manufaa yake	Mtetezi - Anatetea haki za wanacheneo kwa kumshauri Meya kuwaongeza mshahara
Msaliti - Amepewa uwezo wa kuwa kiongozi lakini hawashughulikii, anatumia nafasi hiyo kujinufaisha	Mwaminifu - Ni mwaminifu kwa wananchi waliomchagua. Anatoa ushauri unaofaa kwa Meya
Mwenye mtazamo finyu. Anakosa kuzingatia mpango wa kimaendeleo wa miaka kumi unaofaidi cheneo	Mshauri mwema- Anaonya kamati ya baraza dhidi ya kufanya maamuzi yenye madhara makubwa kwa baraza

5.b.

- Waridi anasema kuwa, “Haraka haraka haina baraka’ Kuhusiana na kuwasili kwa dawa. Anapendekeza kwamba wagonjwa wawe na subira kulikuwa na tetesi kuwa dawa zilikuwa karibu kuwasili
- Dkt. Siki anamwomba Waridi kuwapa wagonjwa tumaini kwani, ganga ganga za mganga huleta tumaini
- Meya anamwambia Bili kuwa, “mazoea yana taabu” uk 26. Hii ni kuhusiana na jinsi walivyozoea kukutana na kushirikiana katika mambo mengi
- Bili anamwambia Meya kuwa, mtumwa hauawi. Hii ni kuhusu uamuzi wa Meya kumlipa mwanakandarasi kwa niaba ya baraza
- Bili anamwambia Meya kuwa kelele za chura hazimzuii ng’ombe kunywa maji kuhusiana na kelele za wafanyikazi wanaoandamana
- Diwani III anaambiana na Siki kuwa lililoandikwa halifutiki kuhusu kukutana kwao siku hiyo. Mkutano wao haukuwa na budi kufanyika
- Diwani III anamwambia Siki kuwa sikio la kufa halisikii dawa kwani Diwani anamshauri Meya lakini Meya anampuuza. Hali inapokuwa mbaya anajuta kwa kutomsikiliza diwani huyu
- Daktari Siki anamwambia Tatu kuwa watahadhari na mgomo wao kwani ni ‘heri nusu shari kuliko shari kamili. Siki anajua kuwa migomo inaweza kuwa na madhara makubwa kwa baraza juu ya matatizo yaliyoko tayari

6. (a) Dagaa au Kijana (1 x 2)
   (b) Kuna urari wa vina
   - Lina beti tano
   - Mishororo mitatu katika kila ubeti
   - Lina pande tatu katika kila mshororo (4 x 1)

   (c) Matumizi ya lahaja mf. Magego – Meno
   Inkisari – h’ondoa – huondoa
   Kuburoga sarufi – Na wake udogo – Na udogo wake (3 x 1)
   (d) Ukara – Vina vya utao na mwandamizi havitiririki, vya ukwapi vinatiririka.
   Ukawafi – Pande tatu
   Tathlitha – Mishororo tatu katika kila ubeti (3 x 1)

(e) Kijana nakupa mawaidha ya kwamba aliye cheoni kuhusishwa na makosa yote, kwa hivyo tia bidii afanyavyo mbogo uache kukaa. Chimbua mihogo utafute riziki (al. 4)

(f) Istiari / jazanda mf Jikaze kimbogo
Methali – mf ukubwa jaa
Msemo mf shika taa (kuwa mwangaza) (2 x 1) taja na kutoa mfano

(g) Toni ya matumaini
Toni ya kuhimizi
Toni ya kuonya (2 x 1)

USHAIRI

7

a. - Ni shairi huru kwa sababu mshairi ametumia (i) mishata mf. katu, eti, niondoke
- Shairi lina umbo la paa la nyumba
- Matumizi ya alama za uakifishaji kwa wingi (al. 2)

b. (i) Anatishwa kwa risasi
(ii) Kupigwa mateke na mikuki
(iii) Kuponda mali yake
(iv) Kuletewa hatimiliki bandia *(mwalimu akubali hoja nyingine yoyote)* Al. 4

c. (i) Huzuni
(ii) Ujasiri (2 x 1)

d. Shairi lina beti saba
Kila ubeti una mishororo sita
Lina umbo la paa la nyumba (3 x 1)

e. Usambamba – Ni urudiaji wa kiwango cha sentensi, kirai (n.k)
mf. (i) Niondoke, mimi niondoke hapa, niondoke hapa kwangu
(ii) Siondoki, siondoki, siondoki niondoke hapa kwangu (2 x 1)

f. Mshairi anasema kamwe hatoki kwake. Anaashiria chini ya mti waliozikwa babu zake na kusisitiza kwamba hawezi akaondoka (al. 3)

g. Inkisari – (i) Sendi – Siendi (ii) Nende wapi – Niende wapi (iii) Kuboroga sarufi mf yangu mimi ni ardhi hii – Ardhi hii ni yangu mimi (1 x 1)

h. Karatasi – Hati miliki
Nimesaki – Nimebaki
Kitovu – Asili (al. 3 x 1)

8. a. Ulumbi ni uhodari wa kutumia lugha kwa ufundi wa kipekee (al. 2)
b. Sifa za mlumbi

1. Hutumia lugha kwa njia inayovutia na kushawishi hadhira
2. Mulumbi huwa jasiri (huhitaji kuwa mkakamavu)
3. Hutumia chuku kwa ufanifu mkubwa
4. Anapaswa kutumia vipengele anwani vya lugha kama shairi, methali, nahau, taswira nk.
5. Hutumia lugha kutegemea muktadha na hadhira yake
6. Huwa na kipawa cha kuwa viongozi katika Jamii (4 x 2)

c. Umuhimu wa Ngomezi

- Ni njia ya kupitisha ujumbe wa dharura katika Jamii mf. vita
- Ni kitambulisho cha Jamii
- Huhifadhi na kuendeleza utamaduni wa Jamii
- Hukuza uzalendo (wanajamii huionea fahari mbinu hii ya kuwasiliana
- Hukuza ubunifu (jinsi wanajamii wanavyokabiliwa na aina tofauti tofauti za ujumbe ndivyo wanavyojifunza mitindo mipya
- njia rahisi ya kuwasilisha ujumbe (4 x 2)

d. (i) Toni katika rununu
(ii) Kamsa/milio kwenye magari mf. ambulensi
(iii) Kengele (2 x 1)

TATHMINI YA PAMOJA YA KAMDARA
Kenya Certificate of Secondary Education
102/1
KISWAHILI
KARATASI YA 1
INSHA

1. **Lazima**
   Ukiwa katibu katika wizara ya elimu, uliongozakamatiyakufanyauchunguzikuhusu visa vya udanganyifu katika mitihani ya kitaifa na jinsi ya kukabiliana na changamoto hii. Andika ripoti utakayowasilisha.
2. Wananchi ndio wakulaumiwa kutokana na kuzorota kwa usalama nchini Kenya. Jadili.
3. Andika kisa kitakacho dhihirisha maana ya methali: usipoziba ufa, utajenga ukuta.
4. Andika kisa kinacho mlizikia kwa maneno haya; ……katu siwezi kuusahau usaliti na aibu aliyoniletea.

TATHMINI YA PAMOJA YA KAMDARA
CHETI CHA KUHITIMU KISOMO CHA SEKONDARI KENYA [KCSE]
102/2
KISWAHILI
[LUGHA]
SWALI LA KWANZA: UFAHAMU (ALAMA 15)

Hulka ya binadamu katika maisha yake ni matarajio ya kupata mambo mazuri zaidi kwa kadiri anavyozidi kuishi duniani. Hulka hiyo haiepukiki kwa mtu yeyote ilimradi yungali hai duniani.

Wapo watu wanaofanya kazi kufa na kupona ili kubadili maisha yao au kujiletea hali, watu hawa matumaini yao ni kuona wanaishi vizuri zaidi kesho kuliko walivyoishi jana.

Kadhalika wavivu nao ambao wana tabia ya kutopenda kujishughulisha kutafuta maisha, mawazo yao yanabaki palepale kutarajia maisha bora. Mtazamo huo wa matarajio ya maisha bora uko pia kwa vyombo vyenye dhamana kwa maisha ya watu katika jamii kama vile serikali. Tofauti na mtu binafsi, ambaye huota ndoto hizo peke yake, serikali hushirikisha mipango inayojiwekea ya kuleta hali bora katika jamii, inafanikiwa.

Ndani ya serikali kuna wadau (washika dau) mbalimbali wenye majukumu ya kuhakikisha kuwa mipango inayowekwa inasimamiwa na kutekelezwa katika muda unaotakiwa, ili kukidhi haja ya kuleta maendeleo katika jamii, tofauti na mtu binafsi ambaye wakati mwingine husimama peke yake katika kutekeleza malengo yake hayo.

Serikali ina nafasi nzuri ya kutekeleza malengo kwa kutumia rasilimali zake wakiwemo watu, madini, misitu, ardhi na nyingine nyingi. Matumizi haya ya rasilimali katika kuleta maendeleo, ni jambo muhimu sana katika kutekeleza mipango yake. Kuna sababu kadha zinazotufanya tuishi miaka nenda miaka rudi tukiwa na kiu ya maendeleo na ndoto ambazo zinashindwa kutimia.

Tatizo kubwa lililopo ni kwamba pamoja na kuwa na wataalamu wazuri na sera nzuri, tumeshindwa kuzitekeleza, badala yake tumekuwa mabingwa zaidi wa kuelezea sababu za kushindwa kutekeleza sera hizo kuliko kujikosoa kwa uzembe unaotufanya na kusababisha kushindwa kutekelezwa kwa sera hizo. Jambo hilo limechangia kurudisha nyuma maendeleo ya nchi yetu kwa miaka mingi. Mipango mingi inayopangwa na serikali, mara nyingi imekwama, matokeo yake badala ya kutafuta udhaifu uliokwamiza kutekelezwa kwa mipango hiyo, nguvu zaidi zinaelekezwa kuhalalisha sababu za kushindwa.

Tunapaswa kujiuliza ni kwa nini tumefikia hapo? Tukipata jibu tukae chini tusioneane aibu, tunyosheane vidole usoni. Tusioneane haya katika kuleta maendeleo.

(Kutoka gazeti la Majira, Oktoba 31, 2003)

Maswali

a) Upe ufahamu huu anwani mwafaka.
   (alama 1)
b) Binadamu wote wana hulka moja. Ifafanue.
   (alama 2)
c) Eleza jinsi serikali ilivyo na uwezo wa kutekeleza ndoto zake (alama 3)
d) Kulingana na taarifa, ni kwa nini serikali hushindwa kuzitekeleza sera zake
   (alama 2)

e) Mwandishi anatoa wito gani katika aya ya mwisho?
(alama 2)

f) Andika methali mbili zinazohusiana na aya mbili za mwisho. (alama 2)

g) Eleza maana ya vifungu vifuatavyo kwa mujibu wa taarifa.
(alama 3)
(i) Kukidhi haja
(ii) Kiu ya maendeleo
iii) Tunyosheane vidole usoni

SWALI LA PILI: MUHTASARI (Alama 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.

UFUPISHO

Katiba mpya imeipa lugha ya Kiswahili hadhi nyingine kuifanya kuwa lugha rasmi kando na kuwa ni lugha ya taifa. Mabadiliko haya muhimu yana changamoto kadhaa.

Kwanza kabisa lugha ya Kiswahili sasa itashindania nafasi sawa na ile ya Kiingereza katika shughuli za kikazi. Swala hapa linahusu majukumu ambayo lugha hizi zitatekeleza. Je, lugha hizi zinatumika mtawalia katika shughuli za kikazi au zitatengewa majukumu maalum?
Lugha ya Kiswahili itachukua nafasi ipi? Kiingereza kitaachiwa nani tukizingatia kuwa kwa muda mrefu lugha ya Kiingereza ndiyo imekuwa lugha tawala katika mazingira haya? Je, wananchi wataweza kufanya maombi kwa lugha ya Kiswahili kando na kuendesha mawasiliano ya kiofisi kwa lugha hii? Kwa kifupi ili kusitokee mgongano wa matumizi ya lugha hizi mbili ni muhimu sana kwa watunga - sera kueleza kinagaubaga mawanda ya matumizi ya lugha hizi mbili katika mazingira ya kikazi.

Changamoto nyingine na muhimu ni kiwango cha maandalizi ya wananchi katika kuyapokea mabadiliko haya. Kwanza, wananchi wanafaa wafahamishwe kuhusu haki yao ya kutumia lugha hii katika mazingira ya kazi. Si ajabu kuwa wao hawana habari kuhusu mabadiliko haya ya kisera. Watumishi wa umma nao wanastahili kupewa mafunzo maalumu kuhusu mbinu za mawasiliano katika Kiswahili ili waendeshe shughuli zao vizuri.

Kwa upande mwingine, vyuo vikuu pamoja na taasisi nyingine za mafunzo zinastahili kutoa kozi ya lazima katika lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wanaojiunga nazo ili kuwaandaa kwa mahitaji haya mapya ya kikatiba. Kadhalika, serikali inastahili kuwaandaa wataalamu zaidi wa lugha ya Kiswahili ambao watahusika katika kuwafunza wanaohusika na utekelezaji sera.

Kuna haja pia ya wataalamu wa lugha kuandika vitabu zaidi kwa lugha ya Kiswahili ambavyo vitatoa mafunzo kuhusu mbinu mbalimbali za mawasiliano. Shughuli hii iambatane na ile ya kutafsiri vitabu vilivyoandikwa kwa lugha nyingine kwa ile ya Kiswahili.
Kwa muda mrefu sasa, kumekuwa na tatizo la mitazamo hasi miongoni mwa wananchi kwa lugha ya Kiswahili. Baadhi ya wananchi wamekuwa na sababu zao za kutoitumia lugha hii wakishikilia kuwa lugha yenyewe ni ngumu.

Aidha, wananchi wengine wamekuwa na uzoefu wa kuzungumza lugha ya kiingereza au lugha nyingine za kigeni huku wakitoa nafasi finyu kwa lugha ya Kiswahili. Serikali Inastahili kutafuta njia ya kuwahimiza wananchi wote kuionea fahari lugha ya Kiswahili, waipende na kuielewa vizuri.

Ni muhimu kufanywe kila juhudi kuhakikisha kuwa wananchi wanatumia Kiswahili sanifu ili wasije wakakivuruga kwa kukiendeleza visivyo au kwa kukiharibu kwa kijilugha cha sheng au kwa lugha za kienyeji.

Vile vile, ni muhimu wananchi watambue kuwa nchi yetu ya Kenya ndiyo kitovu cha lugha hii na hivyo basi wafanye kila juhudi kuitumia ipasavyo ili tusionekane kuwa watumwa katika lugha yetu asili. Tunahitaji viongozi vielelezo nchini ambao wanazungumza Kiswahili sanifu kwa madoido na ufasaha sio tu katika ulingo bali pia katika nyanja nyingine za maisha.

Kwa hivyo viongozi wetu wajiepushe na matumizi ya Kiswahili chapwa ili wananchi wahimizike kuzungumza Kiswahili kwa ufasaha. Ingekuwa hata bora ikiwa wangepewa kipaumbele katika kupokea mafunzo kabambe katika lugha hii. Pengine tungejifunza mengi kutoka nchi jirani ya Tanzania ambayo

kwa kiasi kikubwa ilifaulu kurasmisha Kiswahili na kuleta umoja wa kitaifa.

MASWALI

a) Fafanua changamoto zinazoikumba lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi. (Maneno 70) (alama 6, 1 mtiririko)
Matayarisho.
Jibu

b) Mwandishi ametoa mapendekezo kuhusu namna ya kuimarisha matumizi ya Kiswahili nchini. Yafafanue. (Maneno 80) (alama 7, 1 mtiririko)
Matayarisho
Jibu

MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)

(a) Andika vigezo vitatu vinavyotumiwa katika kuainisha irabu (alama 3)

(b) (i) Eleza maana ya mofimu. (alama 2)
(ii) Toa mfano mmoja mmoja wa mofimu huru na mofimu tegemezi. (alama 2)

(c) Kwa kutoa mifano onyesha majukumu manne ya viambishi awali. (alama 2)

(d) Tunga sentensi ukitumia nomino katika ngeli ya I-ZI kudhihirisha ukubaliano wa kisarufi. (alama 2)

(e) Yakinisha sentensi ifuatayo (alama 2)
Mtu asiyeugua hahitaji daktari.

(f) Andika vitenzi vifuatavyo katika hali ya kutendeana (alama 2)
-la
- nywa

(g) Bainisha yambwa tendwa na yambwa tendewa katika sentensi hii. (alama 2)
Ninamtaka mwanafunzi aniandikie barua.

(h) Tambua aina za vishazi katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Tulimtembelea alipokuwa mgonjwa.

(i) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mishale. (alama 4)
Wale wazuri sana watatuzwa zawadi nyingi.

(j) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo (alama 2)
Mtoto anapendezwa na ziwa

(k) Andika sentensi tatu zenye kudhihirisha matumizi mbalimbali ya KI. (alama 3)

(l) Andika kwa usemi wa taarifa. (alama 3)
“Tafadhali, nifungulie mlango sasa. Nitanyeshewa.” Mtoto akamwambia.

(m) Andika katika ukubwa. (alama 2)
Mwanamwali huyu alijinunulia viatu vya ngozi.

(n) Andika matumizi mawili ya mshazari. (alama 2)

(o) Eleza matumizi ya neno mzee katika sentensi zifuatazo (alama 2)
(i) Baba mzee amelewa
(ii) Mzee amelewa

(p) Tumia neno ‘kuwa’ kama kitenzi kishirikishi kikamilifu katika sentensi (alama 1)

(q) Tumia amba katika sentensi ifuatayo (alama 2)
Alaye ndiye aliaye

ISIMU JAMII (Alama 10)

(a) Eleza tofauti kati ya kuchanganya ndimi na kuhamisha ndimi. (alama 2)

(b) Andika sababu nne za kuchanganya na kuhamisha ndimi. (alama 4)

(c) Kiswahili ni lugha ya kibantu kulingana na ushahidi wa ki-isimu. Thibitisha kauli hii. (alama 4)

MTIHANI WA KAMDARA JET 2015
Cheti cha KuhitimuElimuyaSekondari (K.C.S.E)
102/3
KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI
SEHEMU YA A: USHAIRI.

SWALI LA LAZIMA

1. ***Soma shairinakishauyajibumaswaliyanayofuata.***
(AbdallaAbdilalif, sautiyadhiki)
Chema hakidumu, kingapendekeza,
Saaikitimu, **kitakuteleza**,
Ukawanahamu, kukingojeleza,
Huwanivigumu, kamwehutaweza.

Chemasikiimbi, kwambanakitweza,
Japomaratumbi, kinshaniliza,
Na japosiombi, kipaten'ongeza,
Mtuhaniambi, pa kujikimbiza.

Chemamarangapi, kin'niondoka,
Mwananguyuwapi?Hakukaamwaka,
Kwamudamfupi, aliwatilika,
Ningefanyalipi, elakumzika?

Chemawangubabu, kibwanaBashee,
Alojipatabu, kwambaanilee,
Na yakwesababu, ninitengenee,
Ilhaliwahhabu, maraamtwee.

Chemawanguponi, kipenzinyanyangu,
Hadisikuhini, yumoyonimwangu,
Yu moyonindani, hadikufakwangu,
Ningamtamani, hatarudikwangu.

Maswali

a) Lipe shairi hili anwan imwafaka (al. 2)
b) Eleza bahari **mbili** zinazojitokeza katika shairi hili (al. 4)
c) Ni nini maudhui ya shairi hili? (al. 2)
d) Onyesha matumizi ya aina **tatu** za uhuru wa ushairi (al. 3)
e) Eleza umbo la betimbilizamwisho. (al. 4)
f) Taja na kuonyesha tamathali **mbili** za Lugha zilizoko kwenye shairi hili. (al. 2)
g) Fafanua msamiati huu kwa muktadha wa shairi hili (al. 3)
i) Kitakuteleza
ii) Kinshaniliza
iii) ela.

SEHEMU B: TAMTHILIA
***MstahikiMeya* – T. Arege**
Jibuswali la 2 au 3

2. "Nanyi vile vile msikate tamaa. Endelee ni kushinikiza kumwona Meya. Mlango hatimaye huenda ukasalimu armi."
a) Weka dondoo hili haya katika muktadha wake. (ala.

4)
b) Taja kwa kutoa mifano; tamathal izozote **mbili** za lugh azilizotumika katika dondoo hili. (ala. 4)
c) Kwa kurejelea hoja **sita**, eleza ni kwanini wanao rejelewa wanakaribia kukata tamaa. (ala.12)

3. Onyesha vile mwandishi ameshughulikia ukosefu wa kuwajibika katika tamthilia ya MstahikiMeya. (ala. 20)

SEHEMU C: RIWAYA
Ken Walibora: KidagaaKimemwozea
Jibuswali la 4 au 5

4. ……wanaume wange wastahiwa na wake kidogo, wawaoneka maabiria wenzao katika mashua, dunia ingekuwa pahali pema zaidi pa kuishi.

a) Tambulisha mbinu **mbili** za kifasihi zilizotumika katik adondoo hili. (alama 4)
b) Thibitisha kwa mifano **mitatu** jinsi msemaji hakustahi wanamume wake. (alama 6)
c) Taja**maudhui**yanayojitokezakatikamanenohayayamsemaji. (alama 2)
d) Fafanua maudhui uliyotaja kwa kuitolea mifano mingine **mine** kutoka kwenye riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 8)

5. "Mwandishi wa Kidagaa kimemwozea amepata ufanisi mkubwa katika matumizi yake ya mbinu ya kweli kinzani." Fafanua kwa kutoa mifano mwafaka (al.20.)

HADITHI FUPI
***Damu Nyeusi na Hadhithi Nyinginezo* – S.A Mohamed**
Jibuswali la 6 au 7

6. "Mimi nilitaka mke, mwana mke mbichi ni mvumbike mwenyewe mpaka aive."
a) Weka dondoo hili haya katika muktadha wake (ala. 4)
b) Ni kwa nini msemaji alitaka amvumbike mwanamke mwenyewe? (ala. 4)
c) Eleza migogoro iliyochipuka baina ya msemaji na mwanamke huyu. (ala. 12)

7. Fikirini alicheka kila aliposikia redio ya Kenya ikitangaza "...Msifikiri kwamba Mzungu anatupenda sisi watu weusi"Thibitisha ukirejelea hadithi ya Damu Nyeusi.

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

8. Taja sifa za tanzu zifuatazo za fasihi simulizi
i) Ngomezi (al. 5)
ii) miviga (al. 5)
b) Elezahasaratanozinazohusishwanamivigakatikajamiiyasasa. (al. 10)

KAMDARA JET 2015
MWONGOZO
KARATASI YA KWANZA – INSHA:
102/1.

1. RIPOTI

- Mtahiniwa atimize maneno 400.
- Hii ni insha ya utunzi wa kiuamilifu kwa hivyo sura ya ripoti iwepo, yaani hii ni insha isiyofululiza bali ina vijichwa.

i. Mpangilio wake.

1. Kichwa.
2. Utangulizi.
3. Ndani ya utangulizi ataje waliohojiwa.
4. Ataje tarehe ya uwasilishaji.
5. Ataje mambo mengine muhimu yaliyofanyika.

ii. Matokeo ya udadisi .

- Ayashughulikie na kuonyesha yale mambo yanayosababisha udanganyifu kwa mfano:
- Wanafunzi kutojitayarisha
- Walimu wakuu wa shule kuhusika ili shule zao zipapate nafasi bora ya kujijengea jina lao na la shule yao.
- Wasimamizi wa mitihani kuzembea kazini.
- Wasimamizi wa mitihani kuhongwa/ufisadi.
- Mitihani ya taifa kuwa migumu.
- Nafasi chache za vyuo vikuu kusababisha wanafunzi kuwa na ushindani mkubwa kiasi cha wengine kutumia hila hii.
- Ukosefu wamaadili mema kwa upande wa wanafunzi.
- Ukosefu wa ulinzi wa kutosha.
- Ukosefu wa mpangilio bora darasani/ukumbini wakati mitihani inapofanywa.
- Ukosefu wa sera madhubuti kuhusu mitihani.
- Walimu wa masomo kuhusika/kujihusisha na udanganyifu ili masomo yao yawe bora zaidi.
- Watahiniwa kusingiziwa tu labda kutokana na historia ya hapo awali.
- Watahini kukosa umakini wa kutambua vyema kama mtihani uliibwa au la.[Hoja zingine zozote]

iii. Mapendekezo.

- Wasimamizi mihahani wawe watu wenye maadili na kujiheshimu.
- Watahiniwa watayarishwe mapema na vya kutosha.
- Sheria madhubuti kubuniwa kudhibiti wizi wa mitihani.
- Vyuo vikuu viongezwe maradufu.
- Mtindo kuorodhesha shule bora katika kaunti na taifa uondolewe.
- Ulinzi uimarishwe.
- Nafasi za kazi zibuniwe kupunguza ushindani mkali uliopo.
- Mtihani uwe wastani/kadri na si mgumu sana.
- Somo la dini liimarishwe ili kuleta maadili miongoni mwa wanafunzi.
- Wasimamizi wa mitihani walipwe vizuri kuzuia kuhongwa.

iv. Hitimisho.

- Mtahiniwa atoe maoni, kauli, msimamo mradi yahusiane na mada husika.
- Insha ikikosa sura ifaayo akaadiriwe ifaavyo kasha aoondolewe alama 4 za sura.

2. Wananchi ndio wa kulaumiwa kufuatana na kuzorota kwa usalama nchini Kenya. Jadili.

Kuunga

- Chuki na uhasama baina ya makabila/ vita vya kikabila.
- Uundaji wa vikundi haramu vya vijana.
- Tamaa ya kutajirika k.m. wizi wa mifugo.
- Wachochole kuingilia uhalifu kwa madai ya kujitafutia.
- Wananchi kukataa kufichua wahalifu miongoni mwao/ wnawaficha.
- Umiliki wa silaha hatari na baadhi ya wananchi.
- Mitazamo hasi ya wananchi kuhusu maafisa wa usalama/ hawashirikiani nao.

Kupinga.

- Usalama unakoseshwa na kutokuwepo kwa nafasi za kazi/ wasio na kazi hulazimika kuingilia uhalifu ili

wapate ajira.
- Ukosefu wa fedha za kuendeleza uimarishaji wa usalama.
- Idadi ndogo ya maafisa wa usalama.
- Ufisadi wa maafisa wa usalama.
- Vifaa vya kuendeleza shughuli za usalama k.m. magari, silaha havitoshi.
- Kiwango cha chini cha mafunzo kwa walinda usalama.
- Magaidi wanaotatiza usalama nchini kutoka nchi za kigeni k.v. Somalia ambao huwalemea wananchi.

i. Mtahiniwa asiwe na hoja chini ya tano. Aliye na tatu tu asipite kiwango cha C+, hoja moja au mbili asipite kiwango cha C-
ii. Hoja zote zijadiliwe kikamilifu.
iii. Aweze kuwa na idadi sawa ya hoja katika pande zote. almuradi aonyeshe msimamo wake. Asipofanya hivyo asiadhibiwe lakini asipite kiwango cha B.
iv. Akishughulikia upande mmoja tu bila kugusia upande wa pili asipite asipite kiwango cha C+.

3. Usipoziba ufa utajenga ukuta.
- Kisa kidhihirishe hali ya kufanya au kurekebisha jambo mapema.
- Unapokosa kufanya hivyo utapata matatizo mengi baadaye au ikubidi ufanye jambo kubwa sana kuliko lili la awali.
- Atunge kisa kimoja tu, na wala sio visa.
- Kisa kiwe na urefu ufaao na kioane na methali.
- Kisa kisichooana na methali, apate 03.
- Akiegemea upande mmoja tu wa methali, asipite kiwango cha C+.

4. Kisa cha mwanafunzi kimalizikie kwa maneno ya madokezo aliyopewa.
- Atakayeanza na maneno ya madokezo, atakuwa amepotoka. Kwa hivyo apewe kiwango cha D.
- Asipomalizia kwa mdokezo aliopewa na kisa chake kihusiane na mdokezo, atakuwa hajapotoka kimaudhui bali amepungukiwa kimtindo.
- Atakuwa amepotoka kimaudhui pale tu atakosa kumaliza kwa kauli aliyopewa na kusimulia kisa kisichohusiana na swali.
- Ajihusishe na kisa (atumie nafsi ya kwanza) Asiyejihusisha amelemewa kimtindo.
  Tanbihi: Mwalimu atumie mwongozo wa kudumu kwa maelezo zaidi kuhusu utahini katika viwango mbalimbali.

MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA KAMDARA JET
102/2
KISWAHILI
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA LUGHA 102/2
UFAHAMU

a). Maendeleo / Jinsi ya kuleta maendeleo (alama 1)
b). Hulka ya kutarajia mambo mazuri zaidi maishani. (alama 2)
wanafanya kazi kufa kupona na kuwa na matumaini ya kuishi vizuri zaidi kesho
c). Jinsi serikali iliyo na uwezo wa kutekeleza ndoto zake
i). Inafanya mipango ya kuleta hali bora kwa
ii). Kushirikisha wadau ambao wana majukumu ya kusimamia na kutekeleza mipango katika muda unaotakiwa.
iii). Inatumia rasilimali zake k.v. madini, misitu, ardhi (alama 3×1 = 3)
d). i). Uvivu / Kutopenda kujishughulisha na kazi
ii). Kuelekezeana lawama / Kuegemea zaidi katika kujadili udhaifu badala ya kujadili namna ya kuboresha hali. (alama 2× 1= 2)
e). Wito wa aya ya mwisho
Tuyachunguze mambo yaliyotuangusha na kuketi chini kuyajadili wazi, tukemeane na kurekebishana bila hofu. (2×1= 2)
F). Methali zinazohusiana na aya mbili za mwisho
i) Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu
ii). Jifya moja haliinjiki chungu (2 × 1 = 2)
g). i). kukidhi haja - kutosheleza mahitaji / timiza matakwa
ii). kiu ya maendeleo – uchu wa kuwa na maendeleo / haja
iii). Tunyosheane vidole usoni – tukemeane / tuonyane (3 ×1 = 3)

MUHTASARI

A). Changamoto zinazoikumba lugha ya kiswahili kama lugha rasmi.
- Lugha ya kiswahili kushindania nafasi sawa na ile ya kiingereza katika shughuli za kikazi.
- Lugha ya Kiswahili itachukua nafasi ipi na kiingereza nacho kichukue ipi.
- Kiwango cha maandalizi ya wananchi katika kuyapokea mabadiliko haya
- Kufanyika kwa uandishi wa vitabu zaidi vya Kiswahili
- Mtazamo hasi wa wananchi kuwa kiswahili ni lugha ngumu
- Utoaji wa nafasi finyu kwa lugha ya Kiswahili miongoni mwa wazungummzaji ambao huzionea lugha za kigeni fahari
- Kuharibiwa kwa Kiswahili na sheng au lugha za kienyeji

Hoja 6 × 1 = alama 1 mtiririko =7

b). Namna ya kuimarisha matumizi ya Kiswahili nchini
- Watunga sera kueleza kinagaubaga mawanda ya matumizi ya lugha hizi mbili kazini.
- Watumishi wa umma wapewe mafunzo maalumu kuhusu mbinu za mawasiliano katika Kiswahili
- Vyuo vikuu na taasisi za mafunzo kuwaandaa wanafunzi wao wapya kuhusu mahitaji mapya ya kikatiba
- Wanaohusika na utekelezaji wa sera wapate mafunzo kutoka kwa wataalamu wa Kiswahili
- Kuandikiwa kwa vitabu zaidi vitakavyofunza mbinu za mawasiliano.
- Wananchi wahimizwe kukionea fahari Kiswahili, wakipende na kukielewa
- Viongozi wawe vielelezo kwa kukizungumza Kiswahili sanifu .
- Viongozi wapewe kipaumbele katika kufunzwa kwa Kiswahili

Hoja 7 × 1 = 7 Utiririko1 Jumla alama 8

MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)

(a) Andika vigezo vitatu vinavyotumiwa katika kuainisha irabu (alama 3
- Sehemu ya ulimi
- Mwinuko wa ulimi
- Mkao wa midomo

(b) (i) Eleza maana ya mofimu. (alama 2)
Kipashio kidogo kabisa cha lugha chenye maana ya kisarufi.
(ii) Toa mfano mmoja mmoja wa mofimu huru na mofimo tegemezi. (alama 2)
Huru – Baba dirisha n.k

Tegemezi – Mtoto, a-na-chek-a, madirisha

(c) Kwa kutoa mifano onyesha majukumu manne ya viambishi awali. (alama 2)

(i) Nafsi mf. Nitasoma
(ii) Wakati/hali mf – ta,me
(iii) Ngeli mf kitaoshwa
(iv)- umoja na wingi – mtu – watu
(v) - kirejeshi - atakayesoma
(vi) Ukanusho – hakusoma
(vii) Mtendwa - atatupiga

(d) Tunga sentensi ukitumia nomino katika ngeli ya I-ZI kudhihirisha ukubaliano wa kisarufi. (alama 2)

Sahani ilioshwa na mama
Sahani zilioshwa na mama

(e) Yakinisha sentensi ifuatayo katika wingi. (alama 2)

Mtu asiyeugua anahitaji daktari.
Watu wanaougua wanahitaji madaktari.

(f) Andika vitenzi vifuatavyo katika hali ya kutendeana (alama 2)

- La - liana
- nywa - nyweana

(g) Bainisha yambwa tendwa na yambwa tendewa katika sentensi hii. (alama 2)

Ninamtaka mwanafunzi aniandikie barua.
yambwa tendwa – barua
tendewa - mimi

(h) Tambua aina ya vishazi katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Tulimtembelea alipokuwa mgonjwa.

(i) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mishale. (alama 4)

Wale wazuri sana watatuzwa zawadi nyingi.
S → KN + KT
KN → W + V + E
W → Wale
V → Wazuri
E → Sana
KT → T + N + V
T → Watatuzwa
N → zawadi
V → nyingi

(j) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo (alama 2)

Mtoto anapendezwa na ziwa
Mtoto anapendezwa na titi.
Mtoto anapendezwa na sehemu yenye maji.

(k) Andika sentensi tatu zenye kudhihirisha matumizi mbalimbali ya KI. (alama 3)

Sentensi zionyeshe maana zifuatazo

(i) udogo mf kitoto
(ii) wakati – alikuwa akisoma
(iii) ngeli (ki – u) kitabu kime
(iv) Ki mfanano – kizee, kinyama zozote
(v) Utanusho – hakiliki
(vi) Kiwakilishi cha ngeli ya ki-vi mfano kilianguka.

(l) Andika kwa usemi wa taarifa. (alama 3)

"Tafadhali, nifungulie mlango sasa. Nitanyeshewa na mvua." Mtoto akamwambia.
Mtoto aliomba/alisihi afunguliwe mlango wakati huo kwa kuwa angenyeshewa na mvua.

(m) Andika katika ukubwa. (alama 2)

Mwanamwari huyu alijinunulia viatu vya ngozi.
Janajali hili lilijinunulia majiabu ya gozi/magozi.

(n) Andika matumizi mawili ya mshazari. (alama 2)

Kumaanisha au/ama
Kuandika visawe – baba/abu
Kuandika tarehe – 1/7/15

(o) Eleza matumizi ya neno mzee katika sentensi zifuatazo (alama 2)

(i) Baba mzee amelewa - kivumishi
(ii) Mzee amelewa - Nomino

(p) Tumia neno 'kuwa' kama kitenzi kishirikishi kikamilifu katika sentensi (alama 1)
Baba amekuwa mgonjwa. Hakiki sentensi.
Mama alikuwa mwalimu. Tanb. Neno hili lisitumiwe kama kitenzi kisaidizi.

(q) Tumia amba katika sentensi ifuatayo (alama 2)
Alaye ndiye aliaye
Ambaye hula ndiye ambaye hulia.

ISIMU JAMII (Alama 10)

(a) Eleza tofauti kati ya kuchanganya ndimi na kuhamisha ndimi. (alama 2)
ii). Kuchanganya ndimi – hali ya kutumia zaidi ya lugha moja katika mawasiliano . matumizi haya hujikita katika sentensi moja / mzungumzaji anatoka kidogo katika lugha moja na kuingilia nyingine kasha akarejelea lugha awali.
Kuhamisha ndimi – kubadilisha mkondo wa mazungumzo kutoka lugha moja hadi nyingine ambapo msemaji ana umilisi wa zaidi ya lugha mbili. (2 × 1 = 2)

(b) Andika sababu nne za kuchanganya na kuhamisha ndimi. (alama 4)
- Kupungukiwa na msamiati wa kutumia
- (ii) Kujitambulisha na kundi fulani la watu mf waliosoma, wanahirimu n.k
- Kujihusisha na lugha inayoenewa fahari
- Kutaka kuonyesha kuwa una uwezo wa kutumia lugha mbili au zaidi
- Kutaka kufafanua dhana fulani k.m uyoka (x-ray) Zozote 4 x 1 = 4

(c) Kiswahili ni lugha ya kibantu kulingana na ushahidi wa ki-isimu. Thibitisha kauli hii. (alama 4)
- Kufanana kwa msamiati km. ulimi (kisw) , Rurimi (kikuyu) lulimi (kibukusu)
- Maneno ya Kiswahili yana viambishi km yale ya kibantu mf. M-tu (Kiswahili) , Mu-ntu (zulu), mu-undu (kikuyu)
- Mpangilio wa maneno mf. Mtu mmoja (Kiswahili)
- Mundu umwe (Kikuyu), Muntu umwe (Kimeru)
- Muundo wa maneno kufanana – hutamkwa kisilabi
- Muundo wa maneno kuishia kwa irabu Zozote 4 x 1 = 4

KAMDARA JET 2015
Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Sekondari (K.C.S.E)
MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA FASIHI
102/3
KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI

1. **Ushairi**
   (a) **Anwani** :Chema/ chema hakidumu/chema wangu.
   (b) **Bahari**
   Ukaraguni - kila ubeti una vina tofauti.
   Kikwamba - Neno 'chema ' limeanza beti zote.
   Utenzi - kila mshororo una mizani 12.
   Tarbia - Kila ubeti una mishororo mine.
   Mathnawi- sehemu mbili ukwapi na utao. ***(Zozote 2 x 2 = 4)***
   (c) **Maudhu**i **– maombolezi** - Mshairi anaomboleza kwa kufiwa na wapenzi wake : mwanawe babaye (Kibwana Bashee) na nyanyake (Poni) ***(Kutaja 1, kufafanua 1 = 2)***
   (d) (i) **Tabdila** - Kukingojeleza - kukingojelea
   Yakwe - yake
   (i) **Kuboronga sarufi** - Kipenzi nyanyagu - nyanyangu kipenzi
   (ii) **Inkisari** - Kinshariliza - kimeshaniliza/kimekwisha niliza
   n'ongeza - niongeza , haniambia - haniambii
   kinn'ondoka - kimeniondoka
   alojibu - aliyejipa
   (iv) **Lahaja** - ele -ila
   (e) **Beti za mwisho mbili**
   – Kila ubeti una **mishororo minne**
   – Kila ubeti una ukwapi na utao/vipande viwili/ **mbili sehemu**
   – Kila mshororo una mizani **kumi na miwili**; 6, 6
   – Vina vya **ukwapi na utao** ni tofauti (vinabadilika)
   – Maneno 'chema wangu' ndiyo yanayozianza beti hizi.
   – Kituo ni kimalizio tu**. Kinabadilika**. ***(Zozote 4 x 1 = 4)***
   (f) **Tamathali** - **Takriri** - neno chema
   Balagha - mwanangu yu wapi?
   ela kumzika? ***(Kutaja ½ kufafanua ½)***
   (g) **Msamiati**
   (i) **Kitakuteleza** - kitakutoka ghafla/kitakuponyoka.
   (ii) **Kinshaniliza** - kimenifanya nilie
   (iii) **ela-** isipokuwa bali ***(3 x 1 = 3)***
   SEHEMU B: TAMTHILIA
   Timothy Arege: Mstahiki Meya
2. (a)
   (i) **Msemaji** ni Siki/Daktari Siki
   (ii) **Msemewa** ni Tatu - mmoja wa wa wakilishi wa wafanyikazi
   (iii) **Mahali**: Katika Ofisi ya daktari Siki
   (iv) **Sababu**: Tatu amekuja kumwomba/kumsihi Daktari Siki aende aseme na Meya kama binamu yake,pengine huenda akamsikiliza. ***(Hoja 4 x 1 = 4)***
   (b) **Tamathali za lugha**:
   (i) **Msemo** - Msikate tama
   (ii) **Tashihishi** - Mlango huenda ukasalimu amri ***(Hoja 2 x 2 = 4)***
   (c) (i) Mishahara duni, kulipwa nusu/kukosekana hata baada ya miezi mitatu
   (ii) Kuvunjiliwa mbali kwa maandamano ya wafanyi kazi
   (iii) Kukosekana kwa dawa hospitalini
   (iv) Madiwani kuongezwa mishahara
   (v) Madiwani kutolipa kodi
   (vi) Ufisadi – unyakuzi wa ardhi, kuuza fimbo ya Meya

(vii) Kukosekana kwa ajira kwa **vijana**
(viii) Hali duni ya usafi wa mazingira
(ix) Vifo vya watu hospitalini.
(x) Njaa – mtoto kulishwa kiporo ***(Hoja zozote 7 x 2 = 14)***

3. **Maudhui ya kutowajibika katika Kidagaa Kimemwozea**.

- Meya kulinganisha ufanisi wa eneo na wa miji midogo na dhaifu, badala ya kuendelea kupiga hatua mbele wanapiga hatua kinyumenyume.
- Meya kujifanya hajui watu wanateseka. Amefumba macho kwa matatizo.
- Meya kukataa kuonana na kuwasikiza viongozi wa wafanyikazi, hata anapokutana nao anapuuza mapendekezo yao.
- Kuna baadhi ya watu wanaomuunga Meya mkono, hataki kujua juu ya wengi. Wachache wanatosha.
- Nyimbo za kizalendo baada ya na kabla ya vipindi muhimu, miaka hamsini baada ya uhuru.
- Mipango ya miaka kumi inapuuzwa. Meya anasema kuwa wana mipango ya milenia. Mipango ya miaka kumi ni upuzi.
- Afya bora na ya bure ilihaidiwa wananchi, wanalazimika kulipa.
- Wananchi kutoshirikishwa katika maamuzi. Wengine kama Siki kutimuliwa nyumbani mwa Meya, wanapojaribu kumweleza matatizo ya raia.
- Mikutano nadra kufanywa kama tunavyoelezewa na Diwani I – hufanywa hasa wakati kuna jambo kama mgomo kutokea.
- A hadi za uongo- shehena ya dawa kuwa bahari kuu.
- Kazi ya baraza/madiwani – badala ya kusikiza na kuwatimizia haja, wanafanya maisha ya wanacheneo kuwa mgumu zaidi.
- Uchafu kuenea kila mahali na uvundo kutokeza hata ndani ya majumba.
- Meya kukataa kuongea na wanahabari na wanchi kwa kusingizia kuwa ana wageni.
- Askari kuwafurusha watu kutoka mjini.Mji kubaki mahame
- Viongozi/madiwani wana njaa na tamaa kubwa isiyoweza kushibishwa.
- Washauri wanawatenga wengine. Diwani III anapuuzwa na wengine.
- Kujiongeza mishaharaa kama overtime marupurupu na kadhalika.
- Kula viapo vya kuficha siri za wizi kama wa fimbo ya meya.
- Meya kutojua kuwa hakuna maji safi. ***(Zozote 10 x 2 = 20)***

SEHEMU C: RIWAYA

4. Kidagaa Kimemwozea

a) Mbinu za kifasihi katika dondoo

- Tashbihi – Wawaone kama abiria wenzao.
- Istiari – Mashua (Ndoa inalinganishwa na mashua).

b) Jinsi msemaji hakustahiwa na mumewe

Msemaji ni Bi. Zuhura. Mumewe, Mtemi Nasaba Bora

- Mtemi alimwacha Zuhura katika upweke alipojishughulisha na wanawake wengine kule njee k.m. Lowela.
- Mtemi hakumruhusu Zuhura amwulize alikotoka. Alijia ukali ndipo asisemezwe.
- Alimpiga (ushahidi ni kioo cha shubaka kilichokua na nyufa tele, tokeo la mapambano makali usiku mmoja baina yao.
- Mtemi alimtuhumu Zuhura kuwa na uhusiano na Amani alipowafumania katika chumba chake cha kulala.
- Mtemi alimtaliki Zuhura kwa tuhuma hizo.
- Mtemi alimzuia Zuhura kukinywesha kitoto Uhuru maziwa kilipopelekwa kwake na Amani baada ya kukiokota mlangoni pake.
- Zuhura hakutimiziwa haki yake katika ndoa kwani Mtemi aliporejea alijibwaga kitandani kama gogo la mti. (hoja 3x2= 6)

c) Maudhui inayojitokeza katika maneno ya Zuhura.

- Ukandamizaji wa jinsia ya kike. (2x1=2)

d) Mifano mingine ya ukandamizaji

- Dora hakusaidiwa na majisifu kuwalea watoto wao walemavu. Aidha, upo wakati majisifu alimtenga

kwa miaka kumi na tano alipowazaa watoto wao wa kwanza wenye akili taahira.
- Mama mja mzito aliye kua akijifungua kando ya barabara hakupata usaidizi kutoka kwa Mtemi na Nasaba Bora.
- Lowela alilazimishwa na Mtemi kukitelekeza kitoto alichozaa kwa kukiwacha mlangoni kwa Amani.
- Mamake imani alinyanganywa shamba na nyumba yake kuchomwa na askari waliotumwa na Mtemi kwa maana alikua mjane.
- Bi kize alishurutishwa kuhudhuria mkutano wa siku kuu ya wazalendo, japo hakuelewa hotuba za Kiingereza alizosoma Mtemi.
- Imani alitupwa katika seli moja na Matuko Weye (wazimu) pamoja na Amani – askari hawakujali jinsia yake.
- Msichana mwanafunzi aliyeringwa na Fao baada ya kumtunga mimba.

5. Matumizi ya kweli kinzani katika kidagaa kimemwozea (al.20)

- Maana yake ni kinyume cha matarajioau kinaya.
- Mtemi Nasaba bora, maana yake ukoo bora au uungwana. Lakini vitendo vyake ni kinyume na jina lake hivyo ni kinaya. K.m
- Mtemi Nasaba bora aliwaadhibu wananchi ambao hawakuchanja mbwa wao ilihali wake mwenyewe hakuwachanja.
- Mtemi alimuuliza Amani ikiwa yeye ni mwizi wakati wa kutafuta ajira kwake ilihali yeye menyewe ndiye mwizi mkubwa aliyenyakua mali ya watu.
- Mtemi Nasaba bora alikuwa na tabia mbaya zisizo na ungwana wowote.
- Mtemi anapomwambia Amani kachukue “mwanao” akamtunze (akimrejelea motto uhuru) ni kinaya kwa sababu Uhuru hakuwa mwana wa Amani bali wa Nasaba Bora.
- Mtemi kutumia lugha ya kizungu ambayo wananci wengi hawaelewi ni kinaya badala ya kutumia lugha ya Kiswahili wanayojua.
- Tabia za Nasaba Bora na mwalimu majisifu zilkua kinyume cha maadili ya kasisi baba yao. (yeye aliwataka wapendane na kusoma bibilia) ni kinaya maana hawakupendana hata kidogo wala hawakuwa wakisoma bibilia.
- Zahanati ya nasaba bora ina jina lenye maana ya utu lakini watu wengi huenda kufa huko.
- Ni kinaya kuona kuwa mtemi Nasaba nora alikuwa akisoma bibilia lakini anapoambiwa kuwa Bob Dj alikuwa ameumwa na jibwa “jimmy” alikataa kutoa usaidizi wa kumfikisha kwa matibabu akisema hayo ni stahili yako.
- Katika hotuba ya siku kuu ya wazalendo, mtemi anasema wanajali maslahi ya kila mmoja ilhali wananyanyasa watu na hawajali maslahi yao.
- N kinaya kuwa watu wa sokkomoko walikuwa na uchechefu wa maji ilhali kulikuwa na maji mengi katika mto kiberenge. Walibadilisha mtazamo wao kuhusu mwiko wa kutumia maji yam to huo wakati Imani na Amani walipokunywa maji bila kufariki.
- ni kinaya mwalimu majisifu kuitikia mwaliko wa chuo kikuu cha mkokotoni ilhali hakuwa na ufahamu wa mada ya kuwasilisha.
- Chwechwe Makwece aliletea nchi yake sifa nyingi lakini alipovunjika mguu hakusaidiwa, mguu ukakatwa.
- Watu wa tomoko walipigania uhuru lakini viongozi walioshika hatamu ndio waliofaidika zaidina kuwangandamiza kama mkoloni mzungu.
- Mwalimu majisifu alihojiwa katika idhaa ya taifa ya Tomoko (ITT) kuhusu maswala ya haki, uzalendo na utamaduni. Alitarajiwa kuwa miongoni mwa watetezi aalimu na staid wa utamaduni na uzalendo wa mwafrika lakini tunaona hatimaye majisifu mtu aliyekolea katika ulevi kama pale kwa mama n’tilie.
- Mwalimu majisifu alimpa nasaha mashaka kuwa wasome kwa bidii kwani bara Afrika ilitaka watu waliosoma sana ili kulikomboa toka kwenye utumwa na ujinga, njaa na umaskini ilhali yeye mwenyewe alifika darasani kufunza kwa nadra. (Hoja zozote 10x2=20)

SEHEMU YA D

HADITHI FUPI – KEN WALIBORA, DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE

Mke Wangu

6. (a) (i) Maelezo ya **msimulizi**

(ii) Anajiambia **nafsin**i mwake/anaongea na **nafsi yake**

(iii) Mahali ni kwa kina msimulizi **nyumbani**

(iv) Alitaka kumwoa mke ambaye hakuwa amejifunza mengi ya mijini. Yule **mshamba** ambaye ni yeye/ndiye angamfundisha ***(Hoja 4 x 1 = 4)***

(b) Alitaka mwanamke ambaye hajaathirika na maisha mjini na ambaye hangemsumbua bali yule ambaye yeye mwenyeww angemwelekeza jinsi anavyopenda. (***Hoja 1 x 2 = 2)***

(c) **Migogoro baina ya msemaji** – msimulizi na mwanamke huyu- Aziza:

- Aziza ana mtazamo wa kihafidhina kutokana na malezi yake ya shamba ilhali mumewe ana mtazamo wa kisasa unaoendana na maisha ya mjini pamoja na elimu aliyopata.
- Msimulizi anadhani akioa mwanamke wa shamba ataweza kumwelekeza jinsi anavyotaka yeye lakini anashindwa k.m
  - Amekataa kuvaa viatu,
  - Amekataa kusugua meno kwa mswaki na dawa
  - Mkono wake umeparara n.k
- Aziza haoni sababu ya mumewe. Kuzidi kuwategemea wazazi kwa mahitaji yao ya kila siku, wao ndio wamlishe mumuwe na Aziza
- Aziza hafurahishwi na mtindo wa mumewe baada ya kumaliza masomo,kukosa kazi ya ofisi , ameketi bila kufanya chochote.
- Ubaguzi unaonyeshwa na mumewe wa walio wa tabaka la chini haumfurahishi Aziza ndiposa anamwalika bazazi wa madafu ghorofani.
- Aziza hapendi kukaa tu na kuletewa chakula,kuoshewa nguo na watumishi wa nyumbani bali kuyatekeleza haya mwenyewe. ***(Hoja 6 x 2 = 12)***

Damu Nyeusi

7. **Mifano kuoyesha mzungu hampendi mwafrika**

- Gari la mzungu halimbebi mwafrika.
- Dereva mzungu halisimamishi gari kwa fikirini – anawashukiwa kuwa jambazi
- (ii) Akiwa darasani, Fikirini anaulizwa maswali ya kumdhalilisha na kumdunisha k.m Kwenye uwanja wa ndege hapa Marekani
- Mikahawani, Fikirini aliangaliwa na macho meupe yenye dharau ya wateja wazungu.
- Fikirini kushtakiwa mahakamani eti hakufunga zipu.
- Mwanamke yule mweusi kwa ushirikiano na jibaba, wanamfungia ndani kumlazimisha Kimapenzi.
- Alitishwa maisha yake kwa mtutu wa bunduki na yule jibaba. Dada mweusi anamwelekea kisu chenye makali ubavuni
- Fikirini alidhalilishwa kwa kuvuliwa nguo zote.
- Fikirini alinyang'anywa mali yake yote vikiwemo vitabu
- Fikirini anatusiwa – tumbiri
- Fikirini anatozwa faini mara mbili na polisi mzungu kwa kuvuka barabara huku taa kuelekea magari zikiwa zimewaka rangi nyekundu – wazungu wanaachwa kupita tu.
- Wahadhiri wanatoa alama kwa kupendelea watu weupe na kuwakandamiza weusi.
- Fikirini akienda kununua vitu kwenye duka mlinzi humfuata kwa kushukiwa wizi.

(Hoja zozote 10 x 2 = 20)

8. (a) **Sifa za ngomezi**

- Huwasilisha ujumbe mzito kwa njia iliyofichika kwa mapigo ya ngoma
- Wanajamii wa kundi husika huweza kufasiri ujumbe
- Inatumiwa kutangaza jambo fulani
- Inapatikana kwa wingi katikajamii mbalimbali za kiafrika
- Hupiga marufuku katika eneo la kutolea kafara
- Ngoma hutumiwa kunawasilisha ujumbe wa aina yoyote.(5x 1 = 5)

(b) **Sifa za miviga**

- Huwa na madhumuni maalum ya kufanya sherehe hizo
- Huwa na wakati maalum wa kuitekeleza
- Kuna utaratibu maalum wa kufanya sherehe hiyo
- Kuna sheria/kaida maalum zinazozingatiwa wakati wa shule hizo
- Hujumuisha vitendo maalum – km kusimama
- Aghalabu hutolewa sadaka za vitu mazaao au wanyama
- Huwa na matumizi ya vifaa maalum na mavazi (maleba)

– Hufanywa kwa lugha maalum inayofungamana na sherehe (Mivigi mingine hufanywa kimyakimya bila maneno) ***(5 x 1 = 5)***

(c) **Hasara za miviga** ***(5 x 2 = 10)***

- Baadhi ya miviga huhatarisha maisha na afya ya wanajamii kama vile kumrithi mjane,jando-vifaa butu.
- Hukinza malengo ya kitaifa-ukeketaji wa wanawake.
- Huhusisha ushirikina unaozua uhasama baina ya watu-mazishi.
- Hugharimu pesa nyigi na kuiacha familia katika hali duni kiuchumi.
- Husababisha uchungu –ukeketaji au jando.
- Huendeleza tofauti za kijinsia-unyago na jando-humdhalilisha mke na kumtukuza mume.
- Huasi mabadiliko ya kiwakati-zimepitwa na wakati. **Zozote 5x1 =5**

KAUTI NDOGO YA GATUNDU KUSINI MTIHANI WA KUTATHMINI
Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Sekondari (K.C.S.E)
102/1
KISWAHILI INSHA
Karatasi I

Kiswahili (INSHA)
MASWALI

1. Jopo linaloshughulikia undanganyifu katika mithani ya Kitaifa (KCSE) limekuchagua wewe kama mwanajopo kati ya wanajopo watano. Mmetakiwa kuchunguza kinachosababisha undanganyifu, madhara ya undanganyifu na jinsi ya kukabiliana na undanganyigu huo. Andika ripoti yenu.
2. Tatizo La kigaidi ni changamoto kubwa sana katika usalama na maendeleo ya kiuchumi hapa nchini. Jadili.
3. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali: Mwenye kovu sidhani kapoa.
4. Andika kisa kitakachoishia kwa:
   ..... niliyakumbuka maneno aliyotwambia mwalimu wetu shuleni siku moja. Nilijilaumu si haba na machozi yakanidondoka pukupuku.

MTIHANI WA MAKADIRIO WA WILAYA YA GATUNDU
Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Sekondari (K.C.S.E)
102/2
KISWAHILI
Karatasi ya 2
LUGHA

1. **UFAHAMU**

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Mojawapo kati ya misingi na nguzo za maendeleo uliwenguni ni viwanda. Viwanda ni muhimu kwa kuwa ndivyo vinavyoigeuza malighafi inayopatikana na kuwa bidhaa zinazoweza kutumiwa na watu. Katika nchi zinazoendelea, ambazo hazina uwezo mkubwa wa mitaji viwanda vinavyoimarika ni vile vidogo. Hivi ni viwanda ambavyo huhusisha amali za mikono. Kuimarika kwa viwanda hivi vidogo kunatokana na sababu mbalimbali.

Nchi zinazoendelea huwa na masoko finyu sana kwa kuzingatia uwezo wa ununuzi wa wanaolengwa na bidhaa za viwanda . Katika msingi huu viwanda vikubwa vitawiwa ugumu kufanya biashara katika mazingira ambako masoko yake ni finyu au utashi wa bidhaa zake sio mkubwa. Viwanda vidogo pia vinao uwezo wa kuwaajiri wafanyikazi wengi hasa kwa kuwa havina uwezo wa kugharamia mashine. Uajiri huu wa wafanyikazi wengi ni muhimu katika maeneo mengi ambako tatizo la ajira ni mojawapo wa matatizo sugu. Tofauti na mataifa ya kitasmia (yenye viwanda vingi) mataifa mengi yanayoendelea hayana mifumo imara ya kuwakimu watu wasiokuwa na kazi. Utegemezi wa jamaa wanaofanya kazi kwa hivyo unakuwa nyenzo ya pekee ya kuyamudu maisha.

Kuanzisha viwanda vidogo vidogo hakuhitaji mtaji mkubwa tofauti na viwanda vikubwa. Hali hii

inasahilisha uwezekano wa watu wengi kujasurisha shughuli yoyote ile. Sambamba na suala hili ni kuwa ni rahisi kujarisha bidhaa mpya kwa kiwango kidogo cha kiwanda kidogo. Ikiwa mzalishaji yeyote atazalisha bidhaa mpya kwa mapanu, kwa mfano kama ilivyo kwa viwanda vikubwa, pana uwezekano wa kupata hasara kubwa. Huenda utashi wa bidhaa hiyo uwe mdogo ukilinganishwa na ugavi wa bidhaa yenyewe. Majaribio mazuri huwa ni kwa kiwango kidogo.

Kuwepo kwa viwanda vidogo huwa chocheo kubwa la usambazaji wa viwanda hadi maeneo ya mashambani. Hali hii inahakikisha kuwa nafasi za ajira zimezambazwa nchini hali ambayo inasaidia kuhakikisha kuwa pana mweneo mzuri wa kimapato nchini. Mweneo huo wa mapato unachangia katika kuboresha uwezo wa kiununuzi wa umma. Huu ni msingi muhimu wa maendeleo. Upanuzi na ueneaji wa viwanda vidogo vidogo ni msingi mkubwa wa kujitegemea kiuchumi. Aghalabu viwanda vikubwa huegemea kwenye mitaji ya mashirika ya kimataifa na huwa msingi wa kuendelezwa kwa utegemezi wa kiuchumi.

Maswali

a) Kwa nini viwanda ni muhimu? (alama 2)
b) Ni nini kiini cha matatizo ya uuzaji wa bidhaa katika nchi zinazoendelea? (alama 2)
c) Eleza faida zinazotokana na kuwepo kwa viwanda vidogo vidogo. (alama 4)
d) Usambazaji wa viwanda katika maeneo ya mashambani una faida gani? (alama 4)
e) Fafanua maana ya msamiati huu kama ulivyotumika katika kifungu. (alama 3)
   i) Kujasurisha
   ii) Amali
   iii) Utashi

2. MUHTASARI

Soma kifungu kifuatacho cha habari kisha ujibu maswali yanayofuatia.

Watu wengi, wanaamini kwamba kufundisha watoto nyimbo shuleni ni kupoteza wakati unaofaa kwa masomo ya maana. Lakini muziki nyumbani na shuleni una manufaa mengi.

Muziki ni kitulizo kikubwa sana cha moyo wa binadamu. Muziki una njia ya kipekee ya kuwasiliana. Baadhi ya ujumbe hauwezi kupitishwa kwa njia nyingine ila kwa muziki.

Muziki umetajwa kumsaidia mtoto kwa mambo yafuatayo:
Kuendeza hisia nzuri, za kuburudisha na kuzuzua. Muziki humsaidia mtoto kuweza kukabiliana na tajriba mbaya nazo. Unampa fursa ya kutoa moyoni simanzi na dhiki yake na hivyo kumrejeshea raha tena. Liwazo la muziki ni dhahiri wakati mtoto anapolala pindi anapoimbiwa bembelezi.

Inaaminika pia kwamba muziki unakomaza akili ya mtoto na ni nyenzo muhimu sana katika hafla yake ya kujifanya mambo, hasa kwenye miaka yake ya mapema. Muziki huhitaji umakinifu ili kutambua miondoko na maneno halisi ya wimbo huo na mambo haya humfanya mtoto kuhamisha umakini huu kwenye masomo mengine darasani. Inaaminika pia kwamba kupitia kwa muziki mtoto anaweza kujifunza mbinu ya kukumbuka mambo anayofunzwa masomoni.

Watoto ambao hujifunza muziki mara kwa mara hujipatia mbinu za werevu shuleni haswa kwenye somo la hesabu na werevu wa mambo mengine kwa jumla. Utafiti umeonyesha kwamba watu wazima ambao walijifunza muziki kabla wafikishe umri wa miaka 12 huwa na utumizi mzuri wa maneno magumu na msamiati kuliko wale ambao hawakujifunza kuimba.

Muziki pia husaidia watoto walio na kasoro za kuzungumza au walio na ulimi mzito wa kuzungumza. Watoto au watu wazima walio na shida ya kigugumizi huweza kujieleza kwa ufasaha kwa kupitia muziki na jambo hili huboresha kujiamini kwao kwa kibinafsi. Watoto kama hao huweza kujifunza na kuelewa mila na tamaduni zao.

MASWALI

a) Bila kupoteza maana iliyokusudiwa na mwandishi, fupisha aya ya kwanza hadi ya tatu. (maneno 40 – 45) (alama 7)

MATAYARISHO
NAKALA SAFI

b) Dondoa hoja muhimu zinazojitokeza katika aya ya nne na ya tano. (Maneno 45 – 50)
(alama 5)
MATAYARISHO
JIBU

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a) Andika sifa mbili mbili bainifu za sauti. (alama 2)
i) /e/
ii) /n/

b) Eleza tofauti ya kisarufi ya maneno yaliyopigiwa mstari.
(alama 2)
i) Hiki ni kitabu cha mwalimu
ii) Hiki ni cha mwalimu

c) Ainisha viambishi na mzizi katika kitenzi
(alama 3)

Hawakunichokoza

d) Bainisha aina za vishazi katika sentensi hii
(alama 2)
Watoto walioachwa mayatima wamesaidiwa

e) Andika kwa ukubwa na udogo (alama 4)
Sahani zote zimepelekwa nyumbani
i) Ukubwa
ii) Udogo.

f) Andika sentensi yakinishi kutokana na sentensi ifuatayo.
(alama 2)
Utawala mkubwa wa meya haukuzuilika.

g) Andika katika usemi wa taarifa
“Nitawatuza watahiniwa wote watakaopita mtihani mwaka huu”. Mwalimu aliwaahidi wazazi.
(alama 3)

h) Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo
(alama 3)
Juma alimchinjia mamake mbuzi mzuri kwa kisu.

i) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo. (alama 2)
Wanafunzi waliandikiana barua.

j) Ainisha vielezi katika sentensi zifuatazo.
(alama 2)
(i) Jaribu kujitahidi kisabuni usianguke mtihani.
(ii) Wachezaji wote wameingia uwanjani..

k) Eleza matumizi mawili ya kistari kifupi. (alama 2)

l) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali.
(alama 4)
Ouma alianguka mtihani ila Kamau alifuzu vizuri.

m) Eleza matumizi ya “na” katika sentensi ifuatayo.
(alama 2)
Wageni na wenyeji walikimbiliana.

n) Bainisha kiima na chagizo katika sentensi ifuatayo.
(alama 2)
Walimu hao walifanya kazi yao kwa bidii.

o) Unda nomino mbili mbili kutokana na vitenzi vifuatavyo.
(alama 2)
i) Jaribu
ii) Chuma

p) Kamilisha jedwali (alama 2)

Kufanya	Kufanyiwa	Kufanyisha

La		
Fa		

p) Fafanua aina ya hali iliyotumika katika sentensi hii.
(alama 1)
Wanasiasa wengi hulalamika kila mara.

4. ISIMU JAMII

a) Taja mambo manne yanayopelekea kufifia/kufa kwa lugha,
(alama 4)

b) Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yafuatayo
.....napinga hoja iliyotolewa na waziri wa Finance ya kupiga marufuku matumizi ya plastic bags. Baada ya kumsikiza kwa makini, napenda kumkosoa kwa kudhihirisha kuwa..... kulingana na kifungu nambari .....

i) Bainisha sajili ya mazungumzo hayo. (alama 2)

ii) Huku ukitoa mifano mwafaka, eleza sifa nne za sajili hii kwa mujibu wa kifungu hiki.

MTIHANI WA MAKADIRIO WA WILAYA YA GATUNDU
Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Sekondari (K.C.S.E)
102/3
KISWAHILI
Karatasi ya 3
FASIHI

Tamthilia; Mstahiki Meya
Timothy M. Arege
Swali La Lazima

1. Au unafikiri pakawa na fursa nyingine hii leo ya kuchagua viongozi matokeo yatakuwa tofauti sana?.....Ukipanda huwezi kuvuna kunazi.

a) Eleza muktadha wa maneno haya?
(alama 4)
b) Mzungumzaji na mzungumziwa wanafanana. Thibitisha.
(alama 8)
c) Taja mbinu za kifasihi zinazojitokeza katika muktadha huu.
(alama 4)
d) Eleza maovu yoyote manne yanayokumba wanacheneo.
(alama 4)

SEHEMU B: RIWAYA
Kidagaa kimemwozea
Ken Walibora
Jibu swali la 2 au 3

2. Angewezaje kumwambia kwamba mifugo wake walikuwa katika ukalifu tangu Amani kutiwa mbaroni?"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili? (alama 4)
b) Mzungumziwa hakuwa na utu. Fafanua. (alama 8)
c) Toa mifano ya maudhui ya ukatili katika Riwaya ya kidagaa kimemwezea inayofaa.
(alama 8)

3. Riwaya ya kidagaa kimemwozea inaonyesha jitihada za vijana kujenga jamii mpya. Thibitisha kwa kutoa mifano.
(alama 20)

4. **SEHEMU C: USHAIRI**
Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali:

Hakika siku ya leo, ni siku ya majivuno
Basi pasiwe na choyo, na **usonono**
Tulekezane yaliyo, unawiri Muungano.

Tuzisafisheni nyoyo, pasiwe na miguguno
Yaongoke tutakayo, kusiwe na mabishano
Mbegu hii tupandayo, ilete mema mavuno.

Tufungulie upeo, Mola usiye mfano
Pa kitasa na komeo, tupite bila kinzano
Tupitishe njia hiyo, pasina masongamano

Twakuomba uumbao, mkono **vyanda** vitano
Tushikane hii leo, tuwe moja tangamano
Tupendane kwa pumbao, hali na maridhiano

Aliye ana machukiyo, adui wa Muungano
Naazibe masikiyo, asisikie maneno
Kisha awe kibogoyo, asiwe na moja jino.

Ya Ilahi ujalie, juu wetu Muungano
Nuru yake izagae, na nguvu za mapigano

Hasidi mpe hakie, mateso yaso mfano

Watamati komeleo, kuimba kwangu hukuno
Nataka maendeleo, yasiyo na malumbano
Daima tuwe ni ngao, palipo **msagurano**

4. (i) Lipe shairi hili anwani yake. (alama 2)
(ii) Liweke shairi hili katika bahari mbili ukitumia:
(alama 2)
Idadi ya
(i) Mishororo
(ii) Vina
(iii) Onyesha muundo wa shairi hili. (alama 5)
(iv) Andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari.
(alama 3)
(v) Toa mifano ya idhini ya kishairi iliyotumika katika shairi hili.
(alama 6)
(vi) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi.
(alama 2)
(i) Usonono –
(ii) Msagurano –

SEHEMU D: FASIHI SIMULIZI Jibu swali la 5 au 6

a. Eleza maana ya: (alama 4)
i) ulumbi
ii) soga
b) Eleza umuhimu wa soga katika jamii yetu. (alama 8)
c) Fafanua sifa bainifu za mlumbi (alama 8)
i)
a) Maghani ni nini? (alama 2)
b) Eleza aina zifuatazo za maghani?
(alama 8)
i) Tondozi
ii) Sifa
iii) Tendi
iv) Rara
c) Fafanua sifa za maghani.
(alama 6)
a) Eleza majukumu ya maghani. (alama 4)

SEHEMU E: HADITHI FUPI
DAMU NYEUSI NA HADITHI ZINGINEZO
KEN WALIBORA NA SAID A. MOHAMED)

(i) Mwana wa Darubini (Kristina Mwende Mbai)
"Ulijuaje alikuwa anaangalia kwetu?
a. Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b. Hadithi hii inaonyesha matatizo ya kijamii. Fafanua.
(alama 8)
c. Eleza yaliyotokea baada ya mazungumzo haya. (alama 8)

MTIHANI WA MAKADIRIO WA WILAYA YA GATUNDU
Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Sekondari (K.C.S.E)
102/1
KISWAHILI
Karatasi I
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
SWALI LA KWANZA
Muundo wa ripoti rasmi uzingatiwe.

- Kichwa – kiwe kwa herufi kubwa
- Utangulizi – Historia fupi ya suala linalotafitiwa itolewe ikiwa ni pamoja na kutaja wanajopo watano na muda wa kutafiti.
- Yaliyoshughulikiwa – Taratibu za kufanyia utafiti ziorodheshwe. Hizi ndizo zitafuatwa baadaye katika mwili wa insha.
- Mwili/matokeo ya uchunguzi. Haya ni masuala yaliyoshughulikiwa na jopo pamoja na utaratibu uliofuatwa katika kutafiti yale yaliyoagizwa.
- Matatizo; iwapo jopo lilikumbana na matatizo yoyote, matatizo hayo huorodheshwa chini ya kijianwani cha matatizo.
- Hitimisho: sifa za ripoti zirejelewe.
- Mapendekezo: Jopo litoe msimano wake baada ya kukamilisha utafiti.
- Jina, sahihi na cheo cha mtayarishi pamoja na tarehe ziandikwe.

Tanbihi: Mtahiniwa asipofuata sura ya ripoti rasmi, aondelewe alama 4.

Vidokezo

A. Sababu za undanganyifu
- Kukosa kujiandaa ipasavyo kabla ya mtihani.
- Uzembe wa wanafunzi katika kujiandaa masomoni.
- Baadhi ya wazazi huwa wakali sana kwa watoto wao wasiofanya vyema masomoni.
- Wazazi wengine kutaka watoto wao wajiunge na vyuo vikuu kwa njia yoyote ile.
- Ufisadi kuwa wa hali ya juu kiasi kwamba walioaminiwa kuweka siri katika mitihani kuhongwa na kutoa nakala za mitihani hiyo.
- Ni njia ya kuchumia mali kwa watu wengine kwani soko i tayari ya mitihani.
- Mashindano miongoni mwa shule
- Wakuu wengine kutaka sifa baada ya matokeo ya mitihani.
- Limekuwa kama jambo la kawaida katika baadhi ya maneo fulani.
- Teknolojia mpya – matumizi ya simu na mtandao.

B. Madhara ya undanganyifu
- Matokeo ya mitihani kwa jumla kuathiriwa vikali kwani viwango vingine vya alama huwekwa juu sana.
- Watu wengine huishia jela kwa kujihusisha na undanganyifu huu.
- Watahiniwa waliohusika kukosa matokeo ya mitihani.
- Wanafunzi wasio na hatia huathirika kwa matokeo yao ya mitihani.
- Kukosa imani kwa taasisi ya kushughulikia mitihani nchini (utunzi na usahihishaji)
- Wasiostahili kujiunga na vyuo vikuu na kuwanyima haki wanaostahili.
- Mitihani bandia kuingia sokoni kwa madai kuwa ni ya kweli.
- Matokeo mabaye baada ya kudanganya hufanya wanafunzi wengine kujitoa uhai.
- n.k

c. Jinsi ya kukabiliana na undanganyifu (suluhisho)
- Wanafunzi walenge kupata alama kulingana na uwezo wao.
- Wazazi wawe na matarajio ya matokeo ya mitihani kulingana na uwezo wa watoto wato.
- Shule zishindane kulingana na kiwango chao masomoni.
- Walimu watayarishe watahinwa vilivyo.
- Mfumo wa elimu ufanyiwe marekebisho ili usiegemee kupita mitihani pekee, bali uangazie vipawa vya wanafunzi katika nyanja zingine k.v. michezo, sanaa, nyimbo n.k.
- Wasimamizi wa shule, mitihani na walimu kwa jumla wawe macho wakati wa mitihani.
- Hatua kali zichukuliwe kwa wale watakaojihusisha na undanganyifu n.k

Tanbihi

Zingatia hoja zingine za watahiniwa

1. Katika kujibu swali hili, mtahiniwa anaweza:

a) Kuunga mkono kauli hii

b) Kupinga kauli hii
c) Kuunga na kupinga kisha atoe msimamo wake.
Vidokezo.
Kuunga mkono
Changamoto za usalama.
- Magaidi wanaweza kutokea popote na kuvamia watu bila tahadhari.
- Raia kuwa na hofu wanapotekeleza majukumu yao ya kila siku.
- Watu kupoteza maisha yao uvamizi unapotokea.
- Vijana kutekwa nyara na kuingizwa katika makundi ya kigaidi.
- Vijana kuingizwa katika makundi ya kigaidi na kuzorotesha usalama zaidi.
- Watalii wa kigeni kuhofia kutalii nchini.

Changamoto za maendeleo
- Serikali kutumia kiasi kikubwa cha rasilmali kuajiri askari wa kulinda usalama.
- Maeneo yanayoaminika kuwahifadhi magaidi hawa kukosa wahudumu.
- Watu kupoteza mali wakati wa mashambulizi.
- Wawekezaji kuwa na uoga kufanya biashara nchini.
- Serikali kulazimika kuchukua hatua zenye gharama
- Kubwa kuzuia ugaidi k.v.
    - Ujenzi wa ua kwenye mipaka ya nchi jirani
    - Mafunzo ya kikosi cha walinda usalama, pamoja na mishahara yao.
    - Ununuzi wa magari ya kulinda usalama.

2. Hii ni insha ya methali
Mtahiniwa anaweza kufahamu methali kimaana na kimatumzi (si lazima) kilicho muhimu ni kisa kinachoonyesha ukweli wa methali hii.
- Mwenye kovu – Mtu aliyewahi kukumbwa na jambo fulai baya/lenye kuumiza/lenye kusababisha uchungu fulani.
- Sidhani kapoa – usichukulie kuwa amesahau jambo lile na kutulia.

Maana
Mtu aliyewahi kubumbwa na jambo lenye kutia uchungu atabaki akilikumbuka hasa kwa hasira.
Atakuwa akitafuta nafasi ya kupiliza kisasi hasa ikiwa jambo lile lilisababishwa na mtu anayemjua.
Tanbihi
Kisa kionyeshe hali ya kulipiza kisasi kwa uovu aliotendewa mtu.
Mtahini akikosa kutunga kisa kitakachooana na methali, hajajibu swali.

4. Ni lazima mtahiniwa akamilishe insha yake kwa maneno haya. Sentensi yenye mdokezo iwekewe maneno ya kwanzia ili itiririke vyema.
Kisa kidhihirishe kuwa mwanafunzi alipuuza ushauri/wasia wa mwalimu na hatimaye akajutia mapuuza hayo.

MTIHANI WA MWIGO GATUNDU SOUTH
CHETI CHA KUHITIMU ELIMU YA SEKONDARI 2015
102/2
KISWAHILI
Karatasi 2
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
UFAHAMU

a) Hugeuza malighafi inayopatikana kuwa bidhaa za kutumiwa na watu. (al. 2)
b) Masoko finyu kutokana na uwezo wa wanunuzi. (al. 2)
c) (i) Vina uwezo wa kuwaajiri wafanyakazi wengi.
(ii) Hakuhitaji mtaji mkubwa.
(iii) Ni rahisi kujaribisha bidhaa mpya kwa kiwango kidogo cha kiwanda kidogo.
(iv) Huwa chocheo kubwa la usambazaji wa viwanda hadi maeneo ya mashambani.
(v) Watu wengi wanaweza kuanzisha viwanda hivyo.
d) (i) Nafasi za ajira zimesambazwa.
(ii) Hutoa mweneo mzuri wa kimapato
(iii) Huboresha uwezo wa kiununuzi wa umma.
(iv) Ni msingi mkubwa wa kujitegemea kiuchumi.
e) (i) Kuanzisha
(ii) Kazi
(iii) Hamu
Adhibu kosa la kisarufi litokeapo mara ya kwanza hadi makosa sita (½ x 6 = 3)
Adhibu kosa la hijai litokeapo mara ya kwanza hadi makosa sita (½ x 6 = 3)
Adhibu kosa la hijai hata pale amekosea jibu.

MUHTASARI

A (i) Kupitisha wakati
(ii) Kitulizo cha moyo
(iii) Kuendeleza hisia, kuburudisha na kuzuzua
(iv) Kukubaliana na tajriba mbaya
(v) Unampa fursa ya kutoa moyoni simanzi na dhiki
(vi) Kukomaza akili
(vii) Kuhamasisha umakinifu katika masomo mengine
(viii) Mbinu ya kukumbuka
Maneno 35 – 40
7 x 1 = 7

b) (i) Watoto hujipatia mbinu za werevu shuleni.
(ii) Watu wazima waliojifunza muziki kabla ya miaka 12 huwa na utumizi mzuri wa maneno magumu na msamiati.
(iii) Husaidia watoto walio na kasoro ya kuzungumza/walio na ulimi mzito wa kuzungumza.
(iv) Husaidia watu wazima walio na shida ya kigugumizi.
(v) Watoto huweza kujifunza kuelewa mila na tamaduni. 5 x 1 = 5
Tanbihi: Mwanafunzi atuzwe jumla ya alama 3 za mtiririko kisha kukadiria sehemu zote mbili.

MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a) Sifa za sauti
(i) /e/ - irabu ya mbele na kati.
– Hutamkwa midomo ikiwa imetandazwa.
/n/ - Konsananti ya nazali/:/ king'ong'o.
– Sauti ya ufizi (½ x 4 = 2)
b) (i) Kivumishi (kionyeshi)
(ii) Kiwakilishi (kionyeshi) (1 x 2)
c) Ha – kikanushi cha nafsi
Wa – kiambishi cha nafsi (ya tatu wingi)
Ku – kikanushi cha wakati (uliopita)
-ni- - Mtendwa
- chokozi – mzizi
-a- - kiishio (½ x 6)

d) Watoto wamesaidiwa – kishazi huru
Watoto waliachwa mayatima – kishazi tegemezi (1 x 2)

e) (i) Kubwa: Masahani/majisahani yote yamepelekwa majumbani.
Udogo: Visahani/vijisahani vyote vimepelekwa vijumbani. (2 x 2)
Utawala mkubwa wa meya ulizuilika. (1 x 2)

f) Mwalimu aliwaahidi wazazi kuwa angewatuza watahiniwa wote ambao wangepita mtihani mwaka huo (½ x 6)

g) Mamake – kitondo (1)
Mbuzi – kipozi (1)
Kwa kisu – ala (1)

i) Wanafunzi waliandika barua kwa niaba ya wengine. (1)
Wanafunzi waliandika barua mmoja kwa mwingine (1)

j) Kisabuni – namna mfanano. (1)
Uwanjani – mahali (1)

k)
- Kukata neno ufikapo ukingoni mwa karatasi.
- Kuungia baadhi ya maneno yaasili ya kigeni k.m idd-ul-fitri
- Kuonyesha neno linalohusisha nomino mbili k.m kidhibiti mwendo
- Kutenganisha silabi za neno
- Kuonyesha kipindi cha muda Fulani 1998 – 1999
- Kuandika tarehe 21-3-1999

l)

S						
S1			U	S2		
KN	KT			KN	KT	
	T	N		N	T	E
Ouma	alianguka	mtihani	ila	Kamau	alifuzu	vizuri

m) na – kiunganishi (1)
na – kauli ya kutendeana (1)

n) Walimu hao – kiima (1)
Kwa bidii – chagizo (1)

o) (i) Jaribu – mjarabu/mijarabu
jaribio/majaribio
kujaribu
(ii) Chuma– Uchumi
-Chumo
-Kuchuma
-Mchumi

p)

Kufanya	Kufanyiwa	Kufanyisha
La	Liwa	Lisha
fa	fiwa	fisha

(½ x 4)

q) Mazoea/kurudiarudia/kila mara (1 x 1)

4. **ISIMU JAMII**

a) (i) Lugha moja kusonewa hadhi na isiyoonewa hadhi hufifia.
(ii) Sababu za kiuchumi – watu huishi mijini na kuacha lugha ya kwanza.
(iii) Lugha kuwa na idadi ndogo ya wazungumzaji.
(iv) Ndoa za mseto.
(v) Kuhamia kwingine – watu huishi na kuingiliana na kundi jingine.
(vi) Mielekeo ya watu – wanapoipendelea lugha moja na kuidharau nyingine.
(vii) Kisiasa – Lugha moja kupendelewa kuliko nyingine na viongozi. (zozote 4 x 1)

b) (i) Sajili ya bungeni
(ii)
- Kuchanganya msimbo/ndimi – waziri wa Finance.

- Msamiati maalum – hoja, kifungu nambari.
- Lugha ya adabu – napenda kumkosoa

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
MTIHANI WA MWIGO GATUNDU SOUTH
102/3
KISWAHILI
Karatasi 3

1. a) Haya ni maneno ya Diwani III akizungumza na siki wakiwa nyumbani kwa Diwani III. Hii ni baada ya mgomo wa kufanya kazi kufanyika mjini. 4 x 1
   b)
- Wazalendo – wanapigana na uongozi mbaya wa cheneo
- Ni wanamapinduzi – wanajaribu kuleta uongozi mpya.
- Ni wenye ari katika kazi yao – siki hafuti kazi yake.
- Ni wenye kuaminika – siki anamwanini Diwani III anapozungumza.
- Ni wenye utu – siki alijitahidi katika zahanati ya cheneo.Zozote 4 x 2

c) Balagha
methali
(Mwanafunzi atoe mifano) zozote 2 x 2

d) Migomo ya wafanyakazi
ukosefu wa dawa
mishahara mjini
ukosefu wa mlo wenye lishe. (4 x 1)

SEHEMU B: RIWAYA

2. Haya ni maneno ya mtemi Nasaba Bora kwa nduguye Majisifu wakiwa kwa mtemi Nasaba Bora. Huu ni wakati alipotembelewa na mwalimu majisifu kwake. zozote 4 x 1

   b) (i) Hakupenda watoto wake walemavu
   (ii) Hakufunza kama alivyotakikana katika shule ya upili ya Nasaba Bora.
   (iii) Alikuwa mlevi na mpyaro
   (iv) Aliwibia mswaada wa kidagaa kimemwozea
   (v) Hakuelewana na nduguye zozote 4 x 2

   c) Mswaada wa Amani uliibwa na mwalimu majisifu.
- Unyakuzi wa ardhi ya Chichiri Hamadi na mwinyi Hatibu mtembezi na mtemi Nasaba Bora.
- Kuchoma makao ya mamake imani
- Kufunga Amani na Imani kizuizini bila hatia yote.
- Kuwekelea Yusufu makosa na kumuweka kizuizi.
- Kuweka kitoto nje ya kibanda cha Amani.
- Kupiga Amani kwa kufikiria ana uhusiano na Zuhura na kumwacha akiwa amezirai.
- Kutombeba Amani alipokuwa akitoka siku ya wazalendo. Zozote 4 x 2

3. Madhubuti anachagua kujitafutia kazi yake badala ya ile babake alimtafutia.
- Imani alikunywa maji ya mto kiberenge na kuvunja mwiko uliokuwepo.
- Amani na Imani walikaa chumba kimoja bila kufanya uzinifu wowote.
- Amani aligawa shamba lao kwa watu wengi.
- Imani alilea watoto walemavu wa Dora.
- Amani na Imani walilea kitoto walichopata badala ya kukitupa kama alivyofanya mtemi Nasaba Bora.
- Amani hakulipiza kisasi baada ya mtemi Nasaba Bora kumpiga na kumtupa
- Amani na madhubuti walitafuta ushahidi uliofanya Yusufu achiliwe.
- Amani alikataa kuchukua uongozi baada ya mtemi Nasaba Bora kuondoka.
- DJ aliwasaidia Amani na Imani kupata kazi sokomoko walipoenda. Zozote 10 x 2

4. (i) Muungano
   (ii) Tathlitha
   Ukara
   (iii) Lina mishororo mitatu kila ubeti

Lina ukwapi na utao
Vina vya kati vinabadilika na mwisho havibadiliki
Mizani kumi na sita kila mshororo
Halina kibwagizo.

(iv) Tuweke nyoyo zetu zikiwa nzuri bila kulalamika
Tutakayo yanyooke bila ugomvi
Yale tunayotenda yatuletee mafanikio

(v) Inkisari – Choyo, hakie
Mazida – tuelekezane
Tabdila – machukiyo hunuko
Kuboronga sarufi – ilete mema mavuno

(vi) Usonono – kuhuzunisha
Msagurano – kuzozana

5. Ulumbi – uhodari wa kuzungumza au kuiga mazungumzo kwa usaniina uhodari mkubwa.
Soga – Ni utanzu mdogo wa fasihi simulizi unaotumiwa kwa ajili ya kuchekesha, kukejeli au kuumba au kufanya dhihaka ili kupitisha wakati.

b)
- Hukejeli matendo Fulani ya binadamu kama vile uovu.
- Huburudisha wasikilizaji
- Huelimisha jamii
- Huelekeza wanajamii
- Huonyesha utani ulioko baina ya wanajamii zozote 4 x 2

c)
- Huwa na ujuzi wa kina wa utamaduni husika
- huwa na tajriba ndefu ya maisha
- Huwa na ufundi wa kutumia tamathali za usemi
- Huvalia malemba ili kuvutia hadhira
- Anastahili kuwa na sauti inayosikika bila matatizo yoyote.
- Anastahili kuwa mwenye ushawishi mkali.
- Ana uwezo wa kushirikisha hadhira yake
- Anatumia miondoko na ishara
- Ana uwezo wa kughani mfululizo. Zozote 8 x 1

6. Maghani ni utungo wa kishairi ambao hutongolewa kwa kutumia sauti iliyo kati ya uimbaji na uzungumzaji, yaani kalimia. (al 2)

B. (i) Tondozi – Ni utungo wa kutukuza watu, wanyama au vitu vingine.
(ii) Sifa – Ni utungo unaosimulia kwa undani matukio ya kishujaa yanayohusiana na mtu anayesifiwa kuanzia mwanzo wa mapambano hadi ushindi unapopatikana.
(iii) Tendi – Ni usimulizi mrefu wa kishairi unaotungwa papo kwa papo na huelezea tukio kuu la kihistoria kwenye jamii.
(iv) Rara – Utungo wa kishairi wenye ubunifu mkumbwa unaokusudia kusisimua na unatongolewa kwa kuibwa au kughanwa ukiambatanishwa na ala za muziki.

c) Ni tungo za kishairi
- Husimulia matukio kwa kirefu
- Hutungwa papo hapo na kusemwa mbele ya hadhira
- Huwa na majisifu
- Hutolewa na mtu mmoja au kundi la watu.
- Huwa na uigizaji
- Hutumia tamathali za usemi zozote 3 x 2

d)
- Kuliwaza
- kuhamasisha
- Kutia moyo
- Kusifu
- Kukashifu
- Kujigamba

- Kuburudisha zozote 4 x 1

7. a) Haya ni maneno ya rafikiye mwakitawa akimwambia mwakitawa kuhusu mama mmoja ambaye amekuwa akiangalia nyumba yao kwa kutumia darubini. (4 x 1)

b)

- Uuzaji wa binadamu k.m kananda anauziwa dereva wa kongo
- Uzinifu kati ya mwatela na kananda.
- Wizi wa watoto k.m mwakitawa aliibiwa kutoka kwa mamake na Mwatela.
- Ukatili k.m kananda aligongwa kwa jiwe na Mwakitawa. Zozote 4 x 1

c)

- Mwakitawa alishikwa na woga mwingi
- Babake mwakitawa alifikiria kulipa majambazi wamwangamize kananda
- Mwakitawa alipiga mamaye kananda kwa jiwe na kumumiza
- Babake Mwakitawa alihuzunika sana baada ya kusikia kananda amepigwa,.
- Kulitokea ugomvi baina ya Mwatela na mkewe na akataka mwakitawa kuelezwa kweli kuhusu mamake.
- Kananda alilazwa ili apate matibabu.
- Mwatela pia alilazwa na kupata matibabu.
- Mwatela alitafuta wakili na kumrithisha mali yake kananda.
- Mwakitawa na mamake kananda walikutana na kuungana naye zozote 8 x 1 = 8

TATHMINI YA PAMOJA KAUNTI NDOGO YA GATUNDU KASKAZINI 2015
Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Sekondari (K.C.S.E)
102/1
Kiswahili
Karatasi 1
(Insha)

1. Umeteuliwa kama katibu wa kamati iliyochunguza kuzorota kwa elimu katika wilaya yako. Andika ripoti kuhusu matokeo ya uchunguzi huo.
2. Uvumbuzi wa tarakilishi una athari kubwa katika maisha ya binadamu. Jadili.
3. Fahali wawili wapiganapo nyasi ndizo ziumiazo.
4. Andika kisa kitakachoanza kwa;
   Nilikaa pale kwa mseto wa hisia, nisijue kama nilifurahishwa ama nilihuzunishwa na kisa hicho.....

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA GATUNDU KASKAZINI 2015
Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Sekondari (K.C.S.E)
102/2
KISWAHILI
KARATASI 2
(Ufahamu, Ufipisho, Sarufi na Isimu Jamii)
UFAHAMU (alama 15)

1. **Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.**

Nimekaa kutafakari kwa kipindi kirefu, juu ya mabilioni ya pesa ambayo yametengwa na serikali ili kudhamini miradi ya maendeleo ya wanawake. Kina mama au wanawake wengi wanakiri na kusema kwamba fedha hizo zimewezesha kuwaondoa katika lindi la unyanyasaji kutoka kwa waume zao. Kwani kila mmoja anamheshimu mwenzake kwa sababu ya kipato alicho nacho. Wengi wameweza kuanza biashara ndogondogo ambazo huwaletea angaa kipato kidogo.

Ukweli ni kwamba fedha hizi zimesaidia kuwatoa wanawake wengi katika unyanyasaji, kwani wengi wanaweza kuanzisha kazi za ujasiriamali na hata kuendesha shughuli mbalimbali za maendeleo. Kutokana na mafanikio haya, wabunge waliopitisha hoja bungeni za kuanzisha mpango huu wa kuwakwamua wanawake kimaendeleo wanafaa kupongezwa. Mafanikio haya yamewafanya akina mama kujikimu kimaisha na hivyo kutowatengemea wanaume katika kila jambo.
Ukitaka kujua ukweli kuhusu hili, nenda kwenye masoko utaona akina mama jinsi wanavyyohangaika na biashara zao. Kwa hivyo, ujasiriamali huendelezwa na akina mama zaidi na hivyo wanapaswa kuwezeshwa kwa hali na mali.

Akina mama pia wanafaa kupongezwa kwani wameamua kujitosa kukopa fedha kutoka kwenye taasisi mbalimbali na fedha. Fedha hizo kwa kiwango kikubwa zimewainua kutoka katika ufukara uliokithiri hadi katika maisha ya heshima. Wale ambao hawajaribu kuchukua mkopo ni muhimu wafanye hivyo ili wajikimu kimaisha.
Maisha ya sasa ni magumu, hivyo yanahitaji kusaidiana kwa kila hali na mali. Wanaume kwa wanawake ni vyema wachange bia ili wazumbue riziki. Ushirikiano utarahisisha maisha yao. hata hivyo, sio tu akina mama hao wameondokewa na unyanyasaji waliokuwa wakiupata ndani ya nyumba zao, toka kwa akina baba, bali hata masualama ya mrundikano wa kesi za kugombea ardhi kwa akina mama, zimepungua. Sababu ni kwamba akina mama wengi wameweza kujitafutia ardhi wenyewe kwa fedha walizonazo.
Ukweli ni kwamba hali imebadilika kinyume na hapo awali, ambapo majumba ya kifahari na mashangingi yalikuwa hifadhi ya wanaume, siku hizi wanawake wanamiliki hayo yote.

Maswali.

1. Taja dhamira **mbili** za makala haya. (alama 2)
2. Eleza ni kwa nini msimulizi anawapongeza wabunge. (alama 2)
3. Wanaume walikuwa wakirudisha nyuma maendeleo nchini kivipi? (alama 2)
4. Sera za serikali zimesaidia wanawake kivipi? (alama 3)

5. Eleza kwa nini baadhi ya wanawake wanaishi katika lindi la umaskini kulingana na makala haya. (alama 3)
6. Eleza maana ya msamiati na mafungu yafuatayo kama yalivyotumika katika makala haya. (alama 3)
   i) kutafakari.
   ii) kuwaondoa katika lindi la unyanyasaji.
   iii) Riziki.

UFUPISHO (alama 10)

2. **Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali kulingana na maagizo**.

Imesemwa na kurudiwa tena kwamba, iwapo tuna maono ya kujiondoa katika umaskini wa kupindukia, ni lazima tukipe kilimo umuhimu. Zaidi ya wakenya milioni kumi wamo katika hatari ya kufa njaa katika maeneo mbali mbali kwa sasa kufuaia uhaba wa chakula nchini.

Kiini kikubwa cha njaa hiyo ni mapuuza ya muda mrefu katika sekta ya kilimo. Imesahaulika kuwa karibu asilimia sabini na tano ya wakenya wanategemea kilimo kwa chakula na mapato ya kifedha kila siku. Kilimo hutoa karibu robo tatu ya nafasi za kazi kwa mwananchi na pia kuletea serikali karibu robo ya mapato yake kutokana na mauzo ya mazao katika mataifa ya nje.

Wataalamu wa maswala ya zaraa wanaeleza kuwa pato la nchi linalotokana na kilimo huangamiza njaa mara nne zaidi ya mapato yanayotokana na shughuli nyinginezo za kiuchumi. Hiyo ni kwa sababu shughuli za kilimo hulenga kuzalisha vyakula moja kwa moja.

Imebainika kuwa, katika mataifa mengi yanayostawi, asilimia sabini na tano ya wananchi huishi katika maeneo ya mashambani na idai hii hutegemea kilimo kujimudu kimaisha ilhali hapa Kenya ni asilimia nne pekee ya bajeti inayowekezwa katika kilimo. Kwa wakati huo, ushuru unaotozwa bidhaa za kilimo katika maeneo haya umebainika kuwa mkubwa. Hii imepelekea uwekezaji katika kilimo kupungua na hivyo kuchangia kukithiri kwa baa la njaa.

Wakati umewadia kwa serikali za Afrika na wapangaji wa masuala ya uchumi kuweka juhudi maradufu katika kushabikia kilimo ili kumaliza njaa na umaskini. Kuna haja ya kuwajulisha, kuwahimiza na kuwaelimisha wakulima wa mashamba madogo madogo kuhusu mihimili ya zaraa kama vile uzalishaji wa matunda na mboga ufugaji wa ndege, samaki na ng'ombe mbali na kuweka mikakati ya kuanzisha nafasi za kazi katika sekta ya kilimo.

Serikali itafikia lengo hili iwapo itaanza kufadhili kilimo, kupunguza gharama za pembejeo za kilimo, kuweka sera zinazodhibiti uuzaji na ununuzi wa vyakula hasa baina ya mataifa na kuongeza sehemu ya bajeti inayotengewa kilimo. Bila hilo hatutakuwa na lingine bali kukimbilia mataifa yaliyostawi kuomba misaada ili kuwanusuru raia wetu kutokana na ghadhabu ya njaa.

Maswali.

a) Fupisha aya mbili za mwanzo kwa maneno 50-55.
(alama 8)
Matayarisho.
Jibu

b) Bila kubadili maana, fupisha aya mbili za mwisho. (maneno 55 - 60.)
(alama 6)
Matayarisho.
Jibu

3. **Matumizi ya lugha.** (alama 40)

a) Toa sifa bainifu za sauti /h/
(alama 3)

b) Andika sentensi ifuatayo ilete dhana tatu tofauti.
(alama 3)
Mwaura amekuja.

c) Nyambua kitenzi Lewa katika kauli ya kutenduka kisha utungie sentensi.
(alama 2)

d) Yakinisha sentensi ifuatayo katika hali ya udogo.

(alama 2)
Sitakununulia nguo wala kukutembeza mjini usipomaliza mkate huo.

e) Andika katika umoja. (alama 2)
Nyaraka zetu ziliwasilishwa rasmi kwenu na madiwani wa vyama tawala.

f) Andika sentensi ifuatayo kwa kufuata maagizo. (alama 2)
Nimewaleta askari kituoni ili wawalinde wananchi wote wanaosumbuliwa na majambazi.
(Anza: Wananchi ...)

g) Iandike sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa.
(alama 3)
"Leo nitachimba mtaro uelekeze maji shambani mwangu." mkulima alisema.

h) Tumia neno 'hadi' kama kihusishi cha; (alama 2)
i) Wakati
ii) Mahali.

i) Bainisha matumizi ya viambishi vilivyopigiwa mstari. (alama 2)
Mwalimu anakuita ofisini umweleze ulikoweka kijitabu chake.

j) Bainisha kiima, shamirisho na chagizo katika sentensi hii.
(alama 3)
Mwanafunzi aliandika insha vizuri.

k) Kanusha bila kutumia 'amba' (alama 2)
Nitavaa viatu ambavyo ni safi.

l) Kwa kutolea mifano mitatu, eleza miundo mitatu ya nomino katika ngeli ya A-WA.
(alama 3)

m) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia mishale.
(alama 4)
Watoto wanacheza vizuri ilhali wazazi wakorofi wanawabeza vikali sana.

n) Ainisha mofimu katika sentensi hii.
(alama 3)
Aliyemletea.

o) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo. (alama 2)

p) Wapatie nafasi wabunge wale.
Unda kivumishi kutokana na kitenzi dhulumu na utungie sentensi.
(alama 2)

4. **ISIMU JAMII.** (alama 10)

a) Lugha ya Kiswahili inakabiliwa na matatizo mengi sana. Taja matano na kuyaeleza.
(alama 5)

b) Fafanua mikakati mitano inayoweza kuchapuza kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Kenya.
(alama 5)

TATHMINI YA PAMOJA KAUNTI NDOGO YA GATUNDU KASKAZINI 2015
Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Sekondari (K.C.S.E)
102/3
KISWAHILI
KARATASI 3
FASIHI

SEHEMU A: USHAIRI.

1. **Swali la lazima.**
   GANGA SHINA.

   1. Maradhi na taathira ya tego na ulemavu
      Zimeshajiri ishara za mti kuwa mbovu
      Vitawi kuporapora mti wazidi ukavu
      Ganga shina la uhai tanzuze hazigangiki

   2. Karibu si masihara kwataka kutuma nguvu
      Na magambo kuyapara hata viache koru
      Haiji thama nusura ukichelea mabivu
      Ganga shina la uhai tanzuze hazigangiki

   3. Makongwe yanayokera yakate kwa maumivu
      Na mizizi ya safura iliyo mikandamivu
      Usiwe nayo subira katika utimilivu
      Ganga shina la uhai tanzuze hazigangiki

   4. Rasharasha sio bora dawa iwe rovurovu
      Imwailie imara hadi isombe kitovu
      Uchome moto sangara mti uwe muangaru
      Ganga shina la uhai tanzuze hazigangiki

   5. Fyekafyeka miparura mimea mitatagivu
      Inayonyonya ujira wa miti mishughulivu
      Nasaha zangu dharura kesho utakula mbivu
      Ganga shina la uhai tanzuze hazigangiki

   Maswali.

a) Eleza umbo la shairi hili. (alama 4)
b) Mwandishi ametumia jazanda katika kueleza jambo fulani. Taja jazanda hiyo na ueleze maana yake. (alama 4)
c) Mwandishi anamaanisha nini anaposema “Kutibu si masihara kwataka kutuma nguvu? (alama 2)
d) Mwandishi ametumia inkisari. Taja mifano miwili na uandike inavyotakikana. (alama 2)
e) Eleza maana ya kibwagizo cha shairi hili. (alama 2)
f) Eleza maana ya msamiati huu kama ulivyotumiwa katika shairi hii; (alama 5)
   i) Kupora pora
   ii) Isombe
   iii) Sangara
   iv) Miparura
   v) mishughulivu.

SEHEMU B: RIWAYA
K. Walibora: Kidagaa Kimemwozea.
Jibu swali la 2 au la 3.

2. Dhuluma ni jambo la kawaida katika jumuiya ya Kidagaa Kimemwozea. Jadili. (alama 20)
3. “Huyu mwendawazimu anakuja nini kwenye sherehe hizi? Anafikiri sherehe hizi ni za watu wenye kichaa kama yeye?”
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili.
   (alama 4)

(b) Eleza tamathali mbili zilizotumika katika dondoo hili.
(alama 4)
(c) Thititisha kuwa anayerejelewa ni mwendawazimu na vile vile si mwendawazimu.
(alama 12)

SEHEMU C: TAMTHILIA

Jibu swali la 4 au la 5.

4. "Tuendelee kusonga mbele hatua kwa hatua. Bwana fedha na kazi ...."
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili.
   (alama 4)
   (b) Taja sifa nne za anayesemezwa.
   (alama 4)
   (c) Baraza la Cheneo limeendelea kuwepo mamlakani kwa mbinu kadha . Jadili.
   (alama 12)
5. Hatua tuchukuazo maishani mwetu zaweza kutuathiri na kuathiri nchi pakubwa. Thibitisha kauli hii ukirejelea mhusika Meya Sosi.
   (alama 20)

SEHEMU D: HADITHI FUPI

K. Walibora na S. A Mohamed: Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine.

Jibu swali la 6 au la 7.

6. "Shangazi wakumbuke watoto. Waonee huruma!"
   (a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
   (b) Fafanua mbinu ya kisanaa inayojitokeza katika kauli hii.
   (alama 2)
   (c) Jadili jinsi maudhui ya ukatili yameendelezwa na wahusika wengine katika hadithi.
   (alama 6)
   (d) Eleza sifa nne za anayerejelewa katika dondoo.
   (alama 8)
7. Mwimba wa kujichoma hauambiwi pole.
   Thibitisha kauli hii kwa kurejelea hadithi zozote kumi. (alama 20)

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI.

8. (a) Maghani ni nini? (alama 2)
   (b) Eleza fani zifuatazo za maghani. (alama 4)
      i) Vivugo.
      ii) Tondozi
      iii) Pembezi
      iv) Rara
   (c) Eleza maana ya neno ULUMBI.
   (alama 1)
   (d) Bainisha sifa za mlumbi. (alama 6)
   (e) Eleza umuhimu wa ulumbi. (alama 3)

KAUNTI NDOGO YA GATUNDU KASKAZINI 2015
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA KARATASI YA KWANZA 102/1- INSHA

Swali la 1.

- Mwanafunzi azingatie muundo / sura ya ripoti Kichwa kionyeshe ripoti ya nani / kamati gani, kuhusu nini n.k

Utangulizi.

- Mtahiniwa aeleze
- Dhamira ya kamati
- Wanakamati pamoja na vyeo vyao.
- Muda ambao kamati ilichukua kufanya uchunguzi.
- Mbinu za ukusanyaji data.

Mwili.

Mtahiniwa zingatie;

(a) **Sababu za kuzorota kwa elimu - mfano**

- Kuzorota kwa nidhamu.
- Upungufu wa walimu.
- Kutamauka kwa wanafunzi kutokana na ukosefu wa kazi.
- Shinikizo la marika.
- Umaskini - wengi wanajihusisha na ajira.
- Wazazi kutowajibika katika malezi.
- Matumizi ya dawa za kulevya. n.k

(b) **Matatizo waliyopata.**

- Uchechefu wa fedha
- Ukosefu wa hamasa miongoni mwa waliohojiwa.
- Ukosefu wa mahali pa kukutana. n.k

(c) **Mapendekezo.**

- Yaambatane na hoja za mwanafunzi.

(d) **Hitimisho.**

- Atoe maoni yake kwa kifupi kuhusiana na suala hili.

Swali la 2.

Athari nzuri / chanya.

- Kuchangia katika elimu - intaneti.
- Kupasha habari kuhusu mambo mbalimbali.
- Husaidia kuboresha uwezo wa mawasiliano na lugha.
- Ni msingi wa burudani katika maisha yetu.
- Hurahisisha kazi na kuokoa wakati.
- Hufanya kazi nyingi.

Athari mbaya / hasi.

- Kuweza kutekwa na tarakilishi kiasi cha kuwa na uraibu usioepukika.
- Kuingizwa kwenye utamaduni mwingine kwa kutazama visa na mambo mengine ya kigeni.
- Kuna mambo yanayoweza kuwa ya fedheha na hasa ikiwa watu wanaotumia tarakilishi waheshimiane.
- Huathiri fikra hasa kutokana na ponografia.
- Kupunguza nafasi za kazi.
- Kuwafanya watu kuwa wavivu.
- Baadhi ya mataifa huwa majaa ya kutupa tarakilishi zilizoharibika - uharibifu wa mazingira.

Tanbihi.

- Mtahini ahakiki hoja zaidi za watahiniwa.
- Mtahiniwa azingatie tarakirishi si uvumbuzi mwingine.
- Mtahiniwa aonyeshe sehemu zote mbili japo si lazima idadi ya hoja iwe sawa.
- Akizingatia upande /sehemu moja asipite kiwango cha C+

Swali la 3

- Fahali wawili - Watu wawili wenye nguvu wanapopigana hawaumizani bali nyasi / watu wa kawaida ndio
- huumia.

- Mtahiniwa atunge kisa kudhihirisha hali hii.
- Akitunga kisa kisichooana na methali hii amejitungia swali na kujibu. Awekwe katika kiwango
- cha D- (01/02)
- Pande zote mbili za methali zionekane.

Swali la 4

- Mtahiniwa aweze kujenga kisa ambacho kinamhusisha yeye mwenyewe kama mhusika mkuu.
- Akimjenga mhusika mkuu mwingine amepotoka (D 03)
- Mtahiniwa asibadili wakati uliohusika katika swali. Akifanya hivyo amepotoka.

TANBIHI.

- Mtahini azingatie viwango vya utuzaji katika kutuza.
- Viwango vyenyewe ni A, B, C, D

KAUNTI NDOGO YA GATUNDU KASKAZINI 2015
MAJIBU YA KARATASI YA PILI 102/2

Ufahamu.

1. (a) Kuelimisha akina mama wazinduke ili waweze kujitegemea kiuchumi.
   (b) Kuhamasisha maendeleo ya wanawake. *al 2*
2. Waliunga mkono sera nzuri ya kusaidia wanawake.
3. Wao waliwanyanyasa wanawake kwa sababu ya ubabedume hasa katika kuwanyima wanawake fursa ya kujikimu kimaisha.
4.

– Wao wamepata mikopo na kuanzisha biashara zao wenyewe.
– Wao wananunua ardhi yao sasa.

5.

– Imani potovu eti wanaume ndio wanastahili kuleta riziki.
– Kutokopa fedha za kuanzisha biashara zao wenyewe.
– Kuamini kwamba utajiri ni hifadhi ya wanaume.

6. (i) Kuwaza / kufikiria kwa makini.
   (ii) Kuwaondoa katika umaskini uliokithiri.
   (iii) Pato la kusaidia mahitaji ya kimsingi ya kila siku.
   Muhtasari.
   (a)

– Ili kujiondoa kutoka umaskini ni lazima tuthamini kilimo/tukipe kilimo umuhimu.
– Mamilioni ya wakenya / zaidi ya wakenyea milioni kumi wanaweza kufa njaa / kwa sababu ya njaa.
– Sababu ya njaa ni kupuuzwa kwa kilimo.
– Wakenya asilimia sabini na tano hutegemea kilimo kwa chakula na fedha.
– Kilimo hotoa nafasi za kazi.
– Huletea serekali robo ya mapato yake. *(kila hoja al. 1 x 6 = 6)*

(b)

– Serikali za Afrika na wanaopanga masuala ya uchumi kujitahidi ili kumaliza njaa na umaskini.
– Wanafunzi wakulima wa mashamba madogo kukuza na kuzalisha matunda na mboga na kufuga wanyama na ndege.
– Kuanzisha nafasi za kazi.
– Serikali kufadhili kilimo.
– Kupunguza gharama za pembejeo.
– Kuweka sera zinazodhibiti kilimo.
– Kuongeza sehemu ya bajeti ya kilimo.
– Tusipofanya hivyo tatuzidi kuomba misaada tutoka mataifa. *(al 6 - kila hoja moja 1 x 6 = al 6)*

a - 06
b - 06
ut - 03

** Makosa ya sarufi; kila kosa ilinapojitokeza,huadhibiwa kwa kuondoa $^1/_2$ alama hadi makosa 6 x $^1/_2$ = alama 3. Mtahiniwa akipata 0 makosa ya sarufi huondolewa.*

** Makosa ya hijai/tahajia huondolewa hadi makosa 6 x $^1/_2$ = al 03*

** Mtahiniwa akizindisha kwa maneno 10 aondolewe alama 1, baadaye akizidisha kwa 5 ondoa $^1/_2$*

** Mwanafunzi asipotiririsha kazi yake asituzwe alama za utiririko hasa akiorodhesha hoja au aandnike vistari kabla ya hoja, atuzwe 0 katika sehemu ya utiririko.*

Matumizi ya lugha.

a) Sifa za sauti /h/ *al 3 x 1 = al 3*
   i) kikwamko
   ii) Sighuna / hafifu
   iii) Hutamkiwa kooni / glota *3 x 1 = al 3*
b) Dhana tatu za sentensi.
   i) Mwaura, amekuja.
   Mwaura amekuja!

Mwaura amekuja?
Mwaura: Amekuja.

c) Lewa - Levuka. *2 x 1 = al 2*
d) Nitakununulia kiguo na kukutembeza kijijini. Ukimaliza kijikate hicho. *2 x 1 = al 2*
e) Kuandika kwa umoja.
Walaka wangu uliwasilishwa rasmi kwako na diwani wa chama tawala. *2 x 1 = al 2*
f) Wananchi wote wanaosumbuliwa na majambazi wameletewa askari kituoni ili wawalinde. *2 x 1 = al 2*
g) Usemi wa taarifa.
Mkulima alisema kwamba siku hiyo angechimba mtaro uelekeze maji shambani mwake. *3 x 1 = al 3*
h) (i) Tulicheza kutoka asubuhi hadi adhuhuri (wakati)
(ii) Wezi walinikimbiza hadi nyumbani mwangu (mahali) *2 x 1 = al 2*
i) Ku - Kiambishi cha nafasi ya pili.
ni - Ndani ya
ko - Mahali.
Ki - Udogo wa nomino. *4 x $^1/_2$ = al 2*
j) (i) Mwanafunzi - kiima
(ii) Insha - Shamirisho kipozi.
(iii) Vizuri – chagizo *3 x 1 = al 3*
(k) Kukanusha kwa kutumia 'amba'
Sitavaa viatu visivyo safi. *2 x 1 = al 2*
(l) Umoja wingi
(i) M - WAMtoto - Watoto
(ii) MW - WA Mwalimu - Walimu
(iii) Ki - VI Kiboroto - Viroboto
(iv) ch - vy Chura - Vyura
(v) m - mi Mtume – Mitume *3 x 1 = al 3*
(m) S - S_1 + U + S_2 S_2 - KN + KT

SI - KN + KT	KN - N + V
KN - N	N - wazazi
N - watoto	V - wakorofi
KT - T + E	KT - T + E + E
T - wanacheza	T - wanawabeza
E - vizuri	E - vikali
U - ilhali	E – Sana

16 x $^1/_4$ = al 4

(n) Kuainisha mofimu
A - kiwakilishi cha nafsi ya tatu umoja.
li - kiwakilishi cha wakati uliopita
ye - kirejeshi 'O'
m - mtendewa
let - mzizi
e – kiendelezi mnyambuliko
a – kiishio *6 x $^1/_2$ = al 3*
(o) (i) wale - kiashiria / kionyeshi - kivumishi
(ii) wale - kupata chakula - (kitenzi) *2 x 1 = al 2*
(p) Kitenzi Kivumishi
Dhuluma Dhalimu *2 x 1 = al 2*

Isimujamii.

1. **Ushindani kutoka lugha nyingine kama kiingereza.**

– Hadhi - Kiswahili kimedumisha.
– Athari za lugha ya mama.
– Mitazamo hasi kuhusu Kiswahili.
– Kutokuwepo kwa sera mwafaka kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa muda mrefu.
– Kuhusishwa kwa lugha ya Kiswahili na dini ya kiislamu / eneo la pwani.
– Wamishenari walieneza dini zao kwa lugha ya kiingereza.
– - Kutokouwa na vitabu vya kutosha vilivyoandikwa kwa Kiswahili.

- Uchache wa wataalamu wa lugha za kikabila katika shule za msingi.
- Kuwepo kwa sheria katika shule kuwa Kiswahili kizungumzwe siku moja kwa juma.
- Lugha imetengwa katika matumizi ofisini za kiserikali.

2. Mikakati inayoweza kuchapuza kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Kenya.

- Sera madhubuti - hii itaelekeza hatua za kupanga na kuendeleza lugha. Pia itabainisha nyanja na
- maeneo ya matumizi ya Kiswahili.
- Kuamrisha Kiswahili - kitumiwe kama lugha ya kufundisha baadhi ya masomo, somo la lazima n.k
- Ufadhili wa miradi ya utafiti.
- Maandalizi mema ya walimu na wataalamu wa Kiswahili.
- Kubuni vyombo vya kukuza Kiswahili.
- Kusisitiza matumizi ya lugha sanifu.
- Serikali kufadhili uandishi na uchapishaji wa vitabu vya sarufi.
- Kuingiza Kiswahili kwenye kompyuta.
- Kuunda jopo la kitaifa la wataalamu - lengo lao ni kutoa mwongozo kuhusu Kiswahili.

KAUNTI NDOGO YA GATUNDU KASKAZINI 2015
MAJIBU YA KARATASI YA TATU 102/3

Sehemu A -Ushairi.

1. (a) Umbo la shairi.
- Beti tano
- Tarbia - lina mishororo minne katika kila ubeti.
- Mtiririko - kina cha kati na mwisho kinatiririka
- Mizani ni 16 katika kila mshororo (8 katika
- ukwapi, na 8 katika utao)
- Lina kibwagizo

(b) Jazanda aliyotumia mshairi ni;
- Mti - bara la Afrika
- Vitawi - nchi za Afrika
- Maradhi - Jamii za Kiafrika kuathiriwa na ukoloni na kuuendeleza.

(c) "Kutibu si masihara kwateka kutuma nguvu"Anamaanisha kuwa ili kuutibu ugonjwa huu ni lazima mtu ajikaze / atie bidii wala si mchezo.

(d) Inkisari
Kutuma - kutumia
tanzuze - tanzu zake

(e) Maana ya kibwagizo.
Ni kuwa ili kuutibu ugonjwa lazima mtu aanzie shinani, maana akitibu dalili tu ugonjwa hautapona.

(f) Maana ya maneno.
i) Kuporapora - kupigapiga.
ii) Isombe - ichukue, ibebe
iii) Sangara - mdudu mkali
iv) Miparura - miti yenye miiba
v) Mishughulivu - miti inayotaabika kutafuta chakula.

Sehemu ya B - Riwaya.
- Askari badala ya kulinda usalama wanampiga mama Imani vibaya.
- Nasaba Bora anahusiana kimapenzi na msichana mchanga Lowela.
- Nasaba Bora badala kuwajibikia umaskini wa raia, anaendelea kuchukua kidogo cha walonacho
- Majisifu kutowahudumia watoto wake ambao wana mahitaji maalumu, analalamika tu.
- Fao kuhusiana kimapenzi na wanafunzi wake.
- Nasaba Bora anaendeleza ufisadi badala ya kuupinga, anawahonga polisi, makarani wa mahakama na mahakimu ili kumtia Yusuf gerezani.
- Nasaba Bora anaamrisha kufungwa kwa Amani na Imani ilhali anajua hawakumwua mtoto.
- Nasaba Bora anapuuza kuwachanja mbwa wake. Mmoja wa mbwa hao anamwuma DJ na kusababisha ugonjwa. Nasaba hamwonei huruma, anasema DJ anastahili hayo.
- Viongozi wanawatelekeza raia kwa magonjwa, ujinga na njaa mf. Matuko Weye.
- Wauguzi katika zahanati ya Nasaba Bora kukataa kumtibu Uhuru - baadaye anakufa.
- Nasaba Bora anafuja hela zilizotengewa kujenga hospitali. Badala yake anajenga zahanati.
- Nasaba Bora kutohudumia Bi. Zuhura ipasavyo.
- Majisifu kumwibia Amani mswaada wake wa Kidagaa Kimemwozea.
- Nasaba Bora kumpiga Amani kwa kushuku kuwa ana uhusiano na mkewe.
- Nasaba Bora kusababisha vifo vya Mwinyi Hatibu na Chichiri Hamadi. *zozote 10 x 2 = 20*

3. (a) Mashaka alijiuliza.
Katika uwanja wa Uhuru kuadhimisha
Siku ya wazalendo
Alimrejelea Matuko Weye. *4 x 1 = 4*

(b) (i) Balagha - Anafikiri sherehe hizi ni za watu wenye kichaa kama yeye?
(ii) Kinaya - Matuko Weye si mwendawazimu hasa kwani alitambua uovu wa Nasaba Bora. *2 x 2 = 4*

(c) **Ni mwendawazimu kwa sababu.**
- Ni mzee aliyekuwa hana mke wala watoto.

- Alivaa kaptura juu ya suruali zote zikiwa mararu.
- Hakumiliki chochote na aliweza kulala popote.
- Hakuvaa viatu tangu atoke vitani Burma kwani alikuwa mwehu.
- - Aliboboja maneno ovyo ovyo na alikula vyakula vya kupolea.
- Alipopewa chakula na kitoweo, alikula kitoweo kwanza kisha akala chakula, km - alikula mboga kisha akala sima
- alikula kuku kisha akala chapati.
- Alipenda kupiga kwata na kusema “mark - time”
- “about turn” na ‘left-right’ alipokumbuka miaka yake ya nyuma jeshini.
- Alisimulia vituko na visa vya vitani ambavyo vilikuwa nusu kweli na nusu mfundiro vya akili yake chakaramu.
- Anarejea korokoro alikopelekwa kama ikulu alipoamshwa na kelele za askari, Imani na Amani.
- Pia anajirejelea kama Mtukufu Rais.
- Anamtusi askari aliyemwita wazimu
- Alipotolewa seli alikataa kutoka na kusema kuwa
- kama Rais anawaamuru askari wawaachilie Imani na Amani.
- Alipopewa chakula alikula na kuondoka bila shukrani. *`6 x 1 = al 6*

(ii) Matuko Weye anaweza kuchukuliwa kama asiye na wazimu kwa sababu.

- Alifaulu kupanda jukwaani na kuchukua kipaza sauti bila kutambulikana.
- Hotuba yake inadhihirisha kuwa anafahamu wanavyonyanyaswa na Mtemi Nasaba Bora na anafahamu maovu anayofanya.
- Pia katika hotuba yake anawachochea watu kwa kusema wanataka Mtemi Nasaba Bora aondoke madarakani na anamtahadharisha Mtemi asione kwenda mbele kurudi nyuma si kazi.
- Alifanya kazi za sulubu ili kujikimu maishani.
- Alisema kuwa anamjua sana Amani na hangeweza kudhuru hata nzi na angeweza kumfanya waziri wa Ufisadi na Magendo.
- Anajua kuwa nchi yao ilitawaliwa na watu wa kutoa kitu kidogo ili wapewe madaraka ndipo anamwambia
- Amani kwa kinaya kuwa akitoa kitu kidogo atamfanya waziri.
- Alishtuka sana alipoambiwa na Amani kuwa amepelekwa seli kwa mauaji na kushikilia kuwa hawezi kuua. Anataka Amani aachiliwe huru na badala yake ashtakiwe yeye kwa haya mauaji.
- Anamtaka Imani aolewe na azae watoto watakaoikomboa Tomoko kutoka kwa mkoroni mweusi.
- Anasema kuwa ni afadhali mkoloni mzungu kuliko mkoloni mweusi kwa sababu anawadharau wenzake vibaya sana.
- Anawaambia askari kuwa mtu mwenye akili timamu hangewatia mbaroni watu wema kama Imani na Amani.
- Anashikilia kuwa mahakama ndiyo yenye hatia kwa kuwakamata Imani na Amani ambao hawakuwa na hatia.
- Anamwambia askari kuwa mama aliyemzaa aliwakosea wanadamu. Pia anamkumbusha askari kuwa hata yeye na Mtemi wao watakuja kuongezewa jina marehemu siku moja.
- Anawalaumu askari kwa kumshika na kumlaza njaa kisha kumwachilia kabla ya kumfikisha mahakamani.
- Anamwambia askari kuwa hata wakimuua watazaliwa Matuko wengine watakaoendelea na harakati za ukombozi kutoka pale alipoachia ili waikomboe nchi yao kutoka kwa mkoloni mweusi katika ukombozi wa pili.
- Alipopewa kasri lililokuwa la Majununi baada ya mapinduzi alifurahi mpaka jina la mwisho. *6 x 1 = al 6*

4. **Mstahiki Meya - Timothy Arege**.

(a) (i) Siki anazungumza na Tatu.
(ii) Wako katika zahanati (ofisini mwa Siki)
(iii) Ni baada ya mgomo kutokea na Siki anamshauri Tatu kuendelea kutekeleza mabadiliko kwa njia ya amani.
al 4

(b) Msemewa ni Tatu.
Sifa.

i. Mtetezi wa haki.
ii. Jasiri
iii. Mzalendo
iv. Mshauri
v) Mwanamapinduzi. 4 x1 = 4

(c) (i) Vitisho
(ii) Uongo
(iii) Sheria kandamizi - riot act, mayors act.
(iv) Propaganda - nyimbo za kizalendo.
(v) Mfumo wa tenga - utawale.
(vi) Mapendeleo.
(vii) Vyombo vya madola (askari)
(viii) Ubaraka na ubarakala (ukaragosi) *6 x 2 = 12*

5. Mstahiki Meya.

- Kuongoza nchi kwa udikteta - wafanyakazi walipogoma alikataa kukutana na viongozi.
- Kutumia uongo - Alidanganya kuwa ameagiza dawa
- na zingefika katika muda wa siku sita. Watu waliendelea kufa na Nesi Waridi akaacha kazi.
- Kutozingatia ushauri mzuri - Alipuuza ushairi wa Diwani III na Daktari Siki. Alifanya maamuzi mabaya
- yanayoangusha utawala wake.
- Kutumia mbinu ya tenga utawale. Kwa kutoa nyongeza ya mishahara kwa mapendeleo. Wasioridhika waliandaa migomo, wakasusia kusafisha mji na wageni wakakatiza safari yao.
- Kutowalipa watu kwa wakati ufaao - Migomo inaandaliwa.
- Madiwani kutolipa kodi. Waliolipa ni wale wa tabaka la chini wenye mapato madogo. Uchumi wa baraza
- unazorota.
- Kutumia askari kuwatesa wananchi – Wananchi waliumia na mwishowe wakaungana kupambana na meya kupitia kwa migomo.
- Kutumia vitisho- Alitisha kuwafuta kazi wafanyakazi waliogoma. Hili liliwatia motisha zaidi ya kuandaa
- migomo iliyoangusha utawala.
- Kutumia vibarakala - Diwani I and II walimshauri vibaya, nchi ikawa kwenye matatizo na utawala wake ukaporomoka.
- Kuuza fimbo ya meya - ingekuwa hasara kwa mji pamoja na hatari ya kugunduliwa baadaye wizi huo.
- Kumtumia mhubiri - Alijificha ndani ya dini na kumlipa mhubiri pesa nying hivyo kufilisisha baraza.
- Kutumia propaganda - Kuwachezea wananchi nyimbo za uzalendo. Hatimaye walichoshwa na maneno
- matupu walitaka vitendo.
- Kutumia sheria kali za kujilinda (kv. mayor's act, riotact) wananchi waliumia na wakaandaa migomo ya kutetea haki zao. *10 x 2 = 20*

6. **Damu Nyeusi.**

(a) Yalisemwa na mmoja wa wachuuzi.
Alimwambia Christine
Ni katika kituo cha matatu
Christine alikuwa ametoka ofisini mwa Peter/
Kumjuvya jinsi alivyoavya mimba.
Alikuwa safarini akielekea kwao. *4 x 1*

(b) Sadfa - Ni sadfa kuwa Christine ameavya mimba ilhali mchuuzi anamwambia awaonee watoto huruma. *kutaja 1 maelezo 1 = 2*

(c) (Maudhui ni ukatili)

- Wauguzi ni katili - Margret anamsaidia Christine kuavya mimba.
- Matajiri - Huwaingiza wasichana wadogo katika mapenzi na kuvuruga masomo yao. mf. Peter alitembelewa na Christine kila Ijumaa.
- Peter anawapunja wafrika kwa kununua samaki zao bei ya chini.
- Waajiri waliwakemea wafanyakazi waafrika vikali - Peter aliwatolea wafanyakazi amri kali.
- Waajri walilipa wafanyakazi mishahara duni. *3 x 2 = 6*

(b) Sifa za Christine.

- Mpenda anasa - Anatamani kuwa na uhusiano wa kimapenzi na matajiri. Alitoka chuoni kufuata Peter

- kwa starehe na anasa.
- Anashawishika haraka- Anapoambiwa na Zac kuwa Peter alimpenda alikubali na kuanza kumtembelea.
- Mwoga - Hana ujasiri wa kumweleza Peter kuhusu hali yake ya uja uzito.
- Mzinifu - Anashiriki mapenzi na Peter ilhali hawajaoana.
- Katili - Anaavya mimba.
- Mkosa maadili - Anamruhusu Peter kumbusu hadharani.
- Mwenye majuto - Anajuta baada ya kuavya mimba.
- Mwenye mapuuza - Anapuuza ushauri wa Dorothy kuhusu uhusiano wake na Peter.
- Mnafiki - Awali alikuwa mkristo aliyeokoka lakini vitendo vyake vilikuwa kinyume na maadili. *4 x 2*

7. Hadithi Fupi.
   Mwiba wa kujidunga.
- Samaki wa Nchi za Joto - Christine kujiingiza katika uhusiano na Peter akiwa chuoni kisha anapata mimba,
- kuiavya na kukosa kuolewa.
- Maeko - Jamila kuendelea kukaa katika ndoa iliyojaa mateso kutoka kwa mumewe licha ya kuwa mumewe
- habadili tabia.
- Kanda la usufi - Sela kujiingiza katika mapenzi akiwa shuleni kisha kupata mimba na kufukuzwa shule.
- Masazu kushiriki mapenzi akiwa shuleni kisha kukosa kufaulu mtihani na kuishia kufanya kazi duni.
- Gilasi ya mwisho makaburini - Semkwa na wenzake kuonywa kuhusu kwenda katika baa ya makaburini kisha wanapoenda wanavamiwa na majambazi - vizuu.
- Ndoa ya samani - Amali kumkataa Abu alipokuwa maskini kisha anaachwa hoi wakati wa arusi.
- Mke wangu - Msimulizi kumchagua Aziza akidhani atamvumbika, mkewe anamgeuka.
- Mwana wa Darubini - Mwatela kumbaka Kanada kisha anapozaa anamnyang'anya mtoto kumtorosha kisha Kananda anamtafuta hadi anampata na kurudiana na mwanawe.
- Mizizi na matwi - Bi. Kudura kumwacha mwanawe mchanga pipani kisha kuteseka akimtafuta, miaka mingi
- baadaye.
- Tazamana na mauti - Lucy kuwania kwenda Uingereza kwa vyovyote vile na kwenda kufia huko.
- Kikaza - Wanakijiji kuendelea kuchagua viongozi wasisotahili na kuumia kila wakati.

Fasihi simulizi.

8. Maghani ni utungo wa kishairi ambao hutongolewa kwa kutumia sauti iliyo kati ya uimbaji na uzungumzaji.

(b)
- Vivugo ni ushairi wa kujisifia unatungwa papo hapo na fanani mwanaume.
- Tondozi - Utungo wa kutukuza watu, wanyama, vitu kama magari, miti, milima n.k
- Pembezi - ni aina ya tondozi ambayo imekusudiwa kusifia watu na aina fulani katika jamii kutokana na matendo yao au mchango wao katika jamii.
- Rara - utungo wa kishairi wenye ubunifu mkubwa unaokusudiwa kusisimua hadhira. *Hoja 4 x 2 = 8*

(c) Maana ya ulumbi .
Uhodari wa kuzungumza au kuiga mazungumzo
kwa usanii na uhodari mkubwa. *al 1*

(d) Sifa za mlumbi.
- Mwenye ujuzi wa utamaduni, desturi, mila na sheria za jamii (mzingiro) ujuzi mkubwa wa maisha.
- Ufundi wa kutumia lugha, semi, mafumbo n.k
- Uwezo wa kutumia mbinu mbalimbali za kuwasiliana mfano, nyimbo, ushairi n.k
- Umahiri wa kughani, kusema kwa mfululizo na mwendo wa kasi.
- Kutumia sauti inayosikika bila shida.
- Ufundi wa kutumia kunga za maswali.

(e) Umuhimu wa ulumbi.
- Kipimo cha kimsingi cha mtu kuteuliwa kama viongozi.
- Njia maalum inayotumiwa na jamii kupitisha ujumbe muhimu.
- Njia ya kudumisha utamaduni na thamani za kitamaduni kwa kuzionea fahari.
- Ni kitambulisho muhimu kwa jamii na wanajamii.

MTIHANI WA GATUZI NDOGO YA KIRINYAGA MAGHARIBI
Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Sekondari (K.C.S.E)
CHETI CHA KUHITIMU MASOMO YA SECONDARI
102/1
KISWAHILI
INSHA

1. **Insha ya lazima**
   Andika dayolojia kati ya katibu wa usalama wa ndani na waandishi wa habari kuhusu jinsi ya kuzuia uhalifu nchini
2. Sheria zinazombagua mwanaume na kumpendelea mwanamke zinafaa kutupiliwa mbali. Fafanua
3. Mpiga ngumi ukuta huumiza mkonowe.
4. Andika insha itakayoanza kwa maneno haya
5. Lo, yaliyotendeka katika makazi ya jirani yetu usiku huo yalikuwa ya kutisha sana. Kumbe watu wamegeuka hayawani! Hayawani .....

MTIHANI WA TATHMINI WA KIRINYAGA MAGHARIBI 2015
Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Sekondari (K.C.S.E)
CHETI CHA KUHITIMU MASOMO YA SECONDARI
102/2
KISWAHILI
UFAHAMU, UFUPISHO, MATUMIZI YA LUGHA NA ISIMU JAMII
KARATASI YA PILI

1. **UFAHAMU**

Shule yangu ya upili

Majio yangu katika shule hii ya upili hayakutokea kwa bahati nasibu bali kwa mipango kabambe niliyoianza tangu nikiwa shule ya vichekechea. Nikiwa sitetereki hata kwa wazazi wangu waliponisihi nijiunge na shule nyingine za karibu nikawa sisikii la mwadhini wala la mteka maji msikitini. Nikawa na ragba ya mkanja nikingoja siku ya kujiunga na shule yenyewe. Kweli majuto ni mjukuu na huja kinyume.

Nilizaliwa katika aila yenye nafasi iliyotopea na kubobea katika ukwasi uliodhihirika kutokana na mitaa tulikoselelea kwa muda kabla ya baba kuaamua kununua nyumba yake mwenyewe huko upande wa Karen hivyo tukagura kutoka Runda. Wakati wa likizo tukawa tunaruka hadi pwani ambako mama yangu alikuwa amemiliki jumba lililokuwa katika ufuo wa bahari lililojengwa katika kipande kisichopungua ekari tatu alilotunukiwa wakati wa nikahi yao na wakwe wa baba yangu.
Wavyele wangu wakawa wanaendesha magari meusi ya kifahari ingawa sikuwahi kumwona mama akichangamka kuendesha magari yake ya maana, kila macheo ya siku za kazi gari lililoendeshwa na dereva ambaye alimstahi mama hadi akawa anamfungulia mlango wa gari na kuufunga baada ya mama kujitoma katika tumbo la gari lilimjia na kumrejesha kwa wakati. Nikajiunga na shule ya msingi ya kibinafsi ambako nilishughulikiwa kama kikembe. Wengi wa wale tuliosoma nao walikuwa wa tabaka langu na walikuwa wametoka katika kila sehemu nchini Kenya.

Hayawi hayawi huwa na siku ya kuripoti ikafika. Alfajiri, dereva mmoja akatumwa kwenda hadi Kisumu ili atulaki na kutusafirisha kutoka uwanja wa ndege hadi shule ya upili ambayo ilikuwa yangu ya rohoni. Nasi tukaelekea hadi uwanja wa ndege ili turuke hadi Kisumu. Safari yetu kutoka kitongoji cha kifahari hadi Airport ilikuwa njema, safari yetu tulipoabiri ndege ilikuwa bila bughudha, safari yetu kutoka Kisumu mjini haikuwa na kasoro na tulienda kulingana na mpango. Safari yetu ilikuwa mufti hadi tulipofika katika lango la shule ya kitaifa!
Tulipotia ozi tu!!....jamani.....jamani nikafa moyo. Labda mama aliweza kubaini mabadiliko ya hisia zangu, nilitamauka, nikawa mchege na kusema kweli niliyoyaona sikuamini. Mvua iliyokuwa imepasua hapo awali ilikuwa imeacha vitua vya maji kwenye vijia vya kutembea vilivyochakaa na kubomoka bila yeyote kujali kuvikarabati. Majengo yalikuwa makongwe yaliyojengwa miaka mia moja iliyopita na yalistahili kuitwa makafadhi badala ya pahali pa kumkaribishia mwanafunzi aliyepita kwa alama mia nne na thelathini na tano. Asiye na wake ana Mungu, nikapiga moyo konde lazima nisajiliwe katika shule ya ndoto langu. Ningewezaje kughairi wazo langu baada ya siku hizo zote za maandalizi tena mbele ya wanuna walioniona kama kielelezo chao tangu walipozaliwa. Nikasajiliwa!

Sikujua, hakika sikujua, sikujua shule ya upili ya kitaifa yaweza kuwa hivi. Kweli mwanafunzi aweza kukosa viatu na hata kushindwa kununua rangi ya kupaka viatu hivyo iwapo amenunuliwa na wahisani? Nilimlaumu nina maana hakunieleza kuwa mtu anaweza kula chakula ambacho mbwa wetu hawezi hata kukiangalia. Nilipoingia katika ukumbi wa chakula nilihisi kitefutefu nusura nichafukwe na moyo, makapi ya mboga na uchafu usioelezeka ulinikumba, kisha nikapewa kisahani cha plastiki na kupakuliwa kipande cha ugali ambacho bado kilikuwa na unga na kuachiwa hiari ya kukila au kukitupa. Wenzangu wakawa wanakirambatia chakula kwa kasi huku mmoja wao alipoona jinsi nilivyokiangalia changu akanihisi nimpe chote na kukimaliza fyu. Wote walikuwa na furaha kemkem na kuajabia utukufu wa shule iliyotukuka ya kitaifa ila mimi.

Baada ya mlo 'rojo rojo', tukaelekea darasani nilikopigwa na mghuma mkubwa. Tulikuwa wanafunzi hamsini na watano katika darasa moja tu! Mwalimu mmoja akaja na kutukaribisha shuleni kisha akatuarifu kuwa atakuwa mwalimu wa darasa letu. Nilipomsikia akinena nusura niishiwe na stahamala, kimombo chake kilinishangaza, hasa matamshi yake yalipungukiwa na kudhirisha athari za lugha ya asili. Nilihisi kana kwamba ningemrekebisha lakini sikudhubutu.

Tukafululiza hadi bweni na nikajilaza kitandani chembamba huku mwingine nisiyemjua lakini asiyejua kuwa kuna nguo maalum za kulala akalala uchi katika ghorofa ya juu ya kitanda chetu. Mgeni njoo mwenyeji apone maana baada ya muda wadudu ambao sikuwahi kuwaona aushini mwangu wakanza kunishambulia. Nikaamka baada ya kumnasa mmoja wa wadudu hawa na kuuliza mmoja wa wenzangu ni wepi wadudu hawa na kwa kutojali hata kidogo, akanieleza kuwa hawana neno bali ni kunguni tu, sikujua na kwa kweli mama hakuniambia kuwa kuna wadudu wanaotafuna mtu na hunuka fye! Sikulala kwa hofu huku wenzangu wakiforota kwa njia ya kunighasi. Sikuwahi kudhani kuwa watu wengi wanaweza kulala chumba kimoja huku changu kikiwa na hamamu na vifaa vyote muhimu kikibaki bila mtu!

Tulisomeshwa na walimu wasiojali kana kwamba tunaelewa au la. Hawakushughulika iwapo tulifanya kazi za ziada au la, ndio, hakujali chochote. Kilichonishangaza ni kuwa wanafunzi waliojiunga nasi kutoka shule za umma wenye alama duni waliwapenda na kuelewa haraka walichosomeshwa na hawakujali matamshi yao, labda hawakuyatambua.

Hatimaye tukafanya mtihani wa mwisho wa muhula wa kwanza. Nilishangaa ghaya iliponibainikia kuwa aliyetuongoza alikuwa ghulamu mmoja mshamba niliyempuuza tu mvulana kutoka kijijini ambacho singetambua katika ramani ya nchi ambaye hata vitu vya kimsingi vilimpiga chenga. Nikafanya uchunguzi nikatambua mwenzangu alikuwa na alama mia mbili hamsini na tatu akitoka katika darasa la nane, nilifanikiwa kuwa nambari mia mbili hamsini na tatu kwa jumla ya wanafunzi mia tatu!
Tulipofunga kwa likizo ya Pasaka nikaamua kuchukua hatua nyingine sitawahi kuhama kutoka shule hii ya upili wala kuwa zaidi ya nambari kumi!

Maswali

a) Thibitisha kauli kuwa msimulizi ana msimamo dhabiti (alama 2)
b) Tofautisha jinsi mwandishi alivyofunzwa katika shule ya kibinafsi na shule ya upili.
(alama 3)
c) Taja mambo matatu yanayotuonyesha kuwa msimulizi alilelewa katika aila ya kikabaila kulingana na aya ya pili.
(alama 3)
d) Andika masuala matatu yaliyomshangaza katika shule ya upili (alama 3)
e) Andika tamathali mbili zilizotumika katika kifungu.
(alama 2)
f) Eleza maana ya msamiati huu kama ulivyotumika katika kifungu.
(alama 3)
i) alimstahi
ii) kughairi
iii) kunighasi

MUHTASARI

Tulipigwa na butwaa kwa kupokea habari kuhusu mauaji ya wasafiri 28 waliouwawa kikatili huko

Mandera na kabla kuwasidikiza makaburini wengine waliokuwa 40 wakijitafutia riziki katika chimbo la mawe kuko huko, wakaangamizwa. Tunapinga na kulaani vikali visa vya ugaidi vinavyoendelezwa kutetemesha usalama wa wananchi. Hivi ni vitendo vya kinyama vinavyotekelezwa na watu waliokosa ubinadamu na utu kabisa. Inakera mno kwa vitendo vya kigaidi. Inagadhabisha kuona Wakenya wasio na makosa wakiteswa na kuuwawa kinyama bila huruma na watu wasio na utu. Hatuogopi wala hatuna fedheha kuamba magaidi hawa wamelaaniwa na siku zao zimehesabiwa hapa duniani, damu ya mwananchi asiye na makosa katu watailipia. Napinga vikali pale magaidi hawa wanapohusisha vitendo hivi kuwa vita vya kidini. Vita hivi si vya kidini kwani hakuna dini yoyote iliyo na imani ya kumwua kinyama binadamu asiye na makosa.

Kando na tishio la ugaidi, Wakenya pia wanakabiliwa na hatari za ujambazi, mauaji, unajisi, ubakaji na maovu mengine. Iwapo mbunge anayelindwa na askari wawili atawauwa, je wananchi wa kawaida watakosa kumuua? Katika juhudi za kudumisha usalama, polisi wana jukumu la kutumia kila mbinu kuhakikisha kuwa haki ya kikatiba ya Wakenya kuhusu kulindwa kwa maisha na mali yao imedumishwa. Polisi nao wanashambuliwa huko Kapendo na kumiminiwa marisasi wasiweze kujikinga tukabaki kuwazika licha ya umri wao mdogo ili kukabiliana na tatizo hili, polisi wakaamua kusaka wahalifu. Lakini cha kusikitisha kuwa mbinu ambazo polisi wamekuwa wakitumia hasa hii ya kufanya misako inayoishia kuwanasa mamia ya raia wasio na habari kinachoendelea, inawaongezea Wakenya mateso. Hali hii inawaacha Wakenya kwenye hatari ya kunaswa na majambazi ama polisi.

Matumizi ya mbinu hii ya misako imeishia kunasa raia wengi wasio na makosa. Wanaponaswa, hurundikwa kwenye seli usiku mzima ama siku kadha na hata kama wanaachiliwa huwa tayari wameteseka. Huu ni ukiukaji wa haki za raia. Kadhalika, mbinu hii yaonekana kama hila ya polisi kutaka kuonyesha wanafanya kazi lakini sio mwafaka kwani wanapokuwa wakiwanasa raia mijini na mitaani, magaidi na majambazi wanaendelea na shughuli zao.

Badala ya kusaka wakora kwa kubahatisha kwenye umati, polisi wanapaswa kubuni njia ambazo zitawapa mwelekeo mwafaka zaidi kuhusu wahalifu ili waweze kuwafuatilia. Ushirikiano baina yao na majajusi uwepo. Hii itawezesha polisi kupata habari muhimu kuhusu vitisho vya uhalifu. Maafisa wa usalama pia wanaweza kupata habari muhimu kutoka kwa raia. Ni ajabu kuwa sisi tunaelekeza kidole cha lawama kwa serikali ilhali wahalifu hawa tunaishi nao katika mitaa tunakoishi, viongozi wapinzani wasipinge mikakati yoyote ya serikali kama vile mpango wa nyumba kumi kisa na maana si wazo lao. Iwapo hawapendezwi na mpango kama huo waibuke na mbinu badala tuzijaribu. Suala la 'serikali ingilie kati' hata bwana mlevi anapochapwa na mkewe lisukumwe katika kaburi la sahau.

Maswali

a) Ni nini maoni ya mwandishi kuhusu suala la ugaidi?
Tumia maneno 80 (alama 7, 1 utiririko)
Matayarisho
Nakala safi

b) Kwa kutumia maneno yasiyozidi 50, fupisha aya mbili za mwisho (alama 6, 1 utiririko)
Matayarisho
nakala safi

3. Matumizi ya lugha

a) Badilisha vitenzi hivi viwe katika hali ya kuamuru (alama 2)
1) kuleta .....
2) kuja .....

b) Tumia kiungo 'na' katika sentensi kuonyesha: (alama 2)
1) Ufupisho wa nafsi ya kwanza umoja fulani
2) kihusishi kuonyesha aliyetenda jambo fulani

c) Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo (alama 2)
1) Mwalimu amesema ya kwamba watoto wengi wamekuwa wahuni.
2) Ikiwa nitamwona mama sokoni, nitamweleza kila kitu

d) Ainisha viungo vya kisarufi katika sentensi hii (alama 3)
Alani

e) Tumia kitenzi **'cha'** katika kauli ya kutendesha katika sentensi (alama 2)
f) Tumia kiambishi ngali katika sentesi kuonyesha hali ya kuendelea
(alama 2)
g) Tofautisha kwa kueleza maana ya istilahi hizi: (alama 2)
ghuna
si ghuna
h) Changanua sentensi kwa njia ya matawi (alama 4)
Yeye na mama yule si watu wazuri sana
i) Eleza sifa bainifu za sauti zifuatazo
(alama 4)
i) /l/
ii) /ch/
j) Tumia kielezi cha namna kiigizi katika sentensi (alama 2)
k) Andika sentensi hii upya katika **usemi halisi**
(alama 2)
Mwanafunzi alimsihi mwalimu asimwadhibu wakati huo
l) Onyesha chagizo katika sentensi hii
(alama 2)
Mtoto alikula kwa utaratibu jana jioni
m) Tambua na uainishe shamirisho katika sentensi hii
(alama 3) Hamu amemwandikia mwalimu riwaya kwa kalamu
n) Unda vitenzi kutoka kwa maneno haya kisha uyatumie katika sentensi yakiwa katika hali hiyo ya kitenzi

(alama 2)
i) Marashi
ii) bora
o) Tofautisha kati ya vivumishi hivi kwa kueleza maana ya kila kimojawapo
(alama 2)
i) -ingine
ii) -ingineo
p) Sahihisha makosa katika sentensi hii
(alama 2)
Mtoto mgani mwenye kupiga kelele darasani
q) Tumia maneno haya katika sentensi ili kuyatofautisha (alama 2)
shoka
choka
shoga

Isimu jamii

Nani kuku.....? Sosi poa leo ..... Mate ndo! ndo! ndo!. Ukimanga hii hutaona daktari kwa miaka kumi..... Ng'ombe je? nani? .....nani!... Ni wewe..... poa basi naja.....

a) Ni sajili gani inayorejelewa hapo juu? (alama 2)
b) Andika sifa za sajili hii ukitoa mifano ndani na nje ya muktadha huu
(alama 8)

MTIHANI WA GATUZI NDOGO YA KIRINYAGA MAGHARIBI
CHETI CHA KUHITIMU MASOMO YA SECONDARI
102/3
KISWAHILI
FASIHI

SEHEMU A

1. **Swali la lazima**

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo

1. Ningali kinda nishike, viungo vi teketeke,
Sinipe simi nizuke, na vichaka nivifyeke,
Dhibiti nivuvumke, usidiriki makekeke,
Pulika usikiuke, mpe mtoto hakiye,

2. Mungavunja haki yake, madhara milele kwake,
Wa kiume na wa kike, mpeni yaliyo yake,
Kwa makini mumshike, kadiri makamo yake,
Pulika msikiuke mpe watoto haki yake.

3. Kwanza ni watani wake, Uandae aridhike,
Atuze mtima wake, maudhi yasimshike,
Kuta nne zizunguke, na hofu imbanduke,
Pulika msikiuke, mpe mtoto haki yake.

4. Pili ni chakula chake, 'jengeke siha yake,
Mpe titi alishike, anyonye asihinike,
Kuta nne zizunguke, na hofu imbanduke,
Pulika msikiuke, mpe mtoto haki yake.

5. Mpe tiba 'sidhurike, ndwele asiathirike,
Fikira zimpanuke, atambue rika lake,
Penye daraja avuke, mvushe asighurike,
Pulika msikiuke, mpe mtoto haki yake.

6. Angakuwa chekecheke, apande shule avuke,
Mpe taaluma yake, adhibiti apanuke,
Ufundi na dhima zake, ayashike ajivike,
Pulika msikiuke, mpe mtoto hakiye.

7. Jifanye kipenzi chake, mpende asihinike,
Amani ijae kwake, daima asikereke,
Vizito usimtwike, visivyo vipimo vyake,
Pulika msikiuke, mpe mtoto hakiye.

8. Elimu chuo ashike, apanuke bongo lake,
Atende jukumu lake, ahudumie wenzake,
Ajue wajibu wake, atende asitepweke,
Pulika msikiuke, mpe mtoto hakiye.

9. Hima kwa Muumba wake, muhimidi aongoke,
Roho yake isafike, ahera asisumbuke,
Neema imzunguke, maovu yamuepuke,
Pulika msikiuke, mpe mtoto hakiye.

Maswali

a) Nafsi neni ametaja haki zinazomstahiki mtoto. Zitaje na uzifafanue.
(alama 4)
b) Eleza kwa kutoa mifano mbinu mbili zinazotumiwa na mshairi kutosheleza mahitaji ya kiarudhi
c) Bainisha umuhimu wa tamathali zozote mbili za usemi zilizotumika katika shairi hili

(alama 4)

d) Eleza ubeti wa tano kwa lugha nathari (alama 4)

e) Taja na ufafanue toni ya mshairi (alama 2)

f) Eleza maana ya misamiati ifuatayo
(alama 2)
i) Mtima
ii) Asihinike
iii) mbi
iv) asighurike

SEHEMU B

TAMTHILIA: *Timothy Arege: Mstahiki Meya*

Jibu swali la 2 au 3

2. "Mtu huvuna alichopanda. Ukipanda pojo huweza kuvuna kunaziu"
a) Eleza muktadha wa dondoo hili.
(alama 4)
b) Thibitisha kuwa warejelewa walikuwa wamepanda pojo
(alama 10)
c) Eleza sifa za mnenewa (alama 6)
3. Tamthilia ya Mstahiki Meya inamulika na kupiga vita utawala dhalimu katika mataifa ya kiafrika. Jadili

(alama 20)

SEHEMU C

RIWAYA: Ken Walibora: *Kidagaa Kimemwozea*

Jibu swali 4 au 5

4. "Aliwaonea gere wanawake wengine katika eneo la Sokomoko waliovaa rinda moja....."
a) Weka dondoo hili katika muktadha wake
(alama 4)
b) Eleza sifa na umuhimu wa anayemfanya mrejelewa kuwaonea wanawake wengine gere
(alama 10)
c) Jadili maudhui matatu yanayodokezwa katika dondoo hili
(alama 6)
5. "Mla naye huliwa zamu yake ifikapo."
Thibitisha kauli hii kwa kuirejelea riwaya ya kidagaa kimemwozea.
(alama 20)

SEHEMU D:

HADITHI FUPI: Ken Walibora : *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*

Jibu swali la 6 au 7

6. Onyesha jinsi swala la ubaguzi linavyodhihirika katika hadithi zozote nne
(alama 20)
7. "Hawakurudhisha macho tu, bali pia walicheza michezo ya ujana ama wakijua au kutojua kuwa ujana una tegemeo."
a) Eleza muktadha wa dondoo hili
(alama 4)
b) Dhihirisha namna 'Michezo ya ujana' ya wanaorejelewa ilivyosambaratisha tegemeo la ujana wao.
(alama 8)
c) Jadili ukweli wa kauli kwamba, "Tamaa mbele mauti nyuma" ukirejelea hadithi ya "Tazamana na mauti"
(alama 8)

SEHEMU E

FASIHI SIMULIZI

8. a) Eleza sifa nne za ushairi simulizi
(alama 8)
b) Taja na uelezee aina tatu za magizo (alama 6)
c) Jadili mbinu nne za kimtindo za methali huku ukitoa mifano mwafaka
(alama 4)
d) Eleza umuhimu wa hekaya katika jamii
(alama 4)

MTIHANI WA GATUZI NDOGO YA KIRINYAGA MAGHARIBI 2015
KIDATO CHA NNE
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA INSHA
102/1

1. Hii ni insha ya dayolojia. (Mazungumzo yanahusiana watu wawili au zaidi)

Muundo

a) Kichwa - Kitaje wahusika, wapi na mada.
b) Utangulizi - Kudokeza mazingira ya dayolojia kwa kifupi na maelezo yawe katika mabano
c) Mwendelezo - Mtindo wa kitamthilia utumiwe
d) Mwisho - Uamuzi kuhusu mada ujitokeze pamoja na hitimisho rasmi ya dayolojia.

- Majina ya wahusika yawepo na yaandikwe upande wa mkono wa kushoto
- Majina hayo yafuatwe na nukta pacha.
- Ufafanuzi wa matendo ya wahusika uwe kwenye mabano
- Msemaji mmoja asitawale dayolojia

Hoja

- Kuhamasisha wanachi kuwajibikia usalama wao.
- Kuimarisha taasisi za mahakama na jela.
- Polisi kuimarisha doria
- Kuhimiza kukubali mpango wa usalama wa nyumba kumi
- Kupiga vita ufisadi katika kikosi cha askari na washikadau katika nyanja ya usalama.
- Kuimarisha uchumi na nafasi za kazi
- Kutumia teknolojia ya kisasa kupambana na uhalifu.
- Kuongeza idadi ya walinda usalama.
- Kuwapa waalinda usalama mafunzo zaidi

TAZ: Hoja ziwe na uhalisia

Asipojikita kwenye muundo wa dayolojia aondolewe alama ($4\frac{1}{2}$) za sura

Mtahini ahakiki hoja zingine

Swala la 2

Ni swali la kuonyesha ukweli wa kauli aliyopewa mtahiniwa

Hoja

- Katiba mpya imewatengea wanawake viti na kumwacha mwanamume
- Alama za kuingia vyuo vikuu huwapendelea wasichana
- Mashirika mengi yamebuniwa kuwadhamini watoto wa kike.
- Sheria mpya za urithi zinawapendelea wanawake
- Sheria za talaka na ulezi wa watoto humpendelea mwanamke
- Hazina ya mkopo imetengewa wanawake pekee ili kujiboresha.
- Wasichana katika shule wanafadhihiwa kwa mfano kupewa visondo ilihali wavulana wametelekezwa
- Wanaume wanaodhulumu wanawake wanapata adhabu kali kisheria kuliko wanawake wanaowadhulumu wanaume.

Taz: - Mtahiniwa afanue hoja zaidi ya tano
- Zikipungua, amepungukiwa kimaudhui
- Mtahini ahakiki ufaafu wa hoja zingine

Swali la 3

- Hili ni swali la methali
- Maana ya juu ni kuwa anayegonga ukuta kwa ngumi anajiumiza ama kujijeruhi mwenyewe.
- Maana ya ndani ni kuwa yeyote anayeshindana na anayemzidi nguvu au uwezo huenda akajiumiza mwenyewe

Taz: - Mtahiniwa anaweza kuanza kwa kueleza maana ya methali kisha atunge kisa au visa

- Anaweza kutunga kisa au visa moja kwa moja ili maana ijitokeze.
- Maudhui yadhihirike kwa kuangazia pande zote mbili, la sivyo atakuwa amepungukiwa kimaudhui.

Swali la 4

Hili swali la mdokezo

- Mtahiniwa atoe kisa cha kusisimua kinachoanza kwa maneno aliyopewa
- Mtahiniwa atakuwa amepotoka kimaudhui kisa chake kitakapokosa kuambatana na dondoo.

- Akikosa kuanza kwa kauli aliyopewa na kisa chake kioane na kauli ataadhibiwa kimtindo tu.
- Kisa kisipooana kabisa atakuwa amejitungia swali

MTIHANI WA GATUZI NDOGO YA KIRINYAGA MAGHARIBI 2015
KIDATO CHA NNE
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
102/2

A: Ufahamu

1. Hatetereki anapoishiwa abadilishe wazo kuhusu shule ya ndoto lake.
2. Uamuzi wa kutohama kutoka shule hii hata baada ya kuona yaliyompata. 2 x 1 = 2

B: Shule ya binafsi

1. Alitunzwa kama kikembe.
2. Walimu waliomfunza walitamka kimombo kwa njia bora.

Shule ya upili

Matamshi ya walimu yaliathiriwa na lugha ya asili. walimu wasiojali uelewa wa wanafunzi.
Wasioshughulika wasipofanya kazi za ziada. zozote 3 x 1 = 3

C: Mitaa walikoishi

- Uamuzi wa kununua nyumba Karen.
- Kuruka hadi pwani.
- Mama yake kumiliki jumba katika shamba la ekari.
- tatu ufuoni. zozote 3 x 1 = 3

D:

- Mwanafunzi kukosa viatu.
- Chakula duni katika shule hii.
- Idadi ya wanafunzi katika darasa.
- Kushambuliwa na wadudu.
- Kuongozwa na mvulana wa alama 253. zozote 3 X 1 = 3

E:

- Uhuishi - Tumbo la gari.
- Misemo - Ragba ya mkanja.
- Takriri - Sikujua.
- Methali - Mgeni njoo mwenyeji apone. 2 x 1 = 2

F:

- Alimstahi - Heshimu.
- Kughairi - badilisha.
- Kunighasi - kunikasirisha. 3 x 1 = 3
- Katika sehemu ya ufahamu adhibu ifuatavyo.

1 $\frac{1}{2}$ x makosa 6 ya hijai = 3
$\frac{1}{2}$ x makosa 6 ya sarufi = **3**
Jumla **6**

Ufupisho (Alama 15)

a) Ni nini maoni ya mwandishi kuhusu suala la ugaidi?

- Tunapinga na kulaani visa vya ugaidi.
- Ugaidi ni kitendo cha kinyama kinachotekelezwa na watu waliokosa ubinadamu.
- Ugaidi hauna uhusiano na dini yoyote.
- Polisi wanazembea katika kuzuia matendo ya kigaidi.
- Polisi wabuni njia mbadala ya kukabiliana na ugaidi badala ya kunasa raia wasio na hatia.
- Wakenya wasio na makosa huteswa na kuuawa kinyama.
- Magaidi wana haki ya kulindwa kikatiba. (hoja zozote 7 x 1 = 7)

b) Ufupisho wa aya mbili za mwisho

- Raia wasio na hatia hunaswa.
- Hurundikwa kwenye seli na kuachiliwa huru kama wameteseka.
- Huu ni ukiukaji wa haki za binadamu.
- Hii ni hula ya polisi kujionyesha kuwa wanafanya kazi.

- Magaidi huendeleza shughuli zao.
- Polisi wanapaswa kubuni njia zitakazowapa. (Mwelekeo mwafaka zaidi kuhusu wahalifu ili waweze kuwafuatilia)

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA MATUMIZI YA LUGHA.

a) i) Leta!
ii) Njoo! 2x 1

b) i) nami
ii) Alipigiwa **na** mama yake 2x1


c) i) Mwalimu amesema ya kwamba kishazi tegemezi
Watoto wengi wamekuwa wahuri kishazi huru $^1/_2$ x 2
ii) Ikiwa nitamwona mama sokoni - kishazi tegemezi
Nitamweleza kila kitu - kishazi huru $^1/_2$ x 2

d) A Nafsi ya tatu umoja
L Mzizi
a kiishio
ni kiambishi kiulizi $^1/_2$ x 4

e) Chisha
Tukio la Tsunami liliwachisha wanadamu wote 3 x 1

f) Tungali tunasoma - kadiria jibu la mtahiniwa lazima atunge sentensi 2x1

g) ghuna - sauti nzito
Sauti inayotetemesha nyuzi za kutamkia
si ghuna - sauti hafifu
Hakuna mtetemeko 1 x 2



$^1/_2$ x 8 = 4 (alama 4)

i) i) /L/
-Kitambaza
-Hutamkiwa ufiziri
ii) - Ni konsonati
- Ni kipasuo kwamizo
- Sauti sighuna
- Ni ya kaakaa na ufizi

J) Tumbukia majini chumbwi!

K) Mwanafunzi alimwambia, “Tafadhali, mwalimu, usiniadhibu wakati huu”**au** “Tafadhali, mwalimu, usiadhibu wakati huu” **au** mwanafunzi alimwomba mwalimu, “Tafadhali, usiniadhibu wakati huu. 2x1

L) Kwa utaratibu

jana jioni 1x3

m) Riwaya - kipozi
kalamu - ala
Mwalimu - kitondo

n) Rashia k.m Alijirashia marashi ya rihi ya peponi.
boresha km. Ni vyema kuboresha matamushi yako 1x 2

o) ingineo - zaidi ya
ingineo - ziada 1x 2

p) Mtoto gani aliyepiga kelele darasani.
Mtoto gani ambaye alipiga kelele darasani. 2 x 1

q) Shoka - kifaa cha kupasua kuni
choka - Hisi machovu
shoga - Rafiki wa kike wa mwanamke
Jamila alihimizwa na shoga yake atoroke iwapo amechoka na ndoa yao lakini akamwambia atamkata kwa shoka
3 x 1
Nani kuku? Sosi tamu leo. Mate ndo..... ndo..... ndo..... Ukikimanga hutaona daktari kwa miaka ..... Ng'ombe je?.....

a) Eleza sajili inayorejelewa katika dondoo hili
sajili ya mkahawani / hotelini (1x 2)

b) Andika sifa za sajali hii. Ukitoa mifano ndani na nje ya muktadha huu.

- Matumizi ya maneno au kauli ambazo katika mazingira mengine haziwezi kuwa na maana nani kuku? Ng'ombe je?
- Matumizi ya msamiati maalumu wa hotelini kwa mfano,
  i) Karanga ii) 'Ng'ombe' iii) Chipo iv) Chapo
- Lugha ya ucheshi na utani
- Matumizi ya misimu ukikimanga / surwa
- Kuchanganya ndimi
- Lugha isiyo sanifu k.m Ukimanga
- Tanakali km. mate ndo... ndo... ndo...
- Matumizi ya sentensi fupi 8x 1

MTIHANI WA GATUZI NDOGO YA KIRINYAGA MAGHARIBI 2015
KIDATO CHA NNE MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
102/3

1. a) Haki zinazomstahiki mtoto
- makazi mema
- Usawa wa kijinsia
- Malazi mema
- Matibabu
- Elimu bora (zozote 4 x 1= 4)

b) Mbinu za kishairi zinazotumika kutosheleza mahitaji ya kiarudhi

i) Mazida - kutosheleza idadi ya mizani mfano: Mungavunja - mngavunja
ii) tabdila: kuleta mahadhi katika ushairi
mfano: Muhimidi - mhimidi
yamuepuke - yamwepuke
iii) Inkisari: Kutosheleza idadi ya mizani
kwa mfano 'Sidhurike - Usidhurike
Sinipe - Usinipe
hakiye - haki yake
iv) Kufinyanga sarufi / kuboronga sarufi - ili kuleta urari wa vina. Kwa mfano
i) Mpeni yaliyo yake - Yaliyo yake mpeni
ii) Kwa makini mumshike - Mmshike kwa makini
iii) Penye daraja avuke - Avuke penye daraja
Tan. Mwanafunzi lazima aeleze mahitaji ya kiarudhi (zozote 2 x 2 = 4)

c) Umuhimu wa tamathali

i) Istiari - i) Kuta nne zizunguke
ii) Penye daraja avuke
iii) Mpe taaluma yake
ii) Uhuishi i) Husuda mbi zimwondoke
ii) Apanuke bongo lake
iii) Maovu yamwepuke
iii) Taswira i) Apanuke bongo lake
ii) Titi alishike anyone (zozote 2 x 2 = 4)

d) Lugha nathari ubeti wa tano
Mtoto atibiwe ili asiathiriwe na magonjwa ili akue vizuri pia aweze kutambua rika lake na aelekezwe katika utu uzima. Haki za mtoto zisikiukwe (alama 4)
e) Toni - ushauri; kuelekeza (alama 2)
f) Maana ya msamiati
i) mtima - moyo
ii) Asihimike - asiteseke
iii) mbi - mbaya/mbovu
iv) Asighurike - asiangamie
(ala ½ x 4 = 2)

2."Mtu huvuna alichopanda"

a)
- Msemaji ni diwani wa watu
- Msemewa daktari Siki
- Nyumbani kwa Diwani wa tatu
- siki amemtembelea Diwani wa tatu kumshikinikiza aongee na Meya katika vikao vyao kuhusu matatizo yanayowakumba wafanya kazi (alama 4)

b) Wanaorejelewa walikuwa wamepanda pojo kwa sababu
- Walimchagua viongozi wandanganyifu Kwa mfano: Meya anadanganya kuwa dawa zimeagizwa ilhali ni uwongo
Wanawachagua viongozi fisadi
mfano: Meya ananyakua vipande vinane vya ardhi na kumgawia Bili vinne.
- Wanawachagua viongozi wanaopeana kandarasi kwa njia isiyo halali
- Viongozi waliochaguliwa kama vile Meya, Diwani I na II wanashirikiana kuuza fumbo ya Meya iliyo

kitambulisho cha Umeya
- Wafanya kazi waliogoma wakidai haki zao za:
- Nyongeza ya mishara, gharama ya vitu kupanda, ukosefu wa dawa n.k, wanafurushwa vibaya na askari kwa amri ya Meya.
- Meya kama kiongozi aliyechaguliwa anakataa kushughulikia malamishi ya wafanya kazi. kama Nyongeza ya miashahara, kuletea wafanya kazi vifaa vya kufanyia kazi kama glavu za kuoshea choo. (Zozote 5 x 2= 10)

c) Sifa za mnenewa (siki)
- Mtetezi wa haki
- Ni mwajibikaji
- Ni mwenye busara
- Ni mshauri mzuri
- Ni mvumilivu
- Ni mshawishi
- Ni mwenye utu

Tan. Mwanafunzi lazima afafanue hoja zake

Kutaja alama $^{1}/_{2}$

Maelezo alama ½ (zozote 6 X 1= 6)

3.
- Matumizi mabaya ya askari tawala ambao wanawapiga watu risasi na kuwatupia vitoa machozi.
- Matumizi mabaya ya hazina ya baraza - Hazina inakuwa na nakisi.
- Wawakilishi wa wafanyi kazi kunyimwa nafasi ya kuongea na Meya.
- Ufisadi km. Meya kujilimbikizia vipande vinane vya ardhi na kumgawia Bili vinne.
- Matumizi mabaya ya mamlaka
- mfano. Mayors act na riots act.
- Wafanya kazi kutelekezwa katika utendaji kazi wao. Mfano: hawapewi glavu za kuoshea vyoo.
- Wafanya kazi kunyanyaswa.
- mfano wanalipwa mishahara nusu, Mshahara inacheleweshwa na wakati mwingine hawalipwi. Aidha hawaongezewi mishahara.
- Ukabila na mapendeleo- Meya anampigania mhazili ndio awezo kupata kazi
- Raia kuuliwa ovyo hasa wakati wa maandamano.
- Raia kutelekezwa kwenya njaa na magonjwa na kujifia kama nzi.
- Wanaotetea haki za wafanya kazi wanatengwa
  mfano: Diwani III na siki.
- Walio mamlakani kujiongezea mishahara
  mfano: Meya, Diwani I na II (zozote 10 x 2 = 20)

4. a)
- Maelezo ya mwandishi akimrejelea Bi Zuhura- Mkewe Mtemi Nasaba Bora
- Akiwa chumbani mwake ambako amejilaza kitandani
- Bi zuhura alikuwa na ukiwa kwa kuwa mumewe alikuwa amezoea kurejea usiku sana na kumpuliza kimapenzi

b) i) Sifa za mrejelewa (Nasaba Bora)
- Ni laghai
- Ni kiongozi fisadi
- Ni mwenye tamaa
- Ni mnafiki
- Ana taasubi ya kiume.
- Si mwajibikaji.
- Ni mwongo
- Ni mwaherati.

Tan. Mwanafunzi aeleze hoja zake kikamilifu

Kutaja $^{1}/_{2}$

Maelezo ½ (zozote 5 x 1= 5)

ii) Umuhimu wa Nasaba Bora

- Ni kielelezo cha viongozi wa kiafrika wanaouendeleza ukoloni mambo leo.
- Awakilisha wanaume wenye taasubi ya kiume.
- Ni kielelezo cha viongozi katili katika jamii.
- Anawakilisha wanaume wanaosambaratisha ndoa zao kwa kuwa na uhusiano wa kimapenzi nje ya ndoa.
- Ni kielelezo cha viongozi wenye tamaa wanaojilimbikizia mali ya wanyonge.
- Anawakilisha viongozi laghai katika jamii.

Tan. Mwanafunzi aeleze hoja zake kikamilifu.
Kutaja ½
maelezo ½ (zozote 5 X 1 = 5)

c) Maudhui yanayodokezwa na dondoo

i) Upweke

- Mumewe aliporejea nyumbani alijibwaga kitandani kama gogo la mti
- Anakumbwa na kiu ya njaa ya kimapenzi ya mumewe
- Wanawake wengine walishinda na kukesha pamoja na wanaume zao
- Alikuwa na umaskini wa kimapenzi licha ya kuwa na mali chungu nzima
- Alikosa kustahiwa na mumewe

ii) Ndoa

- Asasi ya ndoa imejaa mateso dhidi ya mwanamke
- Wanaume hawakuiheshimu asasi ya ndoa. mfano Nasaba Bora ana uhusiano wa kimapenzi nje ya ndoa
- Wanawake wanakumbwa na upweke mfano; Bi Zuhura ametelekezwa kimapenzi.
- Wanawake wanaachiwa mzigo wa malezi km. Dora

iii) Ukatili

- Bwana Nasaba Bora anamshuku mkewe kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Amani.
- Wanawake hawashauriwi.

mfano: Majisifu anakataa kumshauri mkewe kuhusu uamuzi wa kumleta Amani kwao.

iv) Umaskini

- Kuna wanawake waliovalia rinda moja siku baada ya nyingine.
- Wanasokomoko wengi walikuwa wahitaji.
- Watoto waliajiriwa kuchunga ng'ombe na hivyo kukatishiwa masomo yao. (Maudhui yoyote 3 X 2 = 6)

5. Mla naye huliwa zamu yake ifikapo

- Nasaba Bora anatoza wanasokomoko pesa ndio Madhubuti aende ng'ambo, madhubuti anaporudi nyumbani kutoka ng'ambo, anamuasi baabake.
- Nasaba bora anawatuma askari kumvamia na kumuua mamake Imani, baadaye yeye (Nasaba Bora) anavamiwa na genge la Oscar kambona na nusura auliwe.
- Nasaba Bora anamwachisha Lowela masomo kutokana na uhusiano wa ki-mapenzi naye, baadaye Mashaka anakatiza masomo yake kwa kuathirika na barua ya Ben Bella ya kukata uhusiano wao wa kimapenzi.
- Nasaba Bora anawatia gerezani Amani na Imani kwa tuhuma za kuua, hata hivyo ng'ombe wake wanaroroma kwa uchungu kwani hawakuwa wamekamuliwa. Aidha, inamlazimu Bi. Zuhura, kumwandalia mwalimu majisifu chai ya mkandaa.
- Nasaba bora anahonga wakubwa jeshini ili kumtafutia Madhubuti kazi; hatimaye, pesa zile zinapotea madhubuti anaporudi kutoka ulaya na kuikataa kazi hiyo; na kutaka kujitafutia nyingine kwa jasho lake.
- D.J analihurumia jimwa jimmy ambalo lilikuwa limefungwa kwa minyororo na kumshauri Bi Zuhura liachwe huru. Mwishowe linapokata minyororo na kuwa huru, linamng'ata Dj mguuni vibaya sana.
- Chechwe makweche analimbikiziwa sifa nyingi kwa kuwa mwana soka hodari nchini Tomoko, hata hivyo anawasahau nduguze na mamake. Aidha anapovunjika fupaja serikali inamtekeleza na pia anakosa ndugu wa karibu wa kumsaidia
- viii)Mwalimu majisifu anadhani ni siri yake mwenyewe kuhusiana na wizi wa mswada na Amani, hatimaye anagundulika na Amani mwenyewe wakati anapomtuma Imani kumwombea vitabu vya kusoma kutoka kwa mwalimu majisifu.
- Mwalimu Majisifu anamkashifu Mashaka kwa kutosoma kitabu cha kidagaa na hata kusema hastahili kuitwa mpwa wake, aidha anapoenda kutoa mhadhara katika chuo cha mkokotoni anashindwa kujibu

maswali kuhusiana na kitabu chenyewe.
- Nasaba Bora anawatesa na kuwauwa watu ili anyakue mashamba yao, baadaye anapomfunulia ukweli Amani kuhusiana na hayo mashamba anatowekea msituni na kujitia kitanzi.
(zozote 10x 2 = 20)

6. Ubaguzi

a. Mke wangu
- Mwanamke anachukuliwa kama ndiye anafaa kuongozwa na mwanamume.
- Wachumba wanapotaka wake, waliosoma wanabaguliwa
- Watu wa daraja la chini hukaa mashambani nao waliosoma wanaishi mjini.
- Wenye vyeo vya juu hawatangamani na wale wa vyeo vya chini.

b. Samaki wa nchi joto
- Sehemu za starehe zilitengewa wazungu kwani wale weusi hawangeweza ada zilizotozwa za juu.
- Wanaoishi katika mitaa bora uliyokuwa na huduma bora ni wazungu, 'ilihali, wale hawakuwa nacho wanaishi katika mitaa duni.
- Waliokuwa wa tabaka la juu walikuwa na watumishi.

c. Damu Nyeusi
- Fikirini alilikuwa akiulizwa maswali ya kuumbua na wazungu.
- Wahadhiri waliwanyima Waafrika alama katika mtihani ingawa walistahili.
- Dereva wa gari anakosa kulisimamisha gari kumchukua Fikirini.
- Waafrika wanapoenda kununua bidhaa katika maduka makubwa wanafuatwa na walinzi wakidhaniwa kuwa wezi.

d. Kikaza
- Viongozi wanakula vizuri huku wananchi wakikosa chakula
- Viongozi wanawabagua wananchi na wanakuwa walafi
- mfano wa kobe.
- Wanawake hawapewi nafasi ya kuongoza.

e. Maeko
- Jamila anapigwa na kutukanwa mara kwa mara.
- Duni anabaguliwa na kulengwa na jamii kwa ulevi wake.
- Jamila anabaguliwa kimapenzi na mumewe.

f. Kanda la usufi
- Mwanamke anabaguliwa kwa kupewa jukumu la ulezi ilhali ulezi ni wa mume na mke
- Sera anabaguliwa shuleni kwa sababu ya mimba.
- Sera alipofukuzwa shuleni, Masazu hakuathirika

g. Maskini babu yangu
- Wenye mali wanaishi katika mitaa bora, uhali maskini wanaishi katika mitaa duni
- Ubaguzi wa kikabila katika ndoa (zozote 5 x 4 = 20)

7. a)
- Haya ni maelezo ya mwandishi
- anawarejea Chris Masazu na wanafunzi wengine wa kiume waliozuru kila sehemu ya shule ya upili ya Askofu Timotheo na kutaka kuacha kumbukumbu ya ziara yao katika shule hii kwa kuwatafuta wanafunzi wa kike ili wawe wapenzi wao
(alama 4)

b) Michezo ya ujana
- Wengi wanajiingiza katika uhusiano wa kimapenzi na kuringwa kama, sela.
- Sela anakatiziwa masomo yake ili aitunze mimba yake.
- Vijana hujiingiza katika ndoa za mapema.
- Kutomakinika masomoni kama Masazu na Sela.
- Watoto wanaozaliwa kutopewa malezi mema (zozote 4x 2 = 8)

c) **Tamaa mbele mauti nyuma**
- Lucy anatamani sana maisha ya London japo hakupata gredi ambayo ingemwezesha kuishi huko.
- Lucy anatamaa ya kufika ulaya hivyo anaamua kuolewa na mzee Crusoe ambaye hakumpenda.
- Lucy ana umri mdogo na anaamua kuolewa na mzee mkongwe, dhaifu na asiye na nguvu za aina yoyote.
- Lucy anaingiwa na upweke na anamchukia mzee Crusoe ila anajifanya anampenda akingoja kifo cha haraka cha mzee Crusoe ili ajitajirishe na pesa zake.

– Alitaka amrithi mzee haraka, hiyo haraka ikimzamisha katika mauti yake. (Zozote 4 x 2 = 8)

8. a) Sifa za ushauri simulizi

– Kuna msimulizi na hadhira.
– Huwa na mpangilio wa beti au fungu.
– Huwa na lugha ya mkato.
– Huelezea hisia za ndani za msemaji.
– Hutegemea sauti na toni.
– Huweza kutambulishwa na ala za muziki.
– Viziada lugha hutumika km. ishara za uso.
– Huweza kutungwa papo hapo km. sifo.
– Huelezea tukio maalum la kihistoria.
– Huhusisha utendaji jukwaani. (zozote 4 x 2 = 8)

b) Aina tatu za maigizo.

– Michezo ya jukwaani.
– Majigambo.
– Vichekesho.
– Ngojera.
– Michezo ya watoto.
– Miviga.
– Ngomezi.

Tan: Mwanafunzi lazima aeleze hoja zake kikamilifu
kutaja 1 maelezo 1 (zozote 3 x 2 = 6)

c) Mbinu za kimtindo za methali

i) taswira/ picha za akilini
Mfano - paka akiondoka panya anatawala.
- Mtupa jongoo hutupa na mtiwe.

ii) Urudiaji/ takriri
Mfano: - Haba na haba hujaza kibaba
- Bandu bandu huisha gogo

iii) Vichezea maneno / mchezo wa maneno
Mfano: i) gunia nzima angerudi na upele
ii)Mkele haendi ukele na angeenda ukele na kujaza mlele

iv) Tanakali za sauti - Chururu si ndo! ndo! ndo!
- Kiliacho pa! kijutie

v) Mbinu za kishairi kwa mfano: Vipande na mizani
- Haba na haba, hujaza kibaba
- Usione kwenda mbele, kurudi nyuma si kazi
hoja – ½ mfanon ½ (Zozote 4 x 1 = 4)

d) Umuhimu wa hekaya.

– Huonya juu ya upumbavu.
– Hutoa maadili kwa wanajamii ili waache kuwatendea wenzao ujanja.
– Huwaokoa wanaodhulumiwa kwa kutumia uwezo mkubwa wa akili walionao.
– Hufunza watu kutenda mema.
– Hufunza kutokana na ulimwengu uliojaa hila na shaka, wema na uadilifu. (zozote 2 x 1 = 2)

MTIHANI WA MWIGO WA WILAYA YA KURIA MASHARIKI 2015
Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari
KISWAHILI
KARATASI YA KWANZA
JULAI/AGOSTI 2015
MUDA: SAA: 1 $^{3}/_{4}$

MASWALI

1. INSHA YA LAZIMA

Wewe ni katibu wa kamati iliyoteuliwa na mkuu wa wilaya kujadili kuhusu madhara ya pombe haramu na mbinu za kuangamiza pombe hiyo wilayani. Andika ripoti ya kamati hiyo.

2. Unyanyasaji wa kijinsia umekithiri katika jamii yetu ya leo. Thibitisha.
3. Sikio la kufa halisikii dawa.
4. Andika insha itakayomalizikia na:
..... Wazima moto waliwasili saa tatu baadaye. Uharibifu wa mali na maisha ulikuwa umeshatokea. Maajabu yaliyoje!

MTIHANI WA MWIGO WA WILAYA YA KURIA MASHARIKI
102/2
KISWAHILI
KARATASI YA PILI
(LUGHA)
JULAI/AGOSTI 2015
MUDA: SAA: 2 ½

1. UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuatia.

Nchi yetu imeraukia mawio ya machafuzi ya kisiasa baada ya shughuli za uchaguzi zilizogonga mwamba mkuu. Hili lilijiri baada ya Tume ya uchaguzi kukoka kuendeleza uchaguzi kwa njia inayostahili. Jambo hili lilizaa msukosuko wa kisiasa usiomithilishwa katika historia ya taifa letu.

Hivi sasa wakenya wanaishi kwenye kambi za watu wasio na makazi. Hiki ni kinaya kikuu kwani matukio haya yamezuka baada ya miongo minne ya uhuru. Vilio vya wakenya vimeshamiri na kupaaza sauti vikilalamikia kukosa makazi, lishe na ndoa kusambaratika. Ndoa zimevunjika baada ya 'wenyeji' kuwatimua 'wageni' na damu kumwagika.

Kenya imekuwa miongoni mwa mataifa yanayowapa faraja wakimbizi kutoka nchi jirani zinazokubwa na vita vya wenyewe. Vita katika Somalia vimesababishwa na koo mbali mbali zinazopigania uongozi hali ambayo imekwamisha shughuli zote za kiuchumi.

Hali ya sasa ya Kenya imechochewa na msururu wa sababu; ukabila na tamaa ya uongozi zilionekana wazi katika miundo ya vyama vikuu vya kisiasa na katika kampeni zao. Wakenya walipiga kura kwa misingi ya kikabila kila upande ukitazamia mtu wao kushinda uchaguzi huo.

Kwa upande mwingine, viongozi hao kutokana na tamaa ya uongozi walikuwa wameamua kushinda uchaguzi huo kwa vyovyote vile. Leo tunavuna matunda ya siasa za ukabila na tamaa ya mamlaka.

Maelfu ya Wakenya ni wakimbizi nchini na katika nchi jirani ya Uganda. Wakenya hao wanahitaji msaada wa chakula na mahitaji mengine ya kimsingi. Serikali na shirika la msalaba mwekundu zimefanya juhudi kuwasaidia wahasiriwa lakini kuna tetezi kwamba ubaguzi umejipenyeza katika ugawaji wa msaada huo.

Waliopewa jukumu la kugawa msaada huo ni sharti waelewe kuwa waathiriwa ni wakenya wenzao na hawafai kubaguliwa kwa misingi ya makabila yao.

Matukio kama haya hayastahili kutukia asilani katika taifa hili.

Twahitaji zao **aali** la viongozi wasiojitwika ubabe bali wawe watumishi wa wananchi wanastahili kutupilia mbali tamaa za kujilimbikizia mali na kung'ang'ania uongozi. Pia katiba inafaa irekebishwe. Wakenya wanastahili kuelimishwa kuhusu undugu na utaifa. Fauka ya haya masuala yanayohusiana na hatimiliki za ardhi yanafaa **kutadarukiwa kwa dhati.**

Maswali

a) Toa anwani mwafaka kwa makala haya.

(alama 1)

b) Taja madhara **manne** ya ukabila.
(alama 2)

c) Shughuli za ugawaji wa misaada zimekubwa na changamoto gani?
(alama 2)

d) Eleza tofauti ya chanzo cha vita nchini Somalia na Kenya. (alama 2)

e) Mwandishi anatoa mapendekezo gani ya kutatua tatizo hili la ukabila.
(alama 4)

f) Eleza kinaya cha maisha ya wakenya kwa sasa.
(alama 2)

g) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika kifungu cha ufahamu.
(alama 2)
i) Mawio -
ii) Tandarakiwa kwa dhati

2. UFUPISHO (ALAMA 15)

Ajira ya watoto ni tatizo sugu linalokumba ulimwengu wa sasa, hasa katika nchi zinazoendelea. Jambo la kusikitisha ni kwamba hivi ndivyo ilivyo katika nchi nyingi za ulimwengu huu. Kuna idadi kubwa ya watoto wanaoajiriwa katika nyanja mbalimbali za jamii. Zipo sababu nyingi zinazowasukuma watoto kutafuta ajira barani Africa kwa mfano, familia nyingi huishi maisha ya ufukara hivi kwamba hushindwa mahitaji muhimu hususan kwa watoto. Kupanda kwa gharama ya maisha kunazidisha viwango vya umaskini. Ukosefu wa lishe pia huwafanya waoto kutoroka nyumbani kutafuta ajira. Janga la ukimwi limesababisha kuwepo kwa idadi kubwa ya mayatima wanaoishi kutafuta ajira ili kuyakimu maisha. Ukimwi umezifanya familia nyingi pia kuwaondoa watoto shuleni ili waweze kuajiriwa kwa lengo la kusalisha pato la familia hizo. Watoto wengine hutoroka makwao kwa sababu ya maonevu. Maonevu haya ni kama vile kupigwa, kutukanwa kila wakati, kunyanyaswa kijinsia na kadhalika. Huko nje hutaabishwa kimwili na kiakili. Hufanyishwa kazi za sulubu zenye malipo duni au wasilipwe kabisa. Hili huwasononesha na kuathiri afya yao.

Wengine hujiingiza katika vitendo vya jinai pale wanapokosa ajira huchukua sheria mikononi mwao, wakaendeleza vitendo vya ukatili kama vile kuwahangaisha watu na kupora mali yao au hata kuwakaba roho. Aidha wengine hujikuta kwenye madanguro ambako huendesha biashara haramu.

Uundaji wa umoja wa Africa hivi majuzi ni hatua muhimu ya kushughulikia matatizo ya Afrika kama vile ajira ya watoto, kuzorota kwa miundo msingi, magonjwa, njaa, umaskini, ufisadi na ukabila. Katika kushughulikia haki za watoto nchi za Africa hazina budi kuzingatia masharti yaliyowekwa na umoja wa mataifa kuhusu haki za watoto. Nchi nyingi za Afrika ziliidhinisha mkataba wa masharti hayo, ikiwemo nchi ya Kenya. Nchi hizi basi lazima zishughulikie haki za watoto kupitia sheria za nchi. Watoto ni rasilmali muhimu na ndio tumaini la kuwepo kwa kizazi cha binadamu.

Maswali

a) Eleza mambo yote muhimu anayozungumzia mwandishi katika aya ya kwanza. (maneno 45 - 50)

(al 6, 1 ya mtiririko

b) Bila kubadilisha maana aliyokusudia mwandishi, fupisha aya mbili za mwisho (maneno 50 - 55)
(Alama 7, 1 ya mtiririko)

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a) Taja vikwamizo **viwili** ambavyo ni kosonanti hafifu
(alama 2)

b) Sentensi hizi ni za aina gani? (alama 2)
i) Uvutaji wa sigara ni hatari kwa afya
ii) Naomba uwaite wanafunzi wale

c) Onyesha silabi inayowekewa shadda kwenye nomino zifuatazo (alama 2)
i) meza
ii) Maneno

d) Nomino 'Risasi' iko katika ngeli gani? (alama 1)

e) Andika sentensi ifuaayo katika hali yakinishi (alama 2)
Askari wasipopiga doria wala kushirikiana na raia hawatakuwa wametuhakikishia usalama.

f) Tunga sentensi **mbili** kuonyesha matumizi mawili tofauti ya alama za mtajo.
(alama 2)

g) Andika katika wakati ujao hali timilifu (alama 2)
Wanafunzi walifanya mtihani wa mwigo

h) Tunga sentensi mwafaka ukitumia kielezi cha:- (alama 2)
i) Namna kiigizi
ii) Cha mahali

i) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali.
(alama 4)
Mwanasiasa mwingine amepoteza kiti chake cha ubunge.

j) Tunga sentensi **mbili** kuonyesha matumizi mawili tofauti ya kiambishi ndi-
(alama 2)

k) Onyesha kishazi huru na tegemezi katika sentensi hii. (alama 2)
Kuimba ambako kutavutia kutashinda tuzo

l) Tunga sentensi yenye fungu tenzi lenye muundo ufuatao
(alama 2)
tS + T + N

m) Andika kwa usemi wa taarifa (alama 2)
Mama watoto aliuliza, “mbona mnajikunyata kama mayatima”.

n) Badilisha vitenzi vifuatavyo viwe katika hali ya kutendeka.
(alama 2)
i) kwea
ii) dhuru

o) Tunga sentensi sahihi ukitumia kihisishi cha kukataa. (alama 2)

p) Bainisha aina za nomino zilizotumika katika sentensi ifuatayo (alama 3)
Kikosi cha askari kiliabiri ndege hadi ujerumani

q) Kanusha kwa umoja
(alama 2)
Mkilia mtapewa maziwa

r) Andika kwa udogo hali ya wingi (alama 2)
Ngoma imepigwa na msichana yule mpaka imepasuka.

s) Unda kitenzi kutokana na nomino ifuatayo.
(alama 1)
Taifa

4. ISIMU JAMII (AL 10)
Eleza makosa matano yanayoweza kutokea wakati wa mazungumzo.
(alama 10)

MTIHANI WA MWIGO WA WILAYA YA KURIA MASHARIKI 2015
102/3
KISWAHILI
KARATASI YA TATU
(FASIHI)
JULAI/AGOSTI 2015
MUDA: SAA: 2 ½

SEHEMU YA A: FASIHI SIMULIZI

1. "Mjukuu wangu, masomo ni jambo muhimu sana. Ufikapo shuleni na kuanza maisha ya shule ya upili, usijingize katika mambo ya dunia anasa na raha nyingi. Vifanye vitabu rafiki wa karibu. Wasikize waalimu na uzingatie wanayoyasema, saidiana na wenzako na utie bidii za mchwa katika masomo. Kumbuka kuwa elimu ndio ufunguo wa maisha mema hapo usoni."

Maswali

a) Tambua kipera cha fasihi simulizi kinachohusishwa na kifungu hiki.
(alama 2)
b) Taja sifa za kipera hiki.
(alama 8)
c) Taja umuhimu wa kipera hiki katika jamii. (alama 8)
d) Matumizi ya kipera hiki huwa na lengo gani katika maisha ya kila siku katika jamii?
(alama 2)

SEHEMU YA B: DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE

2. "Nashangaa vile kwetu tunavyoabudu watu hao wasiojali
a) Eleza muktadha wa dondoo hili
(alama 4)
b) Fafanua hulka za msemewa. (alama 6)
c) Jadili ukweli wa kauli hii. (alama 10)

3. Ndoa ni asasi inayokumbwa na changamoto kadhaa katika jamii ya leo. Jadili ukweli wa kauli hii kwa kurejelea hadithi zifuatazo.
(alama 20)
a) Mke wangu
b) Maeko
c) Mwana wa Darubini
d) Maskini Babu yangu

SEHEMU YA C: RIWAYA - KIDAGAA KIMEMWOZEA

4. "Tunaposherehekea uhuru wetu tunayo furaha tele maana idili na juhudi za watangulizi wetu hazikuwa za bure"
a) Eleza muktadha wa dondoo hili
(alama 4)
b) Kwa kurejelea riwaya nzima onyesha kinyume cha kauli hii. (alama 10)
c) Onyesha sifa za mzungumzaji katika riwaya (alama 6)
5. Jadili mchango wa wahusika Imani na Amani katika ujenzi wa jamii mpya
(alama 20)

SEHEMU YA D: MSTAHIKI MEYA

6. Jina si kitu. Tumbo ndilo muhimu. Tumbo lako na jamaa zako. Watoto wako.
a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
b) Taja mbinu moja ya lugha iliyotumiwa katika dondoo hili. (alama 2)
c) Eleza sifa zozote nne za mzungumzaji.
(alama 8)
d) Dondoo hili linadokeza maudhui fulani katika tamthilia. Yataje na utoe mifano mingine miwili inayothibitisha maudhui hayo.
(alama 6)

7. Jadili mbinu na mikakati wanayotumia wanacheneo kupambana na uongozi dhalimu wa Baraza la jiji la

cheneo.
(alama 20)

SEHEMU YA E: USHAIRI (AL 20)

8. Siafu wamekazana

Nyoka amegutuka, ndani ya shimo kutuna,
Tena amekasirika, hasira zenye kununa,
Nyoka anababaika, shimoni kwa kujikuna,
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika.

Shimoni ataondoka, hilo nataja kwa jina,
Nyoka anajuwa fika, siafu wakiungana,
Nguvu zao zaongezeka, shimoni watagomana,
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika.

Siafu wakijishika, mshiko kushikamana,
Kwamba wanampeleka, sultani wao bwana,
Shimoni wanapofika, nyoka la kufanya hana,
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika

Siafu wanapofika, na nyoka wakikutana,
Nyoka hawezi kufoka, huwa ametulizana,
Ndipo nyoka huondoka, na wana wakilizana,
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika

Kupo na kukanganyika, hilo na natujue sana,
Nyoka anapoondoka, siafu hulaliana,
Huuma hupumzika, hapo hakutafanana,
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika.

Nyoka akishaondoka, na siafu hujazana,
Shimoni wakipeleka, vyakula kutiliana,
Ndilo walilotaka, wale kwa kutulizana,
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika.
(S. Abdu Kandoro)

Maswali

a) Shairi hili linazungumzia nini? (alama 2)
b) Ukitumia vigezo vifuatavyo, eleza aina za shairi hili. (alama 2)
   i) Vipande
   ii) Vina
c) Bainisha matumizi manne ya Jazanda katika utungo huu.
(alama 4)
d) Andika ubeti wa sita kwa lugha nathari.
(alama 4)
e) Onyesha mtunzi alivyotumia kibali chake cha utunzi katika ubeti wa pili.
(alama 4)
f) Fafanua umuhimu wa mkarara wa shairi hili. (alama 4)

WILAYA YA KURIA MASHARIKI
102/1 KARATASI YA KWANZA - INSHA
JULAI/AGOSTI 2015
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

SWALI LA KWANZA – RIPOTI

SURA

- Anwani ionyeshwe
- Kamati – Wahusika
- Kiini cha kuteuliwa kwa kamati hiyo.

Mwili

✓ Utafiti wa kamati na yaliyokubalika kama madhara ya unywaji wa pombe mf.
   i. Magonjwa – Ugonjwa wa ini, kisukari
   ii. Watoto kukosa elimu, mavazi, chakula n.k
   iii. Upungufu wa nguvu za kiume
   iv. Kusambaratika kwa familia

✓ Mapendekezo ya kamati:
   i. Kushtakiwa na kufungwa kwa wahusika.
   ii. Kutozwa faini ya kiwango cha juu kwa wale wanaohusika.
   iii. Kufutwa kazi kwa wale wanaohusika hasa watumishi wa serekali.
   iv. Kuelimisha Wananchi kuhusu madhara ya pombe (kupitia mikutano na vyombo vya habari.
   v. Kuzua nafasi za kazi kwa vijana.
   vi. Kubuni mikakati ya kupunguza Umaskini katika jamii.
   vii. Kuhimiza mafunzo ya kidini yanayopinga matumizi ya pombe.

✓ Hitimisho
   - Mtahiniwa aonyeshe kuwa yeye ni katibu wa kamati husika.

Swali la pili

Hoja za unyanyasaji wa kijinsia

(a) Wanawake

- Kunyimwa nafasi za kujiendeleza kielimu.
- Ndoa za mapema na za lazima.
- Ajira ya watoto (vijakazi)
- Kuingizwa katika ukahaba/ufusika.
- Kubakwa/kunajisiwa.
- Ubaguzi katika kuajiriwa katika nyanja fulani mf. Uhandisi
- Kudhulumiwa kimapenzi kazini/shuleni.
- Kunyimwa likizo awapo mja mzito.
- Kukeketwa au tohara ya lazima.
- Kunyimwa kura katika uchaguzi.
- Kupigwa na wanaume
- Kunyimwa haki ya kumiliki mali.

✓ **Wanaume**

- Ajira ya watototo (utwana)
- Ushoga/ulawiti/usenge
- Kuingizwa katika makundi haramu kwa lazima k.m Mungiki
- Kuchapwa na wake zao.
- Kunyimwa haki zao za ndoa.

Swali la 3

Hii ni insha ya methali. Mtahiniwa asimulie kisa kinachorejelea maana ifuatayo.

✓ Kitu kilichoharibika au mtu aliyeharibika kitabia/kimaadili hawezi hawezi akarekebika kitabia akawa mzuri au kisa kithubitishe hali ya jambo baya zaidi ambalo hata lifanyiwe nini haliwezi kuwa zuri au sawa.

Swali la nne

✓ Lazima Mtahiniwa amalizie kwa maneno haya. Asipomaliza kwa maneno haya atakuwa amejifungia swali.
✓ Kisa kikubaliane na dondoo.

WILAYA YA KURIA MASHARIKI
KISWAHILI KARATASI YA PILI
MWONGOZO WA KUSAHISHA

1. UFAHAMU

a) Athari za uhasama wa kikabila

Athari za uongozi mbaya

Machapuzi ya kisiasa yoyote 1x1=1

b)

- Ubaguzi wa kikabila
- Njaa
- Mauaji
- Ukimbizi
- Uchumi kusambaratika
- Ukosefu wa makazi zozote $4x^{1}/_{2}$=2mks

c) Ubaguzi wa kikabila

d)

- Nchini Somali vita vilisababishwa na uhasama na kiukoo/koo mbalimbali zinazopigania uongozi
- Nchini Kenya vita vilisababishwa na ukabila, tama za uongozi/ mamlaka/ ubinafsi na viongozi

e)

- Marekebisho ya katiba
- Viongozi wawe na maadili mema
- Wakenya wanastahili kuelimishwa kuhusu umoja/undugu/utaifa
- Masuala yanayohusiana na ardhi yafaa yashughulikiwe/yapewe kipao mbele

Viongozi wawe watumishi wala sio wababu/watawala. (zozote 4x1=alama 4)

f)

- Vita vya kikabila kuzuka Kenya, miongo mwao baada ya uhuru.
- Kiziwa cha amani/paraja (kama) kugeuka na kuwa uwanja wa vita/kuwa makao ya wakambizi

g)

i) Mawio-matokeo/athari/maafa

ii) Kutafarukiwa kwa dhati-kushughukiwa/ kupewa kipao mbele

2. UFIPISHO

a)

- Ajira ya watoto ni tatizo sugu nilinalokumba ulimwengu wa sasa
- Zipo sababu nyingi zinazoasukuma watoto kutafuta ajira barani Afrika.
- Familia nyingi huishi maisha ya upukara
- Kupanda kwa gharama ya maisha kunazidisha umaskini
- Ukosefu wa lishe
- Janga la ukimwi limesababisha kuwepo kwa mayatima wanaoishi kutafuta ajira.
- Watoto hutoroka kwao kwa sababu ya maonevu
- Huko nje utaabishwa kimwili na kiakili (zozote 6x1=alama 6)

b)

- Huchukua sharia mikononi mwao
- Kuwangaisha watu na kupora mali yao/kuwapa roho
- Hujikuta kivonge madanguro ambako huendesha biashara haramu
- Uundaji wa umoja w Afrika ni hatua ya kushughulika matatizo barani.
- Ajira ya watoto
- Kuzorota kwa miundo msingi
- Magonjwa
- Njaa, maskini, ufisadi na ukabila
- Nchi za afrika hazina budi kuzingatia masharti yaliyowekwa kuhusu haki za watoto
- Nchi zishughulikie haki za watoto kupitia sheria za nchi.
- Watoto ni rasilimali muhimu
- Watoto ndio tumaini la kuwepo ka kizazi cha binadamu. (zozote 7x1=alama 7)

MATUMIZI YA LUGHA ALAMA 40

a) /f /, /s/, /sh/, /th/ zozote 2x1=alama 2

b)

i) Sentensi ya taarifa

ii) Sentensi ya rai/ombi

c)

i) Meza

ii) Maneno

d) I-ZI

e)

- Askari wakipinga doria na kushirikiana na raia watakuwa wametuhakikishia usalama.
- Askari wanapopiga doria na kushirikiana na raia watakua wanatuhakikishia usalama

f)

- Matumizi ya alama za infaso
- Kunukuu anwani ya shairi/wimbo/ kitabu katika sentensi au makala
- Kupungia neno la kukopwa/kigeni katika sentensi
- Kuandika usemi halisi zozote 2x1=(alama 2)

g) (mwanafunzi lazima atunge sentensi)

h) Wanafunzi watakuwa wamefanya mtihani wa mwigo .. (1x2=alama 2)

i)

- Tapwi } Alianguka matopeni tapwi
- Furifuri } Hapo palifurika watu furifuri
- Chiririchiriri Maji yalichururika chirichiriri

ii)

- Kirangu/ndani/chini/nyuma/kwa dada
- Nakuru/mashariki/ulaya/Kenya
- Darasani/garini/shambani

		S $^1/_2$				
KN $^1/_2$			KT $^1/_2$			
N $^1/_2$	V $^1/_2$	T $^1/_2$	N $^1/_2$	V $^1/_2$	V $^1/_2$	N $^1/_2$
mwanasiasa	mwingine	amepoteza	kiti	chake	cha	ubunge

j)

- Kuonyesha msisitizo mimi ndimi kiranja mkuu
- Kiwakilishi cha nafsi ndiye ndiwe,ndisi
- Kitenzi kishirikishi kipungufu wewe ndiwe msemaji wetu. (zozote 2x1= alama 2)

k) Huru-tutashinda tuzo

Tegemezi-kuimba ambako kutavutia

l) Chacha <u>hajawahi kupalilia mtama</u>
TS T N

Wanafunzi <u>wangali wanafanya mtihani.</u>

TS T N

Yeyote ile 1x2= (alama 2)

m) Mama watoto alitaka kujua sababu za wao kujikunyata kama mayatima .(1x2= alama 2)

1)

i) Kwea-kweleka

ii) Shuru-shurika

n)

- Hata !
- Kamwe! } kamwe usinihusishe, mimi simo.
- Ng'o! najua watamani maziwa yangulakini sikupi ng'o! yeyote 1x2=alama 2

r)
- Kikosi cha askari-Nomino ya jamii/makundi
- Ndege-nomino ya kawaida
- Ujerumani-Nomino ya pekee

s) Usipolia hutapewa maziwa
t) Vigoma vimepigwa na visichana vile mpaka vimepasuka
q) Taifa-taifisha

ISIMU JAMII

- <u>Makosa yanaweza kutoke wakati wa mazungumzo</u>
- Athari ya lugha ya kwanza-ulefu/urefu
- Hali ya kiakili ya msemaji-mgonjwa au mlevi hudondosha sauti
- Kuhamasisha mafunzo na lugha moja hadi nyingine-katoto/kitoto
- Kutodhibiti mfumo n a ngeli katika lugha-ng'ombe hii/ng'ombe huyu
- Kujumuisha kanuni za lugha :mnyambuliko wa vitenzi ⇒soma-somesha

  Penda-pendesha(kosa)
- Kasi ya uzungumzaji huathiri usanifu wa lugha
- Kosa la kimakusudi-dhamira/lengo lakuwashawishi au kuburudisha
- Kosa la kutoelewa maana ya neno kimatumizi au umilisi wa maneno.Kudhani neno 'tetesi' linalo tokana na neno 'teta' ilhali maana yake ni uvumi. Zozote 5x2= alama 10

TATHMINI YA PAMOJA KOUNTI NDOGO YA KURIA MASHARIKI
102/3
MWONGOZO WA KUSAHISHA FASIHI 2015

SEHEMU YA A : FASIHI SIMULIZI

a) Mawaidha (alama 2)

b)

- Ni mawazo mazito kuhusu maisha k.v unyumba, urithi, mapenzi, malezi n.k
- Mawaidha hulenga hadhira maalum
- Hulenga maudhui maalum
- Huibua maadili yanayohitajika kuzingitiwa
- Ujumbe katika mawaidha hujitokeza moja kwa moja.
- Hutolewa na mtu mmoja anayeaminika kuwa mjuzi wa anayezungumziwa
- Hutumia lugha ya kipekee yenye maana kina na ya kuvutia hadhira
- Tamathali nyingi za usem hutumiwa zozote (4x2=8)

c)

- Ni njia mojawapo ya kuendeleza utamaduni wa jamii
- Huwapinda watu kushiriki ipasavyo katika shughuli za utamaduni
- Huelekeza jamii inapotoka
- Hujasirisha waoga na kuwapa ukakamavu wasio nao
- Huelimisha
- Huwaondolea ujinga wengine katika jamii
- Husaidia katika uchanganuzi wa mambo na hali zinzoikabili jamii
- Huamarisha uadilifu katika jamii. (zozote 4x2=8)

d)

- Kuonya
- Kushauri
- Kuelekeza
- Kutahadharisha
- Kuelimisha (zozote 2x1=2)

SEHEMU YA B HADITHI FUPI

3. DAMU NYEUSI

a) Msemaji ni Fikirini

– Anamwambia Fiona

- Wako barabarani
- Hii ni baada ya Fikirini kunaswa na polisi kwa kutofunga zipu na kutozwa faini ya dola mia mbili.

(4x1= alama 4)

b) Fiona

- Mwanamke mweusi pandikizi la miraba minne
- Katili
- Mwongo
- Mwenye vitisho
- Hajithamini
- Mwizi
- Mnafiki

Kutaja = 1 Maelezo = 1 3 x 2 = 6

c) Binafsi

- Watu weusi wanabaguliwa katika nchi ya watu weupe
- Wanaadhibiwa vikali kwa makosa madogo kwa kuwa weusi
- Wahadhiri chuoni wanapendelea wazungu
- Walinzi kwenye maduka makubwa huwakagua zaidi
- Dereva anampita Fikirini kwa kuwa ni mweusi
- Wanafunzi wanakejeli Fikirini
- Wanabaguliwa na weusi wa marekani kwa kuibiwa na kutishwa. (Zozote 5x2=alama 10)

3. MKE WANGU

- Utabaka
- Taasubi za kiume
- Ukosefu wa ajira
- Utamaduni
- Mizozo ya ndoa kuzozana
- Umaskini
- Kutoaminiana
- Ukengeushi
- Ubaguzi (5x1=alama 5)

a) Maeko

- Taasubi za kiume
- Ulevi
- Ushauri mbaya
- Uchochezi
- Mapigo/dhuluma
- Kutowajibika
- Upweke/ukiwa (5x1=alama 5)

b) Mwana wa darubini

- Ulaghai
- Ulevi
- Unafiki
- Mapenzi nje ya ndoa
- Ushauri mbaya
- Malezi duni
- Kufukuzwa kazi

c) Maskini babu yangu

- Ukabila
- Ubaguzi wa rangi
- Vifo
- Ukiukaji wa sheria na haki
- Malezi

(Maelezo kamilifu yatolewe kwa kila hoja)

4. KIDAGAA KIMEMWOZEA

a)

- Maneno haya ni ya Balozi wa Mtemi Nasaba Bora
- Walikua uwanjani wa nasaba Bora
- Anamsifu Mtemi kwa kusema kuwa ana utambuzi kuliko wazungu
- Walikuwa wakisherehekea siku kuu ya wazalendo. (alama 4)

b) Kinyume cha kauli hii

- Nasaba bora alipokuwa katika Wizara ya Ardhi na makao. Alipicha faili za raia badala ya kuwatolea huduma.

- Utawala wa Uingereza na ule wa Tomoko huru unasisatititi juhudi za mashujaa kwa kutowafidia mashujaa k.v Matuko Weye
- Viongozi wa Sokomoko wanausaliti wajibu wao kuboresha uongozi. Wanamsifu nasabara Bora, kiongozi badala ya kumkosoa k.v balozi mashamba aliyoiba.
- Alijitengenezea faili ili zimfae.
- Serikali inamtekeleza chechwe, badala ya kumtuza akichezea timu ya taifa. (zozote 5x2=alama 10)

c) Sifa za mzungumzaji

- Mbinafsi
- Mpyoro
- Mwenye tamaa
- Ni barakala (mpenda cheo)
- Ni mkware/msherati
- Ni mwongo/mdanganyifu
- Ni katili (zozote 6x1=alama 6)

5. Amani

a) Aliongoza mapinduzi yaliyomngoa mamlakani Mtemi ili jamii utawale wa haki na usawa

b) Anapigania jamii yenye kuthamini maridhiano na msamaha-aliwasamehe waliomkosea : Mtem Nasaba Bora Mwalimu majisifu

c) Anataka jamii yenye kuwathamini walemavu-anampa matuko weye kasri la majununi

d) Anataka jamii inayofaulu kwa kutumia njia halali-hakufanyiwa mtihani kamaFao.

e) Anataka jamii yenye kujali maslahi ya wengine-anawajali wote marafiki na adui

f) Jamii yenye kukuza vipawa-ni mwandishi bora

g) Jamii inayothamini elimu-anasema watu wanahitaji elimu ya chuo cha maisha

h) Vijana wanaojiheshimu-hashiriki katika mapenzi ya kiholela ingawa nafasi zilikuwepo

i) Jamii inayokula jasho lake-yeye hamwibii wala kumnyang'anya mtu. Zozote 5 x 2 = 10

Imani

1. Anabadilisha miiko isiyofaa katika jamii-mwiko kuhusu mtu kiberenge
2. Anabadilisha mtazamo wa jamii kuhusu wamelavu hasa mwalimu majisifu
3. Mwenye mapenzi ya dhati-anawaenzi binadamu wote-amani, walemavu, uhuru, Dj na kadhalika.
4. Jamii yenye bidii-habagui kazi wanafanya uyaya kwa mshahara duni
5. Jamii yenye kuwahusisha vijana wa kila jinsia
6. Ni kijana nayejiheshimu-ingawa alishirikiana na Amani kwa takribani kila jambo, hakushawishika kuhusiana naye katika mapenzi ya mapema.
   Zozote 5 x 2 = 10

★ Kadiria hoja zingine

TAMTHILIA MSTAHIKI MEYA

6.

- Maneno haya yanasemwa na Bili
- Anamwambia mstahiki Meya
- Wamo afisini mwa Meya
- Ni baada ya Meya kumshukuru Bili kwa ushauri aliompa uliomwezesha kuwa meya na mara hii anamtaka Bili kumshauri kumhusu mwanakandarasi ambaye ameenda mahakamani kumshtaki kwa kuvunja mkataba kinyume na sheria.

4 x 1 = 4

b) Takriri/urudiaji-Tumbo (alama 2)

c) Mzungumzaji- Bili

- Mshauri mbaya
- Mwenye majisifu
- Mwenye ubinafsi
- Mpenda makuu
- Ana tamaa
- Msaliti
- Fisadi
- Laghai
- Mnafiki
- Mpenda anasa
- Barakala 2 x 4 = 8 (Kutaja 1, Mfano 1)

d) Ufisadi (alama 1)

- Wakati Meya Bili na Diwani I na Diwani II wanakubaliana kuuza fimbo ya Meya ili kujipatia pesa. (alama 1)
- Meya kutumia cheo chake kujinyakulia mashamba na kisha kumgawia Bili vipande vinne vya ardhi (alama 1)

7. Mikakati ya Wanamchemeo ya kujikomboa ni kama vile :

- Walisusia kazi/kugoma
- Walitumia wawakilishi wao kama vile, Tatu Beka
- Waliimba nyimbo za ukombozi
- Walizinduana kama vile Siki na Diwani III
- Waliwasilisha malalamiko yao kupita kwa jamaa za Mstahiki Meya k.v Siki
- Walitumia mbinu ya ushauri kama vile Diwani III

– Usaliti kwa mfano; Meya alisalitiwa na waajiri wake kama Bili mambo yalipokwenda upogo

– Uchochezi za kuhimizana

– Vita vya maneno kama alivyo fanyia Siki kwa Meya

– Wafanyakazi waliaandamana kupinga udhalimu

– Sheria

- Hatimaye Meya anashikwa na askari na kuambiwa ataenda kueleza mbele.

Vyombo vya habari vinatangaza hali ilivyo nah ii inafanya hata wageni kutoroka Cheneo harakati za ukombozi wa kisasa.

USHAURI

9.

(a) Ukombozi wa wanyonge/udhafimu wa wanyonge.

(b)

- Mathnawi –shairi lina vipande viwili
- Mtiririko-vina vya nje na ndani vinatiririka

(c)

– Nyoka-mkoloni/kiongozi Fulani

– Siafu-waafrika wadhulumwa

– Shimo-nchi/ serekali/afisi/mamlaka/Fulani

– Siafu wamekazana-ni harakati za ukombozi

– Nyoka amekasirika-ni ile wasiwasi ya kuondolewa mamlakani

– Siafu wakujishika-ni ile wasiwasi ya kuondolewa mamlakani

– Sultani-kiongozi mpya

– Wana wa nyoka-ni washirika wa kikoloni

– Siafu hulaliana-kutowajibika kwa waafrika/ viongozi wapya

– Vyakula-raslimali za nchi (Zozote 4 x 1 = 4)

(d) Msanii anasema kuwa mkoloni akishoanoka waafrika huanza kungangania madaraka hata kwa kutumi ufisadi kwani ndivyo walivyotaka

Anasisitiza kuwa harakati za ukombozi wa wafrika zimemtia mkoloni wasiwasi (Alama 4)

(e) Kuboronga sarufi/kubananga sarufi/ukiukaji wa kisarufi-shimoni atandoka, hilo nataja kwa jina badala ya ataondoka shimoni, nataja jambo hilo kwa jina

– Shimoni watagombana badala ya watagombana shimoni

Tabdila-anajuwa badala ya anajua

Inkisari-zongezeka badala ya zaongezeka (Zozote 2 x 2 = 4)

(f) Ni kiini cha ujumbe wa shairi hili-unasisitiza harakati za ukombozi wa wafrika/raia

Uwasaidia katika kumbukizi na ukariri/umbaji wa shairi hili

Unadokeza kichwa cha shairi hili kama kingekuwa hakijatajwa. (2 x 2 = 4)

MERU.
CHETI CHA KUHITIMU KISOMO CHA SEKONDARI
102/1
KISWAHILI
KARATASI YA 1

(Insha)

1. Lazima
   Siku za hivi karibuni imekuwa kawaida kwa wanafunzi wa shule ya upili ya Matumaini kusokotwa na tumbo baada ya kila mlo. Ukiwa katibu wa Baraza la Wanafunzi matokeo ya uchunguzi wenu.
2. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali:
   Atanguliaye kisimani hunywa maji maenge
3. Matokeo mema ya mtihani wa katika shule yoyote ya humu nchini hutegemea juhudi za mwalimu mkuu pekee Jadili.
4. Tunga kisa kitakachomalizikia kwa maneno yafuatayo:
   ...mwishowe nilikuja kungamua kwamba jitihada za wenzangu ndizo zilizonisaidia kuvuka daraja hiyo.

MERU.
CHETI CHA KUHITIMU KISOMO CHA SEKONDARI
102/2
KISWAHILI
KARATASI YA 2

Tunapoakisi hatua ambayo mfumo wa kiteknohama umepiga misamba, kizazi cha vichakazi (facebook) kimetoweka na kupisha kile cha kututumiwa (GMO). Sidhalilishi hivi vikembe na vijikembe vya kututumuliwa japo kunao wenye falfasa hasi kuhusu vikembe hivi. Vijetegemeo mji wao ja waso haya.Hivi vya kutitimuliwa vina mitindo anuai ya kujinakia.Kama wewe si kufu au lahiki yao basi wewe jua bayana kuwa umepitwa na wakati. Utembeapo katika vitongoji vya janibu hizi si Gitau hadi Kaanwa, si Thuchi hadi Mutuati...sisemi Mukothima, utapatana na vikembe HIVI VYA KUTUTUMULIWA. Barobaro hujivika magwanda yanayoonekana kama yatabambuka wakati wowote na kuacha wazi sehemu tunazotegemea.

Vijembe navyo huwa vimejisetiri nusu kwa vijigwanda ambavyo vimeundwa kutoka kwenye shashi. Wafahamu shashi?Kile kitambaa kidogo cha kupangusia pua. Japo mimi vizazi hivi huviona maridadi na anisi, ni yakini kwamba maadili yamewapaa kabisa. Maghulamu wa kukutumuliwa hutembea kwa miondoko au kwa kudakia ukipenda. Zamani nikiwa mdogo tulivaa kaptura na shati za kawaida.Tulijinakia kuchezea matope huku tukivaa nguo safi siku ya Dominika pekee.

Vikembe vya kututumuliwa daima vina vidubwasha maskioni vikiburudika kwa mahadhi ya miziki kutoka kwenye simu zao za ruhunu. Hata kikutane na nani au nani sharti ampishe njia.Enzi zetu mwalimu hakuwa akifanya mambo mengine kama vile kula aina fulani ya chakula sisemi hata kwenda haja. Ukipatana naye njiani wee! Sharti utafute mahali ujifiche mpaka mwalimu apite.Vikembe vya kututumuliwa huwa tunaviheshimu sana. Mara nyingi vitakuona vipi na huku vikembe na vijikembe hutembea huku vimepatikana kama mwanakima na mamake. Waso haya wana mji wao.

Ukikutana nvyo njiani utatamani kurudisha saa yako ya maisha nyuma kidogo. Lakini ndugu, ujajani moshi, ukienda .. Hubagui baina ya vikembe na vijikembe kwani wote vipuli vimebanwa katika sikio moja na kama si moja kijikembe cha kututumuliwa huwa na kipuli kirefu kifikiapo hadi begani.Kijikembe hutembea huku kimesetiri miguu yake kwa jumu yake kwa jumu ambazo zimefika hadi kwenye goti. Na visigino je? Yuatembeahuku akihofu ardhi isibonyee au kuseteka./

Enzi zetu kila baada ya shughuli za shule jioni tulikuta faradhi za kila nui zatusubiri. Mojawapoilikuwa kuwapeleka mifugo malishoni. Kizungumkuti kilikuwa pale ambapo katika michezo yetu ya vijana, ng'ombe wataishia katika shamba la jirani. Jioni hiyo sharti uyatayarishe sisemi makalio kwa utovu wa tafsida Lakini mijeledi itazuru hapo si katiyi.

Vile vikembe vyetu vya kututumuliwa vitakuwa pengine kwenye runinga au kwenye simu zao za rununu na wakati mwingine vimepakata vipakatalishi huku vikibovya vidude hapa na pale. Kila shughuli yao

huwa ya mwendo wa pole pole havina mchapuo. Vinyonge hivi si kama vya enzi ya mababu zetu ambao walikuwa wakichapa mpira juu na kuketi kunusa ugoro huku wakisubiri mpira urudi ndiposa waendelee na mchezo wao. Vikembe vya kutumuliwa huupisha tu na kikiteleza na kuanguka kidogo basi, mchezo umekoma hadi kipelekwe si zahanatini Lakini katika hospitali kuu ya daraja latano.

Kila jumapili jirani yangu alikuwa na zamu ya kushughulikia kichwa change kwa wembe wake. Hakuwa na shufaka au huruma ukipenda. Kichwa kilibaki kama kupe. Usishtuke kuviona vikembe vya kututumuliwa vichwa vyao vina ukwasi wa nywele si kipilipili bali kama za Bob Marley. Naona kana kwamba siku hizi kunz uhaba wa vinyoleo

.

Sisemi kizazi kimetukinai, hata chembe. Ni kwa kiteule kwa hivyo tusikipurukushe au kukinyanyapaa. Kila uchao lawana zaradidiwa kuhusu kizazi hiki. Haya ni mambo mazito ja jabali na hivyo basi kinachobaki ni kukihusisha katika ushaui na nasaha. La sivyo sisi wenyewe ndio tutakuja kulio kilio cha mbwa mdomo juu.

Maswali

a) Ipe taarifa hii anwani mwafaka. (alama 2)
b) 'Kizazi chetu kimekosa maadili.' (alama 3)
Thibitisha kwa mujibu wa taarifa hii.
c) Eleza tofauti nne ambazo mwandishi ameangazia kati ya kizazi cha zamani na kile cha kisasa. (alama 4)
d) Mwandishi anamaanisha nini kwa : (alama 3)
   i. ...umepitwa na wakati
   ii. ...vimeundwa kutoka kwenye shashi
   iii. mijiledi itazuru hapo si katiti
e) Eleza maana za maneno haya kama yalivyotumiwa katika taarifa. (alama 3)
   i. kujinaki
   ii. faradhi
   iii. tusikipurukushe

2. SEHEMU B:UFUPISHO(ALAMA 15)

Inaridhisha kuyasikia mengi kuhusu mikakati ambayo serikali imeanzisha kuimarisha maendeleo ya nchi.Ni kweli kuwa maendeleo huhitajika kuonyesha mafanikio ya nchi ili kumaliza umaskini nchini.Ni juzi tu serikali imeanzisha ujenzi wa reli ambao umeibua malumbano mengi pamoja na upanuzi wa uwanja wa ndege wa Jomo Kenyatta ukiwa miongoni mwa miradi mengine mingi.

Kuna mipango kabambe ya kuwezesha usafiri wa maji uimarike zaidi katika mto Nile ili manufaa yake pia yaonekane katika eneo la Afrika mashariki sio tu Misri.

Ustawi wa taifa pia umelengwa kwa kupigia debe swala la pesa mashinani ili serikali za gatuzi ziweze kufadhili miradi moja kwa moja bila kutegemea serikali kuu.Na Ikiwa ugatuzi huu utafaulu basi vijana na wanawake washugulikiwe kwa kuwapa mikopo ya kuanzisha biashara ndogo ndogo.

Maendeleo hayawezi kuimarika bila ujenzi na upanuzi a barabara ili kukuza teknolojia ya mawasiliano.Jambo hili litarahisisha usafirishaji wa bidhaa kutoka sehemu moja hadi nyingine.

Elimu pia ni kigezo muhimu na msingi thabiti wa kuega uchumi kwa kila nchi.Katika mabara yalioendelea asilimia kubwa ya wnanchi huwa na kiwango cha juu cha elimu.Kwa hivyo ni jambo muhimu kwa serikali kutoa elimu ya bure katika shule za msingi hadi shule za upili.Pia kilimo kipanuliwe kwa kutumia mbinu za kisasa na teknolojia mpya iwezeshe kwa hali na mali mashambani ili kuwaajiri watu wengi katika sekta hiyo.

Azma na matumaini ya kila nchi kuendelea hukabwq na matatizo kwa kuwa Fedha zinazohitajika zinashinda hata bajeti y mwaka mzima ya nchi hizo.Kuna uhaba mkubwa wa wataalamu mbalimbali wenye ujuzi wa kufaa katika sekta nyingi hapa nchini.

Pamoja na kuweko kwa viongozi wenye matumbo makubwa ambao humimina Fedha zenye manufaa kwa wananchi,kuna ukosefu wa vifaa vya kisasa vinavyorahisisha utenda kazi.Vikiwepo huwa duni kulingana na viwango vya maendeleo.

Kuna pengo kubwa sana kati ya matajiri na maskini hivi kwamba itachukua muda kuyashawishi matabaka haya mawili.Takwimu sahihi ya mahitaji ya watu katika maeneo fulani yahitajika ili serikali iweze kusambaza miradi kulingana na jinsi eneo lilivyo.Wamiliki ardhi kubwa wamekuwa na mzizi iliyokita kwenye ulingo wakisiasa hivi kwamba ni vugumu na hatari kugusia suala la umiliki wa ardhi.

a) Ni juhudi zipi zilitiliwa maanani kuimarisha uchumi? (maneno 55) (alama 6,1 ya utiririko)
Matayarisho
jibu

b) Kwa maneno yasiyozidi 55 fupisha aya tatu za mwisho. (alama 7, 1 ya utiririko)
Matayarisho
Jibu

3. SEHEMU YA C : MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a) Andika mifano minne ya vitenzi vya silabi moja katika ya kutendesha. (alama 2)

b) Unda sentesi yenye muundo ufuatao : (alama 2)
KN(N+V),KT(t+ V+E)

c) Taja sifa inayotofautisha sauti / ny/na/ng/
(alama 2)

d) Ainisha vihusishi katika sentensihii :
Tulichakura tarakilishi ya mwalimu iliyokuwa kando ya dawati baada ya mtihani kukamilika.
(alama 3)

e) Tumia kiunganishi seuze / sembuse katika sentensi.
(alama 2)

f) Eleza maana tatu za sentensi hii.
Chakula kingine kimeliwa na wageni. (alama 3)

g) Ainisha vitenzi katika sentensi hii.
Hawa ndio wageni tuliokuwa tukingojea kwa hamu.
(alama 2)

h) Hizi ni mofimu za aina gani? (alama 3)
Kiwavi
Miwani
Karatasi

i) Akifisha
Toka nje au niku nyanya akaamuru murithi
(alama 3)

j) Changanua kwa kutumia vishale.
Swali hilo lilikuwa rahisi sana. (alama 4)

k) Yakinisha
Chakula hakiko tayari hivyo wageni wasinawe mikono. (alama 2)

l) Ainisha vishazi katika sentensi hii.
Kama nitamkuta nyumbani nitamshauri asome kwa bidii.
(alama 3)

m) Tunga sentensi ya neno moja yenye sehemu zifuatazo : (alama 3)
Kikanushi
Hali timilifu
Mtendewa
Kitenzi cha silabi moja
Kauli ya kutendesha
Kiishio

n) Andika katika usemi wa taarifa :
“Mkishinda timu hii leo nitamtuza.”Mkufunzi akatwambia.
(alama 3)

o) Tambua yambwa na ueleze ni za aina gani.
Wazazi waliwanunulia wanafunzi bora zawadi nyingi kwa hundi.
(alama 2)

p) Nyambua neno hili katika kauli ya kutendesha. (alama 1)
Jua

4. SEHEMU D : ISIMU JAMII (ALAMA 10)

Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali
Anachukua ile ngoma kijana Rooney,
Kwake chicharito...anachenga moja , mbili

Hatari! Hatari! Hatari kwenye lango..

a) Hii ni sajili gani? (alama 2)

b) Eleza sifa nane za sajilli hii.
(alama 8)

MERU.
CHETI CHA KUHITIMU KISOMO CHA SEKONDARI
102/3
KISWAHILI
KARATASI YA 3

Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine : Ken Walibora , S.A Mohammed, Kanda la Usufi : Rhoda Nyaga

1. "Tutaondoka ndio, Lakini elewa uchungu wa mwana ajuaye ni mzazi."
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   b) Taja na utolee mfano tamathali ya useme iliyotumika katika dondoo hili. (alama 2)
   c) Eleza sifa nne za msemewa. (alama 4)
   d) Eleza madhara ya mapenzi miongoni mwa wanafunzi. (alama 10)

RIWAYA , Kidagaa kimemwozea : Ken Walibora

2. Eleza namna mbinu zifuatazo zilivyotumiwa na mwandishi wa Riwaya ya Kidagaa Kimemwozea
   a) Sadfa
   b) Kinaya (alama 20)
3. "..unautukanisha ukoo wetu mtukufu. Naona aibu kukuita ndugu yangu."
   a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   b) Ni tamathali gani imejitokeza katika usemi huu? (alama 2)
   c) Bainisha na ueleze migogoro kati ya ndugu hawa. (alama 6)
   d) Fafanua umuhimu wa msemewa katika dondoo hili. (alama 8)

TAMTHILIA.Mstahiki Meya : Timothy Arege

4. "Haitokani na maji Sir. Ni harufu ya taka barabarani sir."
   a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   b) Eleza yaliyopelekea kuwepo kwa harufu hii. (alama 4)
   c) Msemaji ana umuhimu gani? (alama 4)
   d) Harufu hii ni ishara ya uozo uliotawala jamii nzi,a ya Cheneo. Fafanua aina zingine za uozo zinazopatikana katika tamthilia hii. (alama 8)
5. Jadili jinsi maudhui yafuatayo yamejitokeza katika tamthilia ya Mstahiki Meya.
   a. Ukoloni mamboleo (alama 10)
   b. Unafiki (alama 10)

FASIHI SIMULIZI

6. a) Nini maana ya maigizo katika Fasihi Simulizi. (alama 2)
   b) Taja vipera vyovyote vine vya maigizo. (alama 4)
   c) Fafanua sifa za mwigizaji bora. (alama 8)
   d) Taja vikwazo vinavyoweza kukumbuka utanzu wa maigizo. (alama 6)
7. **USHAIRI**

Jicho , tavumiliaje , kwa hayo uyaonayo?
Kicho, utasubirije, maonevu yapitayo?
Kwacho, litajalo nalije, nimechoka vumiliyo
Naandika!

Moyo, unao timbuko, maudhui tusikiayo
Nayo , visa na mauko, wanyonge yawakutayo
Kwayo, sina zuiliko, natoa niyahisiyo
Naandika!

Hawa, wanatulimiya, dhiki wavumiliayo
Hawa, mamiya, na mali wazalishayo
Hawa, ndo wanaoumiya, na mafia wakutayo

Naandika!

Hawa, sioni wengine , kwao liko angamiyo
Hawa, huwapa unene,watukufu wenye nayo
Hawa, bado ni wavune, kwa shida waitikayo
Naandika!

Bado, wawapo mabwana, wenye pupa na kamiyo
Bado, tofauti sana, kwa pato na mengineyo
Bado, tuling'owe shina, ulaji pia na choyo
Naandika!

a) Ni nini shabaha ya mwandishi aliyetunga shairi hili?
(alama 2)
b) Eleza kwa kutoa sababu bahari zinazopatikana katika shairi hili.
(alama 4)
c) Je, mwandishi ametumia mbinu zipi ili kutimiza mahitaji ya kiarudhi? (alama 4)
d) Mtunzi wa shairi hili anawasilisha ujumbe gani katika ubeti wa kwanza?
(alama 2)
e) Eleza sura ya shairi hili. (alama 4)
f) Taja mambo yanayomkera mshairi huyu?
(alama 2)
g) Eleza maana za maneno haya kama yalivyotumiwa katika shairi.
(alama 2)
i. zuiliko
ii. mauko

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA – MERU
KISWAHILI- INSHA
MWONGOZO
Swali la kwanza

Hii ni ripoti. Vipengele viwili vikuu vya utungo huu ni maudhui na muundo (sura)

a) Muundo (sura)

Vipengele vifuatavyo vya kimuundo vijitokeze

i) Kichwa- kionyeshe kamati, ripoti yahusu nini, mahali na kipindi cha kushughulika utafiti huu
ii) Utangulizi- ulenge yaliyotukia nakusasababisha hata ya uchunguzi, wanajopo husika, mbinu za kukusanya data.
iii) Mwili- sehemu hii iwe na vijichwa vinavyobeba maudgui
iv) Hitimisho- hurejelea matokeo ya uchunguzi, yaani muhstari way ale yalioelezwa. Changamoto
v) Mapendekezo- maoni ya uelekezi wa wanajopo katika utatuzi wa kiini cha tatizo lao.
vi) Kujitambulisha
- jina la katibusahihi
- sahihi
- tarehe ya uandishi wa ripoti

b) <u>Maudhui</u>

- Kiwango cha usafi na afya ya wapishi kisichoridhisha
- Maji machafu ya mabomba yasiyotibiwa
- Uhifadhi na utunzaji wa chakula maghalani usiofika kiwango kinachokubalika cha usafi
- Takataka kurundikiwa karibu na mazingira ya sehemu za jikoni
- Chakula kilichotayarishwa kwa njia duni
- Uporo
- Kupikiwa chakula chenye sumu ya mgando
- Viungo vilivyopita kiasi
- Kuwepo na viini viletavyo magonjwwa ya kuambukiza

<u>Tanbihi</u>

i) Katika kuandika/ kuwakilisha ujumbe, mtahiniwa azingatie wakati uliopita, nafasi ya tatu, umoja au wingi na lugha rasmi. Mtahiniwa sharti aandike kwa njia nya taarifa
ii) Mtahiniwa atoe hoja tano au zaidi ili kukamilisha na kutosheleza maudhui

<u>Swali ya pili</u>

Hii ni insha ya methali

Mtahiniwa abuni kisa kinachodhihirisha maana kuwa:

i) Ashirikiaye jambo zuri mapema zaidi yaw engine hufaidika zaidi kuliko waliochelewa.
ii) Himizo mtu asikawie kufanya jambo aliloazimia kulifanya kwani akikawia huenda likawafaidi wengine.
iii) Aanzaye jambo kabla yaw engine ana uewzo mkubwa kufaulu kuliko wajiungao baadaye
iv) Tabia ya uchelewevu huweza kumfanya mtu kuyakosa mambo mazuri
v) Mtu anapopata nafasi ya kujinufaisha hana budi kuitumia

<u>Tanbihi</u>

- mtahiniwa katika kisa chake alenge sehemu mbili za methali (i) kutangulia na (ii) manufaa ya kutangulia huko. Akiegemea upande mmoja, asituzwe zaidi ya alama kumi
- mtahiniwa atunae kisa kimoja

<u>Swali la tatu</u>

Matokeo mema, mbali na mwalimu mkuu hutegemea;

- Nidhamu ba bidii ya wanafunzi
- Walimu waliohitimu na kuwajibika
- Vifaa vya kutosha shuleni
- Miundo msingi
- Wizara ya elimu kuendeleza ukaguzi na viwango bora vya elimu
- Washauri ndani na nje ya shule
- Mchango wa wazazi
- Wafanyikazi wa shule kutoa huduma bora
- Uhusiano mwema na majirani wa shule

- Wadhamini wa shule

Tanbihi

- Mjadala huu unaegemea upande mmoja wa kupinga. Mbali na mwalimu mkuu, kuna washika dau wengine ambao mchango wao huchangia pakubwa katika kutengeneza matokeo
- Mtahiniwa atoe hoja tano au zaidi ili kukamilisha na kutosheleza maudhui

Swali la nne

- Hii ni insha ya mdokezo inayohitaji mtahiniwa kuyasanisi mawazo yake na kubuni hadithi inayoafikiana na kifungu cha kumaliza kisa. Kisa kionyeshe kuwa mhusika aliweza kufaulu kutokana na usaidizi au mchango wa watu wengine katika maisha yake.
- Usaidizi huu uonyeshe ulimwezesha mhusika huyo kupata utajiri, madaraka au matarjio Fulani ya kimaisha

Tanbihi

- Mtahiniwa asipoandika fungu la maneno la kumaliziwa ichukuliwe kuwa ameathirika kimtindo.

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA - MERU
KARATASI YA PILI
(ufahamu, ufupisho, matumizi ya lugha na isimu jamii)
MWONGOZO

A. UFAHAMU

a) Kizazi cha kisasa
Kizazi cha kututumiliwa
(anwani ioane na taarifa)

b) **i)** kuvaa mavazi ambayo hayasetiri miili yao kabisa
ii) hawawapishi njia/ hawaheshimu wakubwa wao
iii) hutembea njiani wameshikana bila haya

c) i) kizazi cha zamani kilivaa mavazi ya kawaida lakini cha kisasa huvaa mavazi ambayo huziacha sehemu nyingine zikiwa wazi
iii) kizazi cha zamani kiliheshimu wakubwa hawa walimu lakini cha kisasa hawawaheshimu hata kuwapisha njia
iv) kizazi cha zamani kilikuwa na kazi kama kupeleka ng'ombe malishoni lakini cha kisasa hushinda kutazama runinga na kuchakura katika vipakatalishi au rununu
iv) vizazi vya zamani vilikuwa na nguvu lakini vya kisasa huwa dhaifu
v) vizazi vya zamani vilikuwa na nywele fupi lakini vya kisasa vinaweka nywele kubwa na husokotwa

d) i) wewe si wa kisasaa/ hujazinduka
ii) nguo ndogo sana
iii) utachapwa/ utapigwa

e) i) kujinakia- kujisifu/ kujigamba/ kujibondoa/ kujifaragua
ii) faradhi- wajibu/ jambe la lazima / sharti
iii) tusipurukishe- tusidharau/ tusipuuze

SEHEMU YA B: UfUPISHO

A

- serikali imeanzisha ujenzi wa reli
- upanuzi wa uwanja wa ndege
- kuwezesha usafiri wa maji kuwa bora zaidi katika mto Nile
- kupigia debe mipango ya pesa mashinani
- mikopo kwa vijana na wanawake
- ujenzi na upanuzi wa barabara
- kutoa elimu ya bure kwa shule za msingi na upili
- kuinua kilimo kwa wananchi

b

- pesa zinazohotajika zinashinda hata bajeti ya mwaka
- kuna uhaba wa wataalamu wenye ujuzi
- viongozi wenye matumbo makubwa ambao umimina pesa
- ukosefu wa vifaa vya kisasa
- hakuna takwimu sahihi ya mahitaji ya maneno mbalimbali
- kuwa na pengo kubwa kati ya matajiri ya maeneo mbalimbali
- wanaomiliki ardhi kubwa kuwa na mzizi uliokita kwenye ulingo wa kisiasa
- ni vigumu na hatari kugusia suala la umiliki wa ardhi

SEHEMU YA C: MATUMIZI YA LUGHA

a) Fisha/ lisha/ nywisha au nywesha/ chisha/ fisha
b) Kitabu hicho kilikuwa kizuri sana
c) /ny/ hutamkiwa katika kaakaa gumu lakini sauti /ng'/ hutamkiwa katika kaakaa gumu
d) Baba alinunua gari seuze/ sembuse baiskeli. (shartisentensi ionyeshe kitu kimoja kikiwa kikubwa au na uwezo kuliko kingine)
e) Chakula zaidi ya……
Baadhi ya chakula
Chakula tofauti na
f) Ya- kihusishi cha la' unganifu
Kando ya- kihushishi cha mahali

Baada ya- kihusishi cha wakati

g) Ndio- kitenzi kishirikishi kipungufu
Tuliokuwa- kitenzi kisaidizi
Tukingojea- litenzi kikuu
Tuikuwa tukingojea- vitenzi sambamba

h) Kiwavi- mofimu tegemezi
Miwani- mofimu huru
Karatasi- vitenzi sambamba

i) “toka nje na niku…..!” Nyanya akaamuru Murithi

j) S- KN + KT
KN- N+ V
N- swali
V- hili
KT- t+ V+ E
t- lilikuwa
V- rahisi
E- sana

k) Chakula kiko tayari kwa hivyo wageni wanawe mikono.

l) Ikiwa nitamkuta- kishanzi kitegemezi
Nitamshauri asome kwa bidii- kishazi huru

m) Mfano: sijakulisha

n) Mfukunzi alitwambia tungeshinda timu hivo siku hivo angetutuza

o) Wanafunzi bora- yambwa tendewa

p) Azawadi nyingi- yambwa tendwa
Hundi- yambwa ala

q) Jua- juza/ juvya

SEHEMU YA D: ISIMU JAMII

a) Sajili ya michezo

– Kuchanganya ndimi
– Kubadili ndimi
– Matumizi ya msamiati maalum wa michezo
– Hukiuka kanuni za kisarufi/ kuiboronga sarufi
– Hutumia mbinu ya utohozi
– Matumizi ya lugha ya mkato
– Matumizi ya uradidi wa maneno au kauli Fulani
– Matumizi ya misimu
– Matumizi ya lugha ya taharuki
– Matumizi ya majisifu mengi
– Kuna kutajataja majina ya wachezaji

Kila hoja sharti iandamane na mfano hai
Kama hoja haina mfano hai mtahiniwa atoe sababu za kutumiia aina hiyo ya lugha
Asipotumia mfano au sabbabu atuzwe nusu alama

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA –MERU
KISWAHILI FASIHI (102/ 3)
MWONGOZO

1. **HADITHI FUPI : Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine- Ken walibora**
   Hadithi ya Kanda la usufi – Rhoda Nyaga

a) Muktadha wa dondoo
i) Ni maneno ya mamake Sela
ii) Kwa mzee Butali
iii) Wako nyumbani kwao
iv) Ni baada ya Sela kufukuzwa shuleni kwa sababu ya uja uzito na babake sela anawafukuza kutoka hapo kwake
nyumbani.

b) Tamathali iliyotumika
Methali- uchungu wa mwana ajuaye ni mzazi

c) Sifa za msemewa- mzee Butali babake Sela

– Mwenye hamaki/ hasira ghamidha- anakasirika sana baada ya kugundua sela ni mjamzito….Leo ndio mtanitambua”
– Ni msikivu- alisikiza ushauri wa wazee, na pia wa mwalimu akawakubalia sela na mamake kurudi pale nyumbani, kumrudisha sela shuleni shuleni baada ya kujifungua
– Msamehevu- baadaye anawasamehe sela na mamake na kuwaruhusu kurudi nyumbani
– Ana msimamo dhabiti- hata baada ya kushawishiwa na mkewe, aliwafukuza pale nyumbani iliwabidi waende
kwa majirani walipohifadhiwa.
– Mtamaduni- anaamina malezi ya msichana ni wajibu wa mama. “……mama gani anayemtazama mwana akigeuka afriti?” alimuuliza mama sela
– Mwenye hekima/ busara- alitambua umuhimu wa elimu ya watoto- akampeleka mwanawe shuleni licha ya
umaskini uliowakumba.
– Amewajibika kama mzazi- anampeleka sela shuleni na hata baaada ya kutambua uja uzito alikubali kumrudisha shuleni, na pia kulea mtoto wa sela

d) Madhara ya mapenzi miongoni mwa wanafunzi

– Mimba za mapema- sela anapata mimba akiwa shuleni.
– Kukatiza masomo- ilibidi sela akatize masomo ili ajifungue
– Mgogoro baina ya wazazi- mzee Butali anamfukuza mkewe na bintiye nyumbani, kumlaumu mkewe.
– Huleta fedheha na uchungu kwa wazazi- mzee Butali aliona aibu na akachanganyikiwa asijue la kufanya. Kwa
hasira anauliza mwalimu je, ni kwa nini sisi huwaleta watoto shuleni…..?
– Sela na wenzake waliaibishwa na kuchekwa na wanafunzi wengine kwenye gwaride
– Watoto wanaozaliwa hawapati malezi ya watoto wao, halisi- Kadogo analelewa na Rozina, na wazazi wa sela.
– Maisha duni ya baadaye/ mkondo wa maisha wa wahusika kuvurugika- sela na masazu kutomudu utaratibu
uliofaa ili kuhukua motto wa kutoka kwa wazazi wa Sela.
– Majuto- sela na pia masazu walijutia kwa matendo yao **Alama zozote 5x 2 = 10**

2. **Riwaya: Kidagaa kimemwozea Ken Walibora**

a) Sadifa

– Maelezo ya sadifa- utukiaji wa matukio mawili au zaidi kwa wakati mmoja bila kupangwa na kuathiri matukio ya baadaaye
– Kukutana kwa Imani na Amani kando ya ziwa mawewa wote wakiwa wamekosa matumaini katika maisha.
– Amani na Imani kupata kazi kwa ndugu wawili (Nasaba Bora na Mwalimu Majisifu)
– Amani anaporudi kutoka hospitalini alimkuta Gaddafi na wenzake wakitaka kumuua Nasaba Bora na akamwokoa
– Amani kupewa kitabu kilichotokana na mswada aliokuwa ameandika yeye pamoja na vutabu vingine.
– Madhubutu kumkuta kijana Amani kwao nyumbani aliye na mawazo kama yake ya kuikomboa jamii yao

ya Sokomoko kutokana na minyororo ya ukoloni mambo leo
- Amani kutaka kazi kwa Nasaba Bora na alipofika tu mchungani na mkamaji wake alikuwa 'mgonjwa'
- Mwalimu Majisifu kukaa kwa muda wa miaka kumi bila kuhusiana na mkewe kimapenzi akiogopa kupata vilema lakini siku aliyozidiwa na baridi na kulala na mkewe ilisadifu kuwa alipata mimba na kupata mapacha waliolemaa.
- Mashaka anachumbiana na Ben Bella mwanawe Maozi huku Nasaba Bora akiwa na uhusiano na Lowela Bintiye Maozi
- Imani alipopata barua ya Amani iliyohusu mswada ulioibiwa anaitwa na Dora na kuacha barua mezani na majisifu anaisoma na kuelewa kuwa Amani ndiye mwandishi wa ule mswada alioiba.
- **Kinaya**
- Nasaba Bora kulalamika nduguye Majisifu kuwa anautukanisha ukoo wao mtukufu- nyani haoni kudule
- Nyumbani kwa Imani kunaitwa 'Baraka' lakini tunaona akiandamwa na mikasa kama vile kufiwa na mamake, nyumba yao kuchomwa na shamba lao kuchukuliwa.
- Imani anajawa na tabasamu usoni daima ilhali moyoni anafundo la uchungu
- Ni kinaya kwamba dini zinahubiri amani undugu na rehema lakini maovu mengi hutendwa na wao kama vile kupigana
- Dj alihurumia lile jibwa Jimmy kwa kufungwa minyororo lingali gonjwa, linaishia kumshambulia baadaye
- Majisifu Nasaba Bora wamelelewa katika maadili ya kidini lakini wanaishia kutosikilizana
- Mwalimu majisifu anajibu maswali kinyume nay ale yaliyoandikiwa katika kitabu alochodai kukiandika.
- Kinaya kwa mwalimu majisifu kuacha pombe halali katika jokofu na kwenda kunywa pombe haramu kwa mama N'tilie kibandani.
- Ni kinaya Mtemi Nasaba Bora kutuma askari wakachome nyumba ya akina Imani badala ya kuwahakikishiia usalama
- Dj kupita karibu na kibanda cha Amani ule wakati anapowaza juu ya lile atafanya kuhusu kitoto Uhuru- anamtuma akaite Imani ili amsaidie **Alama zozote 5x 2 = 10**

3. **a) Muktadha wa dondoo**
   i) Ni maneno ya mtemi Nasaba Bora
   ii) Kwa mwalimu Majisifu
   iii) Ni nyumbani Majisifu alikuwa amemtembelea Nasaba Bora washauriane juu ya mambo kadha wa kadha na Mtemi akachukua fursa hiyo kumshauri majisifu dhidi ya ulevi wa kupindukia

   b) Tamathali ya usemi

   Kinaya –Mtemi Nasaba Bora anajivunia utukufu wa ukoo wao ilhali anajulikana kwa maovu kama vile- kuhusika katika mauti ya Chirchir Hanadi, wizi wa mashamba ukware

   c) Migogoro baina ya ndugu hawa
   i) Majisifu alikosa kihudhuria mkutano wa Nasaba Bora sikukuu ya uhuru
   ii) Mtemi Nasaba Bora anachukia ulevi wa kupindukia wa Mwalimu Majisifu
   iii) Mtemi Nasaba Bora amezoea kumzoea na kumkosoa kila wakati mwalimu Majisifu
   iv) Majisifu hakufuhia unafiki wa nduguye wa kijifanya anamjali yeye ilhali hajali maslahi ya wanasokomoko
   v) Majisifu anataka aachiliwe kuandama sela yake ya maisha/ mitazamo yao kimaisha ni tofauti

   d) Umuhimu wa Majisifu
- Ametumiwa kuangizia maudhui ya ughushi/ wizi wa mawazo yaw engine- ameiba na kuchapisha miswada isiyo yake.
- Ni kielezo cha wsomi wanaoshindwa kuyamudu maisha yao- elimu yake haijamwezesha kuthibiti uraibu wa ppombe haramu
- Ametumiwa kubainisha taasubi ya kiume- anamwachia mkewe malezi ya watoto na shughuli zote za nyumbani
- Ni mfano wa wazazi wanaowadharirisha watoto wanyonge- anawatekeleza hata kutaka kuwaua watoto wake walemavu
- Ametumiwa kubainisha ubaguzi wa kinasaba/ kikabila- majisifu anapozembea kazi na kufutwa, bado anapewa ualimu kwa sababu anajulikana kwa viongozi- 'zimwi likujualo halikuli…'
- Mfano wa viongozi wa umma wasiowajibika kazini- muhula mzima hajaenda kazini kufunza
- Ametumiwa kubainisha unafiki- anahimiza mashoka kusoma kwa bidii ili ajiendeleze kimasomo ilhali haendi shuleni kuwafundisha
- Ametumiwa kuonyesha umuhimu wa kusameheana na kuwa na maridhiano anamsamehe ndugu yake

na kufanya juhudi ili Yusuf aondolewe lawama za mauaji pawe na maridhiano

4. **Tamthilia: Mstahiki Meya T. Arege**
   a) **Muktadha**
   i) Ni maneno ya Gedi
   ii) Akimwambia mstahiki Meya
   iii) Ni ofisini mwa meya
   iv) Meya alikuwa akipokea maji aliyokuwa ameagiza ili anywe na akahisi harufu, aliyodharau ilitokana na maji hayo, na akitaka kujua iwapo Gedi alikuwa na hakika kuwa si hayo maji yaliyotoa harufu
   b) **Mambo yaliyopelekea kuwepo kwa harufu hiyo**
   i) Wafanyikazi wamegoma
   ii) Takataka imerudikana
   iii) Kuna uhaba wa maji mjini
   c) **Umuhimu wa mzungumzaji- Gedi**

– Ametumiwa kuangazia udikteta wa Meya- anatumwa kuwaelezea waandamanaji kuwa watafutwa kazi na wengine waajiriwe.
– Ametumiwa kama kielelezo cha ukoloni- mambo leo Meya anafurahi sana anapopigiwa saluti na kuita 'sir' kila anapomuita
– Ametumiwa kuangazia ubarakala- ni miongoni mwa vibaraka wa meya ambao wako tayari kufanya lolote ili wamfurahishe meya\
– Kupitia kwake tunafahamishwa kwa nini wageni wanaotarajiwa hawazi kufika- wafanyikazi wa uwanja wa ndege pia wamegoma kuwaunga wenzao mkono
– Kupitia kwa Gedi tunafahamishwa hatima ya wageni- wangetua mji wa shwauara.
– Anaangazia ufisadi wa meya- aliajiri mhazili ambaye hakustahili hiyo ajira- pia yeye hajafika kazini
– Kupitia kwake tunafahamishwa kwamba wafanyikazi wa bahari ya mafuta pia wamegoma kuwaunga mkono wafanyikazi wa baraza
– Hali ya maji kukosa maji na mahoteli kukosa maji imeangaziwa kupitia kwake

   d) **Harufu ni ishara ya uozo:**

– Ufisadi: mfano Meya na Mwanakadarsi kupanga kuibia baraza kupitia kesi mahakamani
– Uongo: meya kudanganya dawa zimeagaziwa
– Unafiki wa kidini: meya kujificha katika dini ili kuficha uovu wake, mhubiri kumuunga mkono badala ya kuukashifu uovu wake.
– Ubainifu wa mali ya umma: meya kujistarehesha na marafiki katika mahoteli, anapanga kutumia mabilioni kuwafurahisha wageni.
– Ubinafsi- meya kuwapeleka watoto wake kusomea ng'ambo badala ya kuboresha sekta ya elimu na ya afya
– Utabaka- meya na madiwani kuishi maisha ya kifahari huku wafanyikazi wakitopea katika lindi la umaskini uliokithiri
– Matumizi mabaya ya Askari- wanatumwa kuwakomesha na kuwatawanya wanapoandamana na kulalamika
– Wizi wa mali ya umma- meya ananyakua viwanja vya umma
– Kutowajibikia kwa viongozi kutunza mazingira hadi cheneo na njaa na ukame.

5. **UKOLONI- MAMBO LEO**

– Maelezo ya ukoloni mambo leo, ukoloni unajitokeza baada ya nchi kujinyakulia uhuru na wenyeji wenyewe
– Utegemezi- bado mji wa cheneo unategemea mataifa ya nje kufadhili mipango ya maendeleo katika nchi yao- mameya wanaotarajiwa kuzuru cheneo
– Utawala wa meya unatumia mamilioni ya pesa kuwaandalia mameya kutoka ng'ambo katika mahoteli ya kifahari ingawa wana nakisi katika bajeti.
– Utawala wa meya unaagiza vinywaji na vyakula kutoka nje na dawa pia zimeagizwa kutoka nje.
– Utawala wa meya unapuuza mipango ya maendeleo ya miaka kumi ya mji wao huku ukujidai kufuata na kudhamini malengo ya maendeleo ya milema.
– Meya kuppeleka bibi kujifungulia ng'ambo na watoto wake kusomea huko ili wapate uraia wa huko kwa imani kuwa huko ni kuzuri zaidi ya kwao.
– Ubinafsi wa meya wa kunywa maji ya chupa peke yake si uafrika una asili katika uzungu
– Viongozi kuendeleza utabaka/ kujitenga na raia wa kawaida

- Nyumbani kwa mmeya kumepambwa na samani makochi na zulia la kupendeza
- Meya kupenda kutumia lugha ya kizungu mfano 'bllody hen, nonsense"

b) Unafiki katika tamthilia ya mstahiki Meya

- Maelezo ya unafiki- kujifanya au kujisingizia uadilifu/ wema/ uongofu ilhali uhalisi wako kinyume kabisa kwa mawazo na vitendo.
- Viongozi kuwahadaa wananchi kuwa baraza la cheneo ndilo lenye uthabiti mkubwa likilinganishwa nay ale mengine yaliyolinzuka ilhali limekumbwa na mizozo ya wafanyikazi
- Mhubiri kujifanya mcha Mungu na kudai kuwa ana wito wa kuhubiri
- Bili kumshawishi meya kukubali kukutana na viongozi wa wafanyikazi lakini awafanye waonekane kama ndio hawataki suluhisho
- Meya kujifanya kujali maslahi ya walinda usalama, madiwani na kuwaongezea mishahara, kuwaondolea kodi ilhali nia yake ni kuahonga ili wamuunge mkono.
- Meya anawakanya askari dhidi ya kuwaua na kuwaumiza waandamanaji kwani huu ni mwaka wa uchaguzi
- Meya kudai kuwa cheneo ni kisiwa cha kupigiwa mfano- ilhali watu wanakufa njaa, hawawezi kuyamudu mahitaji ya kimsingi
- Meya kuwaandalia madiwani kifahari ilhali wana nakisi katika bajeti na wanatarajiiaili kuendeleza mipango yao

6. Fasihi simulizi

a) Kuigiza ni hali ya kuiga matendo, tabiia za watu/ viumbe
Sanaa ya mazungumzo yanayoambatana na matendo.

b) Vipera vya maigizo

- Michezo ya jukwaani
- Michezo ya watoto
- Vichekesho
- Miviga
- Majigambo
- Ngonjera
- Matambiko
- Ngoma
- Ngomezi

c) Sifa za muigizaji bora

- Jasiri/ mkakamavu
- Mbunifu- anatumia mbinu mbalimbali ili kuvutia
- Mwenye ujuzi wa kutumia ishara za uso, miondoko inayoana na hali anazoiga
- Mwenye uwezo wa kubadili toni na kiimbo kubainisha hali tofauti za matukio
- Mwenye ukwasi na ufasaha wa lugha
- Aweze kuwashirikisha hadhira yake vyema mwenye ufahamu na utamaduni wa hadhira yake ili asije kuiudhi kwa maneno au ishara
- Mfaraguzi- aweze kubadilisha uigizaji wake papo hapo kutegemea hadhira yake.
- Anayeilemea hadhira yake vyema mwenye ufahamu na utamaduni wa hadhira yake ili asije kuiudhi kwa maneno au ishara

d) Vikwazo vya maigizo

- Kukosa mahali pa kuigizia
- Kukosa wakati wa kuigiza
- Uhaba wa maleba yanayofaa
- Kukosa uewzo wa waledi wa lugha
- Kukosa kuelewa ujumbe unaowakilishwa

7. Ushairi

a) Shabaha ya mtunzi wa shairi hili kuwatetea wanyonge wanaoghulumiwa na wenye nguvu japokuwa ndio
wazalishaji/ kupinga vita unyanyasaji wanaofanyiwa wanyonge

b) Aina za bahari katika shairi hili

i) Msuko- mshororo wa mwisho ni mfupi/ mizani chache

ii) Tarbia/ unne- kila ubeti una mishorooro mine
iii) Ukara- vina vya ukwapi vinabadilikabadilika lakini vya mwisho ni sawa 'yo'
iv) Sakarani- shairi limechanganya bahari kadha pamoja
v) Ukawafi- mishororo ya kwanza mitatu imegawa vipande viatu/ ina vina vitatu

c) Mbinu zilizotumiwa kutimiza mahitaji ya kiarudhi katika shairi

i) Inkisari/ ufupishaji wa maneno
Tavumiliaje badala ya nitavumiliaje
Kwacho badala ya kwa hicho
Vumiliyo badala ya kuvumiliana
Kwayo badala ya kwa hayo
Wanotulimiya badala ya wanaotulimia
Ndo badala ya ndio
Wanaumiya badala ya waoumia

ii) Mazida/ kurefusha maneno
Wawapo badala ya wapo
Nalije badala ya lije

iii) Tabdila/ kubadili sauti za maneno- wanotulimiya badala ya wanaotulimia
Mamiya badala ya mamia
Angamiyo badala ya angamio
Tuling'owe badala ya tuling'oe

iv) Kuboronga/ kufinyanga sarufi
'wanyonge yawakutayo badala ya yanayowakuta wanyonge

v) Kwayo sina zuiliko badala ya sina la kinizuia
Hawa sioni wengine badala ya sioni wengine ila hawa

d) Ujumbe katika ubeti wa kwanza
i) Hatavumilia kuendelea kuona wanyonge wakidhulumiwa
ii) Ameamua kutangaza katika maandishi kwa vyovyote vile

e) Sura ya shairi

i) Lina beti tano
ii) Lina mishororo mine kila ubeti
iii) Mshororo wa mwisho umefupishwa
iv) Mishororo ya kwanz mitatu ina migao mitatu/ vina vitatu
v) Mizani za mishororo ya kwanza mitatu ni 2, 6, 8= 8

f) Mambo yanayomkera mshairi

i) Wanyonge waghulumiwa
ii) Wazalishaji ndio hunyanyaswa
iii) Wanyonge ndio hukumbwa na maafa
iv) Wanyonge ndio huwapa mamlaka/ nguvu viongozi
v) Wenye nguvu wametawaliwa na tama/ ubinafsi/ uchoyo

g) Maana ya

i) Zuiliko- kizuizi/ pingamizi/ kikwazo/ kisiki
ii) Mauko- madhila/ maangamizi/ shida/ madharau

GEM SUB-COUNTY
CHETI CHA KUHITIMU KISOMO CHA SEKONDARI
102/1
KISWAHILI
KARATASI YA 1

1. Unataka kuwania Ugavana. Andika tawasifu watakayoisoma wapigakura ili wavutiwe kukuchagua.
2. Tatizo la usalama nchini Kenya ni janga la kujitakia Jadili.
3. Uzuri wa mkakasi ndani kipande cha mti.
4. Andika kisa kitakachoishia maneno haya : ...nilitambua kwamba si vizuri kumtegemea mtu mmoja kwa hali na mali.

GEM SUB-COUNTY
CHETI CHA KUHITIMU KISOMO CHA SEKONDARI
102/2
KISWAHILI
KARATASI YA 2

UFAHAMU.

Binadamu kwa wakati huu amemaka kwa sababu amechafua mazingira yake pasipo tahadhari. Mathalani insi amejaza gesi za sumu zitokazo viwandani nahata kuchafua mito kutokana na maji machafu kutoka katika viwanda hivyo. Takataka zinazotupwa ovyo ovyobila simile. Matokeo ya haya yote ni kwa mfano , tunapata mvua ya aside ambayo huhasiri mimea. Aidha ukanda wa ozoni unaotukinga dhidi ya miale hatari kutoka kwa jua tayari umeharibiwa na hivyo kuongeza joto duniani. Sehemu nyingi zimeanza kugeuka na kuwa jangwa huku sehemu zingine zikifurika kwa maji ya mito na mvua. Maji haya yameanza kumezavisiwa vingi vilivyo baharini. Kutokana na madhara haya,binadamu sasa anatapatapa ili kutafuta makao kwingine kwenye salama. Ndiposa siku hizi nadhari za binadamu zimeelekezwa katika mawanda mengine nje kabisa ya kisayari hiki kidogo kiitwacho Dunia.

Kwa miaka mingi sasa, binadamu amekuwa akitafakari kuhusu uwezekana wa kuishi sayari nyingine. Hii ndiyo sababu mwaka mwaka wa 1969 walimkanyagisha binadamu wa kwa kwanza kabisa mwezini. Lengo lilikuwa kutalii na kuchunguza uwezekano wa binadamu kuishi huko na wale watakaoweza wahamie huko. Kwa bahati mbaya, iligunduliwa kwamba mwezini hakuna kilicho hai huko, hata mimea. Mwezini ni vumbi tupu isiyootesha chochote. Kipatikanacho kwa wingi sana ni madini tu, ambayohayawezi kumfaidi binadamu kwa lolote.

Sayari nyingine alizozitalii binadamu ni zuhura, Mirihi, Mushtarii na tuseme karibu sayari zote zinazolizunguka jua. Kilichogunduliwa ni kuwa upo uwezekano wa sayari kama Zuhura na pengine Mirihi kuwa na mvua Lakini nyingi mno isiyoweza kuruhusu mimea kukua. Nayo, Zuhura inasemekana kuwa joto sana wakati wa mchana bali mirihi ni baridi sana siku zote;baridi kiasi cha kuwa binadamu na wanyama hawawezi kuishi huko. Mushtarii yasemekana kuwa joto ajabu, ambapo hizo sayari nyingine zina joto sana au zina baridi sana. Habari hii imefunga binadamu katika jela la kijisayari chake kiki hiki kiitwacho Dunia anachokichafua kila uchao.

Je, binadamu amekata tama? La hasha! Ndiyo mwanzo na anajaribu sana kuzikata pingu alizofungwana maumbile. Vipi? Amejaribu kuchunguza uwezekano wa kuihama ardhi na kuishi baharini kwa sababu bahari inazidi ardhi mara tatu kwa ukubwa. Ni vipi ambavyo binadamu anavyodhani anaweza kuishi baharani mahali ambapo hakuumbwa aishi humo kama samaki? Jawabu ni kuwa angefanya hivyo kwa kutumia maarifa yake.

Binadamu anaamini kabisa kuwa ana uwezo wa kujenga miji mikubwa humo humo baharini...mikubwa zaidi ya hii tuliyo nayo ardhini.Anaamini kuwa anaweza kuitawala bahari kiasialichoitawala ardhi, na hivyo basi kufanya bahari impe makao na kumlisha maumbile yake kwa kujiundia mashavu kwa mfano, ili avute pumzi ndani ya maji.

Njia ya pili ya kuepukana na pingu za maumbile ni kuishi angani. Hii ina maana ya kujenga miji iliyoelea angani, kama madungu vile. Na kwa vile anga haina kikomo, binadamu atakuwa amejipatia nafasi kubwa ya kuishi bila kujali ongezeko la idadi yake mwenyewe. Yaani atakuwa anajiundia visayari vyake visivyo idadi angani!

Njia ya tatu ni kubadilisha umbo lake ili asihasirike na joto wala baridi. Binadamu wa kisasa anaamini kuwa inawezekana kumuunda upya mtu katika maabara badala ya kufanya hivyo katika mimba. Mtu huyo wa maabara aitwaye *cyborg* kwa lugha ya kiingereza anaweza kuwa na chuma ndani badala ya mifupa na mwili wa kawaida wa udongo na maji nje.

Kiunde huyu atakuwa hadhariki ovyo ovyo kama binadamu wa sasa aliyeumbwa kwa chumvi, maji na protini. Ama kwa njia bora zaidi, binadamu mpya wa maabarani aundwe kwa zebaki. Binadamu huyu wa zebaki hafi wala hakatiikatiki na iwapo atakatika vipande vipande basi kama zebaki, vipande hivyo vitaundika tena upya na kumrudishia umbo lake kamili la awali.

Njia nyingi za kuepukana nauangamizi ni kutumia viunde vyake vya elektroniki kama vile tarakilishi yaani kompyuta na mitambo mengine kama hiyo. Binadamu anaamini kwamba uwezo wa vyombo hivi utakapokamilishwa, basi vitamsaidia kwa lolote lile.

MASWALI

a) Kwani kutumia mifano miwili,eleza vile ambavyo binadamu amechafua mazingira yake.
(alama 2)
b) Ongezeko la joto duniani limeleta hali mbili kinzani za kimazingira, zitaje hali hizo.
(alama 2)
c) Eleza sababu mbili zinazomfanya binadamu kuhangaika na kutafuta makao kwingineko.
(alama 2)
d) Taja mambo mawili yanayomfunga binadamu katika ardhi.
(alama 2)
e) Taja na ufafanue sababu tatu ambazo unadhani huyafanya madini yaliyoko mwezini yasiletwe hapa duniani.
(alama 3)
f) Eleza mambo mawili ambayo binadamu anajaribu kukwepa kulingana na aya mbili za mwisho.
(alama 2)
g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu.
(alama 2)
i mashavu
ii asihasirike

2. UFUPISHO (Alama 15)

Soma makala yafuatayo kisha jibu maswali yanayofuata.

Kuteswa waandishi wa habari bahari na kuwekewa vikwazo katika kazi zao ni jambo ambalo si geni.Mara kwa mara visa vinaripotiwa vya wandishi kudhulumiwa na hata kuuwawa. Visa hivi vikiripotiwa ni nadra kuwaona Wahusika wakichukuliwa hatua za kisheria. Aghalabu ripoti zenyewe zinaishia kupuuzwa katika kapu la sahau.

Riwaya Dharau ya Ini,inamulika suala hili kina cha kikatiwa kauli. Hadithi tunakutana na waandishi wa habari ya maisha katika jamii yenye kani nyingi. Kazi ya waandishi hawa inaingiliana pakubwa na ya mwenyekiti Munene na mwenzake Waziri kisongo.

Lila na Derby ambao wanaandika gazeti la 'Mpapure' wanaendelea kufanya kazi yao kwa ujasiri mkubwa.Inafika wakati wanafichua kashfa ya kijiji cha Madongoporomoka . Kufichuliwa kwa kisa hiki hakuwapi waandishi hawa nafasi ya kuendeleza utafiti wao. Mhariri mkuu wa gazeti la 'Mpapure' BW.Silverstein Makhanu anawakataza kwa madai kwamba kina Lila ni wanawake na hawataweza kuendelea na utafiti huo. Kauli hii inamkarisha sana mwandishi Derby. Baadaye, hadithi, waandishi hao wanashtumiwa kwa kueneza uvumi na kuteswa.

Dharau ya Ini ni riwaya ya kifalfasa.Ni hadithi ambayo imeandikwa kwa lugha ya kuvutia. Ni kisa ambacho kimeshehen ucheshi mwingi. Ni riwaya ya kwanza katika fasihi ya Kiswahili kutumia msimulizi ya nafsi ya kwanza , ya pili na ya tatu kwa pamoja.

Pia, imeunganishwa tanzu zote za fasihi (tamthilia, ushairi, hadithi fupi na hata fasihi simulizi). Lakini msemaji wa kawaida huenda atatizwe na usimulizi ambao unasitasita kila baada ya dakika chache. Hata hivyo Dharau ya Ini ni mchango mkubwa katika fasihi ya Kiswahili.

a) Bila kupoteza maana, fupisha aya mbili za kwanza (maneno 55-60)
b) Fafanua jinsi waandishi Lila na Derby wanavyoteswa na sababu ya kuteswa.(maneno 30-35)

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

(a) i) Eleza maana ya kiambishi. (alama 2)
ii) Tambuishi uamilifu wa viambishi katika neno 'kitakachotolewa' (alama 3)

(b) Toa mifano miwili ya sauti zifuatazo :
i. Sauti ghuna ambazo ni vipasuo. (alama 2)
ii. Sauti hafifu ambazo ni vikwamizo.

(c) Eleza matumizi ya 'kuwa' katika sentensi hizi. (alama 2)
i. Alikuwa mgonjwa.
ii. Alikuwa akifua.

(d) Tumia kihusishi cha wakati kisahihi katika sentensi. (alama 1)

(e) Taja uamilifu wa maneno yaliyopigiwa mistari. (alama 3)
i. Majisifu ameenda wangwani
ii. Hapa ni pangu
iii. Haraka yako itakuponza

(f) Andika udogo hali ya wingi.
Mvulana mkorofi alimkata mbuzi sikio kwa kisu kikali. (alama 2)

(g) Fuata maagizo
i. Mgonjwa amepewa dawa asubuhi. (alama 4)
(kauli ya kutendesheka mazoea)
ii. Poa (nafsi ya kwanza wingi, wakati ujao kauli ya kutendeshana)

(h) i) Eleza maana ya kishazi huru. (alama 1)
ii. Toa mfano wa kishazi huru. (alama 2)

(i) Tumia neno 'teka' katika sentensi ili kutoa maana tatu tofauti. (alama 3)

(j) Changanua sentensi ifuatayo kwa jedwali. (alama 5)
Magadi walichoma kanisa ni maadui wakubwa sana.

(k) Andika katika usemi wa taarifa. (alama 3)
"Nitajificha mumu na shehe hatanipata leo, kesho hata mwaka ujao," Kijuba alisema.

(l) Andika visawe vya maneno yaliyopigiwa mistari. (alama 3)
Lupita ndiye alitakadamu upepelezi wa shamba hili.

(m) Tumia maneno yafuatayo kutunga sentensi moja sahihi. (alama 3)

(n) Andika maneno yafuatayo kutunga sentensi moja sahihi. (alama 3)
Mtoto wa sungura ameuawa.

4. ISIMU JAMII(Alama 10)

…mfanyikazi mmoja wa nyumbani amefikishwa mahakamani katika kaunti ya Maganyakulo kujibu tuhuma za kumbaka kikongwe. Mwendesha mashtaka wa polisi bwana Maliza Twende alisema. Mikaka na Makarne alifumaniwa na mshtakiwa alipelekwa rumande hadi septemba 21 mwaka huu ambapo kesi hiyo itatajwa tena. Licha ya hayo, wengi wanadokeza kuwa Huenda adhabu ya kosa hilo ikuwa ni kifo au kifungu cha maisha.

Mshtakiwa aliomba apewe dhamana na Serikali ili aachiliwe huru. Hatimaye ombi hilo halikukubaliwa kwa kuwa mfanyikazi huyo hakuwa na mdhamini. Muhimu ni kuwa baada ya kesi hiyo kuamuliwa, mshtakiwa anaweza kukata rufaa katika mahakama kuu. Naye mlalamishi ameomba Serikali impe ulinzi kutokana na kuvamiwa na washirika wa mshtakiwa…

Maswali

(a) Tambua sajili hii (alama 1)
(b) Taja sifa nne za sajili hii. (alama 4)
(c) Katika kifungu hiki kuna baadhi ya misamiati ambayo imetumika na aghalabu hupatikana katika sajili nyingine tofauti na ile ya husika
i. Taja sajili hiyo nyingine

(alama 1)

ii. Taja angalau misamiati minne iliyoko katika kifungu hiki na sajili uliyotambua katika c(i) (alama 4)

GEM SUB COUNTY
KISWAHILI PAPER 3
SEHEMU YA A: TAMTHILIA
Mstahiki Meya: T.Arege

1. **Lazima**
   Kutowajibika kwa viongozi barani kumesitishapakubwa maendeleo. Dhihirisha.
   (Alama 20)

SEHEMU YA B :B RIWAYA
Kidagaa Kimemwozea : Ken Walibora
Jibu swali la 2 au la 3

2. " ……Unaa … seema mimi sipakui? Wataka mimi nipike?
   a) Eleza muktadha wa dondoo hii.
   (alama 4)
   b) Kwa kutoa mifano mitatu. Eleza nafasi ya msemmewa na jinsia yake katika riwaya.
   (alama 6)
   c) Eleza umuhimu wa msemaji kwa mujibu wa riwaya nzima. (alama 10)
3. Eleza visababishi vya mafarakano katika ndoa kwa mujibu wa riwata "Kidagaa Kimemwozea".
   (alama 10)

SEHEMU YA C : HADITHI FUPI
Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine
Jibu swali la 4 au la 5

4. "Hapa huingii bila kuninyoshea mkono……."
a) Eleza muktadha wa dondoo hii (alama 4)
b) Eleza sifa nne za mzungumziwa. (alama 4)
c) Kwa kurejerea muktadha wa hadithi nzima thibitisha ukweli kuwa mkono mtupu haulabwi.(alama12)
5. Haki za watoto zimekiukwa pakubwa katika Diwani ya Damu Nyeusi. Dhihirisha kwa kurejerea.
   (alama 20)

i) Kanda lausufi
ii) Maskini Babu yangu
iii) Mwana wa Darubini
iv) Mizizi na matawi

SEHEMU YA D : USHAIRI
Jibu swali la 6 au la 7

6. Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali.
   Ewe hisia!
   Umeniamshia ndoto niloisahau zamani
   Nyimbo ya kale
   Na mdundo usonivutia
   Ila hayawani na mwangu rohoni

   Tulia sasa tulia
   Hebu tulia ewe hisia ulo mtimani
   Nataka katu kusisimka
   Kwa sauti yako laini
   Kwani njia zetu ni panda
   Daima hasirani

   Umesubutu vipi kuniita
   Kutoka mwako ngomeni
   Ulimosahauliwa tangu zamani
   Basi yawache maombolezi yako yaso maoni
   Yawateke hao mashujaa wa kale
   Wafu walo kaburini

   Hebu tulia, usiniingilie
   Usinihangaishe!
   Kukuandama katu haimkini

Kwani hata sasa…. Kwa kukuwaza tu dakika lini
Naona majuto yam bali moyoni
Kama kwamba nimengawa wangu wakati
Na wazimu, majinuni
Basi nenda zako hisia…. Shuu…. hebu tokomea!

Maswali

i) Lipe shairi hili anwani mwafaka. (Alama 1)
ii) Kwa nini Utungo huu ni shairi? (alama 4)
iii) Kwa nini mshairi hataki kukumbushwa yaliyopita? (alama 2)
iv) Andika ubeti wa pili kwa lugha nathari. (alama 4)
v) Taja na ueleze Mbinu mbili za lugha zilizotumiwa katika Utungo huu. (Alama 4)
vi) Fafanua umuhimu wa uhuru wa msahairi uliotumiwa. (alama 2)
vii) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika ushauri. (alama 2)
a)amesubutu
b)majinuni

7. **Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali**

1. Punda kalibebe gari gari limebeba punda
Mwalimu ana pakari muashi vyuma adunda
Jaji ginga msumari sonara osha vidonda
Kinyume mbele

2. Saramala ahubiri muhunzi tiba apenda
Mganga anaabiri bahari anakwenda
Hata fundi wa magari anatomea vibanda
Kinyume mbele

3. Wakali anahiyari biashara kuitenda
Mtazame asikari akazakiaza vitanda
Mkulima mashuhuri jembe limeshamshinda
Kinyume mbele

4. Apakasa daktari ukili anaupinda
Saveya kawa jabari mawe anafundafunda
Hazina wa utajiri mali yote aiponda
Kinyume mbele

5. Msemi huwa hasemi wa inda hafanya inda
Fahali hawasimami wanene walishakonda
Walijitia utemi yamewavunda
Kinyume mbele

6. Kiwapi cha kukadiri twavuna shinda kwa shinda
Tele haitakadari huvia tulivyopanda
Mipango imehajiri la kunyooka hupinda
Kinyume mbele

Maswali

a) Lipe shairi hili kichwa kifaacho. (Alama 1)
b) Fafanua jinsi idhini ya kishairi inayodhihirika katika shairi hili. (alama 4)
c) Mtunzi ametilia shaka masuala kadhaa. Yataje. (alama 5)
d) Andika ubeti wa tatau katika ligha ya kiriwaya. (alama 4)
e) Taja na ueleze mkondo wa shairi hili. (alama 4)
f) Eleza msamiati huu kama ulivyotumika katika shairi : (alama 2)
a) Anapakasa
b) Pakari

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

8. **Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Salimu alikumbana na mwanadada aliyejisikia sukari! Wacha aringiwe ile mbaya ! Alishindwa vya Kuwaelezea marafikize waliomsubiri pembeni akaamua Kuingia mtini.

a) Tambulisha kipera hiki kwa mujibu wa sehemu zilizo pigiwa mstari. (Alama 2)
b) Ni nini maana yake ? (a) hapo juu (alama 2)
c) Eleza sifa zozote nne (4) za kipera hiki. (alama 8)
d) Eleza majukumu yoyote manne (4) ya kipera hiki katika jamii. (alama 8)

GEM SUB-COUNTY
CHETI CHA KUHITIMU KISOMO CHA SEKONDARI
102/1
KISWAHILI
KARATASI YA 1

1. **TAWASIFU YA KUWANIA UGAVANA**

Mtindo

a) Tawasifu- mtu binafsi anajielezea kwa nathari/ mfululizo
b) Maelezo yawe katika nafsi ya kwanza- umoja
1) Mada – TAWASIFU YANGU
2) Utangulizi:
- kujitambulisha
- jina
- mwaka wa kuzaliwa
- mahali pa kuzaliwa
- wazazi
- nafasi katika mzao/ familia
- familia yenu kimuhtasari

3) Mwili
a) **Masomo**
- chekechea
- msingi
- sekondari
- chuo

b) **Kazi/ ujuzi**
Mahali na muda
c) **Mchango wako**
Katika jamii
Katika vyama na shule
Uwezo wako kimaendeleo
d) **Uanachama**
Vyama mbalimbali na nafasi yako (vyeo)
e) **Uraibu**
Shughuli mbalimbali za ziada unazoshiriki
Shughuli unazopenda nje ya kazi yako rasmi
f) **Hitimisho**
Kuwaomba/ kuwahimiza wampigie kura

Tanbihi

i) Shughuli ulizojihusisha nazo katika taasisi za elimu na katika jamii zihusiane na zituelekezee kwenye msukumo wa kutaka ugavana kama vile:
- vyeo/ nyadhifa za uongozi masomoni
- juhudi za maendeleo katika jamii
- juhudi za kusaidia wanajamii
- juhudi za kutetea haki za wanajamii
- utawafanyia nini

- Watarajie nini kutokka kwako
- Eleza uwezo wako

SWALI LA PILI: USALAMA NCHINI

MTINDO

i) Insha ya mjadala
ii) Mtahiniwa atoe hoja za pande mbili
iii) Mtahiniwa ahitimishe kwa msimamo wake. Asimame upande wenye hoja nyingi au katikati iwapo hoja zitatoshana kiidadi

Maudhui

a) **Kuunga mkono**
i) Utepetevu wa walinda- usalama
ii) Ufisa wa Kenya kuingia Somali na al-shaabab
iii) Kutosomesha watoto
iv) Raia kutowajibika kuwafichua wahalifu
v) Mihadarati
vi) Tama
vii) Malipo duni kwa walinda usalama
viii) Umaskini
ix) ukabila

b) kupinga

i) uchache wa walinda
ii) ni tatizo la kimataifa- makundi ya kigaidi
iii) ni tatizo la kimaumbile kama vile mafuriko, radi,maporomoko ya ardhi
iv) umaskini
v) n.k

SWALI LA TATU

Uzuri wa mkakasi ndani kipande cha mti

Insha ya methali

Maana

Tusihadaiwe na uzuri wan je kutokana na mapambo ya kitu au mtu bali ni mihimu kuchunguza undani wake kwa makini ili tubainishe uzuri wake

Mtindo

a) andika kinathari
b) kisa kiunge mkono baada na matumizi ya methali
c) kisa kikuze pande zote mbili kikamilifu
d) si lazima aeleze maana na matumizi ya methali

mielekeo

i) kufurahia uzuri wan je wa mtu au kitu baadaye kugundua ubovu au kasoro zilizofichika
ii) mtu aliyewahadaa watu kwa matendo mazuri hadharini (mbele ya watu) badaye akagunduliwa kuwa mtenda maovu kisirisiri
iii) kiongozi wa kidini au mahali popote aliyehubiri maji na kunywa divai
iv) msichana mrembo sana ambaye alimvutia mwanamume aliyemuoa kumbe akagundua kasoro kubwa kwake baadaye
v) na kadhalika

SWALI LA NNE: MDOKEZO

MTINDO

a) mdokezo wa kumalizia kwa maneno ya mwisho uliyopewa
b) lazima maneno ya mwisho yawe yayo hayo
c) maudhui yahusu
   i) mtahini aliyetegemea mtu mmoja kwa kila mahitaji yake na mtu huyo alipoondoka akawa hajiwezi tena
   ii) mtahini aweze kuwa alishuhudia mume aliyeoa wake wengi akifa halafu wake na watoto wake kuzozana au
   kukosa mahitaji yao/ kuwa katika hali duni
   iii) mtahini kushuhudia raia waliomtegemea kiongozi au tajiri Fulani mmoja kwa mahitaji yao yote kasha

wakaishia ukosefu/ uhitaji mkuu kiongozi huyo alipoondoka.

GEM SUB-COUNTY
CHETI CHA KUHITIMU KISOMO CHA SEKONDARI
102/2
KISWAHILI
KARATASI YA 2

1.
a) Gesi za sumu kutoka viwandani
Maji machafu kutoka viwandani
b) Jangwa
maturiko
c) Madhara yanayosababishwa na jangwa
ongezeko la watu duniani
mazingira machafu
mafuriko
d) Mwezini hakukaliki kwa sababu hakuna hewa
sayari nyingine zina ama joto, baridi au mvua nyingi
maumbile yake hayamwezeshi kukaa kwingine ila tu duniani
e) Gharama y kuchimb n kusfikish madini hayo ni ghali sana
Binadamu anafikiria madini hayo huenda yakawa na sumu
Hakuna uwezakano wa kuyachimba kwa sababu ya ukosefu wa hewa mwezini
f) Anakwepa kifo/ mauti au maangamizi
Anakwepa madhara ya mazingira kama vile joto, baridi na mvua
Anakwepa pingu za maumbile yake kama yalivyo sasa
g) i) mashavu- kifaa cha kuvutia hewa, mapafu, mabuhumu, mayavuyavu, mapumu
ii) Asihasirike- asidhurike, asiharibiwe, asiteseke, asiangamizwe, asiathirike

2. UFUPISHO

a)
i) Kuteswa kwa waandishi wa habari
ii) Kuwekewa vikwanzo katika kazi zao
iii) Visa vya waandishi kudhulumiwa na kuuwawa
iv) Wahusika hawachukuliwi hatua za kisheria
v) Ripoti zinaishia kuupuzwa
vi) Kuna waandishi wa habari ya maisha katika jamii
vii) Kazi yao inaingiliana nay a mwenyekiti munene na mwenzake waziri kisongo

b)
i) Wananyimwa nafasi ya kuendeleza utafiti wao kwa sababu wanafichua kashfa ya kijiji cha madongoporomoko
ii) Wanabaguliwa kijinsia kuwa wao ni wanawake
iii) Waandishi hawa wanashutumiwa kwa kueneza uvumi ka kuteswa
iv) Waliohusika katika kisa cha kuwatesa hachukuliwi hatua

3. MATUMIZI YA LUGHA

a) i) kiambishi ni sehemu ya neno iliyo na maana kisarufi au ni kipashio cha lugha kinachoongezwa kwenye mzizi
ii) ki- kiwakilishi cha ngeli
ta- wakati
ka- hali
cho- kirejeshi “O”
to- mzizi
lew- kauli
a- kiishio
b) i) /b/ /d/ /g/
ii) /f/ /th/ /s/ /sh/ /l/
c) i) hali/ kitenzi kishirikishi
ii) wakati/ kitenzi kisaidizi
d) hadi/ tangu/ halafu/ kasha/ baadaye
e) i) E
ii) W

iii) N

f) vivulana vikorofi vilivikata vibuzi visikio kwa vivisu vikali AMA vijivulana vikorofi vilivikata vijibuzi/ vibuzi vijisikio/ visikio kwa vijijisu vikali

g) i) mgonjwa amepesheka dawa asubuhi
ii) tutapozana

h) i) kishazi huru ni sehemu ya sentensi inayoweza kujisimamia kimaana au ni sentensi iliyokamilika kimaana
ii) mama anatembea (kadiria)
- mgeni aliyewasili jana <u>ameondoka leo asubuhi</u>- kishazi huru

i) <u>teka-</u>
chota maji/ chota
chukua kitu kwa mguu
sebule ndog

S					
KN ½		KT ½			
N ½	S ½	T ½	KN ½		
			N ½	V ½	E ½
Mafundi	Waliochoma kanisa	ni	maadui	wakubwa	sana

AU

S					
KN ½		KT ½			
N ½	S ½	t ½	N ½	V ½	E ½
Mafundi	Waliochoma kanisa	ni	maadui	wakubwa	sana

k) Kijuba alisema kuwa / kwamba angejificha <u>mumo humo</u> na shehe hangempata/ asingempata siku hiyo, siku ambayo ingefuata hata mwaka ambao ungefuata

l) –anza/ tangulia/ sabiki
-udadisi/ uchanguzi/ ufanisi
-konde/ mgunda

m) Kibofu cha Yule kipofu ni kibovu ndiposa haendi haja ndogo

n) Kitungule ameuawa

ISIMU JAMII

a) Matangazo/ redio/ habari/ ripoti/ gazeti

b) Sifa za sajili hii

– Huwa na lugha nyepesi
– Sentensi aghalabu huwa ndefu ndefu
– Hufuata kanuni za usarufi wa lugha
– Huhusisha maelezo ya kina ili kuweka wazi yaliyojiri
– Mara nyingi hutumia wakati uliopita
– Wakati mwingine huhusisha wadhamini

c) **I)** sajili ya kortini/ mahakama/ kesi
ii)

– tuhuma
– mashtaka
– hakimu

- kiapo
- sheria
- kifungo
- mahakama
- dhamana
- rufaa
- mdhamini

GEM SUB-COUNTY
CHETI CHA KUHITIMU KISOMO CHA SEKONDARI
102/3
KISWAHILI
KARATASI YA 3

1.

- Meya na baraza lake linashindwa kuwalipa wafanyikazi/ kuwalipa nusu nusu/ kuwalipa mshahara duni. wanasusia kazi kwa kugoma na kuandamana. Shughuli na maendeleo ya baraza tanatatizika.
- Meya anakosa kuagiza dawa zahanatini. Matibabu yanakuwa duni, wagonjwa wanakufa kwa mfano mpwaye waridi, wahudumu wanajiuzulu, madiwani wanabidika kuwapeleka wapendwa wao ng'ambo kwa gharama ya juu
- Sekta ya elimu inapuuziliwa; huduma inakuwa duni; meya anawapeleka wanawe ng'ambo gharama ya juu.
- Meya na washauri wake wanaendeleza wizi wa mali ya umma mf fimbo na ardhi. Kunakosea usawa katika ugavi wa raslimali. Uzalishaji ukatatizwa na umaskini ukashamiri.
- Baraza la meya linaajiri kinasaba na kimapendeleo. Taaluma inavurugwa, uwajibikaji kikazi unatatizwa.
- Meya anawategemea washauri potovu mfano Bili wao wanalinyonya baraza zaidi, dhiki zikaongezeka barazani.
- Meya na madiwani wake wanaendeleza dhulumu kwa wanyonge. Kwa mfano Diwani wa kwanza na Askari kwa wafanyikazi. Vifo vinatokea waliotegemewa kizazi wanakosekana.
- Meya anakosa kumlipa mfanyikazi wake hivi anamwongezea dhiki hata akamlisha mwanawe chakula kilicholala
- Mhubiri anakosa kuwajibika anapolikubali pendekezo la meya la sadaka. Anaishia kusababisha hasara zaidi kwa baraza.
- Meya kwa kupenda starehe na anasa anajiburudisha kwa gharama ya baraza (ziara ya kajifahari) haya yanachangia nakisi
- Meya anazindua mfumo wa kugawiana gharama zahatinini. Wengi wanashindwa kumudu gharama ya matitabu. Vifo vingi vinatokea
- Siki anakataa kushiriki siasa. Uadilifu unakosekana uongozini. Maongozi yakawa duni zaidi.

2. KIDAGAA KIMEMWOZEA

a)

- Maneno ya Mw. Majisifu
- Alikuwa anakemea mkewe Dora
- Walikuwa nyumbani kwao
- Dora analalamika kutosaidiwa kazi za nyumbani ambazo zimeongezeka imani alipoondoka

b) **Nafasi ya wanawake kwa mujibu wa Dora**

- Walezi- anatazamiwa na mumewe kuwalea wanao bali na kutekeleza shughuli nyinginezo za nyumbani
- Wavumilivu- anavumilia ulezi wa wanaye walemavu, ulevi wa mumewe na kuachiwa shughuli zote nyumbani.
- Hawana usemi katika ndoa. Majisifu anamnyamazisha kwa kumkumbusha kwamba ni yeye aliyeolewa
- Ni wenye mapenzi ya dhati- ashikilia kuwa motto ni motto hata awe bonge la nyama
- Wa kulaumiwa katika ndoa. Dora analaumiwa kwa kuzaa watoto walemavu.

c) Umuhimu wa Mw. Majisifu

- Amekuza maudhui mathalani unafiki, uwongo, mapuuza, wizi
- Amatuchorea picha ya ndoa kama asasi yenye matatizo kadha
- Ameonyesha utepetevu wa wahudumu kwa umma
- Ametumiwa kuangazia hali inayokumba nchi change za bara afrika kuhusishwa na uchechefu wa wataalamu

3. Visababishi vya mafarakano katika ndoa

<u>Majisifu na Dora</u>

- Ulevi- kila kuchao kwenda ibadani
- Mapuuza- malezi ya wana walemavu
- Lawama- kumzalia mashata
- Utelekezaji- jukumule kwa kipindi kirefu
- Majuto- Dora anajutia kuoleka kwa majisifu

- Utepetevu- Dora amlaumu kwa kulaza damu
- Masimango/ matusi "bloody bastard……
- Udhibitii- "shut up"
- Unyanyapaa "wanawake wa siku hizi mmea pembe"

Zuhura na Nasaba Bora

- Kunyimwa uneni- kisa cha uhuru 1 na Amani
- Kupuuzwa kimawazo- pendekezo kumhusu DJ
- Uzinzi- kushirikiana na wengine kimapenzi
- Hadaa/ udanganyifu- kusuluhisha migogoro ya mashamba
- Hulka hasi/ mbaya- kuwafuta wafanyikazi- chanjo kwa mbwa
- Kutelekezwa- Zuhura awaonea gere wanawake walioshinda na waume zao na kugandiana nao kimapenzi

4. a)

i) Msemaji ni bwana mmoja aliyejiita nduguye Amali
ii) Msemewa ni msimulizi/ Abu
iii) Ni mlangoni mwa chumba alimokuwa Amali
iv) Ni wakati wa arusi ya Amali na msimulizi. Msimulizi alikuwa ameandamana na watu wake ili kwenda kumchukua bibi arusi, bwana huyu alipomzuia kuingia chumbani

b)

i) Mwenye bidii- alifanya kazi za aina mbalimbali hata mwishowe akawa tajiri
ii) Mwenye msimamo thabiti- hakukuta tama na kuacha kujitahidi kazini
iii) Mkarimu- aliwasaidia wengi, rafiki na jamaa
iv) Mwenye kisasi- alilipiza kisasi cha kumwacha Amali siku ya arusi kwa kosa alilotendewa hapo awali
v) Ni mvumilivu- alifanya biashara hadi akapata kazi ya uhamali Arabuni

c) Hii ni methali ambayo hudokeza kuwa ukitaka usaidizi Fulani ni lazima nawe uwe tayari kufanya jambo Fulani kwa atakayekusaidia **mifano**

i) Bwana aliyekuwa mlangoni alimtaka Abu 'amnyoshee mkono'. Asingemwachilia dadake kutoka hivi hivi tu bila kupokea kitu.
ii) bwana arusi alilazimika kutia mkono mfukoni na kumpa bwana huyo kitu kidogo alipokuwa ameenda kupeleka pesa kwa Amali mara ya kwanza
iii) mama zena alikataa posa ya msimulizi kwa kudai kuwa msimulizi hakuwa na uwezo wa kutoa mahari
iv) msimulizi anaporudi akiwa tajiri na kupeleka posa mara ya pili anakubaliwa
v) Mama zena anaagiza orodha ya vita pamoja na samani kutoka Arabuni
vi) Arusi ilipopangwa, Amali hakuhusisha jamaa wa msimulizi kwa kuwa walikuwa hawana kitu

5. Ukiukaji wa haki za watoto

Kanda la usufi

- Sela kufurushwa shuleni, kushauriwa kujitafutia nafasi katika shule ya kutwa
- Kadogo kukoseshwa malezi ya mamake mzazi
- Kadogo kuvalishwa matambara
- Kadogo astakimu katika kijumba cha msonge

Maskini Babu yangu

- Msimulizi ashuhudia mashambulizi dhidi ya babuye
- Watoto wa madongo kuleleka katika mazingira machafu ajabu
- Msimulizi kushirikiswa katika uhasama wa kikabila unaomuathiri hata utu uzimani
- Msimuizi afungwa katika chumba chenye giza

Mwana wa Darubini

- Kananda kukoseshwa masomo
- Kananda kuajiriwa uyaya katika umri huo mdogo
- Kananda kudhulumiwa kimapenzi na mwatela
- Mwakitawa kukoseshwa malezi ya mama mzazi
- Sami kuaga katika mkasa wa moto

Mzizi na matawi

- Bi.kudura kumtekeleza Sudi baada ya kumzae nje ya ndoa
- Bi .mkubwa kumdanganya Sudi kuhusu usuli wake hasa

6. Ushairi

a) Hisia/ kumbuka yaliyopita
b) Ni shairi kuwa
– Kuna usawa wa vina vya mwisho kwa mshororo
– Mistari mifupi
– Imegawa katika beti
– Kuna kurudiarudia maneno Fulani
c) Yaliyopita humsumbua sana moyoni/ humweka katika maombolezi
d) Tulia sasa ewe hisia ulio moyoni. Sitaki kisisimka kwa kukumbuka mazuri yaliyopita. Njia yako na yangu haiendi pamoja
e) Mbinu
Tashhisi- ameipa hisia uhai
Tashihi- majuto ya mbali moyoni kama kwamba imegawa wamgu wakati
f) Inkisari- ulo-ulio, kutosheleza idadi ya mizani
Kuboronga sarufi- kutoka mwako ngomeni- kutoka ngomeni mwako- kuleta urari vina
Tabdili- hini- hii- kutosheleza vina
g) Umesubutu- umethubutu
Majinuni- walio na hasira

7. a)
kinyume mbele
shaka ya mambo
dunia rangi rangile
b)
i) inkisari- apenda badala ya anapenda
ii) kuboronga sarufi- sonara osha vidondo
iii) tabdila- asikari badala ya askari
c)
i) punda kalibeba gari
ii) mwalimu anapakari
iii) mwashi anadunda vyuma
iv) sonara anaosha vidonda
v) jaji anagonga msumari
vi) seremala ahubiri
vii) askari akaza vitanda
viii) saveya afunda funda mawe
ix) wakli anahiyari kutenda biashara
x) fundi wa magari atomea vibanda
d) wakili anapenda kufanya biashara. Askari anaharakisha kukaza vitanda. Mkulima stadi anashindwa kulima. Mambo yanaenda kinyume
e) msuko- kibwagizo kimefupishwa
mathnawi- lina vipande viwili
f) anasuka ukili/ anatengeneza mikeka
zana za kutumiwa na makanika

8. a) Misimu
b) ni semi za muda ambazo hubuniwa na kutumiwa katika mazingira maalum na katika kipindi maalum cha wakati
c) Sifa za misimu
– huzuka na kutoweka baada ya muda Fulani
– hutumiwa na kundi Fulani la watu
– baadhi yake hudumu na kusanifishwa
– hupata maana yake kutoka kwa watumiaji pamwe n amuktadha
– huwa si semi sanifu hivyo haipaswi kutumika katika muktadha rasmi
– huundwa kwa mbinu mbalimbali
d) majukumu ya misimu
– kitambulisho cha kundi la watu
– huhifadhi siri za watumiaji

- huibua hisia miongoni mwa watuamiaji
- hukuza uaminifu
- huhifadhi utamaduni
- huondoa urasmi katika mazungumzo
- huwa uwezo wa kuwasa

TATHMINI YA MWIGO YA KAUNTI YA KAJIADO
HATI YA KUHITIMU ELIMU YA SEKONDARI KENYA
KISWAHILI KARATASI 102/1

LAZIMA

1. Ukiwa mhariri wa gazeti la Mulika andika tahariri kuhusu uharibifu wa mito nchini na upendekeze suluhu kwa tatizo hilo
2. Ugatuzi una faida nyingi kuliko hasara. Jadili
3. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali: Ajizi ni nyumba ya njaa.
4. Tunga kisa kinachomalizia maneno yafuatayo…….Nilijitolea kafara na msaada wangu ukazaa natija kwa wengi.

TATHMINI YA MWIGO YA KAUNTI YA KAJIADO
HATI YA KUHITIMU ELIMU YA SEKONDARI KENYA
102/2
KARATASI VLA PILI
KISWAHILI

soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali uliyopewa

Taifa, liwalo lolote, hupenda kuona maandishi yake yako kwenye kiwango cha juu Maandishi ni sehemu ya utamaduni na hakuna taifa linalopenda kuona utamaduni wake uko chini au unadhauliwa na mataifa mengine, Kadiri taifa linavyostawi ndivyo linavyopenda kuwa na maandishi yenye kiwango cha juu, kwani hili huleta fahari:"Maandishi haya yameandikiwa na watu wanaowaza," kila taifa hupenda kusikia mataifa mengine yakisema hivyo kuhusu maandishi yake. Mhakiki ana dhima ya kusema wazi kuhusu kiwango cha maandishi huyu asilia atakapoamua kutunga tena, atashawishika kuandika maandishi yaliyo kwenye kiwango cha juu zaidi. Na waandishi wengine watapatiwa msukumo wa kuandika maandishi yaliyo kwenye kiwango cha juu pia na hivi ndivyo mhakiki anavyosaidia kukuza na kuendeleza maandishi ya taifa lake.

Mhakiki hujiuliza ni kiwango gani mwandishi amefaulu kuwachora wananchi katika harakati zao na kwa kiwango gani ameandika au ameyajadili matatizo yanayoisakama jumuiya hiyo? Je, ni kwa kiwango gani maandishi hayo yatawafanya wauelewe zaidi unyonge wao na kupambana na sababu za unyonge huo? Je,mwandishi amefaulu kwa kiwango gani kupambanua baina ya maadui wa jumuiya hiyo? Ni kwa kiwango gani amepambanua baina ya amali zinazoisaidia jamii kusonga mbele na zile zinazoizorotesha jamii hiyo? Swali hili ni swali la mtazamo. Mhakiki lazima awe akili pevu sana ili aweze kung'amua mambo na akisha yang'amua ayaandike kwa lugha nyepesi, ili mawazo yake yasomeke na kila mtu kwa urahisi. Lugha ngumu na rahisi ni zipi? Hili ni tatizo ambalo mhakiki anapaswa kulielewa na kulitatua; anapaswa kushirikiana na watu wa kila namna ili aelewe wanaongeaje, na atumie lugha yao inapowezekana na inapofaa, kwa kifupi, atumie lugha ambayo itawatumikia wasomi wake.

Ni kiwango gani maandishi hayo yanawazindua na kuwapevusha wasomaji, ni jambo jingine ambalo mhakiki hujishughulisha nalo kila anapofanya uhakiki. Yawapevushe kimawazo na kimtazamo kwa jumla na yajaribu kuwafundisha namna ya kuepukana na kupambana na matatizo yao, yawapevushe ili waweze daima kutambua mawazo au watu gani wanaweza kuwa hatari na sumu kwao. Mhakiki huwasaidia wasomaji kuyabaini maandishi yaliyo sumu kwa jamii na atawasaidia hasa iwapo yeye mwenyewe ni sehemu ya wale wanaopambana na kupigania haki zao. Kuna maandishi mengine ambayo ni mazuri sana na yanagusa hisia za wasomaji kikweli sababu yameandikwa na watu wenye uwezo na fani kupindukia Maandishi hayo ni kama sambusa ambayo juu inametameta lakini ndani imeshindiliwa pilipili nyingi mno. Mhakiki sharti aseme wazi- ayafichue maandishi ya namna hiyo. Kuna maandishi ambayo huwachekesha na kuwaburudisha wasomaji, sababu yameandikwa kwa namna hiyo; na kumbe yanaeneza sumu, na maandishi mengine ingawaje si sumu, huwa pale ili kufurahisha na kuchekesha tu. Kicheko kinasaidia nini? Maandishi haya yanazorotesha harakati kwa kuwachelewesha watu kusoma maandishi yao wote. Mhakiki ni lazima ajiendeleze katika taaluma mbalimbali ili aweze kuwa na mawazo mengi ambayo yatamsaidia kuhakiki maandishi mbalimbali. Mhakiki hodari huichonga jamii yake kimawazo, huimarisha isitetwereshwe na kupofushwa wapotoshi.

Baadhi ya waandishi asilia hueneza kasumba, pengine hufanya vile bila kujitambua Mhakiki lazima awafichue waandishi wanaoeneza mawazo ya kikasumba yasije yakaiambukiza jamii. Mhakiki ni lazima ayafichue na kuyaweka hadharani mawazo yote ya hatari yanayoenezwa kwa makusudi au kwa kutojua

kwa waandishi asilia, kuna baadhi ya watu ambao hupenda kuhakiki vitabu vya watu wanaowaheshimu au marafiki zao, ili kuufanya urafiki baina yao ukomae zaidi, na mara nyingi hujikuta wanaandika muhtasari tu wa maandishi hayo na kujaza sifa kemkem: kamwe siwaiti wahikiki- hawa ni watu hatari sana kwa sababu hawamsaidii mwandishi asilia kujisahihisha ila(kwa kutojua au kwa makusudi) hujiunga na mwandishi asilia, kuizamisha jamii nzima. Lipo kundi jingine ambalo nalo siliiti la wahakiki kundi hili huangalia Fulani ametunga nini na kuanza kuponda vitabu vyake sababu wana fitina zao za siri. Makundi yote haya ni ya hatari sana katika taifa zima, mhakiki asiwe mlevi wa aina yoyote-asilewe Chuki au mapenzi kuhusu watu ambao maandishi yao anayahakiki. Lazima awe razini, asiwe hayawani. Ama sivyo, atakuwa mbomoaji, dufu la mtu.

Maswali ya ufahamu

a) Ipe taarifa hii anwani mwafaka. (alama 1)

b) Mhakiki ana jukumu gani kwa (alama 2)

i. Mwandishi

ii. Msomaji

c) Maandishi huwezaji kugusa hisia za wasomaji? (alama 2)

d) Fafanua ni vipi maandishi huwazindua na kuwapevusha wasomaji. (alama 2)

e) Bainisha aina tatu za wahakiki. (alama 3)

f) Kwa nini mwandishi wa taarifa hii haoni faida ya maandishi yanayochekesha? (alama 2)

g) Eleza maana ya kifungu kifuatacho cha maneno kama kilivyotumika katika taarifa. (alama 1)

Dufu la mtu

2. UFUPISHO

Soma makala yafuatayo kasha ujibu maswali **(alama 15)**

Mwana wa Adamu ni kiumbe cha ajabu! Ni kiumbe kilichopewa uwezo wa kuhodhi na kumiliki kila kitu, kiumbe kilichopewa akili na maarifa fuvu tele ili kutaratibu shughuli na mambi: kiumbe kilichopewa uwezo wa kuwasiliana na kutumia sauti nasibu ili kuwa na urari na muwala; kiumbe kilichopewa uwezo wa kufaidi viumbe wengine kwa njia mbalimbali na jumla jamala; hiki ndicho kiumbe kilichopewa idhini maalum ya kuzaana na kujaza dunia. Huyu ndiye mwana wa mama Hawa ambaye sasa amegeuka ndovu kumla mwanawe.

Kwa sababu ya bongo alizonazo, binadamu ana uwezo wa kutumia teknolojia kwa manufaa yake na ithibati zipo tele. Binadamu ametumia nyambizi kuzuru chini ya bahari, amefika mwezini, amevumbua magala: amevumbua uyoka: amevumbua tarakilishi na sasa shughuli zake ni za kutandaridhi. Mwenyewe yuasema kuwa dunia yake imekuwa kitongoji katika muumano huu.

Chambilecho wavyele, akili nyingi huondoa maarifa. Binadamu amekuwa dubwana linalojenga kushoto na kubomoa kulia na tuna sababu ya kulisoza dubwana hili kidole. Rabana ndiye msanii asiye mfanowe kwani aliisawiri murua. Rabuka akaona yote yalikuwa mema na mazuri: akamwambia binadamu," Haya twende kazi!"

Viwanda vya binadamu vinatiririsha maji-taka ovyo hadi mitoni, maziwani na baharini na matokeo yamekuwa ni vifo vya viumbe vya majini kama samaki ambavyo ni urithi aliopewa na muumba. Hakuna kiumbe kinachoweza kustahimili maisha bila maji safi. Maji yote sasa yametiwa sumu na binadamu kwa sababu ya 'maendeleo' yake. Joshi kutoa katika viwanda vivyo hivyo nalo limehasiri ukanda wa ozone ambao sasa umeruhusu jua kutuhasiri kwa joto kali mno. Siku hizi inasemekana kuwa kuna mvua ya aside inayonyesha katika baadhi ya sehemu za dunia na kuleta madhara makubwa. Labda hata mabahari yamekasirika kwa sababu hivi majuzi katika kile kilichoitwa 'tsunami', bahari lilihamia nchi kavu na kusomba maelfu ya binadamu na kuwameza wazima wazima. Vimbunga navyo vimetokea kwa wingi. Wataalamu wanasema kuwa viwango vya miyeyuko vitazidi kwa sababu ya joto na kiwango cha maji kitazidi pia. Binadamu atatorekea wapi?
Idadi ya binadamu imezidi hadi kiasi asichoweza kukishughulikia kwa sababu anaijaza kiholela kwa sababu anadai kuwa aliruhusiwa kuijaza. Hii ni imani potovu. Anasahau kuwa alipewa ubongo wa kuwaza na kuwazua kabla ya kufanya chochote. Dhiki, maradhi na ufukara zimehamia kwa binadamu na kumtia kiwewe'

Binadamu amefyeka misitu kwa kutaka makao, mashamba, mbao, makaa, ujenzi wa nyumba na

barabara na mahitaji mengine mengi. Wanyama wamefurushwa na wengi kuangamia kwa sababu ya ukosefu chakula na wengine kushindwa kuhimili mabadiliko katika mazingira. Chemichemi za maji zimekauka nalo jangwa limeanza kutuzuru kwa kasi inayotisha. Kazi ya binadamu imekuwa ya kusukia kamba motoni. Itambidi aanze kujenga kwa matofali ya barafu.

a) Bila kupoteza maana iliyokusudiwa na mwandishi wa taarifa, fupisha aya ya kwanza. (alama 5)
(Maneno 40-50)
b) Kwa kuzingatia aya 4 za mwisho, eleza mambo muhimu yanayoshughulikiwa na mwandishi (maneno 95-105) (alama 8)

3. MATUMIZI YA LIGHA (alama 40)

a) Taja vigezo vitatu vya kuainisha konsoonanti za Kiswahili. (alama 3)
b) Onyesha shadda katika maneno yafuatayo
   i. Insha
   ii. Sanaa
c) Kwa kutoa mifano onyesha matumizi mawili ya vifungo (alama 2)
d) Ainisha viambishi katika neon lifuatalo (alama 3)
Hamkuwalisha
e) Tumia kiunganishi cha uteuzi katika sentensi. (alama 2)
f) Tumia kivumishi-**ingineo** katika ngeli ya I-I katika sentensi. (alama 2)
g) Andika upya sentensi ifuatayo kwa kutumia kitenzi **ndi-**
Sisi tulipanga mkutano huo. (alama 2)
h) Tumia kirejeshi cha kati kuunganisha sentensi hizi
Mgeni amefika mapema (alama 2)
Mgeni amekaribishwa
i) Andika udogo na ukubwa wa neon ukuta. (alama 2)
j) Tunga sentensi ukitumia kitenzi –ja kubainisha kauli ya kutendewa. (alama 2)
k) Tumia kiwakilishi kisisitizi cha nomino uteo katika umoja, katika sentensi. (alama 2)
l) Eleza maana ya kishazi. (alama 2)
m) Changanua sentensi ifuatayo kwanjia ya mistari.
Wanafunzi wanashangilia bali wengine hawafurahii. (alama 4)
n) Unda nomino ya dhahania kutoka vitenzi vifuatavyo (alama 2)
   i. Dharau
   ii. –wa
o) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo. (alama 2)
Amenipigia ngoma
p) Andika hii sentensi kwa wingi. Hakimu alimhukumu seremala aliyeiba samani. (alama 2)
q) Andika kwa usemi wa taarifa.
“ninaumwa na kichwa sana leo.” Mwalimu alisema. (alama 3)
r) Andika neon linguine lenye maana sawa:
Piku (alama 1)

4. ISIMUJAMII (ALAMA 10)

a) Kwa nini kulikuwa na haja ya kusanifisha lugha ya Kiswahili. Toa sababu tano. (alama 5)
b) ….sote tunajua kwamba ni kudura. makiwa!
i. Tambua sajili iliyotumika katika dondoo hili. (alama 1)
ii. Eleza sifa nne za sajili hiyo. (alama 4)

TATHMINI YA MWIGO YA KAUNTI YA KAJIADO
hati ya kuhitimu elimu ya sekondari kenya
KISWAHILI
KARATASI YA TATU

1. **LAZIMA: SEHEMU YA A**
USHAIRI

Soma shairi ulilopewa kwa makini kasha ujibu maswali

Ah! siambile ovyo, samba ah! kupuuzwa
Ah! hii niambavyo, si kwaamba nimependezwa
Ah! moyo wamba hivyo, kwayo niliyofanyizwa
Ah! namba nionavyo, vipasavyo kuelezwa.

Ah! si mimi nilivyo, mawazo yametatizwa
Ah! tata za magovyo, fikira zimeshangazwa
Ah! naviwe viwavyo, sioni pa kutulizwa
Ah! namba nionavyo, vipasavyo kuelezwa.

Ah! sililii yavyo, kwa kutaka kunyamazwa
Ah! sipendezwi navyo, sipendezwi kebezwa
Ah! ni hivi ambavyo, mkata heshi kutezwa?
Ah! namba nionavyo, vipasavyo kuelezwa.

Ah! kukicha ya vivyo, na uchao yajalizwa
Ah! havishi viishavyo, na matayo kuambizwa
Ah! sivyo hivi sivyo, vyakanywa na kukatazwa
Ah! namba nionavyo, vipasavyo kuelezwa.

Ah! lau hata ndivyo, basi hata kulekezwa
Ah! wayatenda kwayo, kwamba ndiko kutukuzwa
Ah! tenda utendavyo, ni kuwa watendekezwa
Ah! namba nionavyo, vipasavyo kuelezwa.

Ah! ni vile wambwayo, togo upate tangazwa
Ah! kila upendwavyo, mwisho ‘we utatukizwa
Ah! pendo lianzwavyo, sivyo vya kuishilizwa
Ah! namba nionavyo, vipasavyo kuelezwa.

Ah! kila lenye govyo, halikawii kuvizwa
Ah! nalende lendavyo, ukomo litagotezwa
Ah! ni vipi kulivyo, kukadumu kutulizwa?
Ah! namba nionavyo, vipasavyo kuelezwa.

Ah! dunia ni kyovyo, kizamacho chaibuzwa
Ah! ni mangapi ja’vyo, hayako metokomezwa
Ah! jaa lijaavyo, mwishilio lapunguzwa
Ah! namba nionavyo, vipasavyo kuelezwa.

Ah! kaa ukaavyo, hatimayo yasogezwa
Ah! nauwe uwavyo, atende hulipizwa
Ah! hakuna lilivyo, gumu lisilolegezwa
Ah! namba nionavyo, vipasyo kuelezwa.

a) Taja mambo matatu ambayo mshairi analalamikia. (alama 3)
b) Shairi hili liko katika bahari gani? Toa sababu. (alama 2)
c) Taja na utolee mifano tamathali mbili za lugha zilizotumiwa na mshairi. (alama 4)
d) Huku ukitoa mifano kutoka shairi, eleza matumizi yoyote matatu ya uhuru wa ushairi. (alama 3)

e) Andika ubeti wa kwanza katika lugha ya nadharia.
(alama 4)
f) Tambua toni ya mshairi. (alama 2)
g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa kwenye shairi.
(alama 2)
i. Watendekezwa
ii. Togo

SEHEMU YA B
RIWAYA
Kidagaa Kimemwozea; *Ken Walibora*
Jibu swali 2 au la 3

2. Thibitisha matumizi ya mbinu zifuatazo katika Riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea.*
i. Sitiari (alama 10)
ii. Taswira (alama 10)

3. …..ilibidi kulipa hela nyingi za kadhongo, kuwalipa polisi, makarani wa mahakama, majaji, wajua tena mti hauendi ila kwa nyenzo.
a) Eleza muktadha wa dondoo hili.
(alama 4)
b) Eleza tamathali ya usemi iliyo katika dondoo.
(alama 2)
c) Fafanua maudhui yanayorejelewa katika dondoo hili kwa kutumia mifano saba
(alama 14)

SEHEMU YA C
TAMTHILIA:
Mstahiki Meya: *Timothy M. Arege*
Jibu swali 4

4. **a)** "…….Duniani kuna watu na viatu…." Fafanua muktadha wa dondoo hili.
(alama 4)
b) Thibitisha ukweli wa kauli hii ukirejelea Tamthilia ya Mstahiki Meya.
(alama 16)

SEHEMU YA D
HADITHI FUPI:
Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine: K. Walibora na S.A Mohamed.
Jibu swali la 5 au la 6

5. "……Usipoachana na mambo haya nitaacha kazi,"
a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
b) Thibitisha kuwa mnenewa ni katili. (alama 16)

6. Kwa kurejelea hadithi zifuatazo onyesha jinsi vijana walivyosawiriwa.
i. Gilasi ya mwisho makaburini. (alama 5)
ii. Kanda la usufi
iii. Shaka ya mambo
iv. Tazamana na mauti

SEHEMU E
FASIHI SIMULIZI

7. a) Mbali na kuapiza na kufukuza pepo taja miktadha mine mingine ambapo ulumbi hutumika.
(alama 4)
b) Eleza sifa zozote tatu za ulumbi.
(alama 6)
c) i) Maapizo ni nini? (alama 2)
ii) fafanua umuhimu wa maapizo katika jamii.
(alama 8)

8. Ndimi kisoi, dume la ukoo mtukufu
Ulojipambanua kwa mabingwa
Wachezaji hodari wa ngoma
Ndimi dume liloingia nyanjani.
a) Tambua aina ya maghani inayowasilishwa. (alama 2)
b) Fafanua sifa bainifu za aina hii ya utunzi. (alama 10)

c) Eleza umuhimu wa tungo hizi katika jamii. (alama 8)

TATHMINI YA MWIGO YA KAUNTI YA KAJIADO
hati ya kuhitimu elimu ya sekondari kenya
KISWAHILI
KARATASI YA 1

3. Ajizi ni kuchelewa kutenda jambo au kushindwa kufanya jambo.
   Maana ya methali
_ Uvivu wa kuamua au uzembwe ni ufunguo wa ufukara au umaskini.
   Matumizi yake.
_ Huwahimiza watu wawe wepesi katika kufanya uamuzi au wasiwe na tabia ya kuchelea chelea jambo kama
   wanataka kufanikiwa maishani.
_ Methali nyingine yeneye maana saw ana hii ni “ajizi ni ufunguo wa umaskini.”
_ Kisa chaweza kuafiki hali zifuatazo.
   i. Mwanafunzi kuzembea shuleni hatimaye hafaulu katika mtihani.
   ii. Mkulima asiye tia bidii halafu asipate mavuno ya kulipisha.
   iii. Mfanyibiashara ambaye haweki bidii katika biashara yake apate hasara tupu na hali nyingine zozote.

Tanbihi

1. Mtahiniwa lazima athibitishe ukweli wa methali hii.Asipofanya hivyo amepotoka kimaudhui na atuzwe D$^{03}/_{20}$
2. Atakayekuza dhana ya ajizi tu bila kuonyesha athari atakuwa ameshughulikia upande mmoja tu,asipitishe alama C+ $^{10}/_{20}$
3. Athari(njaa) yaweza kujitokeza katika sura mabalimbali k.m kuanguka mtihani,biashara kuanguka,ndoa kuvunjika.n.k.
4. Akitunga methali nyingine na aitungie kisa achukuliwe kuwa amejitungia swali lake na kulijibu atuzwe D-$^{01}/_{20}$
4. Hili ni swali la mdokezo.Mtahiniwa lazima atunge kisa kitakachoafiki mdokezo huo.Kisa lazima kionyeshe kujitolea kafara (kujitolea kwa vyovyote licha ya vikwazo) na kuzaa natija (kufaidika)
   Kisa cha mtahiniwa kinaweza kuafiki hali zifuatazo:
_ Kiongozi wa wafanyikazi kuwatetea wenzake licha ya pingamizi kutoka kwa mwajiri hatimaye hali yao ya kufanyia kazi inaboreshwa.
_ Safarini anjitolea kuwanusuru wengine wakati chombo au gari lilikuwa laenda mrama.
_ Yeye akiwa motto aliyeajiriwa kuwasaidia ndugu zake na wazazi wakafaidika.
   Zingatia hali nyingine zinaazoafikianan na dondoo.
   Tanbihi

1. Akikosa kumalizia kwa dondoo alilopewa lakini kisa kiafikiane nalo,amepungukiwa kimtindo.
2. Akiongezea maneno baada ya dondoo au katikati achukuliwe kuwa ana upungufu wa kimtindo.
3. Lazima kisa kimhusu yeye mwenyewe.Asiopojihusisha amepotoka kimaudhui na atuzwe D$^{03}/_{20}$

TATHMINI YA MWIGO YA KAUNTI YA KAJIADO
hati ya kuhitimu elimu ya sekondari kenya
KISWAHILI
KARATASI YA 2


a) Dhima ya mhakiki(al.1)
b) Mwandishi-kuinua kiwango cha uandishi cha mwandishi kwa kusema wazi kuwa maandishi yako kiwango chja chini.(al;.2)
   ii) Msomaji :kumsaidia kuyabaini maandishi yaliyo sumu kwa jamii.(al.2)
c) Kwa kuwaburudisha na kuchekesha. (al.2)
d) Yanapojjaribu kuwafundisha namna ya kuepuka na kupambana na matatizo yao.
- Yanapowapevusha ili waweze daima kutambua mawazo au watu gani wanaweza kuwa hatari na sumu kwao. (al 2)

e) i) Mhakiki hodari ni aichongaye jamii yake kimawazo na kuimarisha isitetereshwe na kupofushwa na waandishi
   wapotoshi.
   ii. Wanapoenda kuhakiki vitabu vya watu wanaowaheshimu au marafiki zao ili kukoma urafiki wao.
   iii) Wanaongalia Fulani ametunga nini na kupanda vitabu vyake sababu wana fitina zao za siri. (3x1=3)
f) kwa sababu yanazorotesha harakati kwa kuwachelewesha watu kusoma maandishi yenye mafunzo ya kuwapa mbinu mpya zitakazowasaidia dhidi ya mazingira kwa faida zao. (al 2)

UFUPISHO

a) i) Binadamu alipewa uwezo wa kumiliki kila kitu.
   ii) Binadamu alipewa akili na maarifa ili kupanga mambo yake.
   iii) Alipewa uwezo wa kuwasiliana na wenzake kwa kutumia lugha.
   iv) Alipewa uwezo wa kufaidika kutokana na mazingira yake.
   v) Alipewa uwezo wa kuza na kujaza dunia. Yoyote 5xi=5)

b) i) Binadamu amekuwa dubwana linalojenga na kubomoa.
   ii) Viwanda vinachafua maji na kuua viumbe muhimu kwa binadamu.
   iii) Moshi kutoka viwandani umedhuru ukanda wa ozone na joto kuzidi duniani.
   iv) Idadi ya binadamu imeongezeka zaidi ya uwezo wake.
   v) Maradhi na ufukara yamekuwa matatizo makubwa kwa binadamu.
   vi) Binadamu anafyeka misitu yote.
   vii) Binadamu amewafurusha na kuwaangamiza baadhi ya wanyama.
   viii) Chemichemi za maji zimekauka na kuwa jangwa. (Zozote 8x1=8)



SWALI LA 3
a)
- Mahali pa kutumika
- Nmna ya kutumika
- Marindimo /mtetemeko katiak nyuzi za sauti. (3X1=3)

b) ‘Insha au insha (al.1)
   ii)Sa’naa au sanaa (al.1)
Tanbihi:
Akipigia mstari silabi yenye kutiliwa mkazo apewe alama.
c)
- Kufungua maneno ya ziada /maelezo zaidi.
- Kufungua nambari /herufi za kuorodhesha.
- Katika mazungumzo/mahojiano /tamthilia. Zozote 2x1=al2)

d) ha-kikanushi
   m-nafsi

ku-wakati
wa-kitendwa
ish-kauli
a-kiishio (6 ½ =al.3)

e) Wal,au ama 1x2=2)
f) Nyingineyo (1x2=2)
g) Sisi ndisi tulipanga mkutano huo.
h) Mgeni aliyefika mapema amekaribishwa. (1x2=2)
i) Ukuta- kikuta (udogo) 2x1=)
j) Mf. Mtoto amejiwa na mamke. 1x2=2)
k) uu hu
huu huu
uo huo
huohuo
ule ule chochote kimoja
Tanbihi
Lazima iwe sentensi katika umoja.
l) Kishazi ni fungu la maneno lenye muundo wa kundi Nomino na kundi Tenzi katika muktadha wa sentensi.
(2x1=2)
m) Wanafunzi wanashangilia bali wengine hawfurahii.
S - S1 +U + S2
S1 -KN +KT
KN -N
N -Wanafunzi
KT -T
T -Wanashangilia
U -bali
S2 -KN + KT
KN -W
W -Wengine
KT -T
T -hawafurahii
Maelezo
Vittahiniwa 3= ala.1
Vitahiniwa 12=ala.2

n) I)Dharau –dharau (al.1)
ii)-wa - uwepo (iala.10
o) Amenipigia ngoma
i) Ameniburudisha kwa kupiga ngoma
ii) Amepiga ngoma kwa niaba yangu.
ii) Amepiga ngoma akielekeza kwangu
iii) Amenipiga kwasababu ya ngoma . zozote 2x1=2

✓ ✓✓ ✓ ✓✓

p) Mahakimu waliwahukumu maseremal walioiba samani. Vitahiniwa (3=ala.1) 6=ala.2)✓
q)Walimu alisema kwamba alikuwa anaumwa na kichwa san siku hiyo.✓ (3x1=3)
r) Piku –shinda
zidi
pita
weza (al.1)

4. ISIMU JAMII

- Kuwepo kwa lahaja nyingi- baadhi yazo hazingeeleweka na kila mtu.
- Kulikuwa na haja ya kuwa na hati sawa ya kuandika Kiswahili –Kul;ikuwa na hati nyingi kwa mfano ,Kirumi , kilatini na kiarabu.
- Kulikuwa na haja ya kusawazisha maandishi ya kitaalamu katika kamusi.
- Haja ya kuwa na lugha moja ya mawasiliano na elimu –kutumika katika kamusi.

- Haja ya kuwa na lugha moja ya mawasiliano na elimu –kutumika katika mikutano, shuleni, vyuoni n.k (5x1=5)

b) Sajili ya mazishi /matanga /kilio masikitiko /msiba/ maombolezo/uzikaji.

Sifa

- Msamiati maalum kwa mfano makiwa marehemu.
- Lugha ya kufariji/liwaza
- Yenye matumaini
- Matumizi ya vihihisishi oh, wuui,
- Lugha ya kusitasita
- Huhusisha sana mambo ya kidini na Mungu na Imani za jamii.
- Ni lugha ya hasira.
- Kuchanganya ndimi
- Inaadaman na viziada lugha
- Matumizi ya sentensi fupi
- Matummizi ya sentensi ndefu
- Imesheheni sifa za m wendazake
- Matumizi ya lugha isiyozingatia kanuni za kisarufi. Zozote 5x1=5)

Maneno 6 katika kila mstari kurasa mbili na robo
Maneno 5 katika kila mstari kaurasa mbili na robo tatu.
Maneno 4 katika kila mstari Kurasa tatu na robo tatu
Maneno 3 katika kila mstari Kurasa nne na nusu
Kufikia maneno 174 Insha robo
Maneno 175-274 insha nusu
Maneno 275- 374 Insha robo tatu
Maneno 375 na kuendelea insha

WESTLANDS DISTRICT JOINT EXAMINATION
KISWAHILI
Karatasi ya 1
INSHA
Muda: Saa 1 ¾

MASWALI

1. **SWALI LA LAZIMA**
   Ukiwa Gavana Mtajika wa Kaunti yako umealikwa kuwazungumzia wanafunzi wa kidato cha nne katika shule ya Mafanikio. Andika Tawasifu utakayowasilisha.

2. Eleza jinsi udanganyifu katika mitihani utaathiri maisha ya kizasi kijacho.

3. Andika kisa kitakachothibitisha maana ya methali: Mtenda mema kwa watu atendea nafsiye.

4. Kamilisha tukio kwa maneno yafuatayo:
   "….waliwasili saa tatu baadaye. Uharibifu wa mali na maisha ulikuwa umeshatendeka wala kufika kwao hakukusaidia kwa lolote."

WESTLANDS DISTRICT JOINT EXAMINATION
KISWAHILI
Karatasi ya 2
(Ufahamu, ufupisho, sarufi na matumizi ya lugha na Isimujamii)
Muda: Saa 2 ½

1. **UFAHAMU (ALAMA 15)**
   Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali yanayofuatia.

   Mateso ya wanawakiwa ni suala la kijamiilinalofaa kutazamwa kwa darubini kali. Hata hivyo wanaoathirika zaidi ni watoto ambao bado wako katika umri unaohitaji kulelewa na kupewa mahitaji ya msingi kama mavazi, malazi, Elimu na mengine anuwai. Hali ya kuachwa na wazazi imekuwa ikizikumba jamii tangu enzi za mababu na kila itokeapo, wanajamii huipokea kwa mitazamo tofautitofauti, hivyo kuwafanya wanawakiwa kuathirika sana.

   Baadhi ya jamii zina imani za kijadi pamwe na mila zilizochakaa zinazozifanya kuamini kuwa baadhi ya vifo hutokana na laana. Wngine huchukulia kuwa mwendazake ameondolewa na ulozi. Imani kama hizi huifanya jamii kuwatia watoto walioachwa katika mkumbo ule ule, hivyo kuwaangalia kwa macho yasiyo ya kawaida. Hili husababisha dhana gane. Hali hii husababisha kuwachukulia watoto kama wanaotoka katika kizazi kilicholaaniwa. Jamii basi hukosa kuwapa watoto hawa stahiki yao. Hata wanapojitahidi kuiwania nafasi yao, waliowazunguka huwavunja mioyo. Jitihada zao huishia kuwa si chochote kwa kuwa jamii inawatazama kama waliolaaniwa.

   Punde baada ya mzazi mmoja au wote wawili waendapo wasikorudi, inatarajiwa kwamba aliyeachiwa mtoto, awe mzazi wake, mwanafamilia aur jirani awajibike na kumtnza mwanamkiwa. Kunao kadha wa kadha wanaowajibika – ninawavulia kofia. Hata hivyo wengi hutelekeza jukumu hili walilopewa na Muumba. Si ajabu basi kuona kuwa idadi ya watoto hawa ni waliopotelewa na wazazi wao. Inakera zaidi kugundua kuwa baadhi ya watoto hawa wana mzazi – mmoja. Kwamba mke au mume wa mtu ameaga, au iwe kwamba mzasi mmoja alimzaa mtoto na kumwachia mwenzake mzigo wa ulezi, aliyeachiwa ana jukumu la kumpa mwanawe mahitaji ya msingi. Machoni pa Jalali, kila anayepuuza wajibu huu ana hukumu yake siku ya kiama.

   Ni haki ya kila mtoto kupata Elimu. Katika katiba ya Kenya mathalan, elimu ya msingi, yaani kuanzia shule ye chekechea hadi kitado cha nne ni ya lazima. Tangu hapo hata hivyo, jamii zimekuwa zikiwanyima wanawakiwa wengi Elimu. Kwamba kunao wachache wanaowaelimisha baadhi ya wanawakiwa, ni kweli. Hata hivyo, wengine hukosa hata wa kuwapeleka katika shule ya chekechea, hivyo kuishia kutojua hata kuandika majina yao. Mfikirie mtu katika karne ya 21 asiyejua kusoma wala

kuandika! Nani ajuaye, huenda huyo mwanamkiwa asiyepelekwa shuleni ndiye angalikuwa profesa, daktari, mwalimu, rubani au msomi mtajika na mtaalamu wa uwanja muhimu katika jamii!

Kila mtoto ana haki ya kulelewa hadi kufikia utu uzima kabla ya kupewa majukumu mazito. Katika katiba ya Kenya, utu uzima, ulio umri wa kuanza kufanya kazi huanzia miaka 18. Wanaohakikisha watoto hawa wametimiza utu uzima kabla ya kufanyizwa gange ngumu wanafaa pongezi. Hata hivyo wanawakiwa wamekuwa wakitumiwa na wengi kama punda wa huduma. Wanaaila, wengine huwachukua wanawakiwa kwa machozi mengi wazai wao waagapo na kuapa kuwahifadhi na kuwatunza wana wale wa ndugu zao, kumbe ni machozi ya samba kumlilia swara Hata kabla ya mwili wa mzazi mhusika kuliwa na viwavi, mateso kwa mtoto yule huanza, akawa ndiye afanyaye kazi zote ngumu. Utakuta watoto wao wamekaa kama sultan bin jerehe huku mwanamkiwa yule akiwapikia, kuwafulia nguo, kudeki, karibu hata awaoshe miili! Kazi kama zile za shokoa huwa za sulubu na aghalabu husindikizwa kwa matusi yasiyoandikika.

Baadhi ya waja walionyimwa huruma huwahadaa wanawakiwa na kuwapeleka ng'ambo wakitumia vyambo, kuwa wakifika kule watapata kazi za kifahari. Maskini wale huishia kushikwa shokoa, wakawa watumwa katika nyumba za waajiri wao, bila namna ya kujinasua. Wengine huishia kutumiwa kama watumwa wa 'kimapenzi' katika madanguro, miili yao ikawa ya kuuziwa makahaba waroho wasiojali utu. Kujinasua kule huwa sawa na kujitahidi kuokoa ukuni uliokwishageuka jivu, maadamu wanawakiwa aghalabu hukosa watu wenye mioyo ya huruma ya kuwashughulikia. Wengi huitumia methali '*mwana wo ndugu kirugu mjukuu mwanangwa'* kuwapuuzilia mbali wanawakiwa ambao hukimbiliwa tu wabinafsi hawa wanapofaikia wenyewe.

Maswali

a) Taja anwani mwafaka kwa kifungu hiki. (alama 1)
b) Wanaosumbuka sana miongoni mwa wanawakiwa ni kina nani? (alama 2)
c) Eleza dhana ya 'mwanamkiwa.' (alama 2)
d) Imani na mila za jadi huchukuliwa kuwa chanzo cha uanaukiwa. Taja mambo mawili kuthibitisha. (alama 2)
e) Ni mateso yapi mawili ambayo wanawakiwa hupitia wanapohadaiwa na kupelekwa ng'ambo? (alama 2)
f) 'Baadhi ya watu wa jamii ya wanawakiwa wana unafiki.' Eleza. (alama 3)
g) Eleza maana za maneno au vifungu vifuatavyo kulingana na matumizi katika kifungu. (alama 3)
   i) Pamwe na mila
   ii) Gange ngumu
   iii) Wakitumia vyambo

2. UFUPISHO (ALAMA 15)

Soma taarifa ifuatayo kasha ujibu mawali yanayofuata.

Sanaa ya jadi ni njia moja ya mawasiliano ambayo ni adhimu, hasa barani Afrika. Mawasiliano kupitia kwa sanaa ya jadi ni njia bunifu ya kuwasilisha ujumbe kupitia kwa sanaa tendi kama vile drama, ushairi tendi, masimulizi nyimbo, ngoma na kadhalika. Njia hii imekuwa ikitumika katika jamii nyingi za Kiafrika toka jadi kwa ufanisi mkubwa sana, kuwasilisha ujumbe kwa wanajamii, hasa hekima na busara ya wakongwe kwao chipukizi.

Takribani katika jamii zote za Kiafrika, sherehe yoyote ya jadi haikukosa sanaa tendi. Lazima pangekuweko na sanaa tendi katika sherehe kama vile tohara, kutakaswa na kutawazwa kwa viongozi, mazishi, ndoa na hafla za burudani. Licha ya kuburudihsa na kuchangamsha waliohudhuria, sanaa hizi zilitumika kuwasilisha na kupasha ujumbe. Sanaa hizi hata hivyo hazijapitwa na wakati na bado zinaweza zikatumika sambamba na njia za kisasa na mawasiliano kama vile redio, runinga, magazeti, majarida na wavuti.

Matumizi ya sanaa ya jadi pamoja na njia za kisasa za mawasiliano yana manufaa lukuki. Kwanza, matumizi haya yataweza kuwashirikisha kikamilifu watu wengi katika mawasiliano, hasa akika yahe wa mashambani na wanaotoka katika mitaa ya mabanda ambao huhisi wametengwa na njia za kisasa za

mawasiliano. Aghalabu, njia za kisasa za mawasiliano huchukuliwa na baadhi ya wanajamii kuwa ni milki ya walioelimika, walio mijini na hasa wenye ushawishi mkubwa katika kuunda na kutekeleza sera zinazotawala nchi.

Hali kadhalika, mawasiliano huchukuliwa kuwa ni himaya ya watu wanaojiweka mbele kuwa wajuzi wa kila kitu. Wao huzitumia njia hizo kuendeleza maslahi yao kwa kutoa maamuzi yanayowaathiri hata waliotengwa, bila kuwashirikisha katika maamuzi hayo. Fauka ya haya, njia za kisasa za mawasiliano hutumia lugha ambazo hazifahamiki na wengi. Aghalabu hutumia lugha za kigeni kama vile Kingereza na Kifaransa, ati kwa kuwa ndizo lugha za kimataifa na lugha tukufu, ingawa ujumbe unaowasilishwa na lugha hizo huusiwa kwa namna yenye utata na isiyoeleweka na wengi. Matokeo ya ujumbe huo ni athari kwao pamoja na vizazi vyao. Isitioshe, njia hizi huwa ghali na pia huchukuana na teknolojia inayokanganya. Hali hizi ndizo huchangia kutngwa kwa wanajamii na viongozi, na kuwafanya watumiaji baridi wa njia hizi za mawasiliano kwa kuwakosesha fursa ya kutoa mwitiko ama michango yao kupitia kwa njia hizi.

Kwa upande mwingine, matumizi ya njia ya sanaa za jada hushirkisha watu wote – walioelimika na wasioelimika. Hii ni kwa kuwa njia hii haitegemei matini yaliyoandikwa. Pili, njia hii haitumii teknolojia inayokanganya na iliyo ghali. Zaidi ya haya, njia ya sanaa za jadi hupasha ujumbe huku ikichangamsha, kuburudisha, kuteka na kuwavutia wengi huku ikidumisha urazini na taharuki zao. Aidha, sanaa za jadi hutoa nafasi ya kurudia igizo au onyesho na kuwasilisha jumbe anuai kwa muda mfupi sana.

Sanaa ya jadi, kama njia ya mawasiliano, hutoa nafasi sawa kwa watu wote kuelimika na kupata maarifa bila kubagua kwa misingi ya umri au jinsia. Hii ni kwa kuwa wakubwa kwa wadogo, chipukizi kwa wakongwe, wake kwa waume na wavulana kwa wasichana wanaweza wakashiriki katika maonyesho au maigizo. Sanaa tendi za kiafrika aidha hutoa nafasi kwa hadhira kushiriki. Njia hii pia ni maarufu katika kuzindua, kuhamasisha, na kusambaza ujumbe kwa watu wengi bila kuwachosha wala kuwasinya. Licha ya kuwa ina uwezo wa kumchongoa na kumchambua mtu kwa wakati huo huo, ina uwezo pia wa kumfanya mtu asijihisi kuwa anaingiliwa, kusimangwa, kukashifiwa wala kufanyiwa stihizai. Hivyo basi, hakuna kwenda mahakamani kushtaki na kudai fidia kama ilivyo katika njia za mawasiliano za kisasa. Sanaa tendi huwa hailengi mtu mahususi bali kaumu inayoshiriki, na kila mmoja huathirika kivyake.

Maswali

a) Kwa maneno kati ya 40-50, eleza mambo yote muhimu anayozungumzia mwandishi katika aya ya kwanza nay a
pili. (alama 7)
b) Fupisha ujumbe katika aya ya tatu, nne na tano kwa maneno kati ya 100-110.
(alama 10)

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a) Eleza tofauti kati ya sauti zifuatazo.
(alama 2)
/ng'/na/s/
b) Tofautisha shadda na kiimbo. (alama 2)
c) Andika kinyume cha sentensi hii.
Jogoo akiwa juu ya banda aliwika na kusikika kote.
(alama 2)
d) Geuza sentensi ifuatayo katika udogo wingi.
(alama 2)
Mbuzi alimgonga mtu aliyekuwa akikimbia.
e) i) Eleza maana ya ngeli. (alama 1)
ii) Taja na ubainishe nomino inayopatikana katika ngeli mbli tofauti. (alama 2)
f) Yakinisha sentensi ifuatayo:
(alama 2)
Mwanafunzi asipompata hatampa ujumbe.
g) Tunga sentensi kuonyesha matumizi ya kihusishi cha sababu. (alama 2)
h) Andika sentensi yenye muundo ufuatao: (alama 4)
KN (W+S)$^{-}$+ KT(T+RN (N+V))

i) Sahihisha sentensi ifuatayo:
(alama 2)
Mkutano uliohairishwa ulikusudia kuwapea washindi tuzo.

j. Mbwa aliyepotelea mwituni alipatikana kidimbwini. (Anza: Kidimbwini….) (alama 2)

k. Ainisha mofimu katika neno: (alama 3)
Waliomteremshia

l. Bainisha matumizi ya kiambishi **ndi-** katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

m. Andika sentensi kuonyesha matumizi mawili ya kistari kirefu. (alama 2)

n. Tambua aina za shamirisho katika sentensi ifuatayo:
(alama 3)
Kiti alichonunuliwa babu kwa pesa taslimu na Kefa kinapendeza.

o. Bainisha aina za virai katika sentensi hii: (alama 3)
Dada yao mrembo anatembea kitausi mjini.

p. Tumia kitenzi **chota** katika sentensi kama kishazi huru na kishazi tegemezi.
(alama 2)

q. Unda vitenzi vinavyotokana na nomono zifuatazo:
(alama 2)

i) Sitiara

ii) Mtihani

5. ISIMU JAMII

Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali.

K: Aisee! Kaka hujambo?
S: Sijambo ndugu. How are you today?
K: Am okay.
S: Je, ulipata message yangu?
K: Ipi hiyo?
S: Kuhusu mtihani wa KCSE.
K: Naam, inafaa tudiscuss.
S: Bila shaka kesho itakuwa heri.
K: Sawa, asante.

Maswali

i) Tambua sajili hii. (alama 2)

ii) Jadili kwa mifano **kuchanganya ndimi** na **kuhamisha ndimi** katika mazungumzo ya K na S. (alama 4)

iii) Toafutisha **lakabu** na **misimu**. (alama 4)

WESTLANDS DISTRICT JOINT EXAMINATION
KISWAHILI
Karatasi ya 3
FASIHI
Muda: Saa 2 ½

1. **LAZIMA:**
SEHEMU YA A: TAMTHILIA
Mstahiki Meya: Timothy M. Arege.

1. "Nanyi vilevile msikate tama. Endeleeni kushinikiza kumwona…. Mlango hatimaye huenda ukasalimu amri."
a) Weka dondoo hili katika muktadha wake.
(alama 4)
b) Taja na utolee mfano tamathali zozote mbili za lugha zilizotumika katika dondoo hili.
(alama 4)
c) Eleza ni kwa nini wanaorejelewa wako karibu kukata tama.
(alama 8)
d) Fafanua sifa zozote nne za mzungumzaji wa maneno haya.
(alama 4)

SEHEMU YA B: RIWAYA
Kidagaa Kimemwozea: Ken Walibora
Jibu Swali la 2 au 3.

2. "Nilichodhamiria mimi ni kushirikiana …. Kumnyonyoa kupungu mmoja, ila sikutaka niingie pahala pake niruke
juu nikijihadaa kwamba nitafika mbinguni….."
a) Eleza muktadhaa wa dondoo hili.
(alama 4)
b) Fafanua namna kipunga alivyonyonyolewa.
(alama 8)
c) Eleza umuhimu sita wa kupungu anayerejelewa.
(alama 6)
3. Taja na utoe mfano wa tamathali yoyote iliyotumika katika dondoo.
(alama 2) Amani na Imani wanatoa mchango upi katika ujenzi wa jamii mpya? Jadili.
(alama 20)

SEHEMU YA C: USHAIRI

4. **Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali.**
SIWE

1. Siwe ulosema jana, yakuwa umashuhuri?
Ya kuwa wajuwa sana, aidha huna kiburi?
Nchini wajulikana, mwanasiasa mahiri,'
Bungeni tukuajiri?

2. Siwe ulotushawishi, kwa chumvi na kwa sukari,
Na matamu matamshi, ukaziteka suduri.
Ukanena penye moshi, moto ndiyo yakwe siri,
Nawe ndiye hiyo nari?

3. Siwe uloji'ta moto, uwakao biribiri.,
Kama 'tatia fukuto, Litakalo leta kheri,
Utatufunua mato, Maisha yawe mazuri,
Tukupe kura waziri?

4. Siwe ulosema hayo, na mengi ukabashir.,
Ukamba wafata nyao, nyayo sizo utiriri,
Tusiwe na wayowayo, wa kufikirifikiri,

Tukuachie ujari?

5. Siwe tulokuinua, Mabegani kama mwari,
   Tungawa talemelewa, waume tukajasiri.,
   Kamba tukikuchaguwa, memba kwetu yatajiri,
   Tukaketi kusubiri?

6. Siwe ulotugeuka, kwamba leo u waziri,
   Wajiona melimuka, tena ukawa ayari,
   Walaghai ukicheka, ukuu umekughuri,
   Leo mekuwa hodari?
7. Siwe ulojawa raha, za hino yetu sayari,
   Ukawa ja vile shaha, hatukupati shauri,
   Kutuona ni karaha, wakatiwo twahasiri,
   Ushakiya msitari?

8. Siwe uliyetughura, ukafunga na safari,
   Ukaelekea bara, Kwa wenzio matajiri.,
   Ukatuacha majura, na tama kukithiri,
   Kanama Ushaghairi?

9. Siwe uliyetuasi, ukenda pasi kwaheri,
   Mbona hutambii nasi, tukayajua yetu shari,
   Leo una masidisi, husemi na aso gari,
   Ndio mezidi jeuri?

10. Siwe 'lotwaa mgwisho, ukawa wajifakhiri?
    Chenye mwanzo kina mwisho, hili wajuwa dhahiri,
    Vyaja kutoka vitisho, kwani hayo sidahari,
    Mambo mengi mdawari?

11. Siwe utakayeiza, mwishowo ukidhihiri,
    Siku itayoteleza, kuja kwetu ansari,
    Kuja kutubembeleza, kwa nyunga nalo khamri,
    'Tauya nazo nadhiri.

a) Taja na ueleze habari za shairi hili?
   (alama 3)
b) Fafanua toni ya shairi hili.
   (alama 2)
c) Mtunzi wa shairi hili ana dhamira gani? (alama 2)
d) Onyesha jinsi mtunzi alivyotumia idhini ya kishairi.
   (alama 3)
e) Taja na ufafanue tamathali ya usemi iliyotawala katika shairi hili.
   (alama 2)
f) Menenew alibadilika vipi? Eleza. (alama 4)
g) Andika ubeti wa tisa kwa lugha tutumbi. (alama 4)

5. <u>Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali.</u> (alama 20)

Ajaye kisimani mbele, hunywa maji maenge,
Asinywe yalo na vunju,
Yakampa kigegezi
Yakamtibua roho akaona na kinyaa,
Awali ndio awali awali mbovu hamna.

Ikiwa utalimatia,
Utayaramba makombo,

Uvidata vitu cheche
Kisoma aali kikupe kisogo,
Inajuzu ujihimu
Mwanafuu darasani
Uraukapo bukrata
Katu hutayaramba makombo
Hutokosa kisebeho.

Dereva nawe utingo,
Natija ni asubuhi,
Wateja utawawahi,
Wasaa kuzingatia,
Uwafikishe kazini,
Kwa wasaa ufaao,
Wasije wakateteshwa na
Bosi wao nao wakuapize
Nawe mwanazaraa,
Mpini uukamate kabla,
Jua kutiririsha majasho jasadini,
Ushindwe kung'oa magugu,
Kutoka kwa lako konde.

Mhadimu mwenye zohali,
Yajuzu ujihimu
Maziwa ununue majogoo
Usije ukayadata na hivyo
Ukaandaa chai mkandaa
Wateja wakuambae mithili ya ibilisi.

Maswali

(a) Andika anwani mwafaka kwa shairi hili. (alama 1)
(b) Shairi hili ni la aina gani? Eleza. (alama 2)
(c) Eleza nasaha yoyote inayotolewa kwa wafanyakazi wowote watatu. (alama 3)
(d) Kwa mujibu wa mshairi, eleza dhamira ya shairi hili kwa mwanafunzi. (alama 2)
(e) Taja na utoe mifano ya mbinu zozote mbili za uandishi zilizotumika katika shairi hili. (alama 2)
(f) Taja sifa zozote mbili za kimuundo zilizotumiwa na msanii. (alama 2)
(g) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha nathari. (alama 4)
(h) Onyesha matumizi yoyote ya mishata. (alama 2)
(i) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika kwenye shairi. (alama 3)
(i) wakuapize
(ii) Mhadimu
(iii) ukayadata

SEHEMU YA D: HADITHI FUPI

Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine: ***Ken Walibora na Said A. Mohamed***

Jibu swali la 6 au 7.

6. "….. ukijifungua nitakusaidia kwa njia nyingi"
a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Tambua mbinu ya kisanaa iliyotumika katika dondoo hili. (alama 1)
c) Eleza tansia inayomkumba mnenaji wa maneno haya.
(alama 3)
d) Mwandishi wa hadithi hii ameonyesha kuwa damu ni nzito kuliko maji. Thibitisha.
(alama 12)

7. a) Mwandishi wa hadithi '*Shaka ya Mambo'* ameshughulikia kwa kina masuala mengi yanayohusiana na kazi.
Kwa kutolea mifano thabiti fafanua kauli hii.
(alama 10)

b) Kisengere-nyuma ni mbinu iliyoshamiri katika '*Damu Nyeusi'* kwa kutolea mifano mitano. Thibitisha. (alama 10)

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

8. a) Eleza dhana zifuatazo.
   i) Michezo ya chekechea
   ii) Vivugo
   iii) Kimai
   iv) Maapizo
   v) Simo (alama 10)

b) Fafanua majukumu matano ya Ngomezi. (alama 10)

WESTLANDS DISTRICT JOINT EXAMINATION
KISWAHILI
Karatasi – 102/1
Mwongozo wa Kusahihishia

1. **Muundo**
Zingatia lugha ya mtiririko.

i) Kujitambulisha
- Jina
- Kuzaliwa/Eneo/Kaunti nk.
- Malezi yake
- Elimu
- Msingi
- Sekondari
- Vyuo mbalimbali alivyosoma

ii) Tajiriba
- Kazi aliyofanya/alizofanya kabla ya kuwa Gavana.
- Siasa – kiwango/viwango gani?
- Anatajika kwa jambo/mambo gani.
  Mifano:
  - Elimu ya juu – shahada kadha.
  - Miradi ya maendeleo.
  - Ziara alizofanya.
  - Uwajibikaji wake/maadili kazini.
  - Falsafa yake ya maisha.
  - Malengo yake.
  - Changamoto alizozipitia.
  - Ruwaza/maazimio yake.

Lugha – Mtahiniwa atumie nafsi ya kwanza.
Usemi ya taarifa.
Lugha rasmi itumiwe.

2. **Hoja**
- Maadili yatazorota.
- Njia za mkato maishani.
- Uzembe kazini.
- Ukosefu wa uwajibikaji.
- Mapuuza.
- Kutothamini mitihani.
- Elimu kudorora.
- Kuathirika kwa taaluma mbalimbali.
- Utendakazi utaathirika.
- Nidhamu kutoweka.

3. **Mtenda mema kwa watu atendea nafsiye.**
Maana: Kuwafanyia wema watu ni sawa na kujiwekea akiba. Huenda nao wakakutendea wema utakapouhitaji.
Funzo: Usidhani unafanya kazi ya bure unapomfaa mtu Fulani.
Matumizi: Inaweza kuhimizwa anayefikiria kuwa wema uatendao ni wa bure na kuwa hatafaidika hata akiendelea.
Mtahiniwa aandike kisa kitakachodhihirika pande zote mbili.

4. **Maumbo ya kuzingatiwa.**
i) Kisa kinachofaa kuwa katika wakati uliopita.
ii) Mtahiniwa azingatie kumaliza kisa chake kwa maneno yote yaliyodokezwa.
iii) Mahali pa tukio patajwe.
iv) Baadhi ya matukio;
- Moto
- Wizi
- Ugaidi
- Baharini/majini

- Ajali barabarani

WESTLANDS DISTRICT JOINT EXAMINATION
KISWAHILI
Karatasi – 102/2
Mwongozo wa Kusahihishia

1. **Ufahamu**

a) Wanawakiwa/mateso ya wanawakiwa.**(al. 1)**

b) Ni watoto wanaohitaji kulelewa na kupewa mahitaji/matakwa ya kimsingi kama chakula, malazi, Elimu na mengine. **(al. 2)**

c) Aliyefiwa na mzazi mmoja au wote wawili. **(al. 2)**

d) (i) Laana
(ii) Urogi **(al. 2)**

e) (i) Kushikwa shokoa **(al. 1)**
(ii) Kutumiwa kama vyombo vya kuuzwa maanguroni. **(al. 1)**

f) (i) Hujifanya wana huruma mzazi anapokufa kasha kuwatesa hao wanawakiwa. **(al. 1½)**
(ii) Baadhi huwapeleka wanawakiwa ng'ambo ambako wanateswa. **(al. 1½)**

g) (i) Pamoja na mila. **(al. 1)**
(ii) Kazi ngumu. **(al. 1)**
(iii) Wakitumia mitego/ndoano/ndoana. **(al. 1)**

2) **Ufupisho (Majibu)**

(i) Sanaa ya Jadi kama njia ya mawasiliano.
(ii) Hupasha ujumbe na kuwasilisha hekima ya wakongwe kwa njia bunifu na inayoburudisha.
(iii) Imetumika tangu kale kwa ufanisi.
(iv) Haijapitwa na wakati.
(v) Hutumika sherehe zote za kiafrika.
(vi) Inaweza kutumika sambamba na njia za kisasa za mawasiliano.
(Hoja – al. 4, mtiririko –al. 1=Jumla 5)

b) (i) Sanaa ya Jadi ikitumika na njia za kisasa za mawasiliano ina manufaa mengi.
(ii) Hushirikisha watu wote bila kubagua kinyume na njia za kisasa ambazo zinachukuliwa kuwa za wale wenye nguvu ambao huzitumia kujifanikisha.
(iii) Huwatenga walio wengi kwa kuwa ni ghali.
(iv) Hutumia lugha ngeni na teknolojia inayokanganya.
(v) Hazitoi nafasi ya mwitiko au kuchangia maoni.
(vi) Njia ya sanaa ya Jadi haitumii teknolojia inayokakanganya.
(vii) Hutumia lugha inayoeleweka na wote na ambao si ghali.
(viii) Inapasha ujumbe anuai kwa watu wengi na muda mfupi.
(ix) Huburudisha Hunasa na kudumisha taharuki huku ikihimiza madhira kubadilika bila yeyote kuhisi amekosewa. **(Hoja – al. 8, mtiririko –al. 2=Jumla 10)**

3. a) /ng'/-king'ong'o/Nazali/kipua
-hutamkiwa katika kaakaa laini
- ni ghuna

b) Shadda – Ni mkazo katika kutamka silabi au sauti fulani ya neno ili neno liweze kuleta maana yake halisi. **(al. 1)**
Kiimbo – Ni kupanda na kushuka kwa sauti katika matamshi. **(al. 1)**

c) Jogoo akiwa chini ya banda aliwika na kusikika kote. **(al. 2)**

d) Vibuzi vilivigonga vijitu vilivyokuwa vikikimbia. **(al. 2)**

e) (i) Kundi la nomino lenye sifa zinazofanana kisarufi. **(al. 1)**

(ii)

K.m. nyanya	- I-ZI
	- A-WA
Maziwa	- LI-YA
	-YA-YA
	-LI-YA
Ua	- LI-YA
	-U-ZI
Kipepeo	-A-WA
	-KI-VI

n.k.

(Nomino yoyote moja=Alama 2)

f) Mwanafunzi akimpata atampa ujumbe.

g) kwa vile
kwa kuwa
kwa ajili ya
kwa sababu
kwa minajili

(Mfano wowote mmoja Alama 2)

h) Wote waliokuwa shuleni walituzwa zawadi tele. (Alama 4)

(Hakiki majibu ya wanafunzi)

i) Mkutano ulioahirishwa ulikusudia kuwapa washindi tuzo. (Alama 2)

j) Kidibwini ndimo mlimopatikana mbwa aliyepotelea mwituni. (Alama 2)

k)

wa	-li	-o	-m	-teremshi	-i	-a
nafsi ya tatu wingi	wakati uliopita		kirejeshi tendewa/ shamirisho	nafsi	mzizi	kiendezi kiishio

l) Kusisitiza

m) i) Kusisitiza sentensi ili kuongezea maneno ambayo ni ufafanuzi way ale yaliyotajwa awali.
Kwa mfano:
Vitabu vingi vya sarufi – vile vilivyoteuliwa ni vizuri.

ii) Kuonyesha mabadiliko ya ghafla katika utungaji wa sentensi/kukatizwa ghafla kwa wazo.

iii) Baada ya orodha tangulizi labda kuifafanua zaidi.

iv) Huonyesha kusisitishwa kwa wazo.

v) Kabla ya maneno ambayo ni msisitizo wa dhana iliyotajwa.

(Alama 2)

n) Kiti – kipozi
babu – kitondo
pesa – ala (Alama 3)

o) * Dada yao mrembo – kirai nomino.
* yao mrembo – kirai kivumishi/vumishi.
* kitausi mjni – kirai kielezi/elezi. (Alama 3)

p) Tegemezi:
Mama atakayechota maji…….
Mama akichota maji ……
Mama atakapochota maji…….
Mama angechota maji……..
(Mfano wowote 1=ala 1)
Huru: Mama anachota maji.
(Alama 1)

q) i) Stiri
ii) Tahini (Alama 2)

4. Isimu Jamii

a) Sajili ya vijana
(Alama 2)

b) i) Kuchanganya ndimi – message, tutadiscuss.
(Alama 2)

ii) Kuhamisha ndimi (kauli/sentensi kamili)

How are you?
Am ok. (Alama 2)

c) Lakabu – Jina la kupanga analopewa mtu au kujipa mwenyewe.
Km. maskini wa Mungu, Tinga nk.
(Alama 2)

Misimu – Maneno yanayobuniwa na kutumiwa na kikundi Fulani cha watu wakati Fulani na yanaweza kutoweka au yakaingizwa katika kamusi.
Km. matatu, nduru, ingia mitini n.k.
(Alama 2)

WESTLANDS DISTRICT JOINT EXAMINATION
KISWAHILI
Karatasi – 102/3
Mwongozo wa Kusahihishia

1. **Swali la lazima**
Timothy Arege: Mstahiki Meya

a) (i) Msemaji ni Daktari Siki.
(ii) Anamwambia Tatu, mmoja wa wawakilishi wa wafanyikazi.
(iii) Wako katika ofisi ya Daktari Siki.
(iv) Tatu amekuja kumsihi Daktari Siki aende aongee na Mstahiki Meya kama binamu yake kuhusu matatizo yanayoukabili umma na pengine huenda akasikiliza kilio chao. **(4 ×1=al.4)**

b) (i) **Msemo** – Msikate tama
Tashbihi – Mlango huenda ukasalimu amri. **(2 ×2=al.4)**

c) **Wafanyikzai wako karibu kukata tama kwa sababu:**
- Mishahara midogo isiyokidhi mahitaji yao.
- Kutolipwa mishahara kwa wakati ufaao.
- Ukosefu wa dawa hospitalini. Wananchi wanakufa ovyo huku madaktari na wauguzi wakitazama.
- Kupanda kwa gharama ya maisha.
- Unyonyaji. Viongozi kama Mstahiki Meya madiwani wanajiongezea mishahara na hawalipi kodi.
- Matabaka – Tabaka la viongozi linaishi maisha ya kifahari kwa kusomesha watoto wao nje ya nchi na kutibiwa nje ya nchi wakati walalahoi hawana hata pesa za kumudu lishe bora wala matibabu.
- Wizi wa mali ya umma.
- Ukosefu wa chakula bora. Wananchi wanakula mizizi na matunda ya mwituni na wengine wanapata magonjwa kama utapiamlo.
- Hali duni ya usafi wa mazingira.
- Meya kukataa kukutana na wafanyakazi na kuwasikiza.
- Kuvunjiliwa mbali kwa maandamano ya wafanyakazi.
- Kutolewa ahadi zisisotimizwa. **(Hoja zozote 8×1=al.8)**

d) Sifa za siki.
(i) Mwenye msimamo thabiti.
- Anaupinga utawala mbaya wa baraza la Cheneo.

(ii) Jasiri
- Anamkabili Meya na kumkosea waziwazi.

(iii) Mzalendo
- Anawatetea raia akiunga mkono mapinduzi yanayoendelezwa na wafanyikazi.

(iv) Mwenye bidii
- Anawashughulikia wagonjwa wote zahanitini.

(v) Mvumilivu
- Anavumilia kuona wagonjwa wakiteseka ilhali hana dawa za kuwasaidia na kumhimiza waridi aendelee kuwapa hao wagojwa matumaini.

(vi) Mshauri mzuri

- Alimpa Meya wasia mzuri lakini Meya akampuuzilia mbali na kumwona kama mchochezi.

(vii)Mwenye huruma

- Anamhudumia mamaye Dadavuo Kaole na kupuuza utaratibu wa foleni kama alivyoagiza Waridi.

(viii)Mwanamapinduzi

- Anawazindua wanacheneo kupigania haki zao.

(ix) Mtetezi wa haki. **(Hoja zozote 4×1=al.4)**

2. Kidagaa Kimemwozea

a) (i) Amani akiuambia umati.
(ii) Walikuwa kwenye Uwanja wa Nasaba Bora. Amani akiwa jukwaani.
(iii) Umati ulitaka Amani awe Mtemi baada ya mapinduzi Sokomoko. **(4 ×1=al.4)**

b) (i) Kipungu ni Mtemi Nasaba Bora.
(ii) Matuko Weye alimpinga Nasaba Bora katika sherehe ya siku kuu ya wazalendo.
(iii) Anamwita Nasaba mbaya mbovu.
(iv) Madhubuti aliandika waraka wa kupinga vitendo viovu vya Nasaba Bora.
(v) Madhubuti anajiita 'Madhubuti bin Zuhura' badala ya 'Madhubuti bin Nasaba Bora'
(vi) Bi Zuhura anapinga uongozi mbaya wa Mtemi kwa kumweleza wazi.
(vii)Lowela anamtisha Mtemi kuwa angefichua siri za Mtemi iwapo hangemwachilia Amani na Imani.
(viii)Amani anamshurutisha Mtemi kukiri maovu yake yote.
(ix) Oscar Kambona anamteka nyara Mtemi na kutaka kumwua kwa kuwanyang'anya shamba na kumwua
mamake.
(x) Mawazo ya kifo yalimwandama, akachimba kaburi lake, akajitia kitanzi.
(xi) Madhubuti alihamia kibandani kwa Amani na kuliacha jumba kubwa. **(Hoja zozote 8 ×1=al.8)**

c) **Umuhimu wa kipunga (Mtemi Nasaba Bora)**
(i) Kuonyesha kuwa uongozi mbaya haudumu.
(ii) Anawakilisha viongozi wanaotumia mamlaka kujinufaisha na kuwanyanyasa wengine.
(iii) Kielelezo cha viongozi wanaojihusisha katia mapenzi na wasichana wadogo.
(iv) Anawakilisha wanandoa wasio waaminifu.
(v) Yeye ni mkoloni mamboleo – msaliti mkubwa wa juhudi za uhuru.
(vi) Anaonyesha tama na ubinafsi.
(vii) Anaonyesha ukatili dhidi ya umma – kuchoma nyumba – kunyanganya mashamba na hata kuua.
(viii) Maovu yake yameibua ukakamavu wa madhubuti kumpinga, licha ya kuwa mwanaye.
(Hoja zozote 6 ×1=al.6)

d) (i) Jazanda/Istiari
Mifano: i) Kipungu – Mtemi Nasaba Bora
ii) Kumnyonyoa – kumpinga/kumwondoa mamlakani
iii) Niingie pahala pake – kuchukua uongozi. **(Mfano mmoja al.1=Jumla 2)**

3. Mchango wao.

a) Amani
(i) Aliongoza mapinduzi yaliyomng'oa Mtemi mamlakani.
(ii) Anapigania jamii yenye kuthamini maridhiano, mapatano na msamaha. Aliwasamehe waliomkosea k.m Mtemi Nasaba Bora na mwalimu majisifu.
(iii) Anathamini jamii inayowathamini wahasiriwa wake k.v. Matuko Weye – anampa kasiri la Majununi.
(iv) Anataka jamii inayofaulu kwa kutumia njia halali – hakufanyiwa mtihani kama fao.
(v) Anapenda jamii ya kukuza vipawa – ni mwandishi bora.
(vi) Anapenda jamii inayothamini Elimu – Watu wapate Elimu ya chuo na maisha.
(vii)Kielelezo cha vijana wanaojiheshimu – kutoshiriki mapenzi kiholela licha ya kuwa na fursa.
(viii)Kujitegemea maishani na kuthamini kazi – mchungaji bora! Mchungaji bora!
(ix) Kielelezo cha uvumilivu. → Mswada
Kuibiwa, ukachapishwa → kuishi
Kibandani
(x) Kielelezo cha huruma – alimpa DJ shati baada ya kaptura yake kutafunwa na fahali.
(xi) Ana bidii - kutafuta ukweli kuhusu Amu yake Yusufu na kifo cha Chichiri Hamadi.

- Katika kazi yake ya uchungaji

(xii)Ami yake Kananda – Kumtafutia kazi Kananda – kwa Mwatela.
(xiii)Mwanawe mbao, anamwazimia Kananda darudini kwa rafiki yake.

(xiv)Kananda kumsahehe mwanawe kwa kumuumiza. **(Hoja zozote 12×1=al.12)**

4. a) **Maswala yanayohusiana na kazi.**

(i) Uaminifu kazi – Esther – mwaminifu Grace na Kamata si mwaminifu – pesa za Mteja mzungu.
(ii) Kuna sheria kazini – Esther haruhusiwi kutumia rununu.
(iii) Bidii kazini – Esther.
(iv) Kuna vyeo kazini – Grace ni mkubwa wa Esther.
(v) Kuna kustaafu kazi – Babake Esther.
(vi) Zamu kazini – Esther alimshikia zamu Grace. Waliingia kazini kwa Zamu.
(vii)Swala la kazi kwa vijana – vijana wameenda mjini Nairobi kutafuta kazi – vigumu kupata.
(viii)Kazi ya kilimo – Baba yake Esther alifanya ukulima – Machakos miaka ya 1970's.
(ix) Kazi ya biashara – Mteja mzungu ni mwana biashara mzee mwingi anakodisha nyumba biashara ya matatu.
(x) Kazi inahitaji uvumilivu – Esther alivumilia akingojea kubadilishiwa zamu.
(xi) Usawa wa kijinsia – wote vijana wa kiume na kike wamepata kazi.
(xii)Kuwajibika kazini/kutowajibika. Grace na Kamata waliwacha kazi na kwenda raha zao.
(xiii)Kufanya kazi yenye malipo duni – yasiyoridhisha – Esther.
(xiv)Kazi ya usiku kwa msichana kama Esther? – Hali gumu. **(Hoja zozote 10×1=al.10)**

b) **Kisengere nyuma**

(i) Fikirini kukumbuka tuko la mkahawani uk. 24-25.
(ii) Anakumbuka baridi katika Afrika Mashariki.
(iii) Kuhusu ulevi wa Fikirini uk. 22.
(iv) Kuhusu kudhulumiwa na wahadhiri na wanafunzi chuoni.
(v) Kuhusu alivyopenda vyakula vya kiafrika uk. 24, 29)
(vi) Anakumbuka siku ya mama yake mzazi kufa uk. 29. **(Hoja zozote 5×2=al.10)**

5. a) i)**Michezo ya chekechea**

Michezo ya watoto ambapo wanaigiza shughuli au mambo wanayoyaona katika mazingira yao kama upishi, ukulima, arusi nk. **(alama 2)**

ii) **Vivugo**

Ni tungo za kujisifu au kujigamba. Anayejigamba huwa mwanasanaa (mshairi) anaelewa kwa undani analozungumzia. **(alama 2)**

iii) **Kimai**

- Nyimbo zinazohusishwa na shughuli za majini (mabaharia).
- Huhusishwa na maisha ya wavuvi, shughuli za uvuaji/uvuvi.

(alama 2)

iv) **Maapizo**

- Ni maombi maalumu ya kumtaka Mungu/miungu/mizimu kumwadhibu mhusika hasidi, mkinzani au mwovu.
- Maapizo ni dua ya laana au maombi mabaya kutoka kwa mtu ambaye anahisi ametendewa wovu.

(alama 2)

v) **Somo**

- Ni maneno ambayo sio rasmi yanayotumiwa katika lugha ya maongezi na kikundi Fulani cha jamii. Pia ni semi za kimafumbo huhusishwa na kikundi kidogo cha wanajamii.

(alama 2)

b) Majukumu ya ngomezi.

i) Kitambulisho cha jamii – ufundi wa jamii huonyeshwa kwa kutumia vyombo vya muziki. Ujumbe wa kuzaliwa kwa mtoto huweza kupitishwa kwa mapito tofauti ya ngoma.
ii) Nyenzo ya kukuza uzalendo – wanajamii hufunzwa kuionea fahari mbinu hii yao ya kuwasiliana.
iii) Hukuza ubunifu – wanajamii wanabuni mitindo mpya ya kuwasilisha ujumbe kwa ngoma, hivyo kuimarisha ubunifu.
iv) Njia rahisi ya kuwalisha ujumbe bila kutegemea sauti ya mtu.
v) Huhifadhi na kuendeleza utamaduni wa jamii kutoka kizazi hadi kingine.
vi) Ni nyenzo yakupisha ujumbe wa dharura kuhusu matukio ya dharura kama vile vita – yaani hutumiwa kutoa matangazo rasmi. **(Hoja zozote 5×2=al.10)**

KAUNTI YA THARAKA KUSINI
hati ya kuhitimu elimu ya sekondari kenya
KISWAHILI
KARATASI LA KWANZA

1. **LAZIMA**
   Wewe ni Mwalimu Mkuu. Mwandikie barua ya mapendekezo mwanafunzi wako anayanuia kujiunga na Chuo Kikuu nje ya nchi.

2. Ni hatua zipi zinahitaji kuchukuliwa ili kukubaliana na tisho la ukame nchini.

3. Mwenda juu kipungu hafikii mbinguni.

4. Malizia kwa

   …….Tangu siku hiyo niliamini kwamba ukuukuu wa kamba si upya wa ukambaa.

KAUNTI YA THARAKA KUSINI
hati ya kuhitimu elimu ya sekondari kenya
KISWAHILI
KARATASI LA PILI

1. **UFAHAMU** **(alama 15)**
   Soma taarifa inayofuata kasha uyajibu maswali

   Maisha ya binadamu ni kimoja kikubwa. Hebu jiulize jinsi uhai wako wewe mwenyewe ulivyoanza sembuse unavyoweza kupumua na kuishi siku nenda siku rudi.

   Dini zimefahamisha kuwa sisi binadamu tumeubwa na Mwenyaezi Muumba. Hata hivyo Muumba hutumia mume na mke kutuanzishia maisha yetu humu duniani. Uhai wa hapa duniani huanzia katika tumbo la mwanamke muda mfupi tu baada ya mume na mke kushirikiana katika tendo la kujamiina. Katika ngono hii yenye ufanisi, mbegu moja ya manii kutoka kwa mwanaume, hudunga na kujiingiza katika yai la mwanamke huku ikilirutubisha. Tangu hapo mtu huwa na mama akawa mjamzito. Hatua ya kwanza ya uhai?

   Wanayansi wametuthibitishia kuwa mbegu katika shahawa kutoka kwa mwanaume ina kromosomu ishirini na tatu nalo yai la mwanamke lina idadi iyo hiyo ya krosomomu. Basi katika hatua ya kwanza ya uhai wake, binadamu ana kromosomu arubaini ba sita, krosomomu hizo zote ndizo humfanya mtu kuwa mkamilifu kwa kukadiria mambo mbalimbali adhimu. Kwa mfano, hukadiria kama kiumbe kitakuwa cha kike au cha kiume, mtu mweupe au mtu mweusi, mwerevu au wa wakia chache, mwenye nywele za singa au za kipilipili, atakuwa na damu ya namna gani, michoro ya vidole vyake itakuwa vipi na hata utu wake utakuwa wa namna gani katika siku za usoni.

   Elimu yote anayopata mtu kutoka kwa jamii na mazingira huweza tu kujenga, juu ya yaliyokwisha kuanzilishwa na krosomomu katika yai lililorutubishwa tumboni.

   Haihalisi kabisa kufikiria kwamba katika hatua za mwanzo tumboni mwa mama kiumbe huwa katika hali ya ukupe. La hasha!yeye hujitegemea kwa vyovyote na ana upekee wake. Hatangamani na mama yake. Roho yake humdunda mwenyewe na damu yake ambayo huenda ikawa tofauti kabisa nay a mama yake, humtembea na kumpiga mishipani mwake. Isitoshe, yeye si mojawapo katika viungo vya mwili wa mama yake vinavyomdhibiti katika himaya yake ndogo.

Amini usiami, hapana binadamu hata mmoja ambaye amewahi kuwa sawa kimaumbile na mwingine na wala hatakuweko. Hata watoto pacha kutoka yai moja la mama hawawi sawa, lazima watatofautiana. Si nadra kusikia mtu amepata ajali akahitaji msaada wa damu, na pakosekane kabisa mtu hata mmoja kutoka jamaa yake wa kumwauni. Basi ukistaarajabu ya Musa utaona ya Firauni.

a) Andika anwani mwafaka ya taarifa uliyosoma. (alama 1)

b) Mwandishi ana maana gani anaposema 'ngono yenye ufanisi'? (alama 2)

c) Uchunguzi wa sayansi umekita mzizi imani gani ya kidini?
(alama 2)

d) Taja majukumu yoyote manne yanayotekelezwa na kromosomu.
(alama 4)

e) Katika makala, elimu kutoka kwa jamii na mazingira yaelekea kuwa bure ghali. Kwa nini?
(alama 2)

f) Eleza maana za maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika makala:
(alama 4)

i) Siku nenda siku rudi.

ii) Huwa katika hali ya ukupe

iii) Kumwauni

iv) Himaya

2. UFUPISHO

Soma taarifa ifuatayo kasha ujibu maswali uliyopewa

Kwa mujibu wa utafiti wa wanasayansi, binadamu ndiye kiumbe aliyepevuka zaidi katika fikra kuliko viumbe wengine. Anasemekana kuwashinda viumbe wengine kwa njia nyingi,hata kuweza kuwatala na kuwaratibia maisha yao. Binadamu amepewa uwezo wa kuyatawala mazingira na kukabidhiwa ufundi wa kuweza kuunda vifaa mbalimbali ili kuyakabili mazingira hayo. Uwezo huu ndio umemwezesha kukimu mahitaji ya kizazi kimoja hadi kingine kwa miaka na mikaka. Hata hivyo, kuna tofauti kubwa kati ya binadamu na wanyama. Tofauti hii inaweza kumvua binadamu sifa zake zote na kuuona ukwasi wa maarifa yake kama ishara ya maangamizi ya ulimwengu. Hii ni kutokana na hasara anayosababisha katika mazingira tulivu waliyoumbiwa viumbe wote na Muumba wao.

Lakini ifahamike kuwa mandhari ya ulimwengu tunamoishi humpendeza kila kiumbe, mathalan hewa safi itokayo miliamini, chemichemi za maji, mito na vijito mnamotiririka maji safi, vilele vya milima vilivyofunikwa kwa theluji daima dawamu, yakiwemo mabonde na tambarare zinazohimili uhai wa viumbe wengi.

Vilevile ibainike kuwa uzuri huu wa kiasili hauwezi kufikia kilele bila vichaka na misitu inayoipamba ardhi hii huku ikileta mvua. Mapambo yote haya ni kwa nguvu za maumbile; nguvu ambazo hazisababishwi na kuwa hatari kwa uhai wa binadamu na viumbe wenzake kwa sababu anayaharibu maumbile kwa kiasi kikubwa kinachomtisha binadamu mwenyewe.

Sababu mojawapo ni uchafuzi wa maji kama rasilmali muhimu ya kiasili. Uchafuzi huu umeathiri viumbe na mimea pakubwa, yakiwemo maradhi mbalimbali. Kwa kweli bila maji, uhai utatoweka duniani. Uharibifu mkubwa wa maji machafu yenye sumu hasa kutoka viwandani na kuingia kwenye mito na

bahari, huwadhuru viumbe wengine wenye makao majini. Maji huleta madhara sit u kwa mimea bali hata kwa binadamu kupitia kwa ulaji wa vyakula.

Binadamu ameharibu misitu kwa ukataji wa miti kihoela hasa kwenye sehemu za chemichemi. Hali hii husababisha uhaba wa mvua ambao huleta kiangazi kinachokausha mimea na visima vya maji.

Ujenzi wa viwanda hasa katika nchi zilizostawi unaelezwa na wanasayansi wanaohusika na hali za anga kuwa umesababisha taharuki na wasiwasi mwingi. Hii ni kwa sababu umeonyesha kuharibu utandu unaozuia miale ya jua kupenya moja kwa moja kwenye sayari hii na hapo kuhatarisha uhai. Hii ni kutokana na hewa chafu itokayo viwandani. Kadri binadamu anavyochangia pakubwa katika kuondoa polepole uhai wa viumbe wote ulimwenguni.

Warsha nyingi zimefanywa ili kutahadharisha ulimwengu dhidi ya uharibifu wa mazingira na maliasili. ‘Ajenda’ za mikutano hiyo hasa zinalenga nchi zilizostawi kwani hizi ndizo zinazochafua mazingira kwa kasi zaidi kuliko zile zinazostawi.

Mapendekezo mengi yametolewa katika vikao hivyo ili kusulihisha tatizo hili lakini ni hatua chache mno zinazochukuliwa kurekebisha mambo haya.

Itakuwa bora zaidi ikiwa watu watajipa jukumu la kusafisha mazingira yao. Watoto wafunzwe jinsi ya kuhifadhi mazingira yanapochafuliwa. Wakumbuke kuwa utumwa si karaha kwa sababu afya zetu na viumbe wengine zimo hatarini ikiwa mazingira yatachafuliwa. Kwa hivyo, ni jukumu la kila mmoja wetu kutunza mazingira anamoishi kwa manufaa ya leo na kesho. Viongozi wanaohudhuria kongomano la kila mwaka maarufu kama ‘KYOTO PROTOCAL’wahakikishe kuwa maazimio yote ya kulinda mazingira yametekelezwa, na sheria kali kuidhinishwa dhidi ya raia wao, la sivyo, siku zijazo kutakuwa na mafuriko mengi ambayo yatasababisha visiwa na sehemu zote za Pwani kufunikwa na maji.

a) Eleza kwa ufupi hasara zinazoweza kusababishwa na uharibifu wa mazingira. (Tumia maneno 45- 55) (alama 1 kwa mtiririko)
(alama 5)

b) Eleza hatua ambazo mwanadamu anapaswa kuchukua ili kupunguza madhara ya upanuzi wa viwanda. (Tumia maneno 45) (alama 1 kwa mtiririko)
(alama 6)

3. MATUMIZI YA LUGHA

a) Kimadende hutamkwa vipi? (alama 1)

b) Bainisha chagizo na shamirisho katika sentensi ifuatayo:
mjukuu alipasua kuni asubuhi
(alama 2)

c) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mstari:
Nyumba yao mpya itafunguliwa kesho jioni.
(alama 5)

d) Unda nomino moja moja kutoka na vitenzi vifuatavyo.

i) Dhulumu

ii) Tubu

e) Andika ukubwa wa:

i) Mfupa

ii) Mbwa

f) Tunga sentensi sahihi ukitumuia vitenzi **chwa** na **fa** katika kauli ya kutendewa. (alama 4)

g) Andika sentensi zifuatazo upya kulingana na maagizo uliyopewa. (alama 3)

i) Kati ya vitabu hivi vyote, Kiswahili murua ndicho kizuri zaidi cha kusoma.
(Anza: Kiswahili murua…….

ii) "kuna chai?" motto aliuliza. (malizia kwa…..chai)

iii) Nchi zinazoendelea hazina malighafi yoyote. (Anza : Malighafi …..)

h) Eleza matumizi ya '**kwa**' katika sentensi ifuatayo.
Moja kwa tano ya watu waliosafiri kwa gari la moshi walikula wali kwa mchuuzi. (alama 3)

i) Bainisha viambishi katika neon lifuatalo
Waliotuhanhaisha (alama 3)

j) Kanusha: (alama 1)
Upendapo sahani nyingineyo, nitakupoa.

k) Tunga sentensi kwa kutumia neon 'haraka' kama
Nomino
Kielezi

l) Andika umoja wa:

i) Majadala yayo hayo ndiyo yaliyotumiwa kukusanyia takataka.

ii) Amkeni mwimbe

m) Bainisha na uonyeshe aina za viwakilishi katika sentensi zifuatazo

i) Yule ataajiriwa kazi huko mjini

ii) Cha kuvunda hakina ubani

iii) Wanene watahojiwa

n) Andika sentensi zifuatazo upya ukitumia kirejeshi 'amba' (alama 2)

i) Nyoka aliyemuuma punda wangu ameuawa na wanakijiji waliofika kwa wingi.

ii) Mahali palipotayarishwa pamejaa waumini walitoka nchini kote.

o) Tunga sentensi moja moja ukitumia alama za kuafikisha zifuatazo. (alama 2)

i) Alama za dukuduku

ii) Mshangao

p) Akifisha. (alama 3)

Lo ni nini huyo anayeshambulia mwanangu jirani yangu aliuliza kwa hasira nyingi.

4. ISIMU JAMII

a) Fafanua sifa bainifu tano za sajili ya siasa. (alama 5)

b) Fafanua athari za matumizi ya 'sheng' nchini (alama 5)

KAUNTI NDOGO YA THARAKA KUSINI
hati ya kuhitimu elimu ya sekondari kenya
KISWAHILI
KARATASI LA TATU

1. **LAZIMA : SEHEMU YA A**
   USHAIRI

Kiatu umepasuka, mwenyeo ni masikini
Nakuona wararuka, ukanyagapo njiani
Hivyo ngozi kichunjuka, ‘takusaidia nani?
Uvawavyo miguuni,utazidi kutoboka.

Awali ulisifika, ulipotoka dukani
Mwenyeo aliudhika, upitapo matopeni
Rangi aliyokupaka, kwa leo ungepakwani?
Uvawavyo miguuni, utazidi kutoboka.

Urembo umekutoka, si kama vile zamani
Weupe ulimemeka, mwenyeo ‘kikuthamini
Sasa amefilisika, japo enenda kazini
Uvawavyo miguuni, utazidi kutoboka.

Yakaa umekenuka, wangaliapo usoni
Kama kwamba unacheka, una kicheko kinywani
Tena ulivyopanuka, bila shaka u ta’bani
Uvawavyo miguuni, utazidi kutoboka.

Vidole vinaoneka, vimekunyata humoni
Wayo unadhihirika, kwani soli mashakani
Wafanya nyingi dhihaka, upitapo sakafuni
Uvawavyo miguuni, utazidi kutoboka.

Kwa kweli utatoboka, jinsi hali ya Fulani
Kila unaponyanyuka, ana wewe miguuni
Miezi tele yapita, pasi kulipwa kipeni

Uvawavyo miguuni, utazidi kutoboka.

Mwenyeo yalimfika, kwanzia mwezi wa juni

'Ngawa kazini afika, tajiriye amhini

Hivo huwezi tunzika, kiatu cha mokasini

Uvawavyo miguuni, utazidi kutoboka.

Ijapo amekuchoka, hangekutupa pipani

Kwani unahitaji, kutembea ofisini

Tena inadhihirika, si mzaha si utani

Uvawavyo miguuni, utazidi kutoboka.

Takubidi kutumika, kutuliza wayoni

Kwani huwezi tunzika, wala kulipia deni

Tena umeshadunika, kupelekwa kwa rahani

Uvawavyo miguuni, kupelekwa kutoboka.

MASWALI

a) Ni anwani gani inayofaa shairi hili? (alama 1)

b) Taja na ueleze tamathali ya usemi iliyotumika katika ubeti wan ne wa shairi hili.
(alama 2)

c) Kwa kutoa mifano mitatu, onyesha jinsi **inkisari** ilivyotumika katika shairi hili.
(alama 3)

d) Taja bahari mbili zinazodhihirisha katika shairi hili. (alama 1)

e) Ni mambo gani yanayodhihirisha kwamba kiatu kimetokwa na uembo?
(alama 3)

f) Ni sababu gani zinazomfanya mwenye kiatu kuendelea kukitumia? (alama 2)

g) Huku ukitoa mifano mwafaka, taja mambo yanayoonyesha kwamba hili ni shairi la arudhi.
(alama 6)

h) Taja maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika shairi.
(alama 2)

i) Kenuka

ii) Rahani

SEHEMU YA B

RIWAYA:

<u>Kidagaa kimemwozea</u>; Ken Walibora

2. Fafanua matumizi ya majazi kama fani ukirejea riwaya la *Kidagaa kimemwozea*
(alama 20)

3. "....Mwenda juu kipungu hafikii mbinguni!..."

a) Eleza muktatha wa dondoo hili.
(alama 4)

b) Eleza ukweli wa dondoo ulilolisoma kwa mujibu wa riwaya *Kidagaa kimemwozea.* *.(alama 16)*

SEHEMU YA C

TAMTHILIA:

Msthaki Meya: Timothy M. Arege

4. .....Dawa tulizonazo ni pain killers tu!.....wawashie taa ya tumaini. Ganga ganga za mganga huleta tumaini.

a) Eleza muktadha wa dondoo hili.

b) Onyesha mbinu tatu zinazojitokeza katika dondoo hili.
(alama 6)

c) Kando na ukosefu wa dawa na matibabu mazuri, eleza matatizo mengine matano wanayokumbana nayo wanacheneo.
(alama 10)

5. Jadili jinsi maudhui yafutayo yanavyojitokeza katika tamthilia ya Mstahiki Meya.

i) Unafiki

ii) Umaskini

SEHEMU YA D:

HADITHI FUPI

<u>jibu swali la 6 au 7</u>

6. **<u>Damu Nyeusi na Hadithi nyingine</u> Ken Walibora na Said A. Mohamed**

a) Onyesha jinsi maudhui ya **utamaduni** yanavyojitokeza kwa mujibu wa hadithi ya *Mke wangu.*
(alama 10)

b) Eleza sifa za Mhusika Aziza katika hadithi hii.
(alama 10)

7. **Ndoa ya samani**

a) "Fahami twe'zetu nyumbani"

i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

ii) Fafanua sifa zozote nne za msemaji wa dondoo hili.
(alama4)

b) Fafanua dhana ya fadhaa iliyobainishwa katika hadithi hii. (alama 2)

c) Dhihirisha maana ya 'Kanda la usufi' kwa kurejelea hadithi **kanda la usufi** ya Rhoda Nyaga.
(alama 10)

SEHEMU YA E:
FASIHI SIMULIZI

8. a) Eleza maana ya Fasihi Simulizi.
(alama 2)

b) Eleza matatizo matano yanayokabili fasihi simulizi katika jamii ya sasa.
(alama 10)

c) Tofautisha vipera vifuatavyo vya fasihi simulizi
(alama 4)

i) Maghani na mighani

ii) Ngoma na ngomezi

d) Taja sifa nne za mwigizaji bora.
(alama 4)

KAUNTI NDOGO YA THARAKA KUSINI
KISWAHILI
KARATASI 1

MWONGOZO

1. Lazima

- Barua hii iwe na anwani tu:
  Anayeandika
  Jina la shule
  S.L.P
- pawe na tarehe chini ya anwani
- upande wa atakayeipokea iwe ni : kwa anayehusika
- mint: itaje majina na nambari ya usajili ya unayependekezea
- piga mstari chini ya mintarafu
- maudhui- eleza wasifu kuhusu huyo mwanafunzi, masomo, utendakazi n.k. sifa ziwe nzuri ili apate nafasi
- tamati- ichukue muundo wa barua rasmi
- akifisha
- andika cheo cha aliyeandika mapendekezo
- utangulizi- ianze kwa ujumbe mkuu ulio kwenye mada ya barua

2. Ukame ni hali ya nchi kuwa kavu kiasi cha kutowezesha kupata mavuno ya kutosha
Hatua
- Kunyunyuzia mashamba maji hasa sehemu kame

- Kupanda miti ili kisaidia kuvutia mvua
- Kuhifadhi miti ili kuzuia mmomonyoko wa udongo
- Kutolima kandokando ya mito ili kuhifadhi chemichemi za maji
- Viwanda vinavyotoa kemikali zinazochangia kuharibika kwa hewa kuwekewa sheria za kufuata
- Kutochoma makaa
- Kupunguza idadi kubwa ya mifugo wanaolishwa katika maeneo mbalimbali nchini
- Adhabu ya kisheria kupatiwa wanaoharibu mazingira kama vile kukata miti na kuchoma makaa

3. Mwenda juu kipungu hafiki mbinguni
- insha ya methali
- kichwa kinaweza kunukuu methali nzima
- maelezo ya methali si lazima yatolewe
- kisa kiwe na maudhui ya kudhihirisha maana ya methali
- kisa kitiririke na kuwa na mwanzo, upeo na mwisho

4. Insha ya kumalizia, mtahiniwa ajieleze kwa kutungia kisa kinachosimulia kuwa kitu kipya duni na kinachovutia si kizuri kuliko cha zamani chenye kukufaa.
- malizia kwa maneno uliyopewa bila kuongeza chochote/ (neno) la kibinafsi lolote
- asianze kwa kifungu alochopewa- akifanya hivyo amejitungia swali

KAUNTI NDOGO YA THARAKA KUSINI
KISWAHILI
KARATASI 2
MWONGOZO

1. UFAHAMU

a) Mwanzo wa uhai wa binadamu/ uhai unavyoanza/ maisha ya binadamu n.k

b) Ambapo mimba hutungwa

c) Kwamba Mungu huwatumiia mume na mke kumwanzishia binadamu maisha ya duniani

d) Kromosomu humkadiria binadamu:

Jinsia yake
Aina ya nywele
Rangi ya ngozi yake
Kiasi cha werevu
Aina ya damu
Utu wake

e) Elimu kutoka kwa jamii na mazingira haifai kitu ila tu inajenga tu juu ya yaliyakwisha kuanzilishwa na kromosomu

f) i) kila wakati/ wakati wote
ii) kunyonya au kutegemea
iii) kumnusuru/ kumpa msaada au kumsaidia
iv)mamlaka au ulinzi wa sehemu/ eneo Fulani

2. a)

- huwadhuru/ kuwaua viumbe vya majini
- huleta madhara kwa mimea na binadamu
- kiangazi hukausha mimea na visima vya maji
- husababisha uhaba wa mvua
- maafa kwa mimea na viumbe
- huleta maradhi
- huleta kifo
- husababisha uharibifu wa utandu

b)

- zuia hewa yenye sumu kutoka viwandani
- zuia gesi hatari kusambaa
- kusafisha maji yatokayo viwandani
- elimisha watoto wahifadhi mazingira yao
- watu binafsi kusafisha mazingira
- tahadharisha umma dhidi ya uharibifu wa mazingira na mali asili

3.

a) /r/ hutamkwa kwa ncha ya ulimi Kupigapiga ufizi wakati hewa inaachiliwa Kutoka kinywani. Inaleta uradidi\

b) Chagizo- asubuhi

Shamirisho- kuni

c) Nyumba yao mpya itafunguliwa kesho jioni

S- KN ½ + KT ½

KN- N ½ + KV ½

N- Nyumba

V- yao

V- mpya

KT- T ½ + KE ½

T- itafunguliwa

KE- E ½ + KE ½

E- kesho

E- jioni

d) i) dhuluma -1

dhalimu

udhalimu

ii) toba

e) i) mfupa- fupa/ jifupa

ii) mbwa- jibwa

f) kutendewa- chwewa

kutendewa- fiwa

sentensi zidhihirishe hali ya kutendewa kila sentensi sahihi alama moja moja

g) i) Kiswahili murua ndicho kitabu kizuri cha kusoma kati ya hivi vyote

ii) mtoto aliuliza kama kulikuwa na chai

iii) malighafi hazipatikani kamwe katika nchi zinazoendelea

h) i) kwa I- ulinganifu wa idadi

kwa II- kitamizi

kwa III- pamoja na

i) wa-li-o-tu-hangai-sh-a

j) upendapo sahani nyingineyo, sitakupa

k) i) <u>Haraka</u> haina Baraka

ii) alitembea <u>haraka\</u>

l) i) jalala lilo hilo ndilo lililotumiwa kukusanyia takataka

ii) amka uimbe

m) yule-W- kionyeshi

cha- W- unganifu

wanene- W- sifa

n) i) nyoka ambaye alimuuma punda wangu ameuawa na wanakijiji ambao walifika kwa wingi.

iii) waumini ambao walotoka nchini kote

o) i) sentensi ionyeshe- maongezi yanaendelea ingawa maneno hayajaandikwa

ii) kuna maneno yaliyochwa mwanzoni '.....sikuweza kumsihi"

kutokuwa na maneno katikati ya usemi

Mf. Nyinyi....ila mimi sitaadhibiwa

iii) Mshangao

zionyeshe hisi mbalimbali

p) "Lo! Ni nani huyo anayeshambulia mwanangu?"

Jirani yangu aliuliza kwa hasira nyingi

4. **ISIMU JAMII**

a) Sifa bainifu za sajili ya siasa

i) Imejaa propaganda k.v. Fulani ni muaji (bila idhibati)

ii) Ina ucheshi mwingi k.v. rais na mpira aingize bao

iii) Lugha imejaa mafumbo. Yaani ni fiche k.v. ina vitendawili vinategwa

iv) Istilahi maalum k.v kura, mgombea

v) Lugha shawishi inayovutia wafuasi wengi k.v tafadhali nawasihi mnipigie kura

vi) Ina chuku k.v ahadi nyingi zisizoweza kutimizwa zote

vii) Mjadala uwepo wakati mwingine

b)

- anashindwa kuzungumza lugha sanifu katika mazingira rasmi inapomlazimu
- huchangia ufunzwaji mbovu wa lugha husika kwa wazungumzaji wageni
- huwa vigumu kujifuinza lugha sanifu kwa mzungumzaji wa 'sheng'
- kuna mkanganyo na mgongano miongoni mwa sheng za maeneo tofauti tofauti kwani haina msingi (haijasanifishwa)
- watoto wachanga wanapotangulizwa kwayo hupata athari ya kudumu katika uzungumzaji wa lugha maishani mwao

- huchangia makosa ya sarufi na tahajia katika maandishi

KAUNTI NDOGO YA THARAKA KUSINI
KISWAHILI
KARATASI 3
MWONGOZO

1. USHAIRI
   a) Kiatu

   b) Tashihisi/ uhuishi- usoni
      -umekeuka
   ii) tashbihi- kama kwamba unacheka
   iii) tabaini- unacheka- utabani

   c) Inkisari- 'takusaidia
      'kikuthamini
      'takubidi
      'tabani

   d) Mathnawi- pande mbili
      tarbia- mishororo mine

   e) Kiatu kupasuka
      Ngozi imechunjuka
      kutoboka
      kupanuka

   f) Hana kiatu kingine
   halipwi mshahara
   umaskini

   g) Kuna kibwagizo

      Kuna vitu vya kati 'ka' na vya mwisho

      "ni"

      Ka ni

      Ka ni

      Ni ka

      -shairi limegawika katika vipande viwili ukwapi na utao

      -kuna mishororo mine kwa kila ubeti

      -shairi lina mizani 8, 8 jumla 16 katika kila mshororo wa kila ubeti

      -vina vinatiririka

      h) Kenuka- furahi/ tabasamu

         Rahani- kwenye starehe

2. RIWAYA

   Majazi ni mbinu ya uandishi ya kutumia majina ya mahali au watu yanayoona na hali au tabia Fulani

a) Mashaka- dhiki ya moyo (wasiwasi) maisha yake ni ya dhiki baada ya kuanza mahusiano ya kimapenzi na Ben Bella akiwa bado mwanafunzi. Alipoachwa akawa mwenda wazimu

b) Majisifu- sifa alisifika kwa usanii wa mashairi, nyimbo za taarabu na riwaya ya Kidagaa

Kimemwozea hadi nje ya nche

c) Imani- itikadi ya kitu au pia kuwa mwema. Alikuwa na imani ndiyo sababu akayanywa maji yam to Kiberenge akawa na mtazamo tofauti kuhusu viwete na kuwaonea huruma

d) Amani- hali ya utulivu ingawa alipigania haki, popote alipoenda alipenda utulivu. Hakumwandhibu mwizi wa mswada wake bali alimsamehe

e) Maozi- macho alishuhudia kwa macho yake pamoja na mkewe wanao wakipotoka kimaisha- Lowela na Bella

f) Matuko Weye- kituko ni kioja. Alikuwa mzee mwendawazimu na mwenye vituko ya ajabu kama vile alipokuwa gerezani

g) Ulitima- umaskini au ukata. Amani alitoka sehemu yenye ukata kwa vile hakuwa na chakula, fedha wala nguo. Alitembea kwa miguu hadi Sokomoko

h) Baraka- neema au rehema. Eneo hili lilipata neema ya kuwa na vijana bora sana. Hawa ni pamoja na Chwechwe Makweche na Imani

i) Songoa- kuminya au kukamua kitu. Wananchi wa mji mkuu wa Tomoko ambao ulikuwa Songoa walinyanyaswa vibaya, kufungwa jela bila hatia k.v Yusuf, Amani Chirchir

3.

i) Mawazo ya Amani, akiwazia kuhusu madhubuti wakiwa kwake (kibandani cha Amani) wakati madhubuti aonyesha uasi wake kwa babake.

ii) Ukweli wa mwenda juu kipungu hafikii mbinguni

- Mtemi Nasaba Bora kunyakua mashamba ya watu mwishowe kajitia kitanzi
- Mashaka alimwona Matuko Weye kama mwenda wazimu asiyestahili kuhudhuria sherehe za uzalendo- baadaye Mashaka akawa mwehu
- Mashaka kutania watoto walemevu wa mjombake mashaka pia akawa mwenda wazimu
- Mwalimu Majisifu alitarajiwa kusomea ukasisi ng'ambo lakini alikaidi alipofika huko
- Chwechwe makweche aligura kwao nyumbani bila kurudi na akawa bingwa wa soka lakini baadaye alivunjia fupdaktari aja na kusahaulika
- Chirchir Hamadi- msomi na aliyenunua shamba la Majinui aliuliwa na mtemi na hakuishi shamba alilonunua
- Wazalendo na mashujaa kama Matuko weye na Chwechwe Makweche hawakushughulikiwa n aserikali
- Mwalimu Majisifu alinunua vitu vingi vya starehe nyumbani lakini watoto wake walemavu hawakufahamu kama vipo, majisifu alishinda ulevini pasi kuvitumia.

4. **Mstahiki Meya**

a) Dkt Siki akimwambia Waridi walikuwa zahatini ya Cheneo. Baada ya Siki kuagiza Dadavuo kaole alazwe hospitalini

b) i) Methali- ganga anga za mganga huleta tumaini

ii) Kuchanganya ndimi- pain killers

iii) Msemo- wawashie taa ya matumaini

c)

i) Njaa

ii) Elimu duni

iii) Uongozi mbaya

iv) Mishahara duni

v) Kucheleweshwa kwa mishahara

vi) Maji machafu

vii) Kodi juu

viii) Ukosefu wa lishe bora

ix) Ukosefu wa vifaa vya kazi

5. **TAMTHILIA**

Unafiki

-meya kudai anajali masilahi ya wanacheneo

-Bili kujifanya kama rafiki wa dhati wa Meya anamwacha alipomhitaji zaidi

-mhubiri kudai anafanya kazi ya Mungu anapokea hongo

-Meya kupuuza wosia wa Siki ambao ungemsaidia

-Meya kujifanya amejazwa na roho wa mungu

Umaskini

- Ukosefu wa dawa zahanatini
- Wanacheneo kushindwa kugharamia dawa za matibabu
- Vifo kutokana na ulaji wa uporo usiochemshwa
- Uchafu uliorudikana
- Mishahara duni
- Ukosefu wa maji safi ya kunywa
- Ukosefu wa lishe bora

6. **HADITHI FUPI**

Damu Nyeusi

a)

i) Aziza anashikilia ukale kwa kutembea bila viatu na kupuuzilia mbali vitu vya kisasa

ii) Wazazi kuwachagulia na kuwapendekezea watoto wao wachumba

iii) Wasichana hawapaswi kutembea ovyo ovyo na wavulana wakionekana na watu

iv) Wanawake kuamini kuwa wanawake waliosoma hawafai kuwa bibi wazuri

v) Aziza kuamini kuwa ni jukumu la mke kufanya shughuli zote za nyumbani na sio kufanyiwa na watumishi

b) sifa za Aziza

i) Mshauri

ii) Mtamaduni

iii) Mzinduzi

iv) Mwerevu

v) Jasiri

vi) Mtambuzi

vii) Mkweli

7. a) i) Msemaji ni msimulizi/ Abu anamwambia kakake mdogo wakiwa kwa kina Amali wakati alikataa kumwoa

ii) sifa za Abu

a) mwenye bidii

b) mkarimu/ mwenye utu

c) mwenye kuweka kumbukumbu

d) ana msimano dhabiti

e) mwenye kulipiza kisasi

f) ana mwelekeo mzuri

b) Alikuwa na fadhaa ya kulipiza kisasi ili kutuliza kilio chake. Kwake, Amali hakuoa Abu bali alioa Samani-

utu- ndio muhimi zaidi kuliko fedha

kanda la usufi

- Sela anapojihusisha katika mapenzi na Masazu anapata mimba. Masazu anamlaumu Sela kwa kutojikinga swala lakujikinga ni la wawili lakini hapa ni mzigo Sela
- Masazu anamwacha Sela kubeba mimba kukatizwa masomo, kulaumiwa na kujifungua kwake masazu mimba ni kanda la usufi
- Babake sela analaumu mamake walimu baada ya sela kugundulika ana mimba. Majukumu ya walimu ya kusomesha na kushairi ni kanda la usafi kwa mzee Butali.
- Mzigo wa kukimu familia ni ya baba. Sela anapojiunga na masazu Dafina hafanyi kazi kukimu familia ni kanda la usufi kwa sela
- Sela anachia Rozina na mamake kazi ya kulea kadogo. Kwa sela ulezi wa Kadogo ni kanda la usufi
- Wazee wanamwita mzee Butali ‘pangu pakavu’ anapojikaza kulipa karo ya shule ya Sale- kwao ada ya shule ni kanda la usufi

8. **FASIHI SIMULIZI**

a) Fasihi simulizi ni kazi ya kisanaa inayotumia lugha yam domo au mazungumzo katika uwasilishaji wake kutoka kizazi kimoja hadi kingine

b) Matatizo yanayokabili fasihi simulizi

i. Ukosefu wa utafiti madhubuti

ii. Ukosefu wa walimu wanaoielewa

iii. Ukosefu wa vitabu vya kurejelea

iv. Mtazamo asi kuwa haina manufaa ya kuelimisha watu

v. Baadhi ya vipera ni kinyume cha maadili ya kidini

vi. Baadhi ya vijana wa sasa hawaonei fasihi hii fahari

vii. Kukosa fanani atakayeifanya iwe hai zaidi

viii. Mabadiliko ya jamii kuzingatia mazingira na wakati

c

i. Mighani- hadithi ya kishujaa ambazo zinahusu wahusika wa kihistoria na wanaoaminiwa kuwa waliishi katika jamii husika

ii. Maghani- tungo zinazotolewa kwa kughanwa/ nusu kuimbwa nusu kukaririrwa, zinazoweza kuambatanisha na ala za muziki au kughanwa na mdomo tu

iii. Ngoma- kipera cha maigizo kinachoashiria kupigwa kwa ngoma/ ala kwa ajili ya burudani au kulenga muktadha

iv. Ngomezi- fasihi inayotumia ngoma kuwasilisha ujumbe

d

i. Ajipambe kutegemea kinachoigizwa

ii. Mcheshi wa kuburudisha watazamaji

iii. Awe mfaraguzi

iv. Apaaze sauti ili asikike vizuri

v. Mkwasi wa lugha awe na ufasaha wa lugha

vi. Jasiri mbele ya watu

vii. Aelewe utamaduni wa hidhira yake

MTIHANI WA MWIGO WA WILAYA YA MURANG'A KUSINI KIDATO CHA NNE 2015

102/1
Kiswahili
Karatasi 1
(Insha)
JULAI / AUGOST 2015
Muda: Saa $1\frac{3}{4}$

1. Lazima.
   Andika barua kwa mhariri wa gazeti la Tomoko Leo ukitoa maoni kuhusu sekta ya usafiri wa pikipiki.
2. Mwiba wa kujichoma hauambiwi pole.
3. Viongozi walioko wapaswa watimuliwe mamlakani na wachaguliwe wengine. Jadili.
4. Andika kisa kitakachomalizika kwa maneno haya;
   ... Nilikula yamini kamwe sitawahi kujihusisha na mzaha tena.

MTIHANI WA MWIGO WA WILAYA YA MURANG'A KUSINI KIDATO CHA NNE 2015

102/2
KISWAHILI
KARATASI 2
(Ufahamu, Ufupisho, Sarufi na Isimu Jamii)
JULAI / AUGOST 2015
MUDA: $2\frac{1}{2}$

1. **UFAHAMU**.(alama 15)
   Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yafuatayo.

   Vitabu vingi vya hadithi za watoto vilivyowahi kuandikwa katika lugha ya Kiswahili kufikia sasa vinaweza tu kukidhi mahitaji ya wanafunzi wa darasa la nne hadi la nane na hivyo basi kuacha ombwe pale panapostahili kuwekewa msingi imara - shule ya chekechea hadi darasa la tatu. utafiti uliowahi kufanywa na wanaisimu-saikolojia unathibitisha kwamba uwezo wa mwanafunzi wa kujifunza lugha ya pili huwa katika kiwango cha juu awapo na umri mdogo na kwamba uwezo huo huanza kupungua kadiri umri unavyoongezeka na kufikia kipindi maalum (critical period) ambacho hukisiwa kubisha katika umri wa kubaleghe au kuvunja ungo.

   Hivyo basi, ili kustawisha hulka ya usomaji ya kudumu, waandishi wa fasihi ya watoto wanapaswa kujifahamisha mengi kuhusu ukuaji wa watoto hao wadogo na mikakati ambayo huitumia katika kujifunza lugha ya pili.

   Aidha, wanapaswa kuyafahamu yale yanayowapendeza na kuwachochea katika kusoma ili kuyajumuisha katika vitabu vyao vya hadithi. Mambo haya yatatimia iwapo waandishi hao watakuwa na mafunzo ya kimsingi katika taaluma ya isimusaikolojia.

   Wanafunzi katika viwango tofauti wana mikakati tofauti ya kujifunza lugha ya Kiswahili. Kufikiria kwamba wanafunzi wa madarasa ya chini (darasa la kwanza, pili na tatu) wanaweza kuitumia mikakati sawa na ile ambayo hutumiwa na wenzao wa madarasa ya juu kujifunza Kiswahili si sahihi.

   Watoto wadogo hujifunza mambo mengi kwa kukariri, kuigiza, kuiga, kufuatilia hadithi kwa picha miongoni mwa mbinu nyingine. Ili kufanikiwa katika kuwaandikia, sharti mikakati hiyo ya ujifunzaji izingatiwe.

   Ufundi mkubwa unahitajika si tu katika kuziunda sentensi zao bali pia katika kuifinyanga sarufi. Sentensi zenyewe ziwe fupi, zenye sarufi na msamiati sahili, zilizorudiwarudiwa ili kuzifanya zinate akilini na kuendelezwa kwa mtindo wa nyombo au mashairi mepesi.

   Watoto wadogo huvutiwa sana na nyimbo na mashairi mepesi na hujifunza kwa urahisi kupitia kwayo. Msururu wa vitabu vya 'Someni kwa Furaha' uliotumiwa katika miaka ya themanini na mwanzomwanzo wa miaka ya tisini ni mfano wa vitabu vilivyotekeleza dhima muhimu sana katika kuumua na kuchochea hamu ya wanafunzi kupenda kukisoma Kiswahili.

   Vitabu hivyo vilitumia mbinu mbalimbali zilizoweza kuyateka mawazo ya wanafunzi katika viwango tofauti. Miongoni mwa mbinu hizo ni matumizi ya vibonzo, mashairi na nyimbo za chekechea zenye

maudhui ambayo watoto wangeweza kujinasibisha nayo. Baadhi ya nyimbo hizo zilihimiza umuhimu wa kusomea katika mazingira safi, ushirikiano katika shughuli mbalimbali na umuhimu wa kuyachangamkia masomo. Mfano mzuri ni huu wimbo unaopatikana katika kimojawapo cha vitabu katika msururu huo: *Chawa chawa mchafu, petu ni pakavu Kata nyika utosini, kata nywele kwa mashine Kichwa safi kama nini? Chawa chawa mchafu, petu ni pakavu.*

Mbinu nyingine iliyotumiwa sana katika vitabu hivyo ni matumizi ya picha na vibonzo. Vitabu vya watoto vinapaswa kuwa na picha nyingi au vibonzo vingi kuliko maandishi. Picha na vibonzo vyenyewe viwe vya rangi kwa sababu watoto huvutiwa sana na rangi.

Waandishi wa fasihi ya watoto katika Kiingereza wamefanikiwa pakubwa katika kukumbatia mbinu hii na hivyo basi kuyakidhi mahitaji ya rika tulilolitaja kwa kuandika vitabu ambavyo vimechangia kwa akali kubwa katika kustawisha hulka ya usomaji kuanzia shule ya chekechea hadi darasa la nane. Hali hii ni tofauti na Kiswahili ambapo hulka ya usomaji bado ingali changamoto kubwa kwani huanza kuwekewa msingi katika darasa la nne.

Kiini hasa cha kuendelea kuwepo kwa mielekeo hasi na matokeo mabaya katika somo la Kiswahili ni kule kukosekana kwa vitabu faafu vya hadithi za watoto katika madarasa ya chini vinavyoweza kusaidia katika kujenga hulka ya usomaji mapema iwezekanavyo.

Ombwe hilo linaweza kufidiwa tu iwapo waandishi wataibuka na vitabu ambavyo vitayakidhi mahitaji ya watoto hao wadogo na kuwapa ari ya kukipenda Kiswahili kuanzia umri wa chini.

Maswali.

1. Kipe kifungu anwani mwafaka.
(alama 1)
2. Ni katika umri gani mwanafunzi hujifunza lugha ya pilikwa kwa urahisi?
(alama 1)
3. Waandishi wa vitabu vya watoto watastawisha usomaji wa kudumu kwa njia gani?
(alama 4)
4. Taja dhana potovu kuhusiana na ujifunzaji lugha kwa watoto.
(alama 2)
5. Onyesha njia ambazo kwazo watoto hujifunza kwa wepesi. (alama 3)
6. Vitabu vya watoto vinapendekezwa viwe na sifa gani?
(alama 2)
7. Eleza maana ya msamiati huu kulingana na muktadha wa matumizi.
(alama 2)

(a) Ombwe
(b) Kufidiwa

2. **UFUPISHO (alama 15)**

Watu wengine hawawezi kunywa chai au uji bila kutia sukari. Wanatumia sukari kwa hamu na ghamu bila kutambua kuwa hiyo ni sumu wanayojiongezea mwilini.

Ni ukweli usiopingika kuwa wazee wa jadi waliishi muda mrefu wakiwa na siha njema kuliko sisi. Hii ni kwa kuwa waliishi katika kipindi ambacho sukari inayotengenezwa viwandani haikuweko. Iwapo ilikuweko, ilikuwa bidhaa ya wateule waungwana kutengenezea vitu kama keki, mahamri, vitumbua na kadhalika na akina yakhe hawangeweza kuigharamia.

Watafiti wa masuala ya afya wamegundua kuwa sukari inayotayarishwa viwandani sasa haina virutubishi vyovyote. Halikadhalika, utaratibu wa viwandani wa kutayarisha sukari ili iwe nyeupe na kuichuja huharibu virutubishi vinavyoweza kuwa muhimu mwilini. Umuhimu wa sukari wakausaza kwa kutia ladha tamu tu. Umuhimu huu hauwezi kulinganishwa na madhara yanayoletwa na sukari hii. Baada ya kusagika mwilini, sukari hii huacha masalio ya asidi mwilini yenye sumu inayoathiri siha.

Matumizi ya sukari kwa wingi husababisha madhara mbalimbali mwilini. Kwanza, huchangia kuoza na kuharibika kwa meno pamoja na matatizo ya meno kuuma. Pili, sukari nyeupe imehusiwa na ongezeko la madhara ya kisukari, moyo na hipoglisimia au upungufu wa sukari mwilini. Matumizi holela ya sukari huleta kipandauso au ugonjwa wa gahfla wa kuumwa upande mmoja wa kichwa unaoambatana na kichefuchefu, kutapika na matatizo ya kuona. Pia sukari huleta maradhi ya ngozi na figo, pamoja na ongezeko la kemikali iitwayo kolestroli, ambayo ni ufuta unaonata na ambao unatokana na kutoyeyuka kwa mafuta yote mwilini. Kemikali hii ya kolestroli inaporundikana moyoni, hufanya mishipa inayotoa damu moyoni na kuisambaza mwilini kuwa myembamba na sugu. Moyo hulazimika kusukuma damu kwa nguvu na huenda moyo ukachoka na kukoma kufanya kazi.

Madhara haya ya sukari ndiyo yanayowafanya watu wengi kukiri kuwa sukari, ingawa ni tamu, ni

sumu mwilini. Wataalamu wa lishe wamependekeza ulaji wa vyakula kama nafaka, matunda, mboga na miwa ambavyo vimejaa sukari asilia. Fauka ya hayo, sukari inayotoka katika asali ni bora zaidi kwa mwili wa mwanadamu. Asali huwa na sukari asilia, vitamini, madini na amino asidi. Hivi vyote huwa na manufaa mbalimbali mwilini. Mathalani, asali huupa mwili nishati inayohitajika kuendesha shughuli za viungo. Licha ya hayo, asali huuchangamsha mwili. Asali huwa na kemikali ambazo husaidia watoto kukua vizuri. Huweza kuzidisha kiwango cha himoglobini, hivyo kupunguza uwezekano wa watoto kuwa na anemia (upungufu wa damu). Halikadhalika asali husaidia katika usagaji wa chakula iwapo itatumiwa kabla ya mlo. Matumizi ya kijiko kimoja cha asali kila siku husaidia mwili kujikinga dhidi ya magonjwa ya kukohoa. Asali husaidia pia kuondoa harufu mbaya kinywani.
Asali pia inaweza kutumiwa kujipaka. Inapotumiwa kwa njia hii, hutunza ngozi na kuifanya ing'are huondoa vipele na ugumu wa ngozi, pamoja na kutibu kule ngozi ilikokatikakatika. Halikadhalika, asali hutibu vidonda. Viwanda vingi vya vipodozi vilevile hutumia asali kama malighafi muhimu katika utengenezaji wa bidhaa hizo.

Maswali.

(a) Kwa kurejelea aya ya tatu na ya nne, dondoa mawazo yote muhimu.
(Tumia maneno 90) (al 7, 1 Utiririko)

(b) Fupisha aya ya tano na sita kwa kutumia maneno 70. (al 6, 1 Utiririko)

4. **SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA.** (alama 4)

(a) Yakinisha sentensi hii.
(alama 2)
Yeye siye asiyejua kwetu.

(b) Tenga mofimu katika neno hili.
(alama 2)
Watembeavyo.

(c) Eleza maana ya sentensi ambatano kisha utolee mfano.
(alama 2)

(d) Andika neno lenye sauti moja ya koromeo. (alama 1)

(e) Andika kinyume cha sentensi hii. (alama 2)
Aliamba kwamba wizi ulikuwa umepungua.

(f) Onyesha maana mbili za neno mlango.
(alama 2)

(g) Tumia kiambishi ndi- pamoja na nomino ya ngeli ya KI-VI wingi katika sentensi.. (alama 2)

(h) Badilisha kivumishi kilichoko katika sentensi kwa kivumishi cha kusisitiza. (alama 1)
Mtoto msichana amechelewa shuleni tena.

(i) Changanua kwa njia ya mstari.
(alama 4)
Rinda na mamake walimchukua mtoto aliyekuwa ametoroshwa.

(j) Kiima ni nini? (alama 2)

(k) Nyambua katika kauli ya kutendewa. (alama 2)
Dada analia chumbani.

(l) Onyesha matumizi ya viambishi viwili vya mahali katika sentensi moja.
(alama 2)

(m) Andika sentensi hii katika wingi. (alama 2)
Jaribio la shambulizi lilizimwa na askari.

(n) Fuata maagizo.
(alama 2)

(i) Tunamwombea (ifanye kishazi tegemezi)

(ii) Shiba (ifanye nomino)

(o) Ainisha nomino katika sentensi hii; (alama 2)
Jopo lilitarajiwa kusema ukweli.

(p) Tumia ki ya masharti kuandika upya sentensi hii; (alama 2)
Atakuja kisha tuende kwao.

(q) Andika upya katika wakati uliopita hali timilifu.
(alama 2)
Wanamaliza wali.

(r) Unganisha ili kuonyesha hali ya kuamrisha. (alama 1)

Wewe + Sije

(s) Andika katika msemo halisi. (alama 2)

Alfa alimwomba asimpeleke kwa mwalimu mkuu. Naye angempa zawadi. Akataka kujua kama anakubali.

(t) Eleza aina ya kielezi kilichopigwa mstari.

Kadzo alipambana kiume. (alama 1)

(u) Sahihisha bila kuondoa 'enye'.

(alama 2)

Gari lenye lilitujia halikuwa na utingo.

4. **ISIMUJAMII.**

Kiswahili ni mojawapo ya lugha za kibantu. Thibitisha kauli hii. (alama 10)

MTIHANI WA MWIGO WA WILAYA YA MURANG'A KUSINI KIDATO CHA NNE 2015

102/3
KISWAHILI
KARATASI 3
FASIHI
JULAI / AUGOST 2015
MUDA: 2 ½

SEHEMA YA A: USHAIRI
Swali la lazima.
Soma shairi kisha ujibu maswali.(alama 20)
Telezi.

1. Mvua iliyonyesha, ya maradi na ngurumo
   Kutwa na kucha kukesha, kunyesha pasi kipimo
   Haikuwanufaisha, wewe kazi za vilimo
   Wenye kazi za vilimo walifika na hasara.

2. Mimeya walioipanda, ilitekukatekuka
   Kazi ngumu waliotenda, yote ikaharibika
   Hawakuvuna matunda, waliyo wakiyataka
   waliyo wakiyataka, yakawa ya mbali nao.

3. Wenye kuicha mvua, isiwatose mwilini
   Baadhi yao wakawa, wakimbiliya penuni
   Wengine hawakutuwa, hadi mwao majumbani
   Hadi mwao majumbani, na kukomeya milango.

4. Wenzangu dhihaka kando, nisemayo ni yakini
   Ilibwaga kubwa shindo, mvua hiyo jamani
   Na mijaji kwa mikondo, yakawa barabarani
   Yakawa barabarani, mvuwa kwisha kunyesha

5. Kunyesha iliposiya, kukatapakaa tope
   Zilijaa kila ndiya, isibakiye nyeupe
   Ukawa mwingi udhiya, na kupita zisitupe
   Pa kupita zisitupe, kwa ndiya kukosekana.

6. Japo hivyo zilikuwa, ndiya hazipitiki
   Bali mimi naamuwa, kwenda japo kwa dhiki
   Kumbe vile nitakuwa, ni mfano wa samaki
   Ni mfano wa samaki, kuiendeya ndowana

7. Zikanibwaga telezi, sikujuwa kuzendeya
   Ningekwenda kwa henezi, yasingenifika haya
   Lakini tena siwezi, mwendo huo kutumiya
   Sitawata kutembeya, ila tabadili mwendo.

Maswali.

(a) Kwa kuzingatia mishororo miwili ya mwisho kila ubeti, eleza bahari ya shairi hili. (alama 1)
(b) Onyesha kero zinazosababishwa na mvua. (alama 4)
(c) Eleza kanuni zilizofuatwa kutunga shairi hili. (alama 4)
(d) Onyesha namna mshairi alivyotumia idhini yake. (alama 3)
(e) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha ya nathari.
(alama 4)
(f) Taja mbinu mbili za lugha zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 2)
(g) Andika maana za maneno haya kulingana na muktadha wa shairi. (alama 2)
   (i) kutwa na kucha

(ii) kuicha

SEHEMU B: RIWAYA.
Ken Walibora: Kidagaa Kimwemwozea.
Jibu swali la 2 au la 3

2. ... ukazae watoto..... wakaikomboe Tomoko toka kwa mkoloni mweusi.
   (a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
   (b) Kwa nini Tomoko inahitaji kukombolewa? (alama 12)
   (c) Eleza sifa nne za mnenaji. (alama 4)
3. Kwa kurejelea mbinu zifuatazo za lugha katika riwaya ya Kidagaa Kimemwozea, onyesha jinsi zilivyotumika kufanikisha maudhui;
   (alama 20)
   (i) Sadfa
   (ii) Barua
   (iii) Jazanda
   (iv) Mbinu rejeshi.

SEHEMU C: TAMTHILIA
Timothy Arege: Mstahiki Meya
Jibu swali la 4 au la 5

4. Eleza changamoto za kung'oa uongozi mbaya katika mabaraza ya miji ukirejelea Tamthilia ya Mstahiki Meya.
   (alama 20)
5. "Diwani wa III na daktari Siki ni viongozi wenye uadilifu na wanaowajibika." Thibitisha.
   (alama 20)

SEHEMU D: HADITHI FUPI
Ken Walibora: Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine.

6. Ukitumia mifano mwafaka, fafanua mambo yanayowatumbukiza vizana katika matatizo
   (alama 20)

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI.

7. (i) Ngomezi ni nini? (alama 2)
   (ii) Taja sifa sita za ngomezi. (alama 6)
   (iii) Eleza dhima ya ngomezi katika majiii.
   (alama 12)

MTIHANI WA MWIGO WA WILAYA YA MURANG'A KUSINI 2015
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
KISWAHILI
INSHA 102/1

1. Hii ni insha ya kiuamilifu - Mtahiniwa azingatie vipengele hivi vya kimsingi:-

(a) (i) Sura iwe ya barua rasmi - Anwani mbili.
(ii) Mtajo - Kwa mhariri
(iii) Kichwa cha barua / mada
(iv) Kiwiliwili / Maudhui
(v) Hitimisho - Jina kamili la mwandishi liweko.
- Sahihi itangulie jina.

(b) Hoja za kuzingatia.
Maoni yaweza kuwa faida na / au hasara.
Faida.
- Ajira kwa vijana.
- Kupunguza uhalifu.
- Usafiri wa haraka.
- Usafiri wa kutegemea.
- Kupenya maeneo yasiyofika magari.
- Kuimarisha uchumi wa jamii.

Hasara.
- Kuongezeka kwa ajali.
- Kuongezeka kwa vifo vinavyotokana na sekta ya usafiri.
- Kuzidisha msongamano kwenye hospitali.
- Kuongeza gharama ya huduma za hospitali.
- Kuchangia ongezeko la uhalifu / wizi wa pikipiki.
- Kuzidisha msongamano wa trafiki.

2. Mtahiniwa asimulie kisa au visa vianvyooana na maana na matumizi ya methali.
Mtahiniwa azingatie pande mbili za methali:-
Mtu asitarajie kuliwazwa kwa matatizo ya kujiletea.
Aonyeshe matatizo yaliyompata mhusika.
Matatizo haya yawe yalitokana na mhusika mwenyewe.

3. Hii ni insha ya mjadala.
Ionyeshe pande mbili.
Hoja za kuunga mkono;
- Ufisadi
- Uzembe
- Mapuuza
- Ahadi za uwongo
- Unyakuzi / wizi wa mali ya umma.
- Ujeuri.
- Kiburi.

Hoja za upinzani.
- Kunao wanaochangia maendeleo.
- Ukosefu wa sheria madhubuti za kupambana na maovu ya uongozi.
- Watu waadilifu kuwanii uongozi.
- Imekuwa ada kwa viongozi kushiriki maovu.

4. (i) Kisha chenyewe kioane na maneno haya.
(ii) Insha iwe na kichwa kisichozidi maneno sita.
(iii) Mtahiniwa asiongeze maneno baada ya kifungu alichopewa
(iv) Kisa kionyeshe yule mhusika alijiponza kwa kushiriki mzaha.
(v) Kisa kimhusu yeye mwenyewe (nafsi ya kwanza)

MTIHANI WA MWIGO WA WILAYA YA MURANG'A KUSINI 2015
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
KISWAHILI
102/2

Ufahamu

1. - Uandishi wa vitabu vya watoto.
   - Vitabu vya watoto. *(1 x 1 al 1)*
2. Katika umri mdogo. *al 1*
3. (i) Kujifahamisha mengi kuhusu ukuaji wa watoto wadogo.
   (ii) Kujifahamisha na yanayopendeza na kuchochea watoto katika kusoma. *2 x 2 al 4*
4. Kwamba wanafunzi wa madarasa ya chini wanaweza kutumia mikakati sawa na wa madarasa ya juu. *1 x 2 al 2*
5. (i) Kukariri
   (ii) Kuiga / kuigiza
   (iii) kufuatilia hadithi kwa picha.
6. (i) Sentensi fupi fupi
   (ii) Sarufi na msamiati sahihi.
   (iii) Kurudiwarudiwa
   (iv) Nyimbo na mashairi mapesi yawepo.
   (v) Kuwepo picha nyingi na vibonzo vya rangi. *zozote 2 x 1 al 2*
7. (a) Ombwe - pengo
   (b) Kufidiwa - kujazwa / kutoshelezwa

Ufupisho

(a) Hoja muhimu.

1. Watafiti wa afya wamegundua sukari ya viwandani haina virutubishi.
2. Utaratibu wa kuitayarisha iwe nyeupe huharibu virutubishi vinavyofaa mwili.
3. Sukari imesazwakwa kutiwa ladha tamu tu.
4. Sukari ina madhara. Inaposagika mwilini masalioya asidi yenye sumu.
5. Ikiwa nyingi hudhuru kwa kuozesha na kuharibu meno.
6. Huongeza maradhi ya kisukari.
7. Huleta ugonjwa wa kuumwa na kichwa ghafla,kutapika na kutoona ikitumiwa kiholela.
8. Huongeza kolestroli ambayo ikirundikana moyoni hufanya mishipa nyembamba.

Hoja 7 x 1 utiritiko 1 = al 8

(b) - Madhara ya sukari inaonyesha sukari ni sumu.
- Wataalamu wa lishe wanapendekeza ulaji wa chakula chenye sukari asilia, hasa inayotoka kwenye asali.
- Sukari ya asali ina virutubishi vingi vyenye manufaa mwilini.
- Hupatia mwili nishati na kuuchangamsha.
- Ina kemikali zinazosaidia mtoto kuwa na anaemia.
- Husaidia usagaji wa chakula ikitumiwa kabla ya kula.
- Huondoa harufu mbaya mdomoni.
- Inaweza kujipakwa hutunza ngozi na kuing'arisha.
- Huondoa vipele na ugumu wa ngozi.
- Hutibu vidonda.
- Viwanda vya vipodozi huitumia kama malighafi. *Hoja 6 x 1 utiririko al 1 = al 7*

Sarufi / Matumizi ya lugha.

(a) Yeye ndiye anayejua kwetu. *al 2*

(b) wa - nafsi
tembe - mzizi
a - kiishio
vyo – kirejeshi *4 x ½ (al 2)*

(c) Sentensi mbili sahili zenye kiunganishi, zina mawazo zaidi ya moja m.f; tathmini sentensi ya mwanafunzi iwe
na kiunganishi.

(d) hari, haraka, halafu, ahsante n.k *(1 x 1 al 1)*
(e) Aliambiwa kwamba wizi ulikuwa umezidi. *(2 x 1 al 2)*
(f) Mlango - (i) Uwazi wa kuingilia katika nyumba.
(ii) Sehemu katika biblia. *(2 x 1 al 2)*
(g) Vitabu hivi ndivyo alivyonunua.
Vyama vyao ndivyo vilisajiliwa. *(2 x 1 al 2)*
(h) yuyu huyu
yuyo huyo
yule yule *yoyote 1 x 1 al 1*
(i) S - KN + KT
KN - N + U + N
N - Rinda
U - na
N - mamake
KT - T + N + S
T - walimchukua
N - mtoto
S - aliyekuwa ametoroshwa al 4
(j) Kiima - Sehemu katika sentensi inayochukua mahali pa nomino / kundi nomino.
(k) Chumbani mnaliwa na dada. al 2
(l) Asomeapo ni darasani
Tunakoenda ni sokoni
Mlimokuwa mnashwa ni chumbani *yoyote al 2*
(m) Majaribio ya mashambulizi yalizimwa na askari. *(al 2)*
(n) (i) Tunapomwombea
Tunayemwombea
Tukimwombea
Ambaye tunaombea *yoyote al 1*
(ii) Shiba – shibe *al 1*
(o) Jopo - Ya makundi
Ukweli – dhahania *al 2*
(p) Akija tuende kwao.
Akija tutaenda kwao *al 2*
(q) Walikuwa wamemaliza wali. *al 2*
(r) Usije! *al 1*
(s) "Nakuomba / tafadhali usinipeleke kwa mwalimu mkuu. Nami nitakupa zawadi." Alfa alisema "Je, unakubali? akauliza.
(t) Cha namna mfanano.
(u) Gari lenye kutujia halikuwa na utingo.

Isimujamii.

1. Msamiati wa lugha za kibantu unakaribiana.
2. Baadhi ya vitenzi vya kibantu kinanyambulika.
3. Kiswahili kina irabu tano ambazo baadhi ni kama za lugha nyingi za kibantu.
4. Muundo wa maneno ya kibantu unakaribiana
m.f KKI, IKKI, KIKI
5. Mpangilio wa ngeli za nomino unajitokeza katika lugha nyingi za kibantu *hoja 5 x 2 (al 10)*

MTIHANI WA MWIGO WA WILAYA YA MURANG'A KUSINI 2015
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
KISWAHILI
FASIHI
102/3

1. Ushairi.
   (a) Bahari - Pindu
   (b) (i) Kunyesha usiku na mchana (kutwa kucha)
   (ii) Mimea kuharibika.
   (iii) Barabara kuharibika.
   (iv) Njia hazipitiki.
   (v) Watu kutotoka nje. *(zozote 4 x 1 = 4)*
   (c) (i) Mishororo minne katika kila ubeti.
   (ii) Mizani 16 katika kila mshororo.
   (iii) Kila mshororo umegawika katika vipande viwili.
   (iv) Vina vinabadilikabadilika kutoka ubeti mmoja hadi mwingine. *(4 x 1 = 4)*
   (d) Idhini ya ushairi.
   (i) Lahaja m.f sitawata, ndiya
   (ii) Inkisari m.f walotenda
   (iii) Tabdila m.f mvuwa, iliposiya
   (iv) Mazda - kwenenda, maradi *(3 x 1 = 3)*
   (e) Lugha nathari;
   Mvua iliyonyesha ya radi na ngurumo kutwa na kucha ilinyesha bila kipimo. Haikuwanufaisha wakulima kwa kuwa walifikiwa na hasara. *(al 4)*
   (f) Mbinu za lugha.
   (i) Taswira - barabara zisizopitika
   - barabara zenye matope
   (ii) Tashbihi - Mfano wa samaki.
   (iii) Takriri - ilitekukatekuka, maneno ya mwisho wa mstari 3, mwanzo wa mstari 4.
   (iv) Tashihisi - ikanibwaga telezi
   (v) Lahaja - ndiye, sitawata. (zozote 2)
   (g) (i) Kutwa na kucha - mchana na usiku.
   (ii) Kuicha mvua - kuiogopa.
   (al 2)
2. *Riwaya : Kidagaa Kimemwozea*.
   (a) (i) Msemaji - Mzee Matuko Weye.
   (ii) Msemewa - Imani Mtembezi
   (iii) Seli walikofungiwa.
   (iv) Amani na Imani wameletwa seli alikofungiwa.
   Matuko Weye na anawatetea.
   (b) (i) Unyakuzi wa mashamba k.m la akina Amani.
   (ii) Watu kusingiziwa makosa kisha kufungwa k.m Yusufu, Amani na Imani.
   (iii) Mauaji ya kiholela k.m Chichiri Hamadi.
   (iv) Viongizi na washerati k.m Mtemi Nasaba Bora.
   (v) Ubadhirifu wa pesa za umma k.m Fao alipelekwa ng'ambo kwa pesa zilionuiwa kulipia watoto wa
   maskini.
   (vi) Kodi za lazima k.m Mtemi Nasaba Bora aliwatoza pesa kwa lazima ampeleke mwanawe Urusi
   kusoma.
   (vii) Mapendeleo k.m Nasaba Bora alihonga wakuu wa jeshi mwanawe apate cheo jeshini.
   (viii) Ufisadi k.m Mtemi Nasaba Bora alibadilisha hati miliki za mashamba ajilimbikizie.
   (ix) Mahakama kutoa uamuzi usio wa haki k.m Yusufu anafungwa kwa visingizio.
   (x) Dhuluma kwa waandishi k.m mswada wa Amani kuchapishwa kwa jina la Majisifu.
   (zozote 6 x 2 = 12)
   (c) Sifa za mnenaji.
   (i) Mwanamapinduzi.

(ii) Mpenda haki.
(iii) Jasiri / mkakamavu
(iv) Mwenye urazini / amezinduka.
(v) Mtetezi wa haki. *(zozote 4 x 1 = 4)*

3. (i) Sadfa - Mambo kutokea kwa pamoja bila kupangwa. k.m
- Kukutana kwa Amani na Imani kando ya ziwa Mawewa.
- Kukutana kwa Amani, Imani na D.J kando ya Mto Kiberenge.
- Amani anapotafuta kazi kwa Mtemi mchungaji wa awali ni mgonjwa na hawezi kuendelea na kazi n.k.
- Kifo cha Uhuru kinasadifiana na Majisifu kuja kumtafuta Imani arejee kazini kwake.
- Bi zuhura anapamwita Amani chumbani, mumewe anaingia.

(ii) Barua.
- Ni mbinu ya mawasilianao kwa njia ya maandishi.
- Barua ya Madhubuti kwa babake.
- Barua ya Lowela kwa Mtemi Nasaba Bora.
- Barua ya Ben Bella kwa Mashaka.
- Barua ya Majisifu ya ualishi chuo cha wangwani..
- Barua ya Amani kwa Imani.

(iii) Jazanda.
- Ni ujumbe uliofumbwa.
- Fahali kula kaptula ya DJ na kumwacha bila chochote -Mtemi Nasaba Bora kunyakua mashamba ya maskini
na kuwaacha bila.
- Kutokufa kwa wakereketwa / wanamapinduzi k.m Amani, DJ na Imani ni kutofifisha mapambano ya ukombozi.
- Ndoa ya Amani na Imani ni mwanzo wa ujenzi wa jamii mpya.
- Kifo cha kitoto Uhuru ni uhuru wa nchi ya mkoloni kuondoka. Tomoko haukupewa nafasi ushamiri.
- Kifo cha Mtemi Nasaba Bora ni mwisho wa uongozi mbaya.
- Jibwa Jimmy ni mkoloni mkongwe ambaye athari yake inahisika.
- Safari ya Amani kwenda Sokomoko ni safari ya kusaka haki na ukweli. *(zozote 4 x 1)*

(iv) Mbinu rejeshi/kisengere nyuma /Matukio ya awali kuletwa mbele.
- Amani na Imani walivyokutana.
- Amani alivyosingiziwa akiwa chuoni kishakufungwa.
- Imani akielezea walivyonyang'anywa shambalao.
- Mtemi akieleza alivyopanga mauaji ya Chichiri Hamadi.
- Imani anakumbuka kisa cha Majununi.
- Jinsi Nasaba Bora alivyonunua mkweche wake na mauaji ya paka.
- Sababu za marukufu ya kunywa maji ya mto
Kiberenge. *- Maelezo ya mbinu alama 1*

- Mifano ya mbinu alama 4

(4 x 5 = 20)

Tamthilia

4. (i) Sheria kandamizi k.m Mayor's Act na Riots Act.
(ii) Propaganda za viongozi - mf: Waandamanaji hawakuukawa.
(iii) Ushauri wa kupotosha.
(iv) Ubinafsi wa viongozi.
(v) Matumizi ya vyombo vya dola k.v askari kutibua maandamano.
(vi) Ujinga wa wananchi kuchagua viongozi wabaya.
(vii) Wananchi waadilifu kukataa kuwania uongozi.
(viii) Mapendeleo k.m madiwani na askari kuongezewa mishahara wamuunga mkono Meya.
(ix) Unafiki wa kidini k.m Meya kuita mhubiri kuombea baraza lililojaa uovu aonekane ni mcha Mungu.
(x) Uzalendo bandia k.m nyimbo za kizalendo baada ya vipindi maarufu.
(xi) Kutengwa kwa viongozi waadilifu k.m Diwani wa III
(xii) Ahadi za uongo kuwapa watu moyo wa matumaini au subira.
(xiii) Upurukushani k.m Dida kutojali. *(zozote 10 x 2 = 20)*

5. Daktari Siki.
- Anapeleka malalamiko ya kucheleweshwa kwa dawa kwa Meya.
- Anawapa wagonjwa matumaini.
- Anatahadharisha wawakilishi wa wafanyikazi dhidi ya hatari za migomo.
- Anaendelea na kazi licha ya hali gumu za kikazi k.v mshahara mdogo, tishio la maambukizi mahali pa kazi
  n.k.
- Anashirikiana na Diwani wa III kutafuta suluhisho la matatizo ya wanacheneo.
- Anahimiza wafanyikazi waendelee kutetea haki zao.
- Anawahamasisha wanacheneo watetee haki zao k.m Meya anamuuliza kama alichochea mgomo mwingine.
- Anamueleza Meya ukweli wa mambo kuhusu hali ilivyo Cheneo *(zozote 5 x 2 = 10)*

Diwani wa III.
- Anatetea haki za wafanyikazi waongezewe mishahara pamoja na viongozi.
- Anapendekeza kodi itozwe hata viongozi ili kuimarisha uchumi wa baraza.
- Analalamikia kutengwa katika maamuzi muhimu ya baraza k.v kuidhinisha nyongeza ya mishahara.
- Anaonyesha heshima kwa Meya kwa kuzingatia dhana ya Collective responsibility.
- Anashirikiana na daktari Siki kutafuta suluhu ya matatizo ya wanacheneo.
- Anamzindua Siki kuwania uongozi kuleta mabadiliko.
- Hakubaliani na maoni ya madiwani wenzake.
- Anampinga Meya katika mapendekezo anayoona hayafai. *(zozote 5 x 2 = 10)*

6. Hadithi Fupi: Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine
   i) Hali ngumu ya maisha / umaskini – inamfanya Kananda kutafuta kazi kwa Bw. Mwatela ambako anapachikwa mimba (mwana wa Darubini)
   ii) Abu anakosa msichana wa kuoa kila anapopeleka posa (Ndoa ya Samani)
   iii) Ulimbukeni wa mapenzi unawafanya wasichana kupata mimba wakiwa shuleni k.m Sela na wasichana
   wenzake watatu (kanda la usafi)
   iv) Christine anapata mimba akiwa chuoni. (Samaki wa Nchi za Joto)
   v) Shinikizo la marafiki linafanya kina Semkwa wavamiwe. k.m Semkwa (Glasi ya mwisho)
   vi) Kupuuza ushauri k.m Christine (Samaki wa Nchi za Joto)
   vii) Tamaa ya maisha ya hadhi k.m Chritine (Samaki wa Nchi za Joto),Lucy katika Tazamana na Mauti.
   xiii)Ubaguzi wa rangi k.m Fikirini (Damu Nyeusi)
   ix) Kutegemea wazazi k.m Amali kukosa mume. (Ndoa ya Samani)
   x) Woga k.m Kananda kutishiwa na Mwatela kisha k unyang'anywa mtoto (Mwana wa Darubini)
   xi) Ukatili wa wazazi k.m Sudi kutupwa na mamake (Mizizi na Matawi)
   xii) Tabia ya kidomo na kimbelembele k.m Seruwa alikosa kuolewa na msimulizi (Mke Wangu).
   xiii)Ufuska na anasa k.mChristine (Samaki wa Nchi za Joto) *(zozote 1-x 2 = 20)*

7. Fasihi Simulizi.
   (i) Ngomezi - maana.
   (i)- Ni fasihi ya ngoma. Huhusisha ala za muziki kupasha ujumbe.
   (ii) - Fasihi ya ngoma na ala zingine za sauti. *yoyote 1 x 2 = 2*

   (ii) Sifa za ngomezi.
   - Mdundo wa ala hueleweka na wenyeji / jamii husika.
   - Huwa na ala.
   - Midundo ya ala ina maana maalum.
   - Huongozwa na watu maalum (masogora)
   - Hutenga hadhira teule.
   - Ni ya wakati maalum *zozote 6 x 1 = 6*

   (iii) Dhinia / majukumu ya ngomezi.
   - Kuburidisha wakati hakuna tukio zito.
   - Kukuza ustadi k.m Masogora huonyesha ubingwa katika kutumia ngoma kuwasilisha ujumbe.

- Kuficha ujumbe usifahamike na wasiohusika.
- Kuharakisha mawasiliano.
- Hutahadharisha.
- Hudumisha utamaduni.
- Hudhihirisha ufundi wa kisanaa.
- Kuipa jamii utambulisho.
- Kukuza mila na desturi.
- Husaidia kwenye sehemu zenye mawasiliano magumu.
- Hutoa matangazo rasmi kuhusu jambo.
- Kufahamisha kunapotokea jambo lenye uzito. *(zozote 6 x 2 = 12)*

TATHMINI YA PAMOJA YA GATUZI LA KERICHO 2015
Cheti cha kuhitimu Elimu ya Sekondari (K.C.S.E)
KISWAHILI
Karatasi 1
JULAI/AGOSTI 2015

1. Lazima
Kumekuwa na ongezeko la visa vya ubakaji nchini katika siku za hivi karibuni. Wewe umeteuliwa na waziri wa usalama wa jamii kuwa katibu wa jopo linalochunguza chanzo cha visa hivi na kupendekeza njia za kusitisha uovu huu. Andika ripoti yako.

2. "Ulevi wa pombe haramu umeleta madhara mengi katika jamii ya leo." Thibitisha ukweli wa usemi huu huku ukipendekeza hatua zitakazochukuliwa na serikali na jamii kutatua tatizo hili.

3. Andika insha itakayodhihirisha ukweli wa methali hii.
Sikio la kufa halisikii dawa.

4. Tunga kisa kitakachoisha kwa maneno yafuatayo:
... Hapo ndipo nilipogutuka kutoka usingizini. Mwili wangu ulikuwa umeloa jasho, nao moyo ulinipapa. Ndipo nilipong'amua kuwa yote hayo yalikuwa ruiya tu.

TATHMINI YA PAMOJA YA GATUZI LA KERICHO 2015
Hati ya kuhitimu Elimu ya Sekondari (K.C.S.E)
KISWAHILI- LUGHA
Karatasi 2
JULAI/AGOSTI 2015

SEHEMU YA A

1. **UFAHAMU (ALAMA 15)**
Soma taarifa hii kisha ujibu maswali yanayofuata.
Alipokuwa akiukemea utamaduni na dhana za kikabila katika nyimbo zake, marehemu Bob Marley aliufananisha ubepari na "wanyama wala watu." Katika wimbo "Babylon System" (yaani mfumo wa kibepari), Marley alisema kuwa utamaduni huo ndiyo mzawa wa matatizo yote ya kiutawala ambayo yalikuwa yakiyakumba mataifa ya Weusi katika karne ya 20, wakati nchi zao zilikuwa zikitawaliwa na nchi za mataifa ya Ulaya.

Kwa mantiki hiyo, pengine Marley alikuwa na maono kuwa Afrika haingejikomboa kutoka kwa utumwa wa Kizungu, ikiwa ingeendelea kuziabudu na kuzishadidia tamaduni za Kimagharibi.

Utabiri huo nauoanisha na yanayoendelea nchini, ambapo serikali ya Jubilee imeonekana kushindwa kabisa kuikabili saratani ya ufisadi, ambayo inahatarisha kuliamgamiza taifa hili lenye uchumi dhalili.

Donda hili linazidi kuyatandaza mabawa yake kutoka, tisho kuu likiwa ni uvamizi wa taasisi "takatifu"

ambazo tunazitegemea kulikabili donda hilo.

Ni nani tutategemea kukabiliana na rushwa ikiwa taasisi kama Bunge, Tume ya Maadili na Kukabiliana na Ufisadi (EACC) kati ya zingine muhimu zimepakwa tope na saratani hiyo?

Kimsingi yote tunayopitia ni matunda ya uasi wa tamaduni za Kiafrika na uegemezi wa mifumo ya Kizungu kama mihimili ya jamii na nchi zetu.

Ndoto za watetezi wa Uafrika na nafasi ya Weusi kama marehemu Malcom X na Martin Luther King, zilikuwa ni kuona kuwa wameungana kabisa kukabiliana na matatizo yaliyowakabili bila kuzingatia mazingara waliyokuwepo.

Pindi tu baada ya mataifa mengi ya Kiafrika kujinyakulia uhuru wao katika miaka ya hamsini na sitini, viongozi wakuu walioziongoza nchi hizo kama Kwame Nkrumah, Jomo Kenyatta, Mwalimu Julius Kibarage Nyerere kati ya wengine walianza harakati za kuliunganisha bara hili na kubuni Muungano wa Nchi za Kiafrika (USA) japo ndoto hiyo haikufikia.

Kwa msingi huo, mhimili mkuu wa kiutawala ungekuwa ni mfumo wa kisochalisti, ambao ungekuwa nguzo kuu ya kuyaunganisha mataifa hayo.

Hata hivyo, migawanyiko mikubwa ilianza kushuhudiwa, huku baadhi ya mataifa yakianza kukabiliwa na mapigano ya wenyewe kwa wenyewe, huo ndio ulikuwa mwanzo wa kutaasisika kwa maovu yote tunayoshuhudia sasa-ufisadi na tamaa ya kuogofya kutoka kwa viongozi wetu.

Maswali

a. Ipe taarifa hii anwani mwafaka. (alama 1)

b. Onyesha mambo mawili makuu ambayo msanii aliyapinga. (alama 2)

c. Kwa nini ubepari umelinganishwa na 'wanyama wala watu'.? (alama 2)

d. Kwa mujibu wa taarifa eleza sifa za Bob Marley. (alama 2)

e. Swala linalozugumziwa limerejelewa kama 'Donda'.

i) Eleza mbinu ya lugha iliyotumika.. (alama 2)

ii) Ni kweli kuwa donda hili laelekea kuwa gumu. Thibitisha. (alama 2)

f. Tatizo hili la 'donda' ni kama kujipalia makaa. Fafanua. (alama 2)

g. Eleza maana ya maneno yafuatayo kwa mujibu wa taarifa. (alama 2)

i) Mhimili

ii) Taasisi

2. SEHEMU YA B: UFUPISHO (Alama 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.

Sisi vijana wa Kenya inatupasa kufanya kazi kwa bidii na kwa dhati ya mioyo yetu ili tuweze kupata ufanisi na uwezekano wa kuinua nchi yetu change katika kiwango cha juu. Tukumbuke, "Ajizi ni nyumba ya njaa." Kwa hivyo basi haifai kulaza damu ikiwa matatizo nchini mwetu yametuzonga. Lazima tufanye kazi kwa busara, adabu njema na jitihada kwa moyo mmoja. Sharti tutilie maanani zaidi elimu ya vijana na watu wazima, kilimo, uchumi na amani katika nchi yetu. Tunahitaji taifa lenye watu walioelimika, kwani bila elimu itakuwa vigumu sana kuweza kutekeleza mipango mbalimbali ya mazao mashambani kwani kila kukicha idadi ya watu inaongezeka. Ni sharti tuweze kujitosheleza kwa chakula. Zaidi ya hayo, lazima tujishughulishe na biashara ambapo kwa sasa ni Wakenya wachache sana ambao wanatambua umuhimu wa biashara. Wengi ni wale wenye mawazo ya kwamba lazima kila mmoja aajiriwe maishani. Yatupasa kujitahidi kuleta uchumi katika mikono ya wananchi wa Kenya badala ya kuwaachia wengine ambao hawahusiki.

Mafunzo tunayopata majumbani, shuleni na hata katika jamii, lazima yatuwezeshe kutambua mbinu za kupitia. Tunahitaji elimu tambuzi ambayo itamfanya mwanakenya kujua wajibu wake katika jamii. Tumesinywa na elimu pumbao inayotupumbaza na kutufanya tusione mbele. Sisi vijana tukiwa viongozi wa siku zijazo tutambue kwamba 'Utengano ni uvundo'. Lugha ya taifa ndiyo chombo cha pekee ambacho kinatuunganisha na kuweza kutuwasilishia mapendekezo, mawaidha na hisia zetu. Kukosa ndiko binadamu. Wakati tunapokosea lazima tukubali kuwa tumekosa na kufanya masahihisho mara

moja kwani, “Usipoziba ufa, utajenga ukuta.” Tusikasirike kwa sababu tumesahihishwa makosa yetu na wenzetu. Lazima tujitoe mhanga na kupigania nchi yetu tukiwa wazalendo halisi.

Sisi tukiwa vjana sharti tujishughulishe na kuyaangalia matatizo ya nchi, pia kutafuta njia za kutatua matatizo hayo. Siku zote tutekeleze nidhamu. Ni jambo la kusikitisha kwamba sisi vijana twashutumiwa mara kwa mara kwa kutokuwa na nidhamu shuleni na majumbani mwetu. Ili watu waweze kuishi maisha bora na kuwa na maendeleo, amani na upendo, lazima tuwe na bidii, ushirikiano mwema na kuchagua viongozi wenye mioyo ya maendeleo. Tukiwa viongozi ambao hawajishughulishi na maendeleo basi tutabaki nyuma kama mkia siku zote. Bahati mbaya ni kwamba wananchi wengi siku hizi huchagua viongozi wao kwa kufuata ukoo ama kwa utajiri wake. Kwa hivyo basi ni vyema kuwachagua viongozi kutokana na ufanisi wanaoweza kuleta bali si kwa kutegemea utajiri au ukoo.

Maswali

a) Katika aya ya kwanza mwandishi anawahimiza vijana kufanya nini ili kuchangia katika maendeleo?
(maneno 45-50)
(alama 7)

b) Fupisha aya mbili za mwisho kwa maneno 50 - 60.
(alama 8)

3. SEHEMU YA C: MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)

a) Taja sifa mbili za kutambua irabu.
(alama 2)

b) Tunga sentensi kwa kutumia kitenzi cha katika kauli ya kutendeka.
(alama 2)

c) Tunga sentensi kwa kutumia nomino ifuatayo katika hali ya wingi.
(alama 2)
Uyoga

d) Andika katika usemi halisi.
(alama 3)
Mama alinifokea nitoke hapo mara moja.

e) Unda nomino ya dhahania kutokana na kitenzi kifuatacho na uitungie sentensi sahihi.
Batili (alama 2)

f) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha vishale.
(alama 4)
Mzigo ubebwao una uzani mkubwa.

g) Akifisha:
umoja wa mataifa barani afrika akaanza mwinyi utaimarishwa na viongozi wa nchi hizi ili tuendeleze maendeleo kupitia utandawazi akamaliza
(alama 3)

h) Andika sentensi ifuatayo katika ukubwa wingi.
Mkono wa yule mwizi ulikatwa kwa upanga wenye makali.
(alama 3)

i) **i)** Eleza maana ya shamirisho. (alama 2)
ii) Bainisha shamirisho katika sentensi hii.
(alama 2)
Buzi lililochinjiwa wageni lilipaswa kuuzwa kesho asubuhi.

j) Eleza matumizi matatu tofauti ya kiambishi -ka- (alama 3)

k) Ainisha vitenzi katika sentensi hii.
(alama 2)
Ukweli ulio na uchungu haupendwi.

l) Ainisha viambishi katika sentensi hii: (alama 3)
Kilichofungishwa

m) Andika maana mbili ya neno : Karo_____

(alama 2)

n) Kanusha: (alama 2)
Wao wakimbiapo huwa wameona hatari.

o) Tunga sentensi kwa kutumia kinyume cha kitenzi angika.
(alama 2)

p) Amrisha katika wingi. (alama 1)
Amka

4. SEHEMU YA D: ISIMU JAMII (ALAMA 10)

a) Eleza maana ya mawasiliano. (alama 2)

b) Taja njia tatu ambazo kwazo mwanadamu huwasiliana. (alama 3)

c) Eleza sababu zinazochangia kuwepo kwa uwingi lugha.
(alama 5)

TATHMINI YA PAMOJA YA GATUZI LA KERICHO 2015
Cheti cha kuhitimu Elimu ya Sekondari (K.C.S.E)
KISWAHILI
Karatasi 3
JULAI/AGOSTI 2015

SEHEMU A: USHAIRI - LAZIMA
Soma mashairi A na B halafu ujibu maswali ya yanayofuatia,
SHAIRI A:

1. Jaribu kuwa mpole, kwa wenzio darasani,
Jihadhari na kelele, na utusi mdomoni,
Wala siwe kama wale, wanafunzi maalum,
Wasio akili vichwani, katu usiwaingilie.

2. Ujifanyapo ja vile, watoto wale wahuni,
Juwa jatakwenda mbele, utashindwa mtihani,
Na toka dakika ile, utaingia mashakani,
Jaribu uwe twaani, mwanafunzi zingatile.

3. Mtoto kuwa mpole, nakueleza yakini,
Huwa ni mfahamile, wa elimu akilini,
Ni shida kuangukile, kushindwa na mtihani,
Yataka utamakani, mwanafunzi siliwale.

4. Mwanafunzi nakukanya, kwa yale mawi mwandani,
Sizowee kusengenya, sengenyo madarasani,
Kama hilo ukifanya, utakuwa mashakani,
Ni hayo nilowaonya, kwa hiyo nawaageni.

Shairi B
Aliniusia babu, zamani za utotoni
Kanambia jitanibu, na mambo ya nuksani
Na wala usijaribu, kwa mbali wala jirani
Malifi ni duniani, kuzimu kwenda hisabu.

Liche jambo la aibu, lipalo mtu huzuni
Liuvunjao wajibu, m'bora akawa duni
Lau chamba utatubu, kulipwa hukosekani
Malifi ni duniani, kuzimu kwenda hisabu.

Usipolipwa karibu, lakutoka fahamuni
Lazima lije jawabu, ingawa pindi mwakani
Japo kuwa ughaibu, au mwisho uzeeni
Malifi ni duniani, kuzimu kwenda hisabu.

Kila neno lina jibu, usitafute kwa nini
Mambo yenda taratibu, pupa jingi lafaani
Akopeshae zahibu, atalipwa zaituni
Malifi ni duniani, kuzimu kwenda hisabu.

Ahimilie taabu, hupata mema mwishoni
La raha au sulubu, malifi ni duniani
Mambo bahati nasibu, viumbe tahadharini
Malifu ni duniani, kuzimu kwenda hisabu.

1. a) Linganisha shairi la A na B kimaudhui.
(alama 4)

b) Linganisha na kulinganua mashairi ya A na B ukizingatia sifa za kiarudhi. (alama 4)
c) Katika shairi la A andika ubeti wa nne kwa lugha tutumbi. (alama 4)
d) Taja na ueleze idhini ya mshairi ilivyotumiwa katika shairi A.
(alama 4)
e) Fafanua maana ya mshororo ufuatao ulivyotumika katika shairi la B.
(alama 2)
i) Kanambia jitanibu na mambo ya nuksani.
f) Eleza maana ya msamiati ufuatao. (alama 2)
i) Nuksani
ii) Malifi

SEHEMU B: TAMTHILIA -MSTAHIKI MEYA - T.AREGE

2. "---Hii harufu mbaya ya taka iliyoupamba mji wetu ni kiwakilishi cha uozo ulio ndani."
a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
b) Taja na ueleze mbinu mbili za kifasihi zilizotumiwa katika dondoo hili.
(alama 4)
c) Kwa kurejelea Tamthilia nzima eleza uozo ulio katika mji wa cheneo.
(alama 12)

AU

3. Viongozi katika tamthilia ya mstahiki Meya ni vielezo vya viongozi katika mataifa mengi ya bara la Afrika. Fafanua.
(alama 20)

SEHEMU C: HADITHI FUPI- DAMU NYEUSI- KEN WALIBORA na S.A MOHAMMED

4. Jadili mbinu ya ishara ilivyojitokeza katika hadithi fupi ya Gilasi ya mwisho makaburini.
(alama 20)
AU

5. Kwa kurejelea hadithi zifuatazo jadili jinsi maudhui ya mgogoro yalivyoshughulikiwa. (alama 20)
a) Mke wangu
b) Tazamana na mauti
c) Ndoa ya samani
d) Mwana wa darubini

SEHEMU D: RIWAYA YA KIDAGAA KIMEMWOZEA - KEN WALIBORA

6. Eleza jinsi mbinu zifuatazo zilivyotumika katika Riwaya ya kidagaa kimemwozea:
(alama 20)
a) Jazanda
b) Sadfa
AU

7. "--- Wamechoka hadi ya kuchoka. Mtini nondo anapapatika kutoka kujinasua toka utandabui uliomnasa"
a) Eleza muktadha wa dondoo hili.
(alama 4)
b) Ni masaibu gani yaliyowakumba wanaorejelewa?
(alama 6)
c) Nondo anayejaribu kujinasua kutoka utandabui ni jazanda. Jadili.
(alama 10)

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

8. a) Eleza maana ya maghani. (alama 2)
b) Taja sifa zinazotambulisha maghani. (alama 6)

c) ***Soma mtungo huu kisha ujibu maswali***
Ndimi Kisoi, dume la ukoo mtukufu
Ulojipambanua kwa mabingwa
Wachezaji hodari wa ngoma
Ndimi dume liloingia nyanjani.

Makoo yakatetemeka
Yakang'ang'ania, gozi kusakata nami

Kijiji kizima kilinijua
Wazee walinienzi
Wakamiminiza kiamboni
Mabinti kunikabidhi

i) Tambua utungo huu (alama 1)
ii) Eleza sifa za mtungo huu. (alama 8)
iii) Eleza mbinu za kisanii zilizotumiwa katika mtungo huu.
(alama 3)

TATHMINI YA PAMOJA YA GATUZI LA KERICHO 2015
Cheti cha kuhitimu Elimu ya Sekondari (K.C.S.E)
KISWAHILI
Karatasi 1
JULAI/AGOSTI 2015

1. Hii ni ripoti.
Muundo / sura ya ripoti
i) Anwani - iwe na yafuatayo
- kuhusu - mada na wahusika
- wapi
- lini

ii) Utangulizi
- arejelee mada
- aorodheshe wanajapo

iii) Mbinu ya kukusanya data
iv) Matokeo ya uchunguzi
- Matumizi ya dawa za kuulevya
- Ukosefu wa ajira
- Ukosefu wa nidhamu
- Teknolojia ya kisasa / vipindi visivyo na maadili / ponografia.
- Mavazi mabaya
- Chuki / migogoro ya kijamii

v) Mapendekezo
Mapendekezo yatokane na matokeo ya uchunguzi.
vi) Hitimisho
- mukhtasari wa mambo kulingana na matokeo ya uchunguzi.

vii) Thibitisho
- Jina
- Cheo
- Sahihi
- Tarehe

2. i) <u>Madhara ya pombe haramu</u>
- vifo
- utengano
- kufilisika
- kufutwa kazi
- kutowajibika
- uhalifu
- upofu
- kuzorota kwa afya zao

ii) <u>Suluhu za serikali na jamii</u>
- zitokane na madhara yaliyotajwa.

3. Ni insha ya methali - sikio la kufa halisikii dawa.
- Atunge kisa kinachodhihirisha maana ya matumizi ya methali hii.
- Kisa kidhihirishe pande mbili za methali hii (sikio la kufa) na (halisiikii dawa).

<u>Maana ya methali</u>
- Mtu ambaye siku yake imefika kufa hana budi kufa hata akifanyiwa dawa za aina gani. Vile vile ina maana kuwa jambo ambalo limefikia siku yake ya kuharibika halina budi kuharibika hata kufanywe nini.

4. Ni insha ya mdokezo
- Atunge kisa na akamilishe kwa maneno aliyopewa.

TATHMINI YA PAMOJA YA GATUZI LA KERICHO 2015
Cheti cha kuhitimu Elimu ya Sekondari (K.C.S.E)
KISWAHILI
Karatasi 2
JULAI/AGOSTI 2015

SEHEMU A : UFAHAMU (alama 15)

a) Ufisadi *1 × 1 = 1*
b) i) Utamaduni
ii) Dhana za kikabila *2 × 1 = 2*
c) Ndiyo mzawa wa matatizo yote ya kiutawala. *1 × 2 = 2 alama*
d) i) Mwenye maono
ii) Mtetezi *2 × 1 = 2*
e) i) Jazanda - ufisadi kurejelewa kuwa donda. *1 × 2 = 2*
ii) Donda linatandaza mbawa zake kwenye 'taasisi takatifu' zinazopaswa kuipinga ufisadi. *1 × 2 = 2*
f) Uasi wa tamaduni za kiafrika
Kuegemea mifumo ya kizungu *2 × 1 = 2*
g) i) Mhimili - nguzo / tegemeo / iliyo imara *al. 1*
ii) Taasisi - kituo maalum cha kustawisha / kutoa mfaunzo. *al. 1*
Adhabu - sarufi : popote patokeapo na usiadhibu zaidi ya nusu alama aliyopata mwanafunzi.
Hijai - hadi makosa sita *6 × ½ = alama 3*

SEHEMU B : UFUPISHO *(*alama 15)

a)
- Kufanya kazi kwa bidii na kwa dhati ya mioyo yetu.
- Kufanya kazi kwa busara, adhabu njema.
- Jitihada kwa moyo mmoja.
- Kutilia maanani zaidi elimu ya viijana na watu wazima.
- Kujitosheleza kwa chakula.
- Kujishughulisha na biashara
- Kujitahidi kuleta uchumi katika mikono ya wananchi.

zozote 6 × 1 = 6
utiririko 1 jumla (alama 7)

b)
- Mafunzo tupatayo yatuwezeshe kutambua mbinu za kupitia.
- Tunahitaji elimu - tambuzi.
- Vijana watambue utengano ni uvundo.
- Lugha ya taifa ni chombo cha kuunganisha na kuwakilisha hisia zetu.
- Tukosapo tukubali na tusahihishe.
- Tujitoe mhanga na kuwa wazalendo
- Vijana tuangalie matatizo na kutafuta suluhu.
- Vijana tuwe na nidhamu
- Ili kuishi maisha bora tuwe na ushirikiano.
- Kuchagua viongozi wenye mioyo ya maendeleo.

Makosa sarufi hadi makosa sita. *6 × ½ = alama 3*
Hijai hadi makosa sita *6 × ½ = alama 3*

SEHEMU YA C:
MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)

a) i) Muundo wa midomo
ii) Mkao wa ulimi. *2 × 1 = alama 2*
b) i) Chika
Kadiria sentensi ya mwanafunzi *2 × 1 = alama 2*
c) Uyoga - Ngeli ya U - U *1 × 2 = alama 2*
✓ ✓ ✓ ✓ ✓ ✓

d) " Toka hapa mara moja!" Mama alinifokea. ***6 × ½ = alama 3***

e) Ubatilifu ***kadiria sentensi*** ***1 × 2 = alama 2***

f) S → KN + KT
KN → N + S
N → Mzigo
S → ubebwao
KT → T + N + V
T → una
N → Uzani
V → mkubwa
KT → T + KN_2
T → una
KN_2 → N + V
N → uzani
V → mkubwa
✓ ✓ ✓ ✓ ✓ ✓ ***8 × ½ = alama 4***

g) " Umoja wa Mataifa Barani Afrika," akaanza
✓ ✓ ✓
Mwinyi, "utaimarishwa na viongozi wa
nchi hizi ili tuendeleze maendeleo kupitia
✓ ✓
utandawazi." Akamaliza. ***12 × ¼ = alama 3***

h) Makono ya yale majizi yalikatwa kwa mapanya yenye makali. ***6 × ½ = alama 3***

i) i) Shamirisho ni nomino ambayo inarejelea mtendwa, mtendewa na ala /kitumizi. ***1 × 2 = alama 2***
ii) Buzi - kipozi
Wageni - kitondo ***2 × 1 =alama 2***

j) i) Kuonyesha hali k.m. atakapofika
ii) Kuamrisha k.m. kacheze
iii) Mfululizo wa matendo
iv) Kurejelea mtendaji katika usemi halisi. ***1 × 3 = alama 3***

k) Ulio - kishirikishi kipungufu
Haupendwi - halisi. ***2 × 1 = alama 2***

l) Ki - ngeli ya KI - VI umoja
li - wakati uliopita
cho - kirejeshi
fung - mzizi
ishw - kauli ya kutendeshwa
a – kiishio ***6 × ½ = alama 3***

m) i) Karo - mahali ambapo pamejengwa kwa lengo la kuoshea vyombo / sinki.
ii) Karo - ada ya shule itolewayo na wanafunzi. ***2 × 1 = alama 2***

n) Wao wakimbiapo hawawi wameona hatari.
Wao wakimbiapo huwa hawajaona hatari. ***2 × 1 = alama 2***

o) Angika - angua ***2 × 1 = alama 2***

p) Amkeni ! (Lazima aweke alama ya hisi)
Adhabu
Sarufi - popote patokeapo, usiadhibu zaidi ya nusu alama aliyopata mwanafunzi.
Hijai - makosa - (6 = alama 3)

SEHEMU D : ISIMU JAMII (alama 10)

a) Utaratibu ambao huwawezesha viumbe kupashana ujumbe ambao unahusisha mwasilishi na mpokeaji wa ujumbe.
1 × 2 = alama 2

b) i) Mgusano na ukaribianaji
ii) Mavazi
iii) Sauti

iv) Ishara za mwili. ***zozote 3 × 1 = alama 3***

c) i) Ndoa za mseto
ii) Ujirani wa makabila / mataifa tofauti
iii) Sera za lugha za wakoloni
iv) Sera za lugha za nchi
v) Mavamizi / vita
vi) Dini
vii) Elimu
viii) Umataifa / udiplomasia
ix) Uchumi na biashara
x) Mwingiliano wa watu katika jamii.

TATHMINI YA PAMOJA YA GATUZI LA KERICHO 2015
Cheti cha kuhitimu Elimu ya Sekondari (K.C.S.E)
KISWAHILI
Karatasi 3
JULAI/AGOSTI 2015

1.
a) I. A : Anamtaka mwanfunzi asitusi, asipige kelele awe mpole.
B: Mshauri anamtaka mtu ajiepushe na balaa
II. A: Mwanafunzi asiwe mhuni kuleta huzuni.
B: Mtu aliache jambo linaloweza kuleta huzuni
III. A: Matokeo ya mwanafunzi anayetii ushauri ni mazuri.
B. Lazima kuwe na jibu hata kama litachukua muda. ***zozote 2 × 2 = alama 4***

b) Linganisha
i) Mashairi yote yana vina vinavyotiririka
ii) Mizani ni 16 kila mshororo.
iii) Vipande ni viwili katika kila mshororo.
iv) Mishororo ni minne katika kila ubeti. ***zozote 2 × 1 = alama 2***
Tofauti / ulinganuzi
i) Shairi A halina kibwagizo na shairi B lina kibwagizo.
ii) Shairi A lina beti nne shairi B lina beti tano.

c) Mwanafunzi anakanywa dhidi ya maovu akiwa darasani asianze kusengenya kwani kutamtia mashakani. Mshairi anamuaga mwanafunzi baada ya kumuonya. ***4 × 1 = alama 4***

d) Inkisari - waso badala ya wasio
Tabdila - juwa badala ya Jua.
Mazida - mfahamile badala ya mfahamu
Kuboronga sarufi - kama hilo ukifanya badala ya kama ukifanya hilo.
Lahaja - mawi - mabaya.

e) Mshairi anaonya wanafunzi kama rafiki zake waepukane na mabaya. ***1 × 2 = alama 2***

f) i) Nuksani - balaa /mkosi / kisirani
ii) Malifi - malipo. ***2 × 1 = alama 2***

2.
a) Msemaji - Diwani III
Msemewa - Siki
Mahali - nyumbani kwa Diwani III
Wanazungumza kuhusu uongozi mbaya wa mstahiki Meya.

b) Kinaya - harufi - kupamba mji
Istiara - harufu ni kiwakilishi cha uozo ***2 × 1 = alama 2***

c)- Ufisadi
- Unafiki
- Ubinafsi
- Mauaji
- Ubadhilifu
- Ukatili
- Mapuuza
- Udikteta
- Wizi
- tamaa
- propaganda
- umaskini na njaa
- ukengeushi
- madeni na mikopo ***zozote 6 × 2 = alama 12***

3.- Wanatishia wananchi.
- Wanawahonga wengine - mhubiri
- Wanatenga na kutawala.
- Wanatumia propaganda.
- Wanatumia dini vibaya.
- Wanaua
- Wananyakua ardhi ya umma.
- Wanatumia mali ya umma bila kujali - pesa.
- Wanatumia askari vibaya (vyombo vya dola)

- Wananyanyasa wafanya kazi.
- Wanachukua mikopo bila kujali.
- Wamaekengeuka - hawaonei fahari chochote cha kwao.
- Wanaendeleza ukabila / ufisadi
- Hawajali maendeleo. *zozote 10 × 2 = 20*

4.

i) Ishara ni dokezo linaloelezea kuwepo au uwezekano wa kutokea jambo fulani.
ii) Ndoto zilizomwambia Msoi kwamba pahali walipozoea kwenda yeye na marafiki zake kupitisha wikendi si pahala pa wanadamu hai ni pa wafu.
iii) Picha ya Baa ya makaburini ilikuwa machoni mwake, na akili yake ilishika kumtabiria kitu asichokijua.
iv) Mlangoni alijikwaa na bakuli lake la maua lilivunjika vipande vipande.
v) Alipokuwa akiteremsha miguu, mguu wake wa kushoto ulikosea mizani, akapepesuka na kutaka kuanguka
vi) Alipokuwa akiufunga mlango wa gari alijibana kidole kidogo na kupiga usiahi.
vii) Njiani kulikuwa na mgurumo wa radi na mwanga mwekundu mara moja tu na kisha mvua haikunyesha
viii) Msoi alibadilisha mkao na kutazama kuelekea mavani naye Semkwa akayapa mgongo kinyume cha desturi yao.
ix) Msoi alipozitazama taa zilikuwa na mwako wa huzuni ingawa zilikuwa zimepiganisha rangi kama kawaida.
x) Msoi alikisinzilia kinywaji chake cha maji ya chumvi badala ya kunywa kama wenzake.
xi) Vilevile alikisinzilia chakula na macho yake kila mara akiangalia kule mavani.
xii) Msoi alikataa kucheza na mpenziwe Asha kwa usogora wake wa kila siku. Alimwondosha mwenzake njiani tu.
xiii) Harufu kali ya uvundo ilivamia baa na kuzifurusha zile harufu uzuri za maua na manukato na vyakula.

5.

i) Migogoro ni hali ya kutoafikiana au kutopatana (kati ya) baina ya watu wawili au zaidi au baina ya pande mbili au zaidi; ni kuzozana / kuhitilafiana / kukizana.
ii) Katika hadithi ya Mke wangu kuna mgogoro kati ya msimulizi na mamake kuhusu mke. mamake alitaka kumchagulia Fedhele Salim na Salma Fadhil wawe wachumba wake lakini msimulizi alikataa uteuzi huo na kujichagulia Aziza.
iii) Aziza na mumewe (msimulizi) walikuwa na mgogoro kuhusu kutovaa viatu. Msimulizi alitaka Aziza avae viatu lakini, Aziza alikataa akisema hawezi kutumia ngozi ya ng'ombe aliyekufa.
iv) Aziza alikuwa na mgogoro wa mumewe kuhusu kazi. Mumewe hakuwa na kazi na hakutaka kufanya kazi aliyopendekezewa na Aziza ya kuchoma mihogo. Alidai kuwa hafai kufanya kazi ya aina hiyo kwa vile yeye ni msomi.
v) Aziza pia alikuwa na mgogoro na mumewe kuhusu kufuliwa nguo na kuoshewa vyombo. Aziza alitaka kujifanyia kazi hizo mwenyewe, ilhali msimuliz alitaka afanyiwe kazi hizo na wahudumu.
vi) Aziza anakosa kuafikiana na mumewe kuhusu kutumia burashi na dawa ya kusafisha meno. Alidai kuwa imeundwa kwa manyoya ya nguruwe na hawezi kuitia kinywani mwake. Badala yake alitumia mswaki wa mnazi na kiungo kilichokana na majivu.
viii) Aziza alikuwa na mgogoro na mumewe kuhusu Seluwa. Mumewe na Seluwa walitaniana kwa kuitana 'mke wangu na mume wangu'. Aziza alisema anajuta kuoelewa na msimulizi.

Tazamana na mauti

- Mgogoro wa kibnafsi - Lucy ana tamaa ya kuwa tajiri licha ya kuwa na uwezo -najadili kibinafis njia mbalimbali kufikia utajiri huo.
- Mgogoro wa kimataifa - kupata viza
- Mgogoro kati ya maskini na matajiri / kitabaka
- Migogoro ya kitaifa - vita Somalia - aende kama mkimbizi.

Ndoa ya samani

- Kati ya Abu na mamake Amali kuhusu mahari.
- Mgogoro kati ya babake Amali na Amali kwa kumtaka aolewe haraka.
- Kati ya Amali na Abu-ikiwa mapenzi yao ni dhati au yameongozwa na tamaa.
- Kati ya mamake Amali na babake Amali-mama anakosa kumhusisha babake Amali katika mipango ya ndoa.
- Matajiri na maskini
- Abu na jamaa yake Amali.

Mwana wa Darubini

- Kananda na Bw. Mwatela - ujauzito na kukataa kumwoa.
- Maria na mumewe Mwatela kuhusu ukweli wa mamake mwakitawa.
- Mwatela na kampuni ya Simba Breweries - analewa na kuachishwa kazi.
- Kananda na mwakitawa - mwakitawa anamwona kama jambazi.
- Dereva na kananda - alitoroka baada ya kumuuza Kananda kuwa mtumwa.

6.a) Fahali kula suruali ya DJ - unyanyasaji

- Utandabui - uwezo wa viongozi.
- Kuua tembo kwa ubua - wakuu / viongozi.
- Uchafu mwingi kwenye kasri.
- Uhuru wa kwanza na wa pili.
- Ndege - Kurusha ndege yake kwenye anga ya wenyewe (Amani)

- Chwechwe Makweche - kuitwa 'Horse power'
  Panya - uchafu - maisha 'machafu' ya mtemi.
- Nondo kwenye utandabui - wanyonge kukosa uhuru

b) Sadfa:
Matukio mawili kutokea wakati mmoja bila kupangwa

i) Amani na Imani wanapokutana katika Ziwa Mawewa.
ii) Mtemi anaporejea nyumbai anamfumania Amani na Mkewe kule chumbani mwake.
iii) Ni sadfa kuwa gazeti alilokwa akisoma majisifu lina taarifa ya Chwechwe Makweche ambaye ni nduguye / kakake Imani.
iv) D.J. Anakutana na Imani na Amani kwenye Mto Kiberenge na kuwaelekeza kwa Mtemi Nasaba Bora na magirito waliotaka wafanyakazi.
v) Kupatikana na ajira kwa Nasaba Bora na Majisifu - amani na Imani wanapotafuta kazi - waajiri ni ndugu.
vi) Bi. Zuhura kuwa na chupa za kunyonyeshea wakati Amani anaokota kitoto uhuru mlangoni pake.
vii) Ben-Bella anafika nyumbani wakati Lowela alikuwa ametoweka kutoka nyumbani.
viii) Amani kupatikana barabarani na kupelekwa hospitalini.
ix) Majisifu kuipata barua ya Amani baada ya Imani kuisahau sebuleni.
x) Amani kuomba vitabu vya kusoma kutoka kwa Majisifu na miongoni mwa vitabu hivyo ni '*kidagaa kimemwozea* kilicho sawa na mswada wake.
xi) Majisifu kuenda kumwona Amani hospitalini na siku hiyo Amani anapewa nafasi ya kwenda nyumbani - Majisifu anampeleka kwake.

7.a) Maelezo ya mwandishi.
- Anawarejelea Amani na Imani
- Wameketi kwenye ukingo wa mto Kiberenge.
- Baada ya safari kutoka makwao kuelekea Sokomoko. ***4 × 1 = alama 4***

b)- Uchovu
- Kutembea usiku
- Kutembea mchana kukiwa na jua kali.
- Kulala kichakani.
- Njaa.
- Kiu
- Ukosefu wa fedha.***zozote*** ***6 × 1 = alama 6***

c)- Jazanda ni fumbo - nondo kulingaishawa na wananchi wa tabaka la chini katika riwaya.
- Waafrika Tomoko waliteswa na wakoloni - mashamba na hali nyinginezo - wanapigana na wakoloni - wanaondoka.
- Imani na shida zilizompata kwao Baraka - anaenda Sokomoko.
- Amani - kunyanganywa shamba na babuye kuuawa na Amu Yusufu kutupwa gerezani - anaenda Sokomoko kumtafuta mhini huyo - anampata na kupata mali yake na kumtoa Yusufu gerezani.
- Amani na Imani kukitunza kitoto - kinakuwa kigonjwa kinaaga dunia - wanatupwa gerezani kwa mauaji - wanatetewa - wanatolewa gerezani.
- Madhubuti - utandu wa babake Nazaba Bora - anapotoka Urusi anajinasua kwa kukataa kushiriki ufisadi wa babake.

SEHEMU YA E : FASIHI SIMULIZI

8.a) Maghani ni ushairi ambao hutolewa kwa kalima badala ya kuimbwa. ***2 × 1 = alama 2***

b) i) Ni tungo za kishairi. Yana sifa za kishairi k.m. mapigo ya kimuziki, maneno mateule na muwala. (vina na mizani)
ii) Hasimulia matukio kwa kirefu
iii) Hutungwa papo hapo na kutongolewa mbele ya hadhira.
iv) Hutungwa kwa ufundi mkubwa.
v) Huweza kutolewa na mtu mmoja au kundi la watu.

c) i) Majigambo
ii)
- Hutungwa na kughaniwa na mhusika mwenyewe.
- Hutungwa kwa usanii mkubwa, kutumia sitiari, ishara n.k.
- Hutungwa, kufuatia tukio mahususi katika maisha ya mtunzi.
- Mara nyingi hutungwa na kughanwa na wananume.
- Huwa na matumizi ya chuku. Wahusika hujisifu kupita kiasi.
- Hutolewa kwa nafsi ya kwanza.
- Anayejigamba hubeba vifaa vyake vya kazi.
- Hutungwa papo hapo.
- Anayejisifu hutaja usuli wake wa kinasaba.
- Wanaojigamba huwa walumbi
- Maudhui makuu ni ushujaa. ***zozote 4 × 2 = alama 8***

iii) i) Taswira - kucheza naye, mabini kumiminizwa
ii) Jazanda - Gozi kusakata nami

iii) Takriri - ndimi, dume. ***3 × 1 = alama 3***

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA KAUNTI YA BUSIA
102/1
KISWAHILI
Karatasi 1
(Insha)
Julai/Agosti 2015

1. Wewe ni mkurugenzi wa masuala ya elimu katika kata yako. Umeombwa na Wizara ya Elimu kuandika ripoti kuhusu sababu za kudorora kwa matokeo ya mitihani katika eneo lako. Andika ripoti yako.
2. Baadhi ya shule katika kaunti yako zimekumbwa na mikasa ya moto hivi karibuni. Pendekeza hatua ambazo wasimamizi wa shule wafaa kuchukua ili kukabili tatizo hili.
3. Andika insha itakayodhihirisha ukweli wa methali.
   Ndugu mui heri kuwa naye.
4. Andika insha itakayomalizikia kwa maneno yafuatayo :
   ... nilitanabahi kuwa mchumia juani hulia kivulini. Ndugu yangu alikuwa ametulia chumbani mwake akiwa na furaha riboribo.

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA KAUNTI YA BUSIA
102/2
KISWAHILI
Karatasi 2
Julai/Agosti 2015
UFAHAMU

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Tatizo la *dawa za kulevya* ni moja kati ya matatizo makuu katika jamii zetu. Pombe, ambayo inaweza kujumlishwa katika kundi pana la dawa za kulevya, imetumiwa kama burudani katika jamii kwa kipindi kirefu sana. Katika jamii *za zama za leo,* kuna *shinikizo za kijamii* na kitamaduni ambazo zinawafanya watu wengi kuishia kuitumia pombe au bia na kuvuta sigara. Ikiwa utumiaji wake unaathiri anayehusika pamoja na jamii yake, basi pana sababu kubwa ya kulishughulikia suala hili.

Sote tunafahamu kuwa dawa huwa na mchango mkubwa wa kimatibabu. Lakini ikiwa dawa zimetumiwa kwa sababu ambayo haihusiani na matibabu au kwa njia mbaya, huwa na matokeo mabaya. Chanzo kikuu cha kutumia dawa vibaya ni kuzipata athari fulani zinazohusishwa na dawa zinazohusika. Matumizi ya aina hii huweza kusababisha utegemeaji wa dawa kiasi kwamba mtu hawezi kutenda kazi fulani pasi na kuzitumia dawa zinazohusika. Utegemeaji huu wa dawa unaathiri mwili wa anayehusika na jinsi unavyofanya kazi. Kisaikolojia au kiakili anayehusika huweza kuzitegemea dawa kiasi kwamba hawezi kufanya lolote *pasi* na kuzitumia dawa fulani.

Miongoni mwa watu wanaoathrika kwa kiasi kikubwa na tatizo la dawa za kulevya ni vijana. Kwa nini vijana wanaathirika kiasi hiki? Utumiaji wa dawa za kulevya unawavuta vijana ambao wamo katika harakati za kuwa huru na *kuusaka ujitambuaji.* Baadhi yao wanaelekea kuamini kuwa dawa hizi zitawapa sifa muhimu za kujitambua kama ujasiri, kujiamini, hisia za kuwa huru na kadhalika. Asilimia kubwa ya vijana katika nchi nyingi zinazoendelea na zilizoendelea *wamezongwa* na tatizo hili. Ikiwa asilimia kubwa ya vijana itaathirika, basi pana hatari kubwa ya jamii za ulimwengu kuvipoteza vizazi vya kesho. Suala la dawa za kulevya sio tatizo la nchi zilizoendelea tu wala tatizo la maeneo ya mijini tu. Hili ni tatizo ambalo *linasambaa* kila sehemu kwa kasi ya ajabu sana.

Nchi zinazoendelea zinaaathirika zaidi kwa kuwa maendeleo yao yanakitegemea kizazi cha vijana. Ni katika hali hii ambapo elimu ifaayo ni muhimu ili kusaidia kuwaelimisha wanaohusika pamoja na jamii nzima.

Moja kati ya sababu kuu zinazochangia kuweko kwa tatizo la utumiaji mbaya wa dawa ni kuvunjika kwa muundo na mshikamano wa kijamii ambao ni msingi muhimu sana. Ikiwa msingi huu uliotegemewa na wanajamii umevunjika, kuna uwezekano kuwa baadhi ya wanajamii watashindwa kukabiliana na hali yao mpya. Hawa watajaribu kusaka kimbilio fulani kwenye dawa za kulevya. Hii kwao inakuwa kama

njia ya *kujipumbaza* na kujihakikishia kuwa wanaweza kuikabili hali hii mpya. Katika mataifa mengi, kuna uhamaji mkubwa wa watu kutoka maeneo ya mashambani hadi mijini. Asilimia kubwa ya watu hawa wanakabiliana na matatizo mengi wanapoingia mijini. Matatizo haya ni kama *ukosefu wa ajira,* malazi, chakula na mahitaji ya kimsingi. Pili, wanakumbana na tatizo la *ukiwa* na upweke wa kutengana na jamaa zao waliowasaidia kupambana na hali za maisha. Tatu, wanakumbana na hali ambazo hawakuzizoea katika utamaduni walimokulia. Matatizo yanayohusiana na *ulimbukeni* huo wa maisha ya mjini yanaweza kumtosa mtu kwenye dawa za kulevya.

Je, matumizi ya dawa za kulevya yanaiathiri vipi jamii? Jambo lakwanza ni kutambua kuwa suala la dawa za kulevya ni *tanzia* ya kijamii. Hili silo tatizo ambalo limetengewa *sehemu finyu za jamii;* linaiathiri jamii nzima. Hili silo tatizo la 'rnitaani' tu bali limeziathiri jamaa, maeneo ya kazi, shule na taasisi nyingine zozote. Ni tatizo ambalo linawaathiri watu wa kila umri, kuanzia vijana wa shule hadi watu wazima.

Katika kiwango cha jamaa, matumizi ya dawa za kulevya yanauathari ushikamano na umoja wao. Watumiaji wa dawa za kulevya *wanazugwa na kurengwa* na tabia yao kiasi kwamba haja za watu wengine sio muhimu kwao. Anayehusika anaathirika kiafya na kisaikolojia. Jamaa yake nayo inateseka kumwona mwenzao akiangamia kutokana na kuzitegemea dawa za kulevya. Ikiwa wanaotumia dawa za kulevya ni watu wazima, pana uwezekano watoto wakaishia kuamini kuwa kutumia dawa hizo ni jambo la kawaida na linalofaa. Utumiaji wa dawa za kulevya unaweza pia kuiingiza jamaa inayohusika kwenye matatizo ya uhalifu. Mtumiaji aliyerengwa na dawa za kulevya huwa tayari kufanya lolote lile ili apate pesa za kununulia dawa hizo.

Katika kiwango cha shule, dawa za kulevya huwaathiri vijana vibaya sana. Kwanza, huathiri ukuaji wa kijana anayehusika. Dawa hizi huua seli za ubongo na kuathiri uwezo wa mwanafunzi wa kuweza

kuyafuatilia masomo yake vizuri. Pili, kutegemea dawa za kulevya huweza kuathiri ukuaji wa kawaida wa mwili. Tatu, ukuaji wa kimaadili wa mwanafunzi unaharibika. Dawa za kulevya zinaathiri tabia za wanaohusika na kuwapa hisia ambazo haziwezi kuifaidi jamii. Nne, matumizi ya dawa za kulevya huathiri uwezo wa mwanafunzi kimasomo. Tano, matumizi ya dawa za kulevya shuleni yanachochea kuwapo kwa matendo hasi yanayohusishwa nayo. Matendo haya ni: wizi, uhalifu, ukahaba, unyang'anyi, utovu wa nidhamu na uuzaji wa dawa zenyewe. Jamii yoyote inayotaka kuendelea haina budi kuzipiga vita dawa za kulevya.

a) Mwandishi anasema pombe huweza kuwa dawa za kulevya. Hii hutokeaje ? (alama 1)
b) Dawa ya kawaida inawezaje kugeuka kuwa dawa ya kulevya ? (alama 2)
c) Ni sababu zipi zinazowavuta vijana kutumia dawa za kulevya ? (alama 4)
d) Kuvunjika kwa muundo wa kijamii kunachangiaje matumizi ya dawa za kulevya. (alama 2)
e) Eleza jinsi jamii inavyoathiriwa na matumizi ya dawa za kulevya. (alama 3)
f) Eleza maana ya misamiati hii kama ilivyotumiwa katika kifungu. (alama 3)
   i) Ulimbukeni
   ii) Linasambaa
   iii) Wamezongwa

2. UFUPISHO

Mwezi jana, Serikali ya kitaifa na zile za kaunti ziliwasilisha makadirio yao ya bajeti, miezi miwili kabla ya mwaka wa kifedha kuisha kama zinavyohitajika na katiba. Serikali hizo zilieleza jinsi zinavyonuia kutumia mabilioni ya pesa kufadhili shughuli zao mwaka ujao wa kifedha wa *2013/2014.*

Serikali ya Rais Uhuru Kenyatta ilisema itatumia Shilingi 1.6 trilioni kufadhili maendeleo na shughuli za sekta na idara zake tofauti. Makadirio haya ambayo yaliwasilishwa na kiongozi wa walio wengi bungeni, Bw Aden Duale. Hata hivyo yalikosa kueleza jambo moja muhimu - jinsi kit ita hicho kitakavyopatikana. Nasema hivi kwa sababu kuna habari ambazo zimenipa tumbojoto na wasiwasi mkubwa. Imebainika kuwa kufikia mwishoni mwa Machi mwaka huu, Kenya ilikuwa inadaiwa Shilingi 1.8 trilioni na wafadhili wa humu nchini na wa kigeni.

Kama habari hizi hazijakushtua sitakulaumu kwa sababu huenda ukawa hujui ukubwa wa kiasi hiki cha fedha. Ili uweze kuelewa, nitazigawanya fedha hizi miongoni mwa Wakenya milioni 40 ili tujue kila

mkenya anadaiwa kiasi gani. Kila Mkenya nchini, wakiwemo watoto na wazee wakongwe, anadaiwa Shilingi 45,000! Hivyo basi ili deni hili liweze kulipwa, kila Mkenya atalazimika kutoa kiasi hicho cha fedha.

Ni deni ambalo Rais Uhuru Kenyatta alirithi kutoka kwa mtangulizi wake, Rais Mwai Kibaki ambayo utawala wake ulivunja rekodi ya kukopa. Wahenga hawakukosea waliposema dawa ya deni ni kulipa. Deni hili linapaswa kumkosesha usingizi Rais Kenyatta ambaye anapaswa kutafuta njia za kulilipa bila kuathiri uchumi, maendeleo na utekelezaji wa ahadi nyingi alizowapatia Wakenya wakati wa kampeni.
Hili halitafanyika kama Serikali itatenga fedha nyingi kuwalipa maafisa wake mishahara na marupurupu minono pamoja na kuwapa mabilioni ya pesa kununulia magari ya kifahari. Pengine Rais hajafahamishwa kuwa mwaka ujao wa kifedha Serikali itajipata pabaya kwani Halmashauri ya Ukusanyaji Ushuru nchini (KRA), haitaweza kukusanya kiwango kilichowekewa na Serikali baada ya shughuli ya ukusanyaji ushuru kutatizwa na hofu iliyotanda wakati wa uchaguzi mkuu.

KRA ilikuwa imekusanya Shilingi 560 bilioni kufikia mwishoni mwa Machi ilhali ilikuwa imeagizwa kukusanya Shilingi 881 bilioni.

Serikali za kaunti, ambazo zingali changa, zimependekeza kutumia mabilioni ya fedha ambazo hazitaweza kukusanya. Badala yake zimeiomba Serikali kuu ijaze pengo hila au zipewe idhini ya kukopa. Rais Kenyatta hana budi kuchukua hatua za dharura kuhakikisha kuwa Wakenya hawataendelea kuandamwa na madeni maishani mwao.
(Imenukuliwa kutoka *Taifa Leo* - Mei 9, 2013)

a) Kwa maneno yasiyozidi 70, fupisha aya za kwanza nne. (alama10)
Matayarisho
Jibu

b) Kwa nini serikali haitaweza kulipa madeni yake. (Maneno 40-50) (alama 5)
Matayarisho
Jibu

3. MATUMIZI YA LUGHA

a) Nini maana ya mofimu. (alama 1)
b) Kwa kutumia mifano onyesha aina mbili za mofimu. (alama 2)
c) Tunga sentensi kwa kutumia kiunganishi, mingairi ya (alama 1)
d) Bainisha vitenzi katika sentensi :
Mtoto wake amekuwa mtukutu ingawa hiyo ni tabia ya babake. (alama 2)
e) Kanusha :
Kwenda kwake kazini mapema kulimfanya apandishwe cheo. (alama 2)
f) Tunga sentensi moja kuonyesha tofauti kati ya Guna na Kuna. (alama 2)
g) i) Ni nini maana ya sentensi agizi. (alama 1)
ii) Tunga sentensi moja agizi. (alama 1)
h) Iandike sentensi hii upya kwa kutumia visawe vya maneno yaliyopigiwa mistari.
Majasusi walifika soko ya Tumaini kabla ya ziara ya Rais. (alama 2)
i) Tambua ngeli za maneno yafuatayo : (alama 1)
Ulezi .
Jozi .
j) Bainisha matumizi mawili ya ritifaa. (alama 2)
k) Eleza tofauti kati ya shadda ya kiimbo. (alama 2)
l) Iandike sentensi hii upya kwa kutumia O-rejeshi tamati.
Maua ambayo yanapaliliwa hurembesha bustani hii. (alama 1)
m) Andika ukubwa wa : (alama 1)
Bawabu alimuua mwizi kwa kisu
n) Nini maaan ya kishazi. (alama 1)
o) Bainisha vishazi katika sentensi hii :
Imani alifanya mtihani ingawa alikuwa mgonjwa. (alama 2)
p) Sahihisha kuonyesha uwezekano.
Wangelikuwa na pasipoti wangelisafiri nje ya nchi. (alama 2)
q) Unda kitenzi kutokana na nomino mlo kisha uonyeshe mzizi wake. (alama 2)
r) Tunga sentensi ukitumia kihusishi cha kulinganisha. (alama 1)

s) Changanua kwa kutumia jedwali.
Wazazi wengi sana waliofika shuleni mapema / walileta vyakula vingi mno. (alama 4)

t) Andika katika usemi wa taarifa :
"Mbona unamfanyia karaha mwenzako? Je, utaenda kumwomba radhi ?" Amina aliuliza.

u) Kaa ina maana ya keti. Andika maana zingine tatu. (alama 3)

4. ISIMUJAMII : (ALAMA 10)

a) Taja na ueleze shughuli zozote tano zilizochangia kuenea kwa Kiswahili nchini Kenya kabla ya uhuru.

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA KAUNTI YA BUSIA
102/3
KISWAHILI
Karatasi 3
Julai/Agosti 2015

Ken Walibora na Said A. Mohammed : Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine

1. **Lazima**
Wanaume katika jamii wamesawiriwa kwa uhasi. Jadili ukweli wa kauli hii kwa kurejelea hadithi zozote tano katika diwani na Damu Nyeusi na Hadithi nyingine.
(alama 20)

Timothy Arege : Mstahiki Meya

2. "Siyo kama zamani tena. Cheo kinaweza kumlevya mtu asahau alipokuwa jana. Ni kama mtoto na chakula."
a) Andika muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Taja mbinu mbili za lugha ambazo zimetumiwa katika dondoo.
(alama 2)
c) Fafanua sifa nne za mzungumzaji. (alama 4)
d) Thibitisha kutoka tamthilia ukweli kuwa cheo kinaweza kumlevya mtu.
(alama 10)

Au,

3. Eleza jinsi mwandishi alivyotumia mbinu zifuatazo kufanikisha tamthilia yake :
a) Majazai
(alama 5)
b) Kinaya (alama 8)
c) Jazanda
(alama 7)

Ken Walibora : Kidagaa Kimemwozea

4. "Katika hadithi yako usiniweke pembeni kama tanbihi, mimi na wanawake wenzangu ..."
a) Andika muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Elesa sifa nne za mzungumzaji.
(alama 4)
c) Onyesha jinsi wahusika wa kike walivyowekwa pembeni riwayani. (alama 12)

Au

5. Hatuwezi kuwa binadamu endapo hatuwaoni walemavu kama wenzetu. Eleza mtazamo wa wahusika wafuatao kuhusu walemavu.
i) Dora (alama 4)
ii) Imani (alama 4)
iii) Mashaka (alama 4)
iv) Mtemi Nasaba Bora (alama 4)
v) Mwalimu Majisifu (alama 4)

FASIHI SIMULIZI

6. **Soma utungo huu kisha ujibu maswali.**
Ndimi kisoi, duma la ukoo mtukufu
Ulojipambanua kwa mabingwa
Wachezaji hodari nwa ngoma
Ndimi dume lililoingia nyanjani
Makoo yakatetemeka
Yakan'gang'ania, gozi kusakata nami

Kijiji kizima kilinijua
Wazee walinienzi
Wakamiminika kiamboni
Mabinti kunikabidhi
a) Masimulizi haya yanapatikana katika utanzu gani wa fasihi simulizi ?
(alama 1)
b) Taja kipera kinachohusika katika masimulizi haya. (alama 1)
c) Eleza sifa za kipera hiki. (alama 8)

d) Fafanua umuhimu wa kipera hiki katika jamii.

Au

7. **a)** Eleza changamoto tano zinazoukabili ukusanyaji wa uhifadhi wa fasihi simulizi.
   b) Jadili njia zozote tano ambazo jamii ya kisasa hutumia ili kudumisha fasihi simulizi.
   (alama 10)

USHAIRI

8. **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Chema hakidumu, kingapendeza,
Saa ikitimu, kitakuteleza,
Ukawa na hamu, kukingojeleza,
Huwa ni vigumu, kamwe hutaweza

Chema sikiimbi, kwamba nakitweza,
Japo mara tumbi, kinishaniliza,
Na japo siombi, kipate n'ongeza',
Mtu haniambi, pa kujikimbiza.

Chema mara ngapi, kin'niondoka,
Mwanangu yu wapi ? Hakukaa mwaka,
Kwa muda mfupi, aliwatilika,
Ningefanya lipi, ela kumzika ?

Chema wangu babu, kibwana Bashee,
Alojipa tabu, kwamba anilee,
Na yakwe sababu, ni nitengenee,
Ilhali wahhabu, mara amtwee

Chema wangu poni, kipenzi nyanyangu,
Hadi siku hini, yu moyoni mwangu
Yu moyoni ndani, hadi kufa kwangu,
Ningamtamani, hatarudi kwangu

Maswali

a) Eleza bahari mbili zinazojitokeza katika shairi hili. (alama 2)
b) Lipe shairi hili anwani mwafaka. (alama 2)
c) Onyesha matumizi ya uhuru wa ushairi.
(alama 2)
d) Eleza toni ya shairi hili.
(alama 2)
e) Eleza umbo la beti mbili za mwisho. (alama 4)
f) Eleza aina mbili za urudiaji katika shairi hili. (alama 4)
g) Fafanua msamiati huu kama ulivyotumiwa katika shairi hili :
(alama 4)
   i) kitakuteleza
   ii) kinshaniliza

GATUZI LA BUSIA
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
HATI YA KUHITIMU ELIMU YA SEKONDARI KENYA
KISWAHILI
Karatasi - 102/1
JULAI/AGOSTI 2015

SWALI 1: Mwanafunzi aandike sura ya ripoti rasmi /maalum
Kichwa cha ripoti
Kioneshe jopo linalotayarisha ripoti/ripoti inahusu nini, na mahali palipotokea jambo hilo. Mfano:
RIPOTI YA TUME YA ELIMU KUHUSUKUDORORA KWA MATOKEO YA MITIHANI KWENYE KATA YA MAJENGO

- **Utangulizi**
  Katika hatua ya utangulizi mtunzi aeleze kwa muhtasari madhumini ya ripoti na aliueteua jopo hilo. Aidha ataje wanajopo na nyadhifa zao.
- **Utaratibu**
  Mtunzi aoneshe ni utaratibu gani aliyoutumia katika kukusanya habari
- **Matokeo ya uchunguzi**
  Huu ndio mwili wa ripoti. Mtunzi aandike mambo muhimu/maudhui chini ya vichwa vidogovidogo.
- **Hitimisho**
  Katika kuhitimisha ripoti, mtunzi aweza kurejeleamambo muhimu katika matokeo kasha aonyesha msimamo wake msimamo na baadaye mapendekezo yake.
- **Mapendekezo**
  Mtunzi atoe mapendekezo yake kwa njia yakuorodhesha. Mapendekezo katika swali hili yaweza kuwa njia zinazoweza kusaidia kuimarisha matokeo.
  Baada ya mapendekezo mtunzi aandike au aonyeshe ripoti imendikwaa na nani, cheo chake na tarehe na mahali ripoti hiyo iliandikwa.

Baada ya hoja za swali
- Uzembe wa wanafunzi
- Kuzembea kwa walimu
- Ukosefu wa walimu
- Ukosefu wa vitabu
- Kukamilisha silabasi (walimu na wanafunzi)
- Ukosefu wa miundo msingi
- Wanafuzi wengi kupita kiasi madarasani
- Wanafunzi kufukuzwa shuleni mara kwa mara kwa sababu ya karo

Swali:2
Mwanafunzi aeleze njia kabambe za jinsi ya kukabiliana na moto kama vile:
- Mafuta kuwekw mbali na majengo
- Wanafunzi kutoruhusiwa kutumia mishumaa shuleni
- Meko kuwekwa mbali na madarasa na mabweni
- Uchomaji taka kufanywa kwa uangalifu
- Madarasa na mabweni kuwekewa vifaa vya kuzimia moto
- Vifaa vya stima kukaguliwa kila wakati n.k

SWALI 3:
Mwanafunzi aandike kisa kinachoonyesha kuwa...
- Kuwa na ndugu hata kama ni mbaya bora kuliko kukosa kabisa. Ndugu huyu aonekane mbaya lakini wakati fulani aje amfae.

SWALI 4:
- Mwanafunzi aonyesha kuwa mtu akifanya kazi kwa bidii hufanikiwa. Amalize kisa chake kwa maneno haya.

GATUZI LA BUSIA
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
hati ya kuhitimu elimu ya sekondari kenya
KISWAHILI
Karatasi - 102/2
JULAI/AGOSTI 2015

UFAHAMU: (ALAMA 15)

a) Pombe ikitumwa sana hivi kwamba utumiaji wake unaathiri anayehusika pamoja na jamii yake.1x1=1
b) Hapo ni iwapo dawa hiyo itatumiwa kwa sababu ambayo haihusiani na matibabu au kutumiwa kwa njia mbaya.
c)
- Baadhi ya vijana kuamini kuwa dawa hizo zitawapa sifa muhimy za kujiambua, k.m ujasiri, kujiamini na hisla za kuwa huru.
- Vijana kuwa katika hali ya kuwa huru na kutafuta kutambulikiwa. 2x2=4

d)
- Baadhi ya wanajamii wanashindwa kukabiliana na hali yao mpya.
- Juhudi za kutafuta kimbilio zinawatosa wanajamii kwenye dawa za kulevya. 1x2=2

e) Kuvurugwa kwa ushikamano na umoja wa jamii.
- Watu kupuuza haja za wengine. Jamaa yao huteseka.
- Afya na saikolojia ya mtumiaji kuathirika
- Uwezo wa kimasomo unakwenda chini 3x1=3

f) i) Hali ya kufahamu vizuri mambo fulani
ii) Linaenea, linazagaa, linatapakaa
iii) Wamezungukwa na matatizo, wamezidiwa wamekabwa. 3x1=3

2) SEHEMU B: UFUPISHO
- Serikali kuwasilisha bajeti
- Kueleza jinsi mabilioni, yalivyotumiwa
- Serikali/ya Kenyatta kusema itatumia 1.6trilioni kwa maendeleo.
- Makadirio kuwasilishwa na kiongozi wawalio wengi mbungei.
- Kukosa kueleza jinsi ya kupata kitita hicho
- Habari hizi kunipa wasiwasi.
- Kenya kudaiwa shilingi 1.8 trillioni na wafadhili
- Kutolaumu wale wasioelewa ukubwa wa deni hili.Kugawanya deni hili kwa wakenya wote
- Kila Mkenya kudaiwa shilingi 45000
- Kenyatta kurithi deni kutoka kwa kibaki
- Deni kumkosesha usingizi Rais
- Kutafuta njia ya kulipa bila kuathiri uchumi .Zozote 9x1=9
Mtiririko1

b)
- Serikali kutenga fedha nyingi kwalipa wafanyhikazi
- KRA kutokusanya kiwango kinachohitajika
- Ukusanyaji wa ushuru kukatizwa na hofu wakati wa uchunguzi
- Serikali za Kuwait kupendekeza mabilioni ambayo hawana.

3. **MATUMIZI YA LUGHA**
– Kipashio kidogo cha sarufi chenye maana.

b)
– Mofimu huru-Baba, Mama, mimi (kadiria)
– Mofimu tegemezi- mtoto, piga (kadiria) 1x2=2

c) Mbali ya, bila kujali bila
d) Amekuwa- kitenzi kishirikishi kikamilifu
– Ni- kishirikishi kipungufu 1x2=2
– Amekuwa - kitenzi kishirikishi kikamilifu
– ni- kishirikishi kipungufu 1x2=2

e)
– Kwenda kwake kazini mapema hakukumfanya apandishwe cheo 2x1=2
–

f)
- Kuna kwangua, kwaroza
- Guna- nzito, terema 1x2=2

g) Sentensi inayomtaka msikilizaji afanye jambo fulani
-Ni ya kuamrisha na haina sehemu ya kiima 1x1=1
ii) Ingia ndani! Nioo hapa!
-Kaa chini 1x1=1mk

h)
- Majasusi - Makachero, wapelezi
- Soko- gulio, chete 1x2=2

U- YA
LI-YA

j)
- Kuonyesha sati ng'ong'o m,f Ng'ombe
- Kuonyesha sehemu ya neno iliwachwa m.f takua
- Kuonyesha shadda m.f kitabu

k) Shada ni nguvu katika kutamka sauti au silabi fulani
- Kiimbo ni kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti. 1x2=2

l)
- Maua yapaliliwayo hurembesha bustani hii 1x1=1
- Jawabu liliiua jizi kwa jisa

n)
- Fungu la maneno lenye muundo wa kiima ama kiarifa na ambalo limo ndani ya sentnsi 1x1=1

o)
- Imani alifanya mtihani -kishazi huru
- Ingawa alikuwa mgonjwa- kishazi tegemezi 1x2=2

p) Wangekuwa na pasipoti wangesafiri nje ya nchi 2x1=2

q)
- Mlo -la
- Mzizi -1-

r)
- Kuliko, kama
- Simba ni mkali kuliko chui (kadiria) 1x1=1

s)

S								
KN					KT			
N	V	E	S	T	KN			
Wazazi	Wengi	Sana	Waliofika shuleni mapema		Walioleta	Vyakula	Vingi	Mno

t) Amina alimuuliza ni kwa nini alimfanyia mwenzake karaha na kutaka kujua iwapo angeenda kumuomba radhi.

u)
- Kipande cha ukuni kilichochomwa
- Mnyama mdogo wa majni
- Tumika kwa muda mrefu
- Pendeza

4.
- Biashara - Kiswahili kilifanywa lugha ya biashara kati ya pwani na bara.
- Sera ya lugha- Kiswahili kilifanywa lugha ya taifa nchini Kenya na Tanzania.
- Dini - Kiswahili kilitumika kusambaza dini za Uisilamu na Ukristo.
- Elimu - Wamishenari walitumia Kiswahili kufundisha, kuandika, kusoma, kuhesabu na kazi mbalimbali za ufundi.
- Utawala wa kikoloni- Sera ya lugha ya wajeremani nchini Tanganyika ilisisitiza matumizi ya Kiswahili.

- Vyombo vya habari- magazei mengi ya Kiswahili yalizuka nyakati za ukoloni.
- Siasi- Wahusika wengi katika vita vya ukombozi nchini Kenya na Tanzania walitumia Kiswahili kama lugha ya mawasiliano.
- Hisia za utaifa miongoni mwa viongozi na wananchi
- Utafiti - kina madam, Steere na Krapt walifanya utafiti wa kina kuhusu Kiswahili na hata kuandika vitabu.
- Tamasha mbalimbali za muziki, drama na mashairi
- Uchapishaji wa vitabu, magazeti na majarida ya Kiswahili 5x2=10

GATUZI LA BUSIA
MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
HATI YA KUHITIMU ELIMU YA SEKONDARI KENYA
KISWAHILI
Karatasi - 102/3
JULAI/AGOSTI 2015

FASIHI

1. Maelezo: Kauli hii inamaanisha kuwa wanaume wamechorwa kwa njia mbaya au watende maovu katika jamii.
   i) Katika hadihi ya samaki wa nchi za joto, wanaume wamejitokeza kama.

a) Wakatili-Peter haathiriki kwa vyovyote vile kihisia wakati anapoelezwa na Christiane kuhusu kuavya mimba.
   Hamhurumii Christine, badala yake anamuuliza kama anataka pesa.
b) Ni wakware- Ingawa Peter alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Christine, bado anaonekana akiandamana na wanawake wengine kama yule waliyeandama kule Entebbe Sailing Club na wengine wengi waliomtembelea kwake (kwa mujibu wa Deogracius).
c) Wenye taasubi -Peter anawaona wanawake kama vyombo vya kutimizia ashiki zake. Ndiyo maana Christine alipomtebelea kwake kwa mara ya kwanza, alimpa pombe kisha akamwongoza kwenye chumba cha kulala.
d) Ni wapunjaji /wanyonya -Peter anawaponya wavuvi. Ananunua samaki wa nchi za joto kwa bei rahisi kutoka kwao na kuuza kera bei ya juu katika nchi za ng'ambo.
e) Ni walaghai/matapeli -Sunjah Patel anamlaghai mwenzake Jagjit kwa kumuuzia dola bandia za Marekani.
f) Ni wasaliti- Mr Peter anasaliti Christine na pia mapenzi yao kwa kujihusisha katika mapenzi na wanawake wengine.
g) Wenye dharau -Peter anadharau nchi ya Christine kwa kusema ina mkahawa mmoja tu wa kichina, Imejaa wadudu na malai hutengenezwa kwa namna iliyo duni.

ii) Katika hadithi ya Damu Nyeusi, wanaume ni:

a) Wasaliti- Bob, aliye mwafrika kama alivyokuwa fikirini, alisaliti fikirini kwa kumnyanyasa badala ya kumsaidia.
b) Wenye dharau- Bob alimdharau Fikirini kwa kumwita tumbiri na kushangaa mbona hakubakia kwao kwenye uchawi na ushirikina.
c) Wahalifu - Bob anashirikiana na Fiona katika kumwibia Fikirini na kutishia kumuua.
d) Wabaguzi- Bob anambagua Fikirini na Waafrika wengine kwa kuwaita tumbiri na waafrika wengine kwa kuwaita tumbiri na wachawi.

iii) Hadithi ya mke wangu

a) Wanaume ni wazembe- msimulizi hakufanya kazi yoyote. Aliamka tu na kujirembesha kisha kutembea temea tu.
b) Wabinafsi- msimulizi alitaka mke ambaye angemvumbika mwenyewe hadi aive. Hakujali kuhusu hisia za mke ambaye angemuoa, bora awe wa kumtimizia mahitaji yake.
c) Wenye Taasubi - Msimulizi anachukulia mwanamke kama kiumbe wa kutimiza mahitaji yake. anasema alitaka msichana mbichi ambaye angemvumbika mwenyewe. anawaona wanawake kama watoto wadogo.
d) Wabaguzi na wenye dharau - Msimulizi anambagua bazazi muuza madafu. Anakasirika Aziza anapomkarisbisha aingie nyumbani mwao.

iv) Hadithi ya kikaze

a) Wasaliti - Bwana mtajika anasaliti jamii kwa kumkubali mkwewe ashike kikaza kinyume na itikadi ya jamii.
b) Bwana machupa alisaliti wananchi wenzake kwani ndiye aliyotoa siri za mikutano na mipango ya wananchi kwa Bwana mtajika.

c) Viongozi wabaya- Bwana mtajika ameshindwa kuongoza kijiji cha Tekede vyema na ndio sababu wanakijiji wanamwondoa mamlakani.
d) Wezembe/Watepetevu- Kila mara bwana mtajika alikuwa ndotoni. Alikuwa mzembe na hakujua yaliyokuwa yakiendelea katika kijiji chake cha Tekede.
e) Wanafiki-Bwana machupa alijifanya rafiki wa wananchi wenzake walipozugumzia maswali yaliyowaathiri lakini kumbe alikuwa kibaraka wa Bw Mtajika.
f) Waongo -Bwana mtajika angebadilisha uongo kuwa ukweli ili achanguliwe kama kiongozi

v) Maeko

a) Walevi - Duni alikuwa na tabia ya kulewa sana.
b) Wakatili- Duni alimpiga mkewe kila alipolewa.
c) Wasaliti -Salim anamsaliti rafikiye , duni kwa kumchumbia mkewe, Jamila
d) Wenye taasubi- Duni anampiga mkewe na anapolewa, anamsuta Jamila katika taarabu njia yake.

TanBihi
Hadithi zozote 5
Kutaja hadithi - alama moja
Kueleza mifano yoyote mine katika kila hadithi - Alama 4.
Wahusika sahihi watajwe katika kila hadithi.
Mwanafunzi anayetoa maelezo ya jumla bila kutaja wahusika maalum wasituzwe.

2. (a)

- Maneno yalisemwa na Diwani III
- Anamwelezea Siki
- Ni nyumbani kwa Diwani wa III, alasiri
- Siki Alikuwa amemtembelea Diwani III ili kuzungumza naye kuhusu matatizo yanayowakumba wafanyakazi.

4x1=4

b) i) Tashhisia-Cheo kulevya
ii) Tashbihi-Kama mtoto na chakula 2x1=2 (za kwanza mbili)

c) **Diwani wa III**

- Mwenye msimamo thabiti- Hakushawishiwa na Meya kuwasaliti watu waliomchagua
- Mzalendo - Alipigania haki za wafanyikazi
- Jasiri- Hakuogopa kumweleza Meya ukweli.
- Mwenye kuwajibika - Alifanya kazi yake vizuri.
- Mpenda usawa- Alitaka nyongeza ya mishahara ifanyike kwa wote.
- Mwenyewe utu-Anajali maslahi ya wafanyikazi.
- Mshauri mwema-Alishauri Meya asiongeze mishahara ya madiwani pekee. 4x1=4 (za kwanza nne).

Tanbihi: Mwanafuzi atoe sifa katika hali yakinishi.

d) **Meya na madiwani walilewa vyeo kwa njia zifuatazo.**

- Walipuuza matakwa ya wafanyakazi, ikiwemo kukutana nao.
- Wanadanganya bila hofu yoyote. Meya anasema dawa zingefika katika muda wa siku tatu.
- Wanaendeleza ufisadi - Wananyakua vipande vya ardhi na kuviuza. Wanapanga na kuuza fimbo ya Meya bila hofu yoyote.
- Walijaa kiburi- Meya anasema wananchi wangemchagua tena angetaka.
- Meya alichagua washauri ambao wangemuunga mkono na kutenga watu kama vile Diwani III. Pia alimteua Bila kuwa mshauri wake na kumlipa kwa fedha za umma.
- Meya na washauri wake hawajali wafanyikazi wanachelewesha mishahara yao mbali na mishahara hiyo kuwa duni wanaogeza washauri na Askari mishahara pekee.
- Wamekosa utu- Meya andai kuwa mtoto akifa ni mmoja tu na cheno ina watu wengi.
- Meya na washauri wake wamesorotesha uchumi. Wanaongeza madiwani mishahara kiholela. Madiwani wanaamua kutolipa kodi.
- Meya anatuma mbinu mbaya za utawala kama vile tenga- utawale. Alimtenga Diwani III.

Hoja zozote 5x2=10

3 **a) Majazi**

- Cheneo ni kitu kilichoenea au kilichotapakaa kila mahali. Kwa kurejelea tamthilia, mambo mengi yameenea katika mji wote kama vile ufisadi, migomo, umaskini, magonjwa, udhalimu wa viongozi na mafunzo.

- Mstahiki Meya- Stahiki ni kuwa na haki ya kuwa na au kupata kitu au jambo Fulani. Mstahiki ni mtu anayestahili heshima. Meya ni mwenyekiti wa halmashauri ya mji mkubwa. Kwa kawaida, mtu kama huyu hustahili heshima. Hata hivyo meya hastahili heshima yoyote kwa sababu badala ya kuwasaidia wanacheneo, anawadhulumu. Jina mstahiki Meya, limetumiwa kukejeli cheo cha Meya kutokana matendo yake hasi.
- Bwana Sosi- Katika lugha ya 'sheng', sosi humaanisha kula. Meya anapenda kula,mtena kilafi. Tunamwona akilalamikia udogo wa mayai, licha ya kwamba ana chakula sampulisampuli. Neno hili likichukuliwa kama utohozi wa neno la kiingereza 'source', litaonyesha jinsi Meya alivyo chanzo cha matatizo mengi yaliyo cheneo kutokana na ongozi wake mbaya.
- Kheri- Ni jina la Diwani III. Humaanisha afadhali au bora. Diwani III ni bora au afadhali ukimlinganisha na madiwani wengine kwani anajah maslahi ya wanyonge.
- Siki - kitu kichengu na pia kitu kinachotumiwa kama kiungo au dawa na huwekwa kwa chakula.
    - Daktari Siki aliwapa wagonjwa matumaini licha ya uchungu waliokuwa wanapitia.
    - Alikuwa mchungu kama shubiri kwa mstahiki Meya kwani alimweleza ukweli, Meya alichukuliwa ukweli huu kama uchochezi.
    - "Siki" linaweza kuchukuliwa kama utohozi wa 'sick' ambapo litamaanisha kuwa mhusika ni daktari anayewashughulikia wagonjwa.
- Kafifahari
- Kaji- aina ya samaki aliye mkubwa.
- Fahari-yenye sifa au yenye kupendeza.
- Kajifahari ni mkahawa mkubwa na wa kupendeza kuliko mingine iliiyo cheneo.
- Bili- Ni orodha ya vitu vilviyouuzwa pamoja na kiasi cha fedha zionazodaiwa. Ushauri wote aliotoa Bili unaathiri matumizi ya pesa au mali (Bills) ya mji wa cheneo 'mfano: unyakuzi wa ardhi, swala la mwanakandara, kuuza finbo ya Meya, na kutaka kuzuru mkahawa kwa mara pili.
- Shaura- mji lio jirani na mji wa cheneo na mambo huko ni shwari na ndio sababu ndege zilielekezwa huko.
- Waridi-ua mojawapo linalonukia vizuri na ni la kupendeza lakini ukilikata linanyauka haraka. Waridi alikuwa nasi mkakamavu mwanzoni mwa tamthilia lakini baadaye anatamaushwa na kuwaacha wagonjwa wakiteseka
- Beka- Neno lnalotumiwa na wanawake kuitikia wanapoitwa. Ni sawa na bee! au Abee!
- Beki alipochaguliwa kuwa mwakilishi wa wafanyi kazi, aliitikia na kuwawakilisha vilivyo.

Zozote 5x1, mwanafunzi akitoa maelezo sahihi ya majazi, atuzwe.

b) Kinaya

- Maelezo: Ni mbinu ya kusema kinyume na anachomaanisha au kuswema na kutenda kinyume cha matarajio.
- Anwani 'mstahiki Meya ni kinaya kwa sababu Meya Sosi haonyeshi matendo yanayoonyesha kuwa ni mstahiki.
- Ni kinaya kwa Meya kudai kuwa anapunjwa kwa, kuletewa viyai vidogo ilhali ni yeye aliyewapuja wafanyikazi kwa kuwalipa mishahara duni.
- Ni kinaya kwa Meya kulalamikia mambo madogo kama vile udogo wa mayai.
- Watu walimchagua Meya wakitarajia kuimarika kwa hali zao za maisha. Badalaya haya, Meya anawatelekeza kaika magonjwa, njaa na ukosefu wa lishe bora.
- Ni kinyaya kwa watu kuendelea kuchagua viongozi wale wale ingawa hawaridhishwi na utendaji wao.
- Meya kudai cheneo ni kisiwi chakupigiwa mfano ilhali watu walikufa kwa kula mizizi na matunda mwitu.
- Meya anadai kuwa ana akili nyingi ilhali alimwachia Bili kufanya uamuzi kama vila kuuza fimbo na kufurusha mwanakandarasi.
- Diwani wa I kusema atatangazia watu kujotolea kwa Baraza kutetea demokrasia, ni kinyaya kwani wafanyikazi walipoenda kwa Meya kutoa malamishi walitawanywa na polisi.
- Ni kinaya kwa Diwani II kupendekeza kuundwaa kwa kamati za madiwani ilhali anajua kuwa baraza halikuwa na pesa.
- Meya aliidhinisha nyongeza ya Mishahara ya walinda usalama na kutotozwa kodi kwa madiwani huku akijua baraza lilikuwa na nakisi ya milioni mia moja.
- Ni kinaya kwa mama muuza ndizi kutozwa kodi na madiwani kutolipa.
- Ni kinaya kwa Meya kudai kuwa uamuzi wa madiwani kutolipa kodi ulikuwa demokrasia kwani wengi waliunga mkono.

- Ni kinaya kwa meya kupeleka watoto wake ng'ambo badala ya kununua viwango vya elimu cheneo Zozote nane x 1 =8

c) Jazanda

- Maelezo: Ni mbinu ya lugha ambapo vitu wiwili huliganishwa kwa njia fiche.
- Kutembea nyuma ya punda aliyeudhika uk 14. Hii ni jazanda iliyyotumiwa na Siki anapomwelezea Meya hatari ya kuongoza watu walioudhika kwa sababu ya mateso.
- Afadhali kumrudi mtoto kuliko mtu mzima uk 47. Diwani wa III anamaanisha Meya haambiliki au hasemezeki na watu wengine isipokuwa Diwani I, Diwani II na Bili.
- Sitataka mizuka yao kuniandama uk 19. Meya anamaanisha kuuwawa kwa wanacheneo huenda kukamnyima kura kwa hivyo watahadhari kabla ya hatari.
- Uvundo wa mji ni Jazanda ya uozo wa uongozi wa mstahiki Meya.
- Kuwaua ndege watau kwa jiwe moja (uk 30). Meya anamaanisha atanufaika mara tatu.
  - Atapata mgao kutokana na fidia ya mwanakandarasi.
  - Atanufaika na mianya ya ufisadi katika kandarasi mpya.
  - Kesi itakuwa imekamilika kwani Meya aliogopa kifungo cha miaka saba.
- Mimi na Meya ni mfano wa mafuta na maji uk 45 Siki anamaanisha kwa yeye na meya wametofautiana sana katika maswala ya kijamii, kiuchumi na kitaaluma.
- Upo wakati ulinituma nikashindwa kumwinda ndege wako na kukuletea hadi jikoni (uk 60).Diwani wa kwanza anamaanisha akipewa maagizo yoyote na Meya huyatimiza.
- Lazima kwanza mnihakikishie kuwa hivyo sumu hapata fununu.
- Kutia kidole akatika mzinga wa nyuki uk 14 Meya anamtahadharisha Siki kuwa maneno yake yangemtia matatani.
- Uamkanyaga nyoka mkia- Siki anamtahadha risha Meya kuwa ukoloni mamboleo utamwingiza katika matata.
- Koti jeupe la kazi lililokunjwa vizuri kando ya meza linamaanisha Siki ni daktari uk 34. Zozote 7x1=7.

4 (a)

- Mzungumzaji ni Imani
- Anamwambia Amani
- Walikuwa wameketi barazani kwenye nymba mpya ya Amani
- Hii ni baada ya shamrashamra za kuachiliwa huru amu Yusufu, wakati imani alimtia Shime Amani kuandika tawasifu yake na mambo yote yaliyojiri. 4x1=4

(b) **Sifa za imani**

- Mwenye bidii-alifanya kazi katika nyumba ya Bw majisifu.
- Jasiri- Aliivuta kaftura ya askari mmoja katika juhudi za kumtetea mamake aliposhambuliwa na askari.
- Mwenye huruma - aliwahurumia watoto walemavu wa majisifu na kuwatunza vyema.
- Mvumilivu-Alivumila mateso akiwa katika seli ya Mtemi nasaba Bora. Zozote 4x1=4

i) Maelezo

c)Kuna wahusika wengi riwayani lakini wana nafasi ndogo. Wamechorwa kama wanyonge au wasio na thamani kubwa maishani.

- Imani amejitokeza sana katika riwaya lakini yuko kivulini mwa Amani. Mwishoni mwa riwaya, Amani anaporejea kusoma ili kukamilisha ndoto yake, Imani anakaa tu akisubiri kuolewa.
- Bi zuhura, mkewe mtemi Nasaba Bora hakuwa na usemi wowote katika ndoa yake. Anapuuzwa na mumewe na hata mwishowe kupewa talaka.
- Dora, mkewe majisifu, alikuwa mke wa nyumbani akishughulika na kazi za nyumbani na malezi ya watoto wake walemavu.Anaishia kuwa mpenda ugomvi aliyemshinda mumewe kila wakati na hata kutotaka kumkaribisha Amani nyumani mwao.
- Mashaka, binti ya Nasaba Bora, amechorwa kama msichana ambaye hakuwa na mwelekeo maishani. Aliacha shule na kupata kichaa baada ya uchumba wake na Ben Bella kuvunjika.Aliamua kupenda kwa dhati mtu aliyekuwa mhalify sugu (Ben Bella). badala ya kuzingatia masomoyake.
- Lowela, binti ya maozi, alikuwa na nafasi ya kusoma na kuwa mtu bora maishani.Badala yake anaacha shule ili kuandaman na wazee kama Najaba Bora, kama mpenzi wao. anarejelewa kama 'janajike' lile lililoutukanisha uke;
- Michelle, mchumba wa Major Noon alipuuza juhudi zote alizoganya Major Noon ili kumridhisha. Amechorwa kama msaliti aliyesaliti penzi la Noon kwake. Alimtamausha Major Noon, akaishi bila kuoa

maisha yake yote.
- Bikizee ni miongoni mwa hadhira ya Nasaba Bora. Lake kubwa ni kulalamika kuwa Nasaba Bora anatoa hotuba kwa kiingereza badala ya Kiswahili.
- Hakuna mwanamke anayeonekana kufaulu kama msomi au kiongozi. Imani ambaye angekuwa msomi hakukamilisha masomo yake kutokana na kifo cha babake. (Zozote 6x2)

Tanbihi- Mtahiniwa ataje mhusika na kueleza alivyopuuzwa.

5. **(i) Dora**
- Hataki ifahamike kuwa ana watoto walemavu, hivyo basi anawafungia chumbani anakowapuuzilia.
- Hawajali wanawe- Hafanyi chochote kumshauri mumewe ili watafutiwe msaada na hata shule.
- Anawaona wanawe kama laana. Analalamikia mumewe kuhusu kazi nyingi za kuwalea watoto walemavu.
- Mwishowe anabadilisha mtazamo wake na kuanza kuwajali 4x1=4

Imani
- Anajali walemavu. Anakubali kuajiriwa nyumbani kwa mwalimu majsifu kuwatuza watoto wanne walemavu.
- Anawashughulikia watotot walemavu kwa imani na huruma.
- Ni kielelezo bora dhidi ya wazazi na jamii inyayowatenga walemavu, kupitia kake tunaona umuhimu wa kuwajali walemavu.
- Ana falsafa imara kuwa binadamu hawezi kukamilika bila kuwajali walemavu.

Mashaka
- Anawadharau na kuwadhihaki binamu zake walemavu.
- Anaamini kuwa hatazaa watoto walemavu
- Anaona afadhali Mungu amsababishie mauti kuliko kuzaa walemavu. 2x2=4

Mwalimu majisifu
- Hawajali watoto wake walemavu
- Anawadharau na hata kuwaita masimbi
- Anamlaumu mkewe kwa kumzalia mashata
- Baadaye anabadilika na kuwajali na kuwahurumia wanawe. 4x1=4

Mtemi Nasaba Bora
- Anawadharau walemavu kiasi kwamba hataki kujihuzisha nao- kwa mfano msichana mzuri aliyekutana naye katika gari.
- Hawajali walemavu - Hachukui hatua yoyote kuwasaidia watoto walemavu wa nduguye. 2x2=4

6. a) Utanzu - ushairi simulizi
   b) Kipera - Sifa inayoitwa majigambo/vivungo
   c) Sifa za majigambo
- Hutungwa na kughanwa na mhusika mwenyewe
- Hutungwa kwa usanii mkubwa kwa kutamia sitiani, vidokezo, mfanano na urudiaji
- Anayejibamba huitungia kuvungo kufuatia tukio mahususi katika maisha yake
- Kwa kawaida vivugo hutungwa na kughanwa na wanaume
- Huwa na matumizi ya chuku
- Hutolewa kwa nafsi ya kwanza
- Anayejigamba huweza kubeba baadhi ya vifaa vyake vya kazi au vinavyoonyesha jambo analosifia. Wanaweza kuvaa maleba yanayooana na kazi au jambo ambalo anajisifia.
- Kwa kawaida hutungwa papo hapo. Mengine huandikwa ili kughanwa baadaye katika hafla fulani kama vile harusi.
- Anayejisifu huweza kutaja usuli wake wa kinasaba.
- Wanaojigamba mara nyigi huwa walumbi au washairi wanaoelewa kwa kina wanalolitongoa.
- Maudhui makuu katika majigambo ni ushujaa Zozote 8x1=8

   d) (i)Hukuza ubunifu- kadri mtu anavyotunga na kughani majigambo ndivyo anavyoimarisha uwezo wake wa kubuni mitindo mipya ya utunzi na uwasilishaji.
   (ii) Hukuza ufasaha wa lugha. Watunzi wengi wa majibambo ni ushujaa. Zozote 8x1=8

   e)
- Hukuza ubunifu-kadri mtu anavyotunga na kughani majigambo ndivyo anavyoimarisha uweza wake wa kubuni mitindo mipya ya utunzi a uwasilishaji.

- Hukuza ufasaha wa lugha. Watunzi wengi wa majigambo huwa waliumbi.
- Ni nyenzo ya burudani. Majigambo huongoa walohudhuria sherehe ambapo yatolewa.
- Hudumisha utu na utambulisho wa mwanamume katika jamii. kupitia majigambo, wanaume walidhihirisha nafasi zao katika jamii.
- Ni nyenzoo ya kufanya watu waheshimiwe. Hudumisha air ya kuwafanya wanaume kutoka kuwa mashujaa. Mtu anapofanya kitendo cha ushujaa alijigamba na kuheshimiwa. 5x2=10

7.

- Ukosefu wa utafiti wa kutosha ingawa mengi yameandikwa kuhusu fasihi simulizi, kuna vipera ambavyo bado havijaandikiwa sana.
- Uchache wa wataalamu wa kuitafitia na kuiendeleza. Wasomi wengi hupuuza utafit wa fasihi simulizi.
- Ukuaji wa kazi za kimaandishi. Baadhi ya ngano zimeandikwa, hivyohakuna haja ya utambaji; mtu anaweza kujisomea.
- Maendeleao ya kiteknolojia na kisayansi siku hizi njia za kisasa za kujibururdisha kama vile vipidi vya runinga vinatumiwa badala ya fasihi simulizi.
- Kuhamia mijini na kutangamana na watu wa jamii tofauti kumefanya uhifadhi wa tamaaduni za jamii na urithishaji wake kutowezekana.
- Mtaalamu wa elimu kupuuza hugha za kiasili ambazo ndizo zinazohifadhi na kurithisha fasihi simulizi ya jamii mbalimbali.
- Baadhi ya watu wanaihusisha fashihi simulizi na ukale, hivyo kutoona haja ya kuitafitia wala kuirithisha vizazi vya sasa.
- Fasihi simulizi ilihifadhiwa akilni. Kwa hivyo anayeihifadhi aweza kuibadilisha, anaweza kufa na kutoweka nayo au anaweza kusahau Tano za kwanza x2=10

B

- Utafiti umefanywa ili kukusanya, kurekodi au kuchapisha tanzu za fasihi simulizi
- Uandaaji wa tamasha za drama ambazo huendeleza utanzu wa maigizo.
- Sherehe mbalimbali za kijamii huambatana na tanzu za fasihi simulizi kama vile nyimbo, maigizo kwa sherehe za harusi, mazishi n.k.
- Mashindano na tamasha za muziki ambazo wanafunzi na makundi ya kijamii hushiriki kwa ushindani.
- Baadhi ya jamii zinaendeleaza utambaji wa moja kwa moja wa hadithi nyumbani hasa za mashambani.
- Vyombo vya habari kama vile redio na runinga vimetenga muda kwa kupeperusha vipindi vya utendaji wa baadhi ya tanzu za fasihi simulizi k.m michezo ya kuigiza na nyimbo.
- Makundi ya wasanii huendesha sarakasi ambazo huhifadhi vipera kama vile vichekesho na malumbano ya utani.
- Uchezaji wa ngoma na nyimbo za kitamaduni katika hafla za kitaifa.

8 (a)

i) Karaguni -Kila ubeti ua vina tofauti
ii) Kikwamba-Neno ‘chema’ limeanza kila ubeti.
iii) Tarbia-Mishororo mine katika kila ubeti.
iv)Mathnawi-Kila mshororo una vipande viwili, ukwapi na utao4x1=4(Mwanafunzi ataje na kueleza sababu)

b)

i) Chema
ii) Chema hakidumu
iii) Chema wangu 1x2=2 (Yoyote moja x2)

c) i) Tabdila-Kukingojeleza - kukingojelea yakwe- yake
ii) Kuboronga sarufi-Kipenzi nyanyangu badala ya nyanyangu kipenzi
iii) Inkisari-Kinshanziza - kimeshaniliza/kimekwisha niliza.
n’ongeza - niongeza
-haniambi - haniambii
-Alojipa - ila
iv) Lahaja-ela-ila Zozote 2x1=2

d) Toni ya mashikitiko/huzuni/kilio

e).

- Kila ubeti ua mishororo minne
- Kila ubeti una mishoro yenye vipande wiwili - ukwapi na utao

- Kila mshororo una mizani 12 (6– 6)
- Vina vya ukwapi na utao vinabadilika badilika.
- Kituo (mshororo wa mwisho) ni kimalizio tu. (kinabadilika). 4x1=4

f). (i) Takriri/urudiaji wa silabi kama vile za, ka, e, ngu, ni, bu n.k.
(ii)Urudiaji wa maneo - Neno chema linerudiwa rudiwa katika kila ubet. Neno moyoni katika ubeti wa mwisho,
mshoroto wa pili na wa tatu.

g) (i) Kitakutoka ghafla/kitakuponyoka
(ii) Kimefanya nilie

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA GUCHA SOUTH
102/1
KISWAHILI
KARATASI 1

1. Lazima
   Wewe ni katibu wa kamati ya maendeleo katika kaunti yenu. Andika barua kwa Gavana wa kaunti yenu ukipendekeza miradi ya maendeleo ambayo ungetaka ashughulikie katika kaunti hiyo.

2. Eleza hatua zinazopaswa kuchukuliwa kukabiliana na ongezeko la ajali barabarani.

3. Mti mkuu ukigwa wana wa ndege huyumba

4. Andika insha itayomalizika kwa maneno haya:

   ……..nilisimama nikaangalia nyuma, machozi yakanitoka njia mbilimbili nilipokumbuka wosia wa walimu, wazazi na wenzangu.

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA GUCHA SOUTH
102/2
KISWAHILI
KARATASI 2

1. UFAHAMU : (ALAMA 15)

   Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

   Nchi nyingi duniani zimetia sahihi mkataba wa umoja wa Mataifa kuhusu haki za watoto.Haki hizi ni pamoja na uhai, lishe bora inayotosha na makazi bora yaliyo salama. Hali kadhalika, kila mtoto ana haki ya kupata elimu. Elimu inastahili kutolewa bure, iwe inayofaa na inayopatikana kwa urahisi.Isitoshe,motto hastahili kupigwa, kudunishwa, wala kubaguliwa kwa namna yoyote ile, iwe kitabaka, kirangi, kijinsia au vingenevyo. Mtoto hapaswi kufanya maamuzi yanayoweza kumhatarisha. Fauka ya haya, motto anastahili kushirikishwa katika kufanya maamuzi yanayoweza kumwathiri maishani. Pia, motto ana haki ya kupata huduma za afya. Mahitaji maalum na habari kuhusu masuala mbalimbali.Pamoja na hayo, motto anastahili kupendwa na kuheshimiwa kimawazo na kihisia.

   Haki za watoto zinatakiwa kulindwa na kila mwanajamii, serikali na wazazi wakiwa katika mstari wa mbele. Hii ndiyo sababu serikali za mataifa mengi zimeshirikisha haki hizi katika katiba na sharia za nchi husika. Yeyote anayezikiuka anapasa kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria. Walakini, haki hizi bado zinakiukwa. Watoto wengi kote duniani bado wananyimwa haki zao. Kuna watoto ambao hawajawahi hata kupata kibanda cha kuweka ubavu. Wengi hawa wamejipata wakiselelea kwenye mitaa na hata majaaa ya miji na vijiji ambako hulazimika kupitisha usiku hata katika majira ya kipupwe na masika! Wengine hawapati chakula; licha ya kuwa wanatakiwa kupata chakula chenye lishe bora. Kwao kutarajia mlo awamu tatu kwa siku ni njozi; kwani hata awamu moja ni adimu kupata! La kusikitisha ni kwamba wale wanaotarajiwa kuwa vigogo wa kuzilinda haki hizi ndio wanaongoza katika kupalilia ukiukaji wazo. Kila siku tunasikia na kushuhudia visa vya watoto kupigwa, kushinikizwa kufanya kazi za sulubu kipunda, kunyanyaswa kijinsia, kuishi katika mazingira hatari na hata kuuawa. Baadhi ya wanaohusika na vitendo hivi hasa huwa wazazi au jamaa wa karibu kama vile wajomba, shangazi au wahudumu wa nyumbani.

   Madhila yanayowapata watoto hayatokei tu katika mazingira ya nyumbani. Mateso huvuka mipaka na kufikia ngazi ya kimataifa. Watoto wengi katika mataifa yenye fujo na ghasia hutekwa na kutumikishwa vitani. Linalokata maini ni kwamba baadhi ya viongozi katika mataifa haya hawafanyi lolote kuwanusuru.Lao huwa kuwatazama watoto wanaotakiwa kuwalinda wakigeuzwa kuwa mababe wa kuua na kuuana. Watoto hawa huvishwa magwanda ambayo miili yao minyonge haiwezi kuyahimili. Pia

hulazimika kuvaa mabuti ya kijeshi ambayo **huwa nanga kwao** kubeba, licha ya bunduki zinazokaribia kuwazidi uzani.

Mojawapo ya mambo ambayo viongozi nchini humu walilenga shabaha kuyafikia baada ya kujinyakulia uhuru ni elimu kwa wote. Hata hivyo, hii imekuwa kama ndoto isiyotabirika katika baadhi ya janibu. Ni kweli kwamba sera ya elimu bila malipo katika shule za msingi nchini humu inaendelea kutekelezwa.Hata hivyo, asilimia ya watoto na hata watu wazima wasiojua kusoma na kuandika ingali kubwa. Jukwaa la vijiji nchini humu na hata katika mataifa mengine ya ulimwengu wa tatu limesheheni idadi kubwa ya watoto wasioenda shuleni.Kichocheo kikuu cha hali hii ni kwamba wazazi wa walezi wamejipata katika lindi la ufukara uliokithiri. Hata wanapojitahidi kujinyanyua na kujikuna wajipatapo kuyakidhi mahitaji ya kielimu ya wanao, wao hujipata wakitapatapa katika kinamasi hicho hicho cha ulitima. Matokeo ni kwamba watoto wa matajiri wanaendelea kuelimika huku wa maskini wakibakia kwenye kiza cha ujinga. **Wanaong'ang'a nia kuwepo kwa elimu bila malipo ni kana kwamba ni waota ndoto mchana.**

a) Huku ukitoa mifano mine, eleza hali ya kinyume inayojitokeza katika aya ya pili.
(alama 4)
b) Eleza namna hali ya usalama inavyoathiri utekelezaji wa haki za watoto kwa mujibu wa kifungu.
(alama 3)
c) Kwa kurejerelea aya ya nne, onyesha mchango wa serikali katika kuwajibika haki za watoto.
(alama 3)
d) 'Wanaong'ang'ania kuwepo kwa elimu bila malipo ni kana kwamba ni waota ndoto mchana.' Thibitisha kauli hii kwa kurejelea kifungu.
(alama 2)
e) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika taarifa:
(alama 3)
   i) Vigogo
   ii) Huwa nanga kwao
   iii) Kujikuna wajipatapo

2. UFUPISHO: (ALAMA 15)

Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali.

Wataalamu mbalimbali wamekuwa wakifanya utafiti kuhusu Ziwa Viktoria. Juhudi hizi z uchunguzi zimekuwa zikionyesha kwamba ziwa hili ambalo ndilo la pili kwa ukubwa miongoni mwa maziwa yenye maji matamu duniani linaangamia taratibu. Inakisiwa kuwa kukauka kwa ziwa hili kutahatarisha maisha ya watu zaidi ya milioni 30 ambao hulitegemea kwa chakula na mapato. Utafiti uliofanywa na Taasisi ya Masuala ya Bahari na Uvuvi nchini ulionyesha kuwa ziwa Viktoria linaangamia kwa kiasi cha mita tatu kila mwaka. Hivi sasa baadhi ya fuo zilizokuwa kwenye ziwa hili upande wa Kenya zimekauka. Mandhari ya fuo hizi nayo yameanza kutwaa sura mpya. Badala ya kupata madau na wavuvi wakiendesha shughuli zao katika maeneo haya, huenda isiwe ajabu kupata watoto wakicheza kandanda.

Rasilimali z a samaki ziwani humu zinaendelea kudidimia huku wavuvi wakitupwa kwenye biwi la umaskini. Walisema wasemao kwamba akosaye la mama hata la mbwa huamwa. Wavuvi wamebuni mikakati ya kukabiliana na hali hii ambayo inatishia kukiangamiza kizazi chao. Wengi wao wameamua kufanya biashara maarufu kwa jina 'bodaboda' wengine wameingilia kilimo baada ya kushindwa kujikimu kimaisha kutokana uvuvi. Wavuvi wanaondelea kuvua samaki katika ziwa hili wamejipata katika hali ngumu ya kiuchumi. Hali hii imewalazamisha baadhi yao kuanza kuvua samaki katika maji la mataifa jirani, jambo ambalo limewachongea, wengine wakatiwa mbaroni huku wengine wakinyanyaswa na maafisa wa usalama wa mataifa hayo jirani.

Sekta ya uchukuzi na mawasiliano nayo imeathirika si haba. Shughuli za uchukuzi katika ziwa hili zimetingwa na gugu-maji ambalo limetapakaa kote ziwani. Mbali na gugumaji hili, shughuli za kilimo cha kunyunyizia maji zimetanzwa. Kadhalika, kupungua kwa viwango vya maji humu ziwani ni change moto nyingine ambayo inawashughulisha wanaharakati wa mazingira. Inahofiwa kuwa mataifa ya Afrika Mashariki yanalipoteza ziwa hili hatua kwa hatua. Hakika, wanasayansi wa masuala ya bahari wameonya kuwa ziwa hili litakauka katika kipindi cha karne moja ijapo!

Ni dhahiri kwamba jumuiya ya Afrika Mashariki ina jukumu la kulitunza ziwa hili kwa jino na ukucha. Serikali za nchi husika, hususan Kenya, Uganda na Tanzania zinapaswa kuteleza sharia zinazodhibiti

shughuli za uvivu katika ziwa hili. Mathalan, kuna haja ya kuvua kwa misimu ili kukinga dhidi ya kuangamia kwa rasilimali za samaki. Wavuvi nao hawana budi kushauriwa kuhusu umuhimu wa kufuata kanuni za uvuvi zilizowekwa na kutahadharishwa kuhusu madhara ya kuendesha uvivu kiholela. Sheria kuhusu aina za nyavu za kuvulia pia inapaswa kutekelezwa vilivyo. Aidha, kuna haja ya serikali za muungano huu kukomesha shughuli za kilimo kandokando mwa ziwa hili, pamoja na kwenye mito iliyo katika ujirani wa ziwa lenyewe. Hatua hii itasaidia kukomesha kukomesha kusombwa kwa udongo na mbolea kutoka mashambani hadi ziwani.Hali kadhalika, muungano huu unapaswa kuweka sharia za kusimamia matumizi ya maji. Hili litawadhibiti raia wenye mazoea ya kubadhiri maji.

Isitoshe, serikali za mataifa ya afrika Mashariki hazina budi kuchunguza viwanda vinavyotupa taka ndani ya ziwa hili. Mbali na kuchafua maji, viwanda hivi vinaangamiza mimea na wanyama wa majini. Uchunguzi huo unapaswa pia kuhusisha mito inayomimina maji katika ziwa hili. Viwanda vyote vinavyotumiwa maji ya mito kama vile: Nzoia, yala, Sondu-Miriu, Awach. Kuja na Kagera vinastahili kuchunguzwa pia.

Juhudi za kufikia ustawi wa kiuchumi katika ukanda wa Afrika Mashariki zinapaswa kutulia maanani uhifadhi wa Ziwa Viktoria. Kukauka kwa ziwa hili ni sawa na kukauka kwa maazimio na ndoto zote za serikali za nchi husika za kuboresha hali ya maisha ya raia wake. Wakati ni sasa.

a) Fupisha aya za kwanza kwa maneno 70-75 (alama 9,1 ya mtiririko)
Matayarisho
Nakala safi

3. MATUMIZI YA LUGHA: (ALAMA 40)

a) i) Eleza maana ya kiambishi
(alama 2)
ii) Ainisha viambishi katika neon 'kujisifu'
(alama 2)

b) kwa kutumia mifano ya sentensi eleza matumizi matatu ya neon KWA
(alama 3)

c) i) Ni nini maana ya sauti sighuna?
(alama 1)
ii) Toa mfano mmoja wa kipasuo ambacho ni sauti sighuna
(alama 1)

d) Eleza dhana zinazojitokeza katika sentensi ifuatayo :
Alimpigia mpira

e) Kwa kutoa mifano sahihi eleza maana ya sentensi sahihi na sentensi ambatano.
(alama 4)

f) Andika kwa ukubwa wingi : (alama 2)
Mbwa mweusi amevunjika mguu

g) Tofautisha sentensi zifuatazo. (alama 2)
Ningesoma kwa bidii ningepita mtihani
Ningalisoma kwa bidii ningalipita mtihani.

h) Eleza matumizi ya viakifishi vifutavyo: (alama 2)
i) Mkwaju
ii) Parandesi

i) Tambua aina za vielezi
Mwanafunzi mrefu sana aliimama wima chifu alipopita.
(alama 4)

j) Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo.
(alama 2)
Nitakuona kesho jioni endapo nitakuja mjini.

k) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali.
(alama 4)
Mwanafunzi asomaye sana hupita sana.

l) Andika sentensi ifuatayo upya ukibadilisha nomino zilizomo kuwa vitenzi.

(alama 2)
Nasaha ya mwalimu huwa na manufaa sana kwa wanafunzi.

m) Yakinisha sentensi hii:
Wanafunzi wasipotii sheria wala kushirikiana na walimu hawatakuwa na uhakika wa kupita mtihani yao.
(alama 2)

n) Andika kwa usemi halisi
Baba alimwambia Mayaka kuwa safari yao ingekamilika siku ambayo ingefuata.
(alama 3)

o) Geuza sentensi ifuatayo iwe sharuti. (alama 1)
Wanafunzi waliingia darasani

4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)

a) Eleza sababu tano za ufifiaji na utowekaji wa Lugha. (alama 5)

b) Eleza jinsi ya kuhifadhi Lugha. (alama 5)

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA GUCHA SOUTH
102/3
KISWAHILI
KARATASI 3

TAMTHILIA
Mstahiki Meya na Timothy Arege

1. **'**Kukubali kufuata waliyoauma watu wengine bila kuwashirikisha watu wetu ni hatari. Huu ni ukoloni mamboleo. Ni namna mpya ya kutawaliwa. Chunga unamkanyaga nyoka mkia.'

a) Fafanua mbinu ya lugha iliyotumika katika dondoo hili. (alama 2)

b) Jadili dhana ya ukoloni mamboleo inavyojitokeza katika tamthilia nzima.
(alama 8)

c) '…….Chunga unamkanyaga nyoka mkia.' Onyesha jinsi mnenewa anavyomkanyaga nyoka mkia.
(alama10)

RIWAYA
Kidagaa Kimemwozea na Ken Walibora
Jibu swali la 2 au la 3

2. Jadili anwani Kidagaa Kimemwozea ilivyo mwafaka kwa riwaya hii. (alama 20)

Au,

3. 'wazungu walipoondoka, (inasemekana hawakuondolewa). Waliacha majina yao yameandikwa kwa wino usiofutika.'

a) Eleza dhuluma zilizofanywa na wazungu hawa kabla ya kuondoka kwa mujibu wa riwaya hii.
(alama 8)

b) Thibitisha madai kuwa wazungu walipoondoka waliacha majina yao yameandikwa kwa wino usiofutika kwa mujibu wa riwaya ya Kidagaa Kimemwozea.
(alama 12)

HADITHI FUPI
Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine : Ken Walibora

4. Jadili swala la mapenzi kama lilivyosawiriwa katika Diwani ya Damu Nyeusi na Hadithi nyingine.
(alama 20)

Au,
Hadithi Fupi : Maskini Babangu.

5. 'Mtoto mtantele umemtoa wapi ? Wee ! waacha! Unawezaje kumpata mjukuu wa kitantele? Ee? Usituletee hapa.'

a) Eleza mkutadha wa dondoo hili (alama 4)

b) Eleza jinsi mbinu ya majazi ilivyotumiwa na mwandishi wa hadithi ya maskini Baba yabgu.
(alama 6)

c) Fafanua maudhui ya ndoa yanayohusiana na chanzo cha tukio linalorejelewa katika dondoo hili.
(alama 10)

USHAIRI

6. Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali uliyoulizwa.

1. Wazazi wa nyumba hino, mefika kuwaarifu,

Yaacheni magombano, kaeni kwa usanifu,

Sasa yamezidi mno, mambo yenu kwa marefu,

Kaa ya Lila na Fila, jinsi mnavyopata.

2. Yako ni nje hadharani, maneno mnayofita,
   Vitimi vyenu vya ndani, sisi na tunavipata,
   Ficho yenu mwafichani, na wenyewe mwayabwata,
   Kaa moto ni mafuta, jinsi mnavyopatana

3. Kila kukicha midundo, dhana yu zizini chui,
   Mengi manuka uvundo, mwayasema hayatui,
   Tele nyoyoni mafundo, ya wingi wa uadui,
   Kaa pua ni mnuko, jinsi mnavyopatana.

4. Ya shani mwenu famili, maisha mnayoishi,
   Kila mmoja fidhuli, atoapo matamshi,
   Mwajitenga mbalimbali, hata katika mapishi,
   Kaa kweli ni urongo, jinsi mnavyopatana.

5. Hamuwazi mkapima,neno ovyo mwatamka,
   Wana kwa wao wazima, hamueshi hekaheka,
   Mwajiishia kinyama, hampati kuzindukia,
   Kaa asali ni ndimu, jinsi mnavyopatana.

6. Mawaidha ya unyemi, tulizaneni ubongo,
   Mmepewa taalumi, kila rai kwa mpango,
   Punguzeni yenu ngumi, msije tiana chongo,
   Kaa kikembe ni kawa, jinsi mnavyopatana.

a) Je shairi hili laweza kuwa na kichwa kipi ?
(alama 2)

b) Ni jambo gani hasa linalopigwa vita katika shairi hili ? (alama 2)

c) Katika ubeti wa 3, mshairi asema :

‘Kila kukicha mdundo, dhana yu zizini chui.

Mengi manuka uvundo, mwayasema hayatui’

Eleza maana iliyomo katika kila mstari. (alama 4)

d) Eleza kwa maneno yako mwenyewe maana ya kituo cha ubeti wa 3
(alama 2)

e) Andika ubeti wa sita kwa lugha ya nathari.
(alama 4)

f) Eleza maana ya maneno yafutayo kulingana na shairi hili ulilolisoma: (6 marks)

i) Usanifu

ii) Kuzinduka

iii) Fidhuli

iv) Mwayabwata

v) Mafundo

vi) kawa

7. soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali yanayofuatia.

1. E alifajiri, mwenye nuru tele, inayoangaza,
   Ni alifajiri, mwenye na miale, inayopendeza,
   Kwa alifajiri, japo iko kule, inatupumbaza.

2. E alifajiri, pambo lako zuri, linatushangaza,
   Ni alifajiri, umebashiri, kuwa kumengaza,
   Kwa alifajiri, sote huwa huri, unapotokeza.

3. E alifajiri, ya mchanganyiko, rangi ulopawa,
   Ni alifajiri, kutokeza kwako, ndipo lije juwa,
   E alifajiri, wewe ukiwako, hofu hupungua.

4. Ni alifajiri, unayeamsha, watu walolala,
   E alifajiri, unawakumbusha, kuabudu Mola,
   E alifajiri, watufurahisha, tunapokuola.

5. E alifajiri, hilo lako pambo, linalopendeza,
   E alifajiri, mbali ya urembo, waondoa giza,
   Ni alifajiri, usiye na kombo, wala kuunguza,

6. E alifajiri, huwa kama uwa, unapochomoza,

E alifajiri,tunapokujuwa, tukajitengeza,

Kwa alifajiri, hujiweka sawa, kwa kujitembeza.

7. E alifajiri, kundi la waovu, linapokuona,

   Kwa alifajiri, hupungua nguvu, wakatimukana,

   Kwa alifajiri, na wasuluhivu, kwako hujivuna.

8. E alifajiri, kwenye ulimwengu, wewe ukifika,

   Kwa alifajiri, giza na kungu, vyote huondoka,

   Kwa alifajiri, viumbe vya Mungu, huanza kutoka.

9. Kwa alifajiri, hutakata mbingu, zikanawirika,

   Kwa alifajiri, huwa lake fungu, jogoo kuwika,

   Kwa alifajiri, hufunguka pingu, watu wakatoka.

10. E alifajiri, wekundu mzuri, na weupe wake,

    Kwa alifajiri, mfano wa zari,hilo pambo lake,

    Kwa alifajiri, una na bahari, na kijana chake.

a) Eleza Lugha anayoitumia mshairi katika kuisifu 'E alifajiri'
(alama 4)

b) Taja vitambulisho mbalimbali vyenye kutoa ishara kwamba sasa kunapambazuka.
(alama 4)

c) Giza huwa limesitiri kina nani? Na alifajiri ikiingia hao waliositirika hufanya nini? Kwa nini? (alama 2)

d) Katika ubeti wa tisa, nani 'hufunguka pingu'. Eleza
(alama 2)

e) Ni katika ubeti gani ambapo mshairi anatumia jazanda yenye kuonyesha kuwa alifajiri hupambwa kwa miale ya dhahabu. Thibitisha.
(alama 1)

f) Eleza maana ya tamathali za Lugha zifuatazo:

   i) Nini maana ya giza na ukungu

   ii) Nini tofauti yao kimaana?

   iii) Una na bahari, na kijani chake. (alama 4)

g) Toa neno moja kwa kila neno lifuatalo lenye maana sawa na hilo:
(alama 5)

   i) Nuru

ii) Huri

iii) Tunapokuola

iv) Wasuluhivu

v) viumbe

FASIHI SIMULIZI

8. Eleza tofauti ya Fasihi Simulizi na Fasihi andishi
(alama 20)

Au,

9. a) Nini maana ya ngomezi. (alama 4)

b) Eleza sifa za ngomezi.
(alama 6)

c) Ngomezi ina umuhimu gani katika jamii za kiafrika.
(alama 6)

d) Toa mifano miwili ya ngomezi za kisasa. (alama 4)

MTIHANI WA MWIGO WA WILAYA YA GUCHA SOUTH
102/1
KISWAHILI
KARATASI 1
MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA

1.
- Maji
- Elimu
- Usalama
- Usafiri
- Kilimo
- Biashara
- Viwanda
- Nguvu za umeme n.k
- Mtahiniwa atumie mtindo wa barua rasmi.Atakayekosa kuzingatia sura aondolewe maki 4s.
- Lazima mtahiniwa awe na anwani mbili.
- Lugha na msamiati uwe rasmi.
- Mtindo unaostahili-wima/mshazari.

2. i) Sheria mpaya za usafiri-Michuki
   k.m -Mikanda ya usafiri
   -Vithibiti mwendo kutumika
   ii) Kusitishwa kwa safari za usiku
   iii) Idadi ya abiria kuzingatiwa
   iv) Maafisa wa usalama barabarani kuwa chonjo
   v) Magari mabovu kuondolewa barabarani.
   vi) Vyeti vya madereva kuchunguzwa upya.
   vii) Maafisa wa usalam abarabarani wanaochukua hongo kuchukuliwa hatua za kisheria.
   viii) Wanaotumia dawa za kulevya wakiendesha magari kuchukuliwa hatua kali.
3. a) Aghalabu mti mkuu huweka vitu vingi hasa ndege wanaojenga viota, kutaga na kuangua mayai yao pale. Ikiwa mti huo utaanguka makinda (wana wa ndege) huumia kwa sababu hawawezi kujisaidia wanategemea usalama wa mti huo.
   b) Mtu anayetegemea mtu mwingine au kitu Fulani kukidhi mahitaji yake hupata shida kubwa iwapo kifo au mtu
   huyo ataondolewa kwa sababu moja au nyingine.
   c) Mtahiniwa athibitishe matumizi ya methali kwa kubuni kisa au hadithi mwafaka.
   d) Mwanafunzi azingatie sehemu mbili za methali hii kikamilifu.
   Tanbihi:
   i) Si lazima mtahiniwa atoe maana ya methali
   ii) Si lazima mtahiniwa aandike kichwa cha insha.
4. i) Mtahiniwa aandike kisa kinachomhusisha yeye akitenda makosa.
   ii) Pawe na wosia/maonyo kutoka kwa wazazi, walimu na wenzake
   iii) Akaidi wosia
   iv) Ajipate matatani na kujuta.
   Tanbihi
a) Asiyejihusisha amepotoka
b) Akazidisha maneno ya kumalizia zaidi ya matano, amejitungia swali.
c) Asipoyatumi maneno aliyopewa mwishoni mwa mtungo wake atakuwa amejitungia kisa/amepotoka.

MTIHANI WA MWIGO WA WILAYA YA GUCHA SOUTH
102/3
KISWAHILI
KARATASI 3
MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA

Tamthilia –T. Arege

1. a) Mbinu ya Lugha inayojitokeza hapa ni jazanda/sitiari-ambayo ni ulinganishi wa kimafumbo usiotuma maneno

   ya kulinganisha. **Mfano:** unamkanyanga nyoka mkia. (alama 2)

   b) Ukoloni mamboleo ni mojawapo ya maudhui katika tamthilia hii. Unajitokea kote kama ifuatavyo:

- Waliochukua hatamu za uongozi wanajitia ubwana na kujitenga na raia waliowachagua. Kwa mfano. Meya Sosi anajiona mkubwa na anawatisha madiwani wenzake na hana nafasi ya kuongea na wafanyakazi.

- Anawatumia askari kama vyombo vya kutishia na kusumbua raia badala ya kuwalinda na kuwhakikishia usalama wao.

- Serikali ya Meya inatumia propaganda badala ya kushughulikia mahitaji ya wananchi. Viongezi kama Meya na Bwana. Uhusiano Mwema wanachezea nyimbo za kizalendo wananchi ili kuwapumbaza wasaidai haki zao.

- Viongozi serikalini wanajitajirisha kwa mali ya umma (ufisadi) mfano, Meya na marafiki zake kama Bili wanajigawa mashamba kasha kuyauza.

- Viongozi wanaendeleza ubinafsi kwa mfano, Meya na madiwani wanajiongezea mshahara na kujipa marupurupu mengine huku wafanyakazi wakilipwa malipo duni na yasiyolipwa kwa muda unaofaa.

- Watawala wanatumia mbinu ya tengatawala ambapo Meya na madiwani wanatenganisha Baraza na mji kati ya wale wanaouwaunga mkono na wanashikilia haki na wale wasiomuunga mkono wakitemwa katika vikao vyote vinavyojadili maswala ya jiji.

- Mji wa cheneo bado unategemea mataifa fadhili kwa misaada kwa sababu haujimudu kiuchumi.

- Uongezi wa Meya ni wa kimabavu; htamuodemokrasia. Sheria za Meya's Riot Act zimempa mamlaka makubwa hivi kwamba anafanya atakavyo bila kushauriana na madiwani wenzake; wafanyakazi na hata raia waliomchagua.

- Dhana ya collective responsibility inawazuia madiwani kueleza wananchi hisia zao kwa jambo lolote badala yake wanalazimika kuunga mkono maamuzi ya Baraza hata wanapojua hayafai na yanaumiza wananchi.

- Sera ya kugawana gharama imependelezwa na mataifa fadhili na inatekelezwa bila kushauriana na wananchi. Sera hii inazidi kuwaumiza raia ambao hawayamudu maisha.

- Dhuluma kwa wananchi-wafanyakazi wanaendelea kulipwa malipo duni.Hali ya maisha imezidi kuwa ngumu kwa raia licha ya kuwachangua viongozi. Kwa imani kuwa wangeboresha maisha yao. Hospitali hazina dawa na raia watakuwa walipie huduma huko.

c) '……Chunga unakanyaga nyoka mkia' Onyesha jinsi mnerewa alivyomkanyaga nyoka mkia.

- Meya ndiye mnerewa katika dondoo hili na anamkanyaga nyoka mkia kujimbilikia mali bila kujali wengi wanaoteseka.

- Meya anajitafutia washauri k.m Bili, Diwani I na II wanaomwambia anayotaka kusikia ingawa ni ya uongo (vibaraka)

- Meya hasikilizi ushauri mwema na wa kweli anaoambiwa na Dkt. Siki pamoja na Bwana uchumi wa fedha (Diwani III)
- Meya anazidi kuwaongezea madiwani wenzake mishahara na marupurupu bila kujali hali duni ya wafanyakazi.
- Pia anakubali na kutekeleza sera ya kugawana gharama inayopendekezwa na mataifa fadhili bila kushauriana na wananchi waliomchagua.
- Meya pia anawapuuza viongozi wa wafanyakazi na wafanyakazi ya jumla. Hasikilizi vilio vyao.
- Serikali yake inatoza raia kwa huduma za hospitali. Watu wenyewe hawana pesa za kugharamia matibabu yao.
- Meya na madiwani wenzake wanapora mali ya umma kwa kujigawia mashamba na kujipa marupurupu mengi bila ya kujali waliowachagua.
- Baraza linawalipa wafanyakazi wake malipo duni yasiyowawezesha kuyamudu maisha.
- Viongozi wa mji wa (cheneo wana mapuuza) wanaacha mji kuwa na rundo la takataka linalo hanikiza uvundo kote jijini lakini Meya na watu wake hawajali ingawa wanatarajia wageni kuzuru mji wao.
- Baraza linatumia polisi/askari kuwatawanya wafanyakazi wanapogoma badala ya kushauriana na viongozi waliochaguliwa.
- Serikali haiwajibiki kurekebisha hali yam abo ingawa ishara zote zinaonyesha kuwa huduma kwa wananchi zimezorota.
- Meya anajitenga na watu waliomchangua na hata baadhi ya viongozi wema kama siki kwa sababu ya kiburi chake.
- Meya kuwapokea na kuwatumia vibaraka wanaomsifu na kufuata yote anayoyasema yeye bila kuyahoji wala kumshauri. (zozote 10x1=10)

2. **Jadili anwani kidagaa kimemwozea ilivyo mwafaka kwa riwaya hii. (alama 20**)

- Maana ya kidagaa kimemwozea ni kwamba mambo yamemharibikia. Ni hali ya mambo kumuwia mabaya**.**
- Kidagaa kilimwozea DJ tena wakati kaptura yake iliyokuwa nguo yake pekee ilipoliwa na fahali walipokuwa wakiogelea pale katika mto Kiberenge.
- KIdagaa kilimwozea DJ aliposingiziwa wizi na kufungwa jela ya watoto. Alitakiwa akae huko hadi atakapohitimu umri wa miaka kumi na minane lakini alitoroka kabla ya kumaliza kifungo.
- Kidagaa kilimwoza pia pale alipongatwa na mbwa wa Mtemi Nasaba Bora, Nasaba Bora hakushughulikia matibabu yake kwa vyovyote. DJ alipopelekwa hospitali yaNasaba Beba matibabu mwafaka kwa hivyo alitoroka huko na kutibiwa n mganga wa miti shamba.
- Kidagaa kilimwozea Imani pale babake Mwinyi hatibu Mtembezi alipokufa katika mapambano ya ukombozi. Aliachwa bila baba na mlinzi na umaskini uliwazonga.
- Kidagaa kiliwaozoea Imani na ndugu zake Chwechwe Makweche na Oscar Kambona pale walipokonywa shamba waliloachiwa na babake huko Baraka.
- Kidagaa kilizidi kumwozea Imani na ndugu zake hasa Oscar Kambona pale mamake alipoaga dunia baada ya kuchapwa na askari atoke kwenye shamba lake.
- Imani aliozewa na kidagaa pale alipochomewa nyumba aliyoachiwa na mama yake alipoaga dunia. Aliachiwa bila makao na alitamani kifo kwa sababu hakuona maana ya maisha. Alitoka pale kwa nia ya

kujirusha ziwani lakini lipomkuta Amani pale akaghairi.

- Amani aliozewa na kidagaa pale aliposingiziwa kuwa babake kitoto kilichoyupwa nje y a kibanda chake na kulazimika kukilea.
- Kidagaa kilimwozea Amani pale alipokamatwa pamoja na Imani na kutiwa seli ya Mtemi Nasaba Bora kwa tuhuma ya mauaji ya kitoto Uhuru. Ukweli ni kuwa motto huyu aliugua na wauguzi katika hospitali ya Nasaba Bora walikataa kumtibu.
- Amani anaozewa na kidagaa pale anapofumaniwa na Mtemi Nasaba Bora akiwa na mkewewe chumbani. Mtemi alimchapa Amani na akaenda kumtupa mto Kiberenge akifikiria amekufa.
- Mtemi nasaba Bora aliozewa wa kidagaa pale alipokumbana na Gadaffi aliyetisha kumlipua kwa sababu ya kuchukua shamba lao.
- Kidagaa kilimwozea Mtemi Nasaba Bora pale lowela alipomwandikia barua akitaka awaachilie Amani au Imani la isivyo atoboe siri ya kitoto alichompangaza Amani jukumu la kukilea.
- Kidagaa kilimwozea Mtemi Nasaba Bora pale motto Madhubuti alipoanza kupanga vitendo vyake na kuanza kuwachochea watu dhidi yake.
- Kidagaa kilimwozea Mtemo Nasaba Bora pale Bintiye Mashaka aliporukwa na akili alipotumiwa barua wa Ben Bella ya kuvunja uchumba wake kwa sababu dadake Lowela na Babake Nasaba Bora.
- Kidagaa kilimwozea Mtemi Nasaba Bora alipomtia ndani Amani ni mfano mwingine na kuezewa na kidagaa.
- Mwalimu Majisifu aliozewa na kidagaaa alipoacha dini na kuanza ulevi kupindukia.
- Mwalimu majisifu pia aliozewa na kidagaa kwa kupata watoto walemavu aliosononeka kuwa nao hasa upande wa malezi.
- Bado kidagaa kilimwozea Mwalimu Majisifu aliposhindwa kuwaridhisha wanafunzi wa chuo kikuu kwa mhadhara kuhusu uandishi wake wa riwaya ya Kidagaa Kimemwozea-alilazimika kurudi haraka badala ya kuendelea na mhadara.
- Kidagaa kilimwozea Mwalimu Majisifu alipogunduliwa kuwa aliiba mswada wa Amani na kuchapisha kitabu cha kidagaa kimemwozea. Alikiri kuwa alikuwa na mazoea ya kuchapisha miswada ya watu wengine kwa jina lake.
- Kidagaa kimemwozea Mwalimu Majisifu kwa kufiwa na ndugu yake Mtemi Nasaba Bora. Ingawa hawakuwa na uhusiano mzuri naye, alihuzunika sana na kifo chake. (zozote 10x2=20mks)

3. a) Walinyakua mashamba ya waafrika na kujigawia, km majununi, ambaye alikuwa mjerumani, aligawiwa shamba la ekari mia mbili na sabini.

- Wazungu walijitengea maeneo yao k,m katika nchi ya Tomoko waligawia Sokomoko na kuwaondoa waafrika huko.
- Walijigawa mashamba Mkubwa na kuuza pereto, minazi, mibuni, mikonge na mazao mengine na pembeni mwa mashamba haya waafrika waliishi katika mabanda na ndio waliowafanyia wazungu kazi.
- Wazungu wengine waliishi katika makasi makubwa huku wafanyakazi wao wakiishi katika mabanda katika nchi yao.
- Waafrika hawakuruhusiwa kumiliki mime ya kuzalisha pesa katka nchi yao.
- Waafrika pia hawakuruhusiwa kufuga mifugo ya kizungu iliyoleta faida nzuri. Aliyetaka kufuga angefuga angefuga ile kienyeji na wanafugie nje ya maeneo yaliyotengewa wazungu kama Sokomoko. (zozote 4x2=8)

b) Thibitisha madai kuwa wazungu walipoadaa waliacha majina yao yameandikwa kwa wino usiofutika kwa mujibu wa riwaya ya kidagaa kimemwozea.

- Baadhi ya waafrika waliyatwaa mashamba na makasri yaliyokuwa ya wazungu ma wakayafanya yao.
- Waafrika waliendele kuionea fahari Lugha kizungu ingawa walikisema kwa ndimi zao zilizoboronga majina ya kizungu k.m Foti-Ford, Batulumayo-Bartholomeo makatalima-magdaline, majununi-major noon.
- Waafrika waliokuwa kazini walijizoeza tabia ya kuficha faili za watu ili kujipatia milungula k.m Bwana Nasabu Bora alipokuwa karani katika wizara ya Ardhi na makao.
- Serikali huru ilipoanzisha sera ya kuwapa waafrika makao sehemu zilizotengewa wazungu, watu kama Mtemi Nasabu Bora walijitengerezea faili ili kuyapora yale mashamba ili kukidhi ubinafsi wao.
- Mtemi nasabu Bora alipanga njama za kumuua msomi aliyenunua shamba la ekari mia mbili na sabini ili alichukue liwe lake bila kutoa chochote.
- Waliomiliki mashamba na majumba ya wakoloni kama mtemi Nasabara Bora pia waliweka majibwa ingawa hawakuweza kuyatunza vizuri.
- Walioshika uongozi kutoka kwa wakoloni pia walijitia utukufu wa walitaka watu wawatukuze na kuwaheshimu kama Mungu.
- Viongozi hawa waliwadunisha, kuwadharau na kuwatusi waafrika wenzao. Km Mtemi Nasaba Bora.
- Dhuluma dhidi ya watawaliwa zilizidi lakini hawakulalamika wazi ila kichinichini kwa sababu waliwaogopa watawala.
- Viongozi waafrika waliendelea kuishi kwa makasri huku wafanyikazi wao wakiishi katika mabanda. Km Amani alipewa makao katika mojawapo ya vibanda vya wafanyakazi makabwela alipopewa kazi kwa Mtemi Nasaba Bora. (zozote 6x2=12)

4. Damu Nyeusi.

- Dhana ya mapenzi imesawiriwa katika sehemu mbili yaani kuna mapenzi ya bandia na mapenzi ya dhati/ukweli
- Vijana kuchukulia swala la mapenzi kama uhuru wa kufanya mapenzi kiholela.Hatimaye tunaona wasichana wakipachikwa mimba wasizotarajia. Mifano ni ya Sela na Christine wasichana wengine ambao walionyesha kukosa uwezo wa kuzidhibiti mimba zao waliamua kuziavya. Mfano ni Christine mpenziwe Peter.Baadhi ya wasichana hujifungua na kuwaachia wazazi wao mzigo wa kuwalea wanao. Mfano ni Sela.
- Katika vyuo vingine kulikuwa na wanafunzi ambao walitumika na wanaume matajiri kuwatafutia wapenzi mle vyuoni ili wafanye nap mapenzi kiholela. Mfano ni Zac anatumika na Peter kumshawishi Christine awe mpenzi wake akawa anamtembelea kwake tank Hill. Hata urafiki kati ya Peter na Zac umeimarika tu kwa sababu ya kushirikiana katika ulanguzi wa pesa, samaki na mihadharati.
- Jamii hasa wanawake, washawishika na Imani potovu kwamba wanaume wazungu wanapenda wasichana wa kiafrika ambao ni warefu na wembamba. Imani hii imeponza Christine, kwa kumwandama Peter ambaye anampachika mimba kasha akamwacha akabaki kudharaurika na jamii.
- Waliofika Exotic Resort kujivinjari waliandamana na wapenzi ovyo na kiholela ndipo mandhari yenyewe inasimuliwa kama Ahera.
- Mamaye Amali alikuwa na mapenzi ya bandia kwa Abu kwa sababu alitaka sana mali yake ndipo

akamlazimisha kuandaa harusi ya kukata na shoka kwa kuagazia samani (famicha) kutoka warabuni.

- Mjombaye Abu alikuwa na mapenzi ya dhati kwa mpwa wake, kwani baada ya kukereka wakati pesa yake ulipokataliwaa anampa moyo kuwa asikate tama kwani siku moja mambo yangetengenea.

- Abu alikuwa na mapenzi ya bandia kwa Amali na aila yake ndiyo sababu anatupilia mbali ndoa wakati wa kilele cha kufunga akidi.

- Jamila alimpenda Duni kiasi cha kutosharuriwa kuvunja ndoa yake. Alibaki akitarajia kwamba siku moja mumewe angebadilika ampende akawa anavumilia kichapo, matusi na hata mateso ya Duni.Mwishowe alionea fahari uvumilivu wake kwa kila mara Duni alimwita kwa jina la upendo si 'jamila'

- Sela alikuwa na mapenzi ya dhati kwa Masazu na ndiposa baada ya kuhitimisha elimu yake aliamua kuhamia mjini dafina ili kuishi naye pia alinasihin wafike kitongojini kumchukua motto wao.

- Mzee Butali na mkewe walipenda binti yao hata baada yay eye kufukuzwa katika shule ya Askofu Timotheo bado walimtafutia shule nyingine ya kutwa kuendelea na elimu yake.

- Rozina alimpenda na kumlea Kadogo vyema hadi mamaye alipofika kumchukua kisiri.

- Mapenzi kati ya kamata na Grace yametokea na kwa upande wa pili kumetokea mapenzi kati ya kamata na Esther. Esther alikuwa na mapenzi ya dhati kwa wateja wake. Licha ya Esther kumpenda kamata bado alidanyanyika kimapenzi.

- Mzee kadiri na mkewe walikuwa na mapenzi ya dhati kwa Amali kwao walitaka afunge akidi na mtu tajiri atakayemtunza vizuri maishani.

- Katika hadithi ya Mzizi na Matawi, mwandishi anaonelea kuwa uanaharamu umeenea pakubwa kwa upande wa wazazi ambao wanajitoma anasa za ujana hao. Mfano, mamake Sudi-kudura anatubu kuwa alimtupa mwanawe pipani ili azidi kuendelea na anasa za ujana wake-uk 116. (zozote 10x2=20 mwanafunzi ajadili pande zote mbili)

5. Maskini Beba rigu-Hadithi Fupi

a) Mama mmoja mwenye umbo la kifaru,Mtantele ndiye aliyesema maneno haya. Alikuwa akimwambia Baba Maende. Walikuwa katika janibu moja na mtaa wa Kochokocho iliyokuwa na watu wengi wenye asili ya kitantele.Alisema maneno haya kwa nia ya kupanga wazo la Babu Maende huweza kuwa na mjukuu wa Kitantele (alama 4)

b) Majazi ni mbinu ya kuwapa majina wahusika kulingana na tabia zao. Mbinu ya majazi hutokea pale ambapo mahali au mhusika hupewa jina kulingana na jukumu lake au sifa zake kutumika kuzitambulisha kama:

- Janibuza mtaa wa Kichokocho na sehemu mbalimbali kama vile Madongo poromoka zinapewa majina haya kutokana na hali duni ya wasifu wa maeneo hayo na kuwa na vibanda vingi vibovu msongamano wa watu, rundo la taka na uchafu mwingi.

- Wingi wa watu katika sehemu hii ndiko kulikosababisha mzee Maende kuuliwa alipotembelea.

- Utangamano baina ya watu watantele na Wasabu kunaifanya jamaa ya mzee Maende kushamiri furaha si haba. Mathalani walikoishi kukapewa sifa ya kabucheka kwani jamii hizi zilipotembeleana vicheko kwa furaha zilitanda isitoshe, wenyeji wa Kabucheka walitangamana vyema na wageni hawa wa asali watentele

- Mwandishi ametaja 'Harambee' ambao ni uwanja wa michezo ambao umetumika kuleta dhana ya kushirikiana pamoja katika ishtighala za watu wa sakata ulivyojiweza kufurahisha na kufanya jamii moja.

- Ukoo wa Kitantele unatokana na kufungamanisha kwa maneno mawili yaani kitani kumaarisha nywele ndefu nayo tele kumaarisha nywele ndefu, nayo tele kumaanisha nyingi mno. Kwa hivyo watantele

walitambulika kutokana na nywele zao ndefu kwa mujibu wa asali yao.

- Kochokocho ni mahali palipo kuwa na vitu vingi, vituko vingi pamoja na umayamaya wa watu waliokuwa na shughuli nyingi. (zozote 6x1=6)

c) Kuna mwingiliano wa jamii ya Kisibu na Kitantale kwa sababu ya ndoa kati ya wazazi wa msimulizi waliotoka katika kabila hizi mbili.

- Maendeleo ya kijamii yamechangiwa kutokana na ndoa za aina hizi kama ile ya wazazi wa msimulizi. Usuli wa mamake msimulizi ni wa wafanya biashara na wa babake ukiwa ni wa wakulima. Maingiliano katika mazingira kama haya ndiyo yaliyoimarisha uchumi na ujamaa katika maeneo ya Kubucheka.

- Msimulizi pia anatupa funzo kuwa baadhi ya jamii zimezidi kubakia nyuma kimaendeleo na kutengana kwa sababu ya upinzani katika ndoa kwasababu ya asili tofauti. Yamkini maumbile yam mzee Maende ni tofauti na msimulizi. Hii ndiyo sababu Babu Maende anatuhumiwa kuwa ni mwizi wa watoto wa Kintele.

- Hadithi hii inajenga picha ya jamii ambayo inajumuisha watu wenye asili tofauti kikabila na kitamaduni. Pia tunapata kuona jamii ya Kitantale na Kisubu zikishirikiana pamoja japo zina misimamo tofauti kuhusu ndoa.

- Msimulizi anaonyesha jinsi ndoa baina ya babake na mamake ilivyochangia kuwepo kwa umoja na utangamano baina ya jamii ya Kitautele na Kisubu. Msimulizi alikuwa na usuli wa jamii zote mbili.

- Kadhia kama ile ambayo inamkumba mzee Maende huko Kochokocho ingezuilika iwapo wakatili wake wangekuwa hiari kumsikiza na kubaini usemi wa babuye msimulizi.

- Wanawake wa Kitantele hawakutambua kuwa kuna uwezo wa kuchipuka kwa mapenzi na mwingilliano wa jamii za asili tofauti katika ndoa na ndio huenda kukawa na ukweli katika usemi wa mzee Maende kuwa msimulizi alikuwa ni mjukuu wake. (zozote 5x2=10)

6. Ushauri

a) Kaeni kwa amani nyumbani (alama 2)

b) Kufarakana nyumbani (alama 2)

c) Mstari 1

Wao hugombana kila asubuhi kwa kelele sana mfano wa chui kuwaingilia ng'ombe zizini. (alama 2)

Mstari 2

Wao hugombana kwa matusi mabaya na huyatamuka ovyo matusi hayo bila kuogopa. (alama 2)

d) Maneno yaliyotumika katika kituo cha ubeti wa tatu hayatumiki kwa njia ya kuonyesha kinyume moja kwa moja kama katika vituo moja vingenevyo mf. Lila na fila ubeti 1

Moto na mafuta ubeti 2

Kweli na urongo ubeti 4

Asali na ndimu ubeti 5

Kikombe na kawa ubeti 6 (alama 4)

e) Nawashauri vyema kuwa muwe watulivu mmepewa akili kwamba mfanye mambo yenu kwa utaratibu wa kuelewana.Hivyo jamani punguza mapigano kwani mtakuja kuuana. Nivizuri mpatane daima kama kikombe na kuwa.
(alama 4)

f) I) Kwa wema

ii. Kurudiwa na fahamu mara moja

iii. Mjinga

iv. Mwatoa siri zenu.

v. Hasira za ndanindani

vi. Kifuniko cha kienyeji cha sahani yenye chakula. (zozote 6x1=6)

7. <u>Ushairi</u>

a) Matumizi ya E, alifajiri ambaye mshairi ametumia ni ya aina ya tashhisi ambalo mshairi anaitolea sifa Alifajiri wito wa sifa, uzindushi kama atendavyo kawaida binadamu mambo yake. (alama 2)

b)

i) Nuru teule-ubeti 1

ii) Miale –ubeti 1

iii) Kujitokeza kabla ya jua-ubeti 3

iv) Kiamsha watu waliolala-ubeti 4

v) Waondoa giza-ubeti 5

vi) Ua linachomoza-ubeti 6

vii) Giza na ukungu huondoa-ubeti 8

viii) Kundi la waovu wakiona alifajiri hutoweka ubeti-ubeti 7

ix) Alifajiri jogoo huwika. (zozote 4)

c) Giza husitiri waovu ubeti wa 7, kwa kutenda maovu gizani kama ujambazi (kutumia nguvu) sasa wakiona kumekucha wao husambaratika wasije wakatambulika. (alama 2)

d) Wakati wa alfajiri, watu waliolala usiku huamka kuanza shughuli za siku. Wakati wa usiku ni kama walifungwa pingu za alfajiri, ndipo asubuhi hufunguliwa.

e) Ni katika ubeti wa 10 ambapo mshairi ametumia mfano wa zar. (alama 1)

f) i) Giza-kiza kilicho kinene

Ukungu-kiza kinachofifia kabla ya mapambazuko

ii) Maji ya bahari yenye ufuo

Ulio jaa miti tele.

g) Mwangaza, mwanga

Huria
Tunapokutazama
Wema, waadilifu, mahodari
Hulka, mahuluki. (alama 5)

8.

Fasihi simulizi	**Fasihi Andishi**
Ingawa baadhi ya kazi ni za kimapokeo zinawezekana kutungwa papo hapo k.m sherehe za arusi,ngoma, nyimbo	Utunzi wake huchukua muda kabla ya kuiwasilisha kwa hadhira. Inasomwa popote pale.

Huwasihishwa kwa njia yam domo ambapo utendaji hushirikishwa	Huwasilishwa kwa njia ya maadishi na utendaji, hasa uigizaji katika tamthilia ya ushairi
Huwasilishwa mbele ya hadhira iliyo hai	Hadhira si hai na mtunzi haingiliani moja na hadhira.hali kadhalika, hadhira ni fungu la wasomaji.
Ina umri mkubwa	Ina umri mdogo
Ina tanzu nyingi	Ina tanzu nne pekee, riwaya, tamthilia hadithi fupi na ushairi.
Ni mali ya jamii	Ni mali ya mtunzi/aliyeandika
Uhifadhi wake unategemea kichwa na urithishaji toka kizazi kimoja hadi kingine.huwezi kusahaulika.	Huhifadhiwa kwa njia ya maandishi na haiwezi kusahaulika
Huwezi kubadilika badilika kutegemea ufundi wa mwasilishaji wa kumbukumbu na kuiwasilisha.	Haibadiliki badiliki sana. Haiwezi kurekebishwa bila idhini ya mwandishi
Huwa na wakati maalum na muktadha mahususi wa kuiwasilisha	Haina wakati wahuisi wa kuiwasilisha. Inaweza kusomwa wakati wowote.
Uwasilishaji huandamana na utendaji	Kwa kawaida haiambatani na utendaji isipokuwa inapoigizwa. Hadhari husoma tu kazi iliyoandikwa.
Hushirikisha wahusika wa namna mbalimbali kuanzia; mazimwi, mimea, wanyama, miungu au vitu visivyo na uhai	Ingawa inaweza kushirikisha wahusika wa aina mbalimbali, kwa kiasi likubwa wahusika wake ni binadamu.
Inakuza vipawa vya wawasilishaji.	Andishi hutegemea maandishi ya msanii.
Simulizi haina gharama ya uchapishaji.	Andishi ina gharama kubwa ya uchapishaji
Simulizi hutumia viziada Lugha kama ngoma na ishara	Andishi huitegemea viziada Lugha.
Fasihi simulizi ina fuzo maalum ambalo liko wazi	Fasihi andishi huwa na mafunzo ambayo wakati mwingine hayaeleweki
Fasihi simulizi hujadili matatizo ya jamii	Fasihi andishi hujadili matatizo ya wasomi
Fasihi simulizi wetendaji wake wako na uhuru wa kuongea kupungua jinsi watakavyo.	Fasihi andishi hufuatwa kama iliyoandikwa.

9. Fasihi Simulizi

A. Ngomezi ni fasihi ya ngoma :
Zama za muziki ambazo huwa na mipigo maalum yanayotoa midundo, wizani au toni za kipekee hutumiwa kuwasilisha dhama, wazo au ujumbe fualni ambao hueleweka tu na wanajamii husika. (alama 4)

B.

- Hutumia ala mbalimbali za muziki k.m ngoma, panda, baraghumu, zumari ili kupeleka ujumbe.
- Hueneza ujumbe juu ya vita, kuzaliwa mtoto, ndoa, kifo, vita, mvua.
- Midundo ya vyombo haitumiki kama muziki wa kuburudisha bali huwa njia ya kupitisha ujumbe.
- Kuna aina mbili : ya kwanza ni kutumia ala ili kutoa ujumbe fulani labda wa kuonya watu kama kuna adui anakuja au kuna msiba na ya pili huwa inabeba ujumbe wa kifasihi. Midundo hujulikana na wenyeji lakini wageni huwa hawawezi kuelewa.
- Wanajamii pekee ndiyo wanaweza kuufasiri mdundo wa ala hiyo ya muziki.
- Ujumbe huweza kufichwa kwa wasiohusika.
- Ujumbe maalumu au wa dhamira huweza kupitishwa kwa wepesi na urahisi. (zozote 6x1=6)

C. Umuhimu wa ngomezi:

- Huwa njia ya kutoa taarifa ya kuwafahamisha wanajamii kuhusu matukio mbalimbali.
- Hutahadharisha watu kuhusu matukio ya dharura k.m uvamizi au kuingiliwa na maadui (hatari)
- Hutumika kutoa matangazo rasmi k.m kifo, harusi.
- Hudhihirisha ufundi wa kisanaa.
- Ni njia moja ya kudumisha utamaduni wa jamii.
- Hutekeleza majukumu ya maandishi katika jamii.
- Huharakisha mawasiliano.
- Hufumba njumbe Fulani. (zozote 6x1=6)

D. Ngomezi za kisasa

- Simu za rununu na zingenezo huwa na milio mbalimbali.
- Kengele-hutumiwa shuleni, mahali pa (maabadani) ibada, majumbani.
- Mahakamani kuna mlio wa nyundo ya hakimu baada ya kukata kesi.
- Filimbi hutumiwa michezoni.
- Magari huwekwa milio ya kupiga honi au yaguswapo.
- Kengele za umeme milangoni unapotaka kufunguliwa (ving'ora)
- Mlio ya magari ya polisi. Sauti za taharuki, km. Mwizi ! mwizi !

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA KAUNTI YA NYERI
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya
102/1
KISWAHILI
Karatasi ya Kwanza
(INSHA)
Julai /Agosti 2015

1. **LAZIMA**
   Wewe pamoja na wataalamu wengine wa masuala ya afya, mmekabiliwa na visiki vingi katika kuhamasisha watu dhidi ya kujikinga na kudhibiti ugonjwa wa Ukimwi nchini. Andika makala kwa mhariri wa jarida la Afya Yetu ukilalamikia suala hilo.
2. Eleza changamoto zinazokabili mfumo wa serikali za ugatuzi nchini Kenya.
3. Yaliyopita si ndwele, tugange yajayo.
4. Andika kisa kitakachomalizikia kwa:
   . . . tangu siku hiyo nilitanabahi kuwa marafiki wengine ni kama lumbwi.

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA KAUNTI YA NYERI
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya
102/2
KISWAHILI
Karatasi ya Pili
(Ufahamu, ufupisho, Sarufi na matumizi ya lugha na Isimujamii)
Julai / Agosti 2015

UFAHAMU (ALAMA 15)
Soma taarifa inayofuata kisha uyajibu maswali
Vijana ni tegemeo kubwa kwa kila taifa na bila shaka wao ni viongozi wa kesho kama ilivyo msemo wa kawaida. Isitoshe, takwimu za idadi ya watu nchini Kenya zinaonyesha kuwa idadi ya vijana inachukua asilimia sitini hivi, hii ikiwa ni sehemu kubwa ya wapigaji kura ambao uamuzi wao hutupa viongozi, wanasiasa wema na wabaya. Ndiposa kila taifa lenye masomo ya kuwa na maendeleo, lazima liweze kutambua umuhimu wa vijana ambao ni asasi muhimu ya maisha na viongozi wa kesho. Serikali imejaribu kuanzisha miradi mbalimbali humu nchini kwa minajiri ya kuwainua vijana.

Tumeona kazi kwa vijana na kulifurahia wazo nzuri la serikali kuona kwamba vijana wanapata kazi na pato japo kidogo. Lakini mbona ufisadi na ufujaji wa pesa kama hizi umekuwa kama sumu ya kuharibu kilicho kizuri?Tungependa kuona vijana wakishirikishwa katika utendakazi badala ya kukaa hivi hivi mitaani pasi na kufanya lolote,si mapenzi ya wakenya kuwaona vijana wakiogelea kwenye dimbwi la vileo na dawa za kulevya.

Taifa letu linawahitaji vijana, siyo tu kwa kutumiwa kuwapigia debe vigogo **wa kisiasa lakini tunawahitaji kama mihimili muhimu ya viongozi wa** kesho.Simba akikosa nyama,tumesikia kuwa yeye hula nyasi na mtoto akikosa la mama hata la mbwa huamwa.

Ukosefu wa kazi na hasa kwa vijana umekuwa kama limbukizi la makaaa kwenye tanuri la matatizo kwa vijana na kwa kukosa matumaini, wengi wa vijana wamejitosa kwenye ulevi wa kila aina ya vileo, bora tu mtu ajihisi kuwa yupo mbingu ya tatu kama si ya nne.Hali ya maisha ya vijana imekuwa si hali tena na hasa vijana wanaume. Kwa wale wameoana wamebaki tu kuwa picha kwenye ndoa zao,ulevi umetamalaki maisha yao hivi kwamba hata kupata watoto ni kama tu kupanda mchongoma.

Kaunti mbalimbali za Kenya zinalia, mabibi wakiwalilia waume wao. Kila siku imekuwa ni siku ya maandamano,wakiandamana kwa sababu ya pombe haramu ambazo zimewaoa waume zao na kuwafanya watumwa na si watumwa tu lakini watumwa hanithi ambao hawawezi kupata watoto katika hali zao.

Inafedhehesha kuona hata nyumba nyingi zinaongozwa na kutunzwa na mabibi.

Hivyo basi kilichobaki ni wakenya wote kwa jumla kuendeleza na kuunga mkono sheria ya

Mututho,ili tuwaokoe viongozi wa kesho.Asiyesikia la mkuu mwishowe ...

Maswali

a) Eleza matatizo yanyokumba juhudi za kuwainua vijana. (alama 3)
b) Kulingana na mwandishi, kwa nini ni muhimu kuwashughulikia vijana? (alama 2)
c) Mwandishi anamaanisha nini kwa kusema, limbikizi la makaa kwenye tanuri la matatizo? (alama 2)
d) Kwa vijana ambao ni waraibu wa ulevi, kupata watoto ni kama tu kupanda mchongoma. Eleza (alama 2)
e) Pendekeza njia za kusuluhisha tatizo la ulevi kwa vijana. (alama 3)
f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika kifunguni. (alama 3)
   i) Mihimili
   ii) Asasi
   iii) Pigia debe
   iv) Pombe haramu ipigwe marufuku

2. UFUPISHO (ALAMA 20)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.

Nimekaa na kutafakari kwa kipindi kirefu, juu ya mabilioni ya pesa ambayo yametengwa na serikali ili kudhamini miradi ya maendeleo ya wanawake. Kina mama au wanawake wengi wanafikiri na kusema kwamba fedha hizo zimewawezesha kuwaondoa katika lindi la unyanyasaji kutoka kwa waume zao, kwani kila mmoja anamheshimu mwenzake kwa sababu ya kipato alicho nacho. Wengi wameweza kuanza biashara ndogondogo ambazo huwaletea angaa kipato kidogo.

Ukweli ni kwamba fedha hizi zimesaidia kuwatoa wanawake wengi katika unyanyasaji, kwani wengi wanaweza kuanzisha kazi za ujasiriamali na hata kuendesha shughuli mbalimbali za maendeleo.

Kutokana na mafanikio haya, wabunge waliopitisha hoja bungeni ya kuanzisha mpango huu wa kuwakwamua wanawake kimaendeleo wanafaa kupongezwa. Mafanikio haya yamewafanya akina mama kujikimu kimaisha na hivyo kutowategemea wanaume katika kila jambo.

Ukitaka kujua ukweli kuhusu hili, nenda kwenye masoko utaona akina mama jinsi wanavyohangaika na biashara zao. Kwa hivyo, usajiriamali huendelezwa na akina mama zaidi na hivyo wanapaswa kuwezeshwa kwa kila hali na mali.

Akina mama pia wanafaa kupongezwa kwani wameamua kujitosa kukopa pesa kwenye taasisi mbalimbali za fedha. Fedha hizo kwa kiwango kikubwa zimewainua kutoka ufukara uliokithiri hadi katika maisha ya heshima. Wale ambao hawajaribu kuchukua mikopo, ni muhimu wafanye hivyo ili wajikimu kimaisha.

Maisha ya sasa ni magumu, hivyo yanahitaji kusaidiana kwa kila hali na mali. Wanaume kwa wanawake ni vyema wachange bia ili wazumbue riziki. Ushirikiano utarahisisha maisha yao.

Hata hivyo, sio tu akina mama hao wameondokewa na unyanyasaji waliokuwa wakiupata ndani ya nyumba zao, toka kwa akina baba, bali hata masuala ya mrundikano wa kesi za kugombea ardhi kwa akina mama, zimepungua . Sababu ni kwamba akina mama wengi wameweza kujitafutia ardhi wenyewe kwa fedha walizonazo.

Ukweli ni kwamba hali imebadilika. Kinyume na hapo awali ambapo majumba ya kifahari na mashangingi yalikuwa hifadhi ya wanaume, siku hizi wanawake wanamiliki hayo yote.

a) Ukizingatia aya nne za mwanzo, eleza hoja muhimu kwa maneno kati ya (55 - 60) (alama 7)
b) Bila ya kubadili ujumbe wa mwandishi, fupisha aya tatu za mwisho. (Maneno kati ya 45 - 50) (alama 5)

3. MATUMIZI YA LUGHA. (ALAMA 40)

a) Taja sauti yenye sifa zifuatazo.
   i) Chini-kati, midomo hutandazika. (alama 1)
   ii) Kikwamizo sighuna cha menoni. (alama 1)
b) Andika anavyoitwa mtendaji wa vitendo hivi. (alama 3)
   i) Cheka
   ii) Gomba
   iii) Kaa
c) Bainisha mofimu zinazounda neno 'halijasahaulika'.

(alama 3)

d) Nomino zifuatazo ziko katika ngeli gani.
   i) Makamasi. (alama 1)
   ii) Boga (alama 1)

e) Andika sentensi ifuatayo kwa kufuata maagizo uliyopewa mabanoni.
   (alama 2)
   Nguo hizo zilifuliwa na mtwana (Anza kwa: Mtwana na utumie kiashiria kisisitizi cha mbali kidogo)

f) Tunga sentensi sahihi ukitumia vitenzi vifuatavyo katika kauli uliyopewa.
   i) - la (tendesha)
   ii) fumba (tendata)

g) Andika sentensi ifuatayo katika wakati uliopita hali timilifu.
   Seremala huwajengea watu nyumba.
   (alama 2)

h) i) Taja matumizi yoyote ya alama ya mtajo. (alama 1)
   ii) Dhihirisha matumizi hayo katika sentensi. (alama 1)

i) Hii ni sentensi ya aina gani.
   (alama 1)
   Hamisi na Halima wanaenda sokoni sasa hivi.

j) Onyesha yambwa na chagizo katika sentensi ifuatayo. (alama 3)
   Kasavuli aliandikiwa barua na Amina kwa kalamu.

k) Kanusha katika hali ya wingi. (alama 3)
   Dole lilikatwa kwa jisu.

l) Tumia neno 'kimya' katika sentensi kama:
   i) Kielezi. (alama 1)
   ii) Nomino (alama 1)

m) Geuza sentensi hii iwe katika usemi halisi
   (alama 2)
   Mtoto alisema kuwa angewatembelea kwao mwezi ambao ungefuata.

n) Fafanua matumizi ya 'JI' katika sentensi zifuatazo.
   (alama 2)
   i) Picha hii ilichorwa ma mchoraji yule.
   ii) Najisomea

o) Tumia 'o' rejeshi tamati. (alama 2)
   Wanafunzi ambao walipita mtihani ni wale ambao walisoma kwa bidii.

p) Andika kinyume cha sentensi. (alama 2)
   Mama ameombwa aanike mtama.

q) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mchoro wa mishale. (alama 4)
   Mwembe ule uliokatwa jana utakauka haraka.

r) Badilisha kiambishi awali cha ngeli kiwe kiambishi cha kati.
   (alama 1)

4. ISIMUJAMII (ALAMA 10)

a) Eleza maana ya viziada lugha. (alama 1)

b) Fafanua sababu zozote NNE zinazomfanya mzungumzaji kutumia viziada lugha.
   (alama 4)

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA KAUNTI YA NYERI
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya
102/3
KISWAHILI
FASIHI YA KISWAHILI
Julai / Agosti 2015

1. **LAZIMA : SEHEMU YA A**
TAMTHILIA:
Mstahiki Meya *: Timothy M. Arege*

1. ". . . kwa unyenyekevu tunakuomba kutumia mamlaka hayo."
a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
b) Mamlaka yanayozungumziwa katika dondoo hili ni yepi? (alama 2)
c) Dhibitisha kuwa msemewa alitumia mamlaka yake vibaya. (alama 12)
d) Taja na ufafanue sifa moja ya msemaji inayobainika katika dondoo hili. (alama 2)

SEHEMU YA B
RIWAYA:
Kidagaa kimemwozea *; Ken Walibora*
Jibu swali la 2 au la 3

2. "Huyu mwendawazimu anakuja nini kwenye sherehe hizi? Anafikiri sherehe hizi ni za watu wenye kichaa kama yeye?"
a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Fafanua maisha ya mwenda wazimu anayerejelewa.
(alama 8)
c) Onyesha mwendawazimu huyu alivyotekeleza lengo lake la kuhudhuria sherehe kisha uonyeshe yaliyompata.
(alama 8)

3. Jadili mbinu zifuatazo za uandishi kama zilivyotumiwa na mwandishi wa *Kidagaa kimemwozea.*
(alama 20)
a) Taswira
b) Sadfa
c) Kuchanganya ndimi
d) Tashhisi / Uhuishi.

SEHEMU YA C
HADITHI FUPI
Damu Nyeusi na Hadithi nyingine *Ken Walibora na Said A. Mohamed*
Jibu swali la 4 au la 5

4. Maudhui ya ubaguzi na utabaka yamepewea uzito na waandishi wa Diwani ya Damu Nyeusi na hadithi nyingine. Kwa kurejelea hadithi zozote tano, onyesha ukweli wa kauli hii. (alama 20)

5. "Mimi nilitaka mke, mwanamke mbichi nimvumbike mwenyewe mpaka aive."
a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
b) Kwa nini msemaji alitaka amvumbike mwanamke mwenyewe? (alama 4)
c) Eleza migogoro iliyochipuka baina ya msemaji na mwanamke huyo. (alama 12)

SEHEMU YA D:
USHAIRI
Jibu swali la 6 au la 7

6. Waza hili pulikiza, mja akili tumia,
Waza uweze jijuza, utatimizaje nia,
Waza ukitekeleza, waza matokeo pia,
Waza mlimwengu waza, waza ninakuhimiza!

Waza mwanzo peleleza, zote usijepapia,
Waza na kujiuliza, zipi za kuzingatia,
Waza upate kuiza, hasa zisosaidia,
Waza mlimwengu waza, waza ninakuhimiza!

Waza uweze punguza, dhila pamwe na udhia,
Waza patajitokeza, pema pa kukimbilia,
Waza na utajikweza, kilele ukafikia,
Waza mlimwengu waza, waza ninakuhimiza!

Waza ukiiangaza, michango ukichangia,
Waza na wenza kuuza, ni zipi zao hisia,
Waza ndipo utaweza, vyema kuwahudumia,
Waza mlimwengu waza, waza ninakuhimiza!

Waza likikutatiza, jambo linapotukia,
Waza ikiwa waweza, kutenda likatimia,
Waza kama kupuuza, kwenyewe kutafidia,
Waza mlimwengu waza, waza ninakuhimiza!

Waza ukizungumza, ama unaposikia,
Waza unazotangaza, zifaidi jumuia,
Waza kama kunyamaza, sana kutasaidia,
Waza mlimwengu waza, waza ninakuhimiza!

Waza ikiwa kubeza, huji ukakujutia,
Waza utakavyokuza, kuliko kulichukia,
Waza vipi kwaumiza, kwenyewe kuliridhia,
Waza mlimwengu waza, waza ninakuhimiza!

Waza unalotukuza, lina mia fil mia?
Waza usijepumbaza, visivyo kukadiria,
Waza kwa haki kutuza, wala si kwamba wawia,
Waza mlimwengu waza, waza ninakuhimiza!

Waza na kujiliwaza, janga linapotukia,
Waza mwenzangu tuliza, usikufuru sikia,
Waza usijepooza, dhila ni mpita njia,
Waza mlimwengu waza, waza ninakuhimiza!
Redscar McOdindo.

a) Fafanua manufaa ya kuwaza kama yalivyoelezwa katika shairi. (alama 4)
b) Eleza nafasi ya mbinu ya takriri katika shairi hili. (alama 2)
c) Dondoa na ueleze mifano miwili tofauti ya uhuru wa kishairi katika shairi. (alama 4)
d) Eleza umbo la shairi hili. (alama 4)
e) Andika ubeti wa saba kwa lugha nathari. (alama 4)
f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika shairi. (alama 2)
i) Dhila
ii) Kutafidia.

7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

Ajaye kisimani mbele, hunywa maji maenge,
Asinywe yalo na vunju,
Yakampa kigegezi
Yakamtibua roho akaona na kinyaa,
Awali ndio awali awali mbovu hamna.
Ikiwa utalimatia,
Utayaramba makombo,

Uvidata vitu cheche
Kisoma aali kikupe kisogo,
Inajuzu ujihimu

Mwanafuu darasani
Uraukapo bukrata
Katu hutayaramba makombo
Hutakosa kisebeho.

Dereva nawe utingo,
Natija ni asubuhi,
Wateja utawawahi,
Wasaa kuzingatia,
Uwafikishe kazini,
Kwa wasaa ufaao,
Wasije wakateteshwa na
bosi wao nao wakuapize

Nawe mwanazaraa,
Mpini uukamate kabla,
Jua kutiririsha majasho jasadini,
Ushindwe kung'oa magugu,
Kutoka kwa lako konde.

Mhadimu mwenye zohali,
Yajuzu ujihimu
Maziwa ununue majogoo
Usije ukayadata na hivyo
Ukaandaa chai mkandaa
Wateja wakuambae mithili ya ibilisi.

a) Shairi hili ni la aina gani? Eleza. (alama 2)
b) Eleza nasaha yoyote inayotolewa kwa wafanyikazi wote watatu.
(alama 3)
c) Je, wafanyakazi waliolengwa na mshairi wataathirika vipi endapo hawatafuata ushauri wanaopewa kwenye shairi?
(alama 3)
d) Kwa mujibu wa shairi, mwanafunzi anahimizwa kurauka mapema kwa nini?
(alama 2)
e) Tambua tamathali zozote mbili zilizotumiwa na mtunzi. (alama 2)
f) Taja sifa zozote mbili za kimuundo zilizotumiwa na msanii.
(alama 2)
g) Andika ubeti wa kwanza wa lugha nathari.
h) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika kwenye shairi. (aslama 2)
   i) Wakuapize.
   ii) Jasadini.
i) Onyesha matumizi yoyote ya msitari mshata. (alama 1)

SEHEMU YA E:
FASIHI SIMULIZI
Jibu swali la 8

8. a) Fasihi simulizi ni nini? (alama 2)
b) Fafanua sifa tano za fasihi simulizi. (alama 10)
c) Ni matatizo gani yanayoweza kumkumba mtafiti wa data wa Fasihi Simulizi. (alama 8)

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA KAUNTI YA NYERI
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya
102/1
KISWAHILI
FASIHI YA KISWAHILI
Julai / Agosti 2015

MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA

1. Insha ichukue muundo wa barua rasmi (barua kwa mhariri)
   Mwanafunzi azingatie hoja zifuatazo

a) Swala la dini - baadhi ya madhehebu kupinga matumizi ya mipira. Dini nyingine kutozingatia suala la matibabu
b) Mila na desturi za kijamii kwa mfano urithi wa wanawake katika jamii fulani
c) Imani potovu - baadhi ya watu kuamini ukimwi ni laana inayostahili matibabu ya waganga na wachawi
d) Ukosefu wa dawa za kupunguza makali ya ukimwi
e) Wahasiriwa maskini kuuza dawa zao kwa watu wengine kwa mfano wapishi wa pombe haramu
f) Ukosefu wa elimu
g) Wahasiriwa kuogopa kujitokeza hadharani

2.

- ufujaji wa pesa na matumizi mabaya ya mali ya majimbo na gavana na wawakilishi wa wadi / wodi ukiukaji wa sheria za majimbo
- mvutano kati ya magavana na maseneta kuhusu mamlaka juu ya majimbo changamoto kuhusu uajibikaji wa magavana kwa umma
- ubinafsi na unafiki wa magavana
- migogoro kati ya magavana na wawakilishi wa wodi katika majimbo / kufurushwa kwa magavana na wawakilishi wa wodi
- mfumo huu wa utawala unatumia pesa nyingi kugharamia mishahara ya wananchi walioajiriwa katika gatuzi mbalimbali
- baadhi ya majimbo yana idadi kubwa ya wananchi kwa hivyo wanapogawiwa pesa kutoka kwa serikali kuu, hazitoshi kutimiza mahitaji yao
- mfumo huu wa utawala unatumia pesa nyingi kugharamia mishahara ya wananchi walioajiriwa katika ofisi mbalimbali za majimbo
- kuongezwa kwa ushuru kwa wafanyi biashara ili kutosheleza mahitaji ya serikali za majimbo
- kurudufisha majukumu ya magavana na maseneta

3. Insha ichukue muundo wa mtiririko wa kisa kinachodhihirisha maana ya methali. ‘Mabaya yaliyopita si muhimu, tuwazie / tufikirie / tutazamie mazuri yaliyo mbele yetu

4. **Hii ni insha ya mdokezo**

- Ni lazima mtahiniwa amalizie kwa maneno ya mdokezo
- Kisa kilenge rafiki mnafiki / asiyeaminika / anayebadilikabadilika au aonyeshe ugeugeu wa marafiki

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA KAUNTI YA NYERI
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya
102/1
KISWAHILI
FASIHI YA KISWAHILI
Julai / Agosti 2015

MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA

1. a) Ufisadi na ufujaji wa pesa za kazi kwa vijana
Matumizi ya pombe na dawa za kulevya
Ukosefu wa kazi kwa vijana
Vijana kukosa matumaini maishani
Matatizo ya unyumba ***zozote 3 x 1 = alama 3***

b) Ndio tegemeo la kila taifa (viongozi wa kesho)
Wao ni asilimia 60 ya watu nchini Kenya (wapigaji kura)
Ni asasi muhimu ya maisha na viongozi wa kesho ***zozote 2 x 1 = 2***

c) Kuongeza shida mahali penye shida zingine tayari (kuharibu zaidi)

d) Hawataweza kupata watoto na wake wao kwa sababu ya nguvu za kiume kuathiriwa na pombe ***alama 2***

e) Kuwekwa na kuzingatiwa sheria mwafaka za kukabili ulevi kupindukia
Vijana wapewe nafasi za kazi
Wakubali kufanya kazi yoyote ile. Wasibague kazi
Pombe haramu ipigwe marufuku ***zozote 3 x 1 = alama 3***

f) i) Nguzo muhimu / tegemeo
ii) Asasi - idara / kitengo cha jamii kinachotoa huduma fulani
iii) Kuwatetea / kuwapigania / kuwatangaza zuzuru ubora wa mtu

2. MUHTASARI

a)

- Mabilioni ya pesa yametengwa na serikali kudhamini maendeleo ya wanawake
- Wanawake wamekiri kwamba fedha hizo zimewawezesha kuwaondoa katika unyanyasaji wa waume wenzao
- Wengi wameanza biashara zinazowapa kipato
- Wameanzisha kazi ya usajiriamali na kuendesha shughuli za maendeleo
- Wabunge waliopitisha hoja ya kuanzisha mpango wa kuwakwamua wanawake kimaendeleo wafaa kupongezwa
Wameweza kujikimu

– Usajiriamali huendelezwa na akina mama zaidi hivyo wapaswa kuwezeshwa ***1 x 7 = 7 mtiririko x 2***

b)

- Akina mama wamejitosa kukopa fedha kutoka kwenye taasisi mbalimbali
- Fedha hizo zimewaingiza katika maisha ya heshima
- Maisha ya sasa yanahitaji kusaidiana wanaume kwa wake ili wazumbue riziki kwa urahisi
- Mrundikano wa kesi za kugombea ardhi kwa akina mama zimepungua
- Wengi wameweza kujitafutia ardhi pia wanamiliki majumba ya kifahari ***1 x 5 = 5 mtiririko x 1***

3. a) i) / a /
ii) / th /

b) i) Mchekaji / mcheshi
ii) Mgomvi
iii) Mkaaji / mkaazi ***3 x 1 = 3***

c) Ha - kikanushi
li - ngeli
ja - kikanushi cha hali ya me
sahau - mzizi
lik - kauli / mnyambuliko
a – kiishio ***6 x ½ = 3***

d) i) ya - ya (1)
ii) li - ya (1) (1) (1)

e) Mtwana alizifua nguo zizo hizo ***ala. 2***
f) i) lisha (1)
ii) fumba (1)
g) Seremala alikuwa amewajengea watu nyumba ***2 x 1 = 2***

h) i)
- kuonyesha usemi halisi
- kunukuu anwani ya kitabu au kipindi katika redio au runinga
- kufungia neno la kukopwa (1)

ii) Mwanafunzi atunge sentensi kwa kutumia matumizi aliyotaja. Asipopata la kwanza hapati la pili al. 1
i) Sahili (1)
j) Kasavuli - yambwa tendewa
Barua - yambwa tendwa
Kwa kalamu – chagizo ***3 x 1 = 3***
k) Madole hayakukatwa kwa majisu ***3 x 1 = 3***
l) Mifano
i) Nyamaza kimya mpaka nitakapokuita al. 1
E
ii) Kimya kingi kina mshindo mkuu. al. 1
N
m) " Nitawatembelea kwenu mwezi ujao," mtoto alisema. ***4 x ½ = 2***
Tanbihi: Mwanafunzi akifungua lazima afunge. Asipofunga atuzwe (0)
n) i) Kuonyesha uzoefu wa kutenda jambo / mazoea
ii) Kurejelea mtendaji wa jambo ***2 x 1 = 2***
o) Wanafunzi wapitao mtihani ni wale wasomao kwa bidii. ***2 x 1 = 2***
p) Mama ameagizwa / ameamrishwa / amelazimishwa / ameshurutishwa aanue mtama.
Tanbihi: Akibadilisha mama apoteze nusu ***alama 2 x 1 = 2***
q) S ⟶ KN + KT
KN ⟶ N + V + S
N ⟶ mwembe
V ⟶ ule
S ⟶ uliokatwa jana
KT ⟶ T + E
T ⟶ utakauka
E ⟶ haraka ***8 x ½ = 4***
r) Wanafunzi hawa waliipanda miti (***al. 1)***

ISIMU JAMII

4. a) Ni matumizi ya ishara kv za mikono na uso mtu anapozungumza ili kusisitiza jambo fulani***al. 1***
b)
- Hisia - kwa mfano mtu akiwa na furaha au hasira huadhirika kupitia uso wake
- Hali ya mtu
Kunao walio na tabia ya kutupatupa mikono au kuwagusa wenzao wanapozungumza kwa nia ya kutilia mkazo wanachokisema

- Ukosefu wa muda wa kutosha
Huenda ikawa mzungumzaji ana muda mfupi sana wa kusema aliyonayo. Katika hali hii mzungumzaji huona kuwa ni bora maneno yake yaandamane na ishara

- Kudumisha siri
Ishara hutumika pale ambapo mzungumzaji anataka kusema jambo ambalo ni la siri na hataki wengine wajue mf. Wanaovuta sigara hutumia ishara kuuliza kama mwenzake ana sigara

- Ulemavu
Vigugumizi hulazimika kuambatanisha mazungumzo yao na viziada kwa sababu ya kudodosa kwingi katika mazungumzo yao ***zozote 4 x 1 = al. 4***
c)

- Mazingira yanapobadilika lugha huhitaji kupanuliwa ili kukidhi haja ya mawasiliano. Fafanua njia zozote tano za kupanua msamiati wa lugha ya Kiswahili

  Majibu
- Kuunganisha maneno ili yaunde neno moja. Kwa mfano jopkazi, nguvukazi
- Kutohoa maneno kutoka kwa lugha za kigeni
- Kuchukua maneo kutoka kwa lugha nyingine za kibantu
- Kuunganisha vifupisho ukimwi - upungufu wa kinga mwilini
- Kutumia tafsiri sisisi. Kwa mfano simu ya mkono - mobile handset
- Kuunda maneno kimaksudi kwa kuangalia umbo lake, sifa na kazi ya kitu
- Kuchukua maneno kutoka kwa lahaja za Kiswahili ***zozote 5 x 1 = 5***

JARIBIO LA TATHMINI YA PAMOJA KAUNTI YA NYERI
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya
102/3
KISWAHILI
FASIHI YA KISWAHILI
Julai / Agosti 2015

MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA

1. a) Ni maneno ya Diwani I kwa meya ofisini mwa Meya baada ya mgomo wa wafanyakazi ***1 x 4***
   b) Kuunda kamati shawishi nyingi apendavyo na kuteua viongozi apendavyo ***2 x 1***
   c)
- ubadhirifu wa mali ya umma
- unyakuzi wa ardhi
- wizi wa fimbo ya Meya
- kuongeza madiwani mishahara baraza ilikiwa na nakisi
- swala la sadaka ya mhubiri ya laki moja kila mwezi na kumpa mafuta ya gari
- kupuuza malalamishi ya wafanyikazi
- sheria dhalimu za kukandamiza raia
- kushirikisha wasio wafanyikazi wa baraza la mji wa cheneo k.v Bili kuamua masuala ya baraza
- matumizi mabaya ya magari ya baraza
- kusitisha kandarasi kinyume na sharia ***zozote 6 x 2 = 12***

   d) Mshauri mbaya - kumshauri Meya kutumia mamlaka yake kuunda kamati za madiwani shawishi ***kutaja 1***
   kufafanua 1

2. Huyu mwendawazimu anakuja nini kwenye sherehe hizi ? Anafikiri sherehe hizi ni za watu wenye kichaa kama yeye?" Uk.69

a) Fafanua muktadha wa maneno haya
- Haya ni maneno ya Mashaka bintiye Mtemi Nasaba Bora
- Anaongea na nafsi yake
- Hapa ni katika uwanja wa Nasaba Bora
- Mashaka alikuwa amechukua barua kutoka kwa Ben Bella mpenzi wake na kuelekea katika vyoo vilivyotengewa waheshimiwa na jamaa zao na kumpita Mzee Matuko Weye ndipo akawaza maneno haya ***4 x 1 = 4***

b) Fafanua maisha ya mwendawazimu anayerejelewa
- Mzee Matuko Weye alikuwa mwendawazimu maarufu ambaye hakuwa na mbele wala nyuma
- Aliweza kulala popote pale na alivaa kaptura juu ya suruali, zote mararu
- Aliwahi kwenda Burma kupigania Uingereza katika vita vya pili vya dunia akiwa na akili razini
- Aliporudi kutoka Burma akili yake ilikuwa imeruka akawa havai viatu na riziki yake ikawa imepotea
- Licha ya ukongwe wake alifanya kazi za sulubu
- Alipopewa chakula alipenda kula kitoweo kwanza kisha ale chakula chenyewe k.m. alipopewa sima na mboga alianza kwa kula mboga kisha sima. Pia alipopewa kuku na chapati alikula kuku kwanza kisha chapati. Pia alipopewa chakula au kinywaji alikula na kunywa kisha kuondoka bila shukrani wala rabsha
- Alipenda kupiga kwata na kusema "mark-time, "about-turn", "left-right" alipokumbuka awali alipokuwa jeshini
- Alipita akitoa simulizi za vituko na visa vya vitai nusu vya kweli na nusu visivyo vya kweli ***8 x 1 = 8***

c) Onyesha mwendawazimu huyu alivyotekeleza lengo lake la kuhudhuria sherehe kisha uonyeshe yaliyompata

- Alipanda jukwani haraka haraka baada ya hotuba ya Mtemi Nasaba Bora na kuchukua kipaza sauti
- Alihutubia umati na kuwaambia kuwa walikuwa wamechoshwa na dhuluma wanazofanyiwa na Bwana Mtemi
- Anawazindua waliohudhuria sherehe kwa kuwauliza kama walikuwa wamefumba macho na kutoona dhuluma wanazofanyiwa na Mtemi Nasaba Bora
- Anauambia umati kuwa Mtemi Nasaba Bora anawadhulumu kwa kuwapokonya mashamba, mali, mabinti na hata wake zao
- Wananchi walimsikiliza huku wamekumbwa na kucheka na kumaka
- Mzee Matuko Weye alitolewa jukwaani na askari waliombeba hobela hobela
- Kisha alifungwa katika jela ya chifu alikolala sakafuni kabla ya kuachiliwa baadaye ***4 x 2 = 8***

3. Kidagaa Kimemwozea

i) Taswira

- picha ya Amani na Imani wameketi kando ya mto Kiberenge chini ya mti
- picha ya askari wanaotumwa na Mtemi Nasaba Bora kwenda kulinyakua shamba la mamake Imani, mapigo anayoyapata mamake Imani, kuchomwa kwa nyumba ya Imani na Imani kutorokea kwenye dirisha
- taswira ya sefu ya Mtemi alimotoa bunduki na pia alimoambiwa na Yusufu kuwa ndimo Mtemi alimoweka hatimiliki. Picha hii haikumtoka Amani akilini
- sura ya Mtemi Nasaba Bora - mbilikimo mnene mweusi, mwenye pua tapwanya, miguu matege
- mandhari ya kasri la Mtemi Nasaba Bora magugu yaliyomea kote, uchafu uliokuwepo, nyua zisizotunzwa
- baki la tingatinga aina ya Massey Fergussion
- picha ya Mtemi Nasaba Bora akimwambia msichana yule washuke watembee mjini pamoja naye msichana kainama uvunguni mwa kiti na kutoa mikongojo yake na jinsi Mtemi alivyoshangaa
- kufumaniwa kwa Amani na Bi Zuhura humo chumbani kwa Mtemi

ii) Sadfa

- Amani na Imani kukutana ni sadfa, kisha kukubali kuandamana hadi mjini sokomoko, jambo lililomzuia Imani kujitosa ziwani Mawewa
- Amani na Imani kupata kazi kwa Mtemi Nasaba Bora na mwalimu Majisifu, wawili hawa walikuwa wamewapunja
- Amani kukutana na amuye Yusufu jela kila mmoja akitumikia kifungo chake, Amani alikuja kujua ukweli wa kuwa Yusufu hakumuua Chichiri pia akaarifiwa kuhusu sefu alimoweka hatimiliki Mtemi Nasaba Bora
- inasadifu kuwa Imani anapoipokea barua kutoka kwa Amani kuhusu mswada ulioibiwa anaitwa na Dora na kuisahau ile barua mezani naye Majisifu anakuja na kuipata ile barua na kuisoma akafahamu kuwa Amani ndiye mwandishi wa kile kitabu
- inasadifu kuwa Gaddafi na genge lake wanapomvamia Mtemi anatoka hospitalini na kuwaomba Gaddafi wasimuue Mtemi ***zozote 5 x 1 = 5***

iii) Kuchanganya ndimi

- hali ya kuchanga maneno ya lugha tofauti na ile inayotumika katika sentensi moja
- wajua niko busy sana uk. 47
- refarii anasema ni free kick uk. 108
- basi tumpe ile servant quarter yetu uk. 139
- shut up! Acha kuzungumza kama mwanamke mpumbavu uk. 108
- lakini one day muwapo wadosi msinisahau mwenzenu DJ uk. 10
- basi comrades sote hapa tunafurahi pasipo shaka

iv) Tashhishi / uhuishi

- tumbo lake mwalimu Majisifu lilikataa chai katakata
- wema wako umeniua kabisa uk. 150

- mwalimu Majisifu hakutafuta kazi, zilimtafuta uk. 28
- hapana shaka bahati sasa ilikuwa inamnyoshea mkono kutaka kumsalimia, kumkumbatia uk. 116

4. Damu Nyeusi

a) Mke wangu

- Msimulizi alibagua mke ambaye angemwoa mf. Fedheha, Salma na Seluwa
- Alimbagua Fedhele kwa sababu walikutana usiku saa mbili za usiku, walikuwa amemtia kijana mwanaume katikati yao
- Alimbagua Salma kwa misingi ya utamaduni
- Msimulizi hakutaka muuza madafu aingie nyumbani alipoitwa na Aziza kwa vile ni maskini
- Msimulizi alikuwa wa tabaka la juu, wana nyumba kubwa na alipata kila kitu kutoka kwa wazazi wake
- Muuza madafu alikuwa wa tabaka la chini pia mkewe msimulizi Aziza ***zozote 4 x 1 = 4***

b) Samaki wa nchi za joto

- Peter aliwabagua watu weusi kwa madai kuwa ni wajinga na washirikina
- Mhindi aliyekuwa na Peter alimbagua Christine alimpuuza m.f. hakumsalimia
- Entebbe Sailing Club hakukuwa kunaingia watu weusi kutokana na ada za juu
- Peter nyumba yake ilikuwa kubwa na ilizungukwa na kuta za mawe kwa hivyo ni wa tabaka la juu
- Mandhari ya chumba cha Zac pamoja na vyombo vilivyokuwemo vilidhihirisha Zac ni maskini (tabaka la chini)

zozote 4 x 1 = 4

c) Damu Nyeusi

- Dereva wazungu walikataa kusimamishwa magari katika vituo vya kusimamia magari wakiwaona watu weusi mf. Fikirini
- Watu weusi kuulizwa maswali ya dharau na wahadhiri mbele ya wanafunzi wazungu
- Watu weusi kupelekwa kortini walipovuka barabara taa zikiwa nyekundu lakini wazungu wanaachiliwa wavuke
- Waafrika kufuatwa madukani wakidhaniwa ni wezi m.f. Fikirini
- Waafrika kubaguliwa kimasomo / elimu, mtihani ulikuwa sawa lakini wazungu walipendelewa kwa alama
- Waafrika katika hoteli kutazamwa kwa macho meupe ya chuku m.f. Fikirini
- Fikirini kuitwa na askari na kukamatwa alipotoka haja ndogo kwa kutofunga zipu
- Wazungu kuwaona waafrika kama wa tabaka la chini, ilichangia Fikirini kuulizwa maswali ya dharau

zozote 4 x 1 = al. 4

d) Shaka ya Mambo

- Utabaka kwa upande wa Esther, umaskini ulimbidi aende kutafuta kazi ajilipie masomo
- Mzee Mwinyi alikuwa na mali. Alimkaribisha Esther wakae na familia yake na kumkidhi kwa kila kitu
- Esther alibaguliwa kwa kutopatiwa ruhusa apumzike / kutobadilisha zamu yake
- Kamata alimbagua Esther na kuanza kutembea na Grace

6. a)

- Utajua matokeo ya jambo kabla ya kutenda
- Utajua ni yepi ya kuzingatia kwanza (kuondoa mtanziko)
- Utajua utakimbilia wapi uwe salama
- Utajua la kusema ndivyo usiudhi hisia za unaowahudumia
- Jambo linalokutatiza utajua iwapo utalitenda au kulipuuza
- Utajua iwapo unapaswa kukuza jambo badala ya kulibeza
- Utajua kama unalotukuza ni lenye faida ***4 x 1 = 4***

b) Neno waza limekaririwa kusisitiza umuhimu wa binadamu kuwaza kabla ya kutenda jambo ***2 x 1 = 2***

c) i) Inkisari - kuiza - kuuliza
zisosaidia - zisizosaidia
usijepapia - usije kupapia n.k ***2 x 2 = 4***

ii) Kuboronga sarufi - mja akili tumia - mja tumia akili
Ni zipi zao hisia - hisia zao ni zipi ***2 x 1 = 2***

d) Beti 9

Vina za, a
za, za
Mizan 8, 8 = 16
Shairi lina kibwagizo
Kila mshororo umegawanywa ukwapi na utao

e) Waza iwapo utabeza jambo usije ukajuta
Uwaze pia utakavyolikuza badala ya kulichukia
Ukiwaza utajua ni vipi litaumiza au kuridhisha
Mlimwengu nakuhimiza uwaze ***4 x 1 = 4***

f) Dhila - unyonge, mateso
Kutafidia - kutapasheleza, kutafaa ***2 x 1 = 1***

7. a) Masivina / vue / mavue - halizingatii kanuni za utunzi wa mashairi ya arudhi
alama 2

b) Eleza nasaha yoyote inayotolewa kwa wafanyakazi wowote watatu
Dereva na utingo - kuamka mapema kuwapeleka wasafiri kazini mwao
Mkulima - aamke mapema na kwenda shambani kulima
Mhadimu -aamke ili anunue vitu muhimu vinavyohijatika katika upishi mfano maziwa
alama 3

c) Je, wafanyakazi waliolengwa na mshairi wataathirika vipi endapo hawatafuata ushauri wanaopewa kwenye shairi ?
Dereva na utingo watalaaniwa / kulaumiwa na wasafiri ikiwa hawatawafikisha kazini kwa wakati ufaao
Mkulima atashindwa kufanya kazi kukiwa na joto kwani jua litamchoma
Mhadimu atatorokwa na wateja endapo atawapikia chai isiyo na maziwa baada ya kuchelewa kuyawahi
alama 3

d) Kwa mujibu wa mshairi, mwanafunzi anahimizwa kurauka mapema kwa nini
Awe na wakati wa kutosha wa kusoma
Asikose kiamsha kinywa / staftahi / kisebeho
alama 2

e) Tambua tamathali zozote mbili za semi zilizotumiwa na mtunzi
i) Methali - ajaye kisimani mbele hunywa maji mengi
Awali ni awali mbovu hamna
ii) Msemo / ndau - utayaramba makombo,
kikupa kisogo n.k.
iii) Takiriri - awali ndio awali awali mbovu hamna ***alama 2 zozote mbili***

f) <u>Taja sifa zozote mbili za kimuundo zilizotumiwa na msanii</u>
- matumizi ya beti
- matumizi ya mishororo
- matumizi ya lugha nyepesi
- matumizi ya maneno mengi ya Kiswahili sanifu

alama 3

g) <u>Andika ubeti wa kwanza kwa lugha nathari</u>
Mshairi anasema kuwa mtu ambaye hufanya jambo nzuri mapema kabla ya wengine hunufaika sana. Anaendelea kusema kuwa yule achelewaye hupata hasara na masazo hivyo anawahimiza watu wasiwe wakikawia
alama 3

h) <u>Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika kwenye shairi</u>
Wakuapize - wakulaani / wakuombee mabaya / wakufikirie maovu
Jasadini – mwilini ***alama 2***

i) <u>Onyesha matumizi yoyote ya mstari mshata</u>
Matumizi ya mstari mshata
Wasije wakateteshwa na
Mpini uukamate kabla ***alama 1***

8. a) Fasihi simulizi ni aina ya sanaa inayopokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa mdomo

b) Sifa za Fasihi Simulizi

- Fasihi simulizi ina utendaji. Uwasilishaji wa fasihi simulizi hutegemea maneno na vitendo. Mtambaji hutumia ishara za uso, miondoko ya mwili, miguno, toni na kiimbo anapowasilisha hadithi. Vilevile, mtambaji anaweza kutumia tanakali za sauti kwa kuiga milio ya viumbe fulani ili kusisitiza ujumbe wake.
- Fasihi simulizi ni hai. Yaani ina hadhira hai. Kuna uhusiano wa ana kwa ana kati ya fanani na hadhira yake. Katika uwasilishaji, fanani au msernaji anaweza kushirikisha hadhira zaidi kwa kuwataka kujibu au kuitikia kwa kukariri kiitikio fulani. Iwapo hadhira hairidhishwi na fanani, huweza kumpa maoni au mwitiko ambao
- utamwezesha kuirekebisha na kuiboresha kazi yake papo hapo.
- Fasihi simulizi lazima iwe na mtendaji (fanani) kwa vile fasihi hii hutendwa. Mtendaji anaweza kuwa mwimbaji kama ilivyo katika nyimbo, yeli/manju katika maghani, mtambaji katika ngano au mpigaji ngoma katika ngomezi. Mtendaji katika fasihi simulizi ana umuhimu wa kuuwasilisha utanzu wa fasihi simulizi nakuurithisha kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Wakati mwingine fan ani hubuni tungo za fasihi simulizi na kuziwasilisha papo hapo. Katika majigambo, kwa mfano, anayejigamba hubuni maghani na kuyawasilisha papo hapo.
- Fasihi simulizi huwa na mahali maalumu wa kutendea. Kwa mfano, sherehe za jando huwa na mahali maalumu pa kufanyiwa. Matambiko hufanyiwa chini ya miti mikubwa au pangoni na nyimbo huimbwa katika miktadha na mahali maalumu. Nyiso huimbwa jandoni, kimai huimbwa katika shughuli za baharini kama vile uvuvi na ubaharia, na mbolezi katika matanga.
- Fasihi simulizi ni mali ya jamii. Tanzu za fasihi simulizi zikishatendwa humilikiwa na kila mwanajamii. Hakuna anayeweza kudai kwamba ndiye mmiliki wa ngano, methali, vitendawili au tanzu nyingine za fasihi simuhzi. Mathalani, methali ni tungoza jamii wala si za mtu binafsi. Hata waliozikusanya na kuziandika vitabuni hawazimiliki.
- Wahusika katika fasihi simulizi huweza kuwa mazimwi, mizuka, wanyama, binadamu, milima, mawe, ndege, miungu au vitu.
- Fasihi simulizi ina wakati maalumu wa kuwasilishwa. Ngano,kwa mfano,hutambwa jioni baada ya shughuli za mchana. Nyiso huimbwa tu wakati vijana wanapokuwa jandoni na ulumbi husemwa wakati watu wanapokutana kwa shughuli fulani rasmi.
- Fasihi simulizi huwa na athari ya utegemezi. Uhai wa fasihi simulizi hutegemea uwezo wa fanani kuigiza. Wakati wa kutamba, fanani huiga vitendo vya mhusika wa hadithini ili kuifanya kazi yake kuvutia. Kwa sababu vitendo haviwezi kuingizwa katika maandishi, kule kutegemea fanani au mwasilishaji hufanya fasihi simulizi, kuwa chapwa inapoandikwa. Aidha, tanzu na vipera vya fasihi simulizi hutegemeana. Hadithi hutegemea methali kutoa funzo. Vitendawili navyo hutegemea taswira katika mafumbo.
- Fasihi simulizi ina historia ndefu. Fasihi simulizi pamoja na maisha ya binadamu. Hata kabla ya kuvumbuliwa kwa maandishi, fasihi simulizi ilikuwepo.
- Fasihi simulizi huzaliwa, hukua na kufa. Fasihi simulizi huzuka au huzaliwa na jamii. Hukua jinsi jamii inavyokua kwa kuongezewa tanzu mpya ili kufumbata matukio mapya katika jamii. Hata wakati jamii inapokufa, fasihi simulizi nayo hufa kwa kukosa kizazi cha kuiendeleza. Aidha, kwa vile fasihi simulizi huhifadhiwa bongoni, inaweza kupotea fanani akifa au hata akirukwa na akili.
- Fasihi simulizi huchukua umbo mahususi. Tungo za fasihi simulizi zina maumbo yenye sifa za kipekee. Ngano, kwa mfano, zina sifa ya mianzo na miishio ya kipekee. Methali zina maumbo ambayo hayabadilishwi. Vitendawili navyo vina sifa ya mtindo bainifu wa uwasilishaji.
- Fasihi simulizi hurithishwa na fanani kwa mdomo. Fanani ndiye huiwasilisha kwa hadhira kwa kutumia fani kama vile methali, ngano, mawaidha au nyimbo. Kwa njia hii, yeye hurithisha fasihi simulizi kwa vizazi na vizazi.
- Fasihi simulizi hubadilika kutegemea fanani, wakati na mazingira. Kila fanani ana mtindo wake wa kuiwasilisha. Jinsi fasihi hii inavyopitishwa na mafanani mbalimbali ndivyo inavyobadilika. Aidha, fasihi simulizi hubadilika kutegemea mazingira na wakati. Tashbihi, kwa mfano, hubadilika kutegemea hali hizi. Mathalani weusi waweza kulinganishwa na vitu mbalimbali kama vile -eusi kama makaa, -eusi kama mpingo ama -eusi kama lami

zozote 5 x 2 = 10

c) <u>Matatizo yanayomkabili mkusanyaji wa fasihi simulizi</u>

Baadhi ya matatizo ambayo humkabili mkusanyaji wa data za fasihi simulizi ni pamoja na yafuatayo:

- Gharama ya utafiti. Huenda gharama ikawa kubwa kiasi cha mtafiti kutoimudu. Mtafiti huenda akakosa pesa za kusafiria kwenda katika jamii mbalimbali au kununulia vifaa kama vile tepurekoda.
- Mtazamo hasi wa wanajamii kuhusu ujazaji wa hojaji huenda ukawafanya wengi wao kutojaza hojaji hizo.
- Wanajamii wengine huweza kushuku kwamba mtafiti anawapeleleza na wakakataa kutoa habari.
- Baadhi ya mafanani au wahojiwa huenda wakadai walipwe kabla ya kutoa habari zozote. Ikiwa mkusanyaji hana pesa, basi utafiti wake utakwamizwa.
- Mbinu nyingine za utafiti kama vile hojaji huhitaji watu wanaojua kusoma na kuandika. Ikiwa watu wanaohojiwa hawajui kusoma na kuandika matokeo ya utafiti huenda yasiwe ya kutegemewa.
- Vizingiti vya kidini. Hivi hutokea pale ambapo baadhi ya wahojiwa wanaamini kwamba matendo ya fasihi simulizi kama vile matambiko na ,uimbaji wa taarabu, yanaenda kinyume na imani yao ya kidini, na hivyo kukataa kuhojiwa.
- Kupotea au kufisidiwa kwa vifaa vya kuhifadhia data. Vifaa kama vile vinasasauti, video na santuri za kompyuta huweza kupotea au kuharibika kutokana na hali mbaya ya anga. Yote yaliyokuwa yamehifadhiwa vilevile yatapotea.
- Uchache wa wazee au wataalamu wa fasihi simulizi. Fasihi simulizi ilikuwa maarufu sana miongoni mwa wazee na pengine watu wa umri wa makamo. Kukosekana kwa wazee wanaoweza kutamba ngano ama kueleza vipera vingine kama vile vitendawili hutatiza mkusanyaji wa fasihi simulizi, na kwa hivyo huenda data ya kutegemewa isipatikane.
- Vikwazo kutoka kwa watawala. Watawala huenda wakakataa kutoa idhini ya kufanya utafiti. Baadhi ya taasisi fadhili pia huenda zikakataa kudhamini utafiti katika fasihi simulizi.
- Wadhamini mara nyingi ndio huamua mambo yanayochunguzwa, mahali pa kuchunguziwa na mawanda au upeo wa uchunguzi wenyewe. Aidha, fasiri ya ufafanuzi wa data mara nyingi lazima ilingane na maslahi ya
- wadhamini. Ikiwa mtafiti atatoa fasiri isiyowiana na mapendeleo ya wadhamini,huenda mapendekezo yake yakafutiliwa mbali na pengine udhamini wa utafiti zaidi kusitishwa. Aidha, matokeo ya utafiti mara nyingi huwa mall ya mdhamini ambaye huweza kuyatumia kuikandamiza jamii ya mtafiti.
- Mtafiti huenda asiwe na wakati wa kutosha kuwahoji watu wengi. Muda ukikosekana hatapata habari za kutosha kuhusiana na mada yake.
- Matatizo ya mawasiliano na uchukuzi. Ikiwa mkusanyaji analazimika kwenda mbali kukusanya habari, hasa katika sehemu kame, itakuwa vigumu kufika huko kwa sababu ya ukosefu wa vyombo vya usafiri kama vile magari.
- Matatizo ya kibinafsi. Anayekusanya fasihi simulizi anaweza kushindwa kuidhibiti hadhira. Badala ya kuwauliza maswali, wahojiwa wanaweza kuwa ndio wanaomuuliza mtafiti maswali. Kutojua lugha ya wahojiwa au kukosa mlahaka mwema na wahojiwa kunaweza kuathiri ukusanyaji wa kazi za fasihi simulizi.
- Ukosefu wa usalama. Huenda mkusanyaji wa fasihi simulizi akavamiwa. Aidha, baadhi ya watu si karimu na huenda wakamshuku mtafiti na kumvamia.
- Tafsiri za data pia ni tatizo jingine. Fasihi simulizi huendelezwa kwa lugha za kijamii. Kupata msamiati unaofaa kufasiri lugha changizi/chanzi hadi lugha pokezi ni tatizo. ***zozote 8 x 1 = alama 8***

MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA NYAKACH
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya
102/1
KISWAHILI
Karatasi ya Kwanza
(INSHA)
Julai /Agosti 2015

1. **SWALI LA LAZIMA**
   Andika barua kwa mhariri ukitoa mapendekezo jinsi ya kukabiliana na ukosefu wa usalama nchini Kenya.
2. "Ukosefu wa ajira ni tatizo sugu humu nchini." Pendekeza njia zinazoweza kutumiwa katika kubuni nafasi za kazi humu nchini.
3. Uzuri wa mkakasi ndani kipande cha mti.
4. Anza kwa:
   Ilikuwa usiku wa maneno niliposikia mlipuko mkubwa, kwanza nilidhania ninaota lakini baada ya dakika chache nikazinduliwa na mayowe . . .

MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA NYAKACH
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya
102/2
KISWAHILI
Karatasi ya Pili
(Ufahamu, ufupisho, Sarufi na matumizi ya lugha na Isimujamii)
Julai / Agosti 2015

1. **UFAHAMU (ALAMA 15)**
   Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuatia.
   Kama kuna jambo ambalo limeiparaganya akili yamahuluki ni kuielewa dhana ya demokrasia. Kiumbe huyu heshi kuuliza mkururo wa maswali. Demokrasia ni nini hasa? Tunaweza kula demokrasia? Ni dude gani hili lina kichwa au mkia pekee yake? Je demokrasia inazuia njaa? Demokrasia ni himaya ya wasomi tu au vilevile ni haki ya mafalahi? Kwa muda mrefu kumekuwa na kinyang'anyiro kikubwa katika jamii ambacho azma na matokeo yake yamekuwa ya kutatanisha. Baadhi ya watu wamejitokeza kama mchuzi wa ugali na kuzusha zahama ambazo si za kuyumkinika. Vichwa vya adinasi vikafyekwa kwa miundo na maparange na matumbo yakapasuliwa na kuapakaza utumbo na vijusi kila mahali. Shingo zikapigiwa vigingi na kukomewa ardhini. Demokrasia si mchezo wa lelemama. Ni sharti tujifunge vibwebwe tumwage damu na tufe ili tupate demokrasia ya kweli!" Mmoja wa mibabe wa demokrasia alinguruma kadamnasi ya umati huku ngoma za vita zikirindima." Hata Marekani na ulaya walimwaga damu. Mamilioni ya watu walipukutishwa na kimbunga cha demokrasia. Chini walilaliana kama Vimatu na tunutu. Hawa manafiki wanafikiri hatuwajui. Katu hatutakubali porojo zao. Wanatupikia majungu kisha wakatoweka. Kuna demokrasia ya Afrika na ile ya Ulaya' mkereketwa wa Uafrika akachanganua.

   Demokrasia ya Afrika basi imefuata mkondo huu wa umwagikaji damu. Kila kukijiri uchaguzi zahama hutawala. Walio madarakani hawataki kubanduka. Hutafuta visababu vya kukwepa wimbi la ushinde. Demokrasia ni mchezo wa mizengwe tu ati. Hali hil imesababisha maafa makubwa, uharibifu mkubwa wa mali, majeraha, ukimbizi wa raia ndani na nje ya mataifa husika, dhuluma za kimapenzi dhidi ya wanawake, kuzagaa kwa magonjwa ainati, uhasama wa kikabila. Jambo la kusikitisha ni kwamba raia na viongozi hawaelekei kujifundisha chochote kutokana na hali. Huku mataifa mengi Ulayani na Asia yakikwea daraja moja baada ya nyingine kimaendeleo, Afrika imedumaa tu. Imesalia kuimba ule wimbo wake wa kutokea azali' Tutaendelea vipi na tunadhulimiwa na kaka wakubwa". Siasa ya demokrasia katika bara la Afrika ina tija kubwa hususan kwa wale wachache wanaofanikiwa kudhibiti nyenzo za kutia tonge kinywani. Ulitima wa umma husalia miradi hewa ya tabaka la viongozi ambayo hutumiwa kujinadi zamu nyingine ifikapo tena. Demokrasia ya kweli imo mikononi mwa umma pale utakapojikomboa kimawazo na kwa ujasiri kudai huduma bora, uajibikaji na kuheshimiwa kwa mkataba wa kijamii ulioasisiwa na Jean Jacques Rousseau.
   Maswali
a) Binadamu amechanganyikiwa kwa njia ipi
   (alama 2)

b) Ni vipi Demokrasia ya kweli inaweza kufikiwa. (alama 2)
c) Kwa nini imesemekana kuwa 'Demokrasia ni mchezo wa mizengwe?
(alama 2)
d) Ni athari gani hutokana na kinyang'a nyiro cha Demokrasia?
(alama 4)
e) "Dhiki za raia zimesalia kuwa mradi-hewa wa wanasiasa" Eleza.
(alama 2)
f) Fafanua maana ya maneno na mafungu yafuatayo jinsi yalivyotumika katika taarifa.
(alama 3)
i) Mafahali
ii) wanatupikia mjungu
iii) Ukarabati

2. UFUPISHO (ALAMA 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Binadamu hupenda kujivika vilemba vingi mno.Tunapenda kuheshimiwa na kutukuzwa na kila mtu. Tunapenda kuombwa ushauri na wote ambao wanahitaji ushauri! Tunapenda kutambuliwa popote tuendapo.

Watu wengi hukataa kufanya jambo la halali kwa kuhofia kuitwa wajinga. Mfano mzuri ni pale ambapo mtu amekosea kidogo katika kutenda jambo; utaona kuwa mtu huyo anaona ugumu wa kuomba radhi au samahani ati kwa sababu ataonekana mjinga.

Je, ni mara ngapi mkurugenzi ameita mkutano na katika barua yake akatisha kuwaadhibu watakaochelewa na mwishowe ni yeye mwenyewe anayechelewa? Tena huwa haombi msamaha. Ataulaumu usingizi uliomchukua, au gari lililomleta.

Aghalabu tunapowakuza watoto wetu, tunawafunza maadili mema. Tunawahimiza wale wadogo kwamba ni vizuri kuomba radhi kwa wakubwa wako unapowakosea. Lakini kumbuka kwamba kukosea ni kwa binadamu wote. Mtu anaweza kukukosea kwa makusudi au kwa bahati mbaya. Kwa hivyo tunapaswa kufahamu kwamba, tunapofanya makosa ni lazima tuombe msamaha, iwe ni kwa wakubwa au kwa wadogo, ili kuondoa kero.

Waja wengi huogopa kusimama mbele za watu na kuwasilisha au kutenda jambo fulani. Kisa na maana, mtu hataki kutenda jambo fulani halafu akosee. Hajiamini na anaogopa kuwa huenda watu wakaona kasoro yake. Lakini kumbuka, kukosa njia ndiko kuijua.

Huenda ikawa watu wanajadili maswala ibuka kama vile ufisadi, kuavya mimba, matumizi ya dawa za kulevya, ukimwi, uzuiaji wa kizazi na kadhalika ... labda huyaungi mkono maoni ya watu wengine kwa sababu ya imani na maadili yako. Hata hivyo, hutaki kusimama ukatoa msimamo wako mbele za watu ingawa dhamiri yako imekwazika. Baadaye utasikika ukiwalaumu watu wengine ilhali ulikataa kusimama na kutetea msimamo wako.

Wengi wetu hujichukua kuwa watu muhimu sana. Wanaona kuwa sherehe au mkutano wowote hauwezi kufaulu ikiwa wao hawako. Wanapokuwa kwenye hiyo mikutano wao hutaka watambuliwe. Hupenda majina yao yatajwe. Haya huwaridhisha, lakini swali ni je, kuwepo kwao ni muhimu kiasi hicho? Kumbuka kwamba mkutano ungeendelea vizuri bila kuwepo kwao. Kwa hivyo, tusiwe watu wa kutaka kutambuliwa kila tunapoenda mahali. Pia, tusilalamike ikiwa hatukuhusishwa katika jambo fulani.

Unaposhuhudia jambo fulani, kama wizi au ajali, usiwe na woga wa kutoa usaidizi kwa kutoa ushuhuda. Wengine hata huogopa kutoa usaidizi huo, hata kwa manusura wa ajali za barabarani, eti kwa sababu wanahofia kuitwa mahakamani kutoa ushuhuda. Kuna shida gani kuenda kusema yale uliyoyashuhudia bila kuongeza au kutoa chochote?

Maswali

a) Bila kupoteza maana, fupisha aya ya kwanza hadi ya nne (maneno 60) (alama 7)
b) Fupisha aya nne za mwisho. (maneno 50)
(alama 8)

3. MATUMIZI YA LUGHA.

a) Taja sifa mbili bainifu za irabu /u/
(alama 2)
b) Tunga sentensi kwa kutumia kiwakilishi huru cha nafsi ya tatu umoja. (alama 2)
c) Andika umoja wa sentensi zifuatazo. (alama 2)
i) Wakitaka tuwasamehe waje watuombe radhi kwa waliyotufanyia.
ii) Yaliyosemekana ni kuwa yao yameharibiwa na binamuo
d) Yakinisha (alama 2)
Hasikii la mwadhini wala la mteka maji msikitini.
e) Bainisha shamirisho kipozi na kitondo katika sentensi ifautayo.
(alama 2)
Mama alimpikia mwanawe chakula alichokitamani sana.
f) Tunga sentnesi moja yenye chagizo ya mahali na ya wakati.
(alama 2)
g) Onyesha mfumo wa sauti katika tungo: Mtumbwini.
(alama 2)
h) Tambua vipashio vya sarufi ya Kiswahili. (alama 1)
i) Huku ukitoa mfano, eleza mantiki inayopatikana katika kauli ya kutendua.
(alama 2)
j) Taja matumizi manne ya kiambishi "ki". (alama 2)
k) Eleza maana mbili ya sentensi ifuatayo. (alama 2)
Jambazi lilimwibia Okoth gari jipya.
l) Bainisha vishazi huru na vishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo.
(alama 2)
Nitaenda maktabani ingawa ninaumwa na kichwa.
m) Andika katika kauli ya kutendesha
(alama 1)
Ile pombe aliyokunywa Chacha ilimfanya alewe.
n) Changanua kwa kutumia mtindo wa kielelezo matawi. (alama 4)
Mtoto ambaye amefika ni ndugu yangu.
o) Andika kinyume cha sentensi ifautayo.
Huzuni alisifu nduguye aliyekusanya takataka zote.
(alama 2)
p) Tumia neno 'vibaya' kama:
i) kivumishi
ii) Kielezi
q) Tunga sentensi yenye kihuhishi cha 'a' - unganifu katika ngeli ya U - ZI. (alama 1)
r) Mbwa wetu amekatwa mkia. Geuza katika hali ya ukubwa.
(alama 2)
s) Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya maneno haya.
(alama 1)
Mkembe, mkebe
t) Weka shadda kwenye neno hili (alama 1)
Kiswahili
u) Toa maneno mengine yenye maana sawa na haya:
i) Izara
ii) Anisi
v) Tumia ngali kutunga sentensi ili kuleta maana ya:
(alama 2)
i) Tendo katika hali ya kuendelea
ii) Tendo kutoweza kufanyika kwa sababu ya wakati kupita

4. ISIMUJAMII (ALAMA 10)

<u>Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali</u>

Aziz: Ingia 46! Adams mbao Kenyatta, railways beba! 46 Adams mbao Kenyatta, railways!
Shiku: Namba nane ngapi?
Aziz: Mbao ingia, blue.
Shiku: Nina hashuu
Aziz: Blue Auntie

Shiku: Sina
Aziz: Ingia. 46 Adams mbao, Kenyatta railways gari bebabeba.
Ahendera: Mimi sinako shirini. Chukuako tu kumi.
Aziz: Dinga inakunywanga petrol mzee.
Ahendera: Kumi mingi.
Aziz: Haaya ingia twende. Driver imeshona twende.

Maswali

i) Eleza muktadha wa mazungumzo haya.
(alama 4)
ii) Taja sifa **sita** za lugha ilivyotumika katika mazungumzo haya.
(alama 6)

MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA WILAYA YA NYAKACH
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya
102/3
KISWAHILI
FASIHI YA KISWAHILI
Julai / Agosti 2015

1. **LAZIMA : SEHEMU YA A : SHAIRI**

Soma shairi lifuatalo kisha uyajibu maswali yanayofuata.

Kweli nilikutamani, nikaomba uje kwangu
Nikamwomba Manani, asikie dua zangu
Kasi uje ardhini, wasifariki wanangu
Imekuwaje mvuwa?

Kweli nilikulilia, uzuru shamba langu
Nipate kupalilia, nipate chakula changu
Na maji ya kupikia, na kunywa aila yangu
Imekuwaje mvuwa?

Nilihamu kuja kwako, kwa sababu ya machungu
Machungu yalokuwako, changazi cha ulimwengu
Athari za mkauko, zote azijua Mungu
Imekuwaje mvuwa?

Mbona kaja kwa ghadhabu, na hasira nzima chungu
Badala kuwa sahibu, wa kunijenga mwenzangu
Umeleta uharabu, na kutawanya mafungu
Imekuwaje mvuwa?

Umekuja kwa ukali, na kuvunja nyumba zangu
Umeteka zote mali, mifugo na vyombo vyangu
Umefagilia mbali, kuacha patupu pangu
Imekuwaje mvuwa?

Nilikudhani asali, kumbe wewe ni mchungu
Mbona hata hukujali, ukasomba mama yangu
Hukumwacha hata Ali, kipenzi mjomba wangu
Imekuwaje mvuwa?

Ardhi umeiziba, umesombajembe langu
Wewe umeshibashiba, najifia njaa kwangu
Maradhi yananikaba, mbu ni jirani zangu
Imekuwaje mvuwa?

Umebeba madaraja, kwa hiyo yako mizungu
Kututenganisha waja, kufilisi soko langu
Kwa nini basi ukaja, kuharibu ulimwengu
Imekuwaje mvuwa?

Kheri uje matembezi, kisha urudie mbingu
Wewe nacho kiangazi, muache kutula bangu
K wa kiasi uwe wazi, usikie neno langu
Imekuwaje mvuwa?

Kama usipopungua, nitakusema kwa Mungu
Yeye vyema akujua, tangu ukiwa kwa mbingu
Hakukuleta kuua, bali kulisha wanangu
Imekuwaje mvuwa?

MASWALI

a) Lipe shairi hili anwani mwafaka. (alama 1)
b) Nafsi neni inaelekea kulalamika. Fafanua mambo matano yanayolalamikiwa. (alama 5)
c) Baini toni ya shairi hili. (alama 1)
d) Eleza kinaya katika shairi hili. (alama 2)
e) Andika ubeti wa pili kwa lugha tutumbi. (alama 4)
f) Fafanua mbinu mbili alizotumia mtunzi kutosheleza arudhi.
(alama 2)
g) Kwa nini mtunzi ametumia kiulizi?
(alama 1)
h) Dhana ya "Msuko " imejitokeza katika shairi hili. Thibitisha. (alama 2)
i) Eleza maana ya misamiati ifuatayo ilivyotumika katika shairi. (alama 2)
i) Dua
ii) Sahibu.

SEHEMU YA B : TAMTHILIA

Mstahiki Meya *: Timothy M. Arege*

Jibu swali la 2 au la 3

2. Ndivyo unavyokwenda ulimwengu, lazima ujitahidi kwenda nao maana ukikuacha nyuma kwa hatua huna lako. Bahati haifungui mlango zaidi ya mara moja.

a) Eleza muktadha wa donduo hili (alama 4)
b) Taja tamathali moja ya lugha inayojitokeza kwenye dondoo
(alama 2)
c) Eleza sifa mbili za msemaji na msemewa
(alama 4)
d) Fafanua jinsi mbinu hizi zilivyotumika kwenye tamthilia
i) Taswira (alama 5)
ii) Balagha (alama 5)

3. Sheria na mamlaka ya Meya wa Cheneo zilikuwa zimezidi, hii ndiyo sababu wanachi wanalalamika. Fafanua. (alama 20)

SEHEMU YA C : RIWAYA

Kidagaa Kimemwozea : *Ken Walibora*

Jibu swali la 4 au la 5

4. "Siku nyngi baadaye aling'amua kwamba huo ulikuwa mwanza wa uasi ... uasi uliotishia na hatimaye kuchangia kuuporomosha milki yake"

a) Eleza muktadha wa usemi huu (alama 4)
b) Mwanzilishi wa uasi huu alichangiaje maguezi ya Sokomoko? (alama 4)
c) Fafanua mbinu zozote sita zilizofaulisha ukombozi wa Sokomoko kutoka mikononi Mwa mkoloni mweusi
(alama 4)

5. ***Kidagaa Kimemwozea***

a) Eleza hila zilizotumiwa na viongozi katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* kuendeleza uongozi wao

(alama 10)

b) Jadili usawizi wa dhana ya tamaa na mwandishi Ken Walibora katika kidagaa kimemwozea
(alama 10)

SEHEMU YA D: HADITHI FUPI

Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine : *Ken Walibora na Said A. Mohamed*

Jibu swali la 6 au la 7

6. Hapana shaka nyoyo zao zikimemeta na nyuso zao zikimemetuka, husemi kwamba wao.

a) Eleza mukfadha wa dondoo hili (alama 4)
b) Eleza sifa nne za warejelewa (alama 8)
c) Eleza namna mbinu ya kinaya inajotokeza katika hadithi hii
(alama 8)

7. Tamaa na ubinafsi ndio chanzo cha migogoro na maovu katikajamii. Kwa kurejelea hadhithi zozote tano katika Damu Nyeusi fafanua kaulu hii.
(alama 20)

SEHEMU YA E:FASIHI SIMULIZI

8. a) Eleza istilahi zifuatazo za fasihi simulizi
   i) Vivugo
   ii) Rara
   iii) Pembezi
   iv) Hodiya (alama 4)
   b) i) Fafanua sifa nne za methali
   iv) Methali zinaweza kuainishwa kwa misingi ya tamathali za usemi. Taja huku ukitolea mifano ya methali
   hizo (alama 12)

MATIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA KANTI NDOGO YA NYAKACH
HATI YA KUHITIMU ELIMU YA SECONDARI KENYA
KISWAHILI
Karatasi 1
Julai/Agosti 2015
MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA

SWALA LA KWANZA

1. Ukosefu wa usalama

a) Malipo mazuri kwa askari kuwapa motisha.
b) Kuwapa polisi makaazi mazuri.
c) Kutengeza kamati za usalama hadi mashinani.
d) Kuimarisha miundo misingi mf. barabarani.
e) Kuwapa polisi zane za kutosha ili kukabiliana na magaidi.
f) Miji kumi- kuwajua majirani na yale wanayoyafanya.
g) Sheria kali zinawekwe kwa wavunja usalama.
h) Kuwahimiza wananchi kuwaripoti wahalifu.

i) Kuwapa makundi ya kigaidi muda kusalimisha silaha zao haramu.
j) Kuimarisha usalama mipakani
Sura
Barua rasmi

2) SWALI LA PILI

"Ukosefu wa ajira ni tatizo sugu humu nchini."
Mtahiniwaa afafanue mawazo yake au hoja zake kuhusu njia zinazoweza kutumiwa katika kubuni nafasi za kazi hapa nchini.

Baadhi ya hoja

- Upanuzi wa viwanda.
- Kuimarisha uchumi wa nchi ili pesa zipatikane za kuajiri watu.
- Kuhimiza watu kujiajiri (serikali).
- Kupunguza mishahara mikubwa mikubwa ili pesa hizo zitumike kuajiri watu wengine.
- Uimarishaji wa sekta ya elimu ili watu wapewe ujuzi mbalimbali.
- Masomo shuleni yalenga kufunza ubunifu wa kikazi. Masomo ya ufundi n.k
- Serikali iweke sheria kwa makampuni ya kigeni yanayotaka kufanya biashara nchini kuwa ni lazima yaajiri idadi fulani ya wenyeji ndipo yaruhusiwe kufanya biashara.
- Wafanyikazi wa kigeni watozwe ushuru zaidi kwa mishahara yao ili kuwazuia kuja kuchukua nafasi za kikazi ambazo zingekuwa za wenyeji.
- Seka ya michezo iimarishwe.

3) SWALI LA TATU

Mtahiniwa atunge kisa kinachoafiki methali kwamba uzuri wa nje hauwezi kukifanya kitu kiwe chema, wa ndani una umuhimu zaidi.

4) SWALI LA NNE

- Mtihaniwa aanze insha yake kwa maneno aliyopewa.
- Kisa cha mtahiniwa lazima kioane na yaliyomo katika mdokezo.

Mtahiniwa anaweza shughulika hali zifuatazo

1) Mlipuko wa bomu- aelezea alivyohangaika kutoka katika Jengo na matokeo yake mfano vifo majeruhi n.k.
2) Mlipuko uliosababishwa na kasoro katika nyanja za umeme na matokeo.
3) Shuleni- Wanafunzi kutumia petroli

MATIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA KANTI NDOGO YA NYAKACH
HATI YA KUHITIMU ELIMU YA SECONDARI KENYA
KISWAHILI
Karatasi 2
Julai/Agosti 2015
MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA

1. UFAHAMU
(ALAMA 15)

Ameshindwa kuielewa dhana ya demokrasia. Dhana hii ina fasiri nyingi kutegemea lengo la mtu/kundi la watu/mahali wanapoishi. 2xl=Alama 2

b) i) Pale umma utakapojikomboa kimawazo.
ii) Kwa ujasiri kudai huduma bora.
iii) Uajibikaji pamoja na kuheshimiwa kwa mkataba wa kijamii.
c) i) Kinyang'anyiro cha madaraka.

ii) Wasio na madaraka watumia kila mbinu kuyapata.
iii) Walio madarakani hawataki kubanduka-hutafuta visababu vya kusalia madarakani . 2xl=Alama 2

d) i) Maafa
ii) Uharibifu wa mali
iii) Majeraha
iv) Ukimbizi wa raia nje na ndani ya mataifa husika
v) Dhuluma za kimapenzi dhidi ya wanawake
vi) Uhasama wa kikabila
vii) Kuzagaa kwa aina mbalimbali ya magonjwa Zozote 4xl=Alama 4

e) i) Hutumiwa na tabaka la viongozi kujinadi/hasa wakati wa uchaguzi.
ii) Wanasiasa hujifanya kuwa wanayajali masilahi ya wanajamii kumbe huruma zao ni kilio cha mamba.
f) Mafalahi-wachochole, maskini, raia, penye ukavu
i) Wanatupikia majungu-wanatufitini au wanatukosanisha.
iii) Ukarabati-Urekebishaji, utengenezaji, kubambanya.

MUKHTASARI

Swali (a)

- Binadamu hupenda kujivika vilemba vingi kama vile kutukuzwa na kuheshimiwa, kuombwa ushauri na kutambuliwa.
- Wengi hukataa kufanya jambo la halali kwa kuhofia kuiwa wajinga/ wanapokosa huona ugumu wa kuomba radhi/ samahani kwa sababu ataonekana mjinga.
- Mara nyingi mkurugenzi huita mkutano na kutisha kuadhibu watakaochelewa na mwisho yeye mwenyewe akachelewa.
- Huwa haombi msamaha (bali) hulaumu usingizi au gari.
- Aghalabu tunapowakuza watoto, tunawafunza maadili mema/ tunawafunza umuhimu wa kuomba radhi wanapokosea wakubwa.
- Kukosea ni kwa binadamu wale (na) huweza kuwa kwa makusudi au bahati mbaya.
- Tunapofanya makosa ni lazima tuombe msamaha ili kuondoa kero. (lx7)

Swali (b)

- Waja wengi huogopa kusimama mbele za watu na kuwasilisha/ kutendajambo fulani.
- Huwa hataki kukosea/hajiaminil huenda watu wakaona kasoro yake.
- Hawajui kuwa kukosa njia ndiko kuijua.
- Wanaweza kujadili maswala ibuka na pengine huyaunga mkono maoni ya wengine kwa sababu ya imani/maadili

(nawe) hutaki kutoa msimamo ingawa dhamiri yako imekwazika na baadaye hulaumu wengine ilhali ulikataa kusimama na kutetea msimamo wako.

- Wengi hujichukuwa watu muhimu sana na huona mkutano/sherehe hauwezi kufaulu ikiwa hawako/hutaka watambuliwe/majina yao yatajwe.
- Tusiwe watu wanaotaka kutajwa au wanaolalamika ikiwa hatukuhusishwa kwenye jambo.
- Unaposhuhudia jambo, usiogope kutoa usaidizi au ushahidi (1x zozote 7)

3. MATUMIZI YA LUGHA: (Alama 40)

a) Taja sifa mbili bainifu za irabu/u/. (alama 2)
- irabu ya nyuma
- Irabu mviringe/hutamkwa na mdomo mviriongo. 2x1=2

b) Tunga sentensi kwa kutumia kiwakilishi huru cha nafsi ya tatu umoja (alama 2)
Yeye atasoma kidagaa kimemwozea. (1x2=2

c) Andia umoja wa sentensi zifuatazo (alama 2)

i) Wakitaka tuwasamehe waje watuombe radhi kwa waliyotufanyia.
Akitaka nimsamehe aje aniombe radhi kwa aliyonifania. 1x1=1

ii) Yaliyosemekana ni kuwa yao yameharibiwa na binamuo.
Lililosemekana ni kuwa lake limeharibiwa na binamuye. 1x1=1

d) Yakinisha. (alama2)
Hasikii la mwadhini wala la mteka maji msikitini.
Anaskia la mwadhini na lamteka maji msikitini. 1x2=2

e) Bainisha shamirisho kipozi na kitondo katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Mama alimpikia mwanawe chakula alichokitamanisana.
-Kitendo kipozi

f) Tunga sentensi moja yenye chagizo ya mahali na ya wakati. (alama 2)
-Walinda uwanjani jana joni 1x2=2
mahali wakati

g) Onyesha mfumo wa sauti katika tungo:
matumbwini. (alama 2)
K+KI+KKKI+KI (4x½=2).

h) Tambua vipashio vya sarufi ya Kiswahili (alama 1)
- Sauti
- Silabi
- Neno
- Sentensi ¼ x 4=1

i) Huku ukitoa mfano, eleza mantiki inayhopatikana katika kauli ya kutendua. (alama 2)
- Vitenzi katika kauli hii huwa na maana ya kinyume k.m funga - fungua fukia-fukua kosa-kosoa

j) Taja matumizi manne ya kiambishi “ki” (alama 2)
– Hutumiwa kuonyesha udogo wa nomino k.m kibuzi.
– Hutumiwa kama kiamishi cha upatanisho wa kisarufi ngeli ya ki-vi.
– Hutumiwa kufananisha na vielezi vya namna mfano.
– Hutumika mwanzoni mwa majina ya lugha k.v Kiswahili. ½x4=2

k) Eleza maana mbili ya sentensi ifuatayo (alama 2)
– Jambazi lilimwaibia Okoth gari jipya.
– Jambazi liliiba gari likampa Okoth.
– Jambazi liliiba gari la Okoth. 2x1=2

i) Bainisha vishazi huru na vishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo (alama 2)
Nitaenda maktabani ingawa ninaumwa na kichwa
Kishuzi huru Kishazi tegemezi 2x1=2

m) Andika katika kauli ya kutendesha (alama 1)
– Ile pombe aliyokunywa Chacha ilimfanya alewe.
– Ile pombe aliyokunywa Chacha ilimlevya. 1x1=1

n) Changana kwa kutumia mtindo wa kielelezo matawi. (alama 4)

Mtoto ambaye amefika ni ndugu yangu.

S

KN KT

N S t KN_2

N V

mtoto ambaye amefika ni ndugu yangu

o) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo. (Alama 2)
Huzuni alisifu nduguye aliyekusanya takataka zote.
Huzuni alikashifu nduguye aliyetawanya takataka zote. 1x2=2

p) Tumia neno “vibaya” kama:
Vyombo vibaya vimetupwa (1x1=1

i) Kivumishi
Vyombo vibaya vimetupwa

ii) Kielezi
Aliimba wimbo huo vibaya. 1x1=1

q) Tunga sentensi yenye kihusishi cha ‘a’-
unganifu katika ngeli ya U-ZI. (alama 1)
Ukuta wa nyumba umebomoka. (1x1=1)

r) Mbwa wetu amekatwa mkia. Geuza katika hali ya ukubwa. (alama 21)

Jibua letu limekatwa jikia/kia
Jijibwa letu limekatwa jikia. (1x2=2)

s) Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya maneno haya. (alama 1)
Mkembe, mkebe
Senensi ina maana ya:
mlabe- chombo cha bati kinachotumiwa kuweka vitu vidogo vidogo
mkenbe - mtoto mdogo mwenye umri baina ya mwaka mmoja na miaka sita au kijana balighe ambaye hajoa.

t) Weka shadda kwenye neno hili. (alama 1)
Kiswahili.

u) Toa maneno mengine yenye maana sawa na haya:

i) Izara -Fedheha /Aibu/Dosari 1x½=½

ii) Anisi -Furahisha/pumbaza/fariji 1x½=½

iii) Tumia ngali kutunga sentensi ili kuleta maana ya: (alama 2)
Wanafunzi wangali wanacheza uwanjani (1x1=1

ii) Tendo kutoweza kufanyika kwa sababu ya wakati kupita.
Mwalimu angalikuwa na pesa angalienda ulaya. (1x1=1

4) ISIMU JAMII: (Alama 10)
Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.
AZIZ: Ingia 46! Adams mbao Kenyatta, railways!
SHIKU: Namba nane ngapi?
AZIZ : Mbao ingia, blue.
SHIKU: Nina hashuu.
AZIZ: Blue Auntie.
SHIKU: Sina
AZIZ: Ingia. 46 Adams mbao, Kenyatta railways gari bebabeba.
AHENDERA: Mimi sinako shirini. chukuako tu kumi.
AZIZ: Dinga inakunywanga petrol mzee
AHENDERA: Kumi mingi
AZIZ: Haaya ingia twende. Driver imeshon twende.

Maswali

i) Eleza muktadha wa mazungumzo haya.

– Hii ni sajili ya magari ya uchukuzi
- Inatokea katika kituo cha matatu au barabara gari linaposimama kubeba abiria.
– -Kuna ufingo anayetangaaza kiasi cha nauli kwa wasafiri wanaotaka kulipa malipo nafuu. 1x4=4
– Taja sifa sita za lugha iliyotumika katika mazungumzo haya.
– Kuna matumizi ya lugha maalum k.v 46, ingia twende.
– Kuna kitaja vituo mbalimbali ambako gari litapitia.
– Ni lugha ya kuchanganya ndimi k.v driver
– Inatumia misimu k.v hashru, dinga n.k
– Haizingatii sarufi k.m inakunywanga, sinako n.k
– Hutumia sentensi fupifupi
– Ina uchesh mwingi.

MATIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA KANTI NDOGO YA NYAKACH
HATI YA KUHITIMU ELIMU YA SECONDARI KENYA
KISWAHILI
Karatasi 3
Julai/Agosti 2015
MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA

FASIHI

1. Ushairi

a) Mvua 1x1=1

b)
- Mvua ya ghadhabu fujo badala ya Baraka.
- Madaraja kubebwa.
- mvua kuvunja nyumba yake.
- Mvua kutawanya mifugo yake.
- Mvua kufagilia shamba lake.
- Mvua kusomba mama yake na Ali.
- Kuamvukizwa maradhi/Mbu. Zozote 5x1=5

c) (i) Masikitiko/kutamauka.
(ii) Huzuni 2x1=2

d) Mvua iliyotarajiwa iligeuka balaa 1x2=2

e) (i) Mtunzi anasikitikia mvua iliyonyeshea shamba lake.
ii) Alitaka kupalilia angalau apate chakula.
iii) Aidha, alitaka maji ya kupikia na kunywa pamoja na jamaa wake.
iv) Anasikitikia uharibifu wa mvua.

Tuzo

Iwe kwa aya moja kwenye usemi wa taarifa. Sentensi nne zibainike wazi. 4x1=4

f) Kubananga/kufinyanga/kubirua/ukiushi wa kisarufi/ukiushhi wa kisintaksia; kutosheleza vina. Mfano.
Hasira nzima chugu badala ya chungu nzima
Inkisari kupata mizani. Kwa mfano; uharabu badala ya uharibifu.
Tabdila kuzua upekee wa lugha. Kwa mfano; mvuwa badala ya mvua. Zozote 3x1=3

g) Ina mizani miichache kwenye msororo wa mwisho ukilinganishwa na mishororo mwingine. 8:16 1x1=1

h) (i) Ombi kwa mola.
(ii) Rafiki 2x1=2

SEHEMU B: TAMTHILIA

Mstahiki Meya

2)

a) Msemaji - Bili
msemewa - Meya
mahali -Afisini kwa Meya
Tukio -Bili anamshawishi Meya kwa kutoa mpango mzuri wa namna ya kuifilisi baraza kwa kupitia au kushirikiana na mwanakandarasi
4x1=4

b) Tashbishi 1x2=2

c) Msemaji- Bili
- msaliti
- mfisadi
- Mwenye tama
- Mbinafsi
- mjanja
- mnafiki- Anajifanya rafiki wa Meya lakini analenga kufaidika/maslahi yake.
- mpenda makuu. Alitamani mkewe ajifungulie ngambo.

Msemewa - Meya

- Mlafi-Anabugia chakula kingi - chai na mayai

- Mwoga- Anaogopa kwenda jela
- Katili- haoni shida mtoto mmoja akifa
- Mbinafsi
- Mwenye kuburi- anamwambia Siki kuwa anaweza kuchaguliwa mara kadha.
- Mwenye mapuuza - anawapuuza wafanya kazi.
- Mwenye tama - ya mali
- Laghai/mwongo - Dawa zipo njiani
- Mnafiki
- Mbadhirifu- Anampeleka Bili hoteli za kifahari
- Dikteta- anatumiwa mabavu kutawala
- Mwenye kitisho - mjinga – mbaguzi (Zozote 4x½=2)

d) Taswira

- Waridi anaeleza kuwa hamna maji zahanatini, nzi wamejaa na hii inachora hali halisi ya jisni zahanati ni chafu.
- Uvundo na maji taka inachora picha ya mji ulivyo mchafu.
- Wafanyakazi wanavyokibizwa na polisi kutembeza virungu na risasi inachora picha ya utawala wa kidikteta na mbaya.
- Siki anapomwambia Meya kuwa anaingiza kidole kwenye mzinga wa nyuki unaonyesha hatari.
- Siki alimwambia Meya kutowashirikisha wananchi ni sawa na kukanyaga nyoka -hatari.
- Mwandishi anapotuelezea meza ya makuli ya Meya kwamba imejaa mayai na vya kula anatuchorea taswira ya ulafi. Zozote 5x1=5

Balagha

- Kweli killio chetu kilisikika palepale.Nani atatuchezea? Hii inasisitiza maombi waliokuwa wakiomba - mhubiri na Meya.
- Hilo tumefanya lakini wapi?- kukata tama
- Nende wapi bwana? Mji wenyewe ndio hivyo unavyoona (mji hakuendeki kwa sababu ya uvundo na mgomo).
- Naam kasi yote ya nini Waridi? Au dawa zimeingia?
- Siasa gani hiyo?
- Chaguo la wananchi - kwa nini basi kulalamika?
- Au unafikiri pakawa na fursa nyingine hii leo ya kuchagua viongozi matokeo yatakuwa tofauti sana? (Zozote 5x1=5)

3) Sheria na mamlaka ya Meya kuzidi

- Sheria ya kugawana gharama katika matibabu. Asemavyo Waridi, sheria hii ilitolewa na wakubwa (Uk.3). Kwa mujibu wa sheria hii ni sharti wanaotafuta huduma za afya wazilipie. Huu ulikuwa mzigo kwa wanacheneo.
- Sheria ya misitu imeshika kasi kwa mujibu wa mama Dadavuo Kaole. Sheria hii imefanya bei ya makaa kupanda kiasi kwamba wananchi hawawezi kununua makaa (uk. 5).
- Kuna sheria na mipango ya maendeleo ya miaka mia moja ‘Millenia’ isiyo na manufaa kwa mwanacheneo. Kwingineko, pana sheria na mipango muhimu ya maendeleo ya miaka kumi inayopuuzwa na Meya. Meya hamakinikii mambo muhimu kwa baraza lake.
- Pana sheria inayoongoza kandarasi. Meya anasema kuwa angefungwa miaka saba iwapo angepatikana na hatia ya kuvunja kandarasi (uk.29). Sheria hii ni mzigo kwa baraza kwani linalazimu masharti ya kandaras
- yaheshimiwe hata pale kazi haijatekelezwa kikamilifu. Huu ni ufsadi.
- Meya anatumia sheria kandamizi za baraza kuamuru madiwani kuongezewa mshahaa kila kuchao. Aliamuru nyongeza bila kushaurinana na diwani anayesimamia uchumi na kazi. Huku kuwaongeza wananchi walipa kodi mzigo.
- Aidha, Meya likuwa na mamlaka ya kuajiri watu kazi na kuwafuta. Alifunuafunua faili afisini huku akisema angewafuta kazi baadhi ya wafanyakazi. Alimajiri mhazili ambaye mwenyewe anasema hakufunza kufanya ile kazi. Wanaostahili kazi hukosa kazi kwa njia hii.
- Licha ya kuwa na Baraza la madiwani, inaonekana Meya hakumsikiliza mtu yeyote.
- Uamuzi wake ndio sera na sheria ya Cheneo. Madiwani wanashadidia wazo hili wanaposema Mstahiki Meya alikua na uwezo mkubwa.

- Meya alikuwa na uwezo wa kuwateua wahudumu katika kamati mbalimbali za baraza. Yeye ndiya mwenye uwezo wa kuziunda kamati hizi na kuzibunja apendavyo. kamati zisizo na maana zilifuja fedha za umma.
- Sheria ya kuwajibika kwa kundi la viongozi wenye sauti moja zilimpa Meya uwezo wa kuwalazimisha madiwani wote jukumu ya wajibu wa kumuunga mkono. Maamuzi yote mabaya na mazuri katika baraza yaliungwa na madiwani chini ya uongozi wa Meya. Zosi Huku ni kuwalazimishia watu maamuzi hasi.
- Meya anatumia 'Riot Act' (uk. 49) inayompa mamlaka ya kuwasomea madiwani pinzani na hata kutumia askari kuvunja maandamano au mikutano inayokisiwa kuwa si halali.
- Wananchi wanakosa jukwaa la kuwasilishia malalamisi yao kutokana na sheria hii.
- Meya angetumia 'Mayors Act ' (uk. 88) kumchukulia hatua kali mtu yeyote aliyekisiwa kuwa kizuizi katika uongozi wake. Sheria hii iliwalazimu viongozi wenye mawazo pevu kama Diwani III kunyamazishwa kwenye vikao, kutengwa kasha kulazimishiwa maamuzi yasiyofa.
- Meya ana mamlaka ya kutumia fedha za Baraza kwa hiari yake. Anaamua kugharamia huduma za usafiri wa mhubiri na kuahidi kumplipa shilingi laki moja. Angempa mtu yeyote fedha za baraza.
- Meya ana uwezo wa kujistarehesha atakavyo na rafiki yake. Angeburudika katika mikahawa za kidahari na familia za rafiki yake. Alimwalika Bili na familia yake
- kustarehekwa gharama yake-mgao wa starehe, 'Entertainment vote." Zozote 10x2=20

4) Muktadha

i) maneno ya Mzee Butali
ii) Anaongea na Bi. Margaret/Mwalimu mkuu wa shule ya Askofu Timotheo
iii) Wamo afisini mwa Mwalimu Mkuu.
iv) Anastaajabikiauja-uzito wa Sela huku akiwa mwanafunzi. Anashangazwa na kufeli kwa malezi ya watoto shuleni.

b) Mambo ya kujivunia katika elimu

i) Wasichana wanaendeleza elimu yao hata baada ya ujauzito.
ii) Walimu wanawapa wazazi na wanafunzi ushauri unaofaa. Kwa mfano, Bi Margaret aliapendekezea wazazi wa Sela na wenake kuwatafutia shule za kutwa ili kuwatunza baada ya kujifungua.
iii) Hali ya maisha ya wasichana inachunguzwa kila wakati. Sista alifanya uchunguzi kila mara.
iv) Elimu inatolewa kisawa baina ya wasichana na wavulana
v) Ni elimu inayokuza vipawa vya wanafunzi tofauti na academia. ulikuwa na tamasha zz nyimbo na drama katika shule ya Askofu Timotheo.
vi) Jamii hii inaunga mkono elimu liwe liwalo. Wazee wa kijiji walimshauri Mzee Butali kumrudisha Sela shuleni.
vii) Wazazi wanahusishwa katika maamuzi muhimu kuhusu elimu ya watoto wao. Kwa mfano, mzee Butali na mkewe walialikwa shuleni ili kujadili hali ya mtoto wao Sela.

c) Mzigo wa mwenzio Kanda la Usufi

Methali hii ina maana kuwa mtu huona mzigo, shida na matatizo ya wengine yakiwa nyepesi kama ukanda wa usufi. methali hii hutumiwa kutukumbusha kuwa aghalabu mtu huidharau shida iliyomfika mwenzake au haioni kama ni kitu. mfano.

- Mzigo wa wazazi wa wale wasichana waliotungwa mimva ulikuwa kanda la usufi kwa mkkuu wa shule, Bi. Margaret. Alipoaita shuleni alirejelea kupata mimba ka wale wasichana kama tukio la kawaia. Uk 62.
- Mzee Butali kuwafukuza Sela na mama yake nyumbani kwa kua Sela ni mjamzito. Tatizo hili la malezi ya Sela hayakua mzigo kwa bali ka mamake.
- Chris kujifanya kua ni mgonja ili we na uhusiano wa kimapenzi na Sela. Kwa Sela, Chris ni kanda la usufi. Hakujua kuwa suala hili lingetokea kuwa mzigo kwake.
- Uhusiano a kimapenzi unaonekana kama
- kanda la usufi lakini athari zake zinakua nzito wakati Sela anaringwa mimba na Chris masazu katika mchezo huu.
- Chris anaiona mimba ya Sela kama kanda la usufi anamlaumu ka kutojikinga.
- Mimba ya Sela ambayo ni mzigo kake ilionekana kua mzigo mwepesi sana kwa masazu.
- Sela alipmwarifu Mazazu kuhusu mimba yake, masazu alimwandikia na kumambia, 'Yajapo yapokee' uk 62.
- Sela alitamani sana kua na mwanawe hivyo, kumkosa mwanawe, ukaa mzigo kwake. Mzigo huu ulikua kanda la usufi kwa Masazu. Masazu alishinikiza kna kulazimishwa na Sela wamwendee mwanao kadogo.

- Mzigo wa mimba za wasichana wale watatu ulikuwa ni kanda la usufi kwa wanafunzi wengine. mwalimu mkuu alipotangaza kuwa wasichana wale watatu wamwone ofisini mwake, vicheko vya chini kwa cini vilianguliwa. Uk 62.
- Wasichana wanapopimwa, Sela anagunduliwa kua na mimba. wazazi wanaitwa shuleni. Babake (Mzee Butali) anaelekea kuwalaumu walimu kwa sababu ya bintiye. Walimu wana majukumu magumu ya kuwasomesha na kuwashauri wasichana hawa lakini kwa Mzee Butali ni kanda la usufi.
- masazu akiwa Dafina anafanya kazi ya kijungu jiko. Sela anapojiunga naye anaogezaa mahitaji yao. Mzigo wa kuikimu familia uliachiwa mazazu ni kanda la usufi kwa Sela.
- Sela anamachia mamake na dadake kazi ya kumlea mtoto. Si kazi rahisi, hasa kutokana na ufukara mkuwa unaowasonga. Sela anamfuata Masazu, Dafina na kumacha mtoto wake Kadogo alelewe na Rozina na mamake. kwa Sela, ulezi wa Kadogo ni kanda la usufi.

(6x1=6)

b) Changamoto za wahudumu wa nyumbani/yaya

- Kuchokozwa kimapenzi na mabwana wenye nyumba kwa mfano Bwana Mwatela kwa Kananda.
- Wanauzwa utumwani kwa mfano Mwatela alimuuza Kananda kongo.
- Kupea ahadi za uongo kwa mfano Mwatela anamhadaa Kanda kwamba angemuoa baada ya kujifungua hata hivyo anamnyang'anya mtoto wake.
- Wanatishiwa, kwa mfano, mwatela anamtisha Kananda kua angemuua iwapo angethubutut
- kumwambia mkewe kuwa ujauzito huo ulikua wake Mwatela.
- Wananyang'anywa wanao, kwa mfano, mwatela anamnyang'anya Kananda mwanaye, mwakitaa baadaa ya kujifungua.
- Wanapiganishwa na wanao. mwatela alitumia uongo kumchochea Mwakitawa hadi akamuumiza mamake kwa jiwe.
- Wanakumbwa na upweke. mwakitawa alikua na upweke na huzuni baada ya kutenganishwa na mwaknaye, mwakitawa.
- wanasingiziwa wizi. mwatela anadai kua Kananda alikuwa mmoja wa majabazi waliokua wakitaka kumteka nyara mwakitawa.
- Wanafanyiwa ukatili. Mwatela aliwazia hoja ya kutafuta majambazi wamuue Kananda.
- Hawana uwezo wa kuwachukulia hatua za kisheria watu wanaokiuka haki zao.

5) Kidagaa Kimemwozea

Hila ya viongozi

- Viongozi wanawatia gerezani wanaowapinga Yusufu anafungwa Jela na Nasaba Bora
- Viongozi wanatumia propaganda kwa Nasabaa Bora anasema amekwezwa uongozini na Mungu.
- Kutumia vigaragozi- Balozi kama anamsaifu Nasaba Bora kwa uongozi bora.
- Vitisho- kusema kuwa anayepinga Nasaba Bora anapinga Mungu.
- Matumizi ya Hongo- Nasaba Bora anahonga majaji ili waufiche uovu wake (Zozote 5x2=10

Tamaa

- Tamaa ya sifa na mali imemfanya Majisisu kumwibia Arnani mswada wake.
- Nasaba Bora amawapokonya raia mashamba yao ili ajitajirishe.
- Wakoloni walijitengea mashamba makubwa kule sokomoko.
- Nasaba bora ameficha faili kwa tamaa ya kupewa hongo.
- Tamaa ya mali inawafanya wakoloni na hata viongozi wa Tomoko huru.
- Balozi anamsifu Nasaba Bora ili aendelee kufaidika kutokana na mfumo huo.
- Tamaa ya anasa na kujitakia makuu vinamfanya Michelle kuvunja uchumba na Majununi.
- Lowela anaachia masomo kiato cha tatu kwa sababu ya tama ya anasa.
- Tamaa za kimwili zinamfanya Nasaba Bora kungilia mapenzi na msichana mdogo. Fao pia anasukumwa na tama hiyo hivyo
- Wakuu katika Jeshi la wanahewa wanaongozwa na tama kupokea hongo ili wamwajiri Madhubutu.
- Viongozi wanaongoza na tama kuchukuwa pesa zilizonuia kujenga hospitali kuu hapo Sokomoko.

(Zozote 10x1=10)

6) Hadithi Fupi

a)

- Haya ni maelezo ya mwandishi
- Anasimullia juu ya Duni na Jamila
- Ni asubuhi baada ya Duni kurudi amelewa na kumpiga mkewe usiku wa kutangulia.
- Duni alikuwa amerauka na kumshughulikia mkewe alivyo desturi yake. Walikuwa wameongozana hadi bafuni.

(Zozote 4x=4)

b) Duni

- Mlevi- Alikuwa mlevi wa kupindu
- Mcheshi- kupitia kwa mojibo zake aliwakebehi watu.
- katili- Alimpiga na kumuumiza mkewe kia mara.
- Mpishi bora -Mkewe alimpenda kwa sababu ya pishi maridhawa.
- Mwenye mapuuza- Alipuuza malalamiko ya watu kuhusu fujo zake za usiku.
- JasiriI- Alirudi kila siku usiku akipiga kelele bila kuogopa uwezekano wa kushambuliwa. (Zozote 4x1=4)

Jamila

- Mvumilivu- Anavumilia mateso katika ndoa.
- Mwenye mapenzi ya dhati- anampenda mumewe kwa moyo wake wote.
- Msivi- Alijua siri ya mapenzi yake kwa duni lakini hakumwambia yeyote.
- Mwenye msimamo dhabiti- anakataa kushawishiwa na watu ili avunjea ndoa yake.
- Mwenye matumaini- Hakatishwi tama na tabia a mumewe. (zozote 4x1=4)

c) Kinaya katika

- Ni kinaya kwamba Jamila msichana mrembo wa miaka ishirini na mitatu anakubali kuishi kwa ndoa yenye masaibu mengi.
- Ni knayaka kwa Duni anaishi mtaa wa tabaka la kadri wanaofanya kazi ila yeye anawapigia kelele kia siku akitoka ulevi.
- Ni kinaya kwamba Jamila anaendelea kumpena Duni ambaye hupiga na kumuumiza kila mara.
- Ni kinaya kwamba duni baada kulia kwa kwikwi na kwomba msamaha, hurudia tabia ile ile ya kumdhuhimu mkewe baada ya kulewa.
- Ni kinyaya kwa Duni kumwita Jamila Dii na dakika inayofuata ananmgeukia na kumpiga teke.

7) **Tamaa na ubinafsi ndio chanzo cha migogoro na maovu katika jamii.**

Samaki wa nchi za joto

- Christine ana tama ya mapenzi na Peter ambaye ni mzungu. Hali hii inamfanya kutungwa mimba na Peter kisha baadaye anaiavya mimba hiyo.
- Tamaa ya mali na ubinafsi inamfanya Peter kuwapunja wachuuzi wa Samaki.
- Tamaa pia inamwingiza Peter katika biashara haramu ya kununua na kuuza dola na inaleta mgogoro kati ya Peter na Tajiri - kuhusu noti bandia.

Mke Wangu

- Tamaa ya msimulizi ya kutaka kazi ya offisi inamfanya kukosa kazi na kudharauliwa na Aziza.
- Tamaa ya Fedhela Salim ya anasa inamfanya kukwataliwa na wanaume wa kumwoa.
- Tamaa ya msimulizi kutaka mke ambaye hajasoma na ambaye atamfundisha, inamfanya kumwoa Aziza ambaye anamdharau na wanazozana kila wakati.

Damu Nyeusi

- Tamaa ya masomo ng'ambo inamfanya Fikirini kuteseka
- Tamaa ya mali inafanya wamerakani weusi kuiba na hivyo basi mwafrika yeyote anachukuliwa mwizi.
- Tamaa ya mali inamfanya Fiona kumwibia fikirini na hata kutaka kumwua.

Maeko

- Ubinafsi wake Duni unamfanya kulewa na kuwapigia watu kelele akiwa mlevi na hata kumpiga Jamila.
- Salim naye anamtaka Jamila amwache Hariduni na atoroke naye amwoe kula chakula kitamu inamfanya avumiliea mateso na mapigo kutoka kwa hari duni.

Kanda la usufi

- Chris Masazu ana tama na inamfanya kumpa Sela mimba kisha Sela anaacha shule na mgogoro unazuka kwao Sela, mamake na Sela wanafukuzwa.

- Tamaa ya Askufu Timotheo ya kuwaandikia wavulana Barua inawaingiza katika mapenzi mapema na kuwafanya wafukuzwe shule baada ya kuwa waja wazito.
- Tamaa ya Chris na Sela ya kutaka kuishi na mtoto wao unawasukumia kaika mauti.

Kutaja hadithi al. 1x5=5)
Hoja tatu 3x5=15)

Fasihi Simulizi

Majibu

a) i) Vivugo- Ni majisifu yanayotungwa papo kwa papo na kughaniwa na mtunzi anayesifu.
ii) Rara - Hadithi fupi ya kishairi ambayo husimulia mabo ya kubuni.
iii) Pembezi- Husifu watu wa aina fulani katika jamii kutokana na mchango wao na matendo yao.
iv) Hodi ya- Ni nyimbo za kazi zinazoimbwa wakati watu wanafanya kazi. (Zozote 4x1=4)

b) i)
- Methali zinasehemu mbili
- Hutumia tamathali za usemi
- Ufupi wa urari wa maneno
- Hukubaliana na jamii husika
- Hulnganisha mambo na hali (Zozote 4x1=4)

ii) Jazanda- Avumaye baharini ni papa
ii) Sifiara- Mgeni ni kuku mweupe
iii) Tashihisi- Chui naye ana mkwe
iv) Taktiri- Haraka haraka haina Baraka
v) Taswira- Dunia ni mtu mkavu kiumbe usiegemee
vi) Tashbihi- Juzi na jana ni kama leo
vii) Tashtiti- Pilipili usioila yakwaashiani? (Zozote 6x2=12)

GATUZI NDOGO LA LONDIANI
MATIHANI WA MWINGO WA KUHITIMU KIDATO CHA NNE
hati ya kuhitimu elimu ya secondari kenya
KISWAHILI
Karatasi 1
Julai/Agosti 2015

1. Umeteuliwa kuwa katibu wa jopo linalochunguza chanzo cha wa usalama nchini. Andika ripoti yako.
2. Serikari ya ugatuzi imekumbwa na changamoto nyingi. Tetea kauli hii.
3. Usiopoziba ufa utajenga ukuta.
4. “Tangu siku hiyo nilifahamu fika kuwa mtu yeyote anaweza kufanikiwa maishani bila kujali asili yake mradi tu awe na nidhamu na atie bidii katika afanyalo.

GATUZI NDOGO LA LONDIANI
MATIHANI WA MWINGO WA KUHITIMU KIDATO CHA NNE
hati ya kuhitimu elimu ya secondari kenya
KISWAHILI
Karatasi 2
Julai/Agosti 2015

UFAHAMU

MOJAWAPO ya Nomino ambazo ngeli zake zinakutokubaliana kwingi miongoni mwa wanasarufi wa Kiswahili ni ‘maiti’. Walimu na wapenzi wengine wa sarufi ya Kiswahili huchelea kueleza kwa katika mahali pa ‘maiti’ katika Mfumo mpya wa uanishaji wa ngeli uitwao upatanisho wa kisarufi.

Binafsi, niwahi kukabiliwa na swali lihusulo ngeli ya Nomino ‘maiti’ ingawa jawabu kwa kawaida huambatana na maelezo marefu ambayo dhamira dhamira yake ni kajaribu kuutilia nguvu mwegemeo wangu. Ninadhani hata wewe umewahi kukumbana na hali sawa na hiyo!

Kwa Muhtasari, uanishaji wa ‘maiti’ kingeli una uambaji ngoma wa aina mbili kama zilivyo ngeli nyinginezo kadhaa. Wanasarufi Fulani hudai kwamba Nomino inapaswa kuingizwa katika ngeli ya (I – ZI) ilhali wenye maoni tofauti hushikilia kwamba inapaswa kuwa katika ngeli (A – WA). Sababu zitolewazo na wanasarufi hao kuhusiana na misimamo yao, ukisikiza kwa makini, utaona kwamba zina mashiko ya aina fulani.

Awali, nilieleza kwamba vipo vipengele vingine ambavyo vinaweza kuchukua mkabalakati ila si suala la ngeli! Haiyumkiniki kudai kuwa Nomino moja inaweza kuinia katika ngeli mbili tofauti. Kwa hivyo, kinachohitajika ni ukubalifu kuhusu kuhusu mahali pa Nomino yenyewe katika mfumo mpya wa uanishaji wa ngeli bali si maelezo marefu ya kushawishi.

Katika makala haya, ninadhamiria kuonyesha sababu mbalimbali zinazowafanya wenye mikabala miwili tulioitaja kuliweka neno hilo katika mbili tofauti. Baadaye, nitapendekeza njia ambayo kwayo utata huo unaweza kutatuliwa.

Wanaoshikilia msimamo wa A – WA wanatoa sababu kadha zinazoelekeza tazamo wao. Wanatumia methali jadi zilizotumika nomino maiti pamoja na tamaduni nyingine zinazohusiana na sherehe za matanga na mazishi ya Waswihili kushadidia madai yao. Wanadai kwamba methali hizo zimetumia kirejeshi (ye) na viwakilishi nafasi ambata ‘u’ au ‘a’ kurejelea maiti. Vitambishi hivyo hujitokeza katika ngeli ya A – Wa katika hali ya umoja. Baadhi ya methali hizo ni pamoja na:-

1. Adhabu ya kaburi aijuaye maiti.
2. Maiti haulizi sanda.
3. Aibu ya maiti aijuaye mwosha.

Kwa mujibu wa mila na itikadi wa Waswahili, inasemekana kwamba Kisomo anachosomewa maiti kaburini mara tu baada ya kuzikwa huitwa talkini. Hapa, kiambishi ‘a’ katika neno ‘anachosomewa’ hurejelewa na kudaiwa kwamba kunayo sababu maalumu iliyowafanya Waswahili kutotumia kiambishi kiwacho chochote kila mathalani (i) ya upatanisha wa sarufi katika ngeli ya (I – ZI), na badala yake kutumia kiwakilishi nafsi-ambata (a)

Sababu nyingine itolewayo kuunga mkono madai ya wanasarufi hao ni ile ya heshima au uluwa. Wanasema kwamba ijapokuwa maiti uhai, heshima yake ingalipo na ndiyo sababu hufanyiwa mazishi maalumu. Kwa maiti hiyo hiyo, methali, ‘mimi mbega nafa na uzuri wangu’ hutumiwa kushadidia suala hilo la heshima ya maiti.

Aidha, majina ya heshima ambayo huendelea kutumiwa na walio hai kumrejelea aliyeaga dunia miaka mingi baadaye ni ushahidi mwingine unaolezea sababu ya kuwekwa kwa nomino maiti katika ngeli. Majina hayo
ni ‘marehemu’ na ‘hayati’. Tunasema, ‘Marehemu kakangu alikuwa muungwana sana au; Hayati Mwinyihatibu alitufanyia mambo mengi.’ Ushahidi mwingine utolewao, kuunga mkono msimamo huo ni ule wa kuwepo kwa kisawe cha maiti; mfu, ambacho hutumia kiwakilishi nafsi – ambata (a)
Tunasema, ‘Mfu amezikwa’ wala si ‘mfu umezika’.

Wanasarufi wenye msimamo wa pili hudai kuwa maadamu hamna uhai na hisia katika maiti; kigezo muhimu kielekezacho uingizwaji wa Nomino katika ngeli ya A – WA, basi Nomino inapswa kuingizwa katika katika ngeli ya (I – ZI) kama vilivyo vitu vingine vingi ambavyo havina uhai wa na sarufi hao wanaendelea kudai kwamba haiyumkiniki kudai, ‘Maiti wake anazikwa kesho’ ila tunasema, ‘Maiti yake itazikwa kesho,. Maoni ya wanasarufi hawa ni kuwa mairi ‘inapaswa’ kuchukuliwa kama nomino yenziwe mzoga ambayo iko katika ngeli ya U – I. Wanaendelea kudai kwamba suala la heshima lina umuhimu mdogo likilinganishwa na ‘uhai’ na ‘hisia’

Ipo haja ya kuafikiana kuhusu ngeli moja ya nomino ‘maiti’ na nyingine kadha zenye utata. Ili kufanikiwa kuifanya hivyo, jambo moja moja linapswa kupewa kipau mbele: Kuzibwaga imani na misimamo ambayo tumekuwa nayo kwa muda mrefu kuhusiana na nomino husika na kwa radhi, kukumbatia mjadala na kujifunza upya.

maswali

1. (a) Yape makala uliyosoma anwani mwafaka. (Alama 1)
   (b) Taja mitazamo miwili inayotumika kuanisha neno maiti ki-ngeli
   (Alama 1)
   (c) Si sawa kuweka neno maiti kwa ngeli mbili. Eleza (Alama 1)
   (d) Tetea msimamo wa ki-mila kwa kuanisha maiti katika ngeli.
   (Alama 3)
   (e) Onyesha sababu inayofanya maiti kufanyiwa mazishi maalum.
   (Alama 2)
   (f) Pendekeza mbinu ya kutatua mgogoro uliopo wa kuanisha neno maiti ki-ngeli
   (Alama 2)
   (g) Eleza maana ya;
      (i) Maiti haulizwi sanda. (Alama 1)
      (ii) Adhabu ya kaburi aijuaye maiti. (Alama 2)
      (iii) Mantiki
2. **UFUPISHO**
   Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayaofuata.

   Tume ya kutathmini mishahara (SRC) inafaa kuchunguza kwa makini pendekezo la kutaka umri wa kustaafu kwa watumishi wa uma upunguzwe kutoka miaka 60 hadi 55.

   Kulingana na SRC, kupunguzwa kwa umri wa kustaafu kutasaidia kupunguza mzigo mzito wa mishahara ambayo hupewa wafanyikazi wa umma na kuacha kiasi kidogo tu cha fedha wa ajili ya miradi ya maendeleo. Kufanya hivyo ni sawa na kukata mguu kwa sababu una kidonda kabla ya kuutafutia matibabu.

   Ikumbukwe kuwa, umri wa kustaafu kwa watumishi wa umma nchini uliongezwa miaka mitano iliyopita kutoka miaka 55 hadi 60 baada ya Serikali kung'amua kuwa zaidi ya wafanyikazi 20,000 wa umma na walimu walitaka kulipwa pensheni, hivyo kuwa mzigo mkubwa kwa Serikali.

   Wakati mjadala wa kutaka kupunguza mishahara minono ambayo watumishi wa umma wanapokea na kuacha masazo kwa ajili ya maendeleo kuzuka mwezi Machi, mwaka hu, Rais, naibu wake pamoja na baraza la mawaziri walitangaza mishahara yao ipunguzwe. Rais pia aliwashinikiza wakuu wa mashirika ya umma kufuata nyayo la sivyo wapigwe kalamu nyekundu.

   Mathalani, wasomi wa masuala ya uchumi nchini China, ambapo umri wa wastani wa kustaafu ni miaka 53, wanajikuna kichwa sasa ili kutafuta mikakati ya kuongeza umri huo hadi miaka 65 katika kipindi cha miongo miwili ijayo kutokana na kiasi kikubwa cha fedha kinachotumika kuwalipa wanaostaafu pensheni zao.

   Wasomi wa uchumi nchini humo wanadai kuwa pengo lililopo, baina ya umri wa kustaafu wa miaka ma wastani wa umri ambao. Wachina wanastahili kuishi wa miaka 75, ni kubwa mno hivyo kuongeza uwezekano wa mtu kuendelea kuchukua malipo ya baada ya kustaafu kwa zaidi ya miaka 10. Kwa mujibu wa wanauchumi, hali hiyo imesababisha Msongamano mkubwa katika hazina ya malipo ya uzeeni. Suala hilo lilisababisha Serikali kualika masharika mbalimbali duniani yakiwemo Benki ya Dunia na Shirika la Wafanyikazi Ulimwenguni (ILO) kutoa mapendekezo ya kuhusiana na hali hiyo.

   Benki ya Dunia ilishauri China kuongeza umri wa kustaafu ili kupunguza kiasi kikubwa cha fedha zinazotumika kulipa waliostaafuu malipo ya baada ya uzeeni. Nchini Uturuki, mtu anatakiwa kustaafu baada ya kuifanya kazi kwa kipindi cha miaka 25. Hiyo inamaanisha kuwa mtu akianza kuifanya kazi akiwa na umri wa miaka 20 atatakiwa kustaafu anapotimiza miaka 45.

   Hata hivyo, hatua hii ya kustaafisha watu mapema, imekuwa na athari chungu nzima kiuchumi nchini humo huku ikikadiriwa kuwa kufikia mwaka wa 2045 taifa hilo litakuwa likitumia asilimia 6 ya mapato yake kulipa pensheni, endapo mambo hayatabadilishwa.

   Hayo ni mataifa machache kati ya mengi ambayo yamejaribu kupunguza umri wa kustaafu na kujutia baadaye. Serikali inafaa kutafuta njia mbadala kukabiliana na tatizo hilo na wala sio kuwaachisha kazi mapema.

Maswali

(a) Kwa maneno yasiyozidi 50, Eleza sababu za kuoengeza umri wa kustaafu kutoka miaka 55 hadi 60 na athari zake.
(Alama 7)

(b) Kwa maneno yako mwenyewe Fupisha aya tatu za mwisho. Tumia maneno 70.
(Alama 8)

3. MATUMIZI YA LUGHA

(a) Eleza miundo miwili ya silabi (Alama 2)

(b) Badilisha kiwakilishi kimilikishi kuwa kiwakilishi kionyeshe katika sentensi hii:
Chake kilipatikana chini. (Alama 1)

(c) Tunga sentensi moja kutofautisha mfinyo na mvinyo.
(Alama 2)

(d) Tumia mzizi 'fupi' kama kiwakilishi kitenzi katika sentensi moja. (Alama 2)

(e) Ainisha chagizo katika sentensi ifuatayo;
Wanafunzi wote waliondoka kwenda nyumbani jana alasiri. (Alama 2)

(f) Yakinisha kwa udogo.
Mvulana asiyeeleewa lugha hiyo hakuizungumza vizuri.
(Alama 2)

(g) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha jedwali
Alifika karamuni kisha akaondoka upesi sana.
(Alama 4)

(h) Tumia paradensi kwa sentensi mbili tofauti kudhihirisha matumizi tofauti. (Alama 2)

(i) Taja aina mbili za maktaba. (Alama 2)

(j) Andika katika usemi ripoti.
Nikiondoka leo jioni, "mtalii mmoja akasema, "Nitafika kwetu Jumanne ijayo,"
(Alama 3)

(k) Bainisha virai vumishi katika sentensi zifuatazo.
(Alama 2)
(a) Kijana yule mpole sana ni wake.
(b) Mkulima mwenye lile shamba kubwa ameaga dunia.

(l) Akifisha
Mstahiki Meya alishindwa kabisa kuona thamani ya binamuye Siki kila siku alisikika akisema kwa nini binamu yangu anawachochea wanacheneo.
(Alama 4)

(m) Geuza maneno yalioyopigwa mstari yawe katika hali iliyopewa mabanoni. (Alama 2)
(i) Alitia hazira alipochelewa sana.(kitenzi)
(ii) Babu Hupenda kucheka. (kivumishi)

(n) Unganisha sentensi zifuatazo kwa kutumia kiunganishi cha masharti, hali timilifu; wakati ujao
(Alama 2)
Asha na John wamejisajili.
Asha na John watachagiliwa tena.

(o) Tumia la katika sentensi katika kauli ya kutendeshea.
(Alama 2)

(p) Tunga sentensi moja yenye viwakilishi visisitizi vya ngell ya K U (Alama 2)

(q) Eleza maana tofauti za sentensi ifuatayo.
(Alama 2)

(r) Andika kinyume cha;
Wazee walifukua shimo lililpfunikwa. (Alama 2)

4. ISIMU JAMII

Kwa kurejelea mifano mwafaka, Thibitisha kuwa Kiswahili ni Lugha ya kibantu.
(Alama 10)

GATUZI NDOGO LA LONDIANI
MATIHANI WA MWINGO WA KUHITIMU KIDATO CHA NNE
hati ya kuhitimu elimu ya secondari kenya
KISWAHILI
Karatasi 3

Muda : 2 ½
Julai/Agosti 2015

SEHEMU YA A
TAMTHILIA – MSTAHIKI MEYA
Timothy Arege

1. Fafanua mbinu alizotumia Mstahiki Meya kudumisha (kudhibiti) utawala wake. (Alama 20)

SEHEMU YA B

2. "Nini hii? What is this?
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)
   (b) Eleza masaibu ya kinachoashiriwa. (Alama 8)
   (c) Taja na ufafanue mbinu ya lugha iliyotumiwa katika dondoo hili. (Alama 4)
3. "Mchimba kisima huingia mwenyewe" Jadili kauli hii ukirejelea riwaya ua Kidagaa Kimemwozea. (Alama 20)

SEHEMU YA C
FASIHI SIMULIZI

4. (a) Eleza umuhimu wa aina zifuatazo za ngano katika jamii.
   (i) Ngano za mtanziko. (Alama 6)
   (ii) Fafanua umuhimu wa maagizo ya watoto (Alama 6) (iii) Fafanua sifa tano za RARA (Alama 4)
   (iv) Eleza dhima ya misimu kama kipera cha usemi (Alama 4)

SEHEMU YA D
USHAIRI

5. Soma mashairi yafuatayo kisha ujibu maswali.

SHAIRI A

Tunda la elimu zote, wasema wanazuoni
Nikwamba mtu apate, tutambua manani
Ndipo hadhi aipate, ukumbukwe duniani

Elimu bila ukweli, haizidi asilani
Giza na nuru muhali, katu havitangamani
Uwongo uje kwa kweli, itue nuru moyoni.

Elimu ni kama mali, haicho shikutamani
Ni bora yashinda mali, tala la wanazuoni
Elimu jema naili, iangazayo gizani

Wafu na wasiosoma, watazikwa aridhini
Hadi ndio maulana, wapaao maangani
Elimu jambo dhima, aso nayo maskini

Toa wafu ujana, elimu ukitamani
Na uwe mzee sana, kujua usijihini
Elimu bahari pana, milele hauoni pwani

Elimu ina malipo, utayalipwa mwishoni,
Pale vitafutapo, mbingu usitamani

Mwana chumia fapo, mbingu huwa huzuni

Haki ya kuheshimiwa, ni yao wanachumi
Wao wamengolewa, na ni taa duniani
Kweli wanapojua, watoe bila kuhini.

Elimu bila amali, mti usio majani
Haumtii kivuli, aukaliaye chini
Inakuwa mushkeli, wakighuri insane.

SHAIRI B

Inakeramoyo
Hiianga ambayo
Huwasonya njiani
Watukao mashambani
Wakusalimu kwa bashasha
Wanaoshindakivulini.

Chini ya mwembe
Wa umma

Inakera moyo
Hii sebule amabyo
Huwahanimezaini
Wagota onyundo kutwa
Wakukabidhi chakula
Wanao starehe daima

Chini ya paa
La umma

Maswali

(a) Pendekeza kichwa mwafaka kwa shairi la A na la B (Alama 2)
(b) Haya ni mashairi ya aina gani?
(Alama 2)
(c) Taja sifa zozote tatu za kishairi katika shairi la B. (Alama 3)
(d) Taja mbinu ya lugha iliyotumiwa
(i) Katika mshororo wa mwisho au beti wa saba katika shairi la A (Alama 1)
(ii) Katika ubeti wa nne shairi la B (Alama 1)
(e) Fafanua kwa muhtasari maudhui ya mashairi la A katika nathari
(Alama 3)
(f) Andika ubeti wa mwisho wa shairi la A katika nathari
(Alama 3)
(g) Taja na uonyeshe jinsi Idhini ya ushairi ilivyotumika katika shairi la A
(Alama 2)
(h) Eleza maana ya maneno haya yalivyotumika katika shairi la A
(Alama 2)
(i) Wameongolewa
(ii) Wagotao

SEHEMU YA E
HADITHI FUPI – DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE – Ken Walibora
Jibu swali la 6 au 7.

6. Kwa kurejelea hadithi zozote tano, Jadili matatizo yanayowakumba vijana katika jamii.
(Alama 20)
7. “Nani amekwambia kwamba mimi unanihusudu? Lini nimekulalamikia hivyo au kumlalamikia mtu

mwingine....?

(i) Eleza muktadha wa dondoo hili
(Alama 4)

(ii) Eleza sifa za msemaji wa maneno haya
(Alama 6)

(iii) Onyesha jinsi msemehewa alivyojinyesha uozo wa kijamii (Alama 10)

GATUZI NDOGO LA LONDIANI
MATIHANI WA MWINGO WA KUHITIMU KIDATO CHA NNE
hati ya kuhitimu elimu ya secondari kenya
KISWAHILI
Karatasi 1
Julai/Agosti 2015

1. Hii ni inshan ya ripoti

MUUNDO AU SURA YA RIPOTI MAALUM

1. Iwe na **KICHWA.** Kiandikwe kwa herufi kubwa. Kitaje ni ripoti ya nani kuhusu nini?
2. Iwe na **UTANGULIZI** unaoweleza swala linalochunguzwa. Mtahini anaweza kutoa maelezo au historia fupi kuhusu swala husika. Anaweza kuwaatambua wanajopo na nyadhifa zao kwa usanjari wa kiitifaki.
3. **MATOKEO**
   Mtihini azunngumzie tatizo lenyewe katika mada ndogo ndogo. Mada hizo au hoja hizo zisipungue tano.
   Hivi ndivi vyanzo vya utovu wa usalama:
   Siasa – vyama vya siasa
   Uchochezi ktuka kwa Viongozi
   Chuki na uhasama baina ya makabila
   Umaskini
   Ukosefu wa ajira
   Vikundi haramu vya vijana k.m mungiki, sungusungu, MRC na kadhalika
   Ugaidi
   Dhuluma za kihistoria

KADIRIA HOJA NYINGINEZO MWAFAKA

4. **MAPENDEKEZO**
   <u>Mapendekezo huwa ni suluhisho kuhusu tatizo au swala linaloelezwa katika sehemu ya matokeo. Mtihini aorodheshe mapendekezo yake kulingana na kila tatizo. Hoja ziwe kama hizi. Kadiria ufaafu wa hoja nyinginezo</u>
   <u>Mapendekezo</u>
   Wachochezi kuchukuliwa hatua za kisheria.
   Wananchi kuhamasishwa kuhusu umuhimu wa kuishi pamoja kwa amani
   Serikali wa washikadau kushirikiana ili kukabili tatizo la Umaskini.
   Kubuni nafasi za ajira kwa vijana.
   Serikali kukabili vikundi haramu na Ugaidi vilvyo
5. **HITIMISHO**
   Mtahini atoe Muhtasari wa swala hilo na namna mapendekezo yake yatasaidia kulitatua swala husika.
   Anweza kutoa himizo, ombi au shukrani kwa wanaohusika.
   Aache nafasi kama ya mstari mmoja kisha Aandike:

   Ripoti hii imeandikwa na:
   Jina
   Sahihi
   Wadhifa
   Tarehe

2. Hii ni swali la maelezo. Linaweza pia kuwa la mjadala ambapo mtahini anaweza kuunga mkono kuanzia mwanzo hadi mwisho, apinge kuanzia mwanzo hadi mwisho au aunge mkono. Apinge kasha atoe msimamo wake. Baadhi ya hoja ni kama zifuatazo:

CHANGAMOTO ZA SERIKALI ZA UGATUZI

i. Ukosefu wa usawa katika ugawaji wa fedha gatuzi mbalimbali.

ii. Kutolewa kwa serika kuna Serikali ya jimbo/gatuzi.
iii. Kutoelewa kwa maana ya ugatuzi kwa magavana.
iv. Kuingiliwa hasa siasa kwa mkakato wa ugatuzi.
v. Ukosefu wa mipango katika kutekeleza ugatuzi.
vi. Ufisadi wa baadhi ya uongozi (magavana)
vii. Ukosefu wa uwezo wa kutekeleza majukumu ya serikali za majimbo.
viii. Kudhoofika kwa uchumi wa Serikali.
ix. Uhaba wa wataalamu (wanataaluma)
x. Kutowajibika kwa viongozi wa gatuzi.

3. Usipoziba ufa utajenga ukuta

   Hii ni insha ya methali. Mtahini asimulie kisa au visa vitakavyodhihirisha kuwa unatakiwa kuifanya au kurekebisha jambo mapema. Unapokosa kuifanya hivyo utapata matatizo mengi baadaye au itakubidi ufanye jambo kubwa sana kuliko la awali. Akikosa kuuelewa maana ya methali atakuwa amepotoka. Kiwango chake ni D. Si lazima aeleze maana ya methali. Anaweza kusimulia hadithi ifafanuayo maana ya methali moja kwa moja.

4. Hii ni swali la mdokezo – Swali la kuendelea/kutamatisha. Lazima swali likamilishe kwa kifungu cha maneno. Kisa kioane na kimalizio.
   Tanbihi – Asiyemalizia kwa kifungu, hajajibu swali, ameegemea upande mmoja. Mtahini kama huyo kiwango chake ni D.

GATUZI NDOGO LA LONDIANI
MATIHANI WA MWINGO WA KUHITIMU KIDATO CHA NNE
hati ya kuhitimu elimu ya secondari kenya
KISWAHILI
Karatasi 2
Julai/Agosti 2015

1. UFAHAMU
   (a) Ngeli ya maiti/maiti/mikabala kuhusu ngeli ya maiti.
   (Alama 1)
   (b) (i) Wanaoweka kwa ngeli ya a – wa (Alama 1)
   (ii) Wanaoweka kwa ngeli ya I-Zi
   (c) Vipo vipengele vingine vinavyoweza kuchukua mkabala kati na si suala la ngeli.
   (Alama 2)
   (d) Kisomo anachosomewa maiti kaburini huitwa talkini. Kiambishi – katika neno anachosomewa hurejeelewa na kudaiwa, kwamba kunayo sababu maalumu ya Waswahili kutotumia kiambishi chochote mathalan (i) ya upatanisho wa sarufi wa ngeli ya I-Zi.
   (Alama 3)
   (e) Heshima yake bado ingalipo. (Alama 2)
   (f) (i) Kuzibwaga imani na misimamo ambayo tumekuwa nayo kwa muda mrefu.
   (ii) Kuwa radhi kukumbatia mjadala na kujifunza upya. (2 x 2 = 4)
   (g) (i) Mtu asiyejiweza haulizwi msaada.
   (Alama 1)
   (ii) Aliyepatwa na jambo mbaya ndiye anayeweza kulieleza.
   (Alama 1)
   (iii) Mantiki – maana.
   Ufupisho – Mwongozo
   Sw1 – Serikali iling'amua kuwa zaidi ya wafanyikazi 20,000 wa umma na walimu walipwa pensheni.
   - Ni mzigo mzito wa mishahara ambao unaacha kiasi kidogo cha fedha kwa mradi ya maendeleo.
   Mtiririko – 1
   Hoja 3 x 2 = 6
   Jumla – 7

   Sw2 – Ushauri wa Benki ya Dunia kwa Dunia
   - Nchini Uturuki mtu anastaafu akiwa amefanya kazi kwa kipindi cha miaka 25.
   - Mtu akianza kufanya kazi akiwa miaka 20 anastaafu akiwa na miaka 45.
   - Hatua hii imekuwa na athari za kiuchumi.
   - Mwaka wa 2045 Uturuki itakuwa asilimia 6 ya mapato yake kulipa pensheni.
   - Hii ni mifano ya mataifa ambayo yamejaribu kupunguza umri wa kustaafu na kujutia baadaye.
   - Serikali itafute njia mbadala na wala si kuwaachisha wafanyikazi kazi mapema.

   Mtiririko = 1
   Hoja 1 x 7 = 7
   Jumla = 8
3. **MATUMIZI YA LUGHA. (Al 40)**
   (a) (i) Konsonanti na irabu
   (ii) Irabu moja
   (i) Konsonanti mbili na irabu.
   (ii) Konsonanti tatu na irabu.
   Zozote ½ x 4 = 2
   (b) Hiki/hicho/kile
   Chochote 1 x 1 = 1
   (c) Mfinyo – kubanwa
   Mvinyo – pombe/aina ya kinywaji.
   Atunge sentensi moja.
(Alama 2)
   (d) Mfupi alitueleza kisa kwa kifupi. 1 x 2 = (Alama 2)

(e) Nyumbani jana alasiri. (Alama 2)
(f) Kivulana kinachoelewa lugha hiyo kilizungumza vizuri
(g)

S						
S^1			U		S2	
KN	KT			KN	KT	
#	T	E		#	T	E2
	Alifika	Karamuni	Kisha		akaondoka	Upesi sana

(Alama 4)
(h) Kutoa maelezo zaidi. (Alama 2)
(i) Maktaba ya kitaifa
Maktaba ya …….
Maktaba ya darasa
Maktaba ya kibinafsi
Zozote 2 x 1 = 2
(j) Mtalii mmoja alisema kuwa (kwamba) angeondoka siku hiyo (ile) jioni angefika kwao Jumanne iliyofuata.
(Alama 3)
(k) Yule mpole sana. (Alama 1)
Mwenye lile shamba kubwa. (Alama 1)
(l) Mstahiki Meya alishindwa kabisa kuona thamani ya Binamuye Siki. Kila siku alisikika akisema "Kwa nini binamu yangu anawachochea Wanacheneo?"
(Alama 4)
(m) (i) Alinikarisha alipochelewa sana. (Alama 1)
(ii) Babu ni mcheshi. (Alama 1)
(n) Ikiwa, kama, endapo, iwpo
Iwapo John na Asha watakuwa wamejisajili watachaguliwa tena.
(Alama 2)
(o) Nitamlishia jirani ng'ombe wake. (Alama 2)
(p) Kuku huku kuna siafu wengi. (Alama 2)
(q) Kuongeza idadi. (Alama 1)
Baadhi watakuja. (Alama 2)
(r) Wazee walifukia shimo lililofunuliwa. (Alama 2)

ISIMU JAMII

Kiswahili ni kibantu

- Vitenzi vya kawaida huishia kwa a katika Kiswahili na lugha nyingine za kibantu.
  Lia – la, cheka, theka
- Maumbo ya maneno kwa Kiswahili na lugha za kibantu yana viambishi kim mu-ndu.
- Kuna mfanano wa kimsamiati k.m kuhoa, korora, kooa.
- Shadda huwekwa aghalabu kwa silabi ya pili kutoka mwisho. Kohoa, korora
- Mara nyingi huwa na muundo wa silabi wazi/huru.
- Nomino hupangwa katika ngeli.
  M – wa/mu-ba
- Upatanisho wa kisarufi ni sawa k.m
  Baba analima/Baba arima
- Mpangilio wa maneno katika tungo ni sawa.
  Mtu anakuja le/Mundu anecha juno
- Kuna mnyambuliko wa vitenzi.
  Lia – lilia/Rira – ririra
- Mizizi ya maneno huweza kufanana.
  Zozote 5 x 2

Kutaja hoja 1
Mfano/maelezo 1

MTIHANI WA MWIGO WA WILAYA ZA UGENYA - UGUNJA
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya
Kidato cha Nne
KISWAHILI
Karatasi - 102/1
(INSHA)

1. **LAZIMA**

Kumekuwa na mjadala katika vyombo vya habari vya humu nchini kuhusu visa vya ukosefu wa usalama. Mwandikie barua mhariri wa Gazeti 'Nisome' ukitoa maoni yako kuhusu namna ambavyo visa hivyo vimeathiri maendeleo ya nchi hii.

2. Ustawi na maendeleo ya nchi yategemea mfumo wa ugatuzi nchini Kenya. Jadili.
3. Andika kisa kinaschodhihirisha maana ya methali; Mchelea mwana kulia hulia yeye mwenyewe.
4. Tunga kisa kitakachokamilika kwa maneno yafuatayo;
. . . . ilikuwa ni baada ya hatua yangu ya mwisho ndipo nilipotambua kuwa safari ndefu huanza kwa hatua moja.

MTIHANI WA MWIGO WA WILAYA ZA UGENYA - UGUNJA
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya
Kidato cha Nne
KISWAHILI
Karatasi - 102/2
Julai / Agosti 2015
Muda : Saa 2½

UFAHAMU (alama 15)
Athari ya utandawazi kwa asasi na taasisi ni kubwa. Mabadiliko na mageuzi makubwa yanayotokana na nguvu na mielekeo ya utandawazi yanatoa changamoto nyingi kwa binadamu kokokote waliko ulimwenguni. Chama cha Kiswahili cha Taifa (CHAKITA) kimetambua haja na dharura ya kukabiliana na masuala yanayotokana na utandawazi. Ni kutokana na ukweli huu ambapo CHAKITA kiliwaleta pamoja wasomi na wataalamu kutoka nchi mbalimbali katika kongamano la kimataifa hivi majuzi, ili kuziangazia dharura zinazotokana na mabadiliko ya utandawazi.

Dhana ya utandawazi ina maana pana. Kimsingi, utandawazi uhusisha; biashara, vyombo vya habari na **teknohama**.(Teknolojia ya habari na mawasiliano), uhamiaji wa watu na utamaduni. Ikizingatiwa kuwa utamaduni ni kitovu cha maisha ya binadamu ni dhahiri kuwa utamaduni ni muhimu katika suala la utandawazi. Inatupasa tuangalie athari ya utandawazi kwa utamaduni.

Ili kufanya hivyo muhimu kuzingatia lugha kwa sababu mbili kuu; kwanza lugha ndicho kitovu cha utamaduni ambao ni msingi wa utandawazi. Pili lugha ni mali ghafi ya fasihi - iwe simulizi au andishi. Katika jamii nyingi za kiafrika, fasihi simulizi imekuwa ikisakamwa na kupata upinzani mkubwa sana kutokana na fasihi andishi. Kutokana na haya fasihi simulizi imepuuzwa huku andishi ikitiliwa maanani. Aidha, dhima ya fasihi simulizi katika maendeleo haijatambuliwa na kusisitizwa ipasavyo. Hoja kuu ni kwamba fasihi simulizi ni muhimu na inafaa kuendelezwa kama msingi, na mhimili wa maendeleo ya jamii.

Hakuna maana moja dhahiri inayokubaliwa na wataalamu wote kuhusu dhana ya fasihi simulizi. Kutokana na hali hii, maelezo na mtazamo kuihusu ni finyu. Hata hivyo, licha ya uhuru wa matumizi na maelezo, kimsingi fasihi simulizi huchukuliwa kumaanisha jumla ya **tajriba** ya maisha ya watu. **Tajriba** hizo hudhihirika kupitia mawasiliano ya lugha, mifumo ya kijami kama vile, nyimbo za tobara, hisia imani, ushirikina, tabia, na mazoea; ufundi na mbinu wazitumiazo watu kukidhi mahitaji yao ya kimaisha.

Fasihi simulizi kwa hivyo, ni falsafa ya maisha ya watu. Aina hii ya fasihi husimulia au kueleza hali au matukio katika jamii fulani maalum. Kwa kuwa hudhihirisha utamaduni, fasihi simulizi inaweza kuelezwa kuwa ni **nembo** ya jamii. Ni ushahidi na ithibati ya maisha ya jamii inayosimuliwa kwa namna mbalimbali.

Teknohama inachukua nafasi kubwa katika utolewaji na uasilishwaji wa fasihi simulizi. Maisha ya jamii yameanza kusimuliwa ka njia na namna mbalimbali kutokana na maendeleo ya teknolojia. Tofauti na ilivyokuwa zamani ambapo fani mbalimbali za fasihi simulizi zilitegemea fanani, utandawazi umeibua vyombo ambavyo vinatekeleza majukumu hayo ya fanani. Redio, televisheni, tovuti, tarakilishi, kanda na kamera ni baadhi tu ya vifaa ambavyo sasa vinahifadhi na kuwasilisha aina mbali mbali za fasihi simulizi.

Siku hizi, simulizi kuhusu maisha ya watu: methali, vitendawili, nyimbo, ushirikina, sitiari, misemo na visasili vimehifadhiwa katika maandishi. Mbali na habari hii kuhifadhiwa katika maandishi na hivyo kubadilisha namna ya uwasilishaji, majukumu ya fanani na hadhira pia nayo yanabadilika. Dhima ya msimulizi inazidi kudidimia huku nafasi yake ikitawaliwa na teknolojia. Pia tofauti na ilivyokuwa zamani ambapo hadhira ilijumuika na kushiriki kikamilifu katika masimulizi siku hizi ushiriki wake si wa moja kwa moja. Watu wanaweza kusoma na kusikiliza fasihi wakati na mahali popote pale.

Maswali

a) Teua anwani mwafaka ya makala haya. (alama 2)
b) Wasomi na wataalamu kutoka nchi mbalimbali waliletwa pamoja na CHAKITA kwa madhumuni gani?

(alama 2
c) Tambua maeneo manne yanayohusishwa na utandawazi.
(alama 2)
d) "Utamaduni mhimili wake ni lugha," Thibitisha kauli hii kulingana na makala. (alama 4
e) Ni kwa namna gani fanani na hadhira wameathirika kutokana na teknolojia?
(alama 2)
f) Eleza maana ya msamiati huu jinsi ulivyotumika katika taarifa. (alama 3)
   a) Teknohama.
   b) Tajriba .
   c) Nembo .

2. UFUPISHO . (alama 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali chini yake.

Sheng ni kifupisho cha 'Swahili-English'. Ni mfumo wa mawasiliano ambao umesanifiwa na vijana hasa wale wanaoishi katika sehemu za mijini. Mfumo wenyewe hufuata muundo wa sarufi ya Kiswahili na lugha nyinginezo za kibantu ila hutumia maneno mengi mapya ya kubuniwa na ya mkopo kutokana na lugha nyinginezo za kiafrika.

Maelezo haya ya kiujumla kuhusu maana ya sheng yametolewa na wasomi kadha kama vile, Mkangi (1984) ambaye ameueleza msimbo huu kama lugha mseto au lugha 'kiunzi' ya kizazi kipya cha vijana wa mjini. Pia Ogechi (2002) na Shitemi (2001) wanakubaliana na maoni hayo kwamba sheng ni msimbo wa kijamii unaotumiwa hasa na vijana wa mijini na mashambani nchini Kenya. Maelezo haya yanatoa baadhi ya sifa za kimsingi zinazoutambulisha msimbo huu.

Kwa mujibu wa Mukhebi (1986) sheng ni tukio la kitamaduni ambalo linafungamana sana na mawazo au fikra, hisia na matakwa ya watumiaji wake. Anaeleza kuwa wazungumzaji asilia wa sheng waligundua kuwa kutokana na hali na mazingira yao ya kifukara katika mitaa ya jamii yenye mapato ya chini, hawangeweza kupata elimu yao na kuwasiliana kupitia kwa Kiingereza bali walihitaji mfumo wao wenyewe. Kutokana na ufahamu wao duni wa Kiingereza, iliwawia vigumu vijana hao kuweza kujifunza masomo mseto kwa Kiingereza, masomo yalikuwa ya kimsingi katika mitaala ya shule za msingi wakati huo.

Kuna nadharia mbalimbali zinazojaribu kueleza chimbukizo na asili ya sheng. Hata hivyo, nadharia kuu ni mbili; nadharia ya uhuni na nadharia ya msimbo wa vijana.

Kwa mujibu wa nadharia ya uhuni, sheng ilibuniwa na kuibuka kutokana na wahuni au wakora jijini Nairobi (Kobia, 2006). Waliunda baadhi ya maneno kutoka nyuma kuelekea mbele badala ya muundo wa kawaida wa neno. Kwa mfano, neno 'nyama' lilibuniwa na kuwa 'manya'. Nadharia inahusisha kubuniwa kwa sheng na haja ya wahuni kuwasiliana kwa lugha ambayo watu wengine hawangeweza

kuifahamu. Mazrui (1995) anadai kwamba sheng iliibuka miaka ya thelathini jijini Nairobi kama lugha ya wahuni. Ilikuwa 'lugha' ya wahuni kujitambulisha hasa wale wanaonyakuwa mali ya watu na kutoroka.

Nadharia ya msimbo wa vijana kwa upande mwingine hudai kuwa sheng iliibuka katika mitaa ya Mashariki ya Nairobi mnamo miaka ya sabini Osinde (1986); Shitemi (2001). Kufuatia kupatikana kwa uhuru 1963, Idadi ya wakazi wa Nairobi ilipanda kwa haraka sana kutokana na kumimiika kwa watu kutoka mashambani wakitafuta ajira katika mitaa ya viwanda humo jijini. Wananchi hao maskini waliishia kuishi katika mitaa ya makazi duni ya viwandani Mashariki ya Nairobi ambayo ni kitovu vha maendeleo ya viwanda.

Ijapokuwa wafanyakazi hawa pamoja na jamii zao walilazimika kutumia Kiswahili kwa mawasiliano baina yao, wengi walikichukia Kiswahili kwa vile kilikuwa kimedunishwa sana na sera ya ukoloni kama lugha ya mashambani, lugha ya vibarua au maboi wa kuwatumikia wazungu. Hata hivyo watoto wa wafanyakazi hao hawakupendelea kukitumia Kiswahili kama wazazi wao kwa sababu kadhaa. Kinyume na wazazi wao. Watoto walilazimika kuishi katika hali ya jamii ya utatu-lugha: 'lugha za kinyumbuni' Kiswahili na Kiingereza. Pia, walitambua kuwa ingawa walilazimika kutumia lugha nyingi, ni Kiingereza pekee ambacho kilipewa hadhi kama lugha ya utawala, mamlaka, heshima na uwezo mkubwa wa kiuchumi.

Ili kuepuka matatizo ya kimawasiliano na kama njia ya kusuluhisha utata wa hali hiyo iliyowakabili, vijana hao waligundua msimbo wa mawasiliano kati yao, ingawa ulifuata sarufi ya Kiswahili, uliazima msamiati kutokana na lugha za kiasili na kuunda baadhi ya maneno yake. Msimbo huo ndio uliotokea kuwa sheng hapo baadaye.

Maswali

a) Bila kupoteza maana, fupisha aya tatu za mwanzoni . (kwa maneno 60 - 70)
(alama 6)

b) Eleza nadharia zinazoeleza chimbuko la sheng ukirejelea aya tano za mwisho (maneno 80 - 90)
(alama 9)

3. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA. (alama 40)

a) Eleza tofauti kati ya Irabu na konsonanti. (alama 2)

b) Toa mifano miwili ya ala tuli. (alama 2)

c) Andika sentensi ifuatayo ukibadilisha neno lililopigwa msitari kuwa kivumishi .
(alama 2)
Mgeni alipewa zawadi nzuri

d) Kiimbo ni nini? (alama 2)

e) Tunga sentensi mbili ukitumia neno 'maskini' kama :
i) Kihisishi (alama 2)
ii) Nomino

f) Bainisha matumizi mawili ya parandesi kwa kutoa mifano.
(alama 2)

g) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya mazoea. Mwanafunzi anayefanya bidii ndiye anayefaulu mtihani.
(alama 2)

h) Kanusha sentensi ifuatayo.
(alama 2)
Gari liliharibika, likakokotwa na kupelekwa kwenye karakana.

i) Tambua maana ya vitate vilivyopigiwa msitari. (alama 2)
Mkulima alivuka mto na kwenda kuona mahali palipokuwa pakifuka mvuke mwingi.

j) Tunga sentensi ukitumia nomino yoyote, ukibainisha viwakilishi vya ngeli.
(alama 2)

k) Andika sentensi ifuatayo ukianza na (Filamu . . . .)
Mtoto aliogopa filamu iliyojaa fujo akaanza kulia.
(alama 2)

l) Bainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo.
Mkulima aliyewakatia ng'ombe nyasi kwa mundu ameondoka. (alama 3)

m) Andika sentensi ifuatayo katika usemi taarifa. (alama 3)
Mimi nitawakaribisha wageni leo jioni. kisha nitaondoka kwenda kwetu kesho." Fatuma alimwambia Juma.

n) Tumia neno lingine lililosawa na yaliyopigiwa msitari. (alama 2)
Baba alivaa ndara akaelekea uani kuoga.

o) Tunga sentensi moja inayodhihirisha matumizi matatu ya kiambishi -ji-
(alama 3)

p) Linda kitenzi kimoja kimoja kutokana na nomino zilizopigiwa msitari katika sentensi hizi.
(alama2)
i) Mchumba wangu amewasili.
ii) Tulisogea madhabahuni ili kusali sala ya toba

q) Dunisha sentensi ifuatayo.
(alama 3)
Wazee wengi wa siku hizi hawapendi wanawake wanene.

r) Tunga sentensi iliyo na vishazi huru viwili.
(alama 2)

4. ISIMU JAMII (alama 10)

A. : Hamna! Wasiwasi wangu ni kutoa maelezo fika na mepesi yatakayoeleweka watakaofika. Wajua haya si maswala rahisi

B : Tarakilishi si chombo rahisi kwa yeyote. Maswala mengi ya utandawazi na kasi mawimbi hutatiza,
hasa msamiati huu mpya.

A : Wewe hukumbuki jinsi ilivyokuwa vigumu kuwaeleza wale wanafunzi wa shule za msingi kuhusu
huduma za mdahalishi kama vile barua pepe?

Maswali.

a) Taja sifa za sajili ya wataalamu hawa zinazopatikana kwenye kifungu hiki na nje yake.
(alama 6)

b) Kwa kifupi eleza nadharia zozote mbili zinazohusishwa na chimbuko la Kiswahili.
(alama 4)

MTIHANI WA MWIGO WA WILAYA ZA UGENYA - UGUNJA
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya
Kidato cha Nne
KISWAHILI
Karatasi - 102/3
Julai / Agosti 2015
Muda : Saa 2½

1. **LAZIMA : SEHEMU YA A**
USHAIRI

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

Lakini ndugu waendapi? Huko uendako siko,
Wenda wala huogopoi, ukawaza utokako,
Yule ni mwezio wapi, sione kile kicheko,
Ndugu yule si mwenzako, wenzako haswa ni sisi

Yule anakuthamini, kwa sababu una kitu,
Usambe akutamani, kwa kuwa mwema wa utu,
Kiwa huna humuoni, atakwacha mwanakwetu,
Asikutishe si mtu, si shani kuwa ni fisi

Atakula yako nyama, na mifupa kuguguna,
Wishapo atakusema, siku hizi wajiona,
Usuhuba atagoma, wa leo si kama jana.
Hakuoni utu tena, japo utu hujaasi.

Ndugu fikiri vizuri, upate kutaamali,
Yake yeye ni magari, wewe yako basikeli,
Wala sima achari, yeye maini na wali,
Walani? yeye hajali, katu hana wasiwasi.

Wawe mchunguze sana, ila yake uione,
Naye mkisemezana, yeye aola kwingine,
Huitika na kuguna, hajali muelewane,
Kitambicho si kinene, huna ela kumughasi.

Mbovu wa haya kweli, hiyo si wa kufuata,
Ikisha yako mali, guu kwako akakata,
Mutakuwa mbali mbali, kama watu waloteta,
Usingoje kuja juta, kheri tanga ulikisi

Sijitie kushatadi, ukamba waona mbali,
Ubora kwenu urudi, utuze yako akili,
Tuishi na yetu jadi, kama siku za awali
Tushikane kila hali, ya dunia ni mapisi.

MASWALI

a) Eleza ujumbe wa utunzi huu. (alama 4)
b) Weka shairi hii katika bahari yake kisha utaje mikondo mitatu. (alama 4)
c) Andika ubeti wa nne katika lugha tutumbi. (alama 4)
d) Toa mfano katika shairi inayothibitisha matumizi ya :
   i) Tashtiti (alama 2)
   ii) Inkisari (alama 2)
e) Eleza toni ya mtunzi wa shairi hili. (alama 2)
f) Eleza maana ya maneno haya:
   i) Kutaamali. (alama 1)

ii) Usuhuba (alama 1)

SEHEMU YA B
RIWAYA:
Kidagaa kimemwozea ; *Ken Walibora*
Jibu swali la 2 au la 3

2. Mzoea punda hawezi kumpanda farasi. Thibitisha kauli hii kwa kurejelea riwaya ya *Kidagaa kimemwozea.* (alama 20)
3. Tathmini umuhimu wa mbinu zifuatazo katika kuijenga riwaya *Kidagaa kimemwozea*
   a) Ushairi / nyimbo
   b) Hadithi ndani ya hadithi
   c) Methali (alama 20)

SEHEMU YA C
TAMTHILIA:
Mstahiki Meya *: Timothy M. Arege*
Jibu swali la 4 au la 5

4. Kwa kurejelea tamthilia nzima, thibitisha kuwa Mstahiki Meya hakustahili umeya. (alama 20)
5. ". . . Naona unajaribu kutia kidole chako katika mzinga wa nyuki. Ni hatari . . .
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   b) Eleza umuhimu wa msemewa (alama 6)
   c) Fafanua chanzo cha mgogoro baina ya wahusika katika muktadha. (alama 4)
   d) Tambua na ueleze mbinu za lugha zilizotumika katika dondoo hili. (alama 4)

SEHEMU YA D:
FASIHI SIMULIZI

6. a) Eleza maana ya misimu. (alama 1)
   b) Taja mambo ambayo ni msingi wa kuchipuka kwa misimu. (alama 5)
   c) Eleza tofauti kati ya visasili na visaviini. (alama 4)
   d) Ainisha mifano mitano ya mzungumzo katika Fasihi Simulizi. (alama 5)
   e) Eleza umuhimu wa kusoma Fasihi Simulizi katika shule nchini. (alama 5)

SEHEMU YA E:
HADITHI FUPI
Damu Nyeusi na Hadithi nyingine *Ken Walibora na Said A. Mohamed*
Jibu swali la 7 au la 8

7. "Wanawake ndio adui wao wenyewe". Thibitisha ukweli wa kauli hii ukirejelea hadithi zozote tano kwenye diwani ya *Damu nyeusi na Hadithi nyingine.* (alama 20)
8. ". . . Kama kweli mama yake Mwakitawa alikuwa hai, amekuwa wapi miaka hiyo yote?"
   a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
   b) Taja na ueleze sifa zozote mbili na umuhimu wa msemewa . (alama 4)
   c) Taja na ueleze mbinu iliyotumika katika dondoo hili. (alama 2)
   d) Toa mifano mingine miwili ya matumizi ya mbinu uliyotaja katika (c) kutoka hadithini. (alama 2)
   e) Ni mafunzo yepi anayopata msomaji wa hadithi *"Tazamana na mauti"*? (alama 8)

THE ABOVE (**WILAYA ZA UGENYA - UGUNJA**) IS A REVISION EXERCISE

TATHMINI YA PAMOJA YA SHULE ZA UPILI KAUNTI NDOGO YA KENYENYA
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya
Kidato cha Nne
KISWAHILI
Karatasi - 102/1
(INSHA)

1. **LAZIMA**

Umeteuliwa kuwa katibu wa japo linalochunguza kutafuta suluhisho kwa tatizo la udanganyifu katika mtihani wa kitaifa, jambo ambalo limekuwa tatizo sugu. Andika ripoti ya jopo hilo.
(alama 20)

2. Katiba mpya itaboresha maisha ya Wakenya. Jadili
(alama 20)
3. Ukiona cha mwenzako kikinyolewa na chako tia maji. (alama 20)
4. Andika insha itakayomalizia kwa maneno haya.
. . . nilisimama nikaangalia nyuma, machozi yakanitoka njia mbilimbili nilipokumbuka wosia wa walimu, wazazi na wenzangu.
(alama 20)

TATHMINI YA PAMOJA YA SHULE ZA UPILI KAUNTI NDOGO YA KENYENYA
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya
Kidato cha Nne
KISWAHILI
Karatasi - 102/2
Julai / Agosti 2015
Muda : Saa 2½

1. **UFAHAMU (alama 15)**

Soma taarifa inayofuata kisha uyajibu maswali

Mlachake alikuwa mziwanda miongoni mwa ndugu zake wanne. Alipopigwa darubini, alionekana kuwa mwanagenzi ambaye falau angemakinika angefikia upeo wa ufanisi masomoni kwa kuwa na vipawa adimu vilivyofaa kuchochewa, kufukutwa, kurandiwa na kupigwa msasa. Nia ingekuwepo njia ingepatikana. Wala hakuwa peke yake, kulikuwa na wengi kama yeye. Na kisiki kilichomkingamia kilikuwa kipi? Kisiki kilichokuwepo kilikuwa kwamba licha ya kuwa katika kidato cha tatu na mwenye umri wa miaka yapata kumi na sita, alikuwa mfano wa ajabu ya shingo kukataa kulala chini, hakukomaa. Na mtu ataitwa mtu vipi bila kukomaa? Wenzake darasani walimwita 'toto kuu' kwa kuwa japo alionekana katutumika, tena mlingoti, alidinda kukaramka. Nao utu uzima hufunzwa katika taasisi gani? Jawabu la swali hili lingalipatikana lingalimfaa sana Mlachake.

Na usidhani wasiokomaa ni waziwanda tu, hata vifungua mimba na wanuna wao wote waweza kukomaa kutegemea misukumo, ari na mazingira yaliyo karibu nao. Mtoto azaliwapo, bongo lake huwa ombwe tupu na chochote kiingiacho humo huwa kama kinachoandikwa kwa wino usiofutika, hunata kama gundi. Ukomavu huanzia hapa na mzazi **akifanya waa** katika maneno na vitendo afanyavyo kwa mtoto, huenda akachangia kwa kutokomaa kwake.

Mlachake hakuwa na umbu. Hii ilionyesha kuwa, kwa kuwa wazaziwe walikuwa wamejikopoa wana wanne wa jinsia moja, walimngojea mwana wa jinsia tofauti kwa hamu na ghamu. Si ajabu kuwa pindi alipozaliwa waliamua kufikisha uzazi hatima yake baada ya kupata walichokikamia. Msisimko uliowapata wazazi wa Mlachake ndio uliowapelekea kumtendekeza. Na ni kwa nini wazazi wengi huwa hawatosheki kamwe kwa kuwapata watoto wa jinsi moja tu? Si ajabu kuwaona wengine wakijifungua hata zaidi ya wana kumi, tena katika karne hii ya upangaji uzazi, lengo likiwa kusaka jinsia wasiyojaliwa kuipata. Sijui ni nani atakayeuganga ukongo huu.

Mama Mlachake **alipofunga mkaja**, walisitisha shughuli zao zote, wakawa wanasherehekea kwa vigelegele, wakikipakata kitoto chao kwa zamu zilizorembeshwa kwa mashairi ya sifa za utanashati wa mwanao kwa mahadhi mbalimbali yaliyotiwa udamisi ajabu. Msisimko kama huu kama lazima uwepo huwatokea wampatao mwanao wa kwanza na hasa waliolimatia kujikopoa, hivyo baba mtu akaamua hataitwa tena jongoo asiyeukwea mtungi na mama hataitwa tasa. Hili huzua hatari ya kumdekeza mwana, naye atadeka milele kama huyu Mlachake.

Wazazi wa Mlachake hawakumkomaza. Kila kuchao walimwita 'mtoto', naye akawa mtoto wa kweli hata akafikia kidato cha tatu. Yasemwa kuwa Mlachake alilikamata ziwa la mamaye hata akafikia darasa la tano. Haikuwa ajabu kumpata mamake akimsubiri njiani eti maziwa yanamwasha, naye mwanawe amekishika kilembwe kadamnasi ya watu huko njiani, huku amepakatwa kiweoni. Kisha akishakinai kuama, angeelekwa kwa ubeleko hadi nyumbani alikomkuta babaye aliyemgojea kwa ilhamu na kwa nyimbo za kumuongoa hadi alale.

Hadi afike hapo alipokuwa sasa, Mlachake hakujua hata kunawa uso. Daima alioshwa na mvyele wake bila hata kuona soni kwa kuwa aliamini kuwa bado ni mtoto - mfikirie mtu aliyevunja ungo akioshwa na mamaye! Izara yafaa kumkumba, ila Mlachake alinyimwa soni. Ama ndiye aliyezua maneno, "waso haya wana mji wao"? Kama walisema kuwa avuliwaye nguo huchutama, ikawaje hata Mlachake avuliwe nguo na hata kukoshwa? Jitihada za nduguze kumkebehi na kumwambia ajitegemee na zile za majirani kuwasuta wazazi wa Mlachake ziliambulia patupu.

Hii sasa ni shule ya sita aliyosomea Mlachake tangu aingize mguu wake katika shule ya upili. Kila aingiayo haimweki. Mara atasingizia kuwakosa wazazi wake, mara atalia eti chakula ni kigumu, atasema aona baridi akilala peke yake kwa kuzoea kulala mbavuni mwa wazee wake, homa ikimpata hulia kuwa hatunzwi, mwili haogi na hata anaposhikiwa shokoa na wenzake hajui kunawa hata uso! Huyaacha matongo yakiwa mulika watu. Naye hunuka fee! Mahali alalamo ungedhani ni makao ya beberu kwa mnuko. Harufu aliyotoa viatuni mwake ingesababisha pua kung'oka na mapafu kurudi. Alimradi Mlachake au 'toto kuu,' kama alivyobatizwa, alikuwa zaidi ya mtoto. Na ingawa ni mapema sana kuyawaza haya, je, Mlachake atakomaa, atengenee, apate ajira, apate mbawaze arukie au atakuwa kinda milele? **Atapata kufu** yake hatimaye? Wako wapi hawa vifunga mimba, wanuna au wazinanda waliokomaa wawakomaze wasiokomaa? Ama wewe usomaye wasubiri kwenda likizoni kupakatwa na wazazio? Tabia zisizoafiki umri wa mtu huongonga, na wenye hekima walitufaa waliposema, 'mwendo kikwongonga naye mtapike," na kuwa walisema pia, "mtoto akinyea kiweo hakikatwi," tutakiosha 'kiweo' chenyewe, mtoto aadilishwe aadilike, aadibishwe aadibike.

Maswali

a) Ina maana gani kusema Mlachake alikuwa mziwanda? (alama 2
b) Je, ni kwa nini Mlachake alibatizwa 'toto kuu'? (alama 2)
c) Hali hii ya kutokomaa ilitokana na nini? (alama 2)
d) Je, ni nani wa kulaumiwa kuhusu kisa hiki cha Mlachake? Fafanua.
(alama 2)
e) Ni nini maana ya '. . . baba mtu akaamua hataitwa tena jongoo asiyepanda mtungi'?
(alama 2)
f) Eleza tabia ya Mlachake zinazoonyesha kuwa alikuwa toto kweli.
(alama 2)
g) Ni nini maana ya misemo ifuatavyo:
(alama 3)
   i) Fanya waa
   ii) Funga mkaja
   iii) Pata kufu

2. UFUPISHO (alama 15)

Soma kifungu kisha ujibu maswali

Mengi yamezungumzwa na kuandikwa kuhusu 'sheng' na wataalamu wa lugha na watafiti mbalimbli ambayo hayatashughulikiwa hapa. Jambo la kuzingatia ni kwamba 'kilugha' hiki kimesambaa na kuasi utaratibu wa awali uliozingatiwa katika kukiibusha. Kama tunavyoelewa neno 'sheng' ni utohozi wa maneno mawili, 'swahili' na 'English'. Lakini hali ilivyo sasa ni kwamba baadhi ya msamiati unaoundwa

hauchukui maneno ya Kiswahili na Kiingereza pekee. Maneno mengi ya lugha za kikabila katika janibu zetu yameingizwa kwenye hazina ya msamiati wa 'sheng' na kukifanya kiwe na utata mwingi katika kupambanua mofolojia na sintaksia yake.

'Kilugha' hiki pia hakina utaratibu mahsusi unaofuatwa katika uundaji wa maneno, ndiposa kimesheheni utata mwingi. Ni bayana pia kwamba lugha, kama zilivyo asasi zingine za kijamii hukumbwa na mabadiliko. Mabadiliko haya huweza kuifaidi asasi hiyo ikakua na kustawi au huweza pia kuisheheneza athari mbaya ikazorota au kuchukua sura mpya, kinyume na matarajio ya waneni wake.

Sisi kama wanajamii hatuwezi kuzuia mabadiliko , hususan yale yanayoikumba asasi ya lugha. Hata hivyo, tuna uhuru wa kuchagua lugha itakayotuwezesha kuwasiliana kikamilifu. 'Kilugha' cha 'sheng' kimezusha vurugu kubwa katika mawasiliano kati ya vijana na wazee. 'Kilugha' kimetinga mawasiliano pia baina ya walimu na wanafunzi hasa katika miktadha ya kufunza lugha ya Kiswahili.

Isitoshe, katika jamii pana wazee kwa vijana ambao siku hizi wamajitosa kwenye matumizi ya 'Sheng'. Utaweza kuwasikia wanasiasa kwa mfano, wakiongea 'sheng' huku wakidharau kabisa kanuni za lugha kwenye mikutano ya hadhara bila kujali. Huu si mfano mwema kwa watoto wanaokua na ambao wanakabiliwa na tatizo la kupambanua lugha iliyo sahihi katika vurugu hilo.

Baadhi ya walimu wanaotarajiwa kuwa katika mstari wa mbele kudumisha matumizi bora ya Kiswahili, wamo mbioni kukisakama Kiswahili na mitindo ya 'sheng' bila kujali athari za baadaye za kujifunza lugha miongoni mwa watoto hao. Hapo ndipo ninapotoa kauli kwamba lugha ya Kiswahili imefika kwenye njia panda kwani idadi kubwa ya watu hawawezi kupambanua matumizi bora ya lugha ni yapi.

Suala la mielekeo ya lugha pia limechangia katika upotovu wa matumizi ya lugha yasiyozingatia utamaduni wa kijamii. Nafasi ya Kiswahili humu nchini kwa ujumla ni duni ikilinganishwa na lugha za kigeni kama vile Kiingereza na Kifaransa. Uduni huu unatokana na sababu nyingi ambazo haziwezi kujadiliwa kwa kirefu hapa.

Maswali

a) Kwa kutumia maneno 65 - 75 fupisha aya mbili za kwanza (alama 8, 1 ya utiririko)

2. Bila kubadilisha maana fupisha aya nne za mwisho. TumiaManeno 60 - 70 (alama 7 , 1 ya utiririko)

3. MATUMIZI YA LUGHA. (alama 40)

A. i) Taja sauti yenye sifa zifuatazo:
Mbele, juu, tandazwa. (alama 1)
ii) Tofautisha sauti hizi mbili. (alama2)
/chi/ /j/

B. Andika neno lenye muundo ufuatao wa silabi
i) KKKI. (alama 1)
ii) IK (alama 1)

C. Eleza matumizi mawili ya alama mtajo na utolee mifano.
(alama 4)

D. Geuza sentensi ifuatayo katika wingi hali ya ukubwa. (alama 2)
Nguo iliyoraruka itashonwa tena

E. Tunga sentensi mbili tofauti kudhihirisha matumizi mawili ya kiambishi - ji-
(alama 2)

F. Tambua viambishi katika neno lifuatalo na ueleze majukumu yao.
alipogongewa. (alama 3)

G. Kanusha bila kutumia 'amba' (alama 2)
Nitamtunza mwanafunzi ambaye ni nadhifu.

H. Tumia jedwali kuchanganua sentensi ifuatayo. (alama 4)
Ugali huu hauna ladha kwa vile haukutiwa mtama.

I. Tambua yambwa tendwa, tendewa na tumizi katika sentensi ifuatayo. (alama 3)
Halati amemletea mgonjwa dawa kwa chupa.

J. Onyesha vishazi katika sentensi ifuatayo.
(alama 2)
Walibeba maji ya kutosha walipoenda safari Israel.

K. Andika kwa msemo wa taarifa:. (alama 3)
"Sitadhubutu kumpa nguo yangu." Osebe alisema.

L. Tunga sentensi ukitumia kitenzi 'i'
(alama 1)

M. Andika maana mbili zinazojitokeza katika sentensi.
(alama 2)
Jua nisemalo ni muhimu kwetu

N. Onyesha kielezi, kivumishi, kitenzi na nomino katika sentensi hii.
(alama 4)
Watoto watatu walipeperushwa juu kwa juu na upepo mkali

O. Onyesha chagizo katika sentensi ifuatayo.
(alama 1)
Vifaru wote watalindwa kesho.

P. Sahihisha sentensi hii: (alama 1)
Mwizi mwenye ameshikwa atafikishwa katika mahakamani.

Q. Tunga sentensi ukitumia wakati usiodhihirika. (alama 1)

4. ISIMUJAMII (alama 10)

Eleza huku ukitolea mifano sababu TANO zinazowafanya watu kuchanganya ndimi wanapozungumza.

(alama 10)

TATHMINI YA PAMOJA YA SHULE ZA UPILI KAUNTI NDOGO YA KENYENYA
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya
Kidato cha Nne

KISWAHILI
Karatasi - 102/3
Julai / Agosti 2015
Muda : Saa 2½

1. **LAZIMA : SEHEMU YA 'A'**
USHAIRI

1. Naja sasa ni ndiyani, naja kwetu mzalendo,
Naja nirudi nyumbani, nilowekwa nako kando,
Kwetu' mi nakutamani, kulo na mwingi uhondo,
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini.

2. Naja kwingine kuwapi, kulojaa langu pendo,
Nenda nende kwinginepo, sawa nako kwa muundo,
Kaa kwingine anapi, ela kwenye lakwe gando,
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini.

3. Naja nije rudi papo, paningendeme mgando,
Ningaambwa kwetu hapo, kwamba kwanuka uvundo
Sitakwenda penginepo, tarudi kuko kwa mwando,
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini.

4. Naja sitapakimbiya, ningambwa kuna vimondo,
'takuja kuvielekeya, vingajiya kwa rundo,
Nilipozawa tafiya, sikimbii kwenda kando,
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini.

5. Naja hiwa' mekomaa, kuzidi nilivyo mwando,
Tena najiandaa, kwa fikira na vitendo,
Kwetu nije kuifaa, na kuitiliya pondo,
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini.

6. Naja na jingawa naja, siwaekei mifundo,
Moyo wangu ushatuja, mawi nalotendwa mwando,
Ela wataoningoja, na viwi vitendo,
Nijaye ni ile nyundo, misumari hadharini.

MASWALI

a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka. (alama 2)
b) Onyesha jinsi kanuni za utunzi zilivyotumiwa kulisarifu shairi hili. (alama 5)
c) Kwa kutoa mifano, eleza jinsi uhuru wa ushairi ulivyotumiwa. (alama 3)
d) Taja na ueleze mbinu inayopatikana katika ubeti wa pili mshororo wa tatu. (alama 2)
e) Eleza ujumbe unaopatikana katika ubeti wa tatu. (alama 2)
f) Andika ubeti wa sita katika lugha nathari. (alama 4)
g) Andika maneno haya kwa lugha sanifu: (alama 2)
   i) Mwando
   ii) Ningambwa

SEHEMU YA B
TAMTHILIA:
Mstahiki Meya *: Timothy M. Arege*
Jibu swali la 2 au la 3

2. "Sauti ni sauti tu! wanasema mchana usiku watalala. Waache waseme. Kelele za chura ni kelele tu. Hazimzuii ng'ombe kunywa maji".
   a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
   b) Fafanua ujumbe unaotolewa na sauti hizi. (alama 8)
   c) Onyesha jinsi uongozi wa cheneo ulivyokabiliana na wanaotoa sauti hizi. (alama 8)
3. Wananchi wanakufa njaa ilhali viongozi wanawanda. Fafanua. (alama 20)

SEHEMU YA C
RIWAYA:
Kidagaa kimemwozea ; *Ken Walibora*
Jibu swali la 4 au la 5

4. Fafanua kuwa wazungu walipoondoka waliacha majina yao yameandikwa kwa wino usiofutika kwa mujibu wa riwaya ya *Kidagaa kimemwozea.* (alama 20)
5. "Ndugu usinifikirie mwendawazimu . . . . lakini uchanganuzi wangu unaniambia kuwa wewe si mtu wa kawaida."
   a) Onyesha muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   b) Fafanua umuhimu wa msemaji kwa kurejelea riwaya nzima. (alama 6)
   c) Eleza jinsi mwandishi wa *Kidagaa kimemwozea* alivyosawiri maudhui ya tanzia. (alama 10)

SEHEMU YA D:
HADITHI FUPI
Damu Nyeusi na Hadithi nyingine : ***Ken Walibora na Said A. Mohamed***
Jibu swali la 6 au la 7

6. Huku ukirejelea hadithi ya "Tazamana na mauti," jadili ukweli wa kauli kwamba, "Tamaa mbele mauti nyuma." (alama 20)
7. Fafanua jinsi maudhui ya ushirikina yalivyoendelezwa katika hadithi fupi ya "*Gilasi ya mwisho makaburini*." (alama 20)

SEHEMU YA E:
FASIHI SIMULIZI
Jibu swali la 8

8. a) Eleza maana ya ngoma. (alama 2)
   b) Fafanua sifa zozote tatu za ngoma. (alama 6)
   c) Ngoma ina majukumu gani katika jamii? (alama 12)

THE ABOVE (**KAUNTI NDOGO YA KENYENYA**) IS A REVISION EXERCISE

TATHMINI YA PAMOJA – SHULE ZA UPILI ZA KAUNTI YA MAKUENI – 2015

Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya

KISWAHILI

Karatasi ya 1

INSHA

1. Lazima:

Wewe ni mkaazi wa eneo fulani katika Kaunti ya Maili Mbili. Umekuwa ukifuatilia jinsi mambo yanavyoendelea katika kaunti hiyo ambayo imekuwa na changamoto si haba. Andika ripoti yako kuhusu changamoto hizo.

2. Fafanua njia za kustawisha uchumi katika Kaunti ya Makueni.

3. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali: Pwagu hupata pwaguzi.

4. Andika insha itakayomalizikia kwa maneno yafuatayo: ...nilimshukuru Mungu kwa kuniponya.

TATHMINI YA PAMOJA – SHULE ZA UPILI – JIMBO LA MAKUENI 2015
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya (KCSE)
102/2
KISWAHILI
Karatasi ya 2
LUGHA

1. UFAHAMU (Alama 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.

Siku hizi kuna vitambaa aina aina vya kushonea nguo na pia vingine vinaendelea kutengenezwa. Kuna vitambaa vya pamba, hariri vya mnato, nailoni, sufi na vinginevyo. Kadhalika, vitambaa hivi vina mitindo na rangi za kila aina.

Kuchagua kitambaa cha kushonea nguo si jambo rahisi. Uchaguzi huo ni sharti ufikiriwe kwa makini sana. Mnunuzi wa vitambaa vya nguo anapaswa kufahamu kuwa kuna vitambaa tofauti vyenye sifa tofauti tofauti. Kwa mfano, baadhi ya vitambaa hukwajuka au kuchujuka rangi na kuwa vyeupe, vingine huchanika vinaposuguliwa, vingine hurudi vikifuliwa na vingine hukunjana vinapofuliwa.

Baadhi havipigwi pasi, na havifuliwi kwa maji baridi, vingine hufuliwa kwa maji yenye joto kiasi.Mnunuzi anapaswa kuzingatia sifa hizi zote anapochagua vitambaa vya kushona nguo. Hata hivyo, ni vizuri kufahamu kwamba sio watu wote wanaozifahamu sifa zote muhimu za vitambaa, na wale wanaozijua baadhi za sifa hizi hawazijui zote.

Kuna njia kadhaa anazoweza kutumia mnunuzi ili kujua sifa za vitambaa vya nguo. Mnunuzi kwa mfano, anaweza kuwauliza wauzaji. Ni vizuri hata hivyo, kutahadhari na kuyapima maelezo yanayotolewa kwa uangalifu. Ingawa chini ya kifungu cha sheria cha maelezo ya kibiashara wauzaji wanapaswa kutoa habari sahihi kuhusu bidhaa zao, si wote wanaosema ukweli. Hii ni kwa sababu wengine huhofia kwamba wakitoa habari sahihi huenda wakakosa wateja wa kununua bidhaa zao.

Njia nyingine ambayo mnunuzi anaweza kutumia kujulia habari za vitambaa ni kwa kuangalia maelezo yanayopatikana kwenye vibandiko au vijikaratasi vya maelezo. Kwa mujibu wa sheria za nchi nyingi vibandiko vya aina hii vinapaswa kuwa sahihi lau kutoa habari zisizo sahihi ni kosa linaloweza kumfanya mtengenezaji kuadhibiwa. Maelezo yanayopatikana kwenye vibandiko hivyo ni muhimu kwani hutoa maelezo muhimu kuhusu aina ya vitambaa, namna vinavyoweza kufuliwa na kama vinapaswa kupigwa pasi au la miongoni mwa mambo mengine.

Mtu anaweza kujua aina ya kitambaa pia ikiwa ana ujuzi wa kushika au 'kuhisi'. Mtu anaweza kushika kitambaa kwa utaratibu na kukadiria kama kinakunjanakunjana au la. Hata hivyo, ni muhimu kufahamu kwamba sio wauzaji wote ambao wanapenda vitambaa vyao vishikweshikwe kwani vikishikwa sana huishia kuwa vichafu na kukosa wanunuzi.

Baada ya uchaguzi bora wa kitambaa, uamuzi wa kama mtu fulani atanunua kitambaa kizuri au la ni bei. Ni vizuri kutafuta vitambaa vizuri na visivyo vya bei ghali. Kufanya hivyo kutamsaidia mnunuzi kutotumia pesa ambazo angetumia kufanyia mambo mengine kununulia nguo tu.

Maswali

(a) Toa kichwa mwafaka kwa taarifa hii. (alama 1)
(b) Mwandishi ana maana gani anaposema: (alama 3)
(i) vitambaa vya aina aina?
(ii) baadhi ya vitambaa hukwajuka au huchujuka rangi?
(iii) vingine hurudi vikifuliwa?
(c) Taja njia **tatu** zinazomsaidia mnunuzi kuchagua kitambaa bora, kwa mujibu wa taarifa. (alama 6)
(d) Taja aina ya vitambaa vilivyotajwa na mwandishi katika taarifa. (alama 2)
(e) Je, baada kuchagua kitambaa unachotaka, ununuzi wa kitambaa hicho utategemea nini? (alama 3)

2. UFUPISHO (Alama 15)

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Mwana wa Adamu ni kiumbe cha ajabu! Ni kiumbe kilichopewa uwezo wa kuhodhi na kumiliki kila kitu. Kiumbe kilichopewa uwezo wa kuwasiliana kwa kutumia sauti nasibu ili kuwa na urari na muwala. Kiumbe kilichopewa idhini maalumu ya kuzaana na kujaza dunia. Huyu ndiye mwana wa mama Hawa ambaye sasa amegeuka fisi kumla mwanawe.

Kwa sababu ya bongo alizonazo, binadamu ana uwezo wa kutumia teknolojia kwa manufaa yake na ithibati ipo tele. Binadamu ametumia nyambizi kuzuru chini ya bahari. Amefika mwezini, amevumbua uyoka, amevumbua tarakilishi na sasa shughuli zake ni za kutandaridhi. Mwenyewe yuasema kuwa dunia yake imekuwa kitongoji katika muumano huu.

Chambilecho wavyele, akili nyingi huondoa maarifa. Binadamu amekuwa dubwana linalojenga kushoto na kubomoa kulia na tuna sababu ya kulisoza dubwana hili kidole. Rabana ndiye msanii asiye mfanowe Kwani alisawiri dunia kwa kila lililo jema, kwa siku sita mtawalia na kumpa binadamu mazingira murua. Rabuka akaona yote yalikuwa mema na mazuri, akamwambia binadamu, “Haya twende kazi.”

Viwanda vya binadamu vinatiririsha maji taka ovyo hadi mitoni, maziwa na baharini na matokeo yamekuwa ni vifo vya viumbe vya majini kama samaki ambavyo ni urithi aliopewa na Muumba. Hakuna kiumbe kinachoweza kustahimili maisha bila maji safi. Maji yote sasa yametiwa sumu na binadamu kwa sababu ya ‘maendeleo’ yake. Joshi kutoka katika viwanda vivyo hivyo nalo limehasiri ukanda wa ozoni ambao sasa umeruhusu jua kutuhasiri kwa joto kali mno. Siku hizi inasemekana kuwa mvua ya asidi inanyesha katika baadhi ya sehemu za dunia na kuleta madhara makubwa. Labda hata mabahari yamekasirika kwa sababu hivi majuzi katika kile kilichoitwa ‘tsunami’, bahari lilihamia nchi kavu na kusomba maelfu ya binadamu na kuwameza wazima wazima. Vimbuga navyo vimetokea kwa wingi.

Wataalamu wanasema kuwa viwango vya miyeyuko vitazidi kwa sababu ya joto na kiwango cha maji kitazidi pia. Binadamu atatorokea wapi?Idadi ya binadamu imefikia kiasi asichoweza kukishughulikia kwa sababu anaijaza dunia kiholela kwa sababu anadai aliruhusiwa kuijaza. Hii ni imani potovu. Anasahau kuwa alipewa ubongo wa kuwaza na kuwazua kabla ya kufanya chochote. Dhiki, maradhi na ufukara zimehamia kwake binadamu na kumtia kiwewe. Binadamu ameifyeka misitu kwa kutaka makao, mashamba, mbao, makaa, ujenzi wa nyumba na barabara na mahitaji mengine mengi. Wanyama wamefurushwa na wengine kuangamia kwa sababu ya ukosefu wa chakula na wengine kushindwa kuhimili mabadiliko katika mazingira. Chemichemi za maji zimekauka nalo jangwa limeanza kutuzuru kwa kasi inayotisha. Kazi ya binadamu imekuwa ya kusukia kamba motoni. Itambidi aanze kujenga kwa matofali ya barafu!

(a) Fupisha aya ya **kwanza** bila kupoteza maana asilia. (maneno 45) (alama 6, 1 ya mtiririko)
(b) Eleza mambo muhimu yanayoshughulikiwa na mwandishi katika aya **nne** za mwisho. (maneno 100) (alama 9

3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)

(a) Nomino hizi hupatikana katika ngeli zipi? (alama 2)
(i) Saa
(ii) Dunia

(b) Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa.
"Mimi nitawakaribisha wageni leo jioni. Kisha nitaondoka kwenda kwangu kesho," Fatuma alimwambia
Juma. (alama 3)

(c) Andika kwa ukubwa.
Kiti kilichokuwa kimekaliwa na mwanamke yule kilivunjika. (alama 2)

(d) Yakinisha katika umoja:
Nyuzi zisingekatika zisingepotea. (alama 2)

(e) Bainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo.
Babake Mutua alitumiwa barua kwa posta. (alama 3)

(f) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mistari au mishale.
Ingawa wachezaji wamewasili, wakereketwa hawashangilii. (alama 4)

(g) Bainisha aina ya maneno yaliyopigwa mistari katika sentensi zifuatazo.
Nipatie kazi yoyote.
Yoyote inazidi kulenga juu. (alama 2)

(h) Eleza matumizi ya 'ki' katika sentensi hii:
Kikulacho ki nguoni mwako. (alama 2)

(i) Tunga sentensi katika kauli ya kutendeana ukitumia kitenzi -la. (alama 2)

TATHMINI YA PAMOJA – SHULE ZA UPILI – JIMBO LA MAKUENI 2015
Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya (KCSE)
102/3
KISWAHILI
Karatasi ya 3
FASIHI

SEHEMU A: TAMTHILIA

1. Lazima

T. Arege: *Mstahiki Meya*

Mwafulani I: Hiyo ndio zitafaa nini?
Mwafulani II: Nimeambiwa tuwashauri wasubiri.
Mwafulani I: [Anamtazama] Wasubiri?

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Fafanua umuhimu wa Mwafulani I. (alama 4)
(c) Maudhui ya utegemezi yamejitokeza katika tamthilia. Fafanua aina tofauti za utegemezi. (alama 10)
(d) Fafanua madhara yake kwa jamii. (alama 2)

SEHEMU B: RIWAYA

K. Walibora: *Kidagaa Kimemwozea*

Jibu swali la 2 au la 3.

2. "… Nilitaka kukuuliza kama waelewa usomacho na sasa nadhani labda swali hilo halina mashiko."
(a) Bainisha muktadha wa maneno haya. (alama 4)
(b) Jadili nafasi ya msemaji katika riwaya. (alama 8)
(c) Fafanua sababu ya msemaji kumwambia msemewa kuwa swali hilo halikuwa na mashiko. (alama 8)

3. Jadili maudhui yafuatayo kama yanavyojitokeza katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea*.
(a) Taasubi ya kiume (alama 10)
(b) Ukatili (alama 10)

SEHEMU C: HADITHI FUPI

K. Walibora na S.A. Mohamed: *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*

Jibu swali la 4 au la 5.

4. "... Aliinua uso wake na kumtazama mwalimu mkuu."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Yafafanue matatizo yaliyomkumba mwalimu mkuu kijumla katika kuendeleza kazi yake. (alama6)

(c) Sista niwakulaumiwa pakubwa kutokana na yaliyompata Sela. Fafanua. (alama 6)

(d) Kwa kurejelea hadithi nyingine nne, taja na ueleze mfano mmoja wa waliokumbwa na yaliyompata Sela. (alama 4)

5. Kama sio sadfa Kristina Mwende Mbai katika Mwana wa Darubini hangefanikiwa kupitisha ujumbe wake na kukolea jinsi ulivyo. Thibitisha. (alama 20)

SEHEMU D: USHAIRI

Jibu swali la 6 au la 7.

6. *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo.*

Msambe naja kuteta, nina wema wa kalima,
Moto wanikatakata, maini yangu yachoma,
Ili nipate takata, ukweli wote 'tasema,
Anayekataa pema, pabaya panamuita.

Muacha pema hujuta, aendapo si salama,
Bahati ni kama nyota, humemeta na kuzima,
Sikimbilie mafuta, ukatae kula sima,
Anayekataa pema, pabaya panamuita.

Haraka zina matata, angaza mbele na nyuma,
Tenda mambo kwa kusita, usije ukalalama,
Keti pako ukipata, kwa muradi wa uzima,
Anayekataa pema, pabaya panamuita.

Pema si penye mafuta, au pa wali na nyama,
Pema watu hutafuta, utulivu na hekima,
Si hoja penye ukata, pa watu hali ya nyuma,
Anayekataa pema, pabaya panamuita.

Mahali pema ambata, kwa vitendo na huduma,
Sikae penye matata, palipojaa hasama,
Lau kama pamemeta, hapafai kwa daima,
Anayekataa pema, pabaya panamuita.

Maswali

(a) Lipe anwani mwafaka shairi hili. (alama 1)

(b) Bainisha bahari mbili za shairi hili. (alama 2)

(c) Eleza muundo wa shairi hili. (alama 4)

(d) Fafanua dhamira ya mshairi. (alama 1)

(e) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari. (alama 4)

(f) Onyesha jinsi mshairi alivyoutumia uhuru wake. (alama 3)

(g) Kwa kutoa mifano, bainisha tamathali mbili za usemi zilizotumika katika shairi hili. (alama 2)

(h) Eleza maana ya msamiati ufuatao. (alama 3)

(i) Kalima
(ii) Mafuta
(iii) Ukata

7. *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

Mwananchi: Ingawa ni nchi yangu, mie siipendi sana,
Ina tando la ukungu, kadha mawimbi mapana.
Mzalendo: Wewe u mwana wa wapi, ni bora kujulishana,
Msimamo wako mpi, imara uloshikana?
Mwananchi: Hayo ni maswali gani, au tunataniana?
Hunijui toka lini, mzawa mjulikana!
Mzalendo: Sura yako naijua, ila kadhia hapana,
Vile navyokutambua, sivyo ninavyokuona.
Mwananchi: Mimi usinitazame, angalia kila kona,
Si wake na si waume, vile wavyozongeana.
Ni vurugu na hujuma,si wazee si vijana.
Hatokezi mtu mwema, msafi aso jaana?
Watoto waliosoma, si watu ni Subuhana?
Pa kutoka huduma, wanaenda kujivuna.
Mzalendo: Kweli unanishangaza, ni kama tunagombana.
Ama tunazungumza, bayana kuambizana?
Mwananchi: Unakwea na kuwanda, wengine wakaondeana,
Unachuma usopanda, kuhemera usovuna.
Mzalendo: Nakuona una nyingi, tafakuri za maana,
Maneno yenye msingi, bali doa ni la jana.
Asubuhi na mapema, nuru ipotanzukana,
Giza jekundu kuhama, jeusi likatandana.
Mwananchi: Hujawa kindakindaki, mzalendo mwungwana,
Abadi sikuafiki, koma kunidonadona.
Jukwani mpenda uma, huko chama ndiwe ngwena,
Watafuna watu nyama, vijikongwe na watwana.
Umesoma kitu gani, taaluma za kulana?
Nchi yetu taabani, na shahada umebana!
Sije kwangu kunitubu, niko macho ninaona,
Damu yako ni tabu, osha utoe laana.
Ati wewe mzalendo, mwenye tumbo limenona,
Na madole yenye gando, ya kuhujumu mchana!
Mimi ninakuachia, nisije nikajichuna,
Kemi zangu najutia, sitaki kutatizana.

Maswali

(a) Shairi hili ni la aina gani? Toa sababu. (alama 2)
(b) Eleza maudhui manne yanayodhihirika katika shairi hili. (alama 4)
(c) Eleza jinsi uhuru wa kishairi ulivyotumika katika shairi hili. (alama 2)
(d) Eleza mtindo wa mwandishi ulivyotumika katika shairi hili. (alama 2)
(e) Mshairi anamaanisha nini anaposema ‘watafuna watu nyama, vijikongwe na watwana? (alama 2)
(f) Thibitisha kwamba shairi hili ni la kimapokeo. (alama 2)
(g) Taja toni ya Mwananchi katika shairi. (alama 2)
(h) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika shairi. (alama 4)
i) Bayana
ii) Tafakuri
iii) Kunidonadona
iv) Ngwena

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

8. (a) Eleza maana ya miviga. (alama 2)
(b) Taja na ufafanue aina sita za miviga. (alama 6)
(c) Fafanua hasara sita za miviga. (alama 6)

(d) Eleza changamoto zozote nne zinazokumba ngomezi ya kisasa. (alama 6)

THE ABOVE (**JIMBO LA MAKUENI 2015**) IS A REVISION EXERCISE

Meanwhile,on addition;

Contact 0714497530 for;

Other well designed high school materials

Updated CPA,CIFA,CICT,CPS materials

Several novel collections

Motivational books

Inspirational books

Setbooks and guides

Teaching schemes

KCSE and Mock past papers

Revision materials

KRA services

HELB services

Website Design & development

Guidance & counselling services

CONTACT

0714497530(MR ISABOKE)

(isabokemicah@gmail.com)

Regards